Maamuzi na Maazimio ya
Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu
Liliopo chini ya
Shirika la Ushirikiano wa Kiislamu
Vikao Namba 1 – 25
Maazimio Namba 1 – 255
1405 – 1444 H / 1984 – 2023

Maamuzi na Maazimio ya
Kongamano la Kimataifa la Fiqh a Kiislamu
Liliopo chini ya
Shirika la Ushirikiano wa Kiislamu
Vikao Namba 1 – 25
Maazimio Namba 1 – 255
1405 – 1444 H = 1984 – 2023

Haki za Kunukuu zimehifadhiwa na:

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu

Toleo la Nne

1442 H = 2020



Na linapo wafikia jambo lolote lilio khusu amani au la kitisho wao hulitangaza. Na lau kuwa wangeli lipeleka kwa Mtume na kwa wenye mamlaka kati yao, wale wanao chunguza wangeli lijua. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema yake mngeli mfuata Shet'ani ila wachache wenu tu.

(Surat al-Nisaa: 83)

Yaliyomo

Maamuzi nambari 84 (1/9) 210

Yanayohusiana na 'Biashara ya Dhahabu na Suluhisho la Kisharia Zikutanapo Ubadilishaji wa Pesa na Uhaulishaji' 210

Maamuzi nambari 85 (2/9) 213

Yanayohusiana na 'Utekelezaji wa Kisasa wa *Salam*' 213

Maamuzi nambari 86 (3/9) 216

Yanayohusiana na 'Akiba za Kibenki (Akaunti za Benki)' 216

Maamuzi nambari 87 (4/9) 219

Yanayohusiana na 'Uwekezaji kwenye Hisa na Mikoba ya Uwekezaji' 219

Maamuzi nambari 88 (5/9) 221

Yanayohusiana na 'Uzabuni (Tenders)' 221

Maamuzi nambari 89 (6/9) 223

Yanayohusiana na 'Kadhia za Sarafu' 223

Maamuzi nambari 90 (7/9) 225

Yanayohusiana na 'Maradhi ya Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI) na Hukmu za Kifiqhi Zinazohusiana nayo' 225

Maamuzi nambari 91 (8/9) 229

Yanayohusiana na 'Misingi ya Kutafuta Suluhu katika Fiqhi ya Kiislamu' 229

Maamuzi nambari 92 (9/9) 231

Yanayohusiana na 'Kuzuia Sababu za Kupelekea Maovu (*Sadd Dharaai'*)' 231

UTANGULIZI

Utangulizi wa kwanza na

Mstahiki Katibu Mkuu wa Taasisi ya Ushirikiano wa Kiislamu (TUK)

Dr. Yusuf Bin Ahmad al-Uthaymeen

Himdi zote ni za Allah Mola wa viumbe vyote, sala na salamu zimfikie kiongozi wa mitume wote; Mtume wetu Muhamad Pamoja na Aali zake na masahaba wake wote.

Ammaa Baadu:

Kwa hakika, “Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu” ni mojawapo ya vyombo muhimu vya Taasisi ya “Shirika la Ushirikiano wa Kiislamu”, aidha kongamano hili ni rejea tegemeo la masuala ya ki-fiqhi katika nchi wanachama wa ‘Shirika’ hili, hali kadhalika ni tegemeo kwa jamii zote a kiislamu zinazoishi nje ya ‘Ulimwengu wa Kiislamu’, pia ni chombo cha masuala ya kisheria ya ‘Shirika’ hili.

Kwa mda wa miongo minne (miaka 40) sasa, kongamano hili limekua likitoa mchango mkubwa kupitia maamuzi yake na maazimio ya ki-fiqhi yaliyo imara yaliyokubaliwa na wanazuoni wa madhehebu ya kiislamu mbali mbali katika kubainisha ‘Hukumu za Kisheria’ juu ya kadhia mpya zinazoibuka zama hizi, aidha kongamano hili limeweza kwenda sambamba na mabadiliko ya kimaisha ya zama hizi kwa kutumia mbinu ya ‘ijtihadi ya pamoja’ kwa kuwatumia wataalamu wa Nyanja mbali mbali za kielimu, maarifa na uweledi, wakiongozwa na misingi imara ya itikadi na Imani ya kiislamu Pamoja na kutegemea maagizo ya ‘Sharia ya Kiislamu’ yaliyotakasika na yenye uwezo mkubwa wa kumtimizia binadamu kheri na furaha katika maisha yake katika zama zote na na maeneo yote anayoishi.

Inafaa ijulikane hapa kua ‘Kongamano’ lilizingatia vilivyo tangu kuanzishwa kwake maadili ya kua na msimamo wa kati na kati ‘*wasatia*’, ulingano wa ki-fikra, kukubali maoni ya wengine na kukataa ushabiki na kuchupa mipaka ‘*ghuluw*’. Ni kwa mujibu wa msimamo huo leo tunajivunia kua na kitabu hiki adhimu kilichokusanya ‘maamuzi’ na ‘maazimio’ ya aina yake

yaliyo gusa kila Nyanja ya maisha; kitabu hiki ni mojawapo ya matunda yaliyozalikana kutokana na juhudi kubwa za ‘wanazuoni wanafiqihi waliobobea na wataalamu miongoni mwa ‘umma wa kiislamu’ katika vikao vyao walivyokutana kuanzia kikao namba moja (1) hadi kikao cha ishirini na tano (25) chini ya mwavuli wa Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu (KKFK) katika kipindi cha mwaka 1405 – 1444 H / 1984 – 2023. Aidha kitabu hiki ni dhihirisho la ushirikiano wa karibu sana na wa kina miongoni mwa ‘wanazuoni wa fiqhi na sharia ya kiislamu na wataalamu wa Nyanja nyingine za maarifa mbali mbali.

Nikiwa natanguliza chapa ya kitabi hiki cha ‘maamuzi na maazimio ya kongamano’ napenda kutoa shukran zangu za dhati kabisa kwa niaba ya nafsi yangu lakini pia kwa niaba ya wajumbe na wataaalamu wa ‘Kongamano’ na kuzitanguliza shukrani hizi kwa ‘Maqaam ya Khadimul-Haramain Mfalme Salman ibn Abdulaziz Aal-Saud (Allah ampe nguvu) na naibu wake muaminifu muheshimiwa Muhammad ibn Salman ibn Abdulaziz Aal-Saud (Allah amuhifadhi) kwa mengi na mazuri na misaada ya kila aina wanayoipatia ‘Kongamano’ na kuliwezesha tangu kuanzishwa kwake hadi leo hii. Kwa hili tunawaombea kwa Allah awamiminie malipo mema na ailinde dola ya Saudia na nchi zote za kiislamu pamoja na jamii za waislamu duniani kote na awadumishie neema zake za amani, salama na maisha mema.

Hali kadhalika ni furaha kwangu kutoa shukrani za dhati kwa muheshimiwa ndugu yangu aziz Sheikh Daktari Saleh ibn Abdallah ibn Humeid; Mkurugenzi wa Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu (KKFK), ambae pia ni mshauri katika ikulu ya kifalme na mjumbe wa ‘Jopo la Wanazuoni Wakuu’ na pia imam na khatibu wa Masjid al-Haram wa Makkah kwa juhudi zake kubwa na za kitaaluma katika kufanikisha malengo ya ‘Kongamano’.

Nitakua mwizi wa fadhila nisipotoa shukrani za dhati na heshima kubwa kwa waheshimiwa wajumbe wa ‘Kongamano’ wanaowakillisha nchi za kiislamu mbali mbali na wataalamu wa Nyanja mbali mbali kwa michango yao endelevu kwa ‘Kongamano’.

Kuhtimisha, sina budi ila nimpongeze ndugu yangu Katibu Mkuu wa

‘Kongamano’ Muheshimiwa Daktari Qutub Mustafa Sanu kwa mafanikio haya makubwa katika muda fupi wa uongozi wake kama Katibu Mkuu wa ‘Kongamano’, tunazidi kumuombea Allah amuafikie katika kutekeleza majukumu yake.

Allah pekee ndie mwenye kutuwafikia sote; Ameen.

Dr. Yusuf ibn Ahmad al-Uthaymeen
Katibu Mkuu wa Taasisi ya Ushirikiano wa Kiislamu (TUK)

Utangulizi wa pili na:

Mstahiki Sheikh Dr. Saleh ibn Abdallah ibn Humeid

Mkurugenzi wa Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu’ (KKFK)

Mshauri katika ikulu ya kifalme, Saudia

Mjumbe wa ‘Jopo la Wanazuoni Wakuu’ wa Saudia

Imam na khatibu wa Masjid al-Haram, Makkah

Himdi zote ni za Allah alieweka juu nafasi ya wenye elimu na kunyanyua juu nafasi ya wenye Imani na kuwafanya wote hao kua ni viongozi wanaowaongoza waja wa Allah kupitia uongofu wa Qur’an na uongofu wa Mtume wake; sala na salamu ziwafikie yeye pamoja na aali zake na masahaba wake wote.

Amma Baadu:

Jambo linalopaswa kujulikana ni kwamba ili mwanadamu awe na furaha katika maisha yake basi hana budi kuipata ‘elimu ya fiqhi’ ilia pate itumia katika dini yake na maisha yake, bali katika viashiria vya kupata pepo na kheri nyingi ni mt kuitafuta elimu ya fiqhi na kuifanyia kazi kwa nia halisi ya kutafuta radhi za Allah, ndio maana kasema Mtume SAW (من يرد الله به خيرا يفقهه في الدين) ‘*Yeyote yule ambae Allah anamtakia kheri basi humuafikia kwenye elimu ya fiqhi (ufahamu wa dini)’*[1].

Hii ni kwa sababu ufahamu mzuri katika dini ni njia ya kutambua hukumu za sheria na makusudio yake na hikma zake, pia ni kua na upambanuzi baina ya mambo ya halali na yale ya haramu jambo ambalo linapelekea kua na utekelezaji mzuri wa mambo ya wajibu kwa Allah na utekelezaji wa haki kwa raia kwa njia iliyo sahihi, ndio maana Allah akasema kumuambia Nabii Sulaiman, ambae tayari alikua ameruzukiwa akili, (ففهمناها سليمان) ‘*Tukamfahamisha Sulaiman*’[2].

Kulingana na kasi ya maendeleo na utitiri wa mabadiliko na mageuzi

[1] imepokewa na Bukhari na Muslim.

[2] Surat al-Anbiyaa: 79

yanayofuatana na maingiliano ya kitaaluma, na kutokana na haja kubwa iliopo ya ubainishwaji wa hukmu za kisheria katika mambo mapya yanayojiri na yanayoendelea kuibuka, na kwa kuzingatia umuhimu wa kua na 'ijtihadi ya pamoja' itakayo jumuisha wanafiqihi na wanataaluma nyengine wakae pamoja na wanazuoni na wenye uzoefu wa maisha; kuyazingatia yote hayo na mengineo 'Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu' (KKFK) limekua mstari wa mbele kabisa, tangu kuanzishwa kwake, katika kuleta uwiano wa kifikra baina ya wanazuoni wa kifiqhi wa madhehebu mbalimbali pamoja na wanataaluma wa fani nyingine. Kwa hili tunamshukuru Mwenyeezi Mungu, kwa mafanikio ya juhudi hizi kwani tumeweza kutoa maamuzi mia mbili na hamsini na tano (255) yanayohusiana na kadhia mbalimbali zilizoibuka katika zama hizi na kuzipatia ufumbuzi wa kifiqhi. Maamuzi na maazimio haya yamejikita katika viwango vya hali ya juu katika ubora na udhibiti; hii ni kutokana na mbinu zinazotumiwa na 'Kongamano' wakati linapokabiliana na kadhia inayotakiwa ufumbuzi wa kifiqhi; kupitia njia zile walizopitia wanazuoni wa fiqhi wanapotaka kupata hukmu ya kadhia mpya iliyoibuka ambayo kwanza ni kuifahamu kadhia yenyewe kwa kina kisha ni kuisawazisha na hali halisi iiyopo, baada ya hapo ni kuijengea misingi ya kisheria na utohoaji (istinbati) wa hukmu mpya, baada ya hapo ndio mchakato wa utekelezaji na utumiaji wa hukmu mpya juu ya kadhia iliyojitokeza kwa kufuata taratibu za kielimu na za kitaaluma.

Ni jambo la Faraja na la kutia moyo kuona kwamba 'Maamuzi na Maazimio ya Kongamano' yanakubalika na kufanyiwa kazi katika nchi za kiislamu na wanazuoni wa fiqhi nah ii imelifanya 'Kongamano' kua ni rejea muhimu inayotegemewa na waislamu kote duniani, ziada ya hapo hata wanazuoni na ma-ulamaa wa sharia na masomo ya kiislamu katika vyuo vikuu na vituo vya utafiti ndani na nje ya nchi za kiislamu wanatambua umuhimu wa 'Maamuzi na Maazimio ya Kongamano' na kuyafanya ni rejea muhimu katika shughuli zao za ufundishaji na utafiti ili wanafunzi wao wapate usomi wa karibu baina ya kusoma kwa elimu ya fiqhi kinadharia na kuisoma kivitendo kupitia 'Maamuzi haya na maazimio ya Kongamano' hivyo basi kuwaandaa katika mchakato huu wa 'Ijtihadi ya pamoja na ya kitaasisi' kutohoa hukmu mpya na kuzishusha kwenye matukio mapya au kadhia

mpya. Ijulikane kwamba ukamilishaji wa mchakato huu wa kuyajengea misingi ya kisharia na vipimo yvake na makadirio yake ni kukusanya ‘Maamuzi’ haya yakiambatana na mchakato mzima wa kuyafikia katika ‘Jarida’ (Majalla) maalum la ‘Kongamao’.

Kwa sasa ni furaha ilioje kwa ‘Kongamano’ kukuleteeni chapisho hili jipya lililohakikiwa la ‘Maamuzi yote na Maazimio’ ya vikao vyake mbalimbali kuanzia kikao cha kwanza (1) hadi kikao cha ishirini na tano (25) cha mwisho (1405 – 1444H / 1984 – 2023), toleo (chapisho) hili linakuja miaka kumi na tatu baada ya kutolewa toleo la mwisho la ‘Maamuzi na Maazimio ya Kongamao’ la mwaka 1431H/2011.

Napenda kutumia fursa hii adhimu kutambua na kushukuru kwa msaada mkubwa wa kifedha na kimaana na aina nyingine mbalimbali za usaidizi tinazozipata hapa ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu’ (KKFK) kutoka kwa viongozi wa nchi za kiislamu katika kuliwezesha ‘Kongamano’ hili kuendelea kutekeleza ‘risala’ yake na kufikia malengo yake na kutimiza ratiba zake kwa minajili ya kwahudumia waislamu na uislamu kote ulimwenguni.

Ninathamini kwa kiwango cha juu kabisa ulezi wa aina yake tunaoupokea katoka nchi ya makao makuu Saudi Arabia kupitia maelekezo ya ‘Mtumishi wa Haram mbili tukufu’ Mfalme Salman ibn Abdulaziz Aal-Saud, Allah awaafikie, yeye pamoja na naibu wake (waliy al-‘Ahd) muaminifu Mstahiki Muhammad ibn Salman ibn Abdulaziz Aal-Saud, Allah amlinde, pia sitowacha kumshukuru kwa wingi sana Katibu Mkuu wa Shirika la Ushirikiano wa Kiislamu; Dr. Yusuf ibn Ahmad al-Uthaymeen kwa juhudi zake endelevu kwa ‘Kongamano’ pamoja na shughuli zake na ratiba zake zote.

Sitosahau kuwakumbuka, kuwashukuru na kuwaombea dua (maghfira) wanazuoni wetu waliotangulia mbele ya haki hususan Sheikh Dr. Bakar Abuzayd aliekua Mkurugenzi wa ‘Kongamano’, na Sheikh Dr. Muhammad al-Habib Balkhoja aliekua Katibu Mkuu wa ‘Kongamano’, na Sheikh Dr. Abdulsalam al-Abbadi aliekua Katibu Mkuu wa ‘Kongamano’, Allah awarehemu wote na awalipe malipo mema yale waliyotanguliza katika elimu zao na amali zao kutumikia umma, Allah aziweke amali zao katika

mizani ya mema (hasanaat) yao, na asitunyime na sisi ujira wa mema yao asitufitinishe baada yao na awasulihishe vizazi vyao. Shukrani zetu ziunganishwe moja kwa moja kwa Samahat (Mstahiki) Sheikh Dr. Ahmad Khalid Baabikr Katibu Mkuu wa zamani wa ‘Kongamano’, Allah ampe salama.

Mwisho kabisa siwezi kumalizia bila kutoa shukrani zangu za dhati na heshima kubwa kwa Katibu Mkuu wa ‘Kongamano’, Ma’ali (Mstahiki) Sheikh Dr. Qutub Mustafa Sanu yeye pamoja na wasaidizi wake kwa juhudi hizi kubwa na mafanikio makubwa waliyoyafikia katika kipindi kifupi tangu kushika wadhifa huu miezi miwili iliyopita.

Namuomba Allah Mkarimu atunufaishe kwa toleo (chapisho) hili na atuongoze njia iliyo sawa (iliyonyooka) na aendelee kutumiminia msaada na taufiq ili tuweze pata mafanikio ya hapa duniani na kesho aakhera.

Sala na salamu zimfikie bwana wetu Mtume Muhammad (SAW) pamoja na Aali zake na Masahaba wake wote.

Dr. Saleh ibn Abdallah ibn Humeid
Mkurugenzi wa Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu’ (KKFK)

Utangulizi wa tatu na:

Mstahiki Sheikh Dr. Qutub Mustafa Sanu

Katibu Mkuu wa Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu’ (KKFK)

Himdi zote ni za Allah alietuongoza katika jambo hili, tusingeweza kuongoka sisi pasi na yeye Allah kulitaka hilo. Himdi zote ni zake yeye ambae kupitia kwake mambo mema yanakamilika. Sala na salamu zimfikie kiongozi wa ulimwengu alieletwa kwetu akiwa ni rehema kwa walimwengu wote na taa inayoangazia na kuonyesha njia, zimfikie yeye pamoja na Aali zake waliotahirika na Masahaba wake waliowema na kwa watakaofuata njia yake hadi siku ya malipo.

Amma Baadu:

Haitokua ni taarifa mpya kua ‘Risala’ ya uislamu ndio hitimisho ya risala zote alizozituma Allah kwa binadamu, umwisho wa ‘risala’ hii unadhihiri vyema katika wepesi wa sharia zake na upana wa hukmu zake na kwamba mafundisho yake na maelekezo yake ni muwafaka kabisa na ni yenye kuendana na zama zote nyakati zote na sehemu zote, bali misingi yake iliyo imara na malengo yake ya hali ya juu yamekua na uwezo wa kuelekeza umma jinsi gani ya kukabiliana na mabadiliko ya kimaisha wakati wowote sehemu yoyote kwa mujibu wa manhaj (mfumo) kabambe wa kielimu ulioegemezwa kwenye misingi mikuu ya sharia na malengo makuu ya maslahi ya binadamu katika maisha yake ya hapa duniani na ya kesho aakhera.

Aidha, umwisho wa ‘risala’ hii unadhihiri vizuri katika mfumo mzima wa kujengeka hukmu zake kwa kuzingatia na kuwaletea raia mambo ya maslahi kwao katika maisha ya hapa duniani na ya kesho aakhera, sambamba na kusimamisha misingi ya haki na uadilifu katika jamii na kueneza huruma na kulinda haki za binadamu na kudhibiti mipaka ya uhuru na kuamirisha (kujenga na kuendeleza) huu ulimwengu na kutia furaha katika jamii ya binadamu.

Kulingana na kasi ya mabadiliko katika nyaja zote za maisha ya binadamu hasa katika zama zetu hizi, na uwepo wa maingiliano ya kijamii na

urundikizaji wa matukio, lakini pia kuzingatia umuhimu wa ushirikiano baina ya wanazuoni na wana-fiqihi wa madhehebu mbalimbali kwa upande mmoja; na kwa upande wa pili umuhimu wa ushirikiano baina ya wana-fiqihi na wana-taaluma wa fani nyingine za kimaisha, wote hawa wakishirikiana katika mchakato mzima wa kubainisha ‘Hukmu za kishereia’ katika kadhia mbalimbali zinazowahusu waislamu duniani kote. Kulifanikisha hili ‘Kongamano’ limekua likiandaa katika miongo minne (miaka 40) iliyopita jumla ya vikao 25 vya kielimu na kiutafiti vikiwashirikisha wasomi na wataalamu waliobobea katika fani za sharia na za fiqhi na za maisha, kwa pamoja wameweza kutoa ‘Maamuzi na Maazimio’ yapatayo 255 katika masuala yahusuyo mali, fedha, biashara, familia, mambo ya wanawake na watoto na kadhia nyenginezo zihusuzo mambo ya mitazamo ya kifikra, ulezi, mitaala, utamaduni na masuala ya kijamii na ya kisiasa.

Kwa shauku iliopo ya kuwawezesha umma, kupitia nchi zao, taasisi na kupitia kwa raia wa kawaida, kuweza kuyapata ‘Maamuzi’ haya maridhawa na ‘Maazimio’ yaliyofikiwa kiuweledi, hivyo basi ‘Sekreterieti’ ya makao makuu ya ‘Kongamano’ ina furaha kukuleteeni nyote; maulamaa, wanazuoni, wana-fiqihi, wana-fikra, na wana-taaluma wa fani mbalimbali duniani kote; kukuleteei toleo (chapisho) hili jipya lililohakikiwa ambalo limekusanya ‘Maamuzi na Maazimio’ yote kuanzia kikao cha kwanza (1) hadi kikao cha ishirini na tano (25) cha mwisho (1405 – 1444H / 1984 – 2023). Ijulikane pia kwamba toleo la mwisho kabla ya hili, lilitolewa mnamo mwaka 1432H/2011, na lilikua limekusanya ‘Maamuzi na Maazimio’ mia moja na themanini na tano (185) pekee kipindi hicho, lakini toleo hili, kwa taufiq ya Allah, limeweza kukusanya ‘Maamuzi na Maazimio’ mia mbili na hamsini na tano (255).

Toleo hili limebahatika kupata mapitio ya kiuhakiki ya kina kupitia kamati weledi ya kielimu iliyoundwa kwa kazi hiyo chini ya usimamiziwa Dr. Abdulqahir Muhammad Ahmad Qamar ambae ni Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Fatwa na rejea za kifiqhi, akisaidiwa na Dr. Muhammad Mustafa Ahmad Shuayb, Mkuu wa kitengo cha utafiti na fatwa, aidha akisaidiwa Ustadh Khalid Hussein Jerbiyn, Mkuu wa kitengo cha uchapishaji, Allah awalipe wote malipo mema kwa niaba yetu a kwa niaba ya ‘Kongamano’.

Hapa napenda kutumia fursa hii adhimu kuwapa bishara njema ma-ulamaa na ma-fuqahaa na wataalamu wote kwamba tumeshamaliza kutafsiri ‘Maazimio na Maamuzi’ haya kwenye lugha za Kiingereza na Kifaransa ili kuwawezesha watumiaji wa lugha hizi na wasioelewa Kiarabu, lakini pia, kwa fadhla zake Allah, kazi hivi sasa inaendelea kuyatafsiri haya ‘Maazimio na Maamuzi’ kwenye lugha muhimu zinazotumiwa na waislamu katika mabara ya Afrika, Asia Uropa (Ulaya), tafsiri hizo zinatarajiwa kua tayari mda usiokua mrefu ili faidi ipate kuenea zaidi.

Kuhitimisha utangulizi huu napenda kutoa, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wajumbe na wataalamu wa ‘Kongamano’, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa na heshima kubwa pamoja na kutambua ukarimu mkubwa wa ‘Khadimul Haramain al-Sharifayn’ Mfalme Salman ibn Abdulaziz Aal-Saud (Allah ampe nguvu) na naibu wake muaminifu muheshimiwa Muhammad ibn Salman ibn Abdulaziz Aal-Saud (Allah amuhifadhi) kwa yote wanayofanyia ‘Kongamano’, tunamuomba Allah awalipe malipo mem ana aizidishie Dola hii ya Saudia na dola zote za kiislamu wanachama wa ‘Kongamano’ Allah azizidishie nchi hizi amani, utulivu na maendeleo.

Ni furaha kubwa kwangu mimi kutoa shukrani za dhati kwa Mstahiki Katibu Mkuu wa ‘Shirika la Ushirikiano wa Kiislamu’ ndugu yangu mpendwa Dr. Yusuf Bin Ahmad al-Uthaymeen kwa nafasi maalum alioipatia ‘Kongamano’ na msukumo anaotupatia katika utekelezaji wa shughuli zake.

Pia napenda kutumia fursa hii kumimina shukrani za moyoni kwa Mstahiki Sheikh Dr. Swaleh ibn Abdalla ibn Humeid Mkurugenzi wa Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu’ (KKFK), Mshauri katika ikulu ya kifalme, Saudia, Mjumbe wa ‘Jopo la Wanazuoni Wakuu’ wa Saudia na Imam na khatibu wa Masjid al-Haram, Makkah; kwa ushauri wake wa busara na maelekezo yake ya hekima na msukumo wake wenye tija, tunamuombea Allah amlipe malipo mema na amlinde na kumhifadhi azidi kutumikia uislamu na waislamu.

Mwisho kabisa tunainua mikono yetu na kumuomba mola wetu awalipe, kwa niaba yetu na kwa niaba ya ‘Kongamano’ na kwa niaba ya umma, awalipe ma-fuqahaa wetu na wanazuoni wetu watukufu waliojitolea umri

wao na elimu yao kutumikia ‘Kongamano’ kufikisha huduma zake kwa umma, miongoni mwa hawa wanazuoni ni kama wafuatao:

- Sheikh Dr. Bakar Abuzayd aliekua Mkurugenzi wa ‘Kongamano’, (Rahimahullah).
- Sheikh Dr. Muhammad al-Habib Balkhoja aliekua Katibu Mkuu wa ‘Kongamano’.
- Sheikh Dr. Abdulsalam al-Abbadi aliekua Katibu Mkuu wa ‘Kongamano’.
- Mstahiki Sheikh Muhammad Ali al-Tiskheeri, Mjumbe wa ‘Kongamano’.
- Mstahiki Sheikh Muhammad Mukhtar al-Salaami, Mjumbe wa ‘Kongamano’.
- Mstahiki Sheikh Dr. Abdulsattar Abughuddah, Mjumbe wa ‘Kongamano’.
- Sheikh Anas Abdulnoor Kalisa, Mjumbe wa ‘Kongamano’.
- Sheikh Dr. Wahbah al-Zuhaili, Mjumbe wa ‘Kongamano’.
- Profesa Dr. Muhammad Abdulhalim, Katibu Mkuu wa zamani wa ‘Shirikisho la Vyuo Vikuu vya Kiislamu’ na pia Mtaalamu wa ‘Kongamano’.
- Profesa Dr. Muhammad Abdulhalim Omar, Mtaalamu wa ‘Kongamano’.

Orodha ni ndefu, wote hawa na wengineo, tunamuomba Allah awataqabalie na awaweke maweko mema pamoja na manabii na wakweli na mashahidi na watu wema peponi.

Shukrani zetu nyingi ziwafikie Sheikh Dr. Ahmad Khalid Baabikr Katibu Mkuu wa zamani wa ‘Kongamano’, na wafanyakazi wote wa ‘Kongamano’ wakurugenzi wa idara na wakuu wa vitengo na wafanyakazi wengine wote kwa utiifu wao na utumishi wao kwa umma na kwa ‘Kongamano’.

Sala na salamu na ziada ya barka zimfikie bwana wetu Mtume Muhammad SAW na pia ziwafikie Aali zake na Maswahaba wake.

Sheikh Dr. Qutub Mustafa Sanu

Katibu Mkuu wa Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu’ (KKFK)

Utangulizi fasili juu ya ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu’ (KKFK)

‘Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu’ (KKFK) ni chombo cha kielimu cha kimataifa kilichozalikana na ‘Jumuia ya Ushirikiano wa Kiislamu’ (JUK), chombo hiki kilianzishwa huko Makkah kupitia ‘azimio’ la ‘kikao kilele’ cha tatu cha ‘Jumuia’ (Kumbukumbu: 8/3 – TH (Q.A) kilichofanyika tarehe 19 – 22 Mfungo sita (Rabiul-awal), 1401H sawa na tarehe 25 – 28 Januari, 1981, katika makao yake makuu yaliyopo Jeddah, Saudi Arabia, chombo hiki kina ‘Utu wake wa Kisheria’ na wajumbe wake ni ‘wanafiqhi’, wanazuoni, wataalamu na wanafikra katika nyanja mbalimbali za kifiqhi, kiutamaduni, kimalezi, kisayansi, kiuchumi na kijamii kutoka pembe zote za ulimwengu wa kiislamu, chombo hiki, kiko huru katika uendeshaji wa shughuli zake za ‘Kubainisha Hukumu za Kisheria’ katika kadhia mpya zinazoibuka na zinazowahusu waislamu duniani kote kwa mujibu wa msingi wa Qur’ani na Sunna za Bwana Mtume Muhammad SAW, pia chombo hiki kinajihusisha na tafiti zinazohusiana na matatizo ya maisha ya kileo na kuyatafutia ufumbuzi kwa kutumia misingi ya ‘ijtihad’ inayotokana na turathi ya kiislamu iliyobobea kwenye fikra endelevu ya kiislamu.

Katika kipindi cha miongo minne (miaka 40) sasa, na kwa taufiki yake Allah, ‘Kongamano’ limeweza kuandaa vikao ishirini nan ne (24) vya kielimu, kupitia vikao hivyo pameweza kutolewa ‘Maamuzi na Maazimio mia mbili na thelathini na nane (238) katika kadhia mbalimbali zilizoibuka na mambo mapya yaliyozuka.

Maono

‘Kongamano’ linatazamia liwe ni ‘Chombo Rejea cha kwanza duniani katika mas’ala mbalimbali ya kifiqhi kitakachokua ni kimbilio la nchi za kiislamu na jamii za kiislamu kote duniani kwa minajili ya kupata ufumbuzi na ubainifu wa hukumu mbalimbali za kisheria juu ya matatizo yanayoibuka kutokana na maisha ya kisasa kwa kutumia misingi ya Qur’an tukufu na Sunna za Bwana Mtume SAW na turathi bobezi ya kiislamu.

Risala

Risala ya Kongamano imejikita katika kuielezea sharia ya kiislamu kwa njia iliyo sahihi na nyepesi pamoja na kudhihirisha uwezo wake katika utatuzi na ufumbuzi wa matatizo ya maisha ya kisasa, na pia kubainisha uwezo wake katika kumletea binadamu maisha ya furaha, utulivu na amani hapa duniani na mpaka kesho akhera, yote haya yanaelezwa kwa mujibu wa ufahamu jumuishi ulio mpana na uliokamilika wa misingi ya dini ya kiislamu na nyenzo zake na makusudio yake makuu na hukmu zake.

Maadili

Msimamo wa katinakati (wasatiya)	Nidhamu
Insafu	Ushirikiano
Uadilifu	Uwazi
Ubunifu	Uzalishaji
Ubora wa viwango	Utekelezaji

Malengo

1) Kuleta karibu na kukutanisha viongozi wa fikra na wanafiqhi wa madhehebu mbalimbali yanayojulikana na wataalamu katika nyanja za elimu binadamu na sayansi jamii; wote pamoja kwa lengo la kubainisha msimamo wa kisheria katika matatizo yanayoibuka kutokana na maisha ya kisasa.
2) Kutoa rai za ksiheria na kuzitafsiri kwenye lugha nyingine katika maudhui mbalimbali zinaohusiana na maisha halisi ya watu na kwa namna ambayo itakua ni wepesi uwasilishwaji na utumiaji wa rai kama hizo ili watu wafaidike katika kuboresha sheria na kanuni za nchi zao na ambazo zitawafikiana na hukumu za sharia ya kiislamu.
3) Kshajiisha ijtihadi ya pamoja katika kadhia zinazoibka kutokana na maisha ya kisasa na matatizo yake, na uwezekano wa kuchagua na kutumia rai za kifiqhi zinazozingatia maslahi ya waislamu mmoja mmoja na jamii na nchi kwa jumla kwa mujibu wa makusudioi makuu ya sharia.

4) Kujieka mbali na mivutano ya kimadhehebu na uhupaji mipaka katika dini na kuwakufurisha wafuasi wa madhehebu mengine, na badala yake kukumbatia roho ya wasatia (ukatinakati), kufunguka kwa wengine na kusameheana na wafuasi wa madhehebu mengine ya kiislamu.
5) Kuzifanyia raddi (kubainisha) fatwa zilizotolewa zinazoendana kinyume na misingi thabiti ya dini na zinzokinzana na taratibu ziliokubalika za ijtihadi.
6) Kuandaa mazingira na mifumo ya 'fatwa' kwa jamii za kiislamu zinazoishi katika nchi zisiokua za kiislamu kwa namna ambayo italinda maadili ya kiislamu na utamaduni wake pamoja na kuhifadhi utambulisho wa waislamu hawa ugenini bila kuvuruga nidhamu na sheria za nchi hizo.
7) Kushajiisha ushirikiano na mshikamano wa wanazuoni wa madhehebu tofauti ili wawe kitu kimoja katika yale mambo ya misingi ya dini na kendelea kuheshimiana katika zile tofauti zao ndogo ndogo pamoja na kuzingatia taratibu na adabu za kukhitalifiana na umuhimu wa kuchukua rai za madhehebu mengine wwakati wa kutayarisha fatwa na maamuzi ya kisheria.
8) Kuzishirikisha taasisi za fatwa zilizopo ndani na nje ya nchi za kiislamu ili kuepuka ukinzani na mgongano wa rai katika kadhia husika hasa kwenye mas'ala yanayogusa watu wengi duniani.
9) Kuikuza 'fiqhi ya kiislamu' kwa kuitanua wigo wake na kuiendeleza pamoja na kuzingatia vidhibiti vya utohoaji na misingi ya utumiaji wa dalili kufikia makusudio ya sharia.
10) Kujihusisha na midahalo chanya na wafuasi wa dini na tamaduni nyenginezo kwa lengo la kujenga ufahamu na maingiliano kwa faida ya jamii ya kibinadamu.

Njia (mbinu):

1) Utoaji wa 'fatwa' katika kadhia kubwa zinazogusa waislamu duniani pamoja na kuzitafsiri kwenye lugha mbalimbali na kuzisambaza kwa wingi pamoja na kuzingatia mfumo (manhaj) wa ukatinakati unaowahifadhi waislamu dhidi ya kupindukia kwenye fikra potofu.
2) Kuandaa makongamano na warsha mahsusi kujadili kadhia-ainishwa

au kujadili maudhui zenye ncha nyingi zinazohitaji tafiti za kina.

3) Kutoa ‘rai ya kisheria’ juu ya nyaraka na stakabadhi rasmi zinazotolewa na ‘Taasisi ya Ushirikiano wa Kiislamu (TUK)’ na taasisi nyingine za kiislamu za kimataifa kila inapohitajika kufanya hivyo.
4) Kuorodhesha taasisi na makongamano ya kifiqhi yanayojihusisha na utoaji wa fatwa ndani na nje ya nchi za kiislamu kwa lengo la kua na mawasiliano mazuri na ushirikiano wa karibu baina ya ‘Kongamano’ na taasisi-tajwa.
5) Kuanzisha vituo vya stadi na utafiti wa kiislamu katika nchi nyeti zilizopo nje ya ulimwengu wa kiislamu na kua na mashirikiano ya karibu na vituo vilivyopo kufikia malengo ya ‘Kongamano’, na ufuatiliaji wa karibu wa machapisho hasi na chanya yanayohusiana na uislamu na kuandaa majibu ya kielimu dhidi ya machapisho mikanganyiko.
6) Kutoa machapisho ya ensaiklopidia ya kifiqhi (kwa lugha tatu) yaliyowepesishwa yatakayoangazia kadhia mbalimbali za wakati wa sasa katika nyanja mbalimbali za maisha. Machapisho haya yataandikwa kwa lugha nyepesi kwa watumiaji wa sekta ya habari na utamaduni.
7) Kushajiisha utafiti mkakamavu wa kifiqhi kupitia vitengo na kamati za ‘Kongamano’ na kwa ushirikiano na vyuo vikuu na taasisi nyengine za kielimu zinazojihusisha na changamoto za maisha ya kisasa na matatizo yake.
8) Kuandaa miswada-elekezi ya sheria (kwa lugha tatu) itakayoangazia maeneo na nyanja mbalimbali za maisha ambazo zinahitaji kutungiwa sheria; pamoja na kuzingatia tofauti za kimadhehebu zilizopo, miswaada hii baadae itafsiriwe kwa lugha mbalimbali na isambazwe katika nchi za kiislamu ili iwe rahisi na wepesi kwa wanaohitaji dondoo na rejea au marekebisho ya sheria ya nchi zao.
9) Kuhuisha turathi ya fiqhi ya kiislamu na kuenzi vitabu tulivyoachiwa katika fani za: Misingi ya Fiqhi (*Usul al-Fiqh*), Makusudio ya Sharia (*Maqaasid al-Shari’ah*), Fiqh-linganishi (*al-Fiqh al-Muqaaran*) na kusaidia kuchapisha na kusambaza vitabu ambavyo bado havijafanyiwa hivyo lakini baada ya kuvifanyia kazi ya uhakiki kisha kuvitafsiri katika lugha nyenginezo muhimu ulimwenguni.

10) Kuandaa Kamusi Jumuishi (kwa lugha tatu) la misamiati ya ki-fiqhi na ya ki-usuli na kila msamiati upate maelezo bainifu na yakinifu na kwa kutumia lugha nyepesi.
11) Kusambaza kazi zote za ‘Kongamano’ pamoja na maamuzi yake na fatwa zake na tafiti muhimu zinazotangulizwa na watafiti katika machapisho na mitandao ya intaneti ya ‘Kongamano’ pamoja kisha kuzitafsiri katika lugha nyenginezo muhimu ulimwenguni.
12) Kutafuta usaidizi kutoka kwa wataalamu wabobezi na walio bingwa katika fani zao ili wasaidie katika kazi za ki-utafiti wa maudhui zinazoletwa kwenye ‘Kongamano’.

Idara na vitengo

Muundo wa Sekretarieti Kuu ya ‘Kongamano’ umegawika katika idara na vitengo vifuatavyo:

a) Idara ya mambo ya Diwani na Itifaki; chini yake mna vitengo vitatu:
   - Kitengo cha Itifaki.
   - Kitengo cha mambo ya familia, wanawake, watoto na wazee.
   - Kitengo cha tafsiri (tarjama).
b) Idara ya Mipango na Ushirikiano wa Kimataifa; chini yake mna vitengo vitatu:
   - Kitengo cha Mipango na Ubunifu.
   - Kitengo cha Ushirikiano wa Kimataifa na Mahusiano ya Nje.
   - Kitengo cha Rekodi, Ufuatiliaji na Kutathmini.
c) Idara ya Mambo ya Fedha na Utawala; chini yake mna vitengo vitatu:
   - Kitengo cha Mambo ya Utawala na Mafunzo.
   - Kitengo cha Mambo ya Fedha na Uhasibu.
   - Kitengo cha Stoo na Maktaba.
d) Idara ya Uenezaji, Mahusiano ya Nje na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA); chini yake mna vitengo vitatu:
   - Kitengo cha Uenezaji.
   - Kitengo cha Mahusiano ya Nje.
   - Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).
e) Idara ya Mambo ya Ugharamiaji, Uwekezaji na Miradi; chini yake mna vitengo vitatu:

- Kitengo cha Mambo ya Waqfu.
- Kitengo cha Fedha na Uwekezaji.
- Kitengo cha Miradi.

f) Idara ya Utafiti, Fatwa, Makamusi na Machapisho; chini yake mna vitengo vitatu:
   - Kitengo cha Utafiti na Makamusi.
   - Kitengo cha Fatwa.
   - Kitengo cha Uchapishaji na Uenezaji.

g) Idara ya Mafuzo, Warsha na Makongamano; chini yake mna vitengo vitatu:
   - Kitengo cha Mafunzo.
   - Kitengo cha Warsha na Makongamano.
   - Kitengo cha Mihadhara.

Maamuzi na Maazimio ya Kikao cha Kwanza (1)[1]

Maamuzi ya Kuasisi na Kupangilia

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)
Makkah al-Mukarramah, Falme ya Saudi Arabia
26 – 29 Mfungo Tano (Swafar), 1405
19 – 22 Novemba, 1984

[1] Kikao cha kwanza: Maamuzi ya kikao hichi ni ya kuratibu na kupangilia, kwa hio mtiririko wake hauhusiani na mtiririko wa maamuzi na maazimio yanayoanza kwenye kikao cha pili na kuendelea.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 1

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu katika kikao chake cha kwanza (1) kilichofanyika mji Mtukufu wa Makkah al-Mukarramah kuanzia tarehe 26 – 29 Mwezi wa Mfungo Tano, (Swafar) 1405 sawa na tarehe 19 – 22 Novemba, 1984.

Baada ya kupitia ripoti iliyowasilishwa na kitengo cha 'Mipangilio' pamoja na maudhui-msingi na mapendekezo yake kwenye ripoti hiyo;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Kufanya tafiti juu ya 'Mas'ala mapya' na matukio-ibuka kwa mtazamo unaoambatana na nguvu ya 'dalili ya kisharia', kwa minajili ya kufikia makusudio makuu ya kisharia yanayotambulika, kwa lengo la kuwepesisha na kuondosha uzito kwa mujibu wa misingi ya kisharia na vidhibiti vyake vikuu.

2) Kufaidika na matokeo (natija) ya tafiti na durusu za uhakika za madhehebu mbalimbali ya kifiqhi, na kuhakikisha kua maoni ya kimadhehebu yanachukuliwa kutoka kwenye nyenzo-asilia na vitabu vinavyotegemewa kwenye madhehebu husika.

3) Uandaaji wa tafiti na durusu uzingatie:

    a) Uhalisia wa mambo.
    b) Kutumia 'Ijtihadi' iliyojikita kwenye misingi ya kisharia inayoambatana na makusudio na maslahi makuu ya kisharia.
    c) Utumiaji wa mfumo wa 'Fiqh-linganishi' kwenye tafiti na kadhia zinazodurusiwa.
    d) Kujilazimisha kua na insafu na kutopendelea upande mmoja.
    e) Kujipamba na usamehevu kwenye 'mas'ala ya ikhtilafu', maamuzi yatatolewa kwa kuzingatia wingi wa maoni pamoja kuheshimu mtazamo wa anaepingana na maoni husika.
    f) Maoni-pendekezi na tafiti zijikite kwenye 'dalili sahihi' zinazotokana na misingi ya kiislamu na utamaduni wake, aidha 'hadithi'

zinazotumika kama dalili ziwe zimepekuliwa kwa mujibu wa misingi ya upekuzi (takhrij) unaokubalika ili kuthibitisha usahihi wake.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 2

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu katika kikao chake cha kwanza (1) kilichofanyika mji Mtukufu wa Makkah al-Mukarramah kuanzia tarehe 26 – 29 Mwezi wa Mfungo Tano, (Swafar) 1405 sawa na tarehe 19 – 22 Novemba, 1984.

Baada ya kupitia ripoti iliyowasilishwa na kitengo cha 'Mipangilio' pamoja na maudhui-msingi na mapendekezo yake kwenye ripoti hiyo;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Ufuatiliaji wa tekniki na utungaji wa Sharia za Kiislamu na miradi ya uandikaji wa 'Hukmu za Sharia za Kiislamu' katika nchi yoyote miongoni mwa nchi za Kiislamu ili kujitayarisha kuzipangilia hukmu hizo katika mfumo na mtungo wa kikanuni na vifungu vya kisharia ili kuwepesisha rejea.

2) Kuainisha upaumbele wakati wa uandaaji wa tafiti na durusu uwe katika maudhui yafuatayo:

    a. Mbinu za ufundishaji wa Fiqhi ya Kiislamu na mitaala yake.
    b. Kuifanyisha kazi 'dhana ya Ijtihadi' katika jamii ya kisasa ya kiislamu.
    c. Mifumo ya hukumu na uadilifu katika uislamu.
    d. Kampuni za biashara za kisasa na nyanja zake.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 3

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu katika kikao chake cha kwanza (1) kilichofanyika mji Mtukufu wa Makkah al-Mukarramah kuanzia tarehe 26 – 29 Mwezi wa Mfungo Tano, (Swafar) 1405 sawa na tarehe 19 – 22 Novemba, 1984.

Baada ya kupitia ripoti iliyowasilishwa na kitengo cha 'Mipangilio' pamoja na maudhui-msingi na mapendekezo yake kwenye ripoti hiyo;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Kwa muktadha wa kazi zetu; neno: 'fatwa' linamaanisha maoni mbalimbali yanayoshughulisha akili za umma wa kiislamu yanayohusiana na matatizo yanayoibuka na kuyawasilisha matatizo hayo kwa 'Kongamano' ili yapatiwe ufumbuzi.

2) Kuwepesisha upatikanaji wa elimu ya fiqhi kwa kutumia taratibu zifuatazo:

    a. **Istilahi za kifiqhi:**
        i. Kufaidi kutokana na tajriba zilizotangulia katika kubuni istilahi za kifiqhi na kusaidia usambazaji wa istilahi hizo.
        ii. Kuzipitia zilizopo na kuziboresha
    b. **Saiklopidia za kifiqhi:**
        i. Kuzipitia zilizopo na kurekebisha zinazostahiki kurekebishwa au kukamilisha zinazolazimu kukamilishwa.
        ii. Kushajiisha na kuweka msukumo juu ya miradi ya saiklopidia.
        iii. Kuziimarisha Zaidi kwa kuziwekea 'dalili za kisharia' zinazokubalika.
    c. **Kusambaza vitabu vya kifiqhi:**
        i. Kwa kuandaa orodha ya uhariri na uhakiki wa miswada na vitabu-turathi vilivyopo kwenye maktaba mbalimbali duniani, ili kukijulisha kila kitabu ikiwa ni hatua ya awali ya kukianda uchapishaji wake inapohitajika.
        ii. Kuchapisha upya vitabu vya kifiqhi vinavyokubalika ambavyo vimeisha madukani.

d. **Kuandaa faharisi ya vitabu vya kifiqhi:** kwa kuweka mpangilio wa maudhui zake mbalimbali; jambo ambalo litarahisisha kufaidika navyo.

3) Utoaji wa fatwa ni jambo adhimu, hivyo basi kunahitajika uangalifu na umakini wa hali ya juu katika kuliendea suala hili na kuliwasilisha kwenye kitengo husika ili upekuzi wa kina ufanyike na hatimae fatwa inapotoka iwe inakidhi na kutatua matatizo yanayoikabili jamii ya kiislamu na hivyo kusaidia kuikuza jamii hio katika njia zilizo sahihi.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 4

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu katika kikao chake cha kwanza (1) kilichofanyika mji Mtukufu wa Makkah al-Mukarramah kuanzia tarehe 26 – 29 Mwezi wa Mfungo Tano, (Swafar) 1405 sawa na tarehe 19 – 22 Novemba, 1984.

Imechukuwa maamuzi ya kinidhamu yafuatayo:

1) Kumfawidhi 'Katibu Mkuu' wa 'Kongamano' kwa mda wa mwaka mmoja kuchagua wasomi, watafiti, wahakiki na wataalamu, aidha, kufaidi kutokana na orodha ya 'wasomi wabobezi katika fani za kielimu' iliyowasilishwa kwenye kikao cha 'Baraza'.

2) Kuwahusisha wanataaluma, taasisi na mashirika ya kielimu ili washirikiane nae katika baadhi ya shughuli zake; wakiwemo pia wawakilishi wa jamii za kiislamu katika nchi zisizokua za kiislamu; kwa mujibu wa kifungu cha saba (7) ibara ya pili (2) ya kanuni-msingi ya 'Kongamano'.:

   Kundi A: Wanataaluma

   - Sheikh Mustafa al-Zarqaa.
   - Sheikh Dr. al-Siddiq al-Dharir.
   - Dr. Muhammad Salam Madkour.
   - Sheikh Abdul-Razzaq Afifi.

   Kundi B: Taasisi na mashirika ya kielimu

   - Kongamano la Fiqhi la 'Jumuiya ya Ulimwengu wa Kiislamu (Raabita).
   - Saiklopidia ya Fiqhi Kuwait.
   - Kongamano la Tafiti za Kiislamu la Azhar – Misri.
   - Kongamano la Tafiti za Utamaduni wa Kiislamu (na Taasisi ya Aal al-Bait) – Jordan.

- Jumuiya ya Kiislamu ya Malezi, Sayansi na Utamaduni.
- Baraza la Fikra za Kiislamu – Islamabad, Pakistan.

Kundi C: Sheikh Twaha Jabir al-Alwani; aliependekezwa na Taasisi ya Kimataifa ya Fikra za Kiislamu (IIIT) – Washington, Amerika.

3) Vikao vya vitengo vilitakiwa kukutana kila baada ya miezi mitatu kitengo kimoja baada ya kingine, vikao vifanyike katika makao makuu ya ‘Kongamano’ Jeddah, kilele cha vikao hivi ni ‘Mkutano wa Baraza la Kongamano’ kweny kikao cha kawaida.
4) Wajumbe wa Ofisi ya Baraza wanatakiwa kukutana mara mbili kwa mwaka; kikao cha kwanza kifanyike ndani ya mwaka, na cha pili kifanyike kabla ya kikao cha kawaida cha ‘Baraza la Kongamano’.

Maamuzi na Maazimio ya Kikao cha Pili[1] ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Jeddah, Falme ya Saudi Arabia

10 – 16 Mfungo Saba (Rabii al-Thani), 1406

22 – 28 Disemba, 1985

[1] Maamuzi na Maazimio ya kikao cha kwanza yalikua ya ki-nidhamu na mipangilio.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 1 (1/2)[1]

Yanayohusiana na 'Zaka za Madeni'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha pili (2) kilichofanyika mji wa Jeddah tarehe 10 – 16 Mfungo saba (Rabii al-Thani) 1406 sawa na tarehe 22 – 28 Disemba 1985.

Baada ya kuzipitia tafiti zilizowasilishwa kwenye Kongamano zinazohusiana na **'Zaka za Madeni'**, na baada ya usikivu wa kina wa hoja zilizojadiliwa[2], yalibainika yafuatayo:-

- **Moja:** Hakuna dalili iliothibiti katika Qur'an au katika Sunna za Bwana Mtume SAW inayoelezea 'Zaka za Madeni' kwa uwazi kabisa.
- **Mbili:** Zimepokewa athari (dalili) mbalimbali kutoka kwa Maswahaba na Tabiun kuhusiana na 'Zaka za Madeni' lakini kila mmoja akiwa na mtazamo wake ni jinsi gani ya kutoa zaka za madeni.
- **Tatu:** Nayo madhehebu ya kiislamu wamekhitalifiana kuhusu suala hili la utoaji wa zaka za madeni kulingana na utofauti uliopatikana kwa maswahaba na tabiun.
- **Nne:** Kiini cha ikhtilaf hizo kimetokana na msingi unaosema: Je mali yanayotarajiwa kupatikana (kulipwa) yanapewa hukmu ya kua yameshapatikana (yameshalipwa)?

Hivyo basi; Kongamano limeamua yafuatayo:

- **Moja:** Mdai anapaswa kutoa zaka za madeni ifikapo mwaka iwapo mdaiwa wake ni mmiliki wa mali na ni mlipaji.
- **Mbili:** Mdai anapaswa kutoa zaka za madeni baada ya mzunguko wa mwaka iwapo mdaiwa wake amelemewa au ni mcheleweshaji wa kulipa.

---

[1] Tumeweka mtiririko wa nambari wa Maamuzi yote yaliyopitishwa kwenye vikao, aidha tumeweka nambari maalum ya kila kikao kwenye mabano, nambari ya kwanza ikiashiria Maamuzi na nambari ya pili ikiashiria Kikao

[2] Tizama tafiti hizi na mijadala yake katika Jarida la 'Kongamano' (Toleo: 2, Mjeledi: 1, Uk: 61).

Allah ni mjuzi zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 2 (2/2)

Yanayohusiana na 'Zaka za nyumba na ardhi iliokodishwa na isiokua ya kilimo'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha pili (2) kilichofanyika mji wa Jeddah tarehe 10 – 16 Mfungo saba (Rabii al-Thani) 1406 sawa na tarehe 22 – 28 Disemba 1985.

Baada ya kuzipitia tafiti zilizowasilishwa kwenye Kongamano zinazohusiana na '**Zaka za nyumba na ardhi iliokodishwa na isiokua ya kilimo**', na baada ya usikivu wa kina[2] wa hoja zilizojadiliwa, yalibainika yafuatayo:-

- Moja: Hakuna dalili ya wazi inayolazimisha utoaji wa zaka za nyumba na ardhi zilizokodishwa.
- Mbili: Hakuna dalili vilevile inayolazimisha utoaji wa haraka wa zaka za kodi za nyumba na ardhi iliokodishwa isiokua ya kilimo.

Hivyo basi; Kongamano limeamua yafuatayo:

- Zaka haijawajibika kwa nyumba na kwa ardhi ziliokodishwa.
- Lakini zaka itawajibika kwa kodi itakayopatikana ambayo ni asilimia 2.5 baada ya mzunguko wa mwaka pamoja na kuzingatia masharti na vigezo vya zaka.

Allah ni mjuzi zaidi

≃≃≃

[1] Kuhusu zaka za ardhi za kilimo tizama Maamuzi nambari 91 (13/2).

[2] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 2, Mjeledi 1, Ukurasa 115.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 3 (3/2)[1]

Yanayohusiana na 'Majibu ya masuali yaliyoletwa na Taasisi ya Kimataifa ya Fikra ya Kiislamu (TKFK) iliopo Washington'[2]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha pili (2) kilichofanyika mji wa Jeddah tarehe 10 – 16 Mfungo saba (Rabii al-Thani) 1406 sawa na tarehe 22 – 28 Disemba 1985.

Jopo la wajumbe wa 'Kongamano' liliundwa lifuatilie na kutoa majibu ya masuali yaliyoletwa na **Taasisi ya Kimataifa ya Fikra ya Kiislamu (TKFK) iliopo Washington.** Baada ya kupitia na kutizama kwa kina majibu yaliyotolewa yalibainika yafuatayo: -

- **Moja:** Majibu yaliyotolewa; yameandaliwa kwa muhtasari sana hayakidhi wala hayatoshelezi mahitajio ya muulizaji.
- **Mbili:** Imeonekana na 'Kongamano' kwamba ipo haja ya ufafanuzi wa ziada katika majibu yaliyotolewa ile kuondosha utata uliopo kwa ndugu zetu waislamu waishio nchi za magharibi.

Hivyo basi; Kongamano limeamua yafuatayo:

- **Moja:** Kuitaka Sekretarieti Kuu itafute wataalamu wabobezi ili waandae majibu bainifu yaliyotolewa hoja na yatakayoegemezwa na dalili za kisheria na fatwa za wanazuoni waliotangulia na kuyatoa majibu hayo katika njia maridhawa na ya kukinaisha.
- **Mbili:** Kuitaka Sekretarieti Kuu kuwasilisha majibu yatakayopatikana katika kikao cha tatu (3).[3]

Allah ni mjuzi zaidi

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 2, Mjeledi 1, Uk. 199, na toleo 3, Mjeledi 2, Uk. 1087).
[2] Taasisi hii inajuikana kama: International Institute of Islamic Thought (IIIT).
[3] Tizama Maamuzi nambari 23 (11/3)

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 4 (4/2)[1]

Yanayohusiana na 'Ukadiani'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha pili (2) kilichofanyika mji wa Jeddah tarehe 10 – 16 Mfungo saba (Rabii al-Thani) 1406 sawa na tarehe 22 – 28 Disemba 1985.

Baada ya kutizama suali lililoletwa kutoka 'Baraza la Fiqh ya Kiislamu la Capetown, Afrika Kusini kuhusiana na hukmu ya hili kundi la 'Ukadiani na kikundi kilichozalikana nacho kinachoitwa 'Lahorea' je; makundi haya ni miongoni mwa waislamu au la? Na iwapo asiekuwa muislamu anaweza kutoa hukumu juu ya kundi hili?

Kulingana na tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' katika maudhui haya; zilimtaja anaeitwa Mirza Ghulam Ahmad al-Qadiani alietokea huko India karne iliopita na ambae kwake yeye makundi haya ya 'Ukadiani' na la 'Lahorea' yananasibishwa nay eye kama muanzilishaji wake, na baada ya kupitia kwa umakini kabisa taarifa zinazohusiana na haya makundi mawili, na baada ya kujiridhisha kua huyu Mirza Ghulam Ahmad aliwahi kudai kwamba yeye ni mtume tena anaeteremshiwa wahyi, na madai yake haya ameyathibitisha mwenyewe katika baadhi ya vitabu alivyovitunga kwa kuendelea kudai kua baadhi ya yale aliyoyaandika vitabuni mwake ni wahyi anaoteremshiwa, aliendelea na madai yake haya umri wake wote bali na kuwataka wat una wafuasi wake wamuamini kua yeye ni mtume, aidha imethubutu kwa yakini kua aliendelea kupinga na kukanusha mambo ya msingi ya kiislamu kama kukanusha kwake uwepo wa 'jihad'.

Baada ya 'Konamano' hili pia kupitia fatwa iliotolewa na 'Kongamano la Fiqh la Makkah' (KFM) kuhusiana na maudhui haya;

Hivyo basi; Kongamano limeamua yafuatayo:

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 2, Mjeledi 1, Uk. 209).

Moja: Kwamba kile alichokidai Mirza Ghulam Ahmad kua yeye ni mtume anaeteremshiwa wahyi ni ukanushaji wa waziwazi wa misingi mikuu ya dini ya uislamu inayotutaka kuamini kwa Yakini kabisa kua Mtume Muhammad SAW ni mtume wa mwisho na hakuna mtume mweingine yeyote atakaekuja baada yake yeye, aidha hakuna binadamu mwingine yeyote baada yake yeye atakaeteremshiwa wahyi. Hivyo basi; kwa madai haya ya huyu Mirza Ghulam Ahmad na yeyote yule atakaewafikiana nae katika madai haya yanawafanya wawe ni 'Murtad' (waliotoka kwenye dini ya uislamu). Ama hili kundi lingine la 'Lahorea' nao pia ni 'Murtad' kama wenzao Makadiani, licha ya kwamba hawa ma'Lahorea' wanadai kua Mirza Ghulam Ahmad ni 'Kivuli' na 'Hudhuri' ya bwana wetu Mtume Muhammad SAW.

Mbili: Hairuhusiwi kwa mahakama yoyote isiokua ya kiislamu au hakimu (kadhi) yeyote asiekua muislamu kutoa hukmu yoyote juu ya hawa 'Makadiani' saw ani 'Waislamu' au ni 'Murtad' hususan katika jambo kama hili ambalo wanazuoni wa kiislamu na makongamano yao wameshapitisha 'Hukumu', kwani hukumu ya kua fulani ni Muislamu au ni murtad ni lazima hukumu kama hii itolewe na 'Waislamu kupitia wanazuoni wao na makongamano yao' wanaofahamu kiuhalisia maana ya kusema fulani ni Muislamu au fulani ni Murtad, pia wanaofahamu undani wa uislamu kwa kutumia Ushahidi wa Qur'an na wa Hadith na wa Itifaki (makubaliano, ijma) ya wanazuoni. Kwa hio hukumu iliotolewa na mahakama isiokua ya kiislamu katika hili ni 'batili'.

Allah ni mjuzi zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 5 (5/2)

Yanayohusiana na 'Watoto wa Chupa (Tube Babies)'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha pili (2) kilichofanyika mji wa Jeddah tarehe 10 – 16 Mfungo saba (Rabii al-Thani) 1406 sawa na tarehe 22 – 28 Disemba 1985.

Baada ya kuzipitia tafiti zilizowasilishwa kwenye Kongamano zinazohusiana na '**Watoto wa Chupa (Tube Babies)**', na baada ya usikivu wa kina[2] wa hoja zilizojadiliwa ambazo ziligusa nyanja za ki-fiqhi na za ki-tiba, yalibainika yafuatayo:-

- Maudhui hii bado inahitaji upekuzi mpana zaidi wa nyanja za ki-fiqhi na za ki-tiba.
- Ipo haja ya kufanya mapitio ya kina ya tafiti ziliopita ili kupata picha jumuishi ya nyanja zote.

Hivyo basi; Kongamano limeamua yafuatayo:

- **Moja:** Utoaji wa 'Hukmu' katika maudhui hii umeahirishwa hadi kikao kinachofuata cha 'Kongamano'.[3]
- **Mbili:** 'Kongamano' linamuomba na kumkalifisha Muheshimiwa Sheikh Dr. Bakar Abuzayd, Mkurugenzi wa 'Kongamano', kuandaa utafiti wa kina kwenye maudhui haya pamoja na kuzingatia Nyanja zote za ki-fiqhi na ki-tabibu.
- **Tatu:** Kuielekeza 'Sekretariati Kuu' kuwasilisha zile watakazopokea kwa wajumbe wote kwa uchache miezi mitatu kabla ya tarehe ya 'Kikao' kinachofuata.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 2, Mjeledi 1, Ukurasa 233.
[2] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 2, Mjeledi 1, Ukurasa 115.
[3] Tizama 'Maamuzi namba 16 (4/3).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 6 (6/2)

Yanayohusiana na 'Benki ya Maziwa (Milk Bank)'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha pili (2) kilichofanyika mji wa Jeddah tarehe 10 – 16 Mfungo saba (Rabii al-Thani) 1406 sawa na tarehe 22 – 28 Disemba 1985.

Baada ya kuzipitia tafiti zilizowasilishwa kwenye Kongamano zinazohusiana na '**Benki ya Maziwa (Milk Bank)**', na baada ya usikivu wa kina wa hoja zilizotokana na tafiti mbili zilizojadiliwa ambazo ziligusa nyanja za ki-fiqhi na za ki-tiba kuhusu 'Benki za Maziwa', yalibainika yafuatayo: -

- **Moja:** 'Benki za Maziwa' ni huduma iliyoanzishwa na watu wa Magharibi (Ulaya), kisha baada ya kipindi fulani zikadhihiri kasoro zake za kitaaluma na kisayansi na hilo likawapunguzia watu hamu ya zoezi hilo.
- **Mbili:** Uislamu unazingatia unyonyeshaji ni sawa na uhusiano wa damu; hivyo basi mtoto wa kunyonyeshwa ni sawa na mtoto wa damu, na katika malengo makuu ya Sharia ni 'kuhifadhi nasabu'. 'Benki za Maziwa' zinapelekea kuchanganyika kwa nasabu pasi na kujua muelekeo wa maziwa hayo na Watoto wanaonyonyeshwa nayo.
- **Tatu:** Mahusiano ya kijamii katika ulimwengu wa kiislamu yamejengeka katika mazingira ya kwamba anapozaliwa mtoto mweye mapungufu ya kimwili au udhaifu wa kiwiliwili au ambae anahitaji maziwa ya binadamu basi hua anapatiwa njia mbadala za kunyonyeshwa na asiekua mamake mzazi, hivyo basi inaondosha haja ya kuwepo kwa hizi 'Benki za Maziwa'.

Hivyo basi; Kongamano limeamua yafuatayo:

- **Moja:** Kuzuia uanzilishwaji wa 'Benki za Maziwa ya Kinamama' katika ulimwengu wa kiislamu.
- **Mbili:** Uharamu wa manyonyesho kupitia benki hizo za maziwa.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 2, Mjeledi 1, Ukurasa 383.

Allah ni mjuzi zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 7 (7/2)

Yanayohusiana na 'Vifaa vya Kurefusha Uhai (Life Support)'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha pili (2) kilichofanyika mji wa Jeddah tarehe 10 – 16 Mfungo saba (Rabii al-Thani) 1406 sawa na tarehe 22 – 28 Disemba 1985.

Baada ya kuzipitia tafiti za ki-fiqhi na za ki-utabibu zilizowasilishwa kwenye Kongamano zinazohusiana na '**Vifaa vya Kurefusha Uhai (Life Support)**', na baada ya usikivu wa kina wa hoja zilizotokana na tafiti husika zilizojadiliwa ambazo ziligusa nyanja za ki-fiqhi na za ki-tiba kuhusu 'Vifaa vya Kurefusha Uhai', kuliibuka masuala mengi yanayohusiana na uhai na umauti hasa ikizingatiwa kua endapo vifaa hivi vya kurefusha uhai vitaondolewa kwa mgonjwa basi uhai wake ndio unakatika; hata hivyo kulingana na kuwepo kwa janibu nyingi ambazo hazikua wazi katika suala hili, na kwa kua 'Taasisi ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' iliopo Kuwait iliandaa tafiti za kina kuhusiana na maudhui haya, basi ni vyema kuzirudia tafiti hizo.

Hivyo basi; Kongamano limeamua yafuatayo:

- **Moja:** Kuakhirisha 'Maamuzi' juu ya kadhia hii hadi pale kikao kijacho cha 'Kongamano'[2]
- **Mbili:** Kuielekeza 'Sekretariati Kuu' wakusanye 'tafiti na maamuzi' ya Taasisi ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' iliopo Kuwait na kuandaa majumuisho kwa muhtasari na kuwafikishia wajumbe wa 'Kongamano' kabla ya kikao kinachofuata.

Allah ni mjuzi zaidi

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 2, Mjeledi 1, Ukurasa 383.
[2] Tizama 'Maamuzi' namba 17 (5/3).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 8 (8/2)

Yanayohusiana na 'Masuali yaliyoletwa na Benki ya Kiislamu ya Maendeleo (Islamic Development Bank)'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha pili (2) kilichofanyika mji wa Jeddah tarehe 10 – 16 Mfungo saba (Rabii al-Thani) 1406 sawa na tarehe 22 – 28 Disemba 1985.

Baada ya usikivu makini wa 'Masuali' kadhaa yaliyoletwa na 'Benki ya Kiislamu ya Maendeleo' na kutaka 'Fatwa' juu ya masuali hayo, na baada ya kusikiliza ripoti ya kamati maalum ya wanazuoni iliyoundwa wakati wa kikao hiki ili watayarishe majibu ya kielimu yatakayopelekea upatikanaji wa 'Fatwa' ya masuali husika; imebainika kwamba masuali ya Benki ya Kiislamu ya Maendeleo bado yanahitaji ufuatiliaji wa karibu na mpana kwa kushirikiana na kamati maalum ya Benki hio iliyoundwa mahsusi kutafuta majibu ya masuali yao.

Hivyo basi; Kongamano limeamua yafuatayo:

- **Moja:** Kuakhirisha 'Maamuzi' juu ya kadhia hii hadi pale kikao kijacho cha 'Kongamano'[2]
- **Mbili:** Kuitaka 'Benki ya Kiislamu ya Maendeleo' ilete ripoti kupitia chombo chao cha 'Sharia'.

Allah ni mjuzi zaidi

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 2, Mjeledi 1, Ukurasa 383.
[2] Tizama 'Maamuzi' namba 13 (1/3).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 9 (9/2)

Yanayohusiana na 'Bima na Bima-Jumuishi (Insurance and reinsurance)'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha pili (2) kilichofanyika mji wa Jeddah tarehe 10 – 16 Mfungo saba (Rabii al-Thani) 1406 sawa na tarehe 22 – 28 Disemba 1985.

Baada ya kuzipitia tafiti zilizowasilishwa kwenye Kongamano zinazohusiana na '**Bima na Bima-Jumuishi (Insurance and reinsurance)**', na baada ya usikivu wa kina wa hoja zilizotokana na tafiti mbalimbali zilizojadiliwa ambazo ziligusa nyanja za bima na bima-jumuishi, na baada ya kujadili hoja ziliowasilishwa katika nyanja anuai na misingi ya bima na malengo yake; na baada ya kutizama 'Maamuzi' ya makongamano ya ki-fiqihi na taasisi za ki-elimu kwenye kadhia hii; imeamuliwa yafuatayo:-

- **Moja**: Mikataba ya bima ya biashara yenye malipo maalum (premium) ambayo ndio utaratibu unaotumiwa na makampuni ya bima; kua ni 'Mikataba yenye 'gharar' (udanganyifu) kubwa hali inayopelekea mkataba huu kufisidika kwa maana hio 'Mkataba aina hii ni Haramu'.
- **Mbili:** Mkataba mbadala wa bima unaoheshimu misingi ya miamala ya kiislamu ni 'Mkataba wa Bima ya Ushirikiano' uliojikita kwenye misingi ya kuchangia na kusaidia, na ndio hivyo hivyo pia kuhusiana na 'Bima Jumuishi' iliyokaa juu ya msingi wa 'Bima ya Ushirikiano'.
- **Tatu:** Kuzitaka nchi za Kiislamu kufanyia kazi maamuzi haya kwa kuanzisha 'Mashirika na Makampuni ya Bima ya Ushirikiano' na pia kuanzishwe 'Makampuni ya Bima Jumuishi' ili uchumi wa kiislamu upate kua huru na manyanyaso ya walafi lakini pia kutoenda kinyume na nidhamu (mfumo) tuliowekewa na Allah.

Allah ni Mjuzi zaidi

≋≋≋

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 2, Mjeledi 2, Ukurasa 545.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 10 (10/2)

Yanayohusiana na 'Kuamiliana na faida (riba) za benki na kuamiliana na benki za kiislamu'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha pili (2) kilichofanyika mji wa Jeddah tarehe 10 – 16 Mfungo saba (Rabii al-Thani) 1406 sawa na tarehe 22 – 28 Disemba 1985.

Baada ya kuzipitia tafiti zilizowasilishwa kwenye Kongamano zinazohusiana na **'Miamala ya Ki-Benki za Kisasa'**, na baada ya usikivu wa kina wa hoja zilizotokana na tafiti mbalimbali zilizojadiliwa ambazo zilielezea athari mbaya za miamala kama hii na jinsi inavyoathiri vibaya ukuaji na utulivu wa uchumi duniani hasa katika nchi za 'Ulimwengu wa Tatu', na baada ya kutaamali (kutathmini kwa kina) namna miamala hii ilivyovuruga na kuharibu uchumi wa dunia kwa kulikengeuka katazo la kutisha la Allah la kuharamisha 'miamala yote ya riba', kinyume chake ni kutangaza vita vya wazi baina ya 'Walaji riba' na Allah na Mtume wake.

Hivyo basi; Kongamano limeamua yafuatayo:

- **Moja:** Nyongeza yoyote au ziada juu ya deni lililofika wakati wake wa kulipwa lakini mdaiwa akashindwa kulipa hio nyongeza, au nyongeza yoyote juu ya mkopo inayotakiwa kulipwa mwanzo wa 'Mkataba wa Mkopo' basi aina mbili hizi tajwa ni 'Riba' iliyoharamishwa ki-sharia.
- **Mbili:** Mfumo mbadala unaohakikisha mzunguko wa pesa na kusaidia kutanashati kwa uchumi ni ule mfumo wa kiislamu ambao miamala inafanyika kwa mujibu wa hukumu za sharia.
- **Tatu:** 'Kongamano' limeamua kuzitaka nchi/serikali za kiislamu kushajiisha uwepo na uanzilishwaji wa Benki za Kiislamu zinazozingatia sharia na maadili ya kiislamu ili kukidhi mahitajio ya waislamu ya kupata miamala ya kibenki inayoendana na imani zao.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 2, Mjeledi 2, Ukurasa 735 na 813.

Allah ni Mjuzi zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 11 (11/2)

Yanayohusiana na 'Kuainisha siku itakayoanza (mwandamo wa) mwezi kwa kalenda ya hijriya'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha pili (2) kilichofanyika mji wa Jeddah tarehe 10 – 16 Mfungo saba (Rabii al-Thani) 1406 sawa na tarehe 22 – 28 Disemba 1985.

Baada ya kuzipitia tafiti zilizowasilishwa kwenye Kongamano zinazohusiana na '**Kuainisha siku itakayoanza (mwandamo wa) mwezi kwa kalenda ya hijriya**', na baada ya usikivu wa kina wa hoja zilizotokana na tafiti mbili zilizojadiliwa ambazo ziligusa nyanja za hesabu za ki-falaki zinazothibitisha kuingia kwa miezi ya hijriya; **'Kongamano' limeamua yafuatayo:**

- **Moja:** Kuielekeza 'Sekretariati Kuu' wakusanye 'tafiti za ki-elimu' zitakazoandaliwa na wataalamu waaminifu katika Nyanja za hesabu za ki-falaki na utabiri wa hali ya hewa.
- **Mbili:** Kui'ingiza maudhui hii ya 'Kuainisha siku itakayoanza (mwandamo wa) mwezi kwa kalenda ya hijriya' katika ajenda ya kikao kinachokuja ili kukamilisha maudhui haya katika pande zake mbili; ki-falaki na mahesabu yake na ki-fiqihi na ki-sharia.[2]
- **Tatu:** Kuielekeza 'Sekretariati Kuu' kuwaalika wanataaluma na wanafalaki wa kutosha waje washirikiane na wanafiqihi katika kuifikia picha kamili iliyo wazi katika maudhui haya itakayowawezesha kutoa 'Hukmu ya Sharia'.

Allah ndie Mwenye Kutuwafiqia

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 2, Mjeledi 2, Ukurasa 839.
[2] Tizama 'Maamuzi' namba 18 (6/3)

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 12 (12/2)

Yanayohusiana na 'Hati-Dhamana (*Letter of Guarantee*) ya Benki'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha pili (2) kilichofanyika mji wa Jeddah tarehe 10 – 16 Mfungo saba (Rabii al-Thani) 1406 sawa na tarehe 22 – 28 Disemba 1985.

Baada ya kuzipitia tafiti zilizowasilishwa kwenye Kongamano zinazohusiana na '**Hati-Dhamana ya Benki**', na baada ya usikivu wa kina wa hoja zilizotokana na tafiti mbalimbali zilizojadiliwa **yalibainika yafuatayo:**

- **Moja:** Hati-Dhamana ya Benki ya aina zake za kuanza na kumalizia ima zinadhaminiwa na rehani au bila kudhaminiwa, ikiwa haina dhamana yoyote bbasi maana yake ni kwamba: 'Dhima ya mdhamini imeunganishwa na dhima ya mwingine hivyo basi mdhamini anabeba dhima na dhamana kwa hali zote za yule aliemdhamini; na hii ndio inayoitwa katika fiqhi: 'Dhamana' au 'Kafala'. Ama ikiwa Hati-Dhamana imedhaminiwa na rehani basi hapa uhusiano baina ya Muombaji wa Hati-Dhamana na Mtoaji unakua ni uhusiano wa: 'Wakala'. Uwakala unasihi (unakubalika) kwa malipo au bila ya malipo pamoja na kuendelea uwepo wa uhusiano wa 'Dhamana' kwa faida ya Mdhaminiwa.
- **Mbili:** 'Kafala' ni Mkataba wa kuchangia wenye lengo la kurahisisha na kuwepesisha maisha kwa wengine. Wana-Fiqihi wamekubaliana kutosihi kuweka malipo kwa ajili ya 'Kafala' kwa sababu malipo kama haya yanafanana na nyongeza katika deni ambayo inapelekea muamala kua wa 'Riba' ni hio ni haramu.

Hivyo basi; Kongamano limeamua yafuatayo:

- **Moja:** Haijuzu (haifai) kuchukua malipo juu ya Hati-Dhamana kwa kuzingatia kiwango cha pesa zilizodhaminiwa na mda wake, ni sawa Hati-Dhaman hio ikiwa imedhaminiwa na rehani au la.
- **Mbili:** Inajzu (inafaa) kuchukua ada za ki-ofisi na ki-utawala kwa ajili ya

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 2, Mjeledi 2, Ukurasa 1035.

utowaji wa Hati-Dhamana wa aina zote mbili, hata hivyo malipo kama haya yanatakiwa yawe ni sawa na malipo ya huduma nyingine inayofanana na hii.

Allah ni Mjuzi zaidi

Maamuzi na Maazimio ya Kikao cha Tatu ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Amman, Falme ya Jordan

8 – 13 Mfungo Tano (Swafar), 1407

11 – 16 Oktoba, 1986

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 13 (1/3)

Yanayohusiana na 'Masuali yaliyoletwa na Benki ya Kiislamu ya Maendeleo (Islamic Development Bank)'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tatu (3) kilichofanyika mji wa amman, Falme ya Jordan kuanzia tarehe 8 – 13 Mwezi wa Mfungo Tano, (Swafar) 1407 sawa na tarehe 11 – 16 Oktoba, 1986.

Baada ya usikivu makini wa 'Masuali' yote yaliyoletwa na 'Benki ya Kiislamu ya Maendeleo' na baada ya uwasilishwaji wa tafiti zilizoandaliwa na upekuzi wa hoja zilizojadiliwa; **Kongamano limeamua yafuatayo:**

a) Kuhusiana na malipo ya huduma za mikopo ya Benki ya Kiislamu ya Maendeleo:

- **Moja:** Inajuzu (inafaa) kuchukua malipo ya huduma za mikopo kwa sharti yawe ni malipo muwafaka na huduma zinazotolewa.
- **Mbili:** Kila nyongeza ya malipo zaidi ya huduma zinazotolewa itakua ni haramu kwani inaingia katika 'Riba' ilioharamishwa.

b) Kuhusu miamala ya kukodisha:

- **Moja:** Ahadi inayotolewa na Benki ya Kiislamu ya Maendeleo (BKM - IDB) ya kwamba hawatokodisha vifaa kwa mteja ila baada ya kuvimiliki vifaa hivyo; ni jambo linalokubalika kisharia.
- **Mbili:** Wakala wa Benki ya Kiislamu ya Maendeleo aliepewa maagizo ya kununua vifaa fulani kwa minajili ya kumkodishia mteja wa BKM kwa sharti vifaa vyenyewe viwe vinajulikana na thamani yake pia iwe inajulikana na kwa sharti Wakala wa Benki awe amekabidhiwa vifaa hivyo; basi Uwakala kama huu unakubalika kisharia; na bora zaidi Wakala wa kununua asiwe ni Mteja

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 2, Mjeledi 2, Ukurasa 527, na Toleo 3, Mjeledi 1, Ukurasa 77.

anaekusudiwa kukodishwa vifaa hivyo.

- **Tatu:** Mkataba wa Ukodishaji ni lazima ufanyike baada ya Benki, au kupitia kwa Wakala wake, kuvimiliki vifaa hivyo.
- **Nne:** Ahadi ya kumpatia vifaa hivyo kama zawadi kwa Mkodishwaji baada ya 'Mda wa kukodisha' inakubalika lakini iwe kwenye mkataba maalum.
- **Tano:** Endapo kutatokea maharibiko au kasoro katika vifaa hivyo basi uwajibikaji wake utakua juu ya Benki kwa kua ndie mmiliki wa vifaa hivyo, ila ikigundulikana kwamba maharibiko hayo au kasoro hizo zimesababishwa na uzembe wa mkodishwaji basi ndie atakaewajibika.
- **Sita:** Malipo ya bima kwenye kampuni za kiislamu yatalipwa na Benki kwa kadri inavyowezekana.

c) Kuhusu miamala ya biashara ya kulipa polepole:

- **Moja:** Ahadi inayotolewa na Benki ya Kiislamu ya Maendeleo (BKM) ya kwamba hawatouza vifaa kwa mteja ila baada ya kuvimiliki vifaa hivyo; ni jambo linalokubalika kisharia.
- **Mbili:** Wakala wa Benki ya Kiislamu ya Maendeleo aliepewa maagizo ya kununua vifaa fulani kwa minajili ya kumuuzia mteja wa BKM kwa sharti vifaa vyenyewe viwe vinajulikana na thamani yake pia iwe inajulikana na kwa sharti Wakala wa Benki awe amekabidhiwa vifaa hivyo; basi Uwakala kama huu unakubalika kisharia; na bora zaidi Wakala wa kununua asiwe ni Mteja anaekusudiwa kuuziwa vifaa hivyo.
- **Tatu:** Mkataba wa Mauzo ni lazima ufanyike baada ya Benki, au kupitia kwa Wakala wake, kuvimiliki vifaa hivyo.

d) Kuhusu miamala ya kulipipia biashara ya nje:

Miamala hii inafuata taratibu zilizoekwa za miamala ya biashara ya kulipa polepole kwa awamu.

e) Kuhusu matumizi ya faida zinazotokana na akiba ambazo Benki ya Kiislamu ya Maendeleo inalazimika kuziweka kwenye benki za kigeni:

Ni haramu kwa benki kulinda thamani ya mali yake dhidi ya athari ya kutotulia kwa bei ya sarafu kwa kutmia faida zinazotokana na akiba. Faida hizo zinatakiwa zitumike kwenye kunufaisha umma katika nyanja mbalimbali kama vile, mafunzo, utafiti, misaada ya kibinadamu na ya dharura katika nchi wanachama na pia kutoa misaada ya kitaaluma kwa taasisi na vyuo mbalimbali vyenye malengo ya kuendeleza mbele elimu na maarifa katika jamii nan chi za kiislamu.

Allah ndie Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 14 (2/3)

Yanayohusiana na 'Zaka za hisa kwenye makampuni'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tatu (3) kilichofanyika mji wa amman, Falme ya Jordan kuanzia tarehe 8 – 13 Mwezi wa Mfungo Tano, (Swafar) 1407 sawa na tarehe 11 – 16 Oktoba, 1986.

Baada ya usikivu makini wa '**Zaka za hisa kwenye makampuni**' na baada ya uwasilishwaji wa tafiti zilizoandaliwa na upekuzi wa hoja zilizojadiliwa; **Kongamano limeamua yafuatayo:**

Kuakhirisha utoaji wa 'Maamuzi' hadi kikao cha nne cha 'Baraza'.[2]

Allah ndie Mwenye Kutuafiqia

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 4, Mjeledi 3, Ukurasa 705.
[2] Tizama 'Maamuzi' namba 28 (3/4).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 15 (3/3)

Yanayohusiana na 'Kuwekeza pesa za zaka kwenye miradi na kuwapa wastahiki wa zaka faida inayotokana na miradi hiyo'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tatu (3) kilichofanyika mji wa amman, Falme ya Jordan kuanzia tarehe 8 – 13 Mwezi wa Mfungo Tano, (Swafar) 1407 sawa na tarehe 11 – 16 Oktoba, 1986.

Baada ya usikivu makini wa '**Kuwekeza pesa za zaka kwenye miradi na kuwapa wastahiki wa zaka faida inayotokana na miradi hiyo**' na baada ya uwasilishwaji wa tafiti zilizoandaliwa na upekuzi wa hoja zilizojadiliwa;

Kongamano limeamua yafuatayo:

Kimsingi, inajuzu (inafaa) kuwekeza pesa za zaka katika miradi ya uzalishaji ambayo miradi hio inaishia kumilikishwa wastahiki wa zaka, au miradi hio iwe chini ya usimamizi wa 'taasisi za zaka' zilizosajiliwa kisheria ambazo zinajishughulisha na 'ukusanyaji na ugavi wa zaka' lakini miradi hio ya uwekezaji ifanyike baada ya kukidhi mahitajio ya msingi ya wastahiki-zaka, na pia miradi hio iwe imefanyiwa upembuzi yakinifu kuepusha hasara kwenye pesa za zaka.

Allah ni Mjuzi Zaidi

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 3, Mjeledi 1, Ukurasa 309.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 16 (4/3)

Yanayohusiana na 'Watoto wa Chupa (Tube Babies)'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tatu (3) kilichofanyika mji wa amman, Falme ya Jordan kuanzia tarehe 8 – 13 Mwezi wa Mfungo Tano (Swafar), 1407 sawa na tarehe 11 – 16 Oktoba, 1986.

Baada ya usikivu makini wa '**Watoto wa Chupa (Tube Babies)**' kutoka kwa wataalamu na wana-tiba, na baada ya uwasilishwaji wa tafiti zilizoandaliwa na upekuzi wa hoja zilizojadiliwa; **yalibainika yafuatayo:**

Kuna njia saba za upandaji wa mbegu za Watoto wa chupa zinazojulikana siku hizi;

Hivyo basi, Kongamano limeamua yafuatayo:

- **Moja:** Njia tano zinazofuata zimeharamishwa na zimekatazwa kabisa kwa sababu zinapelekea kuchanganyikana kwa nasaba na kupoteza hadhi ya umama zikiwemo na sababu nyenginezo zinazotahadharishwa:

    1) **Njia ya kwanza:** Ni kuchukua tone la manii ya mume na yai la mwanamke asiekua mke wake, kisha zinapandwa mbegu hizi kwenye uzao wa mke wake.
    2) **Njia ya pili:** Ni kuchukua tone la manii ya mwanamume asiekua mume na yai la mke, kisha zikachkuliwa na kupandikizwa ndani ya uzao wa mke.
    3) **Njia ya tatu:** Ni kuzichanganya nje mbegu za mume na mke, kisha zikachkuliwa na kupandikizwa ndani ya uzao wa mwanamke mwingine aliejitolea kubeba mimba.
    4) **Njia ya nne:** Ni kuchukua tone la manii ya mwanamume ajnabi na yai la mwanamke ajnabi vilevile, kisha zikapandikizwa mbegu hizi kwenye

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 3, Mjeledi 1, Ukurasa 423.

uzao wa mke wa mtu.

5) **Njia ya tano:** Ni kuchanganya nje tone la manii ya mume na yai la mke wake, kisha yakapandikizwa kweye uzao wa mke wake mwengine.

- **Mbili: Njia mbili ya sita na ya saba hamna tatizo kuzitumia ikitokea dharura ya kufanya hivyo lakini ni vyema tahadhari zote zikachukuliwa; nazo ni:**

6) **Njia ya sita:** Ni kuchukua tone la manii ya mume na yai la mke wake na kuchanganywa nje, kisha yapandikizwe ndani ya uzao wa mke.
7) **Njia ya saba:** Ni kuchukua mbegu za mume, kisha kuzipandikiza kwa njia ya mrija ndani ya uzao wa mke wake.

Allah ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 17 (5/3)

Yanayohusiana na 'Vifaa vya Kurefusha Uhai (Life Support)'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tatu (3) kilichofanyika mji wa amman, Falme ya Jordan kuanzia tarehe 8 – 13 Mwezi wa Mfungo Tano (Swafar), 1407 sawa na tarehe 11 – 16 Oktoba, 1986.

Baada ya usikivu makini wa '**Vifaa vya Kurefusha Uhai (Life Support)**' kutoka kwa wataalamu na wana-tiba, na baada ya uwasilishwaji wa tafiti zilizoandaliwa na upekuzi wa hoja zilizojadiliwa;

Hivyo basi, Kongamano limeamua yafuatayo:

Inazingatiwa kua mtu ameshakufa na hukmu zote za kisharia zinazotakiwa kufanyiwa maiti anafanyiwa iwapo kumebainika moja katika hali mbili:

- **Moja:** Yanaposimama mapigo ya moyo na zinaposimama pumzi, na daktari akathibitisha kua hapa ndio mwisho wa pumzi na mapigo ya moyo.
- **Mbili:** Zitakaposimama kazi zote za ubongo, na madaktari bingwa na wataalamu wakathibitisha kwamba ubongo huu hauna tena tamaa ya kuruudi kufanya kazi; bali unazidi kuzorota kuelekea kusimama kabisa.

Basi katika hali kama hii inaruhusika kuondosha 'vifaa vya kurefusha uhai' alvyoekewa mgonjwa hata kama baadhi ya viungo vyake kama vile moyo bado vinaendelea kufanya kazi kwa kuwezeshwa na vifaa hivyo.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 3, Mjeledi 2, Ukurasa 523.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 18 (6/3)

Yanayohusiana na 'Kuainisha siku itakayoanza (mwandamo wa) mwezi kwa kalenda ya hijriya'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tatu (3) kilichofanyika mji wa amman, Falme ya Jordan kuanzia tarehe 8 – 13 Mwezi wa Mfungo Tano (Swafar), 1407 sawa na tarehe 11 – 16 Oktoba, 1986.

Baada ya usikivu makini wa '**Kuainisha siku itakayoanza (mwandamo wa) mwezi kwa kalenda ya hijriya**' katika mas'ala mawili:

- **La kwanza:** Tofauti za 'matlai' na changamoto zake katika kuainisha mwandamo wa mwezi.
- **La pili:** Hukmu ya kuthibitisha mwandamo wa mwezi kwa kutumia hesabu za ki-falaki.

Baada ya uwasilishwaji wa tafiti zilizoandaliwa kutoka kwa wataalamu na baada ya upekuzi wa hoja zilizojadiliwa;

Hivyo basi, Kongamano limeamua yafuatayo:

- **Moja:** Utakapothibiti mwandamo wa mwezi katika mji fulani basi itawawajibikia waislamu popote walipo kuukubali mwandamo huo bila ya kuzingatia utofauti uliopo wa 'Matlai'; hii ni kwa mujibu wa agizo la kuwataka waislamu kufunga na kufungua kwa kuonekana kwa mwezi.
- **Mbili:** Ni lazima uthibitisho wa mwezi utegemee 'kuonekana kwake' hesabu za falaki na vifaa vya darubini vinaweza kutumika tu kama visaidizi; hii ni kwa kuzingatia Hadithi za Mtume SAW mbalimbali sambamba na elimu ya sayansi.

Allah ni Mjuzi Zaidi

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 3, Mjeledi 2, Ukurasa 811.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 19 (7/3)

Yanayohusiana na 'Kuhirimia ndegeni au melini kwa anaekusudia kutekeleza ibada ya hijja au umra'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tatu (3) kilichofanyika mji wa amman, Falme ya Jordan kuanzia tarehe 8 – 13 Mwezi wa Mfungo Tano (Swafar), 1407 sawa na tarehe 11 – 16 Oktoba, 1986.

Baada ya usikivu makini wa '**Kuhirimia ndegeni au melini kwa anaekusudia kutekeleza ibada ya hijja au umra**' na baada ya uwasilishwaji wa tafiti zilizoandaliwa na upekuzi wa hoja zilizojadiliwa;

Hivyo basi, Kongamano limeamua yafuatayo:

Mipaka-maeneo iliyoainishwa katika Sunna za Mtume SAW kwa minajili ya kuhirimia ni lazima ifuatwe kwa anaekusudia Hijja au Umra kwa anaepita kwenye mipaka hio kwa njia ya ardhini au angani au kwa njia ya bahari kwa mujibu wa Hadithi za Bwana Mtume SAW.

Allah ni Mjuzi Zaidi

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 3, Mjeledi 3, Ukurasa 1419.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 20 (8/3)

Yanayohusiana na 'Kutoa Zaka na kuwapatia Mfuko wa Shirika la 'Tadhaamun' la Ushirikiano wa Kiislamu'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tatu (3) kilichofanyika mji wa amman, Falme ya Jordan kuanzia tarehe 8 – 13 Mwezi wa Mfungo Tano (Swafar), 1407 sawa na tarehe 11 – 16 Oktoba, 1986.

Baada ya usikivu makini wa '**Kutoa Zaka na kuwapatia Mfuko wa Shirika la 'Tadhaamun' la Ushirikiano wa Kiislamu**' na baada ya uwasilishwaji wa maelezo bainifu kutoka kwa Katibu Mkuu Msaidizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa ya Kiislamu (OIC) kuhusiana na shughuli zinazosimamiwa na Mfuko wa Shirika la 'Tadhaamun' la Ushirikiano wa Kiislamu, na kuelezea kwamba 'Mfuko' unahitaji msukumo wa kifedha, amependekeza kua 'Mfuko' huo uzingatiwe kua sehemu ya wapokeaji wa zaka;

Hivyo basi, Kongamano limeamua yafuatayo:

Kuielekeza 'Sekretarieti Kuu' kusaidiana na 'Mfuko' wa Shirika la Tadhaamun la Kiislamu kuandaa tafiti ya dharura kuhusiana na ombi hili, na kuleta ripoti ya utafiti huo kwenye kikao kinachofuata cha 'Kongamano'.[1]

Allah Ndie Mwenye Kutuafikia

[1] Tizama 'Maamuzi' namba 27 (2/4).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 21 (9/3)

Yanayohusiana na 'Hukumu za fedha za noti na kubadilika kwa thamani ya sarafu'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tatu (3) kilichofanyika mji wa amman, Falme ya Jordan kuanzia tarehe 8 – 13 Mwezi wa Mfungo Tano (Swafar), 1407 sawa na tarehe 11 – 16 Oktoba, 1986.

Baada ya usikivu makini wa '**Hukumu za fedha za noti na kubadilika kwa thamani ya sarafu**' kutoka kwa wataalamu, na baada ya uwasilishwaji wa tafiti zilizoandaliwa na upekuzi wa hoja zilizojadiliwa;

Hivyo basi, Kongamano limeamua yafuatayo:

- **Moja:** Kuhusu hukumu za fedha za noti: Ni fedha zinazokubalika zenye thamani kamili, fedha hizi zinabeba hukmu zote za 'Dhahabu' na 'Fedha' zinazohusiana na hukumu za: Riba, Zaka, Madeni na hukumu nyenginezo.
- **Mbili:** Kuhusu kubadilika kwa thamani ya sarafu: Hukmu yake itatolewa kwenye kikao kijacho cha nne baada kuyatizama mas'ala haya kwa kina zaidi janibu zake zote.[2]

Allah Ndie Mwenye Kutuafikia

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 3, Mjeledi 3, Ukurasa 1650, na (Toleo 5, Mjeledi 3, Ukurasa 1609.

[2] Tizama 'Maamuzi' namba 42 (5/4)

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 22 (10/3)

Yanayohusiana na 'Hukumu za Hati za Mudhaaraba na Hati za Maendeleo na Uwekezaji'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tatu (3) kilichofanyika mji wa amman, Falme ya Jordan kuanzia tarehe 8 – 13 Mwezi wa Mfungo Tano (Swafar), 1407 sawa na tarehe 11 – 16 Oktoba, 1986.

Baada ya usikivu makini wa utafiti uliowasilishwa kuhusiana na '**Hukumu za Hati za Mudhaaraba na Hati za Maendeleo na Uwekezaji**' kutoka kwa wataalamu, na kwenda sambamba na mpangilio wa 'Kongamano' wa kupata tafiti kadhaa katika maudhui moja ili kuifahamu katika nyanja zake zote;

Hivyo basi, Kongamano limeamua yafuatayo:

Kuielekeza Sekretarieti Kuu kutafuta wataalamu katika maudhui hay ana kuwakalifisha waandae tafiti za kina, ripoti za tafiti hizo ziwasilishwe kwenye kikao cha nne kijacho, ili 'Kongamano' liweze kuchukua 'Maamuzi' makini na muwafaka.

Allah Ndie Mwenye Kutuafikia

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 4, Mjeledi 3, Ukurasa 1809.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 23 (11/3)[1]

Yanayohusiana na 'Masuali yaliyoletwa na Taasisi ya Kimataifa ya Fikra ya Kiislamu (TKFK) iliopo Washington'[2]'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tatu (3) kilichofanyika mji wa amman, Falme ya Jordan kuanzia tarehe 8 – 13 Mwezi wa Mfungo Tano (Swafar), 1407 sawa na tarehe 11 – 16 Oktoba, 1986.

Baada ya kuyapitia kwa makini '**Masuali yaliyoletwa na Taasisi ya Kimataifa ya Fikra ya Kiislamu (TKFK) iliopo Washington**' pamoja na 'Majibu' yaliyoandaliwa na wajumbe na wataalamu;

Hivyo basi, Kongamano limeamua yafuatayo:

Kuielekeza Sekretarieti Kuu kuwafikishia **'Taasisi'** kuhusu 'Maamuzi' na 'Majibu' yaliopitishwa.

Bismillah al-Rahman al-Raheem,

Sala na Salamu za Allah zimfikie Bwana wetu Mtume Muhammad SAW na Aali zake na Masahaba wake wote.

Majibu yaliyopitishwa na 'Kongamano' juu ya masuali ya 'Taasisi'[3]

Suali la tatu:

Nini Hukmu mwanamke wa kiislamu kuolewa na mwanamume asiekua muislamu akiwa na tamaa kwamba atasilimu baada ya kuowana, hasa ikizingatiwa kilio cha wanawake wengi wa kiislamu kua hawapati wanaume kufu nao, na hivyo kupelekea maisha yao kua mazito.

---

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 3, Mjeledi 2, Ukurasa 1087, na (Toleo 2, Mjeledi 1, Ukurasa 199.

[2] Taasisi hii inajuikana kama: International Institute of Islamic Thought (IIIT).

[3] Majibu ya masuali namba 1, 2, 7, 15 na 22 yatajibiwa baadae.

Jawabu:

Ndoa ya mwanamke wa kiislamu kuolewa na mwanamume asiekua muislamu hairuhusiwi kisheria kwa mujibu wa Qur'an, Hadith na Ijmaa ya wanazuoni. Na itakapofungwa ndoa kama hio basi inakua ni batili, na haitakua na athari zozote zitakazokubaliwa kutokana na ndoa hio, halikadhalika Watoto watakaozaliwa kwenye ndoa hio hawatakua ni Watoto wa halali. Kujenga matumaini kwamba mume huyu huenda akasilimu baada ya ndoa bado haijakua ni sababu tosha ya kubadilisha hukmu hii.

Suali la nne:

Nini hukmu ya kuendelea na ndoa ambapo mke amesilimu lakini mume bado hajasilimu hali ya kua wana Watoto tayari na anawaogopea Watoto wake kupotea akiwa mbali nao, pia ana tamaa kwamba huenda mume wake nae pia akasilimu ikiwa wataendelea na ndoa yao? Na ni ipi hukmu iwapo hana tamaa ya mumewe kusilimu lakini mumewe anakaa nae kwa uzuri na mapenzi, na anaogopa lau atamucha mume huyu huenda asipate mume muislamu?

Jawabu:

Anaposilimu mke; mume akakataa kusilimu basi ndoa yao inafusahika; na hawatarusiwa kuishi kama mume na mke, bali mke atawajibika kukaa 'eda', ndani ya kipindi cha eda akisilimu mume basi wanaendelea na ndoa yao, ama kipindi cha eda kikimalizika na mume bado hajasilimu basi uhusiano wao wa mume na mke unakatika. Endapo mume atasilimu baada ya hapo na wakataka kuendelea kuishi pamoja kama mume na mke basi watafunga ndoa upya.

Suali la tano:

Nini hukmu ya kumzika muislamu kwenye makaburi ya wasiokua waislamu, kwani huku haifai kuzika maiti nje ya sehemu zilizoandaliwa kwa shughuli hizo, na hakuna makaburi mahsusi ya waislamu katika sehemu nyingi za Amerika nan chi za Ulaya?

Jawabu:

Kuzika muislamu kwenye makaburi ya wasiokua waislamu katika nchi zisizokua

za kiislamu inajuzu kwa kipengele cha ‘dharura’.

Suali la sita:

Nini hukmu ya kuuza msikiti iwapo waislamu wa sehemu hio wanahama na wakaogopea msikiti huo ima kuharibika au kuchukuliwa na watu wengine? Kwani hutokea sana huku waislamu kununua nyumba kisha kuigeuza na kuifanya msikiti lakini panapotokea dharura ya waislamu kuhama sehemu hio basi msikiti huo unaatilika au unachukuliwa na watu wengine, inawezekana kuuza au kubadilisha sehemu hio na kupata sehemu nyingine kunakopatikana waislamu. Jee nnini hukmu ya kuuza msikiti kama huu au kuubadilisha? Na jee isipopatikana fursa ya kuubadilisha msikiti hu una mwengine ni njia zipi muwafaka za kutumia thamani ya pesa za msikiti uliouzwa?

Jawabu:

Inajuzu (inafaa) kuuza msikiti ambao umeatilika matumizi yake au ikiwa waislamu watumiaji wa msikiti huo wanahama na wakaogopea msikiti huo kutwaliwa na wasiokua waislamu wakauutumia vibaya, na baada ya kuuzwa msikiti kama huo thamani yake inatakiwa inunuliwe msikiti mwingine au sehemu nyingine itakayotumika kama msikiti.

Suali la nane:

Kwa sababu za kimasomo au za kikazi, baadhi ya wanawake wa kiislamu na wasichana mara nyingine hulazimika kuishi kivyao ima peke yao au kuishi na wanawake wasiokua waislamu, Nnini hukmu ya jambo hili?

Jawabu:

Haifai kwa mwanamke wa kiislamu kuishi peke yake katika nchi za ugenini.

Suali la tisa:

Wengi miongoni mwa wanawake huku wanasema kwamba wanaweza kujisitiri miili yao isipokua uso na viganja viwili. Wengine wanasema kua wanakatazwa sehemu zao za kazini kufinika vichwa vyao, ni sehemu zipi zinazoruhusiwa kua wazi katika viungo na mwili wa mwanamke anapokua na wanaume ajnabi ima

kazini au vyuoni?

Jawabu:

Hijabu (vazi) ya mwanamke wa kiislamu kwa mujibu wa maelezo ya wanazuoni ni kujisitiri mwili wake wote isipokua uso wake na viganja vyake viwili pasipokua na mazingira ya fitna, ama ikiogopewa fitna basi hata uso na viganja ni lazima visitiriwe.

Suali la kumi na la kumi na moja:

Wanafunzi wengi wa kiislamu wanaosomea huku hulazimika kufanya kazi ili kujiongezea kipato kwa minajili ya kujikimu na kugharamia masomo yao, kwani pesa za matumizi wanazzotmiwa na wazazi wao au jamaa zao hua haziwatoshi, kwa hio kufanya kazi imekua si suala la hiari, ila kazi nyingi zinazopatikana ni katika hoteli (restauranti) ambazo miongoni mwa vinavyouzwa ni pombe na nguruwe, nnini hukmu ya kufanya kazzi sehemu kama hizi?

Nnini hukmu ya muislamu kuuza pombe na nguruwe? Au kuitengeneza hio pombe na kuwauzia wasiokua waislamu? Ijulikane kwamba kuna baadhi ya waislamu huku wanafanya kazi kama hio.

Jawabu:

Katika mazingira-tajwa iwapo muislamu hakupata kazi ya halali ataruhsiwa kufanya kazi katika restauranti za wasiokua waislamu lakini kwa sharti asihusike binafsi kuuza pombe au kuwahudumia wateja pombe hio au kuibeba au kuitengeneza au kuifanyia biashara, hukmu hii ni sawa sawa pia kwa nguruwe na mfano wake wa vitu ilivyoharamishwa.

Suali la kumi na mbili:

Zipo dawa nyingi tu ambazo zinabeba kiwango cha alkoholi kwa asilimia 0.01% hadi 25%. Nyingi ya dawa hizi na kama zile za mafua, kikohozi, kubana kwa koo na nyenginezo katika magonjwa ya kawaida ya kila siku. Hizi ndizo dawa zinaopatikana kwa asilimia 95%, kupata dawa zisizokua na alkoholi ni vigumu sana, Nnini hukmu ya kutumia dawa hizi?

Jawabu:

Mgonjwa muislamu anaruhusiwa kutumia dawa ambayo ina kiwango fulani cha alkoholi ikiwa haikpatikana dawa nyingine mbadala na ikawa ushauri wa daktari muaminifu unapendekeza hivyo.

Suali la kumi na tatu:

Zipo hamira fulani na gelatini ambazo kutengenezwa kwake pametumika virutubisho fulani vinavyotokana na nguruwe kwa kiwango kidogo sana, je inafaa kutumia hamira na gelatini kama hizi?

Jawabu:

Haifai kwa muislamu kutumia hamira na gelatini zilizotumia nguruwe katika chakula. Zipo hamira na gelatini mbadala ambazo hutumia mimea au mafuta ya wanyama halali.

Suali la kumi na nne:

Wapo waislamu wengi wanaofunga ndoa za mabiniti wao misikitini, lakini pia baadae wanaingia kwenye sherehe za harusi hizo ambapo ndani yake kunakuwepo kucheza na kuimba nasheed au nyimbo, hawana sehemu nyingine za kufanyia sherehe hizo. Nnini hukmu ya kuendesha sherehe kama hizi misikitini?

Jawabu:

Ni jambo zuri sana kufunga ndoa misikitini, lakini haifai kuingiza sherehe ambazo ndani yake kutakua na mambo yaliyokatazwa kama vile mchanganyiko wa wanaume na wanawake (ikhtilaat), na wakawa wanawake hawatojisitiri, na kukawa na kuimba na kucheza.

Suali la kumi na sita:

Nnini hukmu ya ndoa ya mwanafunzi wa kiislamu wa kiume au wa kike ambayo hawakusudii iwe ni ndoa ya kudumu, bali iwe ni ndoa ya mda kwa kipindi wanapokua masomoni, wakimaliza masomo yao na wakiwa tayari kurudi nchi zao basi hapo iwe ndio mwisho wa ndoa hizo, ndoa yenyewe inafungwa kama kawaida, Nnini hukmu ya ndoa kama hii?

Jawabu:

Kimsingi, malengo ya ndoa inatakiwa iwe ni ya kudumu na kuendelea na kuanzisha familia yenye utulivu, ila inapotokea tatizo lisilokusudiwa.

Suali la kumi na saba:

Nnini hukmu ya mwanamke kuonekana sehemu za kazini au chuoni akiwa amechonga nyusi zake na amepaka wanja machoni mwake?

Jawabu:

Upakaji wanja kw wanawake na wanaume inajuzu (inafaa) kisharia, ama kuchonga nyusi haijuzu ila zikiwa nywele za nyusi zimekaa vibaya kwa maumbile ya mwanamke.

Suali la kumi na nane:

Baadhi ya wanawake wa kiislamu wanasikia dhiki kupeana mikono kusalimiana na wanaume wanapokua kazini au chuoni, lakini wanasalimiana hivyo hivyo na kupeana mikono, Nnini hukmu ya kupeana mikono kusalimiana? Hii pia ndio hali inayowakuta waislamu wanaume wanapokutana na wanawake ajnabi nao hutakiwa kuwasalimia wanawake hao na kupeana mikono.

Jawabu:

Haifai kwa mwanamume wa kiislamu kuslimiana kwa kupeana mikono na wanawake ajnabi, na halikadhalika waislamu wa kike kufanya hiyo.

Suali la kumi na tisa:

Nnini hukmu ya kukodi makanisa kwa minajili kusimamisha sala tano au sala za ijumaa na sala za eid mbili, licha ya kuwepo kwa masanamu kwenye makanisa hayo; ijulikane kua kukodi makanisa kwa shughuli za ibada ni rahisi mno ikilinganishwa na bei za kukodi sehemu nyingine, pia kunakuwepo taasisi za mambo ya kheri na vyuo wao wanatoa baadhi ya sehemu zao ili wasilamu watumie bila malipo kwa ibada zao?

Jawabu:

Hakuna katazo lolote kwa waislamu kukodi makanisa inapotokea dharura ya kufanya hivyo, lakini wakati wa sala hawatakiwi kuyaelekea masanamu yaliyopo hapo kanisani, na inapaswa masanamu hayo kufinikwa yakiwa yako upande wa qibla.

Suali la ishirini:

Nnini hukmu ya vichinjwa vya 'Ahlul-kitaab' mayahudi na wakristo na kula vyakula vyao katika restaurenti zao ilhali ya kua hatujui kama walitaja jina la Mwenyezi Mungu wakati wa kuchinjwa wanyama?

Jawabu:

Vichinjwa (nyama) vya 'Ahlul-Kitaab' vinajuzu kuliwa na waislamu iwapo vimechinjwa kwa mujibu wa Sharia ya Kiislamu hata kama haliktajwa jina la Mwenyezi Mungu. Inasisitizwa na 'Kongamano' kulipitia tena suala hili kwa kina na kuleta ripoti kwenye kikao kijacho cha nne.[1]

Suali la ishirini na moja:

Inatokea katika 'Minasaba' na sherehe mbalimbali ambapo waislamu wanaalikwa kuhudhuria sherehe hizo, lakini pia kunakuwepo pombe na mchanganyiko wa wanawake na wanaume, kujitenga au kutohudhuria minasaba kama hii kutawanyima waislamu fursa nyingine katika jamii. Nnini hukmu ya kuhudhuria minasaba kama hii bila ya kuunywa pombe na wao au kula nguruwe au kucheza?

Jawabu:

Haifai kwa muislamu wa kiume au wa kike kuhudhuria sherehe au mahfali ambapo ndani yake knakuwepo kumuasi Allah na mambo ya munkar.

Suali la ishirini na tatu:

Katika majimbo mengi ya Marekani na nchi kadhaa za Ulaya inkua vigumu kuuona mwezi wa Ramadhan au wa Shawwal, lakini maendeleo ya kisayansi yaliyopo katika nchi hizi yanatuwezesha kimahesabu kujua kwa yakini wakati wa kuzaliwa kwa mwezi husika kwa saa na dakika n ahata

[1] Tizama 'Maamuzi' namba 95 (3/10) kifungu cha sita na kuendelea.

sekunde. Jee inafaa, kwa mazingira kama haya, kuzitegemea hesabu hizi kuthibitisha mwezi? Je inajuzu kutmia vifaa kama darubini ya kuangalia mwezi na kukubali maelezo ya wataalamu hawa ambao si waislamu lakini ni wasema kweli?

Ijulikane hapa kwamba waislamu wa Marekani na wa nchi za Magharibi wanapofuata miandamo ya mwezi kutoka nchi za kiislamu imewasababishia migongano mingi na hitilafu za kimadhehebu kuibuka na hivyo kuwakosesha faida nyingi za kua pamoja katika sikukuu. Kuzifanyia kazi hesabu hizi za ki-falaki zitawaondoshea migawanyiko na migongano.

Jawabu:

Kukubalika kwa mwezi mwandamo ni lazima uonekane, hata hivyo hamna tatizo kutumia mahesabu ya kifalaki na madarubini kama visaidizi na kuowanisha baina ya Hadith za Mtume SAW na elimu ya sayansi. Ikitokea mwezi umeonekana sehemu fulani basi imewawajibikia waislamu kote kuufanyia kazi mwezi huo bila kuzingatia tofauti za ‘matlai’ zilizopo, hii ni kwa mujibu wa ufahamu wa agizo la Mtume SAW la kufunga na kufungua kwa kuonekana kwa mwezi.[1]

Suali la ishirini na nne:

Nnini hukmu ya muislamu kufanya kazi katika idara za serikali ya Marekani au serikali nyingine zisizokua za kiislamu, husuusan katika idara za kutengeneza nyuklia au kufanya tafiti-mkakati za kivita na mfano wake?

Jawabu:

Inajuzu kwa muislamu kufanya kazi zilizo halali katika idara za serikali au taasisi za nchi zisizokua za kiislamu iwapo kupitia kazi yake hio haitapelekea kuwadhuru waislamu.

Suali la ishirini na tano na ishirini na sita:

Nnini hukmu ya Mhandisi muislamu kuchora ramani ya majengo ya

[1] Tizama ‘Maamuzi’ namba 18 (6/3)

wakristo kama vile makanisa na mfano wake, ijulikane kua kuchora kwake huku ni sehemu ya kai yake alioajiriwa na kampuni ya ujenzi, asipofanya hivyo henda akafutwa kazi?

Nnini hukmu ya muislamu au taasisi ya kiislamu kutoa mchango wake wa kifedha kwa taasisi ya kielimu iliyo chini ya kanisa?

Jawabu:

Haijuzu kwa muislamu kuchora ramani ya majengo yatakayotumika kama ehemu za ibada za makafiri au kuchangia kifedha au venginevyo taasisi kama hizo.

Suali la ishirini na saba:

Zipo familia nyingi za kiislamu ambazo waume wao wanafanya kazi katika kuuza pombe na nguruwe na mfano wa vitu kama hivyo, wake zao na Watoto wao wanachukizwa na kitendo hicho hasa kwa kua chakula chao kinatokana na pesa zinazipatikana na kazi hio. Je hapo kuna tatizo lolote?

Jawabu:

Inafaa kwa mke na Watoto ambao hawana njia mbadala ya chumo lingine la halali; kula kwa njia ya dharura kutokana na chumo la mume huy lililotokana na haramu kama kuuza pombe na nguruwe na mfano wake baada ya juhudi nyingi za kumkinaisha mume huyu akatafute njia nyinigine mbadala yenye chumo la halali.

Suali la ishirini na nane:

Nnini hukmu ya kununua nyumba ya kuishi na gari la matumizi ya binafsi na na ‘samani’ za nyumbani kupitia mikopo ya benki au taasisi za kukopesha ambazo wanaweka faida fulani juu ya mkopo huo na baada ya kuweka rahani, ijulikane kua usiponunua vitu hivi; nyumba, gari na samani kwa mkopo huu liotajwa basi njia nyingine ya kuvipata vitu hivi ni kwa kuvikodi kwa malipo ya kila mwezi, ukilanganisha malipo ya mwezi ya kukodi na yale kununua basi kukodi yanakua yako juu zaidi ya yale ya kununua kupitia benki?

Jawabu:

Haijuzu kisharia.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 24 (12/3)

Yanayohusiana na 'Miradi ya Ki-elimu ya 'Kongamano'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tatu (3) kilichofanyika mji wa amman, Falme ya Jordan kuanzia tarehe 8 – 13 Mwezi wa Mfungo Tano (Swafar), 1407 sawa na tarehe 11 – 16 Oktoba, 1986.

Baada ya usikivu makini wa ripoti ya 'Kitengo-Mipango' iliyotokana na kikao chake cha tarehe 8 na 9 mwezi wa Swafar, 1407H, sawa na tarehe 11 na 12 Oktoba, 1986, kikao ambacho kilijadili ajenda mbalimbali;

Hivyo basi, Kongamano limeamua yafuatayo:

- **Moja:** Kuwafiki uanzilishwaji kwa miradi ya ki-elimu ifuatayo baada ya kuingiza marekebisho:

    1. Saiklopidia ya Ki-fiqhi-Uchumi
    2. Kamusi la Misamiati ya Ki-fiqhi
    3. Muongozo wa Misingi ya Ki-fiqhi
    4. Jarida la Dalili za Hukumu za Ki-fiqhi
    5. Kuhuisha Turathi za Ki-fiqhi
    6. Muongozo wa Ki-fedha wa Saiklopidia ya Ki-fiqhi-Uchumi
    7. Muongozo wa Ki-fedha wa Kamusi la Misamiati ya Ki-fiqhi
    8. Muongozo wa Ki-fedha wa Kuhuisha Turathi za Ki-fiqhi
    9. Mpangilio-kazi na uendeshaji wa shughuli za 'Baraza'

- **Mbili:** Kuunda kamati ya ki-elimu ya watu wanne watakaoandaa Mpangilio-kazi wa miradi miwili; ‘Muongozo wa Misingi ya Ki-fiqhi’ na ‘Jarida la Dalili za Hukumu za Ki-fiqhi’, kwa kushauriana na Mkurugenzi wa Baraza na Katibu Mkuu

Allah ndie Mwenye Kutuafikia

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 25 (13/3)

Yanayohusiana na ‘Maazimio ya Kikao cha Tatu cha ‘Kongamano’

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tatu (3) kilichofanyika mji wa amman, Falme ya Jordan kuanzia tarehe 8 – 13 Mwezi wa Mfungo Tano (Swafar), 1407 sawa na tarehe 11 – 16 Oktoba, 1986.

Baada ya usikivu makini taarifa kutoka kwa Mtukufu Mrithi wa Ufalme wa Jordan Naibu-Mfalme al-Hassan bin Talaal kuhusu matatizo sugu yanayowakabili wasilamu ulimwenguni katika nyanja za maendeleo ya kiuchumi na na kijamii, na haja iliopo ya kutatua matatizo hayo na kuwawezesha waislamu kupambana na adui ufukara, ugonjwa na ujinga ili kuwaletea maisha yenye heshima kwa binadamu.

Baada ya kuupokea wito wa Mtukufu Mrithi wa Ufalme wa Jordan Naibu-Mfalme ulioelekezwa kwa nchi zote za kiarabu na za kiislamu kusimama pamoja kuisaidia Sudan.

Baada ya kutambua haja iliopo ya kuongeza juhudi kuukomboa Msikiti mtukufu wa al-Aqsa, uliopo karibu na sehemu ya mkutano wa kikao hichi cha tatu.

Na kutokana na imani yake ya kuzipa kipaumbele kadhia za waislamu za kiuchumi, kijamii, mshikamano na umoja na kuzitafutia ufumbuzi kawimu kwa njia za kielimu na kiutafiti na mfano wake;

Hivyo basi, Kongamano limeamua yafuatayo:

- **Moja:** Umuhimu wa kuandaa Mpango-kazi mpana wa kusaidiana nyakati za majanga, Mfuko maalum uanzishwe kwa kazi hii utakaofadhiliwa kupitia pesa za zaka, michango na waqfu.
- **Mbili:** Kuzitaka nchi za kiislamu na umma wa kiislamu kuongeza juhudi wawezayo kuukomboa Msikiti wa al-Aqsa; qibla cha kwanza cha waislamu na msikiti wa tatu kwa utukufu, halikadhalika kuzikomboa ardhi za waislamu zilizotawaliwa kimabavu, haya yafanyike kwa njia kuunganisha juhudi za waislamu na kujenga umma wenye mshikamano utakaojiepusha na kila sababu za migongano na mifarakano na kuitumia Sharia ya Allah katika maiasha yao.
- **Tatu:** Kazi za 'Kongamano' zielekezwe katika nyanja za utafiti wa kielimu na fatwa katika kupambana kadhia mbalimbali zinazowakwaza waislamu kwenye maisha yyao ya kijamii, kiuchumi na kuwaunganisha wawe kitu kimoja ili waweze kukabiliana na changamoto za kila siku na kuweza kuishi maisha yenye heshima yatokanayo na miongozo ya Sharia.
- **Nne:** Kuchanganua baina ya miradi ya kiutafiti na kadhia zinazohitajia fatwa, nguvu za ziada zielekezwe kwenye miradi ya kiutafiti kwa mujibu wa mpango-kazi maalum utakaoandaliwa na Kitengo-mipango cha 'Kongamano', Mpango-kazi huu baadae utaletwa kwenye kikao ha Baraza ili upitishwe.

Allah ndie Mwenye Kutuafikia

≃≃≃

Maamuzi na Maazimio ya Kikao cha Nne ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Jeddah, Falme ya Saudi Arabia

18 – 23 Jumadal Aakhira (Mfungo Tisa), 1408

6 – 11 Februari, 1988

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 26 (1/4)

Yanayohusiana na 'Binadamu kunufaika kwa viungo vya binadamu mwingine aliehai au aliekufa'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nne (4) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia kuanzia tarehe 18 – 23 Mwezi wa Mfungo Tisa, (Jumadal-Aakhira) 1408 sawa na tarehe 6 – 11 Februari, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti za ki-fiqhi na za ki-utabibu zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Binadamu kunufaika kwa viungo vya binadamu mwingine aliehai au aliekufa,** na kwa mujibu wa mijadala na hoja zilizoweka wazi kwamba 'jambo hili' ni sehemu ya maisha ya ki-leo, ambalo limewezeshwa kutokana na maendeleo ya elimu na sayansi, athari zake nzuri zimedhihiri lakini pia zimekuwepo na athari mbaya za kisaikolojia na kijamii hasa jambo hili linapoendewa bila kuwepo kwa vidhibiti vya kisharia vinavyolinda na kuhifadhi heshima ya binadamu kwa kuzingatia makusudio makuu ya sharia ambayo yanahakikisha kheri na maslaha yanapatikana kwa binadamu na yanayowataka binadamu kusaidiana, kuoneana huruma na kupendeleana mazuri.

Baada ya kukusanya nukta mbalimbali za maudhui haya ili iwe rahisi kuyafahamu na kuyawekea vidhibiti na kubaini hukmu zake; **imeamuliwa yafuatayo:**

Kuhusu ufafanuzi na vigawanyo vyake:

- **Moja:** 'Kiungo' hapa inaksudiwa sehemu yoyote ya binadamu kama vile mishipa, seli, damu na mfano wake au kama vile konea ya macho ilioshikana na jicho au iliyotengana nalo.
- **Mbili:** 'Kunufaika' hapa inakusudiwa: Kufaidika kwa mgonjwa kutokana na dharura ya ugonjwa wake kwa minajili ya kuendelea kuishi au kuendelea kukifanyisha kazi kiungo ambacho kimekosa sifa hio, kwa lengo la kumfanya mfaidika aishi maisha ya heshima.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 4, Mjeledi 1, Ukurasa 89.

- **Tatu:** Kuna aina tatu za kunufaika:
  1. Kuhamisha kiungo cha aliehai.
  2. Kuhamisha kiungo cha aliekufa.
  3. Kuhamisha kutoka kwa kijusi (mtoto alietumboni kabla hajazaliwa).

Kuhusu **aina ya kwanza** ambayo ni Kuhamisha kiungo cha **aliehai**; ina hali zifuatazo:

a) Kuhamisha kiungo kutoka sehemu ya mwili na kuipeleka sehemu nyingine ya mwili huohuo, kama kuhamisha Ngozi, mishipa, misuli, mifupa, damu na venginevyo.
b) Kuhamisha kiungo kutoka kwa mtu aliehai kwenda kwa mtu mwingine; hapa inatizamwa kiungo chenyewe iwapo ni kiungo nyeti kwa uhai au si kiungo nyeti. Ikiwa ni kiungo nyeti kinaweza kua ni kiungo kimoja au jozi; mfano wa kiungo kimoja ni kama: moyo na ini; mfano wa kiungo jozi ni kama: figo na mapafu. Ama kwa viungo visiyokua nyeti ambavyo uhai unaweza kuendelea pasi na viungo hiyo basi kuna vile viungo vinavyofanya kazi ya msingi kuna na vile ambavyo havifanyi kazi ya msingi; aidha kuna vile ambavyo vinajiteneneza upya kama damu na kuna visivyojitengeneza upya, halikadhalika kuna vile vinavyoathiri nasabu kama konde za mwanamume na chumba cha yai la mwanamke na seli za mfumo wa mishipa, na vile ambavyo haviathiri chochote.

Kuhusu **aina ya pili** ambayo ni Kuhamisha kiungo cha **aliekufa**; ina hali mbili zifuatazo:

- ✓ **Hali ya kwanza:** Kufa kwa ubongo na kuatilika kazi zake zote pasipo na tamaa ya kurudia tena uhai kwa mujibu wa ushauri wa daktari bingwa.
- ✓ **Hali ya pili:** Kusimama kwa mapigo ya moyo na pumzi pasipo na tamaa ya kurudia tena uhai kwa mujibu wa ushauri wa daktari bingwa. ‘Maamuzi ya Kongamano’ ya kikao cha tatu[1] yamezingatia hali zote mbili hizi.

Kuhusu **aina ya tatu** ambayo ni Kuhamisha kutoka kwa kijusi; ina hali tatu

[1] Tizama Maamuzi namba 17 (5/3).

zifuatazo:

- ✓ Hali ya kwanza: Kijusi kilichodondoka chenyewe.
- ✓ Hali ya pili: Kijusi kilichodondoka kutokana na matumizi ya dawa au kuhujumiwa kwa mama.
- ✓ Hali ya tatu: Watoto wa chupa waliopo nje ya uzao.

Kuhusu hukumu za sharia:

Moja: Inajuzu Kuhamisha kiungo kutoka sehemu ya mwili na kuipeleka sehemu nyingine ya mwili huohuo, pamoja na kuzingatia kua manufaa yanayotarajiwa kupatikana kupitia zoezi hili yatakua ni makubwa kuliko madhara yake, aidha inashurutishwa kua zoezi hili liwe; ima ni kuweka kiungo kilichokosekana, au kukirudisha katika uhalisia wake, au kukianyisha kazi yake ya asili, au kurekebisha kasoro iliyojiktokeza, au kuondosha uvimbe na mfano wa vitu kama hivyo ambavyo vinamuathiri mtu kimwili na kisaikolojia.

Mbili: Inajuzu Kuhamisha kiungo kutoka kwa mtu aliehai kwenda kwa mtu mwingine, ikiwa kiungo hichi ni chenye kujiteneneza upya kama damu au ngozi, kinachozingatiwa katika zoezi hili ni kua ‘Mtoaji’ wa kiungo ni mtu mwenye akili zake timamu na hajatenzwa nguvu au kutishiwa.

Tatu: Inajuzu kufaidika na kiungo kilichotolewa kutoka kwenye mwili chenye tatizo la ugonjwa na kupachikwa mtu mwingine, kama vile konea ya jicho iwapo jicho la mtu limekobolewa kwa ajili ya ugonjwa.

Nne: Ni haramu kuhamisha kiungo nyeti kwa uhai kama moyo kutoka kwa mtu aliehai kwenda kwa mtu mwingine.

Tano: Ni haramu kuhamisha kiungo cha binadamu **aliehai** ambacho kuondoshwa kwa kiungo hicho kunapelekea kuatilisha kazi za msingi katika maisha yake kama vile kuhamisha konea zote mbili za macho, ama ikiwa inaatilisha sehemu ya matumizi ya kiungo hicho basi hukmu yake imetizamwa kwenye kifungu cha nane kijacho.

Sita: Inajuzu kuhamisha kiungo cha **aliekufa** kwenda kwa **aliehai** ambae maisha yake yataokolewa kwa kupata kiungo kama hicho, au kazi za

msingi zinategemea kiuongo hicho; kwa sharti awe maiti huyo alishaidhinisha oei hilo lifanyike kabla kufa kwake au aliandika wosia. Ama ikiwa maiti hajulikani na hana watu wake basi ni lazma ipatikane ruhusa kutoka kwa mtawala alie muislamu.

Saba: Yapaswa kuzingatia haya: Uhalali wa kujuzisha kuhamishwa kwa kiungo katika hali-tajwa hapo juu umeshurutishwa kutokuwepo aina yoyote ya biashara katika zoezi kama hilo. Biashara juu ya viungo vya binadamu haifai kwa namna yoyte ile.

Ama kwa yule anaefaidika na kupatiwa kiungo akiamua kutoa chochote kama bakhshishi au takrima basi hukmu yake inahitaji kutizamwa.

Nane: Hali nyingine zote ambazo hazikutajwa katika maelezo yaliotangulia basi zinahitaji kutizamwa kwenye kikao kijacho.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 27 (2/4)

Yanayohusiana na 'Kuwapatia Zaka Mfuko wa Shirika la Tadhamun la Kiislamu'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nne (4) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia kuanzia tarehe 18 – 23 Mwezi wa Mfungo Tisa, (Jumadal-Aakhira) 1408 sawa na tarehe 6 – 11 Februari, 1988.

Baada ya usikivu makini wa maelezo bainifu yanayohusiana na **Kuwapatia Zaka Mfuko na Wakfu wa Shirika la Tadhamun la Kiislamu** yaliyowasilishwa kwenye kikao cha tatu cha 'Kongamano' na baada ya kusikiliza tafiti zilizowasilishwa katika kikao hiki kuhusiana na 'kuwapatia zaka mfuko huu wa Tadhaamun'; **imeamuliwa yafuatayo:**

- **Moja:** Haijuzu kuwapatia zaka 'Wakfu wa Mfuko wa Tadhaamun' kwa sababu kufanya hivyo ni kuzifunga pesa za zaka nje ya maeneo yaliyoainishwa katika Qur'an.

- Inafaa kwa 'Mfuko wa Tadhaamun wa Kiislamu' kua wakala wa kugawa zaka kwa niaba ya watu au taasisi na kuzifikisha sehemu zake stahiki kwa masharti yafuatayo:

  a) Watimize masharti na vigezo ya kua 'Wakala'.

  b) Iwekwe kwenye Katiba ya 'Mfuko' na malengo yake kwamba watakua wakijihusisha na zoezi kama hili.

  c) Inatakiwa kwa 'Mfuko' iweke 'Akaunti' maalum ya pesa za zaka zinazoingizwa ili zisichanganyike na pesa nyingine ambazo matumizi yake hayana masharti yaliyoainishwa kama kutumia kwenye maslahi ya umma.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 4, Mjeledi 1, Ukurasa 517.

d) Si haki kwa ‘Mfuko’ kutumia pesa za zaka kwenye gharama za kiofisi na kiutawala au kulipia mishahara ya wafanyikazi wake au matumizi mengine yoyote nje ya yale yaliyoainishwa katika Qur’an ambayo ni maeneo manane.

e) Inaruhusiwa kwa ‘Mtoaji zaka’ kwa ‘Mfuko’ kuwashurutisha wafikishe zaka zake katika eneo fulani miongoni mwa yale maeneo manane yaliyoainishwa katika Qur’an. Katika hali kama hii; ‘Mfuko’ utalazimika kufuata masharti waliyoekewa.

f) Inawalazimu ‘Mfuko’ kuzifikisha pesa hizo za zaka kwa wastahiki wake kwa haraka iwezekanvyo bila kucheleweshwa; ndani ya mda usiozidi mwaka mmoja, ili walengwa wa zaka hizo wanufaike nazo ndani ya wakati.

Aidha ‘Kongamano’ limeazimia yafuatayo:

Kufanya juu chini ili kuuwezesha ‘Mfuko’ huu wa ‘Shirika la Tadhaamun la Kiislamu’ kufikia malengo yake yaliyo mazuri, kama yalivyoelezewa kwenye katiba yake. Ikumbukwe kua ‘Mfuko’ huu ulianzishwa kwa mujibu wa ‘Maazimio, ya Kikao-kilele cha pili cha viongozi wa nchi za kiislamu, waliamua viongozi hawa kuanzishwa kwa ‘Mfuko’ huu pamoja na kuusimamia na kuugharamikia kupitia ad ana michango ya nchi wanachama, lakini kutokana na ukweli kwamba sio nchi zote zimekua zikilipa ad ana michango yao, hivyo basi; ‘Kongamano’ linawaomba tena nchi zote za kiislamu na serikali zao na taasisi zao na matajiri wa kiislamu kusimama kidete na kutekeleza majukumu yao kwa kuusaidia ‘Mfuko’ huu ili uwezeshwe kufikia malengo yake ya kutumikia umma wa kiislamu.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 28 (3/4)

Yanayohusiana na 'Zaka za Hisa kwenye makampuni'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nne (4) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia kuanzia tarehe 18 – 23 Mwezi wa Mfungo Tisa, (Jumadal-Aakhira) 1408 sawa na tarehe 6 – 11 Februari, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Zaka za Hisa kwenye makampuni,** na baada ya upekuzi wa hoja zilizojadiliwa **imeamuliwa yafuatayo:**

Moja: Zaka za Hisa zinawalazimu wamiliki wa hisa hizo, uongozi wa kampuni unaweza kuwatolea wenye hisa zaka zao kwa niaba yao iwapo imeelezewa hivyo katika kanuni za kampuni, au kuna azimio lililopitishwa na kikao kikuu cha kampuni husika, au ikiwa sheria za nchi zinawataka viongozi wa makampuni kuwatolea zaka wamiliki wa hisa, au kuna maelekezo kutoka kwa mmiliki wa hisa kwa uongozi wa kampuni hio wamtolee zaka zake za hisa anazomiliki.

Mbili: Kampuni itatoa zaka za hisa kama anavyotoa mtu zaka zake, kwa maana kampuni itazingatia mali yote ya wenye hisa ni kama mali ya mtu mmoja, na kwa msingi huu zitafanywa hesabu za utowaji zaka kwa kuzingatia aina ya mali yaliyopo, na iwapo yamefika Nisabu (Kiwango cha chini kinacholazimu kutoa zaka), na kiwango cha zaka zinazostahili kutolewa, hii ni kwa mujibu wa msingi wa 'Khaltah' yaani kchanganya mali unaokubaliwa na wana-fiqihi.

Ama hisa ambazo hazilazimu kutolewa zaka zinaachwa pembeni bila kuguswa, kama vile hisa mfuko wa umma, hisa za waqf una taasisi za misaada, na pia hisa zza wasiokua waislamu.

Tatu: Iwapo kampuni haikuwatolea zaka wenye hisa kwa sababu yoyote ile, basi ni wajibu wa wamiliki wa hisa kutoa wenyewe zaka za hisa zao kwa kutaka kujua

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 4, Mjeledi 1, Ukurasa 705.

kima cha mali yaliyotokana na hisa zao.

Ikishindikana kujua kima cha mali yaliyotokana na hisa zao, basi atatizama iwapo alinunua hisa hizo kwa lengo la kufaidika na mgao wake unaotolewa kila mwaka, na wala hakukusudia kuzifanyia biashara hisa hizo, basi atatoa zaka za vitendea kazi[1] kwa kipimo cha nyumba na ardhi zilizokodishwa amazo si za kilimo, yaani mmiliki wa hisa hapa hawajibiki kuzitolea zaka hisa zenyewe, bali atatoa zaka kwenye mgao atakaopata ambayo itakua ni asilimia 2.5 (yaani 2.5%) inayotolewa baada ya mzunguko wa mwaka kuanzia siku alipokabidhiwa mgao wake, vigezo vingine na masharti ya zaka yanazingatiwa.[2]

Ama ikiwa mmiliki wa hisa alizinunua kwa lengo la kuzifanyia biashara, basi atazitolea zaka kama zinayotolewa zaka za mali ya biashara, kwa maana hisa hizo zitakapozungukiwa na mwaka na zikawa bado ziko kwenye milki yake basi atahesabu kima na thamani ya hisa hizo pamoja na faida iliopatikana azitolee zaka za 2.5%.

Nne: Anapouza mmiliki wa hisa hisa zake katikati ya mwaka basi atachanganya thamani ya hisa hizo na mali yake mengine ifikapo mwisho wa mwaka ndio atoe zaka zake kwa pamoja. Ama mnunuzi wa hisa atatoa zaka kama ilivyoelezwa hapo awali.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

[1] Tizama ‘Maamuzi’ ya Kongamano ya kikao cha pili Namba 2 (2/2).

[2] Maamuzi, namba 120 (313) yaliotolewa kuelezea kusudio la zaka za hisa na mgawo wa hisa.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 29 (4/4)

Yanayohusiana na 'Kuvua umiliki binafsi kwa ajili ya maslahi ya umma'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nne (4) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia kuanzia tarehe 18 – 23 Mwezi wa Mfungo Tisa, (Jumadal-Aakhira) 1408 sawa na tarehe 6 – 11 Februari, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Kuvua umiliki binafsi kwa ajili ya maslahi ya umma** na kwa mujibu wa misingi ya Sharia inayojulikana inayohishimu 'umiliki binafsi' kiasi ya kwamba imekua kuhifadhi mali na umiliki binafsi, ni katika makusudio ya Sharia makuu Matano, na juu ya jambo hili zipo aya nyingi sana katika Qur'an pamoja na hadithi za Mtume SAW pamoja na matendo ya maswahaba na waliokuja baada yao, wote hao wakisisitiza suala la kuhishimu umiliki binafsi, lakini iwapo kuna haja ya kuhifadhi maslahi ya umma kwa mujibu wa misingi ya Sharia ambapo maslahi binafsi yatadhurika, **basi 'kongamao' limeamua yafuatao:**

- **Moja:** Ni wajibu kulinda maslahi binafsi ya mtu dhidi ya uharibifu wa aina yoyote ile, na wala haijuzu (haifai) kumbana au kumtia dhiki kwenye matumizi ya mali yake, bali ni haki ya mmiliki binafsi kunufaika kikamilifu na anachomiliki kwa mujibu wa Sharia.

- **Mbili:** Haijuzu (haifai) kuvua umiliki binafsi wa ardhi kwa ajili ya maslahi ya umma isipokua baada ya kuzingatia vigezo na masharti ya kisharia yafuatayo:

  a) Ni lazima kuwepo malipo ya haraka na yanayoedana na thamani ya ardhi binafsi inayotakiwa kuvuliwa umiliki binafsi.

  b) Ni mtawala pekee ndie anaeruhusiwa kuvua umiliki binafsi au yule atakaeidhinishwa nae.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 4, Mjeledi 2, Ukurasa 897.

c) Uvuliwaji wa umiliki binafsi uapaswa kufanyika kwa minajili ya ‘Maslahi ya Umma’ kama mfano kujenga msikiti au njia au kupitisha daraja.

d) Haifai kutumia ardhi iliyovuliwa umiliki binafsi kwenye uwekezaji wowote ule, halikadhalika isiharakishwe uvuliwaji umiliki binafsi kabla ya wakati wake.

Yakipanguka masharti tajwa hapo juu au baadhi yake; basi ijulikane kwamba ‘uvuliwaji umiliki binafsi’ hapa itakua ni dhulma na unyakuzi wa ardhi ulioharamishwa na Allah SWT na Mtume wake SAW.

Pia ijulikane kwamba lau nia ya ‘uvuliwaji umiliki binafsi’ itabadilika basi mmiliki wa asili au warithi wake watakua na haki ya kipaombele kurejeshewa milki zao kwa malipo yanayokubalika bila ya kudhulumiwa.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 30 (5/4)

Yanayohusiana na 'Hati-fungani (Sukuk) za Mudaraba na Hati-fungani za Uwekezaji'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nne (4) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia kuanzia tarehe 18 – 23 Mwezi wa Mfungo Tisa, (Jumadal-Aakhira) 1408 sawa na tarehe 6 – 11 Februari, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Hatifungani za Mudaraba na Hatifungani za Uwekezaji** Tafiti ambazo zilikua zimewasilishwa hapo awali kwenye 'Warsha' maalum iliyoandaliwa na 'Kongamano' kwa kushirikiana na 'Taasisi ya Kiislamu ya Utafiti na kuelimisha iliyo chini ya 'Benki ya Kiislamu ya Maendeleo' mnamo tarehe 6 – 9 Mwezi wa Muharram 1408H sawa na 2 – 8 Mwezi wa Septemba 1987 kwa lengo la kutekeleza Azimio namba 22 (10/3) lililokubaliwa kwenye kikao cha tatu cha 'Kongamano'; kikao ambacho kilishirikisha Wajumbe na Wataalamu wa Kongamano' na 'Watafiti wa Taasisi ya Kiislamu' na wataalamu wengine kutoka vituo mbalimbali vya ki-utafiti katika masuala ya kiuchumi, na kwa umuhimu wa aina yake wa maudhui hii na kuzikamilisha janibu zake zote zinazohusiana; ndio 'Azimio hili' linapitishwa kwa lengo la kuongeza uwezo wa 'nguvukazi watu na rasilmali' zinapokua pamoja.

Baada ya kupitia maazimio kumi yaliyokubaliwa kwenye 'Warsha' na kujadili hoja zilizowasilishwa; **'Kongamano' limeamua yafuatayo:**

Moja: Kuhusu lugha ya Kisheria inayokubalika katika uandikaji wa 'Hatifungani za Mudaraba':

1) 'Hatifungani za Mudaraba' ni chombo cha uekezaji kinachosimamia 'Rasilimali' za Mudaraba kwa kutoa 'Stakabadhi' za umiliki wa rasilimali za mudaraba kwa misingi ya hisa zinazolingana thamani zinazosajiliwa kwa

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 4, Mjeledi 3, Ukurasa 1809.

majina ya wamiliki wa rasilimali hizo kwa kuzingatia kua ni wamiliki kwa pamoja kila mtu kwa kiwango chake alichotoa pamoja na ghila (faida) itakayotokana nazo. Inapendekezwa kuitwa chombo hiki cha uwekezaji: 'Hatifungani ya Mudaraba'.

2) Ili hizi 'Hatifungani za Mudaraba' ziweze kukubalika Kisharia zinahitaji kutimiza vigezo vifuatavyo:

- **Kigezo cha kwanza:** 'Hatifungani' inamaanisha umiliki wa pamoja wa hisa katika mradi ambao 'Hatifungani' hizi zimetolewa kwa minajili ya kugharamia mradi husika, umiliki huu utaendelea kubaki kipindi chote cha mradi husika kuanzia kwake hadi kukamilika. Kwa maana hio mmiliki wa 'Hatifungani' atakua na haki zake zote zinazokubalika Kisharia katika kutumia pesa zake kama vile kuuza, kununua, kutoa zawadi, kuweka rahani, kurithi au kurithiwa na mengineo, ikizingatiwa kua 'Hatifungani' ni Rasilimali kwenye Mudaraba.

- **Kigezo cha pili:** Mikataba katika 'Hatifungani za Mudaraba' inajengeka katika misingi ya: Masharti yote ya mikataba yanaainishwa kwenye 'Waraka wa Makubaliano' wakati wa kuandaa 'Hatifungani', na kuafikiwa makubaliano hayo na pande zote husika. 'Waraka wa Makubaliano' ni lazima utaje kwa uwazi kabisa maelezo yote yanayohitajika kwa mujibu wa Sharia katika 'Mikataba ya Mudaraba' kama vile kuainisha taarifa zote za 'Rasilimali' na namna ya mgao utakavyofanyika pamoja na masharti yoyote yatakayojitokeza, ila masharti yoyote yatakayokubaliwa ni lazima yawe yanaendana na 'Hukumu za Sharia'.

- **Kigezo cha tatu:** 'Hatifungani za Mudaraba' zinatakiwa ziwe zinakubali mzunguko yaani kubadili mikono baada ya mda uliowekwa kumalizika, kwa kuchukulia kua hilo limeidhinishwa na mmiliki wa rasilimali wakati wa kuingia kwenye mkataba huu wa kuandika Hati-fungani kwa kuzingatia masharti yafuatayo:

  a) Iwapo mali zilizokusanywa kwa minajili ya Mudaraba baada ya kusainiwa mikataba lakini kabla ya kuanza mradi husika kwa kutumia pesa hizo basi ijulikane kua mzunguko wowote katika kipindi hiki wa

‘Hati-fungani ni sawa na kubadilishana pesa kwa pesa, kwa maana hio: ‘hukmu zote za ubadilishanaji wa pesa’ zitatumika.

b) Iwapo pesa hizi za Mudaraba ni deni, basi hukumu zote zinazohusiana na madeni zitatumika.

c) Iwapo ‘Pesa za Mudaraba’ ni mkusanyiko wa pesa taslimu na madeni na ankari na huduma basi inafaa kuuziana ‘Hati-fungani za Mudaraba’ kulingana na bei watakayoridhiana ikiwa ankari na huduma ndio kiwango kikubwa, ama ikiwa pesa taslimu au madeni ndio kiwango kikubwa basi hukumu za Sharia zitakazozingatiwa ni zile zitakazobainishwa na kupitishwa kwenye kikao kijacho. Katika hali zote miamala hii ya kuuziana Hati-fungani ni lazima isajiliwe na sehemu husika.

- **Kigezo cha nne:** Anaepokea pesa zilizokusanywa kwenye ‘Hati-fungani’ kwa minajili uwekezaji kwenye miradi anaitwa ‘Mudarib’ yaani anaezizalisha zile pesa, ‘Mudarib’ huyu hamiliki kwenye mradi husika ila kile kiwango anachokitoa yeye kwenye kununua ‘Hati-fungani’ isipokua yeye atashiriki kwenye mgao wa faida kwa kiwango walichokubaliana nacho kabla ya kuanza kwa mradi huo kwa mujibu wa ‘Waraka wa Makubaliano’, umiliki wa ‘Mudarib’ kwenye mradi husika unajengeka kwenye msingi huo tajwa. Venginevyo umiliki wa ‘Mudarib’ wa mali yote yaliyokusanywa kwa minajili ya uwekezaji ni umiliki wa ‘amana’ aliyokabidhiwa, kwa maana hiyo: hukumu zote za Sharia zinazoambatana na mali ya amana zitatumika.

3) Pamoja na kuzingatia vigezo vilivyotajwa hapo juu; inafaa kuuziana ‘Hati-fungani za Mudaraba’ kwenye soko la hisa, likipatikana, kwa kufuata vidhibiti vya Kisharia kulingana na ‘kanuni za mahitajio na usambazaji’ na kwa matakwa ya hiari ya wauzianao. Pia inafaa kuuziana kwa kuwekeana mida maalum itakayotangazwa na sehemu husika kuuza au kununua hisa za faida zilizotokana na ‘Mudaraba’ kwa kima maalum. Ni vizuri hapa kupata ushauri wa kitaalam katika kuweka bei za hisa kulingana na mwenendo wa ‘Soko la Hisa’.

4) Haijuzu kwa ‘Waraka wa Makubaliano’ au ‘Hati-fungani ya Mudaraba’ kuwepo kifungu cha kumshurutisha ‘Mudarib’ kubeba dhamana ya

‘rasilimali’ au dhamana ya faida inayonasibishwa na rasilimali, na lau patakuwepo kifungu kama hicho ima kwa uwazi au kwa upenyezi basi sharuti ya dhamana inabatilika na itakua ni haki ya Mudarib kupokea mgao wa faida kwa taratibu zinazojulikana.

5) Haijuzu kwa ‘Waraka wa Makubaliano’ au ‘Hati-fungani ya Mudaraba’ kuwepo kifungu cha kumshurutisha ‘Mudarib’ kuuza hisa zake, lakini inajuzu kupenyeza kwenye Hati-fungani ahadi ya kuuza; na katika hali kama hii basi ni lazima pawepo mkataba wa mauziano ya hisa kwa thamani itakayo kadiriwa na wataalamu na thamani hio ikubaliwe na pande zote mbili za makubaliano kwa hiari yao.

6) Haijuzu kwa ‘Waraka wa Makubaliano’ au ‘Hati-fungani ya Mudaraba’ kuwepo kifungu cha kukatisha ushirikiano kwenye faida, wa ila basi makubaliano haya yanakua batili.

Na hali hii inapelekea yafuatayo:

a) Kutojuzu kushurutisha kuweka kiwango maalum cha faida kwa ima wawekezaji au Mudarib katika ‘Waraka wa Makubaliano’ na Hati-fungani za Mudaraba.
b) Msingi wa mgao wa faida ni ule unaokubalika Kisharia ya kilichozidi baada ya kutoa ‘Rasilimali’. Kiwango cha faida kinajulikana ima kwa kutathmini au kuhesabu pesa za mradi husika, kitakachozidi Rasilimali ima baada ya kutathmini au kuhesabu basi hio ndio faida ambayo itagawiwa kwa wawekezaji na mudarib kulingana na masharti waliokubaliana.
c) Hesabu zote za faida au za hasara za mradi husika lazima ziwekwe wazi na ziwe kwenye umiliki wa wawekezaji.

7) Faida inaanza kulipwa pale tu imeshajulikana ima kwa kutathmini au kuhesabu pesa za mradi husika na baada ya kufanya mgao. Iwapo mradi jusika unazalisha kipato inafaa kwa wawekezaji au mudarib kugawiwa katika kipato hicho lakini itakua ni kama deni litakalohesabiwa wakati wa kufunga hesabu.

8) Hakuna katazo la kisharia kuweka kifungu kwenye ‘Waraka wa Makubaliano’

kwamba kutakua na kiwango fulani cha mgao kila baada ya muhula fulani, mgao huu ima uwe unatolewa katika hisa za wawekezaji kwenye faida zao, iwapo kunafanyika tathmini ya ki-muhula, au utolewe kutokana na kipato cha mradi kwa minajili ya kuzihafidhi pesa hizo kwenye akiba maalum ya dharura lau kutatokea hasara katika rasilimali.

9) Hakuna katazo la kisharia kuweka kifungu kwenye 'Waraka wa Makubaliano' au 'Hati-fungani ya Mudaraba' ahadi ya kima maalum kutoka mtu wa tatu au taasisi fulani kama mchango kwa minajili ya kumjalizia hasara waliyoipata, lakini hii itakua nje ya makubaliano ya msingi ya Mudaraba. Ikimaanisha kwamba akitimiza ahadi hio aliyoitoa au asipotimiza hakutofanya 'Waraka wa Makubaliano' uathirike kwa namna yoyte ile. Kwa hio isiwapelekee wawekezaji au mudarib kukataa kutimiza vifungu vya makubaliano yao kwa hoja ya kwamba mtoa (mtu au taasisi) ahadi ya mchango hakutimiza ahadi yake.

Mbili: Baraza la 'Kongamano' lilipitia miswada mine mingine iliobeba 'Maazimio' ya warsha maalum iliyoandaliwa na 'Kongamano', miswada hii inapendekezwa kutumika kwa minajili ya kufaidika nayo kwenye miradi endelevu ya 'Wakfu' na uwekezaji wake, bila kuharibu masharti yanayojulikana katika kudumisha maendeleo ya wakfu; miswada yenyewe ni kama ifuatayo:

a) Uanzilishwaji wa 'Kampuni' ya pamoja itakayojumuisha taasisi za wakfu na wawekezaji kwa minajili ya kuamirisha na kuzalisha wakfu.
b) Kutumia mali ya wakfu kama vile nyumba au ardhi na kumpa muwekezaji atakae tumia mali zile kuzalisha zaidi kwa makubaliano na yeye awe na mgao wa faida.
c) Kuamirisha wakfu kupitia 'mkataba wa uzalishaji' kupitia Benki za Kiislamu na kupata mgao wa faida.
d) Kukodisha mali ya wakfu kama vile ardhi kwa malipo ya kitu yaani kujenga mjengo fulani juu yake au alipe pamoja na mjengo kodi ndogo.

Baraza la 'Kongamano' limepitisha kwa kauli moja 'Maazimio' ya warsha yanayosuhsiana na miswada hii na kwamba ipo haja ya utafiti wa ziada, na kuitaka 'Sekretarieti' kuandaa warsha nyingine ya kuangalia njia nyingine za uwekezaji, na kuleta mapendekezo katika kikao kijacho.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 31 (6/4)

Yanayohusiana na 'Pesa za Kilemba'[1]

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nne (4) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia kuanzia tarehe 18 – 23 Mwezi wa Mfungo Tisa, (Jumadal-Aakhira) 1408 sawa na tarehe 6 – 11 Februari, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **'Pesa za Kilemba'** na kwa mujibu wa yaliyowasilishwa imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuna aina nne ya makubaliano ya 'Pesa za Kilemba':

1) Makubaliano baina ya mmiliki wa mali na mkodishwaji wakati wa kusaini mkataba.
2) Makubaliano baina ya mkodishwaji na mmiliki wa mali katikati ya mkataba au baada ya mkataba wa kwanza kumalizika.
3) Makubaliano baina ya mkodishwaji wa mwanzo na mkodishwaji mwingine mpya ima ndanin yam da wa mkataba unaoendelea au baada ya kumalizika kwake.
4) Makubaliano baina ya mkodishwaji mpya upande mmoja na mmiliki na mkodishwaji wa mwanzo kwa upande wa pili ima kabla ya mkataba kumalizika au baada ya kumalizika.

Mbili: Wanapokubaliana Mmiliki na Mkodishwaji kwamba mkodishwaji amlipe mmiliki kiwango fulani cha pesa kinachozidi malipo ya kodi ya kila muhula, malipo haya yanaitwa sehemu nyingine kua ni 'pesa za kilemba', basi ijulikane kua hakuna katazo la kisharia kulipa pesa kama hizi lakini itabidi ziingizwe kwenye hesabu ya makubaliano ya gharama za kukodi, na lau itatokea kufusakhi mkataba basi pesa hizo zitahesabiwa ni sehemu ya kodi alizolipa.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 4, Mjeledi 3, Ukurasa 2171).

Tatu: Wanapokubaliana Mmiliki na Mkodishwaji katikati ya mda wa mkataba wao kwamba mmiliki amlipe mkodishwaji kiwango fulani cha pesa ili mkodishwaji asitishe kunufaika kwake na kile anachomiliki manufaa yake kwa mujibu wa makubaliano ya kukodishiwa, basi inajuzu kupokea pesa kama hizi, itakua ni kama mkodishwaji huyu hapa ameuza manufaa yake kwa mmiliki. Ama ikiwa mda wa mkataba umemalizika na hawakuongeza mda mwingine kwa njia yoyte ile ima kwa uwazi au kwa upenyezi au kwa njia ya kuongeza mda wa mkataba kwa kunyamaza pande mbili, basi kwa hali kama hii si halali kwake yeye kupokea pesa hizi kwa sababu mmiliki aliekodisha mali yake anakua na haki ya mali yake pale mda wa mkataba unapomalizika.

Nne: Wanapokubaliana Mkodishwaji wa mwanzo na Mkodishwaji mpya ndani ya mda wa mkataba, amuachie sehemu iliyobaki ya mda kwa malipo fulani lakini yaliyozidi kile kima alichilipa yeye mwanzo basi inajuzu kupokea pesa hizo kisharia, lakini watazingatia yale makubaliano yaliyopo baina ya mmiliki na mkodishwaji wa mwanzo pamoja na kuzingatia sheria za nchi zinazowiana na sharia za Kiislamu.

Ijulikane kua katika mikataba ya mida mirefu, kinyume na vifungu vya mkataba wa kukodisha, haijuzu kwa mkodishwaji wa mwanzo kukodisha mali aliokodishwa yeye kwa mkodishwaji mpya wala kuchukua malipo ya kodi hio ila baada kukubali mmiliki juu ya jambo hilo.

Ama ikiwa mda wa mkataba wa mkodishwaji wa mwanzo umemalizika basi haruhusiwi kumkodisha mkodishwaji mpya wala haitokua ni halali kwake yeye kupokea pesa zozote.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 32 (7/4)

Yanayohusiana na 'Kuuza Jina la Biashara na Ruhusa ya Biashara'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nne (4) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia kuanzia tarehe 18 – 23 Mwezi wa Mfungo Tisa, (Jumadal-Aakhira) 1408 sawa na tarehe 6 – 11 Februari, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **'Kuuza Jina la Biashara na Ruhusa ya Biashara'** na kwa mujibu wa yaliyowasilishwa paliibuka tofauti kadhaa zinazohusiana na utumiaji wa misamiati mipya katika maudhui haya, hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuakhirisha maamuzi ya kadhia hii kwenye kikao cha tano[1] baada ya utafiti wa ziada wa nyanja zote pamoja na kuzingatia yafuatayo:

a) Kutumia mbinu za ki-utafiti zinazojulikana kwa kuanza na utangulizi kasha kuiendea kadhia yenyewe pamoja na kuifafanua upeo wake na misamiati yote inayotumika na inayofanana nayo.
b) Kuashiria matukio ya kihistoria yanayosiana na kadhi hii na maoni na mitazamo ya wanazuoni waliotangulia na mitazamo ya kisheria katika kuzidisha kuiweka wazi kadhia hii.

Mbili: Kuiweka kadhia hii ya 'Kuuza Jina la Biashara na Ruhusa ya Biashara' kwenye maudhui pana itakayojumuisha misamiati mingine kama vile hak-miliki na hati-miliki na haki ya mvumbuzi na haki ya ubunifu na haki ya ujumbe na haki modeli za viwanda na alama za biashara ili faida ya haki zote hizi ziweze kupatikana.

Tatu: Inawezekana kwa watafiti kubahithi haki moja baada moja miongoni mwa hizo haki-tajwa hapo juu, au kuzielezea zote kwa pamoja kwenye muondo utakaokusanya haki zote hizo na zinazofanana nazo.

[1] Tizama 'Maamuzi' Namba 43 (5/5)

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 33 (8/4)

Yanayohusiana na 'Kukodisha Inayoishia Kumiliki, Murabaha (Kutia faida) kwa Anaetoa Amri ya Kununua, na Kubadilika kwa Thamani ya Sarafu'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nne (4) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia kuanzia tarehe 18 – 23 Mwezi wa Mfungo Tisa, (Jumadal-Aakhira) 1408 sawa na tarehe 6 – 11 Februari, 1988.

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuakhirisha maamuzi ya kadhia hizi: 'Kukodisha Inayoishia Kumiliki,[1] Murabaha (Kutia faida) kwa Anaetoa Amri ya Kununua,[2] na Kubadilika kwa Thamani ya Sarafu'[3], kwani ipo haja ya kuyafahamu maswala haya kwa kina kwenye kikao kijacho.

Mbili: Kuiomba 'Sekretarieti' ya Baraza la 'Kongamano' kukamilisha tafiti za maudhui mbili, na kuleta utafiti wa maudhui ya 'Kukodisha Inayoishia Kumiliki' uliowasilishwa kwenye 'Waesha ya Fiqhi' ya kwanza ilioandaliwa na 'Nyumba ya Fedha ya Kuwait' pamoja na maamuzi yaliyotokana na warsha hio iliyofanyika mwaka 1407H sawa na 1987. Aidha wataleta tafiti za 'Murabaha (Kutia faida) kwa Anaetoa Amri ya Kununua' zilizowasilishwa kwenye 'Warsha ya Mkakati wa Kuwekeza wa Benki za Kiislamu' iliyofanyika hapo Amman (Jordan) mwaka 1407H sawa na 1987 wakishirikiana na 'Taasisi ya Kiislamu ya Utafiti na kuelimisha iliyo chini ya 'Benki ya Kiislamu ya Maendeleo' na 'Taasisi ya Kifalme ya Utamaduni wa Kiislamu'.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

[1] Tizama 'Maamuzi' namba 44 (6/5), na pia namba 110 (12/4) amabayo yameelezea aina za miamala inayokubalika na iliyokatazwa ya kukodisha inayoishia kumiliki.
[2] Tizama 'Maamuzi' namba 40 – 41 (5/2 na 5/3).
[3] Tizama 'Maamuzi' namba 42 (5/4) na pia namba 115 (12/9) ambayo yameelezea namna ya kujikinga na mfumuko wa bei.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 34 (9/4)[1]

Yanayohusiana na 'Dhehebu la Ubahai'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nne (4) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia kuanzia tarehe 18 – 23 Mwezi wa Mfungo Tisa, (Jumadal-Aakhira) 1408 sawa na tarehe 6 – 11 Februari, 1988.

Kufuatia Mkutano wa Kilele wa Tano wa Nchi za Kiislamu uliofanyika nchini Kuwait mnamo 26 – 29 Jumada Ula (Mfungo Nane), 1407H sawa na 6 – 11 Februari, 1987 ambao ulililtaka 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu' litoe maoni yake kuhusu 'Madhehebu Hatarishi' yanayoendana kinyume na mafundisho ya Qur'ani Tukufu na Sunna zilizotahirika za Bwana Mtume Muhammad SAW.

Na kwa kuzingatia hatari na uvunjifu unaosababishwa na Dhebu la Ubahai kwa Umma wa Kiislamu duniani kwa kua dhehebu hili linapokea misaada kutoka taasisi maarufu zenye uadui na uislamu.

Na baada ya upembuzi wa kina kuhusu itikadi za kundi hili na kuyakinisha kwamba:

- Muanzilishi wake Bahau alidai utume na kudai kua vitabu vyake alivyovitunga ni sehemu ya 'Wahy' (ufunuo) alioteremshiwa,
- Kuwataka watu wote wamuamini yeye pamoja na kukanusha Utume wa Bwana Mtume Muhammad SAW.
- Akaongezea kua vitabu vyake vimekuja kufuta (*Naskh*) Qur'ani tukufu
- Mbali na kuitakidi kua roho zinahamia kwenye miili mingine ya viumbe (*incarnation*).

Na kwa msingi kwamba huyu Bahau alibadilisha au kuharibu kwa makusudi

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 4, Mjeledi 3, Ukurasa 2189).

mafundisho ya Fiqhi ya Kisslamu kama vile:

- Kubadilisha idadi ya sala za faradhi ma myakati zake; kazifanya tisa zinazosaliwa mara tatu; asubuhi, mchana na jioni.
- Kabadilisha mfumo wa 'Kutayammam' na kuifanya iwe ni kusema: Bismillah al-At'har al-At'har (Kwa Jina la Allah Alietakasika alietakasika).
- Kabadilisha nidhamu ya Funfa (Saumu) na kuifanya iwe ni siku kumi na tisa (19) zinazoishia sikukuu ya Nayrooz, ambayo ni tarehe 21 ya Machi kila mwaka.
- Kabadilisha Qibla na kufanya wafuasi wake wawe wanaelekea nyumba yake ilopo Akka, Palestina (iliovamiwa).
- Kaharamisha Jihadi.
- Kaondosha Sharia za Haddi
- Kalinganisha mume na mke katika mirathi.
- Kahalalisha Riba

Na baada ya kupitia tafiti zilozowasilishwa katika maudhui ya kuleta 'umoja wa Umma wa Kiislamu' ambazo pia zilitahadharisha Harakati-vunjifu zinazogawa na kupasua Umma na zinazopelekea waislamu kua mbali na dini yao au kuritadi.

Imeamuliwa yafuatayo:

Kwamba madai ya huyu Bahau ya kua eti ameteremshiwa Utume na Wahy, na madai yake kua vitabu vyake vimekuja kufuta Qur'ani tukufu na nyongeza au maharibiko aliyoyaingiza kwenye Sharia; yote haya ni upotoshaji na ukanushaji wa yaliyokuja katika dini ya Kiislamu kwa usahihi, hivyo basi Mpotoshaji na Mkanushaji wa yanayojulikana kwa uwazi katika Sharia anastahiki 'Hukmu za Kafiri' kwa mujibu wa itifaki ya wanazuoni.

Aidha 'Kongamano' linausia yafuatayo:

Taasisi za Kiislamu duniani zanatakiwa kwa nguvu zake zote kusimama kidete kupambana na Harakati-vunjifu na potofu kama hizi zinazochafua Imani sahihi na Sharia thabiti za Uislamu.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 35 (10/4)

Yanayohusiana na 'Mradi wa Kuwepesisha Fiqhi'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nne (4) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia kuanzia tarehe 18 – 23 Mwezi wa Mfungo Tisa, (Jumadal-Aakhira) 1408 sawa na tarehe 6 – 11 Februari, 1988.

Baada ya kupitia ripoti maalum iliyoandaliwa 'Kamati Mahususi' kuhusu **'Mradi wa Kuwepesisha Fiqhi'** iliopendekeza mkakati maalum wa jambo hili.

Na baada ya kupitia ripoti ya 'Kamati Ndogo' iliyoumdwa wakati wa kikao hiki kinaendelea kupitia na kutoa mapendekezo yake juu ya suala hili la 'Uwepesishaji wa Fiqhi' na kuitaka 'Sekretarieti' kusimamia utekelezaji wake;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuupitisha 'Mpango-Mkakati ulioandaliwa na kuwasilishwa na 'Kamati Mahususi inayosimamia Mradi wa wa Kuwepesisha Fiqhi', pamoja na kuzingatia marekebisho yalitopendekezwa, na kuitaka 'Sekretarieti' kusimamia utekelezaji wake.

Allah Ndie Mwenye Kutuwafikia

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 36 (11/4)

Yanayohusiana na 'Mradi wa Saiklopidia ya Fiqhi ya Uchumi'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nne (4) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia kuanzia tarehe 18 – 23 Mwezi wa Mfungo Tisa, (Jumadal-Aakhira) 1408 sawa na tarehe 6 – 11 Februari, 1988.

Baada ya kupitia ripoti iliyoandaliwa na 'Kamati Maalum ya Kuanda Mpango-Tekelezi wa Mradi wa Saiklopidia ya Fiqhi ya Uchumi' mpango unaounaopendekeza pia hatua zifaazo kuchukuliwa kuutekeleza mradi huu pamoja na jopo la wataalam watakaosimamia utekelezaji wa mradi huu.

Na baada ya kupitia ripoti ya 'Kamati Ndogo' iliyoundwa wakati wa kikao hiki kinaendelea kupitia na kutoa mapendekezo juu ya utekelezaji wa **'Mradi wa Saiklopidia ya Fiqhi ya Uchumi'** na kuitaka 'Sekretarieti' kusimamia utekelezaji wake na marekebisho yaliopendekezwa;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuupitisha 'Mpango-Mkakati ulioandaliwa na kuwasilishwa na 'Kamati Mahususi inayosimamia **Mradi wa Saiklopidia ya Fiqhi ya Uchumi'**, pamoja na kuzingatia marekebisho yalitopendekezwa, na kuitaka 'Sekretarieti' kusimamia utekelezaji wake.

Allah Ndie Mwenye Kutuwafikia

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu

zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 37 (12/4)

Yanayohusiana na 'Mradi wa Muongozo wa Misingi ya Ki-fiqhi'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nne (4) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia kuanzia tarehe 18 – 23 Mwezi wa Mfungo Tisa, (Jumadal-Aakhira) 1408 sawa na tarehe 6 – 11 Februari, 1988.

Baada ya kupitia ripoti iliyoandaliwa na 'Kamati Maalum ya Kuanda Muongozo wa Misingi ya Ki-fiqhi';

Na baada ya kupitia ripoti ya 'Kamati Ndogo' iliyoundwa wakati wa kikao hiki kinaendelea kupitia na kutoa mapendekezo juu ya utekelezaji wake pamoja na kupendekeza 'awamu saba za Utekelezaji wake na Mswada wa mwisho;

Na baada ya kutathmini maoni mbalimbali yanayohusiana na 'Awamu ya Kwanza na ya Tano,

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuupitisha 'Mswada wa Mwisho' wa Mradi wa Muongozo wa Misingi ya Ki-fiqhi pamoja na awwamu zake saba.

Mbili: Kuitaka 'Sekretarieti' kusimamia utekelezaji wake, na kuchagua katika rai mbili zilizotolewa kuhusiana na awamu ya kwanza na awamu ya tano katika awamu za utekelezaji wake.

Allah Ndie Mwenye Kutuwafikia

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu

zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 38 (13/4)[1]

Yanayohusiana na 'Mbinu za Kupambana na Miporomoko ya Maadili, Nyanja za Umoja wa Kiislamu na Namna ya Kufaidika nazo, Kusilimisha Mifumo ya Elimu katika Nchi za Kiislamu'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nne (4) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia kuanzia tarehe 18 – 23 Mwezi wa Mfungo Tisa, (Jumadal-Aakhira) 1408 sawa na tarehe 6 – 11 Februari, 1988.

Kwanza:

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na '**Mbinu za Kupambana na Miporomoko ya Maadili'** tafiti ambazo zilielezea jinsi ulimwengu unavyohangaishwa na miporomoko ya maadili ambayo imeenea kwa kasi hasa katika nchi za Kiislamu kwa kiwango kisichomridhi Allah wala hayawiani na nafasi ya Umma huu kama viongozi wa dunia wa kuwaongoza binadamu kwenye Imani sahihi na maadili yaliyo mema.

Na kuwiana na malengo makuu ya Uislamu yaliyojikita katika usimamizi wa maadili mema ambayo ni sehemu nyeti ya Dini hii ya Kiislamu, Dini ambayo haikamiliki utiifu wake ila kwa kufuata maagizo yake yote yakiwemo utelezaji wa Sharia na usimamiaji wa maadili mema katika mfumo mzima wa maisha.

Imependekezwa yafuatayo:

a) Kufanya iwezekanavyo kusahihisha na kutilia nguvu msukumo wa ki-itikadi kwa kuieneza kwa upana kabisa ili zijitokeze athari zake katika maisha ya watu.
b) Kufanya juhudi za makusudi kuvisafisha vyombo vyote vya habari katika ulimwengu wa Kiislamu vinavyosikiwa na kusomwa na kutizamwa pamoja na matangazo ya biashara, kuvisafisha na itikadi potofu na kila aina ya

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 4, Mjeledi 3, Ukurasa 2354, 2487).

maasia yanayomkera Allah au mambo yanayoamsha hisia za kijinsia au kusababisha upotokaji wa kifikra au kuporomosha maadili.

c) Kuweka mikakati maalum ya kulinda maadili na turathi za Kiislamu pamoja na kuweka pingamizi dhidi ya silka za kimagharibi na kila aina ya uvamizi wa kifikra na kiutamaduni unaokinzana na silka halisi za Kiislamu. Ipo haja pia ya kuweka usimamizi wa karibu katika harakati za watalii wanaokuja kutembea nchi za Kiislamu ili shughuli hizo za utalii zisitumike kama kisingizio katika kubomoa maadili ya Kiislamu.
d) Kuielekeza mifumo na mitaala ya elimu katika kuandaa kizazi bora kitakachoshikamana na maadilio ya Kiislamu, masomo yafundishwe kwa mitazamo ya Kiislamu na kulipatia somo la Dini ya Kiislamu nafasi kubwa na murwa kwenye mitaala ya elimu katika awamu zote kwa lengo la kuidhatiti Imani na itikadi za Kiislamu na kuwajengea kizazi kipya misingi ya maadili mema, mbali na kutia bidii ili Umma huu ushike nafasi za uongozi katika elimu duniani.
e) Kujenga nidhamu sahihi za familia na kuwepesisha mahitajio ya ndoa na kulea watoto wa kike na wa kiume malezi yaliokua mema ili kizazi cha baadae kiwe ni kizazi chema chenye kufahamu maana halisi ya kumuabudu Allah, kizazi ambacho kitasimamia shughuli za uernezaji na usambazaji wa Uislamu duniani. Mwanamke aandaliwe awe mama anaefahamu nafasi yake katika kukuza na kuelekeza Umma kwa mujibu wa Sharia ya Kiislamu, na kuepukana na tattizo la kuingiza mayaya (hasa wasiokua waislamu) majumbani kama walezi wa kizazi cha baadae.
f) Kuandaa mbinu kabambe zitakazosimamia mifumo ya malezi ya Kiislamu ili kizazi kipya kiinukie katika kushikamana na misingi ya Kiislamu na maadili yake pamoja na kufahamu majukumu yake kwa Mola wake na Umma wake. Kizazi kitakachoepukana ‘Mvungu wa Kiroho’ amabao unapelekea kuangukia kwenye vilevi na mihadarati inayosababisha miporomoko ya maadili. Ziwepo njia mbadala za kuwashughulisha vijana katika mambo muhimu yatayowafaa na kuwanufaisha katika maisha yao pamoja na kuwawekea burudani zilizo halali, mashindano ya michezo, riadha na mifano wake katika mazingira rafiki ya Kiislamu.

Pili:

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye ‘Kongamano’ zinazohusiana na ‘Nyanja za umoja wa Kiislamu na njia za kufaidika nao’ na kwa msingi wa mshikamano wa mataifa ya Kiislamu na Umma wa Kiislamu; msingi ambao ni imara kabisa wenye uwezo wa kujenga mshikamano unaotarajiwa na kujenga utamaduni wa kibinadamu wa kuweza kupambana na maovu na changamoto za usasa na kuleta heshima na maendeleo.

Na kwa kua muungano wa Kiislamu ni chombo imara cha kudumu cha kuleta uwiano miongoni mwa nchi za Kiislamu katika kuwaletea maendeleo kwenye nyanja mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kadhalika, pia katika kuleta mahusiano mazuri ya kusaidiana na kunusuriana na kuoneana huruma ili kuufikisha Umma huu katika ngazi za juu za kimaendeleo.

Imependekezwa tena yafuatayo:

a) Kuilinda Imani ya kiislamu na kuitanguliza katika uhalisia wake, na kutahadharisha na kila lenye kuidhoofisha au kuichafua au kuingiza mipasuko katika safu za Waislamu na kuwafanya wakatane au wachukiane.
b) Kusisitiza nafasi ya ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu” kuendelea na kazi za kiutafiti katika mas’ala mbalimbali ya Kifiqhi kwa malengo ya kupambana na changamoto mbalimbali za kifikra zilizoibuka katika zama hizi na kuifanya Fiqhi ya kiislamu kua ni kimbilio na kitatuzi kwa kila mwenye tatizo pamoja na kuifanya Fiqhi kua ndio ufunguzi wa maendeleo ya Umma na hivyo kuzifanya nchi za Kiislamu kuitumia Fiqhi kama nyenzo za utungaji wa Sheria zake.
c) Ulazima wa kuowanisha nchi za Kiislamu na kuleta ushirikiano wa karibu katika nyanja za elimu na malezi na kushinikiza utamaduni wa kifikra ulioletwa na mafundisho ya Uislamu kwa lengo la kuandaa vizazi vya baadae watakao kua na mshikamano na umoja katika maisha yao ya kiibada, watakao kua karibu karibu katika mitazamo yao kifikra wakishirikiana kwa ukaribu katika kujinaki kwao na utamaduni huu.
d) Kutoa nafasi za kipaombele kwa juhudi za kiutafiti katika nyanja mbalimbali za kielimu na sayansi, na kutenga kwa uchache asilimia 1% katika kipato cha nchi zielekezwe katika juhudi za kiutafiti pamoja na kuanzisha maabara za kisayansi zenye kushirikiana miongoni mwa vyuo vikuu vya Kiislamu.
e) Kufanya kazi kwa karibu na vyuo vikuu vya Kiislamu kwa minajili ya

kuandaa programu za masomo zitakazosheheni nyanja mbalimbali za Fiqhi zitakazofanyiwa tafiti yakinifu, na kuunda kamati kuu itakayokusanya wanafikra waislamu watakaofuatilia tafiti hizi na kuziidhinisha na pia kuweka zawadi maalum kwa tafiti zitakazofika viwango vya ubora wa hali ya juu.

f) Vyombo vya habari vya aina zote katika nchi za Kiislamu; vya kusikilizwa na vya kusomwa na vya kutazamwa ni vyombo venye malengo ya kujenga Ustahiki wa Allah wa kuabudiwa na kueneza kheri na maadili kupitia vyombo hivo, aidha vitumike kupambana fikra hatarishi na potofu na uporomokaji wa maadili yanaypinda na njia ya sawa, na kusaidia kuviunganisa vyomvo hivi.
g) Kusimamisha nidhamu ya uchumi wa Kiislamu ambao hautakua tegemezi wa mashariki wala wa magharibi, bali uwe ni mfumo halisi wa uchumi Kiislamu, pamoja na kuanzisha muungano wa kibiashara baina ya nchi za Kiislamu; muungano ambao waislamu watapata fursa za kuzalisha na kuuza bidhaa zao mioingoni mwao; hivyo kuondoa haja ya kununua bidhaa kutoka sehemu nyingine, kwani uchumi ni sehemu muhimu ya ukuaji wa jamii na kuimarika na njia mojawapo ya kuleta umoja baina ya Umma wa Kiislamu.

Tatu:

Kutokana na kwamba kusilimisha mifumo ya elimu katika nchi za Kiislamu ni dharura isiyoepukika kwa minajili ya kujenga kizazi cha sasa na baadae kikamilifu katika fikra zake na ufahamu na maadili na matendo;

Imependekezwa tena yafuatayo:

Kuzifanya elimu za sayansi zote zinaendana na mitazamo ya Kiislamu; hivyo basi waandaaji wa mitaala watatakiwa wakati wanapoandaa mitaala ya sayansi kuhakikisha kwamba inajikita kwneye misingi na malengo makuu ya Kiislamu. Ili kufikia malengo ya kusilimisha elimu ya sayansi; yazingatiwe yafuatayo:

a) Aakida (itikadi) ya Kiislamu iwe ndio nyenzo za fikra na filosofia ambapo mtazamo mpana wa hii dunia na binadamu na maisha ya hapa duniani yanaunganishwa na Muumbaji wake pamoja na kumjulishsa huyu binadamu na uhusiano wake na Muumba wake na uhusiano wake na hii dunia na

uhusiano wake na mazingira na jamii yake.

b) Kuweka tasawuri ya Kiislamu kuwa ni kioo katika uandaaji wa elimu za sayansi-jamii na elimu za uchumi na elimu za siasa pamoja na kudhihirisha nadharia za Kiislamu zinazowiana na maumbile ya binadamu na zinazomfanya binadamu kumtambua Muumbaji wake katika kila kitu, aidha wakati wa kuweka mitaala kama hii kuwepo ushirikiano wa karibu na taasisi za Kiislamu zinazofanya kazi kama hizi; kama vile: 'Taasisi ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' na 'Shirika la Kiislamu la Elimu-Malezi, Sayansi na Utamaduni' (ISESCO).
c) Kubainisha ufisidifu uliopo katika mifumo ya kisekula inayokinzana na mafundisho sahihi na halisi ya Uislamu pamoja na kubainisha ufisisdifu unaopatikana katika elimu za uchawi na uganga na elimu zilizoharamishwa kwatika Uislamu kama zile zinazofundisha ufuska na uchafu.
d) Kuandika upya historia ya elimu na sayansi na kubainisha maendeleo yaliopitia elimu hizo pamoja na kuelezea michango ya Waislamu katika kila nyanja ya elimu hizo, na ikiwezekana kuzisafisha kutokana na nadharia potofu za kimagharibi zilizoingizwa ambazo zilipotosha mwenendo na muelekeo wa elimu hizo. Aidha kujaribu kurudisha mitazamo ya tasnifu za elimu na misingi ya mbinu za utafiti kwa mujibu wa mtazamo wa Kiislamu. Taasisi za ki-utafiti na taasisi za tasnia ya uchumi wa Kiislamu katika nchi za Kiislamu ziznatakiwa kua mbele kuongoza juhudi hizi.
e) Kurudisha uwiano baina elimu za sayansi zinazotizama ulimwengu, mwanadamu na maisha na Muumba wa vitu hivi; Mwanasayansi anapofanya utafiti wake aone kwamba vitu hivi-tajwa yaani ulimwengu, mwanadamu na maisha ni Sanaa na uhodari na ubunifu wa Muumba wa kila kitu.
f) Kuweka vidhibiti na misingi inayotokana na mafundisho ya Uislamu na inayoambatana na malengo yake makuu katika uandaaji wa mitaala ya elimu za sayansi na kuzidhihirisha kasoro zinazopatikana katika mitaala ya kimagharibi ambayo imekuja kuleta mpasuko mkubwa baina ya elimu ya sayansi na dini, aidha kuelezea pale mitaala ya kimagharibi ilipopinda kwenye elimu za sayansi-jamii na historia a uchumi.

Ikumbukwe kua zipo jitihada zinazochukuliwa za kusilimisha mifumo na mitaal ya elimu mbalimbali, Taasisi ya Kimataifa ya Fikra za Kiislamu (IIIT) iko mstari wa mbele katika kulifanyia kazi jambo hili kwa kuweka mipango-mkakati na taratibu

za utekelezaji wake kupitia warsha na tafiti wanazozifanya. Taaasisi hii itumike kama kigezo katika kuliendea zoezi hili la ‘Kusilimisha Mifumo na Mitaala ya Elimu za Sayansi na Elimu za Sayansi-jamii’.

Allah Ndie Mwenye Kutuwafikia

≅≅≅

Maamuzi na Maazimio ya Kikao cha Tano ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Kuwait, Dola ya Kuwait

1 – 6 Mfungo Nane (Jumadal Ula), 1409

10 – 15 Disemba, 1988

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 39 (1/5)[1]

Yanayohusiana na 'Upangaji wa Uzazi'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tano (5) kilichofanyika mji wa Kuwait, Dola ya Kuwait kuanzia tarehe 1 – 6 Mwezi wa Mfungo Nane, (Jumadal-Ula) 1409 sawa na tarehe 10 – 15 Disemba, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti kutoka kwa wajumbe na wataalamu zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Upangaji wa Uzazi,** na kusikiliza mijadala na hoja za wataalamu kuhusiana na mada hio.

Na kutokana na kwamba malengo makuu ya ndoa kwa mujibu wa Sharia ya Kiislamu ni kuzaa na kulinda jinsi ya binadamu, na kwa maana hio haijuzu kuvuruga lengo hilo, kwani kulivuruga lengo hilo ni kinyume kabisa na makusudio ya Sharia na maelekezo yake yanayozingatia uongezaji wa kizazi na kulinda jinsi ya binadamu kua ni mojawapo wa malengo makuu ya Sharia ya Kiislamu.

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Haijuzu kutunga kanuni inayowanyima wanandoa uhuru wao wa kuzaa.

Mbili: Ni haramu kuchomoa uwezo wa mume au wa mke wa kuzaa, yaani kuhasi au kutasisha ila ikiwa kuna dharura inayokubalika Kisharia.

Tatu: Inajuzu kuweka nidhamu ya uzazi wa mpangilio wa mda:

- Kwa lengo la kurefusha awamu za kuzaa au kusimamisha uzazi kwa kipindi fulani iwapo kuna dharura ya kufanya hivo inayokubalika Kisharia na pia kwa kushauriana ridhaa za pande mbili; mume na mke, na

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 4, Mjeledi 1, Ukurasa 73.

- kwa sharti hatua kama hio isisababishe madhara mengine.
- Njia zitakazotumika ziwe zinakubalika Kisharia
- Isipelekee kukatika kwa kizazi au kutobeba ujauzito baadae.

Allah ni Mjuzi zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 40 & 41 (2/5 & 3/5)[1]

Yanayohusiana na 'Utekelezaji wa Ahadi na Muamala wa 'Murabaha kwa anaetoa amri ya manunuzi (*Aamir Bi al-Shirai*)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tano (5) kilichofanyika mji wa Kuwait, Dola ya Kuwait kuanzia tarehe 1 – 6 Mwezi wa Mfungo Nane, (Jumadal-Ula) 1409 sawa na tarehe 10 – 15 Disemba, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti kutoka kwa wajumbe na wataalamu zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na mada mbili hizi **Utekelezaji wa Ahadi na Muamala wa 'Murabaha kwa anaetoa amri ya manunuzi (*Aamir Bi al-Shirai*)** na kusikiliza mijadala na hoja za wataalamu kuhusiana na mada hizo;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Miamala ya biashara ya 'Murabaha' kwa anaetoa amri ya kununua inajuzu iwapo bidhaa-lengwa ipo mikononi mwa anaetakiwa kuuza na angeweza kuikabidhi mara tu wanapokubaliana, na pia atakua ni mwenye kubeba dhamana yoyote lau bidhaa hio husika haikuwasili au ina kasoro iliyojificha na mfano wake, pamoja na kuzingatia kua masharti yote ya biashara yametimia na hakuna kikwazo chochote kinachozuia muamala huo ukamilike.

Mbili: Kwa mujibu wa Sharia; Ahadi inayotolewa ima kwa anaenunua au kwa anaeuza inakua yenye kumlazimu mtoa ahadi hio ila itokeapo dharura isioepukika, lakini hata hivyo iwapo muahidiwa ataingia kwenye gharama au hasara kwa sababu mtoa ahadi ameshindwa kutimiza ahadi yakebila dharura inayokubalika Kisharia basi itamlazimu mtoa ahadi huyo kulipa gharama zozote zilizojitokeza au atimize ahadi aliyoitoa.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 5, Mjeledi 2, Ukurasa 754, 965).

Tatu: Inajuzu ahadi ya pamoja ya pande zote mbili katika miamala ya ‘Murabaha’ kwa sharti kwamba kila upande una nafasi ya ‘Hiari’ yaani hiari ya kufuta ahadi, kwani miamala ya ‘Murabaha’ ni sawa na miamala ya biashara ambapo muuzaji anatakiwa awe na umiliki kamili wa kile anachotaka kukiuza, bila ya hivo atakua ameeingia katika katazo la Mtume Muhammad SAW la mtu kuuza asichomiliki.

Imeonekana kua Benki nyingi za Kiislamu zinajihusisha na miamala ya kulipia manunuzi kwa njia ya ‘Murabaha’; **hivyo basi imependekezwa yafuatayo:**

Moja: Benki za Kiislamu zinashauriwa kujitanua zaidi katika miamala yake kwenye nyanja za kukuza uchumi kama vile uanzilishaji wa miradi ya viwanda na miradi ya biashara au miradi ya ‘Musharaka’ na miradi ya ‘Mudaraba’.

Mbili: Aidha Benki za Kiislamu zinashauriwa kutathmini njia za uhakika za utekelezaji wa miamala ya ‘Murabaha’ na kuweka misingi imara itakayozuwia mitikisiko ya utekelezaji na itakayosaidia kuchunga taratibu za Kisharia zinazohusiana na miamala hii.

Allah ni Mjuzi zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 42 (4/5)[1]

Yanayohusiana na 'Kubadilika kwa Thamani ya Sarafu'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tano (5) kilichofanyika mji wa Kuwait, Dola ya Kuwait kuanzia tarehe 1 – 6 Mwezi wa Mfungo Nane, (Jumadal-Ula) 1409 sawa na tarehe 10 – 15 Disemba, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti kutoka kwa wajumbe na wataalamu zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Kubadilika kwa Thamani ya Sarafu** na kusikiliza mijadala na hoja za wataalamu kuhusiana na mada hio;

Na baada ya kupitia 'Maamuzi ya Kongamano' namba 21 (9/3) ya kikao cha tatu kwamba: 'Hukumu za fedha za noti: Ni fedha zinazokubalika zenye thamani kamili, fedha hizi zinabeba hukmu zote za 'Dhahabu' na 'Fedha' zinazohusiana na hukumu za: Riba, Zaka, Madeni na hukumu nyenginezo';

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo: Ulipaji wa madeni yaliyothibiti kwa sarafu fulani inatakiwa yalipwe kwa sarafu ileile, kwani haijuzu kufungamanisha madeni na viwango vya bei inavyobadilika.

Allah ni Mjuzi zaidi

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 5, Mjeledi 3, Ukurasa 1609).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 43 (5/5)[1]

Yanayohusiana na 'Haki-Miliki'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tano (5) kilichofanyika mji wa Kuwait, Dola ya Kuwait kuanzia tarehe 1 – 6 Mwezi wa Mfungo Nane, (Jumadal-Ula) 1409 sawa na tarehe 10 – 15 Disemba, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti kutoka kwa wajumbe na wataalamu zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Haki-Miliki** na kusikiliza mijadala na hoja za wataalamu kuhusiana na mada hio;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Jina la Biashara, Anwani ya Biashara, Alama ya Biashara, Utungaji, Uvumbuzi na Ubunifu hizi zote ni Haki-miliki za watu wake, katika desturi za zama hizi Haki-miliki hizi zina thamani ya pesa wanazokubaliana, hivyo basi haijuzu kwa mwingine kuzinyakua au kuzivuruga.

Mbili: Inafaa kwa mmiliki wa haki-miliki hizi kuzitumia haki zake kama vile kuziuza na mfano wake na pakikosekana aina yoyote ya udanganyifu au ghushi.

Tatu: Haki za Utungaji na Uvumbuzi na Ubunifu zinahifadhiwa kwa wahusika wake, na wahusika wake tu ndio wenye haki ya kufanya wanachotaka katika miliki zao haijuzu kwa mwengine kuzivuruga haki hizi.

Allah ni Mjuzi zaidi

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 5, Mjeledi 3, Ukurasa 2267).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 44 (6/5)[1]

Yanayohusiana na 'Kukodi Inayoishia Kumiliki'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tano (5) kilichofanyika mji wa Kuwait, Dola ya Kuwait kuanzia tarehe 1 – 6 Mwezi wa Mfungo Nane, (Jumadal-Ula) 1409 sawa na tarehe 10 – 15 Disemba, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti kutoka kwa wajumbe na wataalamu zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Kukodi Inayoishia Kumiliki** na kusikiliza mijadala na hoja za wataalamu kuhusiana na mada hio;

Na baada ya kupitia 'Maamuzi ya Kongamano' namba 13 (1/3) ya kikao cha tatu kuhusiana na majibu ya masuali ya Benki ya Kiislamu ya Maendeleo (BKM – IsDB) kwenye ibara (B) inayohusu shughuli za ukodishwaji wa vifaa;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kujikita katika miamala miwili tu miongoni mwa miamala ya ukodishwaji inayoishia kumiliki, nayo ni:

- Muamala wa kuuza kwa malipo ya pole pole, kuwepo dhamana za kuridhisha.
- Muamala wa kukodisha ambapo mmiliki ambae ni mkodishaji atampatia mkodishwaji baada ya kukamilisha malipo ya kodi waliokubaliana katika mda waliokubaliana nafasi ya moja katika mambo yafuatayo:
    - Kuongeza muda wa kukodi tena.
    - Kusitisha mkataba wa kukodi na mmiliki kuregeshewa mali yake.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 5, Mjeledi 4, Ukurasa 2593).

- Kununua kile kilichokodishwa kwa thamani iliyopo sokoni baada ya kumalizika kwa mda wa kukodi.

Mbili: Zipo njia nyingine za kukodi zinazoishia kumiliki lakini imeamuliwa kua zitatizamwa kwenye kikao kijacho, baada ya kupata mifano ya mikataba inayotumika na kwa kushirikiana na Benki za Kiislamu kuzifanyia tathmini ili kufikia maamuzi muwafaka.

Allah ni Mjuzi zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 45 (7/5)

Yanayohusiana na 'Kugharimia Ujenzi wa Nyumba na Kuzinunua'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tano (5) kilichofanyika mji wa Kuwait, Dola ya Kuwait kuanzia tarehe 1 – 6 Mwezi wa Mfungo Nane, (Jumadal-Ula) 1409 sawa na tarehe 10 – 15 Disemba, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti kutoka kwa wajumbe na wataalamu zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Kugharimia Ujenzi wa Nyumba na Kuzinunua** na kusikiliza mijadala na hoja za wataalamu kuhusiana na mada hio;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Maamuzi kamili kuhusiana na kadhia ya **Kugharimia Ujenzi wa Nyumba na Kuzinunua** yatatolewa kwenye kikao cha sita ili kutoa mda wa ziada wa tabhithi na utafiti.[1]

Allah ndie Mwenye Kutuwafikia

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 5, Mjeledi 4, Uk. 2773 na Toleo 6. Mjeledi 1, Uk. 81).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 46 (8/5)

Yanayohusiana na 'Kuweka Mipaka ya Faida (*Bei-elekezi*) kwa Wafanyi-Biashara'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tano (5) kilichofanyika mji wa Kuwait, Dola ya Kuwait kuanzia tarehe 1 – 6 Mwezi wa Mfungo Nane, (Jumadal-Ula) 1409 sawa na tarehe 10 – 15 Disemba, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti kutoka kwa wajumbe na wataalamu zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Kuweka Mipaka ya Faida kwa Wafanyi-Biashara** na kusikiliza mijadala na hoja za wataalamu kuhusiana na mada hio;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Msingi unaokubalika Kisharia ni kwamba watu wako huru katika biashara zao; kuuza na kununua na kufanya wanavyotaka katika wanavyomiliki na mali yao, hii ni kutokana neno la Allah katika Surat al-Nisaa: 29

(يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ لاَ تَأْكُلُواْ أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ إِلاَّ أَن تَكُونَ تِجَارَةً عَن تَرَاضٍ مِّنكُمْ وَلاَ تَقْتُلُواْ أَنفُسَكُمْ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا)

> "*Enyi mliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na mkafuata sheria Yake kivitendo! Si halali kwa baadhi yenu kula mali ya wengine kati yenu pasi na haki, isipokuwa ikiwa itaambatana na Sheria na chumo la halali litokanalo na kuridhiana baina yenu*".[1]

Mbili: Hakuna mipaka ya faida iliyowekwa na Sharia ambayo Mfanyi-biashara anatakiwa kuizingatia, bei zilizopo sokoni na aina ya bidhaa yenyewe na Mfanyi-biashara mwenyewe ndivyo vitakavyoamua bei kwa kuzingatia maadili ya Kiislamu ya huruma na kuwepesishia watu katika

[1] Surat al-Nisaa: 29.

maisha yao.

Tatu: Maagizo ya Kisharia yapo kwenye kuhakikisha kwamba miamala ifanyike katika taratibu na njia zilizosalimika na uharamu na udanganyifu na ghushi, aidha mfanyi-biashara anatakiwa kua mbali kufungia bidhaa (hording) ili zipande bei, hii inadhuru waja.

Nne: Kiongozi/Mtawala hatakiwi kuingilia suala hili la kuweka mipaka ya faida (bei elekezi) ila pale anapohisi kua kuna ukiukwaji wa wazi wa maadili ya biashara, basi hapo ataruhusiwa kuingilia kwa lengo la kusimamisha haki na uadilifu na kuondosha sababu zinazopelekea mifumuko ya bei kiholela.

Allah ni Mjuzi zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 47 (9/5)[1]

Yanayohusiana na 'Desturi ('*Urf*)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tano (5) kilichofanyika mji wa Kuwait, Dola ya Kuwait kuanzia tarehe 1 – 6 Mwezi wa Mfungo Nane, (Jumadal-Ula) 1409 sawa na tarehe 10 – 15 Disemba, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti kutoka kwa wajumbe na wataalamu zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Desturi** na kusikiliza mijadala na hoja za wataalamu kuhusiana na mada hio;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Ibachokusudiwa katika **Desturi** hapa ni yale mambo yaliyozoweleka katika jamii na wanakubaliana nayo mambo yenyewe yanaweza kua ni maneno au vitendo au kutofanya vitu fulani, mambo haya yanaweza kua yanazingatiwa Kisharia au hayazingatiwi.

Mbili: Ikiwa Desturi hii ni ya baadhi ya watu basi inazingatiwa kwa wale watu husika, na ikiwa ni ya watu wote basi inazingatiwa kua ni watu wote.

Tatu: Desturi inayozingatiwa Kisharia ni ile iliyotimiza masharti yafuatayo:

a) Isiwe inakhalifiana na Sharia, Desturi yoyote inapokhalifiana na Sharia au kwenda kinyume chake basi inakua ni Desturi fasidi (mbaya).
b) Iwe Desturi hio husika inatumika na inajulikana.
c) Iwe Desturi hio husika ipo wakati utekelezaji wa muamala.
d) Iwe Desturi hio husika haikukataliwa na wanaoamiliana, wakiikataa basi haitozingatiwa.

Nne: Haitakiwi kwa Mwana-Fiqihi; Mufti au Kadhi, kubaki kwenye vitabu

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 5, Mjeledi 4, Uk. 2921).

peke yake bila kutizama mabadiliko ya mila na desturi.

Allah ni Mjuzi zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 48 (10/5)[1]

Yanayohusiana na 'Utekelezaji wa Hukumu za Sharia ya Kiislamu'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tano (5) kilichofanyika mji wa Kuwait, Dola ya Kuwait kuanzia tarehe 1 – 6 Mwezi wa Mfungo Nane, (Jumadal-Ula) 1409 sawa na tarehe 10 – 15 Disemba, 1988.

Baada ya usikivu makini wa tafiti kutoka kwa wajumbe na wataalamu zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Utekelezaji wa Hukumu za Sharia ya Kiislamu** na kusikiliza mijadala na hoja za wataalamu kuhusiana na mada hio;

Na kwa kuzingatia kua 'Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu' liloibuka kutokana na matakwa ya kheri kutoka 'Kikao cha tatu cha Muungano wa Nchi za Kiislamu kilichofanyika huko Makkah al-Mukarramah, kwa lengo la kutafuta mafumbuzi ya Kisharia ya matatizo yanayowakabili Umma wa Kiislamu, na kudhibiti kadhia za Waislamu kwa mujibu wa Sharia ya Kiislamu, na kuondoa pingamizi zinazokwaza utekelezaji wa Sharia ya Kiislamu na kuweka mazingira salama ya utekelezaji wake, yote haya kwa kutambua Uungu wa Allah katika utekelezaji wa Hukumu zake na kuifanya Sharia yake iwe juu, pia kupitia chombo hiki, inalenga kuondosha migongano na ukinzani miongoni mwa viongozi wan chi za Kiislamu na raia zao, na kuondosha kila aina ya mitafaruku na chuki ma uhasama katika nchi za Kiislamu ili Amani na utulivu utande katika miji ya Waislamu.

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

a) Wajibu wa kwanza kiongozi anaetawala waislamu ni kutekeleza Sharia ya Kiislamu.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 5, Mjeledi 4, Uk. 3471).

b) Kuzitaka serikali zote za nchi za Kiislamu kuharakisha utumiaji na utekelezaji wa Sharia ya Kiislamu na kuifanya kua ndio chimbuko la hukumu zote katika nyanja za maisha.

c) Kuzitaka jamii zote za Kiislamu raia na dola zao kushikamana na Dini ya Allah na kuitekeleza Sharia Yake kwa kua Dini hii ni Imani na akida, na ni Sharia na Hukumu, na ni maadili na mfumo mzima wa maisha.

Pia imeusiwa yafuatayo:

a) 'Kongamano' kuendelea na jitihada zake za kufanya tafiti za kina katika nyanja za utekelezaji wa Sharia ya Kiislamu na kufuatilia yale yanayofanyiwa kazi katika nchi za Kiislamu.

b) Kuziowanisha juhudi za 'Kongamano' na zile za Taasisi nyingine zinazofanya kazi katika maeneo ya utekelezaji wa Sharia ya Kiislamu, aidha 'Kongamano' lisaidie kuandaa mipangilio na taratibu zitakazosaidia kuondoa pingamizi au utata dhidi ya utekelezaji wa Sharia ya Kiislamu katika nchi za Kiislamu.

c) Kuzikusanya kanuni zilizotungwa kutokona na Sharia ya Kiislamu katika nchi mbalimbali za Kiislamu na kufaidika nazo.

d) Kutoa wito wa kurekebisha mitaala ya elimu na vyombo vya habari mbalimbali na kuzielekeza katika kufanikisha lengo la utekelezaji wa Sharia ya Kiislamu, na kuandaa kizazi kipya kitakachoinukia na kupenda kutawaliwa kwa Sharia ya Allah.

e) Kutanua wigo wa kuandaa wasomi na wataalamu katika fani za sharia, uwakili na uanasheria ili kutengeneza jopo muafaka litakalosimamia utekelezaji wa Sharia ya Kiislamu.

Allah ndie Mwenye Kutuwafikia

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 49 (11/5)

Yanayohusiana na 'Kamati ya Kiislamu ya Kimataifa ya Kanuni'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tano (5) kilichofanyika mji wa Kuwait, Dola ya Kuwait kuanzia tarehe 1 – 6 Mwezi wa Mfungo Nane, (Jumadal-Ula) 1409 sawa na tarehe 10 – 15 Disemba, 1988.

Baada ya kupitia waraka maalum unaohusiana na 'Kanuni ya msingi-pendekezi' ya kuanzishwa kwa **Kamati ya Kiislamu ya Kimataifa ya Kanuni** iliyohaulishwa kutoka kikao cha kumi na saba (17) cha mawaziri wan chi za nje wan chi za Kiislamu kilichofanyika hapo Amman, nchini Jordan, Azimio namba (17/45 - S);

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Kuwafiki kuusoma mswada wa 'Kanuni ya msingi-pendekezi' ya kuanzishwa kwa **Kamati ya Kiislamu ya Kimataifa ya Kanuni** na kazi za kamati hii zitakua ni sehemu za shughuli za 'Kongamano'

Allah ndie Mwenye Kutuwafikia

≅≅≅

Maamuzi na Maazimio ya Kikao cha Sita (6) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Jeddah, Falme ya Saudi Arabia

17 – 23 Shaaban, 1410

14 – 20 Machi, 1990

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 50 (1/6)

Yanayohusiana na 'Kugharimia Ujenzi wa Nyumba na Kuzinunua'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha sita (6) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 17 – 23 Mwezi wa Shaaban, 1410 sawa na tarehe 14 – 20 Machi, 1990.

Baada ya usikivu makini wa tafiti kutoka kwa wajumbe na wataalamu zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Kugharimia Ujenzi wa Nyumba na Kuzinunua** na kusikiliza mijadala na hoja za wataalamu kuhusiana na mada hio;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Nyumba ni miongoni mwa mahitajio ya msingi ya mwanadamu, hivyo basi inatakiwa itafutwe kwa njia na taratibu zinazokubalika Kisharia kutokana na mali yaliokua ni ya halali, njia zinazotumika kupitia mikopo ya Benki za Nyumba na mfano wake, mikopo inayolipwa kwa faida iwe nyingi au kidogo, basi ijulikane kua huo Muamala wa Riba ulioharamishwa.

Mbili: Zipo njia nyingine nyingi tu za kujipatia nyumba na kumiliki ambazo zinakubalika Kisharia (ukiachia kukodi) nazo ni:

a) Serikali inaweza kuwapatia raia wake wanaohitaji kununua nyumba mikopo maalum isiokua ya riba kupitia mfuko maalum utakaoanzishwa na Serikali kwa lengo hilo, deni hilo litakua linalipwa polepole kwa mujibu wa uwezo wa wakopeshwaji bila kuwekewa faida ya wazi au ya upenyezi inayojificha chini ya nembo ya (malipo ya huduma), ila ikiwepo dharura ya matumizi ya ziada juu ya deni basi wanaweza kuwalipisha hayo malipo ya dharura kwa namna iliyoelezewa kwenye 'Maamuzi' namba 13 (1/3) ibara (a) ya kikao cha tatu cha 'Kongamano hili'

b) Ikiwezekana kwa Serikali zenye uwezo, ni kuwajengea raia wake nyumba kasha ikawauzia kwa wanaotaka kwa malipo ya polepole kwa vigezo vilivyobainishwa kwenye ‘Maamuzi’ namba 51 (2/6) ya kikao hiki.

c) Wawekezaji ima watu binafsi au makampuni wanaweza kuingia kwenye miradi hii ya kuwajengea watu nyumba na kuwauzia kwa malipo ya polepole.

d) Inawezekana pia kumiliki nyumba kupitia muamala wa ‘Istisnaa’ ambapo kupitia muamala kama huu mnunuzi wa nyumba anaweza kuanza kulipia nyumba kabla haijajengwa, iwapo maelezo kamili ya ujenzi yatapatikana pasopo na utata wowote utakaopelekea mvurugano wa baadae, bila ya kuwepo ulazima wa kumaliza malipo mapema, bali wanakubaliana kuendelea na malipo ya polepole kwa kuzingatia masharti na vigezo yaliyowekwa na Wana-fiqihi katika miamala ya ‘istisnaa’ ambayo wameitafautisha na miamala ya ‘Salam’ (mikopo)

Na imeusiwa yafuatayo:

Kuendelea kutafuta njia nyingine zinazokubalika Kisharia zinaweza kumilikisha nyumba kwa wanaohitaji.

Allah ndie Mwenye Kutuwafikia

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 51 (2/6)

Yanayohusiana na 'Kuuza kwa Malipo ya Polepole'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha sita (6) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 17 – 23 Mwezi wa Shaaban, 1410 sawa na tarehe 14 – 20 Machi, 1990.

Baada ya usikivu makini wa tafiti kutoka kwa wajumbe na wataalamu zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Kuuza kwa Malipo ya Polepole** na kusikiliza mijadala na hoja za wataalamu kuhusiana na mada hio;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Inajuzu nyongeza ya thamani ya bidhaa inayolipwa baadae ikilinganishwa na bidhaa inayolipwa taslimu, aidha inajuzu kuainisha thamani ya bidhaa itakavyolipwa sasa na itakavyolipwa baadae kwa malipo ya polepole ndani kipindi kitakacotajwa, biashara haitosihi mpaka wakubaliane mwanzo kama biashara hii ni ya kulipwa taslimu au ni ya kulipwa baadae, ikiwa kuna utata wowote au haijafahamika vizuri au hawajakubaliana kwa uwazi juu ya biashara husika kama ni ya malipo ya taslimu au ya baadae basi haijuzu biashara kama hii.

Mbili: Haijuzu Kisharia katika biashara ya malipo ya baadae kuweka kiwango cha faida kwenye thamani ya taslimu kwa kisingizio cha ucheleweshwaji.

Tatu: Anapochelewa mnunuzi wa kulipa polepole kulipa deni lake kwa wakati, haijuzu kumuongezea malipo ya ziada, kufanya hivyo ni riba.

Nne: Ni haramu kwa mdaiwa anaelipa polepole kuchelewesha kulipa kwenye mda waliokubaliana, lakini hata hivyo haijuzu kumuwekea malipo

ya zaida kwa ajili ya kuchelewa.

Tano: Inajuzu Kisharia kwa muuzaji anaelipwa polepole kuweka sharti la kumaliza kulipwa pesa za awamu zote kabla ya mda waliokubaliana endapo mnunuzi amechelewesha kufanya malipo ya awamu za mwanzo, na pia iwapo walikubaliana hivyo hapo mwanzo.

Sita: Si haki kwa muuzaji kuendelea kumiliki kile alichokuiza baada ya biashara kukamilika, lakini inajuzu kwa muuzaji kudai rahani fulani kama dhamana kuhakikisha malipo ya pesa zake.

Na Imeusiwa yafuatayo:

Kuakhirisha mchakato wa vipengele vingine vinavyohusika na biashara ya malipo ya polepole hadi pale tafiti yakinifu zitakapowasilishwa kuhusiana na:

a) Punguzo kwenye bili za kubadilishana za malipo ya polepole na benki.
b) Kuharakisha kulipa deni kabla ya wakati wake kwa kupunguza kiwango chake (kwenye mas'ala ya punguza ulipwe haraka).
c) Athari zitakazojitokeza anapokufa mmoja wa pande mbili wakati malipo ya polepole hayajakamilika.

Allah ndie Mwenye Kutuwafikia

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 52 (3/6)

Yanayohusiana na 'Hukmu ya Mikataba Kupitia Vyombo vya Mawasiliano vya Kisasa'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha sita (6) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 17 – 23 Mwezi wa Shaaban, 1410 sawa na tarehe 14 – 20 Machi, 1990.

Baada ya usikivu makini wa tafiti kutoka kwa wajumbe na wataalamu zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Hukmu ya Mikataba Kupitia Vyombo vya Mawasiliano ya Kisasa** na kusikiliza mijadala na hoja za wataalamu kuhusiana na mada hio;

Na kwa kua kumekua na maendeleo makubwa katika vyombo vya mawasiliano ambazo watu hutumia kwa kupitisha mikataba ya miamala ya fedha na mengineo kutokana na kasi ya mawasiliano;

Na kwa kurudia fatwa za wanazuoni zinazohusiana na masuala ya:

- Kupitisha mikataba ya miamala kwa njia ya barua na njia ya ishara na njia ya mtu wa kati;
- Na kinachojulikana kwamba mikataba baina ya waliopo pamoja inashurutishwa wawepo kwenye kikao cha pamoja (*Itihad al-Majlis*) isipokua wakati wa kutoa wasia au kufawidhi wasia au kuwakilisha;
- Na ulazima wa uwepo wa '*iyjaab na qabul*' yaani kupendekeza (kuweka ofa) na kukubali na kutokuwepo ishara yoyote itakayoashiria kutoridhika kutoka upande wowote, na kuendelea kukamilisha muamala hadi kufunga mkataba kwa mujibu wa desturi zinazojulikana;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Panafungwa mkataba baina ya wawili ambao hawako pamoja na wala hawaonani uso kwa macho, wala hawasikiani, bali njia ya mawasiliano baina yao ni kupitia barua au mtu wa kati, na hapa pia inaingia mawasilano ya telegramu, teleksi, faksi, kompyuta, katika hali kama hii mkataba utakua umefungika pale pendekezo la muamala litakapomfikia anaekusudiwa nae akakubali.

Mbili: Panafungwa mkataba baina ya wawili walioko mbalimbali lakini kwa wakati mmoja kama vile kwa njia ya simu au mobile basi mkataba wowote baina yao ni kama wameifunga wakiwa pamoja, na hukmu za wanazuoni zinazojulikana zilizoelezewa hapo juu kwenye utangulizi ndizo zitakazotumika.

Tatu: Iwapo mpendekezaje kupitia njia hizi ameweka pendekezo lake na akalifunga kwa mda fulani, basi atawajibika kubakia katika mda ule bila ya kubadilisha kauli yake.

Nne: Hukmu zilizotajwa hapo juu haziingizi hukmu za ndoa na ubadilishanaji wa sarafu na miamala ya *Salam*; kwa sababu kwenye ndoa kuna ulazima wa mashahidi wawepo, aidha kubadilishana sarafu ni lazima pawepo makabidhiano ya papo kwa papo, na miamala ya *Salam* ni lazima malipo ya rasilimali yafanyike mubashara.

Tano: Kuhusu uwezekano wa kufanyika udanganyifu au makosa kwenye mikataba, sharia za '*ithbati*' na ushahidi zitatumika.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 53 (4/6)

Yanayohusiana na 'Makabidhiano: Aina zake - hasa aina mpya - na Hukmu zake'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha sita (6) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 17 – 23 Mwezi wa Shaaban, 1410 sawa na tarehe 14 – 20 Machi, 1990.

Baada ya usikivu makini wa tafiti kutoka kwa wajumbe na wataalamu zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na **Makabidhiano: Aina zake - hasa aina mpya - na Hukmu zake** na kusikiliza mijadala na hoja za wataalamu kuhusiana na mada hio;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Makabidhiano ya mali yanakua kwa uhalisia wake yaani kupokea kwa mkono, au kupokea vinavyopimwa kama vile vyakula, au kupokea mali katika hali kuhaulishwa ma kusafirishwa na kuhamishwa kwenda kwa mkabidhiwa yanakamilika tu pale mkabidhiwa anapokua na uhuru na uwezo wa kuyatumia mali yake yale hata kama hajakabidhiwa mkononi. Kukabidhiana mali kunatofautiana kulingana na mazingira, na desturi zinazotumika.

Mbili: Miongoni mwa aina za makabidhiano yanayokubaliwa Kisharia na Kidesturi ni kama zifuatazo:

1. Risiti ya benki inayoonyesha kwamba pesa fulani ameingiziwa mteja kwenye akaunti ya benki katika hali zifuatazo:
    a) Anapomuekea pesa mteja kwenye akaunti yake moja kwa moja au kupitia hawala ya kibenki.
    b) Anapokubaliana mteja na benki kununua sarafu fulani kwa

sarafu nyingine, malipo ya manunuzi hayo yakatwe kwenye akaunti yake.

c) Inapokata benki malipo, kwa maagizo ya mteja, kiwango fulani cha pesa kutoka akaunti fulani kwenda akaunti nyingine kwa sarafu nyingine, ima katika benki hio hio au kutoka kwenye akaunti yake ya benki nyingine, kwa faida yake au mtu mwingine, benki hapa zinatakiwa kuzingatia misingi ya mikataba ya sarafu kwa mujibu wa Sharia ya Kiislamu.

d) Inakubalika kucheleweshwa hadi kuiva kwake, miamala ya kusarifu pesa katika muda unaojulikana kwa mujibu wa desturi za soko la pesa, mfaidika au mteja hatoruhusika kutumia pesa zake ndani ya muda uliowekwa mpaka uishe ndipo awe na uwezo wa kutumia au kusarifu pesa zake.

2. Anaweza kutowa hundi (cheki) ikiwa anayo akiba ya pesa zinazoweza kutolewa kwa sarafu aliyoandika kwenye benki yake.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 54 (5/6)

Yanayohusiana na 'Kupandikiza Seli za Ubongo na Mfumo wa fahamu (Neva)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha sita (6) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 17 – 23 Mwezi wa Shaaban, 1410 sawa na tarehe 14 – 20 Machi, 1990.

Baada ya usikivu makini wa tafiti na maamuzi zinazohusiana na **Kupandikiza Seli za Ubongo na Mfumo wa fahamu (Neva)** ambazo zilikua ni sehemu za maudhui zilizojadiliwa kwenye warsha ya sita ya Fiqhi-Tiba iliyofanyika Kuwait kuanzia 23 – 26 Mfungo Sita (Rabiul Awal), 1410 sawa na 23 – 26 Oktoba, 1990, wakishirikiana na 'Kongamano hili' na 'Jumuiya ya Kiislamu ya Elimu za Tiba';

Na kwa mujibu wa maamuzi yalioafikiwa kwenye warsha-tajwa hio kwamba haikukusudiwa kwa namna yoyote ile kuhamisha ubongo wa mtu na kuupandikiza kwa mtu mwingine, bali lengo la kupandikiza ni kutibu kasoro za tishu fulani za ubongo kwa kutoa ute wa kemikali fulani kwa kiwango muwafaka na kupandikizwa kwenye ubongo wenye kasoro au kutibu mvungu ulijitokeza kwenye mfumo wa neva (mishipa), kutokana na kishondo cha ajali na mfano wake;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Ikiwa nyenzo za tishu zinazohitajika zinachukuliwa kutoka kwa mgonjwa huyo na kupandikizwa nazo yeye mwenyewe, na ikiwa mfumo wake wa kinga unakubali mahamisho hayo kwa kua seli hizo ni za mwili huohuo, basi hakuna katazo la Kisharia kufanya hivyo.

Mbili: Ikiwa nyenzo za tishu zinazohitajika zinachukuliwa kutoka kwa 'foitasi-mnyama, basi hakuna katazo la Kisharia ikiwa njia hii itafanikiwa na

bila kuleta athari mbaya. Kwa kua Madaktari-bingwa wamethibitisha kua njia hii imefanikiwa kwenye majaribio yaliyofanywa kwa wanyama na hivyo basi kuna matarajio ya kufanikiwa kwa binadamu baada ya kuchukua tahadhari za kiutabibu kuepuka kukataliwa na mfumo-kinga.

Tatu: Ikiwa nyenzo za tishu zinazohitajika zinachukuliwa kutoka kwa seli hai za ubongo wa foitasi akiwa katika wiki yake ya kumi (10) au kumi na moja (11) basi hukmu yake inategemea njia iliyotumiwa:

a) Njia ya Kwanza: Ni kuzichukua moja kwa moja kutoka foitasi-binadamu (foetus) akiwa ndani ya tumbo la mama yake, kupitia oparesheni ya tumbo-uzazi, kinachofuata kwenye njia hii ni kuua foitasi mara tu baada ya kuchukua seli kutoka kwenye ubongo wake, njia hii ni **haramu** Kisharia ila ikiwa foitasi imetoka yenyewe kwa kuharibika kwa mimba na bila ya kukusudia, au kutolewa kwa foitasi kwa ushauri wa Daktari-bingwa kulinda maisha ya mama-mzazi kwa kua foitasi ishakufa, lakini hata hivo ni lazima kuzingatia masharti yatakayoelezewa kwenye maudhui ya 'Namna ya Kufaidika na Foitasi' katika 'Maamuzi' namba 59 (8/6) ya kikao hiki.

b) Njia ya Pili: Ni njia-tarajiwa itakayojitokeza mustakbali ya karibu ya kuzalisha seli za ubongo katika maabara na kufaidika nazo, hakuna tatizo juu ya hilo iwapo nyenzo za seli za kutengenezwa ni halali ma zimepatikana kwa njia halali.

Nne: Mtoto anaezaliwa bila ya ubongo (anencephaly): Madamu amezaliwa akiwa hai basi haijuzu kuchukua chochote katika mwili wake hadi pale itakapothubutu kua amekufa kwa kufa mti-kati wa ubongo wake, hakuna tofauti kati ya mtoto huyu na watoto wengine waliozaliwa sawasawa katika jambo hili. Akiwa amekufa basi uchukuliwaji wa viungo vyake utafuata hukmu na masharti yanayozingatiwa katika kuchukua kiungo cha aliekufa kama vile idhini, na kutokuwepo mbadala mwingine na kwamba ipo dharura na masharti mengineo, yote hayo yameelezewa katika 'Maamuzi' namba 26 (1/4) katika Maamuzi ya kikao cha nne cha 'Kongamano hili'. Aidha hakuna katazo la Kisharia la kumueka kiumbe huyu aliezaliwa bila ubongo kwenye mashine-saidizi za kumbakisha hai hadi pale

itakapothubutu kua amekufa kwa kufa mti-kati wa ubongo wake, wakati huu inawezekana kujua ni viungo gani vinavyofaa kutumika kwa mwengine kwa kufuata masharti yaliyotajwa hapo awali.

Allah ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote.

Maamuzi nambari 55 (6/6)

Yanayohusiana na 'Mayai (ya mwanamke) yaliyopaliliwa mbolea yaliyozidi kiwango kinachihitajika'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha sita (6) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 17 – 23 Mwezi wa Shaaban, 1410 sawa na tarehe 14 – 20 Machi, 1990.

Baada ya usikivu makini wa tafiti na maamuzi zinazohusiana na **Mayai (ya mwanamke) yaliyopaliliwa mbolea yaliyozidi kiwango kinachihitajika** ambazo zilikua ni sehemu za maudhui zilizojadiliwa kwenye warsha ya sita ya Fiqhi-Tiba iliyofanyika Kuwait kuanzia 23 – 26 Mfungo Sita (Rabiul Awal), 1410 sawa na 23 – 26 Oktoba, 1990, wakishirikiana na 'Kongamano hili' na 'Jumuiya ya Kiislamu ya Elimu za Tiba';

Na baada ya kupitia maamuzi ya kumi na tatu (13) na kumi nan ne (14) yalioafikiwa kwenye warsha ya tatu (3) iliyosimamiwa na 'Jumuiya ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' iliyofanyika Kuwait mnamo tarehe 20 – 23 Shaaban, 1407; sawa na 18 – 21 Aprili, 1987, kuhusiana na **Mayai (ya mwanamke) yaliyopaliliwa mbolea,** na maamuzi ya tano (5) ya warsha ya kwanza ya 'Jumuiya ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' iliyofanyika Kuwait 11 – 14 Shaaban, 1403; sawa na 24 – 27 Mei, 1982 katikika maudhui hiohio;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kulingana na maendeleo ya Kisayansi yaliyopatikana yanaoonyesha uwezekano wa kuhifadhi mayai yasiyopaliliwa mbolea sehemu fulani na kuyatumia wakati yanapohitajika; basi ni wajibu wakati wa kupalilia mbolea mayai hayo kuchukua kiwango kinachohitajika pekee kwa minajili ya kupandikizwa mkusudiwa ili kuepuka kupalilia mayai mingi yasiyohitajika.

Mbili: Inapotokea kuna mayai ya ziada yaliopaliliwa mbolea basi

yatawachwa nje ya hifadhi ya tiba mpaka yakose uhai wake yenyewe.

Tatu: Ni haramu kutumia mayai ya mwanamke yaliyopaliliwa kuyapandikiza kwa mwanamke mwengine, na hapa ni lazima pachukuliwe tahadhari ili kuepuka utumiaji wa mayai yaliyopaliliwa kutengeneza mimba isiokua ya halali.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote.

Maamuzi nambari 56 (7/6)

Yanayohusiana na 'Kutumia Foitasi (Mjusi) kama chanzo cha kupachika viungo'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha sita (6) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 17 – 23 Mwezi wa Shaaban, 1410 sawa na tarehe 14 – 20 Machi, 1990.

Baada ya usikivu makini wa tafiti na maamuzi zinazohusiana na **Kutumia Foitasi (Mjusi) kama chanzo cha kupachika viungo** ambazo zilikua ni sehemu za maudhui zilizojadiliwa kwenye warsha ya sita ya Fiqhi-Tiba iliyofanyika Kuwait kuanzia 23 – 26 Mfungo Sita (Rabiul Awal), 1410 sawa na 23 – 26 Oktoba, 1990, wakishirikiana na 'Kongamano hili' na 'Jumuiya ya Kiislamu ya Elimu za Tiba';

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Haijuzu Kutumia Foitasi (Mjusi) kama chanzo cha viungo vinavyohitajika kupachikwa kwa mtu mwingine ila katika hali na vigezo vifuatavyo:

a) Haijuzu kutoa mimba (kuiharibu) kwa makusudi kwa minajili ya kutumia Mjusi kua ni chanzo cha viungo vinavyohitajika kupachikwa kwa mtu mwingine, isipokua pale mimba inapoharibika yenyewe bila ya kukusudia, au inapotolewa makusudi lakini kwa dharura ya Kisharia na ushauri wa daktari bingwa wakati maisha ya mama mzazi yataonekana kua hatarini iwapo Mjusi hakutolewa tumboni mwake.

b) Iwapo Mjusi huyu baada ya kutolewa tumboni mwa mamake ana nafasi ya kuendelea kuishi basi anatibiwa ili kulinda maisha yake badala ya kumtumia kama chimbuko la viungo vya kupachikwa watu wengine, ama iwapo Mjusi huyu hana nafasi ya kuendelea kuishi basi

pia haifai kumtumia ila baada ya kufa kwake kikamilifu na kwa masharti yaliyotajwa kwenye ‘Maamuzi’ namba 26 (1/4) ya ‘Kongamano’ hili.

Mbili: Haijuzu kabisa kuzifanya oparesheni ya kupachika viungo kua ni sehemu ya biashara.

Tatu: Oparesheni za kupachika viungo ni lazima zisimamiwe na jopo la wataalamu wanaoaminika.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 57 (8/6)

Yanayohusiana na 'Kupachika viungo vya Uzazi'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha sita (6) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 17 – 23 Mwezi wa Shaaban, 1410 sawa na tarehe 14 – 20 Machi, 1990.

Baada ya usikivu makini wa tafiti na maamuzi zinazohusiana na **Kupachika viungo vya Uzazi** ambazo zilikua ni sehemu za maudhui zilizojadiliwa kwenye warsha ya sita ya Fiqhi-Tiba iliyofanyika Kuwait kuanzia 23 – 26 Mfungo Sita (Rabiul Awal), 1410 sawa na 23 – 26 Oktoba, 1990, wakishirikiana na 'Kongamano hili' na 'Jumuiya ya Kiislamu ya Elimu za Tiba';

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kupachika hormoni za uzazi (Sexual Glands): Kwa kua pumbu na kioto cha mayai vinaendelea kubeba na kutoa sifa za kiurathi (Hereditary attributes) hata baada ya kupachikwa mtu mwingine, hivyo basi ni haramu kuvipachika kwa mtu mwingine.

Mbili: Kupachika viungo vya uzazi (Reproductive organs): Kupachika baadhi ya viungo vya uzazi ambavyo havibebi sifa za kiurathi – isipokua viungo vya siri – inajuzu Kisharia lakini baada ya kuzingatia vigezo vilivyoainishwa kwenye 'Maamuzi' namba 26 (1/4) ya 'Kongamano' hili.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≋≋≋

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 58 (9/6)

Yanayohusiana na 'Kupachika kiungo kilichokatwa baada ya utekelezaji wa Hukmu ya Haddi au Kisasi'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha sita (6) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 17 – 23 Mwezi wa Shaaban, 1410 sawa na tarehe 14 – 20 Machi, 1990.

Baada ya usikivu makini wa tafiti zilizowasilishwa zihusuzo **Kupachika kiungo kilichokatwa baada ya utekelezaji wa Hukmu ya Haddi au Kisasi** na kusikia hoja na mijadala juu yake;

Na baada ya kuzingatia makusudio ya Sharia ya utekelezaji hukmu ya haddi ambayo ni kukemea na kuzuwia watu wasiangukie kwenye makosa ya jinai, na kuiacha athari ya adhabu ili iwe ni kumbusho la kila wakati na kwa kila mtu juu ya uzito wa makosa ya jinai na hivyo kupelekea kupungua au kuondoka kabisa, na kwa kua kukirejesha kiungo kilichokatwa kunahitaji zoezi hilo lifanyike punde tu baada ya kukatwa kama inavyojulikana katika fani ya tiba ya kileo, ili jambo hili lifanyike maandalizi kabambe na ya mapema kabla ya utekelezaji wa hukmu ya ukatwaji, na itaonyesha kwamba kuna aina fulani ya kushusha hadhi au kudharau ukali wa Sharia;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Haijuzu Kisharia kukirudisha kiungo kilichokatwa kwa sababu ya utekelezaji wa hukmu ya haddi, kwani kuiacha athari ya haddi ndio kukamilisha malengo makuu ya haddi yenyewe na kuepusha uwepo wa hali ya dharau katika utekelezaji wenyewe, na isije ikaonekana kama inagongana na hukmu yenyewe japo ki-nje tu.

Mbili: Kwa kua Sharia ya kisasi inalenga kusimamisha haki na insafi kwa aliedhulumiwa na kulinda haki mzima ya jamii na kuweka mazingira ya

amani na utulivu; kwa maana hio haijuzu kukirudisha kiungo kilichokatwa kwa sababu ya utekelezaji wa hukmu ya kisasi ila katika hali zifuatazo:

a) Aidhinishe aliedhulumiwa baada ya utekelezaji wa hukmu ya kisasi kwamba anaweza kurudishiwa kiungo chake kilichokatwa.

b) Awe aliedhulumiwa ameweza kukirudisha kiungo chake kilichokatwa kwa dhulma.

Mbili: Inajuzu kukirudisha kiungo kilichokatwa kwa sababu ya utekelezaji wa hukmu ya haddi au kisasi kimakosa.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 59 (10/6)

Yanayohusiana na 'Soko la Pesa'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha sita (6) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 17 – 23 Mwezi wa Shaaban, 1410 sawa na tarehe 14 – 20 Machi, 1990.

Baada ya kupitia tafiti na mapendekezo yaliyoafikiwa kwenye warsha ya 'Soko la Pesa' iliyofanyika Rabat, Morocco mnamo tarehe 20 – 24 Mfungo saba (Rabiu Thani), 1410 sawa na 20 – 24 Oktoba, 1989 kwa kushirikiana na 'Kongamano' hili na 'Taasisi ya Kiislamu ya Utafiti na Elimu' iliopo chini ya 'Benki ya Kiislamu ya Maendeleo' na kwa makaribisho ya wizara ya Awqaf na mambo ya Kiislamu nchini Morocco.

Na kwa mujibu wa kinachojulikana katika Sharia ya Kiislamu ya kuhimiza kwenye chumo la halali na kuwekeza mali na kuyakuza kwa njia za uwekezaji wa Kiislamu uliojikita kwenye misingi ya kushirikiana katika hali za faida na hali za hasara na madeni.

Na kwa kua 'Soko la Pesa' linachangia kwa kiasi kikubwa kutanashati mzunguko wa fedha na uwekezaji, na kwa kua kujishughulisha na soko hili na kutaka kujua hukumu zake ni jambo la msingi la kuwafanya watu waifahamu misingi ya dini yao katika mambo mapya yanayozuka na kuweza kufaidika na jitihada za wanazuoni katika kubainisha hukumu za miamala ya pesa hususan hukumu za 'Soko la Pesa' na nidhamu za uwajibikaji sokoni, na kwa umuhimu huohuo ni kuyatanashati masoko mengine ambayo yanawapa fursa wawekezaji kurudi tena kuwekeza kwa umakini na hivyo kuchangamsha fursa za mizunguko ya pesa (liquidity) na kushajiisha wawekezaji wakijua wanaweza kuingia na kutoka kwa amani kabisa.

Na baada ya kupitia matokeo ya tafiti zilizowasilishwa kuhusiana na

nidhamu na kanuni za masoko ya pesa na vifaa vya utendaji-kazi wawke;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kujishughulisha na ‘Masoko ya Pesa’ ni miongoni mwa nyajibu za kuhifadhi na kukuza mali kwa watu wanapokua pamoja kwenye biashara na kushirikiana, hupelekea wao kutimiza wajibu wao juu ya mali yao ima uwe ni wajibu wa kidini au wajibu wa kidunia.

Mbili: ‘Masoko ya Pesa’ haya – licha ya umuhimu wa uwepo wake – katika hali ya uwepo wake sasa hayaridhishi katika kuhakikisha kua malengo ya uwekezaji kw amtazamo wa Kiislamu yanafikiwa. Kwa hali hii jitihada za makusudi zinahitajika na kwa mashirikiano baina ya Wana-fiqihi na Wana-uchumi kupitia mifumo yote na nidhamu za ‘Masoko ya Pesa’ na kurekebisha pale panapohitajia hivyo kwa mujibu wa misingi ya Sharia ya Kiislamu.

Tatu: Suala zima la ‘Soko la Pesa’ linajikita kwenye mifumo ya kiutawala na kiuendeshaji, hivyo basi ili mifumo hii ifanye vizuri inahitajika utumike msingi wa ‘Maslahi ya Umma’ (Al-Masalih Al-Mursalah - indefinite interest) katika shughuli zote ambazo hazigongani na misingi ya Sharia au mafundisho yake, ni mfano wa kanuni au nidhamu zinazopitishwa na serikali katika kuratibu na kusimamia shughuli za raia, haifai kwa mtu yeyote kwenda kinyume na sheria kama hizo au kuzikwepa iwapo zinaendana na misingi ya Kisharia.

Imependekezwa yafuatayo:

Kukamilisha kutizama taratibu na misamiati inayotumika katika ‘Masoko ya Pesa’ kwa kuandaa tafiti za kutosha za kifiqhi na za kiuchumi.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 60 (11/6)

Yanayohusiana na 'Hati-fungani 'Sukuk' (*Bonds*)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha sita (6) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 17 – 23 Mwezi wa Shaaban, 1410 sawa na tarehe 14 – 20 Machi, 1990.

Baada ya kupitia tafiti na mapendekezo yaliyoafikiwa kwenye warsha ya 'Soko la Pesa' iliyofanyika Rabat, Morocco mnamo tarehe 20 – 24 Mfungo saba (Rabiu Thani), 1410 sawa na 20 – 24 Oktoba, 1989 kwa kushirikiana na 'Kongamano' hili na 'Taasisi ya Kiislamu ya Utafiti na Elimu' iliopo chini ya 'Benki ya Kiislamu ya Maendeleo' na kwa makaribisho ya wizara ya Awqaf na mambo ya Kiislamu nchini Morocco.

Na baada ya mapitio ya nyaraka yanayoonyesha kwamba Hati-fungani ni: Stakabadhi inayomlazimu mtowaji wake kumlipa anaepewa stakabadhi hio kima fulani ifikapo wakati ulioainishwa pamoja na kulipa faida waliokubaliana kabla kwenye stakabadhi hio, aidha; kuweka manufaa yanayolipwa kwa masharti ima kwa njia ya zawadi au kufanya kura au kutowa kima fulani au punguzo;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Hati-fungani zinazobeba dhima ya kulipa kima na faida inayonasibiana na kima hicho au kutoa manufaa yaliyowekewa masharti basi hukmu yake ni: Haramu Kisharia kwa mtowaji wake au kwa Mnunuzi wake au kwa anaezizungusha, kwa kua ni mikopo ya riba ni sawa mtowaji wa hati-fungani hizi iwe ni sekta binafsi au sekta ya umma, wala haijalishi majina yanayotumika hapa; stakabadhi, au hati-fungani za uwekezaji au akiba, kadhalika kuziita faida za riba kua ni faida au kipato au kamisheni.

Mbili: Aidha; hati-fungani zenye kuponi ya sufuri ni haramu pia kwa kua ni

mkopo unaouzwa kwa bei duni ya kima chake asilia, watowaji wa hundi hizi hufaidika na tofauti inayopatikana wakichukulia ni punguzo la hizi hati-fungani.

Tatu: Vilevile ni haramu utowaji wa hati-fungani zenye ‘hundi ya zawadi’ kwa hii nayo pia ni mkopo wenye sharuti la manufaa au nyongeza kwa kundi la wakopeshaji au baadhi yao, aidha hali hii inafanana na Kamari.

Nne: Zipo Hati-fungani mbadala ya hizi zilizoharamishwa – kutoa au kununua au kuzungusha – nazo ni Hati-fungani zilizojikita kwenye ‘Mudaraba’ wa mradi au shughuli ya uwekezaji fulani, ambapo hakuna faida au manufaa anayopangiwa mmiliki bali anakua na mgao wa faida kwa mujibu wa makubaliano kulingana na hisa alizonazo kila mtu, na faida haigawiwi ila baada ya kupatikana kiuhalisia. Tunaweza kuurejea mfumo kamili wa Hati-fungani (sukook) katika ‘Maamuzi’ namba 30 (5/4) ya ‘Kongamano’ hili kuhusu: Hati-fungani (sukook) za Mudaraba.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 61 (12/6)

Yanayohusiana na ‘Maudhui na Warsha-Pendekezwa Kutoka Kitengo cha Mipango’

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha sita (6) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 17 – 23 Mwezi wa Shaaban, 1410 sawa na tarehe 14 – 20 Machi, 1990.

Baada ya kupitia ripoti ya ‘Kitengo cha Mipango’ iliyowasilishwa kwenye ‘Sekretarieti Kuu’ ya ‘Kongamano’ ambayo wajumbe wa Baraza la Kongamano walipewa nakala zao, ripoti hii imekusanya maudhui-pendekezi mbalimbali zinazotakiwa kufanyiwa utafiti nazo ni kama zifuatazo:

- Haki za Kimataifa katika Fiqhi ya Kislamu ya Leo.
- Ndoa na Mirathi katika Fiqhi ya Kislamu ya Leo.
- Fikra za Kiislamu Leo.
- Ibada katika Fiqhi ya Kislamu ya Leo.
- Miamala na Uchumi katika Fiqhi ya Kislamu ya Leo.
- Usul al-Fiqh (Misingi ya Fiqhihi) kwa mujibu wa zama za sasa
- Elimu ya Tiba na Elimu ya Sayansi.
- Matukio na mambo yanayozuka mengine.

Aidha; ripoti hii imependekeza kuitishwe warsha zitakazojadili mada zifuatazo:

- Haki za Mwanamke na Majukumu yake Katika Uislamu.
- Haki za Kimataifa katika Uislamu.
- Haki za Binadamu kwa kushirikiana na ‘Muungano wa Nchi za Kiislamu’ (OIC).
- Haki za Mtoto katika Uislamu pamoja na kuzingatia ‘Mkataba wa Kimataifa’ wa Haki za Mtoto.

- Wasiokua Waislamu ndani ya nchi ya Kiislamu: Haki zao na Majukumu yao.
- Waislamu wa zama hizi baina ya kushikamana na usuli au kufuata usasa.
- Kuandaa Katiba-elekezi ya Kiislamu.
- Msimamo wa Uislamu juu ya Sanaa za kisasa (uchoraji, kuimba, muziki, usanii).
- Mfumo wa Utawala wa Kiislamu: misingi yake na kadhia zilizopo zama hizi.
- Vyombo vya Habari vya kisasa kwa mtazamo wa Kiislamu.
- Hukumu za mabadiliko ya sarafu inayobadilika badilika thamani yake katika Fiqhi ya Kislamu.
- Mshikamano wa Kijamii katika Uislamu na matumizi yake ya sasa.
- Hati-fungani za hazina na stakabadhi za uwekezaji.
- Mambo ya hiari na ya baadae yanayotumika katika ‘Masoko ya Pesa’.

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuyazingatia mapendekezo haya na kuitaka ‘Sekreterieti Kuu’ kuchagua miongoni mwa mapendekezo haya yale yanayohitajika zaidi hususan yale yaliyotangulia kupendekezwa kwenye kikao kilichopita.

Mbili: ‘Sekreterieti Kuu’ ijipange kuandaa warsha-pendekezi na kutanguliza maudhui nyeti zaidi kulingana na uwezo uliopo.

Allahi Ndie Mwenye Kutawafikia

≋≋≋

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 62 (13/6)

Yanayohusiana na 'Mapendekezo ya kikao cha sita cha Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha sita (6) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 17 – 23 Mwezi wa Shaaban, 1410 sawa na tarehe 14 – 20 Machi, 1990.

Linausia yafuatayo:

Moja: Kuwataka Waislamu kote duniani kua na mshikamano na umoja na kujilazimisha kufuata sera za Kiislamu katika kutatua matatizo yao, na kusimamia majukumu yao ya kuufikisha Uislamu kwa watu wengine kote duniani na kuufikisha kwao ukiwa ni utatuzi wa matatizo yao badala ya kubeba fikra potofu zilizofilisika, aidha linwataka Waislamu wote kujihusisha na matatizo ya ndugu zao wanaoishi nchi za mashariki na kuwasaidia kwenye suala zima la kupata haki zao na kulinda utu wao na kuendelea kupata haki zote za kibinadamu.

Mbili: 'Kongamano' linapinga uhamiaji wa mayahudi kutoka Usovieti (USSR) kuja katika miji mitakatifu ya Palestina nchi ya 'Israa' na 'Miiraaj', na kulichukulia jambo hili kua hatarishi kwa Amani ya Umma wa Kiislamu duniani kote, aidha 'Kongamano' limazitaka nchi za Kiarabu na za Kiislamu kuungana na kupambana na hatari hii inayokua na kuchukua hatua za zinazowezekana kuikomboa nchi ya Palesina inayokaliwa pamoja na kukomboa maeneo matukufu kutoka kwa walowezi wa Kizayuni, na kusaidia wanaharakati wa Kipalestina waliosimama kidete kupambana na adui wa Kizayuni hadi kufikia malengo yao ya ukombozi.

Tatu: Kujishughulisha na vyombo vya habari katika nchi za Kiislamu na kuviwekea mazingira ya kufanya kazi ya kurekebisha, kuongoza na

kutumikia malengo ya Uislamu na kukabiliana na changamoto hatarishi za wakati huu, ‘Sekreterieti Kuu’ inaombwa kuandaa warsha mahususi ya vyomvo vya habari.

Nne: Kuandaa warsha ya Sanaa zilizoenea wakati huu, kama vile usanii, uigizaji, kuimba, muziki, kucheza na nyenginezo ambazo hakuna vyomvo vya habari leo ila hua wanatumia sanaa hizo.

Tano: Kuandaa tafiti-toshelezi katika maudhui ya ‘Kafara ya Mauaji’ ili maamuzi sahihi yachukuliwe kuhusiana na kadhia hio.

Sita: Kuakhirisha kujadili maudhui ya ‘Hisa’ ili kutoa nafasi ya tafiti za ziada.

Saba: Kuandaa warsha katika maudhui ya ‘Mambo ya hiari na ya baadae yanayotumika katika ‘Masoko ya Pesa’’.

Nane: Kuunda kamati, kwa ushirikiano na ‘Sekreterieti Kuu’ itakayojumuisha Wana-fiqihi na Wana-uchumi watakaojibu masuali ya ‘Benki ya Kiislamu ya Maendeleo’ kuhusu kushiriki katika kampuni za pamoja kwenye soko la hisa.

Allah Ndie Mwenye Kutuwafikia

Maamuzi na Maazimio ya Kikao cha Saba ya Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Jeddah, Falme ya Saudi Arabia

7 – 12 Mfungo Pili (Dhul Qaada), 1412

9 – 14 Mei, 1992

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 63 (1/7)[1]

Yanayohusiana na 'Masoko ya Pesa: Hisa, Chaguzi (Hiari), Bidhaa na kadi za mkopo'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha saba (7) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 7 – 12 Mwezi wa Mfungo Pili (Dhul Qaada), 1412 sawa na tarehe 9 – 14 Mei, 1992.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Masoko ya Pesa: Hisa, Chaguzi (Hiari), Bidhaa na kadi za mkopo,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizojadiliwa kuhusiana na maudhui-tajwa;

Limeamua yafuatayo:

Moja: Hisa

1- Kununua hisa za makampuni:

a) Kwa kua msingi wa Sharia unajikita kwenye 'uhalali wa miamala' hivyo basi inajuzu kwa mtu au taasisi kuanzisha kampuni ya hisa itayojishughulisha na mambo au biashara iliyo halali.
b) Wanazuoni hawajakhitalifiana juu ya uharamu wa kununua hisa kwenye kampuni inayojishughulishsa na biashara iliyoharamishwa, kama vile miamala ya riba, au uzalishaji wa bidhaa haramu au kuzifanyia biashara.
c) Hukmu ya msingi ni kuharamisha kununua hisa kwenye kampuni ambazo zinaamiliana na mambo ya haramu kama vile riba na mfano

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 7, Mjeledi 2, Uk. 1273 na Toleo 7, Mjeledi 1, Uk. 73, na Toleo 9, Mjeledi 2, Uk. 5).

wake, ijapokua miamala yao mingine ni halali.[1]

2- Dhamana:

Dhamana ni makubaliano wanayowafikiana nayo wakati wa kuanzisha kampuni ambapo fulani anakubali kwa hiari yake kuchukua dhamana ya kuuza hisa zote au baadhi yake zinazotolewa na kampuni hio, hii ni ahadi ya kujifunga ya kuuza hisa zilizosalia, jambo hili kimsingi halina katazo la Kisharia iwapo mchukua dhamana huyu hataongeza thamani ya hisa kwa kisingizio cha kujilipa dhamana yake, lakini inajuzu kupokea malipo juu ya kazi nyingine anayoifanya kama vile kuandaa mikataba na juhudi za uuzaji (marketing) wa hizo hisa.

3- Malipo ya polepole ya thamani ya hisa wakati wa dhamana:

Hakuna katazo la Kisharia la kulipa kima fulani cha thamani ya hisa wakati wa dhamana na kulipa kima kilichosalia baadae polepole, kwani kufanya hivi ni sawa na kushiriki kwa malipo ya awali na kuahidi kuzidisha kwenye rasilimali, hakuna katazo juu ya hili kwa kua inatumika kwenye hisa zote, na dhimma ya kampuni itabaki kwenye rasilimali yote waliyoitangaza kwa wengine, huu ndio msingi wa kuamiliana na watu wengine kuhusu kampuni husika.

4- Hisa ya Mmiliki wake:

Kwa kua kinachouzwa kwenye hisa ya mmiliki wake ni sehemu hisa zinazopatikana kwenye kampuni; hivyo basi stakabadhi ya hisa ni waraka unaothibitisha umiliki wa hisa, hakuna katazo la Kisharia kuuza hisa na kuzizungusha kwa utaratibu huu.

5- Sehemu ya mkataba katika mauzo ya hisa:

Sehemu ya mkataba katika mauzo ya hisa ni katika zile hisa za zilizowazi miongoni mwa mali ya kampuni, na stakabadhi ya hisa ni waraka unaothibitisha umiliki wa hisa.

[1] Tizama ‘Maamuzi’ namba 77 (8/8), na ‘Maamuzi’ namba 87 (4/9).

6- Hisa zenye hadhi:

Haijuzu kutoa stakabadhi za ‘hisa zenye hadhi’ zenye malumbukizo ya fedha yanayopelekea kudhaminiwa malipo kutoka rasilimali au kutoka kwenye faida au malipo ya mwisho wakati wa kufunga hesabu au wakati wa kugawa faida, lakini inajuzu kuzipatia hisa fulani malumbukizo ya fedha yanayohusiana na taratibu za kiutendaji na kiutawala.

7- Miamala ya hisa kwa njia za riba:

a) Haijuzu kununua hisa kwa mkopo wenye riba iwe ni kupitia kwa dalali au mtu mwengine kwa kuweka rahani hisa ile mpaka itakapolipiwa, kufanya hivyo ni riba na kuweka rahani hisa hio, na yote hao yameharamishwa Kisharia kwa kulaani mwenye kula riba na mlishaji na muandishi na mashahidi wake.
b) Kadhalika haijuzu kuuza hisa ambayo muuzaji bado hajaimiliki ispokua alipewa ahadi tu kutoka kwa dalali kua atamkopesha hisa ifikapo miadi ya kumkabidhi, kufanya hivyo ni katika kuuza asichokimiliki muuzaji, katazo hili linakua zito zaidi pale pale anaposhurutisha kulipwa yule dalali thamani ya hisa ili yule dalali anufaike kwa malipo atakayoyaweka kama mkopo na kupata faida juu yake.

8- Kuiuza hisa au kuiweka rahani:

Inajuzu Kuiuza hisa au kuiweka rahani lakini kwa kuzingatia kanuni za kampuni kama ikiwa kanuni za kampuni zinatowa nafasi kwa yeyote anaetaka kuuza na kumuuzia amtakae au kumeshurutishwa kuuziwa wale wenye hisa wa zamani kwa nafasi ya kipaombele, kadhalika inazingatiwaw iwapo kanuni ya kampuni imeelezea uwezekano wa kuweka rahani kwa washirika kwa bei ya hisa za kawaida.

9- Kuuza hisa pamoja na kuweka malipo ya uuzaji:

Hakuna katazo la kuongeza kima fulani juu ya thamani ya hisa kwa ajili ya kugharamia huduma za kiutawala, iwapo kima hiki kinawiana na huduma.

10- Kuuza hisa kwa bonasi au kwa punguzo:

Inajuzu kuuza hisa mpya kwa lengo la kuimarisha rasilimali za kampuni ima kwa kuuza hisa za zamani kwa bei ya sasa kulingana na ushauri wa wataalamu wa mali ya kampuni au kwa kutumia thamani iliyopo sokoni.

11- Dhamana ya kampuni katika ununuzi wa hisa:

Baraza limeonelea kuakhirisha kuchukua 'Maamuzi' juu ya kipengele hiki hadi kikao kijacho ile kutoa nafasi zaidi za utafiti makini ufanyike.

12- Kubaini dhima ya kampuni ndogo ya hisa ya pamoja:

Hakuna katazo la Kisharia kuanzisha kwa kampuni ndogo ya hisa ya pamoja kwa rasilimali zake, kufanya hivyo ni kuwajulisha wateja wa kampuni wanaotaka kuamiliana na kampuni hio, taarifa zikiwa wazi maanake hakuna utata kwa anaeamiliana na hio kampuni. Aidha hakuna katazo la Kisharia kwa wamiliki wa hisa kua na dhima ya wazi mbele ya wanaowadai bila ya kua na malipo juu ya dhima hii, na hizi ni kampuni ambazo zina washirika wanaodhaminiana na washirika wenye dhamana ndogo.

13- Kununua hisa kupitia kwa madalali walioruhusiwa pekee, na kushurutisha malipo ya miamala ndani ya soko la hisa:

Inafaa kwa taasisi rasmi husika kuratibu jinsi biashara ya hisa itakavyoendeshwa na kwamba ifanyike tu kupitia kwa madalali walioruhusiwa (leseni), kufanya hivyo ni kuongeza ufanisi na kulinda maslahi ya wote. Aidha inajuzu kushurutisha malipo kwa watakaoruhusiwa kufanya miamala hapo sokoni, hii ni sehemu ya uratibu na nidhamu zitakazolinda maslahi ya wote.

14- Haki ya kipaombele:

Baraza limeonelea kuakhirisha uchukuaji wa maamuzi katika suala hili hadi kikao kijacho, ili kutoa nafasi zaidi za utafiti.

15- Cheti cha Umiliki:

Baraza limeonelea kuakhirisha uchukuaji wa maamuzi katika suala hili hadi kikao kijacho, ili kutoa nafasi zaidi za utafiti.

Mbili: Chaguzi (hiari):

a) **Namna ya mikataba ya chaguzi:** Kusudio la mikataba ya chaguzi ni kujitoa katika ulazima au kujifunga kuuza au kununua kitu fulani kilichoainishwa kwa bei iliotajwa ndani ya kipindi fulani au wakati fulani-tajwa ima moja kwa moja au kupitia wakala anaesimamia haki za pande mbili.
b) **Hukmu yake Kisharia:** Mikataba ya chaguzi – kwa namna inavyofanyika leo kwenye masoko ya pesa ya kimataifa (*global financial markets*) – ni aina mpya ya mikataba iliyozuka, haina mifano yake katika mikataba inayojulikana Kisharia, lakini kwa kua kinachofungiwa mkataba hapa si mali wala si manufaa wala haki ya mali basi huo ni mkataba usiojuzu Kisharia, na kwa kua mkataba huu haujuzu basi vilivile haijuzu miamala inayotokana nayo.

Tatu: Miamala katika bidhaa na sarafu na fahirisi (index) kwenye masoko yanayosimamia:

1- Bidhaa:

Miamala ya bidhaa kwenye masoko yanayosimamia inafanyika kupitia mojawapo ya njia nne zifuatazo:

Njia ya kwanza: Uwepo wa kifungu kwenye mkataba wa mauzo kinachohakikisha haki ya mnunuzi kukabidhiwa bidhaa aliyoinunua na haki ya muuzaji kukabidhiwa thamani ya bidhaa aliyoiuza; bidhaa husika iwepo wakati wa muamala au risiti inayowakilisha umilikaji wa hio bidhaa kwa mnunuzi. Mkataba huu unajuzu Kisharia kwa masharti ya mauziano yanayojulikana.

Njia ya pili: Uwepo wa kifungu kwenye mkataba wa mauzo kinachohakikisha haki ya mnunuzi kukabidhiwa bidhaa aliyoinunua na haki ya muuzaji kukabidhiwa thamani ya bidhaa aliyoiuza papohapo chini ya dhamana ya menegimenti ya soko. Mkataba huu unajuzu Kisharia kwa

masharti ya mauziano yanayojulikana.

Njia ya tatu: Mkataba unaahidi kukabidhi bidhaa iliyoainishwa hivi sasa lakini itakabidhiwa baadae na malipo yafanyike wakati huo wa kukabidhiwa bidhaa, na kuweka sharuti kua muamala utakua umekamilika yanapofanyika makabidhiano ya bidhaa na thamani yake. Mkataba huu haufai kwa kua vyote viwili vinacheleweshwa, lakini badala yake wanaweza kuurekebisha mkataba huu ukawa ni mkataba wa 'Salam' kwa masharti yake yanayojulikana, ikifanyika hivyo basi inajuzu, aidha haijuzu kuuza bidhaa iliyonunuliwa kwa njia ya 'salam' kabla haijakabidhiwa.

Njia ya nne: Mkataba unaahidi kukabidhi bidhaa iliyoainishwa hivi sasa lakini itakabidhiwa baadae na malipo yafanyike wakati huo wa kukabidhiwa bidhaa, lakini bila ya kuweka sharuti kua muamala utakua umekamilika yanapofanyika makabidhiano ya bidhaa na thamani yake, bali inawezekana kubadilisha mkataba kwa mkataba mwengine. Aina hii ya mikataba ndio inayotumika sana katika masoko ya bidhaa, lakini mikataba aina hii haijuzu.

2- Miamala ya sarafu:

Miamala ya sarafu kwenye masoko yanayosimamia inafanyika kupitia mojawapo ya njia nne zilizotajwa kwenye miamala ya bidhaa. Haijuzu kununua au kuuza sarafu kupitia njia ya ya tatu na ya nne. Lakini inajuzu kununua au kuuza sarafu kupitia njia ya kwanza na ya pili baada ya kutimiza masharti yajulikanayo.

3- Miamala ya Fahirisi (index):

Fahirisi ni namba za kimahesabu maalum kwa njia ya takwimu, kusudio lake ni kiwango cha mabadiliko katika soko-husika ambapo miamala ya mauziano hua yanafanyika katika baadhi ya masoko ya pesa. Haijuzu kuuza au kununua kwa njia hii ya fahirisi kwa sababu ni aina ya Kamari; yaani kununua kitu ambacho hakipo kiuhalisia.

4- Mbadala wa Kisharia wa miamala hii ya haramu katika bidhaa na sarafu:

Ipo haja ya kuanzishwa kwa masoko ya pesa ya Kiislamu ya bidhaa na sarafu yenye misingi ya Miamala inayokubalika Kisharia kama vile; miamala ya 'Salam', 'kubadilisha sarafu', 'ahadi ya kununua kwa baadae' na 'istisnaa' na mingineo. 'Kongamano' linaonelea umuhimu wa kufanyika utafiti-toshelezi utakaobaini miamala mbadala na taratibu zake katika soko la Kiislamu lenye nidhamu.

Nne: Kadi za Mikopo (Credit Cards):

a) **Ufafanuzi wake:** Kadi za Mikopo ni hati inayotolewa kwa mtu binafsi au taasisi -kulingana na makubaliano baina yao– hati hii inamuezesha kununua bidhaa au kupata huduma kutoka kwa anaeikubali hati hio bila ya kulipa thamani papohapo kwa kua mtoaji wa hati hio amedhamini malipo. Miongoni mwa matumizi ya hati hii pia ni kutoa pesa taslimu kutoka benki. Kadi hizi za mikopo zipo anwai:

   - Zipo ambazo utowaji wake au ulipaji wake unachukua moja kwa moja kutoka kwa akaunti ya benki ya mbebaji kadi hio na wala si kutoka kwa akaunti ya mtoaji wa kadi hio isipokua imedhaminiwa tu, na nyingine ni zile ambazo malipo yanapofanyika pesa zinatolewa kutoka kwa akaunti ya mtoaji kadi kisha baadae pesa zilizotolewa zinalipwa kutoka kwa akaunti ya mbebaji katika nyakati walizokubaliana.
   - Zipo nyingine zinazotoza malipo ya riba kwa malipo ya pesa yaliyochelewa kulipwa katika mda uliowekwa, na zipo ambazo hazitozi malipo ya riba.
   - Nyingi miongoni mwa hizo kadi zinatoza malipo ya huduma kila mwaka, na zipo zisizotoza malipo ya huduma.

b) **Hukmu ya Sharia juu ya Kadi za Mikopo:** Baada ya mapitio ya haraka haraka; Baraza limeamuliwa kuakhirisha uchukuaji wa maamuzi katika suala hili la 'Kadi za Mikopo' hadi kikao kijacho, ili kutoa nafasi zaidi za utafiti.[1]

[1] Tizama 'Maamuzi' namba 96 (4/10).

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 64 (2/7)[1]

Yanayohusiana na 'Biashara ya Kulipa Polepole (*installment*)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha saba (7) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 7 – 12 Mwezi wa Mfungo Pili (Dhul Qaada), 1412 sawa na tarehe 9 – 14 Mei, 1992.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Biashara ya Kulipa Polepole (*installment*),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizojadiliwa kuhusiana na maudhui-tajwa;

Limeamua yafuatayo:

Moja: Inajuzu Kisharia kufanya biashara ya malipo ya polepole, hata kama bei ya polepole itazidi ikilinganishwa na ile ya papohapo.

Mbili: Nyaraka za biashara (Cheki, hundi, hati) ni aina ya uwakilishaji wa deni lilioandikwa.

Tatu: Makato kwenye nyaraka za biashara hayajuzu Kisharia, kwa kua yatapelekea nyongeza ya riba iliyoharamishwa.

Nne: Inajuzu kuweka punguzo la deni kwa minajili ya kuharakisha kulipwa deni hilo kabla ya wakati wake, ni sawa iwe ni kutokana na ombi la mdai au mdaiwa kwa msingi wa (punguza uharakishe), punguzo hili haliingii kwenye riba ikiwa hakukua na makaubaliano hapo awali, na kwa kua uhusiano wa mdai na mdaiwa unawahusu wao wawili tu, basi haijuzu uwepo wa mtu tatu kati yao, la sivyo itaingia kwenye hukmu ya makato kwenye nyaraka za biashara.

Tano: Inajuzu kwa wanaodaiana kuweka makubaliano mapya ya mdaiwa

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 7, Mjeledi 1, Uk. 193 na Toleo 7, Mjeledi 2, Uk. 9).

kulipa awamu zilizosalia zote mara moja ikiwa mdaiwa ameonyesha ishara ya kukwepa kwa makusudi kulipa awamu fulani, wala hakua ni mweye kulemewa na deni.

Sita: Iwapo ulipaji wa deni (la polepole) unaharakishwa ima kwa sababu ya kifo cha mdaiwa, au kufilisika kwake au kuchelewa kulipa awamu nyingine kwa makusudi; katika hali zote hizi-tajwa inajuzu kuweka punguzo la deni kwa minajili ya kuharakisha kulipwa deni hilo.

Saba: Kidhibiti cha ‘Kulemewa’ ambacho kinaruhusu kumuongezea mda wa kulipa ni: Mdaiwa asiwe na mali yaliozidi matumizi yake ya msingi ya kumuwezesha kulipa deni lake pesa tasilimu au mali mengine.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 65 (3/7)[1]

Yanayohusiana na 'Mikataba ya *Istisnaa* (Kutengenezewa Bidhaa)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha saba (7) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 7 – 12 Mwezi wa Mfungo Pili (Dhul Qaada), 1412 sawa na tarehe 9 – 14 Mei, 1992.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Mikataba ya *Istisnaa* (Kutengenezewa Bidhaa),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizojadiliwa kuhusiana na maudhui-tajwa;

Na kuzingatia 'Makusudio Makuu ya Sharia' katika maslahi ya Umma na kuwepesisha miamala na mikataba, na kwa kua 'Mikataba ya Istisnaa' ina nafasi kubwa katika kutanashati shughuli za kiviwanda na uzalishaji wa bidhaa na kufungua milango ya mizunguko ya pesa na kukuza uchumi wa Kiislamu;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Mkataba wa Istisnaa –ni mkataba unaohusisha kazi na bidhaa zilizopo kwenye dhima- unaunganisha na kulazimisha pande mbili panapotimia masharti na vigezo.

Mbili: Masharti ya Mkataba wa Istisnaa ni kama yafuatayo:

a) Kuainisha aina yake, sifa zake na viwango vyake vya bidhaa inayotakiwa kutengenezwa.
b) Kubainisha mda utakaotumika.

Tatu: Katika mkataba wa istisnaa inajuzu kuchelewesha malipo yote, au kulipa polepole kwa awamu kadha na kwa mda kadha.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 7, Mjeledi 2, Uk. 223).

Nne: Inajuzu kuweka kifungu cha ‘faini’ kwenye mkataba wa istisnaa kwa mujibu wa makubaliano endapo mmoja wao amekwenda kinyume na makubaliano ila ikitokea dharura isiyoepukika.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 66 (4/7)[1]

Yanayohusiana na 'Biashara ya kujiekea haki ya kukinunua ulichokiuza (Bay'i al-Wafaa)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha saba (7) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 7 – 12 Mwezi wa Mfungo Pili (Dhul Qaada), 1412 sawa na tarehe 9 – 14 Mei, 1992.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Biashara ya kujiekea haki ya kukinunua ulichikiuza (Bay'i al-Wafaa),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizojadiliwa kuhusiana na maudhui-tajwa ambayo ni: Mtu kuuza bidhaa kwa sharti kwamba mnunuzi anapolipa thamani ya bidhaa hio basi yule mnunuzi atamuuzia yule muuzaji wa awali bidha ile;

Limeamua yafuatayo:

Moja: Biashara hii kiuhalisia wake ni mfano wa mkopo unaoleta manufaa, kwa hio ni aina fulani ya kula riba kupitia mlango wa nyuma, wanazuoni walishapitisha kutosihi kwa muamala kama huu.

Mbili: Mkataba huu haujuzu Kisharia.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 7, Mjeledi 3, Uk. 9).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 67 (5/7)[1]

Yanayohusiana na 'Matibabu'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha saba (7) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 7 – 12 Mwezi wa Mfungo Pili (Dhul Qaada), 1412 sawa na tarehe 9 – 14 Mei, 1992.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Matibabu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizojadiliwa kuhusiana na maudhui-tajwa;

Limeamua yafuatayo:

Moja: Kujitibu:

Kimsingi inajuzu kujitibu kwa mujibu wa Sharia na ilivyokuja kwenye Qur;an na Sunna za Bwana Mtume SAW na matendo yake na pia ijulikane kua 'Kuihifadhi nafsi' ni mojawapo wa makusudio makuu ya Sharia.

Hukmu za kujitibu zinatofautiana kulingana na mazingira na watu:

- Kujitibu inakua wajibu (lazima) kwa mtu ambae kwa ugonjwa alionao asipojitibu itapelekea ima kuiangamiza nafsi yake au kupoteza kiungo chake au kulemewa, au iwapo ugonjwa huo ni wa kuambukiza wengine.
- Inapendekeza (ni vizuri) kujitibu iwapo kuacha kujitibu inapelekea kudhoofisha mwili lakini haifikii kiwango kilicotajwa hapo juu.
- Kujitibu inakua ni halali ikiwa si katika hali mbili-tajwa hapo juu.
- Kujitibu inakua makruh (inachukiza) iwapo kujitibu itapelekea kudhoofisha mwili na kuzidisha ugonjwa zaidi ya ule unaotibiwa.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 7, Mjeledi 3, Uk. 563).

Mbili: Kutibu maradhi yaliyokatiwa tamaa

a) Kwa mujibu wa Imani ya Kiislamu, maradhi na ponyo zipo mikononi mwa Allah SWT, kujitibu na kutafuta dawa ni kuchukua sababu alizoziweka Allah za kutafutia tiba ya maradhi, hivyo basi haifai kwa Muislamu kukata tamaa ya kutopata ponyo au tiba ya maradhi bali anatakiwa kuzidisha matumaini ya ponyo kutoka kwa Allah. Na ni juu ya matabibu (madaktari) kumsaidia mgonjwa wao na kuimarisha matumaini yao na kuwahudumia vizuri na kuwapunguzia maumivu ya kimwili na y kinafsi hata kama wanajua fika kama ugonjwa huu hauna tiba.
b) Kile kinachozingatiwa katika maradhi yaliyokatiwa tamaa inategemea maoni ya daktari bingwa na elimu ya tiba ilipofikia na mazingira ya mgonjwa mwenyewe.

Tatu: Idhini ya Mgonjwa

a) Idhini ya kumtibu mgonjwa ni lazma ipatikane iwapo mgonjwa mwenyewe yuko katika hali ya fahamu na kuelewa, iwapo amekosa fahamu au haelewi basi walii/msimamizi (guardian) wake atasimamia kutoa idhini kwa mujibu wa vigezo vya Kisharia na kwa kuzingatia maslahi makuu ya mgonjwa huyo. Na iwapo walii atakataa kutoa idhini wakati imejulikana fika kua kutibiwa kwake ndio maslahi yake makuu basi walii huyu amekua ni pingamizi, hapo itabidi haki ya uwalii hii apewe mtu mwengine awe walii wake.
b) Walii anaruhusiwa kumlazimisha anaemuwakilisha kufanyiwa matibabu katika mazingira ya magonjwa ya kuambukiza au chanjo za kujikinga.
c) Katika mazingira ya dharura ambapo maisha ya mgonjwa yako hatarini idhini hapa inakua sio lazma.
d) Katika kufanya tafiti za ki-tiba ni lazima ipatikane idhini ya yule anaetakiwa kufanyiwa utafiti wa ki-tiba ikiwa ni mtu mwenye akili zake timamu, haikubaliki pafanyike ghilba ya aina yoyote au hadaa has wakiwa walengwa hawa ni wafungwa au ni watu maskini au kuwaghilibu kwa pesa na mfano wake, na hizo tafiti zaki-tiba zisiwe na athari nbaya au madhara juu yao. Haifai kuwafanyia tafiti za ki-tiba

watu wenye ulemavu wa akili ispokua panapopatikana ruhusa kutoka walii wao.

Inausiwa yafuatayo:

'Sekreterieti Kuu ya Kongamano' inaombwa kusimamia zoezi la kuandaa 'Tafiti za Ki-tiba zifuatazo kwa minajili ya kuwasilishwa kwenye kikao kijacho:

- Kufanya tiba kwa kutumia vitu vilivyoharamishwa na ambavyo ni najisi, na vidhibiti vya utumiaji wa dawa.
- Tiba ya urembo.
- Dhamana ya Tabibu (Daktari).
- Tabibu mwanamume kumtibu mwanamke na kinyume chake, Daktari asiekua waislamu kutibu waislamu.
- Tiba ya Ruqya.
- Maadili ya Tabibu, ikiwa mada hii itakua ndefu basi ijadiliwe kwenye zaidi ya kikao kimoja.
- Msongamano kwa wanaotafuta tiba na kupanga nafasi za kipaumbele.
- Tafiti za magonjwa ambayo mara nyingi matabibu wanashidwa kuyapatia tiba kama vile:
  - ✓ Mtu ambae ugonjwa wa saratani umemuenea; je mtu huyu anatibiwa au anapewa vitulizo vya maumivu tu?
  - ✓ Mtoto mwenye mvujo wa ubongo (kufa kwa bongo) sambamba na kupoza kwa bongo na kudogoka; je mtoto kama huyu anafanyiwa amalia (oparesheni)? Na je anapopatikana mtoto huyu muwasho wa apendisi (appendix) au muwasho katika mapafu anatibiwa au anaachwa?
  - ✓ Mtu mzima mkongwe aliepata mgando au ukakamavu wa moyo, aidha ana ugonjwa wa kupoza (paralyse) na figo iliolemewa; je anatibiwa figo iliolemewa kwa njia ya dayalisi (dyalisis)? Na je moyo wake unaposimama ghafla anasaidiwa au anaachiliwa? Na je anapopatikana na muwasho wa mapafu anatibiwa au anaachiliwa?
  - ✓ Mtu ambae ubongo wake umeumia vibaya sana (hajafika

kiwango cha kufa kwa ubongo) licha ya kua baadhi ya sehemu ya ubongo huo bado zinafanya kazi lakini amepoteza fahamu na hakuna matarajio ya kuboreka kwa hali yake; je mtu kama huyu unaposimama moyo wake anasaidiwa au anaachiliwa? Na je anapopatikana na muwasho wa mapafu anatibiwa? Na ni kina nani watakaoamua kutotibiwa katika hali kama hizi zilizotajwa, ni jopo la madaktari au jopo la madaktari pamoja na kamati ya maadili au jopo la madaktari pamoja na familia ya mgonjwa?

- Msimamo wa Sharia unahitaji kubainishwa katika hali-tajwa kama hizi.

Allah Ndie Mwenye Kutuwafikia

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 68 (6/7)[1]

Yanayohusiana na 'Haki za Kimataifa kwa Mtazamo wa Uislamu'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha saba (7) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 7 – 12 Mwezi wa Mfungo Pili (Dhul Qaada), 1412 sawa na tarehe 9 – 14 Mei, 1992.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Haki za Kimataifa kwa Mtazamo wa Uislamu,** na baada ya kupongeza kwa juhudi kubwa zilizotumika katika kuandaa tafiti zilizowasilishwa kwenye kikao hichi cha saba kuhusuiana na maudhui-tajwa, na kwa kuona kua umuhimu na upana wa maudhui haya 'Kongamano' linaona bado ipo haja ya upanuzi wa tafiti katika nyanja zote za maudhui, na baada kusikiliza hoja mbalimbali zihusuzo maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuunda kamati-andalizi itakayoandaa waraka maalum na kuandaa warsha mahsusi itakayopitia nyanja zote za maudhui haya ili watoke na 'Mswada wa Kanuni' ya 'Haki za Kimataifa katika Uislamu' amabo utawasilishwa kwenye kikao kijacho cha 'Baraza la Kongamano'.

Mbili: Vipengele vya 'Waraka wa Warsha' vizingatie yafuatayo:

1) Nyenzo za Kanuni ya Kimataifa ya Kiislamu na Mahusiano ya Kimataifa; ni Qur'an tukufu na Sunna tukufu za Bwana Mtume Muhammad SAW na matendo ya Makhalifa wake pamoja na yaliyopokewa kutoka kwa wanazuoni katika jitihada zao na tafiti zao kuhusiana mada hii.

2) Makusudio/Malengo Makuu ya Sharia ya Kiislamu ambayo athari zake zinaonekana kwenye maiasha ya kila si ku ya Muislamu kama

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 7, Mjeledi 4, Uk. 9).

vile:

a. Makusudio ya Sharia.
b. Sifa kuu za Uislamu.
c. Maana ya ‘Umma’ na umoja wake.
d. Mitazamo ya Wana-fiqihi katika kuigawa dunia.
e. Misingi ya kihistoria ya hali iliopo sasa katika Ulimwengu wa Kiislamu.
f. Mahusiano ya nchi za Kiislamu (Raia wa Kiislamu na Wachache wasiokua waislamu).
g. MAhusiano ya nchi za za Kiislamu na zile zisizokua za Kiislamu.
h. Misimamo ya nchi za Kiislamu katika makubaliano, mikataba na taasisi za Kimataifa.

Tatu: Kamati-andalizi hii intakiwa kuandaa nyaraka bainifu zitakazokua ni miongozo kwa watafiti wakati wanapobahithi katika vipengele-tajwa; na jambo hili linatakiwa likamilishwe ndani ya miezi michache ijayo.

Allah Ndie Mwenye Kutuwafikia

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 69 (7/7)[1]

Yanayohusiana na 'Uvamizi wa Kifikra'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha saba (7) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 7 – 12 Mwezi wa Mfungo Pili (Dhul Qaada), 1412 sawa na tarehe 9 – 14 Mei, 1992.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Uvamizi wa Kifikra,** na ambazo zimebainisha jinsi uvamizi huu ulivyoanza na hatari yake na athari zake na namna uvamizi huu ulivyoathiri mpaka sasa katika nchi za Kiislamu na za Kiarabu. Aidha tafiti hizi pia zimeashiria mifano ya upotoshaji na mikakati inayodhamiriwa kuchafua jamii za Kiislamu duniani kote na kuzuwia ueneaji wa Uislamu na harakati zake duniani. Vilevile tafiti hizi zimebainisha nafasi ya Uislamu katika kulinda na kuhifadhi Umma wa Kiislamu dhidi ya njama za uvamizi huu pamoja na kupangua mingi miongoni mwa mikakati-haribifu ya uvamizi huu. Tafiti hizi zilijikita kwenye kuelekeza namna ya kupambana na uvamizi huu hatarishi na kuuhami Umma wa Kiislamu katika nyanja zote dhidi ya athari mbaya za uvamizi huu.
Baada ya usikivu wa hoja na mijadala kuhusiana na maudhui haya;

Imeusiwa yafuatayo:

Moja: Kusimamia utekelezaji wa Sharia ya Kiislamu na kuifanya Sharia hio kua msingi mahusiano ya kisiasa za ndani na za kimataifa.

Mbili: Kujibidiisha katika kusafisha mifumo na mitaala ya elimu ili yaendane na malengo ya kuinua Umma na kizazi kijacho kwa misingi ya 'Malezi ya Kiislamu ya Kisasa' na kwa namna itakayowapatia maandalizi muwafaka yatakayowafunua macho juu ya dini yao pamoja na kuwapatia kinga kamili

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 7, Mjeledi 4, Uk. 311).

dhidi ya uvamizi wa kifikra.

Tatu: Kuboresha mifumo ya ‘Uandaaji wa Walinganizi’ ili wafahamu kiini cha Uislamu na mfumo wake katika kujenga maisha sahihi ya binadamu na pia kuwawezesha kuzifahamu elimu za kisasa ili iwe rahisi kwao wao kuamiliana na watu wa sasa.

Nne: Kuipatia misikiti nafasi ya ulezi kamili katika maisha ya Waislamu ili kuwawezesha kupambana na kila aina ya uvamizi huu wa kifikra na athari zake pamoja na kuwaelimisha juu ya ufahamu sahihi wa dini yao.

Tano: Kuzijibu tuhuma-batili zinazoletwa na maadui wa Uislamu kwa taratibu za kielimu na Imani thabiti na kifua mbele kua dini hii imekamilika, hakuna haja ya kujibu tuhuma hizo kwa njia za udhaifu na kukubali kushindwa.

Sita: Kujishughulisha na kuzifahamu fikra za kigeni zinazoingizwa na kuzisoma kwa umakini ili kubaini mapungufu yaliopo kwenye fikra hizo kiusomi na kielimu na kwa uaminifu.

Saba: Kujishughulisha na muamko wa Kiislamu uliopo na kuziunga mkono taasisi zinazofanya kazi katika nyanja za ‘Da’wa na Ulinganizi’ kwa lengo la kumjenga Muislamu sahihi ambae atakua ni mfano wa kuigwa mbele ya jamii ya kibinadamu amabe anawasilisha picha kamili ya Uislamu katika ngazi ya mtu binafsi na ngazi ya ya jamii mzima katika nyanja zote za kimaisha; kisiasa, kijamii, kiutamaduni na kiuchumi.

Nane: Kujishughulisha na Lugha ya Kiarabu na kujitahidi kuieneza na kushajiisha juhudi za kuifundisha ulimwenguni kote, kwa kuzingatia kua hii ndio lugha ya Qur’an na kuifanya iwe lugha ya kufundishia katika nchi za Kiarabu na za Kiislamu taasisi za kielimu kuanzia ngazi za msingi, sekondari hadi chuo kikuu.

Tisa: Kujibidiisha katika kubainisha uzuri wa Uislamu na kwamba misingi ya dini ya Kiislamu imekuja kwa lengo la faida na furaha ya binadamu za hapa duniani na pia za kesho akhera. Jambo hili linatakiwa lifanyike kwa kiwango cha kimataifa na kwa kutumia lugha hai (kuu) duniani.

Kumi: Kufaidika vilivyo na mbinu za kisasa katika tasnia ya habari ili kuliwezesha neno la haki na la kheri kufika sehemu zote duniani.

Kumi na moja: Kujishughulisha na kupambana na matatizo ya kisasa kwa utatuzi habiti unaopatikana katika Uislamu na kufanya liwezekanalo kutumia suluhisho hizi za Kiislamu katika kutatua matatizo haya, mafanikio ya kiutekelezaji bi mojawapo wa njia muwafaka za 'Da'wa'.

Kumi na mbili: Kutilia nguvu mshikamano wa Waislamu na kuudhihirisha umoja wao katika nyanja zote, na kujaribu kutatua hitilafu zao na migogoro yao kwa njia za Amani kwa mujibu wa Hukumu za Kiislamu zinazojulikana, na kutozipatia nafassi njama za uvamizi wa kifikra katika kubomoa umoja wa Kiislamu na kupandikiza mbegu za khusma na migogoro miongoni mwa Waislamu.

Kumi na tatu: Kuongeza juhudi katika kujenga nguvu za Waislamu na kujitosheleza kiuchumi na kijeshi.

Kumi na nne: Kuzitaka nchi za Kiarabu na za Kiislamu kunusuru Waislamu wanaoteswa na kunyanyaswa sehemu mbalimbali duniani na kuwatetea pamoja na kuwahami dhidi ya uadui wowote wanaofanyia kwa kadri ya uwezo uliopo.

Aidha 'Baraza' limeusia yafuatayo:

'Sekreterieti Kuu ya Kongamano' iendelee kujihusisha na kadhia muhimu za maudhui haya katika vikao vitakavyokuja na 'Warsha' watakazoziandaa kutokana na umuhimu mkubwa wa maudhui ya 'Uvamizi wa Kifikra' na haja iliopo ya kuweka mikakati kabambe ya kukabiliana na yanayojitokeza kama athari za uvamizi huu, inapendekeza kuanzwe na kadhia za 'Uvangelisti' (Uenezwaji wa Ukristo (kuritadishwa) katika jamii za Kiislamu) na 'Umashariki' (Kampeni maalum za Wamagharibi za kuupotosha Uislamu) katika kikao kijacho.

Allah Ndie Mwenye Kutuwafikia

≅≈≅

Maamuzi na Maazimio ya Kikao cha Nane (8) ya Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam

1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414

21 – 27 Juni, 1993

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 70 (1/8)[1]

Yanayohusiana na 'Kuzitumia Rukhsa na Hukmu Zake'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Kuzitumia Rukhsa na Hukmu Zake,** na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: 'Rukhsa za Kisharia' ni zile hukumu maalum zilizowekwa amabzo zinakua na tahfifu fulani kulingana na sababu zilizoekewa, hakuna ikhtilafu baina ya wanazuoni kuhusu uwepo wa rukhsa za kisharia kama hizi na kuzitumia ipatikanapo sababu ya kufanya hivyo baada ya kuhakikisha uwepo wa hizo sababu na kuzitumia rukhsa hizo pale iliporuhusiwa tu pamoja na kuzingatia vigezo na masharti yaliyowekwa.

Mbili: 'Rukhsa za Kifiqihi' ni zile hukmu zilizotokana na jitihada za madh-hebu fulani kujuzisha kitu fulani wakati kuna jitihada za madh-hebu mengine kukataza jambo hilo. Kutumia Rukhsa za wanazuoni maana yake ni kutumia hukmu ilio na tahfifu zaidi ikilinganishwa na ya mwanachuoni mwengine; kufanya hivi inajuzu kwa kuzingatia vigezo vilivyotajwa kwenye kipengele cha nne (4).

Tatu: Utumiaji wa rukhsa katika mambo ya kawaida ni sawa na miamala ya ki-fiqhi ya asili ikiwa utumiaji huo unaleta maslahi yanayokubalika ki-sharia, na iwapo rukhsa hizo zimetokana na jitihada za pamoja za wanazuoni

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 8, Mjeledi 1, Uk. 41).

wanaokubalika ki-elimu na wenye Ucha-Mungu.

Nne: Haijuzu kuchukua rukhsa za ki-madhehebu kwa utashi wa nafsi, kwani kufanya hivyo kunaweza kupelekea ukwepaji wa maagizo ya sharia, utumiaji wa rukhsa unapaswa ufanyike kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo:

a) Kauli za wanazuoni zinazojuzisha rukhsa ziwe ni zenye kukubalika kisharia.
b) Iwepo haja ya kutumia rukhsa husika, ili kuondoa uzito, haja-tajwa inafaa iwe ni kwa wepesi wa umma au wa mtu mmoja.
c) Mchukuaji wa rukhsa anatakiwa awe na uwezo wa kuchagua au awe anamtegemea mwanachuoni anaekubalika.
d) Isipelekee uchukuaji huu wa rukhsa kuingia katika udanganyifu uliokatazwa katika kifungu cha sita (6) kinachokuja.
e) Isiwe uchukuaji huu wa rukhsa ni sababu ya kumfikisha mtu kwenye malengo yasiyoruhusiwa kisharia.
f) Nafsi ya mchukuaji rukhsa ihisi utulivu katika rukhsa hio.

Tano: Udanganyifu katika kufuata madhehebu ni pale mtu anapoyaendea mas'ala ya kifiqhi yenye ncha mbili zinazofungamana au zaidi lakini akawa mtu huyu anayaendea mas'ala haya kwa namna ambayo haijawahi kutokea kwa mwanachuoni mtegemewa kufanya namna kama hio.

Sita: Udanganyifu katika rukhsa unakatazwa katika hali zifuatazo:

a) Inapopelekea kuchukua rukhsa kwa utashi wa nafsi tu, au kuzikiuka vipengele vilivyoainishwa kwenye suala zima la utumiaji wa rukhsa.
b) Inapopelekea kutengua hukumu ya mahkama ya kadhi.
c) Inapopelekea kutengua hukumu ambayo iliwahi kutumika katika tukio kama hilo.
d) Inapopelekea kukhalifu maamuzi ya pamoja (ijmaa) ya wanazuoni.
e) Inapopelekea katika hali ya mparagano ambayo haikubaliki mbele ya wanazuoni.

Allah ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 71 (2/8)[1]

Yanayohusiana na 'Ajali za Barabarani'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Ajali za Barabarani,** na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya; na kwa kutizama jinsi ajali za barabarani zilivyokithiri na kuongezeka na hatari zilizojitokeza za roho za watu na mali yao kupotea; na kwa kuzingatia maslahi ya umma yangelindwa vizuri zaidi iwapo patawekwa sharia maalum za kuruhusu vyombo barabarani zitakazokidhi masharti ya usalama kama vile vyombo madhububti, umiliki wa vyombo, leseni za uendeshaji vyombo zenye kuzingatia masharti kama vile umri wa muendeshaji (dereva), uwezo wake, uoni wake na ufahamu wake wa sheria za barabarani na utayari wa kuzifuata, na kuweka kiwango cha mwendo (kasi) kinachokubaliwa na uzito wa mizigo inayobebwa na kila chombo;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja:

a) Ni wajib kufuata sheria kama hizo iwapo hazigongani na sharia za Kiislamu, kwani kufanya hivyo ni sehemu ya kutii viongozi katika maagizo yake na mipangilio yake ya kulinda maslahi ya umma, aidha inatakiwa sharia hizo zijiegemeze na sharia za Kiislamu ambazo hazijatumika katika eneo hili.
b) Katika kuyaendea maslahi ya umma ni kutunga sheria za adhabu

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 8, Mjeledi 2, Uk. 171).

kama vile kuweka faini kwa anaekhalifu sharia hizo ili kuzuia wanaohatarisha usalama wa wengine barabarani na maeneo ya masoko miongoni mwa wanaotumia vyombo vya barabarani, kwa mujibu wa hukmu za 'Hisba' kulinda usalama na uwiano wa umma.

Mbili: Ajali za barabarani zinazotokana na matumizi ya vyombo zitahukumiwa kwa mujibu wa sharia za jinai za kiislamulicha ya kwamba ajali nyingi huenda zikawa si kwa kukusudia lakini dereva atawajibika kwa kila dhara analomsababishia mwengine**,** sawa dhara hilo liwe ni kwenye mwili au mali ya muathiriwa. Dereva anaweza kusameheka katika hali zifuatazo:

a) Iwapo ajali imetokana na sababu za nje zisizoweza kuepukika licha ya kwamba alijitahidi kuiepuka ajali hio.
b) Iwapo ajali hio imesababishwa na muathiriwa mwenyewe moja kwa moja.
c) Iwapo ajali imesababishwa na mtu mwengine, kwa hali hii basi huyo mwengine atawajibika.

Tatu: Ajali zinazosababishwa na wanyama basi wamiliki wa wanyama hao watawajibishwa iwapo walizembea kuwadhibiti wanyama wao hao. Maamuzi ya mwisho yatatolewa mahakamani.

Nne: Iwapo wote dereva na muathirika wamesababisha ajali basi kila mmoja kati yao atawajibika kwa dhara alilomsababishia mwengine katika mwili, roho au mali.

Tano:

a) Pamoja na kuzingatia maelezo ya ziada yanayofuata; ijulikane kua anaehusika na tendo la ajali atawajibika hata kama hakukusudia, ama msababishaji wa ajali atawajibika pale anapokusudia au kuilazimisha ajali hio.
b) Wote mtendaji na msababishaji wa ajali wanapoingia kwenye ajali; basi mtendaji ndie atakaewajibika, ila iwapo msababishaji alichupa mipaka kwenye kusababisha ajali hio na mtendaji hakuchupa mipaka.
c) ZInapokutana sababu mbili tofauti na kila moja imechangia kuleta

dhara basi kila msababishaji atawajibika kwa kiwango cha dhara alichomuathiri mwengine, na wakilingana kwenye kiwango cha dhara au ikashindwa kujulikana kiwango cha dhara basi wote watashirikiana sawa kwa sawa katika uwajibikaji.

Allah ndie Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 72 (3/8)[1]

Yanayohusiana na 'Biashara ya Urbuni'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Biashara ya Urbuni,** na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Maana ya biashara ya 'Urbuni' (malipo ya awali - dhamana) ni kuuza bidhaa ambapo mnunuzi anatanguliza kulipa kima fulani kwa muuzaji kwa makubaliano kwamba akiinunua bidhaa hio basi atalipa pesa zilizosalia, ama akiamua kutonunua basi kile kima alicholipa kama 'urbuni' kitasalia kwa muuzaji. Na kwa mfano huu wa biashara basi hata miamala ya kukodi inakua hivyo hivyo kwa kua kukodi ni aina ya biashara ya matumizi kwa manufaa ya mkodishwaji.

Mbili: Inajuzu biashara hii ya urbuni iwapo mda wa kusubiri umeainishwa na siku au tarehe fulani. Malipo ya urbuni yatahesabiwa (yatazingatiwa) kama sehemu ya thamani ya bidhaa inayokusudiwa iwapo biashara itakamilika, lakini urbuni itakua ni haki ya muuaji endapo mnunuzi kaamua kutonunua na mda waliokubaliana ushapita.

Allah ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 8, Mjeledi 1, Uk. 641).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 73 (4/8)[1]

Yanayohusiana na 'Biashara ya Mnada'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Biashara ya Mnada,** na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya; na kwa kua biashara za minada ni miongoni mwa biashara zilizoenea kwa wingi zama hizi, na kwa kua pamekua na ukiukwaji wa taratibu; hivyo basi ipo haja ya kudhibiti namna miamala hii inavyoendeshwa ili kulinda haki za wanaoamiliana kwa mujibu wa sharia za Kiislamu na kama ilivyokubalika na taasisi na serikali mbalimbali na kuziwekea vigezo vya kinidhamu, na kwa lengo la kuweka bayana hukumu za kisharia ya miamala hii;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Mnada ni muamala wa biashara unaotegemea kuwaita wanunuzi ima kwa sauti au kwa maandishi kushiriki katika biashara ya mnada, biashara inakamilika kwa ridhaa ya muuzaji.

Mbili: Zipo anwai kadhaa za mnada kama vile miamala ya kuuza na miamala ya kukodisha na miamala mengineo, aidha biashara ya mnada inakua ya hiari ya kawaida au inakua ya lazima kama ile inayoratibiwa na amri ya mahkama, hali kadhalika biashara hii ya mnada inatumiwa na taasisi za umma na taasisi binafsi na mashirika ya serikali na watu wa kawaida.

Tatu: Taratibu zote zinazotumika katika miamala ya minada kama vile

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 8, Mjeledi 2, Uk. 25).

kurekodi, kurasimu, kudhibiti na kuweka masharti ya kiutawala au kisheria ni lazima mambo yote hayo yasigongane na hukmu za sharia ya Kiislamu.

Nne: Inajuzu kuomba malipo ya dhamana kwa anaetaka kuingia mnadani, lakini malipo hayo yatarudishiwa wenyewe endapo hawakufanikiwa kubarikiwa mnada, ama kwa kwa yule aliebarikiwa mnada basi malipo yake ya dhamana yatahesabiwa kwenye thamani ya makubaliano.

Tano: Hakuna katazo la kisharia la kuweka tozo ya kiingilio kwenye soko la mnada.

Sita: Inajuzu kwa benki za Kiislamu au nyenginezo kuweka miradi ya uwekezaji kwa lengo la kupata faida bila kujali muekezaji yuko katika mkataba wa mudaraba na benki au la.

Saba: al-Najash (Udanganyifu) ni haramu, na inakuja katika sampuli hizi:

a) Ni mtu asietaka kununua, lakini anamzidishia mteja thamani ya bidhaa ili ahadaike aone kua bidhaa hio ina thamani kubwa.
b) Mtu asietaka kununua anajifanya kama anapendezwa na bidhaa husika na kuisifu ubora wake ili amdanganye mteja ainunue kwa thamani kubwa.
c) Kudai madai ya uongo kwa mmiliki wa bidhaa au wakala wake au dalali kwamba bidhaa husika imenunuliwa kwa bei kadhaa ya juu ili aipandishe thamani bidhaa hio.
d) Miongoni mwa njia za kisasa za *al-Najash* (udanganyifu) ni kutumia media na matangazo ya biashara yanayoelezea hali isiokua halisi ya bidhaa na kuipandisha thamani, mteja anadanganyika na kuinunua bidhaa hio.

Allah ndie Mjuzi Zaidi

≃≃≃

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 74 (5/8)[1]

Yanayohusiana na 'Hatua-Tekelezi za Kisharia za Kuanzisha Soko la Kiislamu'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Hatua-Tekelezi za Kisharia za Kuanzisha Soko la Kiislamu,** ambazo ni mwendelezo wa maudhui ya **"Masoko ya Kiislamu ya Pesa na Sarafu"**, tafiti ambazo zilijadiliwa kwenye vikao vilivyopita hasa kwenye kikao cha saba (7) na katika warsha zilizoandaliwa kwenye kikao hicho kwa lengo la kufikia njia muwafaka za uanzishwaji wa **'Soko la Pesa'**, soko hilo litakua ni chombo cha kuhifadhi na kukuza pesa ziliopo kwa wingi katika baadhi ya nchi za Kiislamu ili kutekeleza mipango ya maendeleo endelevu na uwiano katika nchi za Kiislamu nyingine. Baada ya usikivu wa kina wa hoja na mijadala iliyoibuka kuhusu mbinu gani muwafaka zaidi za kuanzisha soko la pesa la Kiislamu ili soko hili liwe imara na barabara kabisa kwa kutumia hisa, sukook (hati-fungani), na mikataba maalum ya kusimamisha soko la Kiislamu kwa misingi ya Kisharia;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Hisa

'Kongamano la Fiqhi ya Kiislamu' lilitoa 'Maamuzi' yake namba 63 (1/7) yanayohusiana na 'Masoko ya Pesa': Hisa, Chaguzi (Hiari), Bidhaa na Sarafu' na likabainisha hukumu zake kwa namna ambayo itawezesha kuanzishwa kwa Soko la Kiislamu la Fedha.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 8, Mjeledi 2, Uk. 373).

Mbili: Sukook (Hati-fungani)

a) ‘Kongamano la Fiqhi ya Kiislamu’ lilitoa ‘Maamuzi’ yake namba 30 (5/4) yanayohusiana na Hati-fungani (Sukook) za Mudaraba na Hati-fungani za Uwekezaji.
b) ‘Kongamano la Fiqhi ya Kiislamu’ lilitoa ‘Maamuzi’ yake namba 44 (6/5) yanayohusiana na **‘Kukodi Inayoishia Kumiliki’.** Hati hizi zina nafasi nzuri katika soko-fedha la Kiislamu kwenye sekta ya manufaa.

Tatu: Biashara ya *Salam* (Kununua sasa kukabidhiwa bidhaa baadae)

Kwa kua biashara ya Salam, kwa masharti yake, imetanuka sana kiasi kwamba mnunuzi anapata fursa ya kuwekeza fedha zake zilizomzidi na kupata faida ya ziada, hali kadhalika muuzaji anafaidika na pesa hizo kuzidisha uzalishaji wa bidhaa, pamoja na kukazia Maamuzi ya Kongamano namba 63 (1/7) yanayohusiana na kutojuzu kuuza bidhaa iliyonunuliwa kwa njia ya Salam kabla haijakabidhiwa bidhaa husika.

Nne: Mkataba wa *Istisnaa* (Kutengenezewa Bidhaa): Kongamano lilishatoa Maamuzi yake namba 65 (3/7) yanayohusiana na mikataba ya *Istisnaa*.

Tano: *Bay’ al-Aajil* (Mauzo ya baadae)

Bay’ al-Aajil (Mauzo ya baadae) ni aina nyingine ya uwekezaji ambapo shughuli za mauzo zinawepesishwa, hivyo mnunuzi anafaidika kwa uwepo wa bidhaa hivi sasa, na kufanya malipo baadae, hali kadhalika muuzaji nae anafaidika kwa ongezeko la thamani ya bidhaa yake, matokeo ya muamala huu ni kutanuka kwa mzunguko wa bidhaa na kuenea katika jamii.[1]

Sita: Wa’d (Ahadi) na Muwa’ada (Ahadi ya pamoja)

Kongamano lilishatoa Maamuzi yake namba 40 na 41 (2,3/5) yahusuyo Wa’d (Ahadi) na Muwa’ada (Ahadi ya pamoja) katika miamala ya ‘Murabaha’ kwa anaeamrisha kununua (Aamir Bishiraai).

[1] Tizama Maamuzi namba 51 (2/6) na Maamuzi namba 64 (2/7) yahusuyo biashara ya malipo polepole.

Inapedekeza yafuatayo:

Kualika watafiti, wanazuoni na wanauchumi kuandaa tafiti katika maudhui ambazo hazikupekuliwa kwa kina ili kubaini uwezekano wa kutekeleza na kufaidika kisharia katika Soko la Pesa la Kiislamu, tafiti zenyewe ni hizi:

a) Hati-fungani (sukuk) za Musharaka za aina zote.
b) Hati-fungani (sukuk) za kukodi au kukodisha inayoishia kumiliki.
c) Malipo mbadala ya deni la *Salam,* Kuwakilisha au kushirikiana kwenye deni, punguzo la deni, kusuluhiana kwenye deni na mfano wa mambo kama hayo.
d) *Muwa'ada* (Ahadi ya pamoja) kwenye miamala isiokua ya Murabaha, hususan *muwa'ada* katika kubadili sarafu.
e) Kuuza deni.
f) Suluhu katika soko la fedha (malipo mbadala na mfano wake).
g) Kusafisha.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 75 (6/8)[1]

Yanayohusiana na 'Kadhia za Sarafu'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Kadhia za Sarafu,** na baada ya usikivu wa kina wa hoja na mijadala iliyoibuka kwenye mada husika;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Inafaa kwa nidhamu za kazi, sheria na taratibu zote zinazohusiana na mikataba ya wafanyakazi inayoainisha viwango vya mishahara, kufungamanisha mishahara hio na kiashiria cha 'ongezeko endelevu', lakini kwa sharti iwapo jambo hili halitopelekea kwa uchumi wa nchi kudhurika.

Kusudio la kufungamanisha mishahara na kiashiria cha 'ongezeko endelevu' ni kuweka nidhamu maalum ya ongezeko la mishahara kila baada ya mda fulani kulingana na mabadiliko na mifumuko ya bei kwa mujibu wa maelekezo ya wataalamu wenye ujuzi na utambuzi wa mas'ala haya kwa lengo la kulinda vipato (mishahara) vya wafayakazi dhidi ya sarafu inayokosa nguvu za ununuzi kutokana na mifumuko ya bei inayopeleka bidhaa na huduma kupanda bei kiholela.

Kufaynya hivi imetokana na msingi kwamba kuweka masharti inaruhusiwa ila ikiwa sharti hilo linahalalisha haramu au linaharamisha halali. Ijulikane kua malipo yanayolumbikizana yakawa madeni basi hukumu za madeni zilizobainishwa kwenye Maamuzi namba 42 (4/5) zitatumika.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 8, Mjeledi 3, Uk. 1650 na Toleo 5, Mjeledi 3, Uk. 1609).

Mbili: Inajuzu kwa mdai na mdaiwa kukubaliana siku ya malipo –sio kabla- kwamba deni wanalodaiana linaweza kulipwa kwa sarafu tofauti na ile sarafu iliyotumika wakati wa deni iwapo bei ya sarafu itakayozigatiwa ni ile ya siku ya kulipa. Halikadhalika inaruhusiwa kulipa deni la polepole kwa kutumia sarafu tofauti na ile sarafu iliyotumika wakati wa deni iwapo bei ya sarafu ni ile ya siku ya kulipa. Inashurutishwa katika hali zote kua hakuna salio la deni litakalobaki kwa mdaiwa bila kulilipa kwa mdai wake pamoja na kuzingatia Maamuzi ya Kongamao namba 50 (1/6) yahusuyo kukabidhiwa deni.

Tatu: Inajuzu kwa pande zote mbili za mkataba wakati wa kutia saini mkataba kuainisha thamani ya malipo ya baadae au ujira wa kulipwa baadae utakaolipwa kwa sarafu husika mara moja au kwa awamu kadhaa kwa kutumia sarafu mbalimbali au kwa kiwango cha dhahabu. Malipo yafanyike kwa mujibu wa makubaliano. Aidha inajuzu kufanya malipo kama ilivyotajwa katika kifungu kilichotangulia.

Nne: Haijuzu kurekodi deni lililopatikana kwa sarafu fulani na kutaka lilipwe deni hilo kwa thamani ya dhahabu au sarafu nyingine isiokua sarafu ya asili ya deni, yaani kumlazimisha mdaiwa alipe deni analodaiwa ima kwa dhahabu au kwa sarafu nyingine waliokubaliana kulipa.

Tano: Kuweka msisitizo juu ya ‘Azimio la Kongamano’ namba 42 (4/5) lililohusiana na ‘kubadilika kwa thamani ya sarafu’.

Na inapendekeza yafuatayo:

Tunaiomba Sekreterieti Kuu itafute watafiti wabobezi katika mas’ala ya sharia na uchumi wenye uchu wa fikra ya Kiislamu ili waandae tafiti za kina katika maudhui mbalimbali zinazohusiana na mas’ala ya sarafu, tafiti hizo ziwasilishwe kwenye vikao vya Kongamano vinavyokuja inshaallah, miongoni mwa maudhui zinazokusudiwa ni kama zifuatazo:

a) Uwezekano wa kutumia ‘Sarafu ya Kisheria’ kama vile ‘Dinar ya Kiislamu’ hususan katika miamala ‘Benki ya Kiislamu ya Maendeleo’ ili iwe ndio sarafu inayotumika kukopeshea wateja na kulipana, aidha kusajili madeni ya kulipwa baadae ili wakati wa kulipana

italinganishwa thamani ya Sarafu hii ya Kisheria na sarafu nyingine ya kigeni iliyochaguliwa kama vile Dola za Kimarekani.

b) Mbadala wa Kisharia wa kufungamanisha madeni ya kulipwa baadae na viashiria vya mabadiliko ya bei.
c) Ufahamu wa ‘Mgando wa Sarafu’ na athari zake katika kulipa madeni ya baadae.
d) Viwango vya mifumuko ya bei ambavyo vinaweza kuzingatiwa kua sarafu zimetulia au zimekosa thamani.

Allah ndie Mjuzi Zaidi

≋≋≋

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 76 (7/8)[1]

Yanayohusiana na 'Matatizo ya Benki za Kiislamu'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Matatizo ya Benki za Kiislamu',** na baada ya usikivu wa kina wa hoja na mijadala iliyoibuka kwenye mada husika, na baada ya Baraza la Kongamano kupitia nyaraka zilizowasilishwa kuhusiana na matatizo ya benki za Kiislamu pamoja na mapendekezo-elekezi ya kutatua matatizo hayo yanayogusa pande zote kama vile kisharia, kiutawala na kiufundi, na matatizo mengine yanayohusiana na pande za nje mbalimbali, baada ya usikivu kwa makini juu ya matatizo hayo;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuandaa orodha ifuatayo yenye vipengele vine kwa Sekreterieti Kuu ili watafute wataalamu husika wawasilishe katika vikao vya Kongamano vinavyokuja kulingana maoni ya Kamati-Mipango juu ya vipengele watakavyovipatia kipaombele.

Kipengele cha Kwanza: Pesa za akiba na yanayofungamana nayo

a) Kulinda pesa za uwekezaji kwa njia zinazoendana na hukmu za mudaraba.
b) Kubadilishana pesa baina ya benki na benki pasipo na misingi ya faida (riba).
c) Uwandaaji wa mazingira ya Kisharia ya uwekaji wa pesa za akiba na mifumo-chambuzi ya uhasibu.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 8, Mjeledi 3, Uk. 1650 na Toleo 5, Mjeledi 3, Uk. 1609).

d) Benki kumkopesha mteja pesa kwa sharti afanye miamala yake ya uwekezaji na benki husika au katika mradi fulani maalum.
e) Nani atakaebeba gharama za Mudaraba (Muwekezaji au chombo cha uwekezaji)
f) Kuchanganua uhusiano baina ya wawekaji akiba na wenyehisa.
g) Udalali katika mudaraba, kukodisha na dhamana.
h) Kuchanganua mudarib ni nani katika benki ya Kiislamu (wenyehisa, au bodi ya wasimamizi, au bodi ya watekelezaji).
i) Mbadala wa Kiislamu wa akaunti za kukopa.
j) Zaka za benki za Kiislamu kutokana na mali zake na akiba zake.

Kipengele cha pili: Murabaha

a) Murabaha katika hisa.
b) Kucheleweshe kusajili umiliki katika biashara za murabaha ili kuhakikisha haki ya benki imelindwa wakati wa malipo.
c) Murabaha inayocheleshwa kulipwa na kumuwakilisha anaeamuru kununua kua ni mdhamini.
d) Kucheleweshe kulipa madeni yanayotokana na murabaha au miamala ya malipo ya baadae.
e) Bima ya madeni.
f) Kuhawilisha (kuuza) deni.

Kipengele cha tatu: Kukodisha

a) Kukodisha tena mali iliyokodishwa kwa mmiliki au kwa mwingine.
b) Kukodi huduma-watu na kuzikodisha huduma hizo.
c) Kuzikodisha hisa au kuzikopesha au kuziweka rehani.
d) Utunzaji wa mali yaliyokodishwa.
e) Kununua mali kwa mtu kwa masharti aje akodi mali hio.
f) Kushikanisha baina kukodisha na mudaraba.

Kipengele cha Nne: Mikataba

a) Sharti la makubaliano juu ya haki ya benki kufuta mkataba iwapo deni la malipo ya polepole litacheleweshwa wakati wakati wake.

b) Sharti la makubaliano juu ya kubadilisha vifungu vya mkataba iwapo deni la malipo ya polepole litacheleweshwa wakati wakati wake.

Inapendekeza yafuatayo:

Moja: Benki za Kiislamu ziendeleza midahala na benki kuu za nchi za Kiislamu kwa minajili ya kuziwezesha benki za Kiislamu kutekeleza majukumu yake katika kuwekeza fedha za wateja wake kulingana na misingi ya Kiislamu inayoratibu shughuli za mabenki na zinazowiana na hali halisi ya benki hizo. Aidha benki kuu zisimamie mahitajio ya benki za Kiislamu kwenye kufikia malengo yake katika maendeleo ya taifa kwa mujibu wa nidhamu za ufuatiliaji zinazoendana na hali halisi ya shughuli za mabenki ya Kiislamu, na kuzitaka Jumuiya ya Nchi za Kiislamu (OIC) na Benki ya Kiislamu ya Maendeleo (IDB) kuitisha vikao maalum vya benki kuu za nchi za Kiislamu ili kuzipa nafasi kutekeleza mahitajio ya pendekezo hili.

Mbili: Benki za Kiislamu zijipange kuandaa viongozi na wafanyakazi watakaokua na uweledi na ujuzi wa namna benki za Kiislamu zinavyofanya kazi, na pia kuandaa programu maalum za mafundisho kwa kushirikiana Taasisi ya Kiislamu ya Utafiti na Mafundisho na taasisi nyinginezo zinazojihusisha na mafundisho ya benki za Kiislamu.

Tatu: Kuifanyia kazi kwa karibu miamala hii miwili ya *salam* (Kununua sasa kukabidhiwa bidhaa baadae) na *istisnaa* (Kutengenezewa Bidhaa) kwani miamala hii miwili ndio mbadala wa Kiislamu ya kugharamia uzalishaji wa bidhaa.

Nne: Kupunguza kadri iwezekanavyo kutumia utaratibu wa murabaha kwa anaeamrisha kununua na badala yake kuuingiza muamala huu kwenye program-tekelezi za benki ili kuepuka kuingia kwenye kukiuka maelekezo ya Sharia yanayoratibu miamala kama hii, lakini hamna tatizo kujishughulisha na miamala mingine ya kiuwekezaji kama vile; mudaraba, musharaka na kukodisha, pamoja na yote hayo kujizatiti katika ufuatiliaji na kutathmini kila baada ya mda fulani, aidha inatarjiwa kufaidika na hali zilizopo zinazokubalika katika mudaraba kwa lengo la kudhibiti kazi za

mudaraba na uhasibu makini wa matokeo yake.

Tano: Umuhimu wa kuanzishwa kwa ‘Soko la Biashara’ miongoni mwa nchi za Kiislamu badala ya kutumia soko la bidhaa la kimataifa liliopo ambapo ndani yake kunakua mikhalafa mingi inayokinzana na Sharia ya Kiislamu.

Sita: Kuzielekeza pesa zilizozidi kusimamia miradi na malengo ya maendeleo katika nchi za Kiislamu mbalimbali kupitia ushirikiano maalum baina ya benki za Kiislamu kuiipatia msukumo mifuko ya ywekezaji ya pamoja na kuanzisha miradi mikuu ya pamoja.

Saba: Kuharakisha uanzishwaji wa faharisi (viashiria) vinavyokubalika Kiislamu ili view mfumo-mbadala ya viashiria vya kutizama mienendo ya faida (riba) katika kuangalia viwango vya faida kwenye miamala.

Nane: Kutanua muundo-msingi wa ‘Soko la Fedha la Kiislamu’ kwa njia za hizi benki za Kiislamu wakishirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB) kutanua wigo wa ubunifu wao katika kushirikiana na kubadilishiana vifaa-tekelezi vya mifumo ya Taasisi za Fedha za Kiislamu miongoni mwa nchi za Kiislamu.

Tisa: Kuzitaka taasisi na halmashauri husika kuandaa nidhamu na mifumo itakayoweka misingi imara ya mbinu (fomula) za uwekezaji za Kiislamu kama vile: *mudaraba*, *musharaka*, *muzara’a* (mikataba ya kilimo), *musaqaa* (mikataba ya kilimo cha umwagiliaji), *salam*, *istisnaa* na kukodisha,

Kumi: Kuziomba benki za Kiislamu kuanzisha kituo cha taarifa kitakachokusanya taarifa za kutosha za wale wanaoamiliana na benki za Kiislamu na wafanya-biashara wakuu ili kiwe kituo hicho ni hadidu-rejea ya benki za Kiislamu na kufaidika nazo katika kushajiisha wawekezaji waaminifu wanaojulikana nakujiepusha na wadanganyifu.

Kumi na moja: Kuziomba benki za Kiislamu kuoanisha shughuli za ‘vyombo vya udhibiti wa Kisharia’ walivyonavyo na kuanzisha ‘Chombo-Shirikishi kitakachosimamia shughuli za benki zote za Kiislamu.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 77 (8/8)[1]

Yanayohusiana na 'Kushiriki kwenye Hisa za Makampuni yanayoamiliana na Riba'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993.

Baada ya kupitia 'Mapendekezo ya Warsha ya Uchumi' iliyoratibiwa na 'Sekreterieti Kuu' ya Kongamano hapo Jeddah kwa kushirikiana na 'Taasisi ya Kiislamu ya Utafiti na Mafunzo' iliyo chini ya Benki ya 'Kiislamu ya Maendeleo' juu ya; nini hukmu ya **Kushiriki kwenye Hisa za Makampuni yanayoamiliana na Riba**, pamoja na tafiti zilizoandaliwa kwenye Warsha hio. Kwa kuona umuhimu wa maudhui haya na kuweza kuzikamata nyanja zote na kuelewa kila kinachohusiana nayo pamoja na kujua maoni ya wanazuoni juu ya mas'ala haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuitaka 'Sekreterieti Kuu' iendelee kukusanya tafiti nyingine za ziada ili kuliwezesha 'Kongamano' liweze kuchukua maamuzi muwafaka katika kikao kijacho.[2]

Wabillah al-Taufiq

≃≃≃

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 6, Mjeledi 2, Uk. 1273. Na Toleo la 7, Mjeledi 1, Uk. 73. Na Toleo 9, Mjeledi 2, Uk. 5).

[2] Tizama 'Maamuzi namba 63 (1/7) na 'Maamuzi namba 87 (4/9).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 78 (9/8)[1]

Yanayohusiana na 'Kadi za Mikopo (Credit Card)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Kadi za Mikopo (Credit Card)**, na baada ya usikivu wa kina wa hoja na mijadala iliyoibuka kwenye mada husika, na kwa kuona umuhimu wa maudhui haya na kuweza kuzikamata nyanja zote na kuelewa kila kinachohusiana nayo pamoja na kujua maoni ya wanazuoni juu ya mas'ala haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuitaka 'Sekreterieti Kuu' iendelee kukusanya tafiti nyingine za ziada ili kuliwezesha 'Kongamano' liweze kuchukua maamuzi muwafaka katika kikao kijacho.[2]

Wabillah al-Taufiq

≃≃≃

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 8, Mjeledi 2, Uk. 571).

[2] Tizama 'Maamuzi namba 63 (1/7) na 'Maamuzi namba 87 (4/9).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 79 (10/8)[1]

Yanayohusiana na 'Usiri kwenye Kazi za Udaktari'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Usiri kwenye Kazi za Udaktari**, na baada ya usikivu wa kina wa hoja na mijadala iliyoibuka kwenye mada husika;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Siri ni jambo ambalo mtu humtaka mwingine alihifadhe au alifiche ima kabla au baada ya jambo lenywewe, jambo la siri hujulikana kama ni siri kwa viashiria vinavyokubalika kwenye jamii kwamba jambo hili ni la siri kama vile mambo ya ndani ya mtu au ksoro zake ambazo hapendi watu wengine wazijue.

Mbili: Siri ni amana kwa yule alieaminiwa, na Sharia ya Kiislamu inalizimisha kutunza amana yoyote uliyoaminiwa nayo, na utunzaji wa amana pia ni miongoni mwa ustaarabu na adabu njema.

Tatu: Kimsingi, ufichuaji wa siri umekatazwa, na uficuaji wa siri bila ya kuwepo sababu ya msingi inayokubalika ni jambo ambalo linamuajibisha aliefanya hivyo.

Nne: Ulazima wa kuhifadhi siri unasisitizwa zaidi kwa wale wanaofanya kazi ambazo utowaji wa siri ni kuivunja kazi yenyewe kama vile kazi za utabibu (udaktari), kwani watu wanawaamini madaktari kiasi ya kwamba wako tayari kuwafichulia mambo yao ya ndani kwa lengo la kupatiwa ima ushauri au tiba, wenye haja ya tiba wanatoa mambo ya siri ya ndani

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 8, Mjeledi 3, Uk. 15).

yanayowahusu kwa madaktari, siri ambazo hawako tayari kuzitoa hata kwa jamaa zao wa karibu.

Tano: Iwapo kuficha siri kutaleta madhara zaidi kuliko kuifichua, au iwapo kuna maslahi zaidi kuifichuahio siri kuliko kuificha basi inajuzu kufichua siri hio, katika hali kama hii kuna mambo mawili:

a) Ni mazingira ambayo ufichuaji wa siri unakua ni lazima; hii ni kwa mujibu wa ibara ya kifiqhi inayosema: ni vyema kutenda dhara jepesi ili kuepuka dhara kubwa, na ibara nyingine ya kifiqhi inayosema: katika kulinda maslahi ya umma mtu anaweza kubeba dhara ili kuepusha dhara kwa umma, ikilazimika kufanya hivyo. Hali hizi ziko aina mbili:

   - Kukiga dhara kwa jamii.
   - Kukiga dhara kwa mtu binafsi.

b) Mazingira ambayo inajuzu kufichua siri; kwa malengo ya:

   - Kuleta maslahi kwa umma; au
   - Kuiepushia dhara jamii.

Katika hali hizi ni lazima kuzingatia malengo makuu ya Sharia kama yale ya kulinda dini, nafsi (roho) ya binadamu, akili, kizazi na mali.

Sita: Sehemu zinazolazimu au zinazojuzu kufichua siri ni lazima ziainishwe kwa uwazi kabisa kwenye nidhamu ya msingi ya sharia za kazi za tiba na katika nidhamu nyenginezo, aidha zitolewe maelezo bayana siri hizo zinafichuliwa vipi, wakati gani, kwa nani. Taasisi husika zinatakiwa ziwajulishe watu wote juu ya haya.

Inapendekeza yafuatayo:

Kuzitaka jumuia za watedaji wa mambo ya tiba, wizara za afya na vyuo vya elimu ya tiba kuingiza mambo haya katika mitaala yao na kujishughulisha kuwajulisha watendaji wote katika sekta ya afya juu ya maudhui haya, pamoja na kuadaa mitaala (curriculum) inayohusiana nayo na kufaidika na tafiti zinazowasilishwa kwenye maudhui haya.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 80 (11/8)[1]

Yanayohusiana na 'Maadili ya Daktari: Jukumu lake na Uwajibikaji wake'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Maadili ya Daktari: Jukumu lake a Uwajibikaji wake**, na baada ya usikivu wa kina wa hoja na mijadala iliyoibuka kwenye mada husika;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha utoaji wa maamuzi katika maudhui ya 'Maadili ya Daktari: Jukumu lake a Uwajibikaji wake' na maudhui ya 'Kujitibu kwa kutumia vitu vilivyoharamishwa' lakini pia inapendekeza itizamwe kanuni za kazi za utabibu (udaktari) zilizoandaliwa na Jumuia ya Kiislamu ya Elimu a Tiba', Kuwait pamoja na kuitaka 'Sekreterieti Kuu' kuendelea kukusanya tafiti a ziada katika maudhui haya na kuziwasilisha kwenye kikao kijacho.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 8, Mjeledi 3, Uk. 5).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 81 (12/8)[1]

Yanayohusiana na 'Daktari wa Kiume Kumtibu Mwanamke'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Daktari Mwanamume Kumtibu Mwanamke**, na baada ya usikivu wa kina wa hoja na mijadala iliyoibuka kwenye mada husika;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kimsingi anapokwepo daktari mwanamke mahiri basi atatakiwa yeye atibu wagonjwa wa kike, asipopatikana; inafaa kwa daktari mwanamke asiekua muislamu ambae ni muaminifu, asipopatikana; basi daktari mwanamume muislamu, asipopatikana; inafaa kwa daktari mwanamme asiekua muislamu ambae ni muaminifu, lakini ataruhusiwa tu kukagua kwenye mwili wa mwanamke zile sehemu husika pekee zinazohitajia kupimwa na kutibiwa, anatakiwa kuepuka kutizama sehemu nyingine zisizohitajika kadri inavyowezekana.

Aidha inatakiwa pindi atibiwapo mgonjwa wa kike na daktari wa kiume awepo 'Mahram' yaani mume au ndugu yake wa kiume au mwanamke mwengine muaminifu ili kuepuka 'faragha' yaani upweke wa mume na mke pekee.

'Taasisi za Afya' zinatakiwa kuongeza juhudi zao kushajiisha wanawake wakasomee elimu za tiba na kubobea katika nyanja zake mbalimbali hususan zile zinazohusiana na magonjwa ya wanawake na kuzalisha, hii ni kutokana na uhaba wa wanawake katika fani hii za tiba, ili tusiangukie kutumie vipengele vya dharura.

Wabillah al-Taufiq

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 8, Mjeledi 3, Uk. 9).

≋≋≋

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 82 (13/8)[1]

Yanayohusiana na 'Maradhi ya Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Maradhi ya Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI)**, na baada ya usikivu wa kina wa hoja na mijadala iliyoibuka kwenye mada husika; imebainika kwamba utendaji wa dhambi za zina na ulawiti ni sababu kuu magonjwa ya kijinsia ambayo hatari ya zaidi ni ukimwi (inayoambatana na upungufu wa kinga mwilini), hivyo basi kupambana na madhambi (machafu) haya na kuzielekeza vyombo vya habari na utalii katika muelekeo mzuri ni miongoni mwa sababu muhimu katika kjilinda na maovu haya, na bila shaka yoyote; kufuata mafundisho ya Uislamu na kupambana na maovu haya na kuvitakasa vyombo yva habari (mawasiliano) na kupia marufuku filamu chafu na kudhibiti utalii basi haya yote ni miongoni mwa sababu za msingi za kujilinda na magonjwa haya.

Imeamuliwa yafuatayo:

Iwapo mume au mke amesibiwa na ugonjwa huu basi amjulishe mwenzake na wasaidiane katika taratibu zote za kujikinga.

Inapendekeza yafuatayo:

Moja: Kuzitaka idara na taasisi husika katika nchi za Kiislamu kuchukua taratibu zote za tahadhari na kinga dhidi ya ukimwi, na kuweka sheria za

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 8, Mjeledi 5, Uk. 9).

adhabu kwa kila anaesabaisha kumuambukiza mwengine ugonjwa huu kwa makusudi. Aidha inapendekeza kwa serikali ya Saudi Arabia kuzidisha juhudi zao katika kuwalinda 'Wageni wa Rahman' (Mahujaji) na kuchukua taratibu na tahadhari zifaazo kuwalinda dhidi ya uwezekano wa kuambukizwa na ugonjwa huu wa ukimwi.

Mbili: Kutoa huduma kwa waliosibiwa na ugonjwa huu, inamlazimu kila aliesibiwa au aliebeba virusi vyake ajiepushe na kila jambo ambalo litapelekea kupasha wengine, pia inatakiwa kuwapatia watoto wenye virusi vya ukimwi elimu tosha kwa njia muwafaka.

Tatu: Kuitaka 'Sekreterieti Kuu' iwaombe madaktari na wanazuoni (wanafiqihi) waandae tafiti zifuatazo ili kukamilisha maudhui haya katika vikao vinavyokuja:[1]

a) Kumtenga mgonjwa wa ukimwi na mbeba virusi vyake.
b) Msimamo wa sehemu za kazi juu ya wagonjwa wa ukimwi.
c) Utoaji mimba kwa mwanamke mwenye virusi vya ukimwi.
d) Kutoa haki ya kufusahi (kufuta) ndoa kwa mke ambae mumewe ana virusi vya ukimwi.
e) Je, aliesibiwa na ugonjwa wa ukimwi ni sawa na kusema kasibiwa na maradhi ya kufa?
f) Kuna athari yoyote kwa mama mwenye ugonjwa wa ukimwi kumpunguzia haki yake ya kulea watoto wake?
g) Ni ipi hukmu ya sharia kwa mtu aliekusudia kuambukiza ukimwi kwa mwengine?
h) Kutibu (kuwalipa) waliosibiwa na virusi vya ukimwi kwa njia ya kuhamishiwa damu au vijinasaba vyake au kupachikwa viungo.
i) Kupitia mchakato wa ukaguzi wa tiba kabla ya kufunga ndoa ili kujikinga na hatari za magonjwa ya kuambukizana kama vile ukimwi.

Wabillah al-Taufiq

[1] Tizama 'Maamuzi namba 90 (7/9)

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 83 (14/8)

Yanayohusiana na 'Kuratibu Uandaaji wa Tafiti na Uwasilishwaji wake kwenye Vikao vya Kongamano'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993.

Baada ya kupitia taratibu za uchapishaji wa tafiti za 'Kongamano' na masharti yaliyowekwa kwenye tafiti hizo, na baada ya kusikiliza kwa makini changamoto zinazopatikana kwa waliokalifishwa kuandaa tafiti na kuainisha mda maalum wa kuwasilisha tafiti zao ili 'Sekreterieti Kuu' ipate mda wa kutosha kuzipitia tafiti hizo na kuzitathmini kwa mujibu wa 'taratibu za uchapishaji wa tafiti' zilizotajwa hapo juu;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Ifikapo mda ulioainishwa kuwasilishwa kwa tafiti kutoka kwa wataalamu waliopewa kazi hizo, Sekreterieti Kuu itakua na haki ya kuzingatia tafiti zilizowasilishwa na kuzitanguliza mbele ya kikao chca 'Kongamano' na kuziachia mbali tafiti zilizochelewa kufika kwa wakati.

Mbili: 'Sekreterieti Kuu' haitapokea tafiti zilizoandaliwa na wataalamu bila ya makubaliano ya awali kutoka Sekreterieti Kuu.

Tatu: Walioalikwa pekee miongoni mwa wajumbe wa 'Kongamano' na wataalamu na watafiti ndio watakaoshiriki kwenye mijadala ya tafiti.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅



Maamuzi na Maazimio ya Kikao cha Tisa (9) ya Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Abudhabi, Falme za Muungano wa Kiarabu (UAE)

1 – 6 Mfungo Pili (Dhulqa'ada), 1415

1 – 6 April, 1995

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 84 (1/9)[1]

Yanayohusiana na 'Biashara ya Dhahabu na Suluhisho la Kisharia Zikutanapo Ubadilishaji wa Pesa na Uhaulishaji'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tisa (9) kilichofanyika mji wa Abudhabi, Falme za Kiarabu Zilizoungana (UAE) 1 – 6 Mfungo Pili (Dhulqa'ada), 1415, sawa na 1 – 6 April, 1995.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Biashara ya Dhahabu na Suluhisho la Kisharia Zikutanapo Ubadilishaji wa Pesa na Uhaulishaji,** na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuhusu Biashara ya Dhahabu

a) Inajuzu kununua dhahabu na fedha kwa kutumia hundi (cheque) iliyosainiwa kwa sharti makabidhiano yafanyike papo kwa hapo.
b) Kushadadia kile walichokubaliana wengi ya wanafiqihi ya kutojuzu kuuziana dhahabu iliyofuliwa kwa kutumia dhahabu isiofuliwa itakayokua nyingi kwenye uzani wake kuliko ile iliofuliwa, kwani hakuna biashara ya dhahabu kwa dhahabu inayozingatiwa kwa kutofautisha ubora au ufuaji, kwa hivyo, 'Kongamano' linaonelea kua hakuna haja ya kupitia mas'ala haya kwa kua mas'ala haya hayapo tena katika biashara halisi za siku hizi kwa kua dhahabu siku hizi haitumiki tena kama sarafu baada ya kuingizwa sarafu za noti kuchukua nafasi hio ya dhahabu lakini inazingatiwa kua ni jinsi nyingine.
c) Inajuzu kubadilishana kiwango fulani cha dhahabu kwa kiwango

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 9, Mjeledi 1, Uk. 65).

kingine kidogo cha dhahabu na kuongezea kitu kingine, hii itakua ni kama kununua dhahabu kwa kutumia jinsi nyingine, ni sawa na kusema dhahabu iliozidi imenunuliwa kwa ile jinsi tofauti.

d) Kwa kua mas'ala yanayofuata yanahitajia ufahamu na utafiti wa ziada kisharia, basi maamuzi juu ya mas'ala haya yameakhirishwa mpaka pale maelezo-bainifu yatakapopatikana na kuweza kutofautisha; mas'ala yenyewe ni haya:

   - Kununua hisa kwenye kampuni zinazofanya kazi ya kuchimba dhahabu na fedha.
   - Kumiliki na kumilikisha dhahabu kupitia makabidhiano ya hati maalum zinazobainisha kiwango-ainishwa cha dhahabu kinachopatikana katika hazina ya ntoaji hati hii kwa namna ambayo itamuezesha mmiliki wa hati hii kuimiliki dhahabu-tajwa na hivyo kumpatia uwezo wa matumizi yake wakati wowote atakao.

Mbili: Suluhisho la Kisharia Zikutanapo Ubadilishaji wa Pesa na Uhaulishaji

a) Inajuzu kwa hawala ambazo muhaulishaji wake amelipia sarafu fulani na anataka zihaulishwe kwa sarafu hiohio, ni sawa kuwe na malipo ya uhaulishaji au hamna. Ikiwa hamna malipo ya uhaulishaji basi hio inazingatiwa kua ni hawala kwa wanazuoni wa Kihanafi ambao hawashurutishi kua hawala ni deni kwa muhaulishwaji, ama kwa wanazuoni wengine hio inajulikana kama: 'Saftaja' ambayo maana yake ni mtu (mtoaji) anampatia mwengine pesa ili amrejeshee mtoaji au wakala wake kwenye nchi nyingine, sasa muamala huu ukiwa na malipo basi inahesabiwa ni uwakilishaji wenye, ama iwapo wahaulishaji hawa wanawafanyia watu kazi hii basi watakua ni wenye kubeba dhimmi wa mali wanayoyapokea kwa mujibu wa sharia ya dhimma ya wakala.

b) Iwapo hawala zinatakiwa zilipwe huko zilikohaulishwa kwa sarafu nyingine tofauti na ile iliyolipwa inakotoka basi muamala huu utakua umekusanya kubadilisha na kuhaulisha kama ilivyoelezewa hapo juu kwenye ibara (a), itabidi mwanzo ufanyike muamala wa kubadilisha kabla kuhaulisha, ambapo mteja (zabuni) atakabidhi pesa kwa benki

na benki itasajili pesa walizokabidhiwa pamoja ubadilishaji wa pesa hizo kwenye sarafu-lengwa kisha ndipo muamala wa uhaulishaji uendelee kwa namna ulivyoashiiriwa.

Allah ndie Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 85 (2/9)[1]

Yanayohusiana na 'Utekelezaji wa Kisasa wa *Salam*'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tisa (9) kilichofanyika mji wa Abudhabi, Falme za Kiarabu Zilizoungana (UAE) 1 – 6 Mfungo Pili (Dhulqa'ada), 1415, sawa na 1 – 6 April, 1995.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Utekelezaji wa Kisasa wa '*Salam*',** na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuhusu '*Salam*'

a) Bidhaa zinazoweza kufanyiwa biashara kwa njia ya '*salam*' ni kila bidhaa iayoujuzu kuuzwa ambayo inaweza kuainishwa na kuthibiti kua ni deni kwa mbeba dhima, ni sawa bidhaa hio iwe ni ghafi au mazao ya kilimo au bidhaa inayotengenezwa viwandani.
b) Kwa biashara ya *Salam* ni lazma mda wa kukaidhi bidhaa uainishwe au tarehe itajwe au ifungamanishwe na jambo kuu fulani kama vile 'wakati wa mavuno'.
c) Kimsingi kwenye biashara ya *Salam* malipo yanatakiwa yafanyike kwenye kikao cha makubaliano, lakini inajuzu kuchelewesha kidogo kwa siku mbili tatu hata kama ni sharti hilo, ila mda wa kuchelewesha malipo hautakiwi ulingane au upite mda wa *Salam*.
d) Hakuna katazo la kisharia kwa mnunuzi wa *Salam* kudai rehani au mdhamini kutoka kwa muuzaji wa *Salam*.
e) Inajuzu kwa mnunuzi wa *Salam* kutaka kubadilisha bidhaa waliokubaliana kwa bidhaa nyingine – lakini sio pesa – baada ya

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 9, Mjeledi 1, Uk. 371).

kupita mda waliokubalina, ni sawa kinachobadilishiwa iwe ni jinsi ileile ya bidhaa waliokubaliana au jinsi nyingine, hii ni kwa sababu hakuna riwaya yoyote iliyopokelewa kukataza jambo hili, alimradi kinachobadilishiwa iwe ni bidhaa inayowezekana kufanyiwa biashara ya *Salam*.

f) Endapo muuzaji wa *Salam* ameshindwa kukabidhi bidhaa kwa wakati, basi mnunuzi atakua na hiari ima kusubiri bidhaa yake au kufuta makualiano na kudai pesa zake, ikiwa muuzaji kachelewa kwa sababu zilizo nje ya uwezo wake basi ni bora kumpa mda.
g) Haijuzu kuweka sharti la adhabu kwa kuhcelewa kukabidhi bidhaa, kufanya hivyo ni sawa na kudai ziada juu ya deni jambo ambalo halifai.
h) Haijuzu kulifanya deni kua ni malipo ya *Salam*, kwani hio itakua ni sawa na kuuza deni kwa deni.

Mbili: Kuhusu Utekelezaji wa Kisasa wa '*Salam*'

Miamala ya *Salam* kwa ulimwengu wa leo ni kifaa muhimu cha kugharamia uzalishaji na chenye uwezo mkubwa kwenye uchumi wa Kiislamu na katika shughuli za benki za Kiislamu, kwani kifaa hiki kina ulaini wa kuweza kuitikia mahitajio mbalimbali ya kugharamia ya mda mfupi, wastani na hata mrefu, pia kina uwezo wa kuhudumia mahitajio ya watu wa tabaka mbalimbali miongoni mwa wateja; wakiwemo wazalishaji-wakulima, wanaviwanda, wakandarasi na wafanyabiashara, aidha kifaa hiki kina uwezo wa kugharamia gharama za uendeshaji na shughuli nyenginezo za rasilimali.

Kwa maana hio; nyanja za utekelezaji wa miamala ya *Salam* zimekua nyingi zikiwemo:

a) Miamala (mikataba) ya *Salam* inaweza kugharamia shughuli mbalimbali za uzalishaji-kilimo, kwani benki za Kiislamu zinaweza kuamiliana na wakulima wanaotarajia kua na bidhaa katika mavuno yao ya msimu au mavuno yaw engine ambayo wanaweza kununua na kukabidhi iwapo mavuno yao hayakukidhi makubaliano, pesa hizi wanazolipwa zikiwa ni muamala wa *Salam* zitawanufaisha sana

wakulima hawa na kuwapunguzia uzito wa kuzalisha kilimo chao.

b) Inawezekana pia kutumia miamala (mikataba) ya *Salam* katika kugharamia shughuli za uzalishaji kilimo na viwandani, hususan kwenye awamu za mwanzo za uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa zilizotengenezwa kwa njia ya kuzinunua bidhaa hizo kupitia miamala ya *Salam* na baada ya hapo kuziuza kwa bei yenye kuleta faida.
c) Aidha inawezekana kutekeleza mikataba ya *Salam* katika kugharamia wenye kazi za mikono na wakulima wadogo wadogo na wazalishaji bidhaa wadogo wadogo kwa njia ya kuwapatia vitendea kazi za uzalishaji kama vile vifaa, mali ghafi, rasilimali ili wakabidhi bidhaa wanazozalisha na kwa mnunuzi wa *Salam* aweze kuuza bidhaa hizo.

Baraza linapendekeza yafuatayo:

Kukamilisha aina nyingine za Utekelezaji wa Kisasa wa '*Salam*' baadaa ya kuandaa tafiti-tahasusi.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 86 (3/9)[1]

Yanayohusiana na 'Akiba za Kibenki (Akaunti za Benki)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tisa (9) kilichofanyika mji wa Abudhabi, Falme za Kiarabu Zilizoungana (UAE) 1 – 6 Mfungo Pili (Dhulqa'ada), 1415, sawa na 1 – 6 April, 1995.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Akiba za Kibenki (Akaunti za Benki),** na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Akiba zinazoweza kuombwa wakati wowote (akaunti za biashara au current account) ni sawa ziwe kwenye benki za Kiislamu au zile za riba, zinabeba hukmu ya deni (mkopo) kwa mtazamo wa kifiqhi, hii ni kwa kua benki inayopokea akiba hizi wanabeba dhamana ya kulinda mali haya na wanatakiwa kua tayari wakati wowote kurudisha dhamana hio inapohitajika. Haijalishi hukmu hii ya deni iwapo benki (wakopeshwa) wana pesa au hawana.

Mbili: Akiba za Kibenki zinagawika sehemu mbili kulingana na hali halisi ya miamala ya kibenki:

a) Akiba zinazolipiwa mgao wa faida, kama ilivyo katika benki za riba, hio inakua ni mikopo ya riba iliyoharamishwa, ni sawa akiba ziwe zimewekwa kwenye akaunti ya current au akiba za baadae, au akiba inayotwaliwa baada ya kutoa taarifa, au akiba ya kukuza (faida).
b) Akiba zinazowekwa kwenye benki zinazofuata mfumo wa Sharia ya Kiislamu zinaingia kwenye mkataba wa uwekezaji wa akiba hizo ambazo zinachukuliwa kua ni rasilimali ya mudaraba na faida

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 9, Mjeledi 65, Uk. 667).

ipatikaayo itagawiwa kwa mujibu wa hukmu za mudaraba zijulikanazo kwenye fiqhi ya Kiislamu ambazo miongoni mwazo ni kutobebeshwa mudarib (benki) dhamana ya rasilimali za mudaraba.

Tatu: Dhamana katika akiba zinazoitishwa wakati wowote (Current Accounts) zinabebwa na wakopeshwaji (wenye hisa benki) kwa kua wao ndio wanaofaidika na faida zitokanazo na uwekezaji wa akiba hizo, wawekaji akiba kwenye mifuko ya uwekezaji hawatoshiriki kubeba dhamana za current accounts kwa kua wao si washiriki wa kukopeshwa wala kufaidika na faida hizo.

Nne: Inajuzu kuziekea akiba dhamana ya rehani, ni sawa akiba hizo ziwe ni zile kuitishwa wakati wowote (current) au akiba za uwekezaji, kuziekea akiba rehani haikamiliki ila baada ya mchakato mzima ambapo muweka akiba kwa dhamana ya rehani hataweza kuchukua pesa husika ndani ya mda wa rehani wote. Na iwapo benki ambayo akaunti hio ya current imefunguliwa ndio muweka rehani basi italazimu pesa hizo za akiba zihamishwe kwenda kwenye mfuko (akaunti) wa uwekezaji, kwa namna dhamana itaondoka kwa kua imebadilisha kutoka ‘mkopo’ kwenda ‘mudaraba’ na kwa maana hio mwenye akaunti hii anastahiki kupata gawio la faida na wakati huohuo kumzuia mkopeshaji kufaidika.

Tano: Inajuzu kuzigandisha akaunti iwapo kuna makubaliano baina ya benki na mteja.

Sita: Kimsingi, miamala yote inatakiwa ifanyike kwa misingi ya uaminifu, ukweli na uwazi katika kutoa maelezo kwa namna ambayo inaondosha utata na utatanishi, na iwe inaendana na hali halisi na kuwiana na maelekezo ya Sharia. Mambo haya yana msisitizo zaidi kwa benki kwa kua ni chombo kinachoaminiwa (dhaniwa) kua na uaminifu na kujiepusha na kila aina ya udanganyifu.

Allah ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 87 (4/9)[1]

Yanayohusiana na 'Uwekezaji kwenye Hisa na Mikoba ya Uwekezaji'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tisa (9) kilichofanyika mji wa Abudhabi, Falme za Kiarabu Zilizoungana (UAE) 1 – 6 Mfungo Pili (Dhulqa'ada), 1415, sawa na 1 – 6 April, 1995.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Uwekezaji kwenye Hisa na Mikoba ya Uwekezaji,** ambapo imebainika kua maudhui haya yamebeba vipengele vinavyohusiana na kununua hisa za makampuni ambayo kampuni hizo malengo yake na shughuli zake zinakubalika kisharia lakini wanakopa au kuweka mali yao kwenye akiba ya faida, maamuzi juu ya kadhia hii hayajafikiwa licha ya kuwepo kwa warsha mbili kutafutia ufunguzi, na licha ya kuwepo kwa maamuzi ya mwanzo ya msingi yaliyotolewa na 'Kongamano' kwenye kikao chake cha saba (7) na maamuzi yaliyofuatia kwenye kika cha nane (8)[2] kuitaka Sekreterieti Kuu kuendelea kutafuta wataalamu waandae tafiti-yakinifu kwenye maudhui haya ili maamuzi sahihi na muwafaka yaweze kuchukuliwa kwenye kikao kijacho, lakini baada ya kuanza kujadili hoja zilizoibuka, imebainika kua maudhui haya bado yanahitaji utafiti na upekuzi wa kina zaidi ili kuweka vigezo na vidhibiti kwa kampuni aina hizi ambazo zinapatikana kwa wingi sana katika nchi za Kiislamu na nje yake.

Hivyo basi; imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuakhirisha uchukuaji wa maamuzi katika kadhia hii hadi pale tafiti za kina zimeandaliwa zitakazogusia nyanja zote za kitaaluma na kisharia ili 'Kongamano' liweze kuchukua maamuzi sahihi kwa mujibu wa pendekezo

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 9, Mjeledi 2, Uk. 5. Na Toleo 6, Mjeledi 2, Uk. 273. Na Toleo 7, Mjeledi 1, Uk. 73).

[2] Tizama Maamuzi namba 63 (1/7) na Maamuzi namba 77 (8/8).

la kikao cha nane (8).

Mbili: Kufaidi kotokana na tafiti tatu zilizowasilishwa kuhusiana ‘Sanduku na Stakabadhi za uwekezaji’ ili kuandaa kanuni iliopendekezwa kwenye maamuzi namba 30 (5/4).[1]

Wabillah al-Taufiq

≋≋≋

[1] Tizama Maamuzi namba 30 (5/4)

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 88 (5/9)[1]

Yanayohusiana na 'Uzabuni (Tenders)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tisa (9) kilichofanyika mji wa Abudhabi, Falme za Kiarabu Zilizoungana (UAE) 1 – 6 Mfungo Pili (Dhulqa'ada), 1415, sawa na 1 – 6 April, 1995.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Uzabuni (Tenders),** na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya, na kuambatana na taratibu za 'Kongamano' kutoingia kwenye kuchukua maamuzi pasipo na uwepo wa tafiti maridhawa zinazoangazia kila nyanja na upeo wa kitaaluma na miondoko ya kifiqhi;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuakhirisha utoaji wa maamuzi juu ya nukta zilizowasilishwa kama maudhui haya; kutokana na umuhimu wake na ulazima uliopo wa kukamilisha utafiti katika nyanja zake zote na kupata ufahamu-zamivu juu maoni yaliyopo pamoja uelewa mpana wa harakati zote ambazo uzabuni unafanyika, hususan kujua maeneo yaliokua na uharamu ndani yake kama vile stakabadhi za feda za riba na hati za hazina (treasury bonds).

Mbili: Wajumbe na wataalamu wa 'Kongamano' wanatakiwa kuwapatia 'Sekreterieti Kuu' – ima kabla ya kikao kuisha ikiwezekana au baada ya kikao katika mda usiokua mrefu – nukta za kitaaluma na/au za kisharia zinazohusiana na maudhui hii ya uzabuni, sawa ziwe kwa upande wa mchakato ibara za mikataba ambayo uzabuni unasimamia ufungaji wa mikataba kama hio.

Tatu: Kuandikia wataalamu ili waandae tafiti nyingine katika maudhui ya

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 9, Mjeledi 1, Uk. 179).

uzabuni ambapo wanataaluma na wanafiqihi na watu wenye utambuzi katika fani hii wataweza kuchangia kwa namna moja au nyingine.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 89 (6/9)[1]

Yanayohusiana na 'Kadhia za Sarafu'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tisa (9) kilichofanyika mji wa Abudhabi, Falme za Kiarabu Zilizoungana (UAE) 1 – 6 Mfungo Pili (Dhulqa'ada), 1415, sawa na 1 – 6 April, 1995.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **'Kadhia za Sarafu,** na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya, imebainika kua kunapatikana miondoko (mitazamo) mingi inayoliendea tatizo la 'Mifumuko ya Bei' (*inflation*) ambalo linapelekea 'Mporomoko wa Sarafu' (nguvu za ununuzi – *purchasing power*), miongoni kwa suluhisho ya tatizo hili:

a) Hali hizi zisizokua za kawaida zinatakiwa ziwiane na utekelezaji wa maamuzi ya 'Kongamano' ya kikao cha tano (5)[2] yanayosema: "*Ulipaji wa madeni yaliyothibiti kwa sarafu fulani inatakiwa yalipwe kwa sarafu ileile, kwani haijuzu kufungamanisha madeni na viwango vya bei inavyobadilika*"
b) Katika hali hizi zisizokua za kawaida inatakiwa kwenye utekelezaji wake kuzingatia msingi wa viashiria vya gharama za maisha (kuzingatia nguvu za ununuzi za sarafu).
c) Msingi wa kufungamanisha baina ya pesa za noti na dhahabu utumike (kuzingatia kima cha pesa kwa thamani ya dhahabu wakati wa kufunga mikataba).
d) Kuutumia msingi wa 'Suluhu ni Wajib' katika hali kama hizi baada ya kutathmini madhara ya pande zote mbili za deni (mdai na mdaiwa).
e) Kutofautisha baina ya kushuka kwa thamani ya sarafu itokanayo na sababu za 'kanuni ya kutaka na kuuza' (law of supply and demand), na sera za serikali kushusha thamani ya sarafu kupitia tangazo rasmi

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 9, Mjeledi 1, Uk. 351. Na Toleo 3 Mjeledi 3, Uk. 1650 Na Toleo 5, Mjeledi 3, Uk. 1609).
[2] Tizama maamuzi namba 42 (4//5).

lilio wazi, jambo ambalo litapelekea kwa sarafu kukosa thamani yake.

f) Kutofautisha baina ya kushuka kwa nguvu za ununuzi wa sarafu inayotokana na sera za serikali, na kushuka kunakotokana sababu za nje.
g) Kuzingatia kwenye hali hizi msingi wa ‘Hali halisi ilivyo’ ambayo ni kuzingatia hali zilivyo kwa wakati husika.

Kwa mujibu wa miondoko kama hii iliotajwa ndio inayohitaji utafiti wa ziada.

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: ‘Sekreterieti Kuu’ ya Kongamano ikishirikiana na mojawapo ya Taasisi za Kiislamu za Fedah, waandae warsha maalum itakayoshirikisha wataalamu katika fani za uchumi na sharia wakiwemo wajumbe na wataalamu wa ‘Kongamano’, ili wapate kutizama kwa marefu na mapana ni njia zipi muafaka zaidi ambazo wanaweza kukubaliana ulipaji wa madeni yaliyo kwenye dhima kwenye hali kama hizi zisizo za kawaida zilizotajwa hapo juu.

Mbili: Warsha inayokusudiwa ijadili agenda hizi:

a) Kubaini kwa undani kiini cha ‘Mfumuko wa Bei’ na aina zake na nyanja zake zote za kitaaluma zinazohusiana nayo.
b) Kubaini athari za ‘Mfumuko wa Bei’ kiuchumi na kijamii na namna ya kulitatua tatizo hili kiuchumi.
c) Kupendekeza suluhisho za kifiqhi za kutibu tatizo la ‘Mfumuko wa Bei’ kama ilivyoashiriwa kwenye utangulizi wa ‘maamuzi’.

Tatu: Matokeo ya warsha hii pamoja na nyaraka zilizojadiliwa ziwasilishwe kwenye ‘Baraza la Kongamano’ katika kikao kijacho.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 90 (7/9)[1]

Yanayohusiana na 'Maradhi ya Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI) na Hukmu za Kifiqhi Zinazohusiana nayo'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tisa (9) kilichofanyika mji wa Abudhabi, Falme za Kiarabu Zilizoungana (UAE) 1 – 6 Mfungo Pili (Dhulqa'ada), 1415, sawa na 1 – 6 April, 1995.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Maradhi ya Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI) na Hukmu za Kifiqhi Zinazohusiana nayo,** na **kupitia 'Maamuzi namba 82 (13/8)** na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kumtenga Mgonjwa

Taarifa za kimatibabu zilizopo kwa sasa zinathibitisha kwamba uambukizaji wa ugonjwa wa 'Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI)' hausambazwi kwa njia ya kuishi pamoja na mkonjwa au kumshika kimwili au pumzi au wadudu au kula na kunywa pamoja au kwenye mabirika (Swimming Pool) ya kuogelea au makalio au vifaa vya ulaji na mfano wa vitu kama hivyo katika maisha ya kawaida ya kila siku, lakini unasambazwa kimsingi kupitia mojawapo wa njia hizi:

1) Mawasiliano ya kijinsia kwa namna yoyote ile.
2) Kuhamisha damu iliyoathirika na vitokanavyo na damu.
3) Utumiaji wa sindano iliyoathirika hasa miongoni mwa mateja wa mihadarati na pia viwembe vya kinyozi.
4) Mama mzazi muathirika anamsambazia mwanawe wakati wa mazazi.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 8, Mjeledi 3, Uk. 9).

Kwa mujibu wa hayo yaliyotangulia kuwatenga waathirika pasipo na hofu ya wao kuwaambukiza wengine, marafiki na jamaa zao, si jambo la lazima kisharia, lakini taratibu za tahadhari zitachukuliwa kulingana na ushauri wa daktari.

Mbili: Kukusudia kuusambaza ugonjwa

Kukusudia kuambukiza ugonjwa wa wa Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI) kwa namna yoyte ile ni '*Haramu*' na nia katika madhambi makubwa kabisa, aidha mtenda wa dhambi hili anastahiki adhabu kali, kiwango cha adhabu kitaendana na ukubwa wa tendo lake na athari mbaya atakayo wapatia watu na jamii kwa ujumla.

Ikiwa lengo la huyu anaesambaza kwa makusudi ni kuyaeneza maradhi haya mabaya kwenye jamii, basi tendo lake hili linachukuliwa kosa kuu la jinai na ufisadi katika jamii ambalo liastahiki adhabu ya 'Hiraba' iliyotajwa katika Qur'an:

"إِنَّمَا جَزَٰٓؤُاْ ٱلَّذِينَ يُحَارِبُونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ وَيَسۡعَوۡنَ فِي ٱلۡأَرۡضِ فَسَادًا أَن يُقَتَّلُوٓاْ أَوۡ يُصَلَّبُوٓاْ أَوۡ تُقَطَّعَ أَيۡدِيهِمۡ وَأَرۡجُلُهُم مِّنۡ خِلَٰفٍ أَوۡ يُنفَوۡاْ مِنَ ٱلۡأَرۡضِۚ ذَٰلِكَ لَهُمۡ خِزۡيٞ فِي ٱلدُّنۡيَاۖ وَلَهُمۡ فِي ٱلۡأٓخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ"

Hakika malipo ya wale wanaompiga vita Mwenyezi Mungu na wanaojitokeza wazi kumfanyia uadui na kuzifanyia uadui hukumu zake na hukumu za Mtume Wake na kufanya uharibifu katika ardhi kwa kuwaua watu na kupora mali, ni wauawe au wasulubiwe pamoja na kuuawa (Kusululubiwa ni kufungwa mhalifu juu ya bao) au ukatwe mkono wa kulia wa mpiga vita na mguu wake wa kushoto. Iwapo hatatubu {kwa kuendelea na uharamia wake}, ukatwe mkono wake wa kushoto na mguu wa kulia, au wahamishwe wapelekwe mji usiokuwa wao, wafungwe kwenye jela ya mji huo mpaka iyonekane toba yao. Na haya ndiyo malipo Aliyoyaandika Mwenyezi Mungu kwa wenye kupiga vita; nayo ni unyonge wa duniani. Na huko Akhera itawapata adhabu kali iwapo hawatatubia".[1]

Ama ikiwa kusudio lake la kusambaza ugonjwa huu ni kumuambukiza mlengwa fulani, na akaambukizwa lakini hajafa, basi alietenda kosa hili

[1] Surat al-Maida: 33.

atapewa adhabu inayoendana na kosa hilo, na lau mhanga wa kuambukizwa atakufa basi adhabu ya kuuawa itazingatiwa.

Ama ikiwa kusudio lake la kusambaza ugonjwa huu ni kumuambukiza mlengwa fulani, lakini hakuambukizika basi alietenda kosa hili atapewa adhabu inayoendana na kosa hilo; *Kuaziriwa*.

Tatu: Utoaji wa mimba kwa mama aliesibiwa na maambukizi ya 'Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI)' kwa mwanawe haitokei ila baada ya mimba kukua – baada ya kupulizwa roho kwa mtoto – au wakati wa mazazi, utoaji wa mimba haifai kisharia.

Nne: Mama aliesibiwa na maambukizi ya 'Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI)' kumlea mtoto wake mzima na kumnyonyesha

Kwa kua taarifa za kimatibabu zilizopo kwa sasa zinaonyesha kua hakuna hatari ya maambukizi kutoka kwa mama aliesibiwa na maambukizi ya 'Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI)' kwenda kwa mwanawe anaemlea au kumnyonyesha, ni sawa tu na kuishi maisha ya kawaida na mtu alietharika, kwa maana hio hakuna katazo la kisharia kwa mama huyu kuendelea kumyonyesha na kumlea mwanawe, ila ikiwepo ripoti ya daktari inayokataza jambo hilo.

Tano: Haki ya mume au mke aliesalimika kutaka kufarikiana na mwenzake alieathihrika

Mke alieasalimika anaruhusiwa kuomba kufarikiana na mumewe alieathirika kwa kuzingatia kua uambukizaji wa maradhi ya 'Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI)' unafanyika panapo mahusiano ya kijinsia.

Sita: Ugonjwa wa 'Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI)' unazingatiwa kua ni ugonjwa wa mauti kisharia pale zitokeapo athari zake na muathirika akawa kwenye hali mahututi na hawezi kuendelea na shughuli zake za kawaida na umauti ukawa karibu nae.

Inapendekeza:

Moja: Kuakhirisha kutoa maamuzi kwenye maudhui ya haki za 'Kitandani' panapo maambukizi ya 'Ukimwi' baina ya 'wanandoa' hadi pale tafiti zitakapokamilika.

Mbili: Kuongeza msisitizo nyakati za misimu ya hija kuwakinga mahujaji dhidi ya magonjwa ya miripuko, hususan ugonjwa wa ‘Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI)’.

Wabillah al-Taufiq

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 91 (8/9)[1]

Yanayohusiana na 'Misingi ya Kutafuta Suluhu katika Fiqhi ya Kiislamu'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tisa (9) kilichofanyika mji wa Abudhabi, Falme za Kiarabu Zilizoungana (UAE) 1 – 6 Mfungo Pili (Dhulqa'ada), 1415, sawa na 1 – 6 April, 1995.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Misingi ya Kutafuta Suluhu katika Fiqhi ya Kiislamu,** na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Utafutaji wa Suluhu ni pale pande mbili za utesi (wanaozozana au kukhtalifiana) wanapokubaliana kuweka mtu kati yao ili asuluhishe utesi uliopo baina yao kwa hukmu itakayoambatana na Sharia ya Kiislamu. Jambo hili la kutafuta suluhu ni jambo zuri kisharia, nisawa liwe baina ya watu au baina nchi kwa nchi katika mizozano ya kimataifa.

Mbilli: Utafutaji wa Suluhu ni mkataba usiolazimisha pande mbili za utesi na kwa mtoaji hukumu, kwa hio inajuzu kwa moja ya pande mbili za utesi kukataa kusuluhishwa iwapo mchakato wa suluhu bado haujaanza, aidha inajuzu kwa mtoaji hukmu ya sulhu kujiuzulu – licha ya kwamba ashakubaliwa na pande zote mbili – madamu bado hajatoa hukmu yake, lakini haijuzu kwake yeye kumueka hakimu mwingine pasipo na idhini ya pande mbili, kwani idhini ya mwanzo ilimuhusu yeye kama yeye.

Tatu: Haijuzu kutoa hukmu kwa zile kadhia ambazo si haki ya mja bali ni haki ya Allah, kama vile '*adhabu za hududi*' (adhabu ambazo tayari

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 9, Mjeledi 4, Uk. 5).

zilishaainishwa kwenye Qur'an) au hukmu ambayo kutolewa kwake inakwenda kuthibitisha au kufuta hukmu nyingine ya mtu wa tatu asiehusika, kama vile '*Lian*' (talaka ya kulaaniana baina ya mume na mke kwa kisingizio cha zinaa) kwa kua hapa haki ya mtoto imefungamana na mojawapo ya pande za mzozano. Aidha haijuzu kutoa hukmu kwa hakimu ambae upeo wake wa kazi haumruhusu kuingilia kadhia hizi, hakimu yeyote anapotoa hukmu katika mambo asiyoruhusiwa basi hukmu yake hii iyakua ni batili na haitofanyiwa kazi.

Nne: Kwa yeyote anaetoa hukmu anatakiwa awe ametimiza vigezo vya kua kadhi (hakimu).

Tano: Ilivyo hukmu ya sulhu inapotolewa ni itekelezwe kwa hiari, lakini iwapo mmoja amekataa kuitekeleza hukmu hio iliotolewa basi kadhia hio itafikishwa mahakamani ili litoke agizo la kulazimisha utekelezaji wa hukmu ya sulhu hio, na mahkama haitakua na uwezo wa kubatilisha ila ikionekana kwamba pamefanyika dhulma ya wazi kabisa katika sulhu hio au inakinzana na hukmu ya sharia.

Sita: KAtika mazingira ya kutokuwepo kwa 'Mahkama za Kimataifa za Kiislamu' inajuzu kwa nchi au taasisi za Kiislamu kutafuta suluhu kwenye 'Mahkama za Kimataifa' zisizokua za Kiislamu kwa ajili ya kutafuta kile kinachoruhusiwa kisharia.

Inapendekeza yafuatayo:

Kuzitaka nchi wanachama wa 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC) kukamilisha taratibu stahiki za uanzishwaji wa 'Mahkama ya Uadilifu ya Kiislamu ya Kimataifa' na kuiwezesha ili itekeleza majukumu yake kwa mujibu wa nidhamu zilizowekwa.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 92 (9/9)[1]

Yanayohusiana na 'Kuzuia Sababu za Kupelekea Maovu (*Sadd Dharaai'*)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha tisa (9) kilichofanyika mji wa Abudhabi, Falme za Kiarabu Zilizoungana (UAE) 1 – 6 Mfungo Pili (Dhulqa'ada), 1415, sawa na 1 – 6 April, 1995.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Kuzuia Sababu za Kupelekea Maovu (*Sadd Dharaai'*)',** na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Kuzuia Sababu za Kupelekea Maovu (*Sadd Dharaai'*)' ni katika misingi ya asili ya sharia ya kiislamu, nayo ni: kuzuia yale mabo ambayo ni *mubaah* (halali) lakini yanaweza kupelekea mtu kupitia kwayo kuingia au kutenda mambo ambayo ni mabaya au yaliyokatazwa.
2) *Sadd Dharaai'* sio tu inakatazwa kwenye mambo yenye utata au kwa akiba ya maneno tu, lakini inatumika katika kila jambo ambalo hatimae linamfikisha mtu kwenye haramu.
3) *Sadd Dharaai'* inatutaka kuzuia aina zote za hila zinazopelekea kutenda yaliyokatazwa au kubatilishwa yaliyoamrishwa na sharia, tofauti iliopo baina ya *hila* (ujanja) na *sababu* (kisingizio) ni uwepo wa kusudio kwenye hila na sio kwenye sababu.
4) Sababu (*Dharaai*) zipo anwai:

    a) Itifaki ya wanazuoni ya kuzikataza: nazo ni zile sababu ambazo zimekatazwa ndani ya Qur'an tukufu na Sunna tukufu za Bwana

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 9, Mjeledi 3, Uk. 5).

Mtume Muhammad (SAW) au zile sababu zinazopelekea kwa uhakika au kwa dhana kuu kwenye madhara ya wazi, ni sawa ziwe njia hizo ni mubaah (halali) au mustahab (inapendekezwa) au ni waajib (lazima). Miongoni mwa aina hizi ni makubaliano ambayo panadhihirika ndani yake kusudio la kuingia kwenye haramu kwa kutaja waziwazi.

b) Itifaki ya wanazuoni ya kuzikubali: nazo ni zile ambazo maslahi yake ni makubwa ikilinganishwa na madhara yake.
c) Wanazuoni wamekhtalifiana juu yake: nazo ni zile sababu ambazo kwa mtazamo wa ki-nje ni sahihi lakini zina fiche ya ndani ya kufikia kwenye makatazo.

5) Kidhibiti cha Kuruhusu *Dharaai'*: Iwe inajulikana fika kwamba ni nadra kupelekea kwenye madhara, au upelekeaji wa maslahi ni mikubwa kuliko upelekeaji wa madhara. Ama Kidhibiti cha Kukataza *Dharaai'*: ni pale inapojulikana fika kwamba inapelekea kwenye madhara kwa uhakika au aghalabu au maharibiko (madhara) yake ni makubwa ikilinganishwa na maslahi yake.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Maamuzi na Maazimio ya Kikao cha Kumi (10) ya Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Jeddah, Falme ya Saudi Arabia (KSA)

23 – 28 Mfungo Tano (Swafar), 1418

28 Juni – 3 Julai, 1997

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 93 (1/10)[1]
Yanayohusiana na 'Mambo Yanayofunguza Saumu Kwenye Matibabu'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha kumi (10) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia (KSA) 23 – 28 Mfungo Tano (Swafar), 1418, sawa na 28 Juni – 3 Julai, 1997.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Mambo Yanayofunguza Saumu Kwenye Matibabu,** na baada ya kuzingatia tafiti, hoja na mapendekezo ya Warsha ya Fiqhi-Utabibu zilizowasilishwa kwenye kikao cha tisa (9) cha Jumuiya ya Kiislamu ya Sayansi za Tiba wakishirikiana na 'Kongamano' na Taasisi nyenginezo hapo Dar-Baydhaa (Casablanca), Morocco katika kipindi kuanzia 9 – 12 Swafar, 1418 H sawa na 14 – 17 Juni, 1007, na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya kwa kushirikiana na wanafiqihi na madaktari na kutizama dalili za Qur'an na Sunna na katika maneno ya wanafiqihi;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Mambo yafuatayo hayafunguzi saumu:

a) Tone la dawa linalotiwa kwenye jicho au sikio au pua au kuosha sikio au kibomba cha pua, kwa sharti ya kujiepusha kussingie kitu kupitia kwenye koo.
b) Tembe za matibabu (dawa) zinazowekwa chini ya ulimi kwa minajili ya kutibu kiungulia (muasho wa kifua) na nyenginezo, kwa sharti ya kujiepusha kussingie kitu kupitia kwenye koo.
c) Kinachoingia kwenye tupu ya mbele ya mwanamke kam dawa au kusafisha au darubini au kidole kwa minajili ya uchunguzi wa kimatibabu.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 10, Mjeledi 2, Uk. 7).

d) Kuingiza darubini au uzi na mfano wake kwenye mfuko wa uzazi.
e) Kinachoingia kwenye njia ya mkojo ya mwanamume au mwanamke kama vile bomba (nyembamba), au darubini, au kizuizi cha miale, au dawa maji ya kuoshea kibofu cha mkojo.
f) Kuchimba jino, au kung'oa, au kusafisha, au kupiga msuwaki, kwa sharti ya kujiepusha kussingie kitu kupitia kwenye koo.
g) Kusukutua, kuosha kinywa na kupiga kibomba sehemo ya mdomoni, kwa sharti ya kujiepusha kussingie kitu kupitia kwenye koo.
h) Sindano zinazodungwa kwenye ngozi au misuli au mishipa, isipokua zile ambazo zinabeba maji na chakula; hazifai.
i) Hewa ya Oksijini.
j) Hewa za kufisha ganzi, bora mgonjwa asipatiwe nyevunyevu za chakula.
k) Kinachopenya ndani ya mwili kupitia kwenye ngozi kama vile mafuta, marahamu na vigandisho vya dawa vinavyowekwa kwenye ngozi vilivyosheheni dawa au kemikali.
l) Kuingiza bomba (nyembamba) ndani ya mishipa kwa lengo kupiga picha au kutibu mirija ya moyo na mengineyo katika viungo.
m) Kuingiza darubini kupitia ukuta wa tumbo ili kuchunguza tumbo za ndani au kufanyia upasuaji (operesheni).
n) Kuchukua sampuli za ini au viungo vingine lakini bila ya kuingiza dawa.
o) Kuingiza darubini kupitia utumbo wa ndani (maeda) lakini bila ya kuingiza dawa au vitu vingine.
p) Kuingia kwa kitu chochote au dawa kwenye ubongo au uti wa mgongo (spinal cord) kwa ajili ya matibabu.
q) Kutapika bila ya kukusudia, tofauti na kukusudia.

Mbili: Ni vyema kwa tabibu (daktari) muislamu kumshauri mgonjwa wake kuakhirisha matibabu ambayo yanaweza kutibiwa baada ya kufutari miongoni mwa aina zilizotajwa hapo juu.

Tatu: Kuakhirisha kutoa maamuzi katika hali zifuatazo, kwani ipo haja ya kufanya tafiti za ziada kubaini athari zake kwa saumu pamoja msisitizo juu hukmu zinazojulikana kutoka kwa Mtume SAW na kwa masahaba zake:

a) Vibomba vya pumu na kuvuta pumzi zenye nyoshi za dawa.
b) Kuumika (hijama) na kutoa damu (safd).
c) Kuchukua sampuli ya damu kwenye maabara kwa ajili ya uchunguzi, au kutoa damu kutoka kwa mchangiaji, au kuingizwa damu kutoka kwa mtu mwingine.
d) Sindano zinazotumika kutibu figo kupitia kwenye tumbo au kwenye figo bandia.
e) Sindano za dawa zinazopitia kwenye tupu ya nyuma au darubini au kidole kwa minajili ya uchunguzi wa kimatibabu.
f) Amalia za upasuaji (Operesheni) kwa kumpoteza fahamu (ganzi) mgonjwa ikiwa mgonjwa huyu alishatia nia ya kufunga na hakuna kitu cha majimaji au chakula kinachoingia ndani.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 94 (2/10)
Yanayohusiana na 'Kutegenezwa kwa Binadamu Bandia (Human Cloning)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha kumi (10) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia (KSA) 23 – 28 Mfungo Tano (Swafar), 1418, sawa na 28 Juni – 3 Julai, 1997.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Kutegenezwa kwa Binadamu Bandia (Human Cloning),** na baada ya kuzingatia tafiti, hoja na mapendekezo ya Warsha ya Fiqhi-Utabibu zilizowasilishwa kwenye kikao cha tisa (9) cha Jumuiya ya Kiislamu ya Sayansi za Tiba wakishirikiana na 'Kongamano' na Taasisi nyenginezo hapo Dar-Baydhaa (Casablanca), Morocco katika kipindi kuanzia 9 – 12 Swafar, 1418 H sawa na 14 – 17 Juni, 1997, na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya kwa kushirikiana na wanafiqihi na madaktari;

Imefikfiwa yafuatayo:

Utangulizi:

Hakika Allah SWT Amemuumba binadamu katika umbile lililokua zuri zaidi, Akamkirimu kwa sifa za hali ya juu kabisa, kama alivyosema:

"وَلَقَدۡ كَرَّمۡنَا بَنِيٓ ءَادَمَ وَحَمَلۡنَٰهُمۡ فِي ٱلۡبَرِّ وَٱلۡبَحۡرِ وَرَزَقۡنَٰهُم مِّنَ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَفَضَّلۡنَٰهُمۡ عَلَىٰ كَثِيرٖ مِّمَّنۡ خَلَقۡنَا تَفۡضِيلٗا"

"Kwa hakika tumewatukuza watu wa kizazi cha Ādam kwa akili na kuwapelekea Mitume, tukawadhalilishia wanyama barani wa kuwapanda na vyombo baharini vya kuwabeba, tukawaruzuku vilaji na vinywaji vizuri

na tukawapa daraja kubwa juu ya viumbe wengi".[1]

Amempamba na akili na kumtukuza kwa majukumu na kumjaalia awe '*Khalifa*' (mrithi na kiongozi) katika hii ardhi na kumuwezesha kuisimamia, na juu ya yote Akamkirimu kubeba *risala* (ujumbe wa Allah) yake inayowiana na umbile lake la asili (*fitra* au usafi wa asili), bali ujumbe wa Allah ni *fitra* yenyewe kama Alivyosema:

"فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا ۚ فِطْرَتَ ٱللَّهِ ٱلَّتِي فَطَرَ ٱلنَّاسَ عَلَيْهَا ۚ لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ ٱللَّهِ ۚ ذَٰلِكَ ٱلدِّينُ ٱلْقَيِّمُ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ"

"Basi simamisha uso wako, kwenye msimamo wa dini ya Uislamu ambayo Mwenyezi Mungu Ameifanya ilingane na maumbile ya watu. Hapana ugeuzaji wa uumbaji wa Mwenyezi Mungu na Dini Yake, kwani hiyo ndiyo njia iliyonyoka, lakini wengi wa watu hawajui".[2]

Uislamu umekua na pupa katika kulinda umbile lake la asili (*fitra*) la binadamu liedelee kubaki safi kupitia malengo makuu matano ya Uislamu yenye kusudio la kumlinda, kumuhifadhi na kumsafisha binadamu; nayo ni: Kumlindia dini yake, nafsi (roho) yake, akili yake, kizazi chake na mali yake, na kuyahifadhi mambo hayo dhidi ya kila kila kitu hatarishi chenye kuyaharibu, ima kwa kusababisha maharibiko au matokeo yake, haya yote yanathibitishwa zaidi kwa ushahidi wa Hadith Qudsi aliyoipokea imam Qurtubi kwa riwaya ya al-Qadhi Ismail:

"إني خلقت عبادي حنفاء كلهم، وإن الشياطين أتتهم فاجتالتهم عن دينهم... إلى قولـه: وأمرتهم أن يغيروا خلقي"

"Hakika Mimi (Allah) nimewaumba waja wangu wakiwa wasafi wote, lakini shetani (iblisi) wakawajia na kuwapotosha na dini yao" …. Mpaka pale aliposema: *"wakawaamrisha wageuze umbile langu niliowaumbia".*[3]

Na kwa hakika Allah alimfundisha binadamu alichokua hakijui, na akamuamrisha kuendelea kutafiti na kutafakari na kuzingatia maumbile ya

[1] Surat al-Israa: 70.
[2] Surat al-Rum: 30.
[3] Tafsir ya Imam al-Qurtubi: 5: 389.

allah kwenye aya nyingi za Qur'an; zikiwemo: "*Je, Hamuoni?*",[1] "*Je, Hatizami binadamu?*",[2] "*Hakika ya hayo ni ukumbusho kwa wenye akili*",[3] "*Basi na atizame binadamu ameumbwa na kitu gani? Ameumbwa na tone la manii yenye kutoka kwa kasi*",[4] "*Hakika hizi ni alama kwa wenye kufahamu*"[5] na aya nyenginezo nyingi.

Uislamu hauweki pingamizi au kizuizi juu ya uhuru wa kufanya utafiti wa kielimu (Scientific research) kwani kufanya hivyo ni mojawapo wa njia za kumtambua Allah na maumbile yake kwa viumbe wake, lakini sambamba na hilo Uislamu hautaki kuacha milango hii ya utafiti bila ya vidhibiti na bila ya kupitisha matokeo ya utafiti kwenye kipimo cha sharia ili kupitia kipimo hiki kiweze kupambanua cha halali na cha haramu, hivyo haifai kufanya jambo lolote eti kwa kua jambo hilo linafanyika, lakini lazma litizamwe jambo hilo linaleta manufaa (faida) gani kwa jamii au linaondosha madhara gani, utafiti wa kielimu lazima mwishowe uwe unalenga heshima ya binadamu na kumtukuza na kumuelekeza kwenye lengo lake la asili la kuumbwa na kuletwa hapa duniani, na hafai binadamu kufanywa ndio sehemu ya majaribio ya kisayansi au kuharibu asili ya umbile lake na utu wake au tafiti zinazopelekea mporomoko wa jamii au kubomoa misingi ya mahusiano ya kifamilia na udugu inayojulikana katika historia ya binadamu na chini ya kivuli cha Sharia ya Allah na hukmu Zake.

Katika mapya yaliyozuka ya kinachodaiwa ni Sayansi ya zama hizi; ni kile kinachopazwa sauti na vyombo vya habari ulimwenguni kinachoitwa: 'Utengenezaji wa Kiumbe Bandia'. Kwa hivyo imelazimu kubainisha nini hukmu ya sharia juu ya jambo hili, na hii ni baada ya kuwasilisha taarifa hizi mbele ya jopo la wataalamu na wanasayansi waislamu katika uwanja huu.

Maana ya Uumbaji (*cloning*) bandia:

Inavyojulikana katika taratibu (Sunnah) za Allah za uumbaji ni kwamba

[1] Surat Ta-Ha: 89.
[2] Surat Yaasin: 77.
[3] Surat al-Zumar: 21.
[4] Surat al-Tariq: 4-5.
[5] Surat.

kiumbe cha kibinadamu kinapatikana kwa utaratibu wa matone (manii) aina mbili (kutoka kwa baba na mama), kila kiii cha tone hilo kinabeba idadi kadhaa ya vijinasabu (chromosomes) ambazo kwa idadi vinakua ni nusu ya vijinasabu vinavyopatikana kwenye seli (cell) za binadamu. Linapokutana tone la baba (mume) linaloitwa: kidudu-manii kukutana na tone la mama (mke) linaloitwa: yai, basi matone hayo hugeuka kwa pamoja na kutengeneza tone-kijusi linalobeba mfuko wa kuanza kuchora ramani kamili ya kizazi kipya, mfuko huu una uwezo wa kukithirisha kizazi. Mfuko huu unapoingia kwenye ufuko wa uzazi wa mama unaanza kukua na kukamilika mpaka unakua tayari kuzaa kiumbe kingine kwa idhini ya Allah.

Wakati mfuko huo ukiwa kwenye safari yake; unaongezeka maradufu na kugeuka kua seli (cell) mbili zinazofanana kisha zinakua nne na baadae nane; bado zinaendelea kuongezeka maradufu mpaka zinafika awamu ambapo zinaanza kujitandua na kujitambulilsha. Inapochanika mojawapo ya seli kwenye awamu ya kabla kujitambulisha na kujigawa vipande viwili vinavyofanana basi patazaliwa watoto pacha wawili wanaofanana. Paliwahi kufanyika utenganisho wa kimaabara kwa wanyama kwenye awamu hii pakazilwa mapacha wanaofanana, lakini jambo kama hili halijawahi kufanyika kwa binadamu, jambo hili linachukuliwa kua ni aina ya ‘uumbaji bandia’ au uzalishaji wa kiumbe kwa kua inatoa (kuzalisha) kiumbe (kopi) kinachofanana na kiumbe asili, mbinu hii ya uzalishaji inajulikana kama: ‘uumbaji bandia’ kwa kugawa.

Pia iko mbinu nyengine ya kutengeneza kopi ya kiumbe kamili, mbinu hii inachukua ule ‘mfuko wa ramani kamili’ ya kiumbe (Asidi-nasaba, *DNA*), mfuko huu unachukuliwa kutokana na kiini cha seli miongoni mwa seli za mwili na baadae kuuweka kwenye seli ya yai lililotolewa kiini, kwa utaratibu huu panatengezeka tone-kijusi kilichobeba mfumo kamili wa ‘mfuko wa ramani’, mfuko huu una uwezo wa kukithirisha kizazi. Mfuko huu unapachikwa kwenye ufuko wa uzazi wa mama unaanza kukua na kukamilika mpaka unakua tayari kuzaa kiumbe kingine kwa idhini ya Allah. Mbinu hii ya utoaji kopi (kiumbe bandia) inajulikana kama uhamisho wa vijinasabu (Asidi-nasaba, *DNA*) au ‘kupachika vijinasabu mbadala kwenye seli ya yai’ na hii ndio taswira ya ibara ‘Uumbaji bandia’ inavyofahamika

pale ilipotumika kwa yule mnyama kondoo (*Dolly*), hapa ijulikane kua kiumbe huyu hakuwa kopi ya asili, kwani yai la mama lililotolewa kiini chake bado linaendelea kua na masalio ya vijinasabu katika ule ute wake uliokua umeshikana na kiini kilichotolewa. Masalio haya bila shaka yanakua na athari ya wazi katika kuhamisha sifa za kizazi kipya kilichotolewa kwenye seli za mwili. Jambo kama hili bado halijawahi kufanyika kwa binadamu.

Kwa hio, utoaji wa kopi ya kiumbe (cloning) ni kuzalisha kiumbe hai mmoja au wengi kutokana na ima kuhamisha kiini cha seli ya mwili kwenda kwenye yai lililotolewa kiini chake, au kuligawa yai ambalo tayari lisharutubika na kabla ya awamu ya kutandukana mishipa na viungo. Ni jambo lisilofichika kwamba operesheni kama hizi na mfano wake haziwezi kua ni uumbaji au sehemu ya uumbaji, Ameseme Allah SWT:

> *“Au wamemfanyia Mwenyezi Mungu washirika walio umba kama alivyo umba Yeye, na viumbe hivyo vikawadanganyikia? Sema: Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wa kila kitu. Na Yeye ni Mmoja Mwenye kushinda”*[1]*!* ()

Pia Akasema:

> *“Je! Mnaiona mbegu ya uzazi mnayo idondokeza? Je! Mnaiumba nyinyi, au ni Sisi ndio Waumbaji? Sisi tumekuwekeeni mauti; na wala Sisi hatushindwi Kuwaleta wengine badala yenu na kukuumbeni nyinyi kwa umbo msilolijua. Na bila ya shaka mlikwisha jua umbo la kwanza, basi kwa nini hamkumbuki?*”.[2]

Akasema tena:

> *Kwani mwanaadamu haoni ya kwamba Sisi tumemuumba yeye kutokana na tone la manii? Kisha sasa yeye ndio amekuwa ndiye mgomvi wa dhaahiri. Na akatupigia mfano, na akasahau kuumbwa kwake, akasema: Ni nani huyo atakaye ihuisha mifupa nayo imekwisha mung’unyika? Sema: Ataihuisha huyo huyo aliye iumba hapo mara ya*

[1] Surat al-Ra’ad: 16.
[2] Surat al-Waaqi’ah: 58 – 62.

mwanzo. Na Yeye ni Mjuzi wa kila kuumba. Aliye kujaalieni kupata moto kutokana na mti wa kijani nanyi mkawa kwa huo mnawasha. Kwani aliye ziumba mbingu na ardhi hawezi kuwaumba mfano wao? Kwani! Naye ndiye Muumbaji Mkuu, Mjuzi. Hakika amri yake anapo taka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa.[1]

Akaendelea Kusema:

"*Na kwa yakini tumemuumba mtu kutokana na asli ya udongo. Kisha tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti. Kisha tukaiumba tone kuwa damu iliyo ganda, na tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama. Kisha tukamfanya kiumbe mwengine. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji*".[2]

Kwa mujibu wa yaliyotangulia katika tafiti zilizowasilishwa na hoja na misingi ya kisharia iliojadiliwa kwenye 'Baraza la Kongamano';

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuharamisha utoaji kopi wa binadamu (human cloning) kwa njia mbili zilizotajwa au njia nyengine yoyote ile ambayo itapelekea kuzalikana na kukithiri kwa binadamu.

Mbili: Itokeapo ukiukwaji wa hukmu ya sharia iliobainishwa kwenye ibara (moja) hapo juu basi athari zozote zitakazojitokeza lazima lazima ziwasilishwe ili kubaini hukmu zake za kisharia.

Tatu: Kuharamisha mazingira yote ambapo mtu wa kando ataingizwa baina ya mume na mke ima kwa kutumia mfuko wake wa uzazi, au yai, au kidudu-manii, au seli ya mwili kwa lengo la utoaji kopi ya kiumbe.

Nne: Hakuna katazo la kisharia kufaidi na teknologia ya 'Utoaji kopi' na 'Handasa ya Urathi' (Genetic Engineering) katika fani za baiolojia, vijidudu-hai, mimea na wanyama, yote hayo yafanyike ndani ya mipaka na vidhibiti

[1] Surat Yaasin: 77 – 82.
[2] Surat al-Mu'minun: 12 – 14

vya sharia kwa namna ambayo italeta maslahi na kuepusha madhara.

Tano: Kuzitaka nchi za Kiislamu kutunga kanuni na sheria zifaazo ili kuziba mianya ya moja kwa moja au ya kupitia kwa nyuma dhidi ya taasisi za kiutafiti za ndani au za kigeni na wanasayansi wa kigeni kuzitumia nchi za Kiislamu kama mawanda ya majaribio ya 'Utoaji kopi binadamu' na kuyashajiisha.

Sita: Ufuatiliaji wa pamoja baina ya 'Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu' na 'Jumuiya ya Kiislamu ya Sayansi-Tiba' juu ya maudhui haya ya 'Utoaji kopi binadamu' na mapya yanayoibuka kisayansi, na kudhibiti istilahi (misamiati) zake, na kuandaa warsha na vikao maalum ili kubaini hukmu za sharia zinazofungamana nayo.

Saba: Kutoa wito kwa uanzishwaji wa 'Kamati Maalum' za wanataaluma, wanasayansi na wanazuoni wa sharia ili ziweke 'Vidhibiti vya Kimaadili' katika tafiti za kisayansi kwenye nyanja za baiolojia ili ziwe ni miongozo kwa nchi za Kiislamu.

Nane: Kutoa wito kwa uanzishwaji na kusaidia 'taasisi za kielimu' zitakazojihusisha na tafiti za kisayansi kwenye nyanja za baiolojia na 'Handasa ya Urathi' lakini kwenye maeneo yasiokua ya 'Utoaji kopi binadamu' kwa mujibu wa vidhibiti vya kisharia, ili ulimwengu wa Kiislamu usibaki nyuma na kua tegemezi kwa wengine kwenye nyanja hizi.

Tisa: Kuandaa misingi imara ya kuamiliana na mapya yanayoibuka kisayansi kwa mtazamo wa Kiislamu, na kuzitaka vyombo vya habari kujikita kwenye mwamba wa imani wanapoamiliana na kadhia hizi, na kujiepusha kubeba fikra potofu zinazokinzana na Uislamu, na kuelekeza maoni ya umma kua na msimamo wa kuyakinisha uvumbuzi mpya wa kisayansi kabla ya kuchukua maamuzi kwa mujibu wa maelekezo ya Allah SWT:

> "*Na linapo wafikia jambo lolote lilio khusu amani au la kitisho wao hulitangaza. Na lau kuwa wangeli lipeleka kwa Mtume na kwa wenye mamlaka kati yao, wale wanao chunguza wangeli lijua. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema yake mngeli mfuata*

Shet'ani ila wachache wenu tu".[1]

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

[1] Surat al-Nisaa: 83

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 95 (3/10)[1]
Yanayohusiana na 'Vichinjwa (Wanyama Wanaochinjwa)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha kumi (10) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia (KSA) 23 – 28 Mfungo Tano (Swafar), 1418, sawa na 28 Juni – 3 Julai, 1997.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Vichinjwa (Wanyama Wanaochinjwa),** na kusikiliza hoja zilizoibuka juu ya mas'ala haya kwa kushirikiana na Wanafiqihi, Madaktari na Wataalamu wa Lishe na kwa kuzingatia kua 'Uchinjaji' ni katika hukumu zinazosimamiwa na Sharia ya Kiislamu kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah, na kwamba kwenye kuzingatia hukmu zake ni kujikita na kuinua jina la Uislamu na sharia zake zinazomuandaa Muislamu, kama alivyosema Mtume SAW:

«من صلى صلاتنا، واستقبل قبلتنا، وأكل ذبيحتنا، فذلك المسلم الذي له ذمة الله ورسوله»

"*Mwenye kuswali swala yetu, akaelekea kibla chetu na akala vichinjwa vyetu; basi huyo ni Muislamu aliepewa dhimma ya Allah na Mtume wake*".[2]

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Uchinjaji wa kisharia (halali) unafanyika kwa mojawapo ya njia zifuatazo:

1) Kuchinja (*al-Dhabh*): nayo inatimiya kwa kukata koo na mizizi (mishipa) yake, na hii ndio njia ilio bora zaidi kisharia katika kuchinja ng'ombe, mbuzi, kuku na wengineo.
2) Kuchinja (*al-Nahr*): nayo ni kumdunga mnyama kwa kisu kwenye shingo yake sehemu iliyozama kwenye koo, njia hii bora zaidi

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 10, Mjeledi 1, Uk. 53).
[2]

kisharia katika kuchinja ngamia na mfano wake, lakini pia inafaa kwa ng'ombe.

3) Kuchinja (*al-'Aqr*): nayo ni kumjeruhi mnyama asiekamatika sehemu yoyote katika mwili wake, nisawa awe mnyama mwitu anaeruhusiwa kuinjwa au mnyama mkali na hatari katika wanyama wanaofugwa. Muinjaji akimpata mnyama akiwa bado yuko hai basi ni wajibu kumchinja au kumdunga.

Mbili: Ili uchinjaji uwe sahihi; yazingatiwe masharti yafuatayo:

1) Mchinjaji awe balegh (amebalighi), mtambuzi (akili timamu), muislamu au mtu wa kitabu (myahudi au mkiristo), vichinjwa vya wapagani, wasiokua na dini, wakanushaji uwepo wa Mwenyezi Mungu, majusi (wanaoabudu moto) na walioritadi na makafiri wengine wasiokua watu wa kitabu (ahlul-kitab) haviliwi.
2) Kisu kinachotumika kuchinjia lazima kiwe kikali sana, nisawa kisu hicho kiwe kimetengenezwa kwa chuma au kity kingine alimradi kinakata vizuri na kutoa damu, kucha na jino haviruhusiwi.
   Si ruhusa (halali) kula mnyama aliejinyonga au alienyongwa (*al-Mun'khaniqa*), aidha si ruhusa (halali) kula mnyama aliegongwa kwa mawe au mfano wake hadi kufa (*al-Mauqudha*), pia si ruhusa kula (al-*Mutaraddiya*) mnyama aliekufa kwa kuanguka kutoka juu au kuanguka ndani ya shimo, kadhalika haifai kula (*al-Nateeha*) mnyama aliekufa kwa sababu ya kupigwa pembe na mnyama mwenzake, na kula mnyama aliewinjwa na mnyama mwitu asiefundwa, lakini akimuwahi bado hajafa akamchinja basi inajuzu kumla.
3) Mchinjaji anatakiwa kusoma '*Bismillah*' jina la Allah wakati wa kuchinja. Haitoshi kutumia sauti iliyorekodiwa kama redio au tepu wakati wa kupiga '*Bismillah*', iwapo mchinjaji amesahau kuleta '*Bismillah*' inafaa kumla mnyama huyo.

Tatu: Kuzingatia maadili ya uchinjaji yaliyowekwa na sharia ya Kiislamu kama vile kua na huruma na upole kwa mnyama kabla ya kumchinja wakati wa kumchinja na baada ya kumchinja. Hivyo basi kisu kisitiwe makali mbele ya mnyama anaekusudiwa kuchinjwa, au kuchinjwa mnyama mbele ya mwenzake, asichinjwe kwa kisu ambacho si kikali, au kumuadhibu

(kumtesa) mnyama, au kumkata sehemu ya mwili wake, au kumchuna, au kumzamisha kwenye maji moto au kumsumua mabele yake ila baada ya kuhakikisha mnyama huyu amechinjika vizuri na roho yake imeshatoka (amekufa).

Nne: Mnyama anaekusudiwa kuchinjwa anatakiwa awe na afya nzuri asiwe na magonjwa ya kuambukiza au kuifanya nyama hio iwe ni yenye madhara kwa walaji wake, jambo hili linatakiwa kusisitizwa zaidi kwa nyama zinazoletwa sokoni au zile zinazoagizwa kutoka nchi za nje.

Tano:

1) Kimsingi, uchinjaji wa kisharia unatakiwa ufanyike bila ya kumtia mnyama kisunzi (kizunguzungu), kwa hakika utaratibu wa uchinjaji wa Kiislamu kwa kuzingatia masharti yake na maadili yake ni bora zaidi na wenye huruma zaidi kwa mnyama na kumpunguzia maumivu (machungu) ya kuchinjwa. Taasisi husika katika uchinjaji (vichinjio) zinatakiwa kuboresha ala (zana) za uchinjaji hususan kwa wanyama wakubwa ili malengo yanayokusudiwa yafikiwe vizuri zaidi.
2) Pamoja na kuzingatia yaliyobainishwa kwenye ibara (a) hapo juu; wanyama wanaochinjwa - baada kutiwa kusunzi – kichinjo cha kisharia wanafaa kuliwa yanapotimizwa masharti yafuatayo ambayo ni kuhakikisha mnyama alietiwa kisunzi hakufa kabla hajachinjwa; wataalamu wameeka vigezo vya kuzingatiwa nazo:
    a) Awekewe mabapa mawili ya ya umeme upande wa kichwa cha mnyama kuelekea kisogoni mwake.
    b) Nguvu za umeme (voltage) zinazotumika ziwe kati ya volts 100 hadi 400.
    c) Ukali wa umeme (current) uwe kati ya ampere 0.75 hadi 1.0 kwa mbuzi, na kati ya ampere 2 hadi 2.5 kwa ng’ombe.
    d) Muda wa kupitisha miale (mishtuo) ya umeme uwe kati ya sekunde 3 hadi 6.
    e) Haijuzu kumtia mnyama kisunzi kwa kutumia bastola yenye sindano ya kugonga au nyundo au kupuliza kwa njia ya kizungu.
    f) Haijuzu kuwatia kuku visunzi kwa mshtuo wa umeme (electric shock), uzoefu unaonyesha kwamba kufanya hivyo kunapelekea

idadi kubwa kufa kabla ya kuchinjwa.

g) Haijaharamishwa kula mnyama aliechinjwa baada ya kutiwa kisunzi kwa kutumia mchanganyiko wa oksidi ya karboni na hewa au oksijini, au kwa kutumia bastola yenye kichwa mviringo lakini bila ya kumuua mnyama kabla kuchinjwa.

Sita: Waislamu wanaoishi katika nchi zisizokua za Kiislamu wanatakiwa kutafuta kwa njia za kisheria wapewe vibali vya kuchinja kwa njia ya Kiislamu bila kutia wanyama visunzi.

Saba: Inajuzu kwa waislamu wanaotembelea nchi zisizokua za Kiislamu au wanaoishi humo, kula vichinjwa vya ahlul-kitab vile ambavyo ni halali kwa asili, lakini baada ya kuhakikisha kua havikuchanganyika na vitu vilivyoharamishwa, ama ikiwabainikia kua vichinjwa hivyo havikuchinjwa kisharia basi itakua haramu kula.

Nane: Kimsingi, uchinjaji wa kuku na wanyama wengine unatakiwa ufanyike kwa mkono wa mchinjaji, lakini hamna tatizo kutumia mashine za kuchinjia kuku iwapo masharti ya uchinjaji wa kisharia yaliyotajwa kwenye ibara (Mbili) iliyotangulia yamezingatiwa, aidha inajuzu kupiga '*Bismillah*' kwa kundi la kuku linalopita kichijioni, likiingizwa kundi lingine basi atapiga '*Bismillah*' nyingine.

Tisa:

a) Iwapo uagizaji (uingizaji) wa nyama kutoka nchi ambazo raia wake wengi ni *ahlul-kitab* na waachinja wanyama wao katika vichinjio za kisasa lakini wanazingatia masharti ya uchinjaji wa kisharia yaliyotajwa kwenye ibara (Mbili) iliyotangulia, basi nyama hizo zinakua ni halali; kwa mujibu wa Qur'an:

"*Leo mmehalalishiwa kila vilivyo vizuri. Na chakula cha walio pewa Kitabu ni halali kwenu, na chakula chenu ni halali kwao. Na pia wanawake wema miongoni mwa Waumini, na wanawake wema miongoni mwa walio pewa Kitabu kabla yenu, mtakapo wapa mahari yao, mkafunga nao ndoa, bila ya kufanya uhasharati wala kuwaweka kinyumba. Na anaye kataa kuamini bila shaka a'mali yake imepotea, naye katika Akhera atakuwa miongoni mwa wenye*

khasara".[1]

b) Nyama zinazoagizwa (ingizwa) kutoka nchi ambazo raia wake wengi si *ahlul-kitab* basi nyama hizo zinakua ni haramu, kwa kuhofia kua wanyama hao walitolewa roho za na watu wasiofaa kuchinja kisharia.
c) Nyama zinazoagizwa (ingizwa) kutoka nchi zilizotajwa kwenye ibara (b) juu, iwapo zilisimamiwa uchinjaji wake na taasisi ya Kiislamu inayokubalika na akawa mchinjaji wake ni muislamu au *ahlul-kitab* basi nyama hizo ni halali.

'Kongamano' linapendekeza yafuatayo:

Moja: Serikali za Kiislamu ziwasiliane na serikali zisizokua za kiislamu ambapo kuna waislamu waaoishi humo au wakazi ziwape fursa za kuchinja kwa njia ya Kiislamu bila kutia wanyama visunzi.

Mbili: Ili kujinasua na matatizo yanayotokana na uagizaji wa nyama kutoka nchi zisizokua za kiislamu, ni lazma yazingatiwe yafuatayo:

a) Kuweka mipango maalum ya kukuza rasilimali-wanyama katika nchi za kiislamu hadi kufikia kiwango cha kujitosheleza.
b) Kujaribu iwezekaavyo kuagiza nyama kutoka nchi za kiislamu.
c) Kuagiza wanyama wakiwa hai na kuwachinja ndani ya nchi za kiislamu ili kuhakikisha kwamba masharti ya uchinjaji wa kisharia yanazingatiwa.
d) Kuitaka Jumuiya ya Nchi za Kiislamu (OIC) kuunda chombo maalum cha kiislamu kazi yake ni kusimamia nyama zote zinazoingizwa kwenye nchi za kiislamu, chombo hiki kitasimamia mas'ala yote ya uchinjaji wa kisharia pamoja na kuweka taratibu zote na kanuni za uendeshaji shughuli zake, wafanye hivyo kwa kuwashirikisha wataalamu wa sharia na fani za utendaji, pia waweke katika zile nyama zilizokidhi vigezo vya kisharia nembo maalum ikiwa ni 'Alama ya Kimataifa (International Trade Mark) ya Biashara yenye usajili wa kimataifa na inayolindwa kikanuni.
e) Kuzitaka nchi za kiislamu kukitambua chombo hiki kilichotajwa kwenye ibara (d) pamoja na kuitambua nembo yake na kukipatia

[1] Surat al-Maaida: 5.

mashirikiano katika kutekeleza majukumu yake.

f) Mpaka pale agizo la (d) litakapofanyiwa kazi; wauzaji wa nyama wote na waingizaji watatakiwa kuhakikisha kua masharti ya uchinjaji wa kisharia yanazingatiwa hususan kwa zile nyama zinzoingizwa nchi za kiislamu, ili wasiwaingize waislamu kwenye kula haramu kwa kuzembea kwenye uagizaji bila kuhakikisha uhalali wa uchinjaji wake.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 96 (4/10)[1]
Yanayohusiana na 'Kadi za Mikopo (*Credit Cards*)'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha kumi (10) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia (KSA) 23 – 28 Mfungo Tano (Swafar), 1418, sawa na 28 Juni – 3 Julai, 1997.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Kadi za Mikopo (*Credit Cards*)**, na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya kutoka kwa wanazuoni na wanauchumi;

Imeamuliwa yafuatayo:

a) Kuikalifisha 'Sekreterieti Kuu' kufanya uchunguzi-yakinifu na wa kivitendo wa aina zote, masharti na makubaliano yanayofungamana na 'kadi za mikopo' zinazotolewa na benki.
b) Kuunda kamati maalum kupitia uhalisia wa kadi na kuainisha matumizi yak e na tofauti zake pamoja na kuziwekea vidhibiti vya kisharia, hii ni baada kujua aina za kadi zinazotolewa na nchi za kiarabu na za kigeni.
c) Kuandaa jopo la utafiti kujadili maudhui haya kwa mujibu wa maandalizi yaliyotangulia na kutayarisha matokeo yaliyokamilika ili yawasilishwe kwenye kikao kijacho.

Na inapendekeza yafuatayo:

a) Umuhimu wa kubuni misamiati ya kiuchumi inayohusiana na upeo wa kisharia inayohusiana na miamala inayojuzu na ile iliyoharamishwa kulingana na hali halisi ya mambo. Inapendekezwa kutumia misamiati ambayo tayari inapatikana kabla ya kubuni mingine ili iweze kubeba maana na matumizi halisi ya hukmu za sharia na kuziowanisha na

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 8, Mjeledi 2, Uk. 571, Na Toleo 10, Mjeledi 2, Uk. 467).

misamiati ya kiuchumi inayotokana na turathi za umma wa kiislamu.

b) Kuvitaka vyombo husika katika nchi za kiislamu kuzuwia benki zisitowe ‘kadi za mikopo’ za riba, ili kuwalinda waislamu wasiangukie kwenye tope la riba ilioharamishwa, na pia kulinda uchumi na mali ya raia.
c) Kuunda chombo cha sharia, fedha na uchumi chenye jukumu la kulinda raia na kutetea haki zao dhidi ya ulafi wa mabenki kwa mujibu wa mipaka ya kisharia, na kuweka nidhamu ya fedha itakayolinda uchumi wa kitaifa pamoja na kuweka kanuni za kuilinda jamii na raia dhidi ya ulafi wa mabenki ili kujiepusha na athari mbaya zitakazojitokeza.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 97 (5/10)[1]
Yanayohusiana na 'Nafasi ya Mwanamke wa Kiislamu katika Maendeleo'

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh lililoibuka kutoka Taasisi ya Nchi za Kiislamu, katika kikao chake cha kumi (10) kilichofanyika mji wa Jeddah, Falme ya Saudi Arabia (KSA) 23 – 28 Mfungo Tano (Swafar), 1418, sawa na 28 Juni – 3 Julai, 1997.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Nafasi ya Mwanamke wa Kiislamu katika Maendeleo**, na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuitaka 'Sekreterieti Kuu' kuunda 'Kamati Maalum' itakayopitia mapendekezo yaliyoandaliwa kuhusu Nafasi ya Mwanamke wa Kiislamu katika Maendeleo, matokeo yatakayopatikana yawasilishwe katika kikao kijacho, *Inshaallah*.

Wabillah al-Taufiq

≃≃≃

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 10, Mjeledi 3, Uk. 435).

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Kumi na Moja (11) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Manama, Falme ya Bahrain

25 – 30 Rajab, 1419

14 - 19 Novemba, 1998

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 98 (1/11)[1]

Yanayohusiana na 'Umoja wa Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na moja (11) kilichofanyika mji wa Manamah, Falme ya Bahrain 25 – 30 Rajab, 1419, sawa na 14 - 19 Novemba, 1998.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Umoja wa Kiislamu,** na kutokana na hoja zilizoelekeza kua maudhui haya ni mojawapo ya maudhui muhimu sana ambapo Umma wa Kiislamu unahitajia utafiti wake ufanyike katika pande mbili; kinadharia na kivitendo; na kwamba kazi na juhudi za kuunganisha umma kifikra, kikanuni na kisiasa na kuurudisha umma kwenye *tauhidi* (imani sahihi) halisi ni katika malengo adhimu ya 'Kongamano la Kimataifa';

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Umoja wa Kiislamu ni jambo la faradhi aloliamrisha Allah SWT na kuufanya umoja huu kua ni sehemu ya umma, pale aliposema:

> "*Na shikamaneni kwa Kamba ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja, wala msifarikiane*".[2]

Akasema tena: "*Kwa hakika huu umma wenu ni umma mmoja*".[3] Nae Mtume SAW akasisitiza juu ya suala hili la umoja kwa maneno na vitendo, akasema:

(المسلمون تتكافؤ دماؤهم وهم يد على من سواهم ويسعى بذمتهم أدناهم)

> "*Damu za waislamu zinalingana (ziko sawa), na wao kwa pamoja ni umma ulioshikamana kitu kimoja, na anaeonekana ni mtu wa chini anapewa heshima*

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 11, Mjeledi 3, Uk. 5).
[2] Aal-Imran: 103.
[3] al-Anbiyaa: 92.

kama wengine".[1]

Aidha, Mtume SAW alithibitisha umoja wa umma huu kivitendo; pale alipojenga udugu baina *Muhajiriin* na *Answar* na akukitisha umoja huu kwenye katiba ya kwanza kabisa ya kusimamisha dola ya kiislamu ya Madina al-Munawwara kwa ibara inayosema: "*Umma mmoja tofauti na watu wengine*".

Kwa hakika nususi (maandiko matakatifu) kama hizi kutoka kwenye Qur'an tukufu na Ahadith za Mtume SAW na mfano wake zinaelekeza waumini wawe chini ya bendera ya uislamu, wameshikamana na Kitabu (Qur'an) na Sunnah, na waachane kabisa na chuki za kihistoria na migogoro ya kikabil na tamaa binafsi na bendera za ubaguzi. Wakati waislamu walipoyasimamia hayo dola yao ilipata nguvu tangu wakati wa Mtume SAW hadi wakati wa *makhalifa* wake, na dini ya uislamu na dola yake ikaenea pembe za dunia; mashariki na magharibi, utamaduni wa kiislamu ukawa unaongoza utamaduni wa binadamu duniani, utamaduni wa kiislamu ulikua ni utamaduni mkubwa sana uliojikita kwenye misingi ya kumuabudia Allah, kwa hili, maadili ya uadilifu, uhuru na usawa yakapatikana duniani.

Mbili: Umoja wa Kiislamu umejikita kwenye kumuabudu Allah kwa itikadi na kwa maneno na kwa vitendo, kwa kufuata uongofu wa Kitabu cha Allah na Sunnah za bwana Mtume Muhammad SAW, pamoja na kuihifadhi dini hii ambayo ndio inayowaunganisha waislamu katika misimamo ya pamoja kwenye nyanja nyingi za maisha; zikiwemo nyanja za kifikra, za kiuchumi, za kijamii na za kisiasa.

Lakini pale umma huu wa kiislamu ulipojimegua na misingi ya umoja; sababu kadha za migawanyiko zikaibuka, na zama za ukoloni zilipofika na nembo yao ya: "*Wagawe Uwatawale*", basi umma ukakatika vipande vipande vilivyokuja kuunanishwa kwa misingi ya kikabila na kutenganisha waarabu na waislamu, na ikawa juhudi kubwa za wakoloni zinaelekezwa kuzidisha mpasuko na kupalilia migawanyiko kwa njia mbalimbali walizozitumia.

Tatu: Tofauti (ikhtilafu) za kifiqihi zilizopo ambazo zinatokana na jitihada za

[1]

wanazuoni katika kuzifahamu *nususi* (maandiko matakatifu) na viashiria vyake, ni jambo la kawaida, na jambo hili kwa hakika limeongeza ukwasi wa kisharia katika kyaendea yale malengo makuu ya sharia na tahsisi zake katika kuwepesisha na kuondoa uzito.

Nne: Ulazima wa kulinda hesima ya Maswahaba wote RA, na kuwataka wanazuoni kuendelea kuangazia nafasi zao na fadhila zao katika kutufukishia sisi ujumbe huu wa uislamu kwa uaminifu kizazi hadi kizazi, na kukumbusha haki yao juu ya umma, aidha kuzitaka serikali za kiislamu kutunga sharia maalum za kukekemea na kuadhibu kila anaewatweza (dhalilisha) maswahaba kwa namna yoyote ile, kufanya hivyo ndio kuchunga na kulinda heshima zao na kuondosha mojawapo ya sababu farikishi.

Tano: Ulazima wa kushikamana na kitabu (Qur'an) na Sunnah na uongofu wa wema waliotangulia miongoni mwao maswahaba wa Mtume SAW; radhi za Allah ziwefikie wote, na wale waliowafuata kwa wema, aidha ulazima wa kujiepusha na njia potofu na kila kinacholeta furka na fitna miongoni mwa waislamu, na kuzielekeza juhudi kwenye ulinganizi (*da'wah*) wa Uislamu na kueneza maafundisho yake mema kwa wasiokua waislamu.

Mapendekezo:

Ni jambo lisilofichika kua zama hizi thizi ni zama za mikusanyiko (mijumuiko) ya kimakundi yenye idiolojia zake za kifikra, kijamii, na kiuchumi na yenye kubeba nembo za utandawazi (globalization) na usekula (kutokua na dini) na usasa (kukata asili za imani) na ufungukaji wa vyombo vya habari parwanja bila ya pingamizi au vidhibiti, jambo hili limeufanya 'Ulimwengu wa Kiislamu' kua mlengwa wa msingi katika hujma za kuharibiwa tamaduni zake na maadili yake ya kiroho na kifikra, na imekua vigumu kuulinda 'Umma wa Kiislamu' dhidi ya uvamizi hatarishi huu ila kwa kuungana na kuondoa sababu farikishi zilizopo ndani yetu, ikizingatiwa kua Umma wetu wa Kiislamu unamiliki rasilimali adhimu za kusimamisha na kulinda umoja wetu; zikiwemo umoja wa kiitikadi, umoja wa kijamii, umoja wa kiuchumi, umoja kikanuni na umoja wa kiutamaduni.

Hivyo basi inapendekezwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya ‘Maamuzi ya Kongamano’ namba 48 (10/5) Yanayohusiana na ‘Utekelezaji wa Hukumu za Sharia ya Kiislamu’ pamoja na mapendekezo yaliyuibuka chini ya maudhui haya, aidha kuweka msisitizo juu ya ya ‘Maamuzi ya Kongamano’ namba 69 (7/7) Yanayohusiana na ‘Uvamizi wa Kifikra’ katika pendekezo la kwanza.

Mbili: Kuweka msisitizo kwa serikali za kiislamu juu ya suala la kuunga mkono juhudi zinazofanywa na ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu (OIC) na ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh’ kwa vyombo hivi viwili ni wawakilishi wa umoja wa waislamu duniani kisiasa na kifikra.

Tatu: Kutupilia mbali migogoro ya kihistoria, kwani kuendelea kuin’ga’ngania inazidi kupalilia mizizi ya chuki na kufarikiana katika umma.

Nne: Ulazima wa kua na dhana njema na kuaminiana kati ya waislamu dola kwa dola na raia kwa raia, na kuzielekeza vyombo vya habari kukuza mshikamano na kueneza maadili ya upendo na udugu na kukubali mawazo tofauti bila chuki.

Tano: Kufaidi na kadhia za msingi zilizopo ambazo ni sababu ya kuunganisha umma kama vile: Kadhia ya *al-Quds* (*Baitul-Maqdis*) na *Masjid al-Aqsa*; kibla cha kwanza cha Mtume SAW na sehemu aliokwenda kwenye safari yake ya *israa* na kuanzia safari yake ya *mi’raj* hapo, ili kuuepusha mji huu wa *Quds* na hatari zinazoukabili za kuyahudishwa (*kufuta athari zake za Kiislamu na kuufanya uwe mji wa kiyahudi*), na kuweka msisitizo kua kadhia hii ndio kadhia ya msingi ya waislamu wote kote duniani.

Aidha washiriki wa ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ wanazitaka serikali za Kiislamu kuongeza juhudi zao maradufu katika kuishughulikia kadhia hii na mfano wake; na kuharakisha kuchukua hatua zifaazo, zikiwemo:

a) Kukemea dhulma zinazofanyiwa Wapalestina za kunyan’ganywa ardhi zao au kuhamishwa na kupewa ardhi hizo Mayahudi (walowezi wa kizayuni), kiasi ya kwa Wapalestina wananyimwa ardhi zao na kudhulumiwa na kuteswa na kudhalilishwa na kuuawa na kunyan’ganywa haki zao za binadamu za msingi.

b) Kuunga mkono haki za Wapalestina zote juu ya ardhi yao tukufu; hii ikiwa ni pamoja na kuwasaidia katika harakati zao na mapambano yao ya ukombozi dhidi ya wavamizi wa kizayuni.
c) Kuzikemea harakati za kizayuni na uvamizi wa maisraeli kwa yale wanayoyafanya ya kila aina ya ukatili mateso na madhila na uadui wa kinyama dhidi ya watu wa Palestina wanaopigania haki yao ya ukombozi na kizikomboa sehemu zao takatifu.

Sita: Kujihusisha na mapendekezo yaliyotolewa ambayo yanaharakisha kuleta suala la umoja katika kipindi hichi; kama vile:

a) Kuandaa mitaala ya elimu kwa misingi ya Kiislamu.
b) Kuweka mpango-mkakati wa Kiislamu wa pamoja juu ya suala la vyombo vya habari (media).
c) Uanzishwaji wa 'Soko la Pamoja la Kiislamu'.
d) Uanzishwaji wa 'Mahkama ya Haki ya Kiislamu'.

Saba: Kuitaka 'Sekreterieti Kuu' ya 'Kongamano la Fiqhi ya Kiislamu' kuunda 'Kamati Maalum' yenye wajumbe na wataalamu wa 'Kongamano' ili waandae 'Mpango-vitendo' unaoweza kutekelezeka na utakaozingatia hali halisi ya umma wa kislamu wa zama hizi, mpango huo usheheni nyanja za kiutamaduni, kijamii na kiuchumi, aidha mpango huo uweke hatua-tekelezi za kufikia lengo la 'umoja' katika nyanja hizo zilizotajwa pamoja na kufaidi na juhudi zilizopo kwa sasa ndani ya mipangilio ya taasisi rasmi za kiarabu na za kiislamu, na kufaidika na taaluma za wajuzi mbalimbali katika nyanja hizi. Ili kuhakikisha kwamba 'Kamati hii Maalum' inaanza kazi zake na kutekeleza mipango iliyokusudiwa; tunapendekeza kuanzia sasa kwamba 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu (OIC) iamuru uundwaji wa 'Kamati' hii.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 99 (2/11)[1]

Yanayohusiana na 'Usekula (Kuitenga Dini)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na moja (11) kilichofanyika mji wa Manamah, Falme ya Bahrain 25 – 30 Rajab, 1419, sawa na 14 - 19 Novemba, 1998.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Usekula (Kuitenga Dini),** na kwa mujibu wa mijadala ya hoja ambayo imeashiria juu ya hatari ya Usekula kwa Umma wa Kiislamu;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Usekula, ambao uhalisia wake ni kutenganisha dini na maisha, uliibuka kule Ulaya kama kitendo cha kukataa dhulma zilizokua zikisimamiwa na Kanisa.

Mbili: Usekula ulienezwa (sambazwa) nchi za Kiislamu kupitia Wakoloni na wasaidizi wao, na ghilba na njama, Usekula huu ulitumika kama kifaa cha kuuchana Umma wa Kiislamu, na kuitilia shaka imani (itikadi) sahihi ya Uislamu, na kuichefua historia safi ya Uislamu, na kughilibu kizazi kipya kwamba kuna mgongano baina ya 'akili' na '*nususi*' (Maandiko ya Qur'an na Sunnah) za kisharia, na wakafanya juu-chini kuiondoa Sharia ya Kiislamu na kuweka badala yake Kanuni za kutungwa na binadamu, huku wakishajiisha ufuska na miporomoko ya maadili.

Tatu: Kutokana na Usekula huu; pameibuka fikra potofu na vunjifu nyingi zilizokuja kuvamia nchi za Kiislamu chini ya misamiati mbalimbali kama vile; Ubaguzi, Ukomunisti, Uzayuni, Ufreemason na nyenginezo, fikra hizi zilipelekea kwa nchi za Kiislamu kupoteza rasilimali zake na kuporomoka

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 11, Mjeledi 3, Uk. 259).

kwa hali ya uchumi jambo ambalo lilipelekea nchi za Kiislamu kutawaliwa (koloniwa) khasa Palestina na Quds, hii ikiwa ni dhihirisho la wazi kwamba Usekula haukadhamiria kheri kwa Umma wa Kiislamu.

Nne: Usekula ni mfumo wa kibinadamu uliojengeka kwenye misingi ya ukafiri inayokinzana na Uislamu kwa kila upande, na Usekula huu unaungana –kimalengo- na Uzayuni wa Kimataifa na fikra potofu za kuporomosha maadili, kwa maana hio usekula ni mfumo hatarishi wa kikafiri usiokubalika mbele ya Allah na Mtume wake na waumini wa kweli.

Tano: Hakika ya Uislamu; ni *Dini* na *Dolan* na mfumo kamili wa maisha, na ndio mfumo unaomfaa binadamu zama zote na sehemu zozote, wala Uislamu hautambui '*kutenganisha dini na maisha'*, lakini Uislamu unalizimisha hukmu zote na sheria zote zitokane na Uislamu na kuyafanya maisha yaendane kwa mujibu wa maelekezo ya Uislamu katika nyanja zote; sawa ziwe katika siasa au uchumi au jamii au malezi na mifumo ya elimu au mawasiliano (*media*) na nyenginezo.

Hivyo basi inapendekeza yafuatayo:

a) Kuwasihi watawala wa nchi za kiislamu kusimama kidete na kulinda waislamu na nchi zao dhidi ya njama na mbinu za *Usekula,* na kuchukua tahadhari zifaazo kuwahami.
b) Wanazuoni wanatakiwa kuongeza juhudi zao kupamana na Usekula na kutahadharisha Umma dhidi yake.
c) Kuweka mipango-mikakati kamilifu ya kimalezi na kimitaala kwenye taasisi za elimu kuanzia msingi hadi vyuo vikuu, vituo vya utafiti na mitandao ya taarifa ili lugha ya kupambana na usekula iwe moja, mitaala iwe moja, mawaidha yawe mamoja, lakini pia kujihusisha zaidi na juhudi za kuamsha risala ya msikiti na kuzidisha mawaidha bainifu na kuandaa walinganizi (*Du'at*) mahiri wabobezi wanaoendana na changamoto za zama hizi na kuweza kutoa ufumbuzi wa matatizo-tatanishi na kuyalinda malengo makuu ya Sharia ilio safi

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 100 (3/11)[1]
Yanayohusiana na 'Uislamu Dhidi ya Mfumo Hatarishi wa Usasa'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na moja (11) kilichofanyika mji wa Manamah, Falme ya Bahrain 25 – 30 Rajab, 1419, sawa na 14 - 19 Novemba, 1998.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Uislamu Dhidi ya Mfumo Hatarishi wa Usasa,** na kwa mujibu wa mijadala ya hoja ambayo imeashiria juu ya hatari ya *Usasa*, na kuweka wazi ukweli juu ya '*Usasa*' kua mfumo mpya wa kifikra uliojikita kwenye kuipa akili '*sifa ya uungu*' na kukata mambo yasiyoonekana (*ghaibu*) na kukanusha *wahy* (Ufunuo alioteremshiwa Mtume SAW) na kubomoa kila jema linalojulikana katika imani na maadili na khulka.

Miongoni mwa misingi muhimu ya fikra hizi za '*Usasa*':

- Kuifanya akili kua tegemeo kuu, na kutosheka na elimu itokanayo na majaribio ya kisayansi tu bila kuzingatia 'akida (imani) ya uislamu iliyo sahihi.
- Kuitenga dini kabisa na shughuli zote za kiutamaduni, kijamii, kiuchumi, kisiasa na usaidizi wa kibinadamu, kwa maana hio '*Usasa*' ni ndugu yake '*Usekula*'.

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: 'Usasa' kwa ufahamu ulioelezewa hapo juu; ni mfumo hatarishi wa kikafiri usiokubalika mbele ya Allah na Mtume wake na waumini wa kweli kwa kuaa unakinzana na misingi ya uislamu na mafundisho yake; lichca ya kwamba wafuasi wa mfumo huu kujidhihirisha kama kwamba wao ni watetezi wa uislamu wenye ari.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 11, Mjeledi 3, Uk. 467).

Mbili: Kwenye misingi ya uislamu na sharia yake kunapatikana ya kumtosha binadamu katika zama na sehemu zozote kwa kua misingi yake ni imara iliyokita na kutulia; kiasi ya kwamba maisha yote ya binadamu yanajiakisi na misingi hii, lakini pia ndani mfumo wa kiislamu kunapatikana misingi laini inayoendana na mabadiliko na maendeleo ya binadamu na kuweza kupokea mapya bila ya haja ya misingi mipya nje ya uislamu; mapya yanayoibuka yanawekwa kwenye vipimo kabambe vya sharia, na kutolewa hukumu zake.

Hivyo basi inapendekeza yafuatayo:

a) 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC) ismamie kuunda 'Kamati Maalum' ya 'wanafikra wa kiislamu' ili waweze kupiga darubini mienendo yote ya fikra hii ya 'Usasa' naa matokeo yake na athari zake, aidha kuandaa tafiti za kielimu zenye upeo mpana kwa minajili ya kutanabahisha upotofu uliopo ili kukilinda kizazi kipya cha Umma wa Kiislamu dhidi ya athari hatarishi za *Usasa*.
b) Kuwasihi watawala wa nchi za kiislamu kusimama kidete na kulinda waislamu na nchi zao dhidi ya njama na mbinu za *Usasa*, na kuchukua tahadhari zifaazo kuwahami.

Wabillah al-Taufiq

≃≃≃

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 101 (4/11)[1]

Yanayohusiana na 'Kuuza Deni na Hati za Mikopo (*Loan Debentures*) na Mbadala wa Kisharia katika Sekta za Umma na Binafsi'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na moja (11) kilichofanyika mji wa Manamah, Falme ya Bahrain 25 – 30 Rajab, 1419, sawa na 14 - 19 Novemba, 1998.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Kuuza Deni na Hati za Mikopo na Mbadala wa Kisharia katika Sekta ya Umma na Binafsi,** na kwa mujibu wa mijadala ya hoja ambayo imeashiria juu ya umuhimu wa maudhui haya yanayopatikana katika nyanja za miamala ya fedha ya kisasa;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Haijuzu kuuza deni la baadae kwa asiedaiwa kwa malipo ya sasahivi ya jinsi ya deni hilo au isiokua jinsi hio, kufanya hivyo kunapelekea kuingia kwenye *riba*. Aidha, haijuzu kuliuza deni hilo kwa malipo ya baadae ya jinsi ya deni hilo au isiokua jinsi hio, kufanya hivyo kunapelekea kuuza deni kwa deni ambayo hio imekatazwa kisharia. Hakuna tofauti ya deni hilo liwe limetokana na mkopo au biashara ya malipo-baadae.

Mbili: Kuweka msisitizo juu ya 'Maamuzi ya Kongamano' namba 60 (11/6) yanayohusiana na ***'Hati-fungani (Bonds)'*** katika kikao chake cha sita (6) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 17 – 23 Mwezi wa Shaaban, 1410 sawa na tarehe 14 – 20 Machi, 1990, na kwenye ibara ya (Mbili) ya 'Maamuzi ya Kongamano' namba 64 ((2/7) yanayohusiana na "*Nyaraka za biashara (Cheki, hundi, hati)"* katika kikao chake cha saba (7) kilichofanyika mji wa Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 7 – 12 Mwezi wa

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 11, Mjeledi 1, Uk. 53).

Mfungo Pili (Dhul Qaada), 1412 sawa na tarehe 9 – 14 Mei, 1992.

Tatu: ‘Kongamano’ lilipitia aina nyengine za *‘Kuuza Deni’* lakini likaonelea kuakhirisha uchukuaji wa maamuzi ili kutoa nafasi zaidi za utafiti, na kuitaka ‘Sekreterieti Kuu’ kuunda ‘Kamati Maalum’ kuzipitia kwa kina aina hizi nyengine na kupendekeza ‘Mbadala wa Kisharia’ ya kuuza deni ili ziwasilishwe kwa mara ya pili kwenye kikao kijacho.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 102 (5/11)[1]

Yanayohusiana na 'Biashara za Sarafu (*Kubadilisha pesa za kigeni*)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na moja (11) kilichofanyika mji wa Manamah, Falme ya Bahrain 25 – 30 Rajab, 1419, sawa na 14 - 19 Novemba, 1998.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Biashara za Sarafu (*Kubadilisha pesa za kigeni*),** na usikivu wa hoja zilizoibuka;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya 'Maamuzi ya Kongamano' namba 21 (9/3) yanayohusiana na *Hukumu za fedha za noti na kubadilika kwa thamani ya sarafu,* na 'Maamuzi' namba 63 (1/7) yanayohusiana na '*Masoko ya Pesa, (Miamala ya sarafu)* ibara ya (Tatu): '*Miamala katika bidhaa na sarafu na faharisi (index) kwenye masoko yanayosimamia'* namba (2): '*Miamala ya sarafu'* na 'Maamuzi' namba 53 (4/6) yanayohusiana na *'Makabidhiano'*, ibara ya (Mbili, 1-c).

Mbili: Haijuzu kisharia biashara ya sarafu kwa malipo-baadae, aidha haijuzu kuahidiana kulipana baadae, katazo hili ni kwa ushahidi wa kitabu (Qur'an) na Sunnah na Ijmaa ya Umma.

Tatu: Hakika ya riba na biashara za sarafu pasipo na kuzingatia vigezo vya sharia ya kiislamu ni miongoni mwa sababu kuu zamitikiso ya uchumi duniani ambayo imeporomosha nyuchumi za nchi nyingi.

Hivyo basi inapendekeza yafuatayo:

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 11, Mjeledi 1, Uk. 431).

Ulazima wa uwepo wa usimamizi wa kisharia juu ya masoko ya fedha, na kuyalazimisha kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa maelekezo ya sharia ya kiislamu katika sarafu na biashara nyenginezo, maelekezo ya sharia ndio kinga thabiti dhidi ya majanga ya kiuchumi.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 103 (6/11)[1]

Yanayohusiana na 'Mikataba ya Utengenezaji wa Marekebisho (Ukarabati)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na moja (11) kilichofanyika mji wa Manamah, Falme ya Bahrain 25 – 30 Rajab, 1419, sawa na 14 - 19 Novemba, 1998.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Mikataba ya Utengenezaji wa Marekebisho (Ukarabati),** na baada ya usikivu wa hoja zilizoibuka;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: 'Mkataba wa Matengenezo' ni aina ya mikataba mipya ambayo hukumu za kawaida za mikataba ndizo zinazotumika, kwa maana hiyo kila 'mkataba wa utengenezaji' utawekwa kwenye kipimo cha mikataba ya kawaida, na uhalisia wake ni '*mkataba wa mabadilishano ya manufaa*' ambapo upande mmoja wa mkataba unawajibika kuchunguza na kutengeneza kinachohitaji kutengenezwa iwe ni kifaa au kitu chochote kile ima kwa kila kipindi fulani au kila dharura inapojitokeza ndani mda fulani ulioainishwa, wakati upande wa pili unawajibika malipo yaliyoainishwa, mtengenezaji anaweza kujiwajibisha kazi ya matengenezo peke yake au matengenezo na vipuri vinavyohitajika.

Mbili: 'Mikataba ya Utengenezaji' iko anwai nyingi, kati ya hio iko ambayo hukmu zake ziko wazi, nayo ni:

a) 'Mkataba wa Utengenezaji' usiounganishwa na mkataba mwengine, ambapo 'mtengenezaji' anajiwajibisha '*utendaji kazu tu*' au kazi na

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 11, Mjeledi 2, Uk. 5).

vipuri vidogo vidogo ambavyo havina uzito wowote kwa kawaida mbele ya pande zote mbili za mkataba.

Mkataba huu unachukuliwa kua ni '*mkataba wa kazi ya ujira*', mkataba huu unajuzu kisharia kwa sharti kazi yenyewe iwe inajulikana (imeainishwa) na malipo ya kazi hio kadhalika yanajulikana (yameainishwa).

b) Mkataba wa Utengenezaji' usiounganishwa na mkataba mwengine, ambapo 'mtengenezaji' anajiwajibisha '*utendaji kazu tu*' na mwenye kazi anajiwajibisha vipuri na vitendea kazi. Mkataba huu unachukuliwa kua ni '*mkataba wa kazi ya ujira*', nao unajuzu kama aina iliyotangulia.

c) 'Utengenezaji unaoshurutishwa' kwenye mkataba wa mauziano juu ya muuzaji ndani ya kipindi maalum kilichoainishwa. Mkataba huu umekusanya 'kuuza na kushurutisha' nao unajuzu kisharia; nisawa utengenezaji uwe pamoja na vifaa vya utengenezaji au bila ya vifaa.

d) 'Utengenezaji unaoshurutishwa' kwenye mkataba wa ukodishanaji (*ijara*) kwa mkodishaji na mkodishwaji. Mkataba huu umekusanya 'kukodisha na kushurutisha' na hukmu yake ni kua: ikiwa utengenezaji ni katika aina ya *ijara* ambayo manufaa yake hayakamiliki pasipo na hayo matengenezo basi inamlazimu mmiliki wa kinachokodishwa matengenezo bila ya 'sharti' na haijuzu kumshurutisha mkodishwaji kugharimika matengenezo, ama ikiwa ni matengenezo yasiokua ya msingi kwa manufaa ya kinachokodishwa basi inajuzu kumshurutisha ima mkodishaji au mkodishwaji kwaw kuainisha bayana bila kuwepo hali ya utata. Ziko pia aina nyengine ambazo 'Kongamano' limeonelea kuakhirisha uchukuaji wa maamuzi ili utafiti wa ziada ufanyike.

Tatu: Katika aina zote zilizotangulia inashurutishwa kuwepo uwazi wa bayana usiokua na utata wowote utakaopelekea mzozano (sintofahamu), aidha iwapo vipuri vitatolewa na mtengenezaji pia ni lazima ziainishwe, kuainisha malipo ya kazi ni sharti la lazima katika hali zote.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 104 (7/11)[1]
Yanayohusiana na 'Njia za Kufaidika na Fatwa Nyakati za Majanga (*Fiqh al-Nawazil*)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na moja (11) kilichofanyika mji wa Manamah, Falme ya Bahrain 25 – 30 Rajab, 1419, sawa na 14 - 19 Novemba, 1998.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Njia za Kufaidika na Fatwa Nyakati za Majanga (*Fiqh al-Nawazil*),** na baada ya usikivu wa hoja zilizoibuka;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kufaidi kutokana na turathi za fatwa za kifiqhi nyakati za majanga (*nawazil*) za aina mbalimbali ili kupata suluhisho za mambo mapya yanayoibuka zama hizi; sawa ziwe ni zile zinazohusiana na '*taratibu za fatwa*' kwa mjibu wa vigezo vya '*ijtihadi*' na utoaji wa hukmu kutoka kwenye nususi na misingi ya kifiqhi, au zile zinazohusiana na '*tanzu za fiqhi*' ambazo tayari wanazuoni washazitolea hukmu ya mambo yanayofanana katika zama zao.

Mbili: Kuhakiki (*kuhariri*) vitabu muhimu vya fatwa, na kuhuisha vitabu-andamizi vya fiqhi kama vile: '*al-Tanbihaat 'ala al-Mudawwanah*' (Taaliki juu Kazi za Fiqh) cha al-Qadhi 'Iyadh, '*al-Barnaamij*' (Mtaala) cha Sheikh 'Adhoom, '*Fatwa za Imam al-Ghazali*', '*Taqweem al-Nadhar*' (Misingi ya Uchambuzi) cha Ibn al-Dahhan, na vitabu vingine vya 'Matendo ya Watu wa Madina' katika Fiqh ya Madhehebu ya Maliki, na katika miji mashuhuri ya madhehebu hayo kama vile Fez, Al-Qayrawan na Qortuba. Aidha kuhariri kitabu cha '*al-Maarudhaat*' cha Abu al-Su'ud na vitabu vengineyo ambavyo vitakua ni njia ya kudhihirisha '*uhai wa fiqhi*'.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 11, Mjeledi 2, Uk. 281).

Tatu: Kuandaa kitabu-pambanuzi kinachobainisha ‘misingi ya fatwa’ na ‘mbinu za watoaji fatwa’ na misamiati itumikayo katika madhehebu mbalimali ya kifiqhi, na njia za upembuzi zinazojulikana katika kila madhehebu, zikiwemo fatwa zilizofanyiwa kazi na watu wa Madina ambazo ni sehemu ya madhehebu ya maliki na madhehebu mengine, aidha kusambaza kitabu cha ‘*Utangulizi kwenye Fiqh al-Nawazil*’ cha Rais wa ‘Kongamano’.

Nne: Kuingiza vitabu vingine vya fatwa kwenye mpangilio mzima wa ‘*Muongozo wa Misingi ya Ki-fiqhi*’ (Saiklopidia ya Misingi ya Ki-fiqhi) ili kuifikia misingi ambayo fatwa zinajengewa juu yake, na ambayo misingi hio haipatikani kwenye ‘*Majarida ya Kifiqhi*’.

Hivyo basi inapendekeza yafuatayo:

Moja: Kua na tahadhari juu ya fatwa amabazo haziegemezwi kwenye misingi ya kisharia wala ambazo hazikutegemea dalili inayokubalika kisharia, lakini zinategemea maslahi yanayodhaniwa; ambayo yanakataliwa kisharia kwa kua yametokana na utashi wa nafsi au yametokana na kuathirika na mazingira-kinzani ya misingi ya sharia na makusudio yake makuu.

Mbili: Kuwataka wanaosimamia mambo ya fatwa miongoni mwa wanazuoni au taasisi na kamati kutumia na kuyachukulia kwa uzito ‘Maamuzi na Maazimio’ ya Makongamano ya Fiqhi’, ili kudhibiti utoaji wa fatwa na mipangilio yake katika ulimwengu wa kiislamu.

Tatu: Utoaji wa fatwa ubakie tu ndani ya jopo la maulamaa (wanazuoni) wanaosifika kwa Ucha-Mungu na kujichunga.

Nne: Wanaosimamia mambo ya fatwa wanatakiwa kujikita kwenye misingi ya fatwa iliobainishwa na wanazuoni, hususan hii ifuatayo:

a) Kujilazimisha kutumia dalili za kisharia kutokana na Kitabu (Qur’an), Sunnah, Ijmaa, Qiyas na dalili nyenginezo, aidha kujilazimisha kufuata ‘misingi ya utoaji (*istinbati*) dalili’.
b) Kutilia bidii suala la mpangilio wa ‘vipaombele’ katika kuegesha

maslahi na kuepusha madhara.

c) Kuchunga ‘Ufahamu wa hali halisi’ yaani ‘Fiqhi ya zama hizi’ (*Fiqh al-Waaqi’*) pamoja na mabadiliko ya kila siku ya maeneo na zama kwa namna ambayo haitapingana na msingi wowote wa sharia.
d) Kuenda sambamba na hali za mabadiliko na kuchukua msimamo wa kati na kati baina ya kulinda maslahi na kufuata hukmu za sharia.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 105 (8/11)[1]

Yanayohusiana na 'Maumbile (jeni), Uhandisi-maumbile na Jinomu ya Kibinadamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na moja (11) kilichofanyika mji wa Manamah, Falme ya Bahrain 25 – 30 Rajab, 1419, sawa na 14 - 19 Novemba, 1998.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Maumbile (jeni), Uhandisi-maumbile na Jenome ya Kibinaadamu,** na baada ya kupitia 'Maamuzi na Maazimio' ya kikao cha kumi na moja (11) cha 'Warsha ya Fiqhi-Tiba' kilichofanyika kwa pamoja baina ya 'Kongamano la Fiqh ya Kiislamu', Jeddah na 'Jumuiya ya Kiislamu ya Sayansi za Tiba' (Kuwait), na Ofisi ya Kanda ya 'Shirika la Afya Duniani' (WHO) Alexandria, na Shirika la Kiislamu la Elimu-malezi, Sayansi na Utamaduni (ISESCO), katika kipindi kati ya 23 – 25 Jumada al-Akhira (Mfungo Tisa), 1419, sawa na 13 – 15 Oktoba, 1998 hapo mjini Kuwait;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha utoaji wa 'Maamuzi' juu ya maudhui ya 'Urithishaji, Handasa ya Urithishaji na *Jenomu* ya Vijinasaba vya Binadamu' ili kutoa nafasi zaidi za utafiti wa kina.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 11, Mjeledi 3, Uk. 533).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 106 (9/11)

Yanayohusiana na 'Kikao cha Wataalamu Juu ya Nafasi ya Mwanamke wa Kiislamu katika Maendeleo'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na moja (11) kilichofanyika mji wa Manamah, Falme ya Bahrain 25 – 30 Rajab, 1419, sawa na 14 - 19 Novemba, 1998.

Baada ya kuyapitia maudhui haya na kusikiliza hoja mbalimbali na maoni;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha utoaji wa 'Maamuzi' juu ya maudhui ya 'Kikao cha Wataalamu Juu ya Nafasi ya Mwanamke wa Kiislamu katika Maendeleo' ili utafiti zaidi ufanyike. Kwa lengo hili, pameundwa kamati iliyowakusanya Fadhilat Sheikh Dr. Bakr Bin Abdallah Abuzayd (Rais wa Baraza la Kongamano) na Fadhilat Sheikh Ali al-Taskhiri na Qadhi Mohamed Taqi Usmani. Watawasilisha ripoti yao kwenye kikao kijacho cha 'Kongamano'.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Kumi na Mbili (12) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Riyadh, Falme ya Saudi Arabia

25 Jumada al-Akhira (Mfungo Tisa) – 1 Rajab, 1421

23 - 28 Septemba, 2000

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 107 (1/12)[1]

Yanayohusiana na 'Mikataba ya Uagizaji (*Supply*) na Uzabuni (*Tender*)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na mbili (12) kilichofanyika mji wa Riyadh, Falme ya Saudi Arabia 25 Jumada al-Akhira (Mfungo Tisa) – 1 Rajab, 1421, sawa na 23 - 28 Septemba, 2000.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Mikataba ya Uagizaji (*Supply*) na Uzabuni (*Tender*),** na baada ya usikivu makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya na kwa ushirikiano wa wajumbe wa 'Kongamano' na wataalamu wake pamoja na idadi kubwa ya wanafiqihi;

Imeamuliwa yafuatayo:

1- Mkataba wa Uagizaji (*Supply*):

Moja: Mkataba wa Uagizaji (Supply): ni mkataba ambao '*upande mmoja'* unajilazimisha kwa mujibu wa mkataba huo kukabidhi (kusalimisha) bidhaa husika kwa vipindi vinavyofuata kila baada ya muda fulani kwa '*upande wa pili*', kwa malipo yaliyoainishwa ima yalipwe sasa au baadae, yote au baadhi yake.

Mbili: Iwapo bidhaa husika inayotakiwa kuagizwa (supply) inahitaji itengenezwe basi mkataba wa *istisaa'* ndio utakaofanya kazi. Maamuzi kuhusu *istisnaa'* tayari yalishatolewa na 'Kongamano' kwenye kikao chake cha saba (7) 'Maamuzi' namba 65 (3/7).

Tatu: Iwapo bidhaa husika inayotakiwa kuagizwa (supply) haihitaji itengenezwe, na inafahamika vizuri pamoja na kujilazimisha kuisalimisha

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 12, Mjeledi 2, Uk. 391).

wakati fulani, basi mkataba huu utafanyika katika mojawapo ya njia mbili:

a) Muagizishaji anaharakisha kulipia bidhaa hio kamili wakati wa makubaliano, mkataa huu unapewa hukmu ya mkataba wa *Salam* na unajuzu kwa masharti yaliyobainishwa katika 'Maamuzi' namba 85 (2/9).
b) Iwapo muagizishaji hatolipa malipo kamili wakati wa makubaliano, basi mkataba huu haujuzu, kwa sababu utakua umejikita kwenye 'kuahidiana' (*muwa'ada*) inayolazimisha pande zote mbili. 'Maamuzi' ya 'Kongamano' namba 40 na 41 yalishatoka yakionyesha kua 'Kuahidiana inayolazimisha' inafanana na mkataba kwa mkataba ambao ni kuuza deni kwa deni. Ama ikiwa 'kuahidiana' (*muwa'ada*) sio lazimishi kwa upande mmoja au pande zote mbili basi inajuzu lakini kwa sharti mauziano yafanyike kwa mkataba mpya au kwa kukabidhi bidhaa.

2- Mkataba wa Uzabuni (*Bidding*):

Moja: Uzabuni: Ni mchakato wa kufikia bei ilio rahisi zaidi kwa kununua ima bidhaa au huduma, nayo ni pale mtaka bidhaa au huduma anapotowa mualiko wa wazi kwa kila anaetaka kufanya uzabuni kuwasilisha zabuni zao kwa masharti na vigezo maalum.

Mbili: Uzabuni unajuzu kisharia, uzabuni ni kama mnada, kwa hio hukmu zote za mnada zinatumika hapa, sawa uzabuni wenyewe uwe ni wa watu wote au kikundi fulani, uwe wa ndani au wan je, uwe wa dhahiri au wa siri. Kuhusu mnada tayari yalishatolewa 'Maamuzi ya Kongamano' namba 73 (4/8) ya kikao chake cha nane (8).

Tatu: Inajuzu kubana washiriki wa uzabuni ibaki kwa wale walioruhusiwa tu au wenye vibali vya kiserikali, lakini ni lazima utoaji wa vibali au kuruhusiwa kufanyike kwa misingi ya haki na uadilifu.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 108 (2/12)[1]

Yanayohusiana na 'Kadi za Mikopo Zisizolindwa na Akiba'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na mbili (12) kilichofanyika mji wa Riyadh, Falme ya Saudi Arabia 25 Jumada al-Akhira (Mfungo Tisa) – 1 Rajab, 1421, sawa na 23 - 28 Septemba, 2000.

Kwa mujibu wa 'Maamuzi ya Kongamao' namba 63 (1/7) ya maudhui ya 'Masoko ya Fedha' kwenye kipengele cha 'Kadi za Mikopo' ambapo ilikubalika kua maamuzi juu ya suala la 'kadi hizi' na hukmu zake yatatolewa kwenye kikao kijacho.

Na kwa kuashiria 'Maamuzi ya Kongamano' namba 96 (4/10) kwenye kikao chake cha kumi (10), na baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Kadi za Mikopo Zisizolindwa na Akiba**, na baada ya usikivu wa hoja juu ya mas'ala haya kutoka kwa wanazuoni na wanauchumi, na baada ya kurejea taarifa zote zilizopo kuhusiana na Kadi za Mikopo kwenye maamuzi namba 63 (1/7) ambayo kpitia taarifa hizo tumeweza kutizama suala la 'Kadi za Mikopo Zisizolindwa na Akiba**'** kua:

'Ni hati itolewayo na mtoaji (benki) kupewa mtu wa kawaida au '*mtu wa kikanuni*' (mbebaji kadi) kwa makubaliano yaliopo baina yao yanayomuwezesha kununua bidhaa au huduma kutoka kwa anaeikubali (aneitambua) hati hio (mfanya-biashara) bila ya kufanya malipo ya (taslimu) papohapo kwa kua '*mtoaji kadi*' amedhamini malipo. Malipo yenyewe yanaweza yakalipwa ima kutoka kwa akaunti ya mtoaji kadi ambapo malipo hayo yakakatwa kutoka kwa akaunti ya mbebaji kadi katika mida waliokubaliana, baadhi yao wanaweka *faida za riba* baada ya kupita mda waliokubaliana ikiwa malipo bado hayajafanywa kwa wakati, wengine

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 12, Mjeledi 3, Uk. 459).

hawaweki *faida*.

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Haijuzu kutoa ‘Kadi za Mikopo Zisizolindwa na Akiba’ wala kuamiliana nazo iwapo zimeshurutishwa kuwekwa nyongeza ya *faida ya riba*, hata ikiwa mbebaji kadi ameazimia kulipa ndani ya mda waliokubaliana usiokua na riba.

Mbili: Inajuzu kutoa ‘Kadi za Mikopo Zisizolindwa na Akiba’ iwapo hazikushurutishwa kuwekwa nyongeza ya *faida ya riba* juu ya deni la asili. Hapa kuna tanzu zifuatazo:

a) Inajuzu kwa mtoaji kadi kumtoza mbebaji kadi malipo ya ada ima wakati wa kutolewa kadi au wakati wa kuongeza mda wa matumizi, tozo hii inahesabiwa kua ni malipo ya huduma zinazopatikana kupitia matumizi ya kadi hio.
b) Inajuzu kwa mtoaji kadi kumtoza mfanya-biashara tozo ya manunuzi yaliyofanywa na mbebaji kadi kwa sharti awe mfanya-biashara huyo anauza kupitia kwa kadi bei hiohio anayouza kwa pesa taslimu.

Tatu: Utoaji (withdraw) wa pesa kwa mbebaji kadi ni sawa na kukopa kutoka kwa mtoaji kadi, hakuna tatizo hapa ikiwa hakutakua na nyongeza ya riba, tozo za matumizi ya kadi si katika nyongeza za riba ikiwa hazikushikanishwa na ukopaji, aidha tozo za matumizi za kila mda fulani. Lakini nyongeza yoyote inayotozwa kwa kila muamala wa manunuzi au huduma inaharamishwa kwa kua hapo inakua ni riba iliyoharamishwa kisharia kama ilivyobainishwa kwenye ‘Maamuzi ya Kongamano’ namba 10 (10/2) na namba 13 (1/3).

Nne: Haijuzu kununua dhahabu na fedha au kununua sarafu kwa kutumia kadi isiyolindwa na akiba.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 109 (3/12)[1]

Yanayohusiana na 'Sharti la Adhabu (*Penalty Clause*)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na mbili (12) kilichofanyika mji wa Riyadh, Falme ya Saudi Arabia 25 Jumada al-Akhira (Mfungo Tisa) – 1 Rajab, 1421, sawa na 23 - 28 Septemba, 2000.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Sharti la Adhabu (*Penalty Clause*),** na baada ya usikivu makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya na kwa ushirikiano wa wajumbe wa 'Kongamano' na wataalamu wake pamoja na idadi kubwa ya wanafiqihi;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: '*Sharti la Adhabu*' katika kanuni ni makubaliano baina ya wanaowekeana mkataba ya kukadiria malipo atakayostahiki mshurutishaji kutokana na madhara atakayoyapata iwapo upande wa pili hautatekeleza au hakutimiza waliyokubaliana au amehelewa kutekeleza.

Mbili: 'Baraza la Kongamano' linapenda kuweka msisitizo juu ya 'Maamuzi' yake yaliyatangulia kuhusiana na '*Sharti la Adhabu*' kwenye maamuzi yake ya *Salam* namba 85 (2/9) yanayosema: "*Haijuzu kuweka sharti la adhabu kwa kuchelewa kukabidhi bidhaa, kufanya hivyo ni sawa na kudai ziada juu ya deni jambo ambalo halifai*", aidha na maamuzi yake katika *istisnaa'* namba 65 (3/7) yaanyosema: "*Inajuzu kuweka kifungu cha 'faini' kwenye mkataba wa istisnaa kwa majibu wa makubaliano endapo mmoja wao amekwenda kinyume na makubaliano ila ikitokea dharura isiyoepukika*", na kwenye maamuzi yake ya 'Biashara ya malipo-polepole' namba 51 (2/6) yanayosema: "*Anapochelewa mnunuzi wa kulipa polepole kulipa deni lake kwa wakati, haijuzu*

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 12, Mjeledi 2, Uk. 91).

kumuongezea malipo ya ziada, kufanya hivyo ni riba".

Tatu: Inajuzu kwa *Sharti la Adhabu (faini)* kuingizwa kwenye mkataba wa asili, kama ambavyo inajuzu kuliweka sharti hili kwenye mkataba unaofuata lakini kabla hakujatokea madhara.

Nne: Inajuzu kwa *Sharti la Adhabu (faini)* kuingizwa kwenye mikataba yote ya fedha isipokua tu ile mikataba ambayo makubaliano ya msingi ni ukopeshaji; kwa sababu hapa pataingia riba iliyowazi kabisa. Kwa maana hio, inajuzu kuweka sharti hili kwenye mikataba ya ukandarasi kwa upande wa mkandarasi, na mikataba ya uagizaji kwa muagizaji, na mikataba ya *istisnaa'* kwa mtengenezaji iwapo hawakutekeleza yale waliokubaliana au wamechelewa kutekeleza.

Lakini haijuzu kuweka sharti hili – kwa mfano – katika mikataba ya 'Biashara malipo-polepole' kwa sababu ya mdaiwa kuchelewa kufanya malipo ya awamu ziliobakia, nisawa iwe kuchelewa huku ni kwa sababu ya kulemewa au kuzembea, wala haijuzu katika mikataba ya *istisnaa'* kwa mtengenezewa bidhaa akichelewa kulipa.

Tano: Madhara ambayo yanajuzu kufidiwa malipo ni yale madhara fedha zenyewe, na hasara ya uhakika iliomfikia muathirika, na chumo alolikikosa kwa uhakika, lakini si madhara mengineo kama yale ya *kimaanawi.*

Sita: *Sharti la Adhabu (faini)* liasitishwa kufanya kazi ikithubutu kwa mshurutishwa kwamba kushindwa kwake kutekeleza makubaliano kumetokana na sababu zilizo nje ya uwezo wake, au ikithubutu kwamba hakuna *dhara* lolote lililomfika mshurutishaji.

Saba: Kwa ombi la mojawapo wa pande mbili za mkataba; inajuzu kwa mahkama kubadilisha kiwango cha fidia ikiwepo sababu ya kufanya hivyo, au ikiwa kiwango kilichowekwa ni kikubwa mno.

Inapendekezwa yafuatayo:

Kuandaa warsha maalum ya tahasusi ili kutizama masharti na taratibu muwafaka zitakazopendekezwa kwa mabenki ya kiislamu kuhakikisha

madeni yao yanarejeshwa.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 110 (4/12)[1]

Yanayohusiana na 'Kukodisha Inayoishia Kumiliki na Hati za Uajiri'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na mbili (12) kilichofanyika mji wa Riyadh, Falme ya Saudi Arabia 25 Jumada al-Akhira (Mfungo Tisa) – 1 Rajab, 1421, sawa na 23 - 28 Septemba, 2000.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Kukodisha Inayoishia Kumiliki na Hati za Uajiri,** na baada ya usikivu makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya na kwa ushirikiano wa wajumbe wa 'Kongamano' na wataalamu wake pamoja na idadi kubwa ya wanafiqihi;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kukodisha Inayoishia Kumiliki

Moja: Vidhibiti vya aina zinazojuzu na zilizokatazwa:

a) Kidhibiti cha katazo: Ni pale inapokutana mikataba miwili wakati mmoja juu ya bidhaa hiohio kipindi hichohicho.
b) Kidhibiti cha rukhsa:
    1) Ni uwepo wa mikataba miwili tofauti kila mkataba unajitenga na mwengine, kiwakati; unafungwa mkataba wa biashara baada ya mkataba wa *ijara* (kukodisha), au uwepo wa ahadi ya kumiliki baada ya kumalizika mda wa ijara, ijulikanae kwamba hiari ni sawa na ahadi katika hukmu.
    2) Mkataba wa kukodisha (ijara) uwe ni wa ukweli sio kufunika biashara (mauzo).
c) Dhamana ya kitu kilichokodishwa iwe juu ya mmiliki na wala sio

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 12, Mjeledi 1, Uk. 313).

mkodishwaji, kwa maana hio mkodishaji atabeba dhamana ya maharibiko yoyote yatakayojitokeza ila yale maharibiko yaliyosababishwa na mkodihwaji au uzembe wake, mkodishwaji halazimiki kulipa fidia yoyote ikiwa kilichokodishwa kimeharibika.

d) Iwapo kwenye mkataba kuna kifungu cha bima juu ya kilichokodishwa, basi bima hio ni lazima iwe ya *bima ya ushirikiano kiislamu* sio ya bima ya kibishara, mgharamikaji wa hili atakua ni mmiliki mkodishaji na sio mkodishwaji.
e) Hukmu za *Kukodisha Inayoishia Kumiliki* ni zilezile za kukodisha ndani ya mda wote wa ukodishaji, na hukmu za biashara (mauzo) ni wakati wa kumiliki.
f) Gharama za matengenezo ya kilichokodishwa zitakua juu ya mkodishaji sio mkodishwaji ndanni ya mda wote wa ukodishaji, isipokua gharama za uendeshaji.

Mbili: Aina ya mikataba iliyokatazwa:

a) Mkataba wa *ijara* (kukodisha) unaoishia kumiliki kilichookodishwa kwa kiwango cha malipo anacholipa mkodishwaji ndani ya mda wa makubaliano bila ya kuingia kwenye mkataba mwengine, yaani ijara mwisho wa mda wake inageuka kua kumiliki yenyewe.
b) Ukodishaji wa kitu kwa mtu fulani kwa malipo fulani kwenye mda fulani, sambamba na mkataba wa mauzo ulionin'ginizwa hadi pale yatakapokamilika malipo yote ya mkataba wa ijara waliokubaliana ndani ya mda waliokubaliana, au katika wakati fulani ulioainishwa mustakbali.
c) Mkataba wa ijara wa ukweli ulioambatanishwa na biashara ya kuuza kwa kuweka *hiari ya sharti* kwa faida ya mkodishaji, na biashara inakua ni ya malipo-polepole ya kipindi kirefu kilichoainishwa (mwisho wa mda wa ukodishaji).

Hizi ndizo fatwa na maamuzi yaliyotolewa na taasisi kuu za kielimu ikiwemo '*Jopo la Wanazuoni Wakuu*' wa Saudi Arabia.

Tatu: Aina ya mikataba iliyoruhusiwa:

a) Mkataba wa *ijara* ambapo mkodishwaji anawezeshwa kunufaika na

kile kilichokodishwa kwake kwa malipo maalum kwenye mda maalum, lakini sambamba na mkataba huo kukaambatanishwa na mkataba mwengine wa kumzawadia mkodishwaji kile alichokodishwa, lakini hii ifanyike baada ya kua mkodishwaji ameshalipa malipo yote ya ijara na kuandikiana mkataba mpya, au kutoa ahadi ya kumzawadia baada ya kufanya malipo yote ya ijara, hii ni kwa mujibu wa 'Maamuzi ya Kongamano' kuhusiana na kupeana zawadi namba 13 (1/3).

b) Mkataba wa *ijara* ambapo mmiliki anamkhiyarisha mkodishwaji baada ya kumaliza malipo yote ya ijara ndani ya mda waliokubaliana, amuuzie kile kilichokodishwa kwa bei iliopo sokoni baada ya kumaliika kwa mda wa ijara, hii ni kwa mujibu wa 'Maamuzi ya Kongamano' namba 44 (6/5).
c) Mkataba wa *ijara* ambapo mkodishwaji anawezeshwa kunufaika na kile kilichokodishwa kwake kwa malipo maalum kwenye mda maalum, lakini sambamba na mkataba huo kukaambatanishwa na ahadi nyengine ya kumuuzia mkodishwaji kile alichokodishwa, baada ya kufanya malipo yote ya ijara, thamani ya kuuza watakubaliana pande mbili kwa pamoja.
d) Mkataba wa *ijara* ambapo mkodishwaji anawezeshwa kunufaika na kile kilichokodishwa kwake kwa malipo maalum kwenye mda maalum, na mmiliki atampatia mkodishwaji haki ya kuchagua (*khiari*) ya kumiliki alichokodishwa wakati wowote anapotaka, lakini mauzo yatafanyika wakati wake kwa mkataba mpya na kwa bei ya sokoni wakati huo, hii ni kwa mujibu wa 'Maamuzi ya Kongamano' namba 44 (6/5) au vile watakavyokubaliana wakati huo.

Nne: Zipo aina nyingine za 'Mikataba ya *ijara* (kukodisha) inayoishia kumiliki' lakini kuna *ikhtilafu* baina ya wanazuoni na inahitajia utafiti wa ziada ili ziwasilishwe kwenye kikao kijacho *inshaallah*.

Hati za Uajiri:

'Kongamano' limeamua kuakhirisha maudhuhi ya *Hati za Uajiri* ili utafiti wa ziada ufanyike na hatimae ziwasilishwe kwenye kikao kijacho *inshaallah*.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 111 (5/12)[1]

Yanayohusiana na 'Uwekezaji wa Mali ya Waqfu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na mbili (12) kilichofanyika mji wa Riyadh, Falme ya Saudi Arabia 25 Jumada al-Akhira (Mfungo Tisa) – 1 Rajab, 1421, sawa na 23 - 28 Septemba, 2000.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Uwekezaji wa Mali ya Waqfu,** na baada ya usikivu makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya na kwa ushirikiano wa wajumbe wa 'Kongamano' na wataalamu wake pamoja na idadi kubwa ya wanafiqihi;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha utoaji wa maamuzi kwenye maudhui ya *Uwekezaji wa Mali ya Waqfu* ili utafiti wa ziada ufanyike; hususan kwenye vipengele vifuatavyo:

1) Uwekezaji wa waqfu.
2) Waqfu wa sarafu.
3) Kuuza na kununua waqfu (*Ibdal-Istibdal*).
4) Kuchanganya mali za waqfu.
5) Kupambanua baina ya waqfu na mfuko (dhamana).

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 12, Mjeledi 1, Uk. 39).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 112 (6/12)[1]

Yanayohusiana na 'Ithibati kwa Kutumia Viashiria au Dalili'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na mbili (12) kilichofanyika mji wa Riyadh, Falme ya Saudi Arabia 25 Jumada al-Akhira (Mfungo Tisa) – 1 Rajab, 1421, sawa na 23 - 28 Septemba, 2000.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Ithibati kwa Kutumia Viashiria au Dalili;**

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha uchukuaji wa maamuzi juu ya maudhui ya '*Ithibati kwa Kutumia Viashiria au Dalili*' kwa kua tafiti zilzowasilishwa hazikuangazia mapya ya zama hizi na kutolea hukmu zake.

Wabillah al-Taufiq

≃≃≃

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 12, Mjeledi 3, Uk. 5).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 113 (7/12)[1]

Yanayohusiana na 'Haki za Watoto na Wazee'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na mbili (12) kilichofanyika mji wa Riyadh, Falme ya Saudi Arabia 25 Jumada al-Akhira (Mfungo Tisa) – 1 Rajab, 1421, sawa na 23 - 28 Septemba, 2000.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' zinazohusiana na maudhui ya **Haki za Watoto na Wazee,** na kuyazingatia mapendekezo yaliyotolewa '*Warsha ya Fiqhi-Tiba*' iliyofanyika Dola ya Kuwait kwa kushirikiana na 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu' na ''Jumuiya ya Kiislamu ya Sayansi za Tiba' (Kuwait), katika kipindi kati ya 9 – 12 Rajab, 1420, sawa na 18 – 21 Oktoba, 1999 kuhusiana na maudhui ya '*Haki za Wazee*', na baada ya usikivu wa hoja zilizoibuka kwa ushirikiano wa wajumbe wa 'Kongamano' na wataalamu wake pamoja na idadi kubwa ya wanafiqihi;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Haki za Watoto katika Uislamu:

Utoto unaoheshimika ni msingi wa jamii bora iliyostawi, Uislamu umeweka nafasi maalum ya watoto, umeanzia wakati wa kuchumbia mke/mume; awe mwema, kufanya chaguo liwe zuri kwa kua ni lenye athari kwa mtoto atakaezaliwa na kukulia kwenye mazingira ya upendo na mshikamano wa familia.

Juu ya hili imeamuliwa yafuatayo:

1) Sharia ya Kiislamu imewajibisha; kumlinda mtoto (mjusi - *janeen*) akiwa bado yutumboni mwa mamake dhidi ya kila dhara ambalo

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 12, Mjeledi 4, Uk. 293).

lingemdhuru yeye au mamake kama vileo na mihadarati.

2) *Janeen* (mjusi) ana haki ya kuishi; kwa hio asidhuriwe au kutlewa mimba yake au kwa namna yoyte ile ambayo itapelekea kubovuka kwa maumbile yake, au kumsababishia kilema.
3) Kila mtoto baada ya kuzaliwa kwake ana haki za *madia* na *maanawia*; ama haki zake za *kimadia*: ni kama haki za kumiliki, kurithi, kupokea wasia, kupokea zawadi, na waqfu, na haki zake za *kimaanawia*: ni kumchagulia jina zuri, na nasaba (ukoo) nzuri, dini na uraia (utaifa- uzalendo).
4) Watoto mayatima na waliookotwa na waliopotea na wahanga wa vita na watoto wengineo ambao hawana wasimamizi kwenye maisha yao; watakua na haki zao kamili zitakazosimamiwa na jamii na serikali (dola).
5) Kuhakikisha kwamba mtoto anaezaliwa ananyonyeshwa kipindi cha miaka miwili iliyotimia.
6) Mtoto ana haki ya malezi bora katika mazingira yaliyokua salama, mama mzazi ni mstahiki zaidi wa jambo hili; venginevyo basi ni jamaa zake wa karibu kwa utaratibu unaokubalika kisharia.
7) Ijulikane kua kumsimamia mtoto juu ya nafsi yake na kumuhifadhia mali yake ni miongoni mwa haki zake ambazo haijuzu kuzembea, na afikapo umri wa kubalighi na akiwa na akili zake timamu basi arejeshewe mali yake.
8) Miongoni mwa haki muhimu kabisa za mtoto; ni kumpa malezi bora, kumfundisha maadili mema, kumpatia elimu na taaluma na ujuzi na stadi za kazi zitakazomuwezesha kufanya kazi na kuchuma maisha yake ukubwani mwake. Haki hizi zinatakiwa zisimamiwe vizuri sana, na kwa wale watoto wenye vipaji (talanta) wasaidiwe zaidi kuibua na kukuza vipaji vyao, yote hayo yafanyike ndani ya mwavuli wa Sharia ya Kiislamu.
9) Uislamu unakataza wazazi wa watoto na wasimamizi wao; kuwatelekeza watoto wanaowasimamia ili wasije wakapotea au kunyanyasika, aidha uislamu unakataza kuwatumia vibaya au kuwakalifisha kazi ambazo zitawaumiza kwenye miili yao au akili zao au nafsi zao.
10) Ni dhambi la jinai kubwa kuwaumiza watoto kwenye imani (itikadi)

zao, au nafsi zao, au heshima zao, au mali yao, au akili zao.

Mbili: Haki za Wazee:

Uislamu umejihusisha sana na utukufu wa binadamu katika awamu zake zote; kwa mtazamo wa utukufu uliowekwa na Uislamu kumkirimu binadamu ni pale Allah SWT alipsema: "*Na hakika tumewatukuza wanaadamu*",[1] na pia akasema: "*Na Mola wako Mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema*",[2] na akasema Mtume SAW:

"ما أكرم شاب شيخًا لسنِّه إلا قيّض الله له من يكرمه عند سنه"

"*Hakuna kijana atakaemtukuza mtu mzima kwa utu uzima wake isipokua nae Allah atamletea wakati wa utu uzima wake mwenye kumtukuza*",[3]

akasema tena:

"ليس منا من لم يرحم صغيرنا ويعرف شرف كبيرنا"

"*Si katika sisi yule asiyehurumia wadoo zetu na yule asiyeheshimu wakubwa zetu*".[4]

Juu ya hili imeamuliwa yafuatayo:

1) Kuhamasisha wazee juu ya kulinda afya zao za viwiliwili na za kiroho na za kijamii, na kuendelea kuwakumbusha juu ya hukmu za dini mbalimbali wanazozihitajia katika ibada zao na miamala na mambo yao kwa ujumla, aidha kuwasaidia kujenga uhusiano mzuri na mola wao kwa kutafuta radhi zake na maghfira.
2) Kushinikiza umuhimu wa wazee katika jamii na stahiki zao zote.
3) Familia zao ziendelee kua kituo muhimu cha wao kupata starehe za maisha ya kifamilia, na watoto wao na ajukuu wao waendelee kuwatukuza, wafurahikie uungwaji kizazi na jamaa zao, marafiki na majirani zao, na ikiwa hawana familia zao basi nyumba za wazazi zichukue nafasi za familia.

---

[1] Surat al—Israa: 70.
[2] Surat al—Israa: 23.
[3] Imepokewa na Imam al-Tirmidhi.
[4] Imepokewa na Imam al-Tirmidhi, na Imam Ahmad katika *Musnad* yake.

4) Kuihamasisha jamii ifahamu nafasi za wazee na haki zao kupitia mitaala ya elimu na matangazo ya runinga (televisheni), misisitizo uwe kuwafanyia wema wazazi wawili.
5) Kujenga nyumba za wazee ambao hawana familia zao za kuwasimamia.
6) Kulifanyia kazi suala na somo la tiba ya uzeeni lifundishwe katika vyuo na taasisi za afya, ikiwemo kuwafunda baadhi ya matabibu (madaktari) kuweza kutambua na kutibu magonjwa ya uzeeni, na kunazisha vitengo maalum mahospitalini vyaa maradhi ya wazee.
7) Kutenga sehemu na viti maalum kwa wazee kwenye vyombo vya usafiri na sehemu za maegesho ya magari kwa minajili ya kupata huduma bora.
8) Kulifanyia kazi 'Tamko la Kuwait' juu ya haki za wazee.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≋≋≋

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 114 (8/12)[1]

Yanayohusiana na 'Tamko la Kiislamu juu ya Nafasi ya Mwanamke katika Maendeleo ya Jamii ya Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na mbili (12) kilichofanyika mji wa Riyadh, Falme ya Saudi Arabia 25 Jumada al-Akhira (Mfungo Tisa) – 1 Rajab, 1421, sawa na 23 - 28 Septemba, 2000.

Baada ya kupitia mapendekezo ya '*warsha ya wataalamu*' kuhusu **Nafasi ya Mwanamke katika Maendeleo ya Jamii ya Kiislamu,** iliyofanyika Tehran, 'Jamhuri ya Kiislamu ya Iran' katika kipindi kati ya 17 – 19 Dhul-Qaada (Mfungo-pili), 1415, sawa na 17 – 19 Aprili, 1995; katika kutekeleza 'Maamuzi' namba 10/7 ya 'Mkutano wa Kilele wa Saba wa Kiislamu', mapendekezo ambayo yalifanyiwa marekebisho kupitia 'kitengo cha fatwa' kwenye vikao viwili; tisa (9) na kumi (10) vya 'Kongamano'. Kwa kuweka msisitizo wa maadili ambayo Uislamu umemuekea mwanamke, maadili ambayo yamepigwa vita na 'makongamano ya wanawake ya kimataifa' hususan 'Kongamano la Cairo (Misri) na lile la Beijing (China) na yaliyofuata baada ya hapo, na kwa mujibu wa matamko bainifu ya kiislamu mbalimbali kupambana na vita hivi korofi;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Miongoni mwa malengo ya kiislamu; ni kujenga jamii ambayo wote mwanamme na mwanamke wana nafasi adhimu ya kusaidiana katika ujenzi na maendeleo, na kwa hakika ya Uislamu ni kua umempatia mwanamke haki zake kamili kwa misingi inayoendana na maumbile yake, utu wake, uwezo wake, nguvu zake, malengo yake na nafasi yake ya msingi katika maisha. Katika filosofia ya uislamu; jamii ni kitengo

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 12, Mjeledi 4, Uk. 293).

kilichokamilika kinachomtima mwanamme na mwanamke kama nguzo za msingi, aidha Qur'an tukufu na Sunnah za Bwana Mtume SAW zimetia mkazo juu ya suala la umoja wa kiislamu ambao umejengeka kwenye misingi ya jamii ambapo mwanamme na mwanamke ndio viungo muhimu wenye nafasi kuu katika kuimarisha jamii ya kiislamu.

Mbili: Familia iliyojengeka kwenye misingi ya *ndoa halali* ndio jiwe la msingi la mjengo wa jamii iliyosalimika, kwa maana hio; Uislamu unakataa katakata aina zozote nyingine zinazodaiwa kua ni familia, aidha unakataa uhusiano wowote ule mwengine nje ya mfumo huu wa kisharia, Kwa nafasi ya umama aliyonayo mwanamke na sifa nyengine mahsusi; ana nafasi adhimu katika kuleta utulivu na matumaini kwenye huu mjengo wa kifamilia.

Tatu: Umama, ni mojawapo wa kazi kubwa za mwanamke kwenye maisha yake, na hatoweza kuitekeleza risala hii nyeti vilivyo katika kuandaa vizazi vya baadae ila iwapo mwanamke huyu amepata haki zake zote za Kiislamu ili aweze kusimamia majukumu yake kikamilifu katika nyanja za maisha zinazohusiana nae.

Nne: Mwanamke na mwanamme wana haki sawa katika heshima ya kibanadamu, aidha kama alivyo mwanamke ana haki pia ana na majukumu yanayoendana na maumbile yake na uwezo wake na alivyo mwenyewe, licha ya kwamba wote mwanamme na mwanamke wana sifa-maumbile tofauti lakini wanakamilishana katika utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa sharia ya kiislamu.

Tano: Wito wa kumuheshimu mwanamke katika nyanja zote, na kukataa ukatili dhidi yake; ambao bado unapatikana katika jamii nyingi ukiwemo *ukatili wa nyumbani* (domestic violence), udhalilishaji wa kijinsia, upigaji wa picha chafu, ukahaba, biashara ya ngono; vitu ambavyo vinaonekana kupatikana kwa wingi katika jamii mbalimbali zinazomdharau mwanamke na kuchafua heshima yake na kukataa haki zake za kisharia; mambo haya kwa hakika ni vitendo vya ki-*munkar* vilivyoingizwa kutoka nje na hazina nafasi katika Uislamu.

Sita: Kuvitaka vyombo vya mawasiliano-habari kutilia mkazo nafasi nyeti ya mwanamke na kukataa aina zote za utumiaji mbaya wa mwanamke katika vyombo hivyo na matangazo yao, na uenezaji-haribifu wa maadili na khulka zinazopelekea kudharauliwa kwa mwanamke na kuvunnjiwa heshima yake.

Saba: Inatakiwa kuongeza juhudi katika kupunguza maumivu na machungu ya wanawake na walio dhaifu hasahasa wanawake wa kiislamu ambao bado wanaendelea kuteseka na kudhalilika katika majanga ya vita na uvamizi wa nchi zao na ufukara-shinikizo za minyonyoro ya uchumi ya kigeni.

Nane: Haiwezekani kupatikana kwa maendeleo endelevu mapana ila kwenye misingi ya maadili na khulka njema, hii ikimaanisha kukataa aina zote za maadili-potoshaji ya kigeni ya kiutamaduni na kijamii yanayoingizwa ndani ya jamii za kiislamu, aidha kukemea hujma mbalimbali zinazoelekezwa dhidi ya mifumo na mafundisho ya uislamu yanayohusiana na mwanamke.

Tisa: Kukemea vikali sana sera za baadhi ya serikali za kumzuia mwanamke wa kiislamu uhuru wake kamili katika kufuata na kutekeleza maagizo ya dini yake na yale aliyofaradhishiwa na Allah kama vile kujiheshimu na kujisitiri (*hijab*).

Kumi: Kuandaa mazingira kwa taasisi za elimu ya mwanamke kutenganishwa na wanaume ili kuwapa watoto wa kike uhuru kamili wa kutekeleza haki zao za kisharia.

Kumi na moja: Sharia ya Kiislamu na vyanzo vyake vya msingi vichukuliwe kua ndio rejea ya pekee katika kutafsiri au kufafanua ibara yoyote kwenye *tamko* hili.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 115 (9/12)[1]

Yanayohusiana na 'Mfumuko wa Bei na Kubadilika kwa Thamani ya Sarafu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na mbili (12) kilichofanyika mji wa Riyadh, Falme ya Saudi Arabia 25 Jumada al-Akhira (Mfungo Tisa) – 1 Rajab, 1421, sawa na 23 - 28 Septemba, 2000.

Baada ya kupitia '*tamko la mwisho*' la 'Warsha ya Fiqh-Uchumi' iliyodadisi na kubahithi 'kadhia za mifumuko ya bei' (kwenye vikao vyake vitatu vilivyofanyika Jedda, Kualalumpur na Manama) na maazimio yake na mapendekezo yake, na baada ya usikivu makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya na kwa ushirikiano wa wajumbe wa 'Kongamano' na wataalamu wake pamoja na idadi kubwa ya wanafiqihi;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya kuyafanyia kazi 'Maamuzi' yaliyopita namba 42 (4/5) yanayosema: "*Ulipaji wa madeni yaliyothibiti kwa sarafu fulani inatakiwa yalipwe kwa sarafu ileile, kwani haijuzu kufungamanisha madeni na viwango vya bei inavyobadilika*".

Mbili: Katika mazingira yanayotarajiwa kufumuka kwa bei; inaruhusiwa kuchukua tahadhari kwa kufanya makubaliano ya miamala ya deni kwa sarafu nyengine isiokua ile inayotarajiwa kufumuka (kushuka), kwa kufunga mkataba wa deni kwa mojawapo wa njia hizi:

a) Dhahabu au fedha.
b) Bidhaa inayofanana (homogeneous commodity).
c) Kapu la bidhaa zinazofanana.

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 12, Mjeledi 4, Uk. 10. Na Toleo 5, Mjeledi 3, Uk. 1609).

d) Sarafu nyengine iliyotulia zaidi.
e) Kapu la sarafu (Currency basket).

Deni linalolipwa kupitia mojawapo ya njia zilizotangulia hapo juu lazima liwe ni sawa na asili ya deni lilipokopeshwa; kinacholipwa ni kile kilichokopwa kiuhalisia. Aina hizi zilizotajwa ni tofauti na ile aina iliyokatazwa ambayo wawili wanakubaliana muamala wa deni la baadae kwa sarafu isiokua ile ya asili ya mkopo au kwa Kapu la sarafu, aina hii tayari ilishatoka 'Maamuzi ya Kongamano' namba 75 (6/8 - Nne) ya kukataza.

Tatu: Haijuzu kisharia kukubaliana wakati wa kufunga mkataba wa madeni kufungamanisha malipo yake kwa njia zifuatazo:

a) Kufungamanisha na sarafu ya kimahesabu.
b) Kufungamanisha na kiashiria cha gharama za maisha au viashiria vingine.
c) Kufungamanisha na dhahabu au fedha.
d) Kufungamanisha na thamani ya bidhaa fulani-ainishwa.
e) Kufungamanisha na kiwango cha ukuaji wa kipato cha taifa.
f) Kufungamanisha na sarafu nyengine.
g) Kufungamanisha na thamani ya faida (riba).
h) Kufungamanisha na kiwango cha thamani za *kapu la bidhaa*.

Hii ni kwa sababu ufungamanishi huu unapelekea udanganyifu mkuu na utata ulio mbaya kiasi ya kwamba kila upande anakua hajui kipi chake kipi cha mwenzake, hapa linapotea sharti la msingi la mikataba; *uwazi*. Sasa iwapo vifungamanishi-tajwa hivyo vina muelekeo wa kupanda itamaanisha kutofanana baina ya deni na ulipaji wake, hii ndio riba.

Nne: Ufungamanishi-kiashiria wa malipo (*mishahara*) na kodi (*ijara*):

a) Kuweka msisitizo juu ya kuyafanyia kaza 'Maamuzi ya Kongamano' namba 75 (6/8) ibara: Moja; inayojuzisha ufungamanishi-kiashiria wa malipo (*mishahara*) kulingana na mabadiliko ya viwango vya bei.
b) Inajuzu kwa miamala ya kodi ya mda mrefu kukubaliana pande zote mbili za mkataba juu ya kiwango cha malipo kwa awamu ya kwanza, na kukubaliana kua awamu zinazofuata yatafungamanishwa na

kiashiria fulani; kwa sharti kiwango cha malipo kiwe kinajulikana kila awamu mpya itakapoanza.

Aidha, Kongamano linapendekeza yafuatayo:

1. Kwa kua miongoni mwa sababu kubwa za mifumuko ya bei ni ongezeko la pesa zinazotengenezwa (chapishwa) na taasisi husika kwa sababu mbalimbali zinazojulikana; tunazitaka taasisi hizi kua na uangalifu wa ziada na kusaidia kuondosha sababu hizi zinazopelekea ufumukaji ambao unadhuru jamii kwa kiasi kikuu, aidha kujiepusha na kugharamia ufumukaji kwa kisingizio cha kuziba mianya ya bajeti au kulipia miradi ya maendeleo, lakini wakati huohuo tunawasihi waislamu kote duniani kujilazimisha kikamilifu kufuata maadili ya kiislamu katika utumiaji (ununuzi); ili kuziepusha jamii zetu za kiislamu na aina zote za ubadhirifu, israfu na matumizi mabovu; vyote hivyo ni mioingoni mwa tabia zinazozalisha mfumuko wa bei.

2. Kuongeza ushirikiano wa kiuchumi baina ya nchi za kiislamu hususan katika nyanja za biashara za kimataifa, na kujizatiti zaidi kutumia bidhaa zilizotengenezwa ndani ya nchi za kiislamu badala ya kuendelea kuagiza (import) kutoka nchi za nje, aidha kuziwezesha nchi za kiislamu kua na ushindani mzuri dhidi ya nchi zilizoendelea kiviwanda.

3. Kuandaa tafiti kwa ngazi za benki za kiislamu, kuainisha athari zinazojitokeza za mfumuko wa bei juu ya mali (assets) waliyonayo, na kupendekeza njia muwafaka kulinda mali hayo na wawekezaji wao dhidi ya athari za mifumuko ya bei, aidha kuandaa tafiti na mbinu-bunifu za kiuhasibu za kupambana na tatizo hili la mfumuko kwa ngazi za taasisi za fedha za kiislamu.

4. Kuandaa tafiti juu ya utumiaji wa vifaa vya ugharamiaji na uwekezaji wa kiislamu (*financing and investment instruments on inflation*) Kupambana na mifumuko ya bei na athari zake zinazotarajiwa kujitokeza kisharia.

5. Kudadisi uwezekano wa kurudi kwenye mfumo wa kufungamanisha sarafu na dhahabu, kama njia moja ya kuepuka ufumukaji-bei.

6. Kutambua kwamba kukuza uzalishaji na kuongeza nguvu za uzalishaji zinazotumika kwa sasa ni miongoni mwa visaidizi vikuu vya kupambana na ufumukaji-bei katika mda wa kati na mda mrefu, kwa hio inatakiwa kufanya juhudi za kuongeza na kuboresha uzalishaji katika nchi za kiislamu, ifanyike hivyo kupitia mipango-kazi na taratibu muawafaka zitakazoshajiisha kukuza kipato cha mwananchi na kumjengea uwezo wa kuweka akiba na kuwekeza; kufanya hivi itatuwezesha kufikia maendeleo-endelevu.

7. Kuzitaka serikali za nchi za kiislamu kuweka uwiano mzuri wa bajeti zao kuu (ikiwemo, bajeti za kawaida na za maendeleo ambazo zinategemea mapato ya fedha ya kawaida kuzigharamikia), kwa kujilazimaisha kupunguza (kubana) matumizi na kuyaelekeza vizuri kwa mujibu wa desturi za kiislamu. Itokeapo kwamba bajeti zinahitaji kugharamikiwa; basi njia inayokubalika ni kutumia vifaa vya ugharamikiaji vya kiislamu vilivyojikita kwenye misingi ya kushirikiana, kuuziana na kukodishana, mikopo ya riba ni lazima iepukwe iwe ni kutoka kwa mabenki au taasisi za fedha au utoaji wa hati za deni.

8. Vidhibiti vya kisharia vizingatiwe wakati wa kutumia vifaa vya sera ya fedha, nisawa zile zinazohusiana na mabadiliko katika mapato ya umma au mabadiliko katika matumizi ya umma, sera zote lazima zijikite kwenye misingi ya uadilifu na maslahi ya umma kwa jamii na kulinda mafukara, na kila mmoja abebeshwe mzigo wa mapato kila mtu kwa kadiri ya uwezo wao wa kifedha unaodhihiri kwenye *dakhl* (chumo) ya kila siku na utajiri walionao.

9. Ulazima wa kutumia vifaa vyote vinavyokubalika kisharia vya sera za fedha na sera za sarafu, aidha kutumia mbinu za kukinaisha na sera za kiuchumi na za kiutawala; yote hayo kwa minajili ya kuzikomboa jamii za kiislamu dhidi ya madhara ya mifumuko-bei, malengo ya sera hizo yawe ni kupunguza viwango na ukali wa ufumukaji-bei na

kuviteremsha kwa viwangi vya chini kabisa inavyowezekana.

10. Kuweka dhamana zinazolazimu za kuyafanya maamuzi ya benki kuu yawe huru katika kusimamia mambo ya sarafu na kushikamana nazo lwa lengo la kuleta '*utulivu wa sarafu*' na kupambana na ufumukaji-bei, na kuchunga uwiano-endelevu baina ya benki kuu na taasisi za kiuchumi na za kifedha ili kuhakikisha kua malengo ya maendeleo ya kiuchumi na utulivu wa kiuchumi-sarafu yanafikiwa, kadhalika kuweza kupambana na ukosefu wa ajira.

11. Kudadisi na kufanya upembuzi wa miradi na taasisi za umma ambazo hazifikii malengo ya kiuchumi yaliokusudiwa, na kutizama uwezekano wa kuzibinafsisha taasisi hizo ziwe sekta binafsi ili ziendane na harakati za soko kwa mujibu wa taratibu za kiislamu, hio itakua na athari nzuri katika kuinua uwezo wa uzalishaji na kupunguza mzigo wa gharama kwa bajet ya umma, jambo hili huenda likachangia kupunguza ufumukaji-bei.

12. Kuwataka waislamu wote raia kwa serikali kujilazimisha na taratibu za kiislamu na misingi yake ya kiuchumi, ya kimalezi, ya kimaadili na ya kijamii.

Pendekezo kuhusiana na suluhisho la ufumukaji-bei:

Kuhusiana na suluhisho-pendekezi la ufumukaji-bei; 'Kongamano' linaonelea kuiakhirisha mada hii na kuiwasilisha kwenye kikao kijacho inshaallah.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 116 (10/12)

Yanayohusiana na 'Kuitafsiri Qur'an Tukufu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na mbili (12) kilichofanyika mji wa Riyadh, Falme ya Saudi Arabia 25 Jumada al-Akhira (Mfungo Tisa) – 1 Rajab, 1421, sawa na 23 - 28 Septemba, 2000.

Baada ya kuupitia waraka-kazi uliobeba maudhui ya **Kutafsiri Maana ya Qur'an Tukufu** uliohawilishwa kutoka 'Sekreterieti Kuu' ya kikao cha 'mawaziri wa *auqaf* na mambo ya kiislamu' ulioandaliwa kutoka 'Kiwanda cha Mfalme Fahd cha Uchapishaji wa Msahafu Mtukufu' unaohusu vigezo na masharti mahsusi na taratibu za 'Kutafsiri Maana ya Qur'an Tukufu', baada ya udadisi mpana na usikivu makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya na kwa ushirikiano wa wajumbe wa 'Kongamano' na wataalamu wake pamoja na idadi kubwa ya wanafiqihi;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuzipitisha nukta zote za waraka-kazi uliowasilishwa kuhusiana na **'***Kutafsiri Maana ya Qur'an Tukufu***'.**

Na imependekezwa yafuatayo:

Kuanzishwa kwa taasisi maalum itakayosimamia shughuli za kutafsiri Qur'an Tukufu na elimu zake, taasisi hii ifungamanishwe na 'Kiwanda cha Mfalme Fahd cha Uchapishaji wa Msahafu Mtukufu'.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 117 (11/12)

Yanayohusiana na 'Kuanzishwa kwa Chombo cha Kiislamu cha Qur'an Tukufu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na mbili (12) kilichofanyika mji wa Riyadh, Falme ya Saudi Arabia 25 Jumada al-Akhira (Mfungo Tisa) – 1 Rajab, 1421, sawa na 23 - 28 Septemba, 2000.

Baada ya kudadisi na kuzipitia nukta zote zilokuwemo ndani ya waraka-kazi uliobeba maudhui ya **Kuanzishwa kwa Chombo cha Kiislamu cha Kimataifa cha Qur'an Tukufu,** uliowasilishwa na 'Wizara ya *auqaf* na mambo ya kiislamu' nchini Qatar, na baada ya usikivu makini wa hoja;

Imeamuliwa yafuatayo:

Ipo haja ya ushirikiano wa karibu kati ya nchi hzi mbili; Saudi arabia na Qatar kupitia wizara zao za '*auqaf* na mambo ya kiislamu' pamoja na 'Kiwanda cha Mfalme Fahd cha Uchapishaji wa Msahafu Mtukufu' kilichopo hapo Madina; juu ya suala hili.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 118 (12/12)

Yanayohusiana na 'Mji Mtukufu wa *al-Quds'*

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na mbili (12) kilichofanyika mji wa Riyadh, Falme ya Saudi Arabia 25 Jumada al-Akhira (Mfungo Tisa) – 1 Rajab, 1421, sawa na 23 - 28 Septemba, 2000.

Baada ya kupitia taarifa hatarishi na mapendekezo ya dhulma yaliotolewa na viongozi wa kiyahudi (zayuni) kuhusu mji mtakatifu wa Quds;

Imeamuliwa yafuatayo:

1. Mji wa *Quds* ni sehemu nyeti katika imani (itikadi) ya waislamu wote duniani, kwa sababu katika mji huu ndipo palipofanyika miujiza ya safari ya Mtume SAW ya *Israa* na *Mi'raaj* iliyotajwa katika Qur'an.
2. Mji mtukufu wa *Quds* ni mji wa kiislamu na msikiti wake uliobarikiwa (*Masjid al-Aqsa*) itaendelea kubaki hivyo kwa *nasi* (maandiko) ya Qur'an, na kamwe hautabadilika na hakuna nafasi ya mazungumzo kuugawa mji huo.
3. Hakika ya *Masjid al-Aqsa* uliobarikiwa ni msikiti wa waislamu pekee; mayahudi hawana nafasi wala uhusiano wowote na msikiti huo, tahadhari nzito itolewe dhidi ya kuugusa msikiti huo au kuuchafua, serikali ya kizayuni itabeba majukunu yote na kuwajibika dhidi ya uadui wowote utaofanyika kwa msikiti huu wa *Aqsa*, kadhia ya msikiti huu haifai kamwe kuletwa kwenye mazungumzo na mayahudi; msikiti huu uko juu ya mazungumzo aina yoyote.
4. Haiwezekani katu kupatikana kwa Amani yenye uadilifu au utulivu katika eneo hili (Palestina) ila baada ya kukomesha uvamizi wa kiyahudi dhidi ya *Quds* na msikiti wake uliobarikiwa na baada ya kurudi kwa watu wake Wapalestina kwa jamaa zao.

Na inapendekezwa yafuatayo:

Kuwataka viongozi (watawala) washiriki wa kongamano hili na waislamu wote kwa jumla katika nchi za kiarabu na zile za kiislamu kusimama imara kuulinda mji huu uliotekwa unaotawaliwa kimabavu pamoja na msikiti wake uliobarikiwa na kusimama pamoja na watu wake (wapalestina) wanaopambana dhidi ya uyahudishaji wa mji huu au kuufanya mji huu uwe ni mji wa kimataifa (njia ya kuwanyima wapalestina haki zao), kuugeuza mji huu uwe wa kiyahudi au wa kimataifa ni jambo lisilokubalika katu na kwa namna yoyote ile.

Wabillah al-Taufiq

≋≋≋

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Kumi na Tatu (13) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Kuwait

7 - 12 Shawwal (Mfungo Mosi), 1422

22 - 27 Disemba, 2001

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 119 (1/13)[1]

Yanayohusiana na 'Uwekezaji wa Waqfu na Mapato Yake'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tatu (13) kilichofanyika nchini Kuwait 7 - 12 Shawwal (Mfungo Mosi), 1422, sawa na 22 - 27 Disemba, 2001.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Uwekezaji wa Waqfu na Mapato Yake,** ambazo zilikua zimewasilishwa kwenye kikao cha kumi na mbili (12) na kwenye kikao hichi, na baada ya kupitia 'maamuzi ya kongamano' ya kikao cha nne (4), na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya na kwa ushirikiano wa wajumbe wa 'Kongamano' na wataalamu wake;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha maudhuhi ya *Uwekezaji wa Waqfu na Mali Zake* na utoaji wa maamuzi; ili tafiti za ziada zifanyike na hatimae ziwasilishwe kwenye kikao kijacho *inshaallah*.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

[1] Tizama Jarida la 'Kongamano' (Toleo 13).

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 120 (2/13)

Yanayohusiana na 'Zaka za Kilimo'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tatu (13) kilichofanyika nchini Kuwait 7 - 12 Shawwal (Mfungo Mosi), 1422, sawa na 22 - 27 Disemba, 2001.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Zaka za Kilimo,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya na kwa ushirikiano wa wajumbe wa 'Kongamano' na wataalamu wake;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Gharama zote zinazohusiana na unoshaji (umwagiliaji maji) wa kilimo hazitolewi kwenye hesabu ya zaka, gharama hizo tayari zimeshazingatiwa na sharia kwa kiwango cha kulazimu zaka.

Mbili: Gharama zote zinazohusiana na utayarishaji wa ardhi na uchimbaji wa majedwali na kuhamisha michanga hazitolewi kwenye hesabu ya zaka.

Tatu: Gharama zote zinazohusiana na kununua mbegu, mbolea (samadi), na dawa za kukinga mimea dhidi ya magonjwa ya kilimo na mfano wake zihusuzo nsimo wa kilimo; iwapo gharama hizo zimelipwa na mtoaji zaka basi hazitolewi kwenye mfuko wa zaka, ama ikiwa alidharurika kukopa kwa kua hakua na pesa hizo basi mwanzo zitatolewa pesa hizo kwenye mfuko wa zaka, tegemeo la hukmu hii ni taarifa (*aathaar*) mbalimbali zilizopokelewa kutoka kwa maswahaba RA wakiwemo Ibn Umar na Ibn Abbas RA zinazosema kua: "*Mkulima mwanzo anatowa pesa anazodaiwa kisha baadae anafanya hesabu ya zaka kwa kilichobaki*".

Nne: Gharama za uwasilishaji zaka za kilimo na matunda kwa wastahiki wake zinatolewa kwenye zaka zenyewe.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 121 (3/13)

Yanayohusiana na 'Zaka za Hisa Zinazomilikiwa kwa Lengo la Kufaidika na Chumo Lake'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tatu (13) kilichofanyika nchini Kuwait 7 - 12 Shawwal (Mfungo Mosi), 1422, sawa na 22 - 27 Disemba, 2001.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Zaka za Hisa Zinazomilikiwa kwa Lengo la Kufaidika na Chumo Lake,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya na kwa ushirikiano wa wajumbe wa 'Kongamano' na wataalamu wake.

Na baada ya kupitia 'Maamuzi ya Kongamano' namba 28 (3/4) yanayohusiana na '*zaka za hisa kwenye makampuni*' yaliyosema kwenye ibara: (Tatu):

"*Iwapo kampuni haikuwatolea zaka wenye hisa kwa sababu yoyote ile, basi ni wajibu wa wamiliki wa hisa kutoa wenyewe zaka za hisa zao kwa kutaka kujua kima cha mali yaliyotokana na hisa zao.*

Ikishindikana kujua kima cha mali yaliyotokana na hisa zao, basi atatizama iwapo alinunua hisa hizo kwa lengo la kufaidika na mgao wake unaotolewa kila mwaka, na wala hakukusudia kuzifanyia biashara hisa hizo, basi atatoa zaka za vitendea kazi[1] *kwa kipimo cha nyumba na ardhi zilizokodishwa ambazo si za kilimo, yaani mmiliki wa hisa hapa hawajibiki kuzitolea zaka hisa zenyewe, bali atatoa zaka kwenye mgao atakaopata ambayo itakua ni asilimia 2.5 (yaani 2.5%) inayotolewa baada ya mzunguko wa mwaka kuanzia siku alipokabidhiwa mgao wake, vigezo vingine na masharti ya zaka yanazingatiwa*".

Imeamuliwa yafuatayo:

[1] Tizama 'Maamuzi' ya Kongamano ya kikao cha pili Namba 2 (2/2).

Iwapo kampuni (isiyotoa zaka) ina mali yanayowajibika kutolewa zaka kama vile pesa taslimu, mali ya biashara na madeni yaliyopo kwenye dhima ya wadaiwa na pesa hizo zote hazijatolewa zaka zinazostahiki na mwenyehisa akashindwa kujua kwa yakini katika hesabu za kampuni hio hisa zake hasa ni kiasi gani; basi itamlazimu mwenyehisa afuatilie kwa makini na kwa kina kadri iwezekanavyo ili aweze kutoa zaka zinazohusu hisa zake, hii ikiwa kampuni haijafikia kiwango cha kulemewa (deficit) na kufinikizwa na madeni wanaodaiwa.

Ama ikiwa kampuni haina mali yanayowajibika kutolewa zaka, basi itatumika hapa hukmu iliyotolewa kwenye Maamuzi namba 28 (3/4) ya kwamba: ataoa zaka kutokana na faida tu na sio kutokana na hisa zenyewe.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≃≃≃

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 122 (4/13)

Yanayohusiana na 'Musharaka Inayopunguka (*Diminishing Musharaka*) kwa Mujibu wa Mikataba Mipya ya Kisasa'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tatu (13) kilichofanyika nchini Kuwait 7 - 12 Shawwal (Mfungo Mosi), 1422, sawa na 22 - 27 Disemba, 2001.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Musharaka Inayopunguka (*Diminishing Musharaka*) kwa Mujibu wa Mikataba Mipya ya Kisasa,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya na kwa ushirikiano wa wajumbe wa 'Kongamano' na wataalamu wake;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha maudhuhi ya 'Musharaka Inayopunguka (*Diminishing Musharaka*) kwa Mujibu wa Mikataba Mipya ya Kisasa' na utoaji wa maamuzi; ili tafiti za ziada zifanyike na hatimae ziwasilishwe kwenye kikao kijacho *inshaallah*.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 123 (5/13)

Yanayohusiana na 'Mudharaba Shirikishi katika Taasisi za Fedha (Akaunti za Uwekezaji)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tatu (13) kilichofanyika nchini Kuwait 7 - 12 Shawwal (Mfungo Mosi), 1422, sawa na 22 - 27 Disemba, 2001.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Mudharaba Shirikishi katika Taasisi za Fedha (Akaunti za Uwekezaji),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya na kwa ushirikiano wa wajumbe wa 'Kongamano' na wataalamu wake;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Maana ya *Mudharaba Shirikishi*:

Mudharaba Shirikishi ni aina ya mudharaba ambao unaleta pamoja wawekezaji kadhaa; wawekezaji hawa wanampatia mtu au kampuni mali yao ili yawekezwe na kuzalishwa, mtu huyu au kampuni hii wanaoachiwa mali haya kuwekeza ima wanapewa uhuru wa kutizama wapi pazuri pa kuwekeza au wanaweza pewa eneo fulani la uwekezaji, pamoja na kumuidhinisha ima kwa uwazi au kwa ishara kwamba niswa achanganye mali ya wawekezaji na yale ya kwake, aidha kumkubalia baadhi ya nyakati kutoa mali yao yote au baadhi panapotokea dharura ya kufanya hivyo lakini kwa masharti yatakayoainishwa.

Mbili: **Uhalali wa *Mudharaba Shirikishi*:**

Mudharaba Shirikishi huu umejemgeka kwenye misingi ya 'Maamuzi ya Wanazuoni' yanayojuzisha ushirikiano wa wenye mali na rukhsa ya wao kumshirikisha '*Mudharib*' pamoja nao kwenye rasilimali, hali hii haikai mbali

nan a zile aina za '*mudharaba halali*' iwapo pande zote husika zitafuata vidhibiti vya kisharia vya mudharaba, pamoja na kuzingatia yanayotakikana kwenye ushirikiano huu bila kutoka kwenye muktadha wa sharia.

Tatu: Washirika wa Mudharaba:

Wawekezaji kwa pamoja ni '*wenyemali*', uhusiano kati yao; akiwemo *mudharib* (akichanganya mali yake na yao), ni uhusiano wa *kushirikiana*. Aliekubaliwa kua mzalishaji wa mali hayo anaitwa: *mudharib* anaweza akawa mtu au kampuni kama vile benki na taasisi za fedha. Uhusiano baina yake (*mudharib*) na wawekezaji unaitwa: *mudharaba* (au *Qiradh*) na huyu *mudharib* ndie anaechukua maamuzi ya uwekezaji na usimamizi na mipangilio. Na iwapo *mudharib* huyu atamuakilisha mtu wa tatu katika shughuli za uwekezaji basi huu itakua ni '*Mudharaba wa Pili*' baina ya mudharib wa kwanza na yule aliewakilishwa kuwekeza, hapana mahusiano hapa baina yake na '*wenyemali*' (wamiliki wa akaunti za uwekezaji).

Nne: Kuchanganya Mali kwenye *Mudharaba Shirikishi*:

Hakuna katazo la Kuchanganya mali ya '*wenyemali*' baina yao au mali yao na yale ya *mudharib*, bora jambo hili lifanyike kwa radhi zao ima za wazi au kwa ishara, aidha katika mazingira ya kampuni kusimamia mudharaba na kupangilia uwekezaji usiokua na madhara kwa 'wenyemali' basi kila mmoja angejua kiwango chake kwa asilimia (%) katika rasilimali, uchanganyaji huu unazipatia rasilimali hizi nguvu za ziada kutanashati na kutanuka na hivyo kuzidisha faida.

Tano: Ulazima wa Mudharaba Kuainishwa Mda:

Kimsingi, mudharaba ni mkataba usiolazimu; moja ya pande mbili ana haki ya kuufuta mkataba, ila kuna hali mbili ambapo haki ya kufuta mkataba inakua haipo tena:

a) Mudharib anapoanza kazi; hapa mkataba wa mudharaba unakua wa lazima mpaka pale ifikapo wakati wa kufunga hesabu.
b) Atakapochukua ahadi '*mwenyemali*' au *mudharib* kutofuta mkataba wao kwa kipindi fulani, basi inawalazimu kutimiza ahadi yao, kinyume

chake ni kuvuruga mwenendo mzima wa uwekezaji ndani ya mda huo.

Sita: Kuainisha mda wa mudharaba:

Hakuna katazo la kisharia la kuainisha mda wa mudharaba kwa itifaki ya pande zote mbili, mda-ainishwa ukipita na mkataba nao unakua umekwisha bila ya kuwepo haja ya kuufuta, athari ya kuainisha mda itabaki kwenye kuzuia wahusika kuingia kwenye miamala mingine mipya baada ya kupita huo mda, lakini sio kwenye kuendelea na mgao na kufunga hesabu zilizopo.

Saba: Kugawa faida kwa njia ya (nambari) kwenye *Mudharaba Shirikishi*:

Hakuna katazo la kisharia la kugawa faida kwa kutumia utaratibu wa '*nambari'* ambao unazingatia kiwango cha pesa cha kila muwekezaji na mda aliotumia kubakia kwenye uwekezaji, kwa kua mali ya wawekezaji wote kwa pamoja yalichangia kutengeneza faida kila mtu kulingana na kiwango cha pesa na wakati aliokuwepo kwenye uwekezaji, hivyo itakua ni kutenda haki na kufanya uadilifu kila mgao ukaendana na kiwango cha pesa zilizowekezwa na mda uliotumika. Ijulikane kua wawekezaji wanapoingia kwenye 'Mudharaba Shirikishi' kwa namna ulivyo ni ishara ya kukubali kivitendo kusamehe vijitatizo vidogo vya hapa na pale, aidha ushirikiano huu ni kutoa fursa kwa kila mshirika kufaidi kwa mali ya mwenziwe, na hii isiwe ni sababu ya kukatisha ushirikiano na faida, ugavi huu umeridhiwa kwa viwango vya pamoja vinavyotokana nayo.

Nane: Uundaji wa Kamati ya Kujitolea Kulinda Haki za Wenyemali (Kamati ya Washirika):

Kwa kua wawekezaji (wenyemali) wana haki juu ya *mudharib* zilizojikita kwenye masharti ya uwekezaji yaliyo wazi na yale yaliyokubaliwa na wao kuingia kwenye 'Mudharaba Shirikishi', basi ijulikane kua hakuna katazo la kisharia la Uundaji wa Kamati ya Kujitolea itakayolinda haki hizo na kufuatilia utekelezaji wa masharti yaliyokubaliwa bila ya kuingilia katika maamuzi yake ya kiuwekezaji ila kwa njia ya ushauri usiolazimu kwa

mudharib.

Tisa: Mdhamini wa Uwekezaji:

‘Mdhamini wa Uwekezaji’ hapa inakusudiwa benki au taasisi ya fedha yenye *tasnifu* na utambuzi wa hali ya juu katika mas’ala ya fedha, wanakabidhiwa mali na hati-fungani zinazowakilisha mali ili taasisi hii au benki hii iwe ni yenye kuaminiwa, na kumzuia (kumdhibiti) *mudharib* asijihusishe na vitendo vinavyokinzana na masharti ya mudharaba. Aidha, hakuna katazo la kisharia bora tu jambo hilo liwe limewekwa wazi kwenye hati ya makubaliano (Taasisi na Mudharaba) ili ‘wenyehisa’ wawe wanajua, na kwa sharti ya ‘Mdhamini wa Uwekezaji’ asiingilie katika maamuzi; kazi yake iwe tu kulinda na kuhakikisha vigezo vya uwekezaji vya kisharia na kitaaluma vinazingatiwa.

Kumi: Kuweka kiwango cha faida ya mudharaba na vishajiishi kwa mudharib:

Hakuna katazo la kisharia la kuweka kiwango kinachotarajiwa cha faida na kuainisha kua endapo faida itakua itazidi ile iliyotarajiwa basi mudharib ataongezewa sehemu katika ziada hio, lakini hii ni baada kuainisha kiwango cha faida kwa pande zote mbili bila kujali kiwango cha faida yenyewe.

Kumi na moja: Kuainisha mudharib iwapo mudharaba unasimamiwa na ‘*mtu wa kimaanawi*’ (benki au taasisi ya fedha):

Iwapo mudharaba unasimamiwa na benki au taasisi ya fedha basi mudharib hapa anakua ni ‘*mtu wa kimaanawi*’ bila kujali mabadiliko yanayotokea kwenye baraza kuu au halmashauri ya utawala au kamati-tekelezi, wala hakuna athari yoyote juu ya uhusiano kati ya ‘wenyemali’ na mudharib panapotokea mabadiliko yoyote katika pande mbili hizo madamu walishakubaliana juu ya ‘hati ya makubaliano’ iliyo wazi na iliyokubaliwa juu ya suala la kuingia kwenye mudharaba shirikishi, aidha mudharaba hautoathirika kwa kuchanganyikana baina ya ‘*mtu wa kimaanawi*’ anaesimamia mudharaba na ‘*mtu wa kimaanawi*’ mwengine. Endapo mojawapo wa matawi ya ‘*mtu wa kimaanawi*’ yamejitenga na yakawa na

‘*utu wa kimaanawi*’ unaotofautiana; basi ni haki ya ‘wenyemali’ kuamua kutoka kwenye mudharaba hata kama mda-ainishwa bado haujapita.

Kwa kua ‘*mtu wa kimaanawi*’ ndie anaesimamia mudharaba kupitia kwa wafanyikazi wake basi atabeba jukumu la malipo yao, kama ambavyo atabeba jukumu la gharama nyengine zisizokua mubashara kwa kua gharama zote hizo zitasimamiwa na sehemu ya mgao wa faida yake, Ama mudharaba hawatabeba gharama isipokua zile za mubashara zinazohusu mudharaba, na gharama za kazi ambazo mudharib haruhusiwi kuzifanya kama vile huduma za nje zinazohitajika ambazo si katika maeneo ya wafanyikazi wake.

Kumi na mbili: Dhamana ya uwajibikaji katika mudharaba na hukmu ya dhamana ya mudharib:

Mudharib ni mwenye kuaminiwa na habebi dhamana ya uwajibikaji wa hasara au maharibiko yanayojitokeza ila ikiwa amekusudia hivyo au amezembea kwa makusudi; kufanya hivyo ni uvunjaji wa masharti ya kisharia na vidhibiti vya uwekezaji vilivyoainishwa ambavyo ndio msingi wa makubaliano mwanzoni. Hukmu hii inafanya kazi kwa mudharaba ya mtu mmoja au mudharaba shirikishi, na wala haibadiliki kwa kisingizio cha kuifananisha na ‘ijara shirikishi’ au kuekeana ‘sharti lazimishi’, lakini hakuna katazo la kisharia kuwepo kwa upande wa tatu utakaobeba dhamana ya uwajibikaji kwa mujibu wa ilivyokuja kwenye ‘Maamuzi ya Kongamano’ namba 30 (5/4) ibara ya (9).

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 124 (6/13)

Yanayohusiana na 'Bima ya Afya na Utumiaji wa Kadi za Afya'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tatu (13) kilichofanyika nchini Kuwait 7 - 12 Shawwal (Mfungo Mosi), 1422, sawa na 22 - 27 Disemba, 2001.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Bima ya Afya na Utumiaji wa Kadi za Afya,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya na kwa ushirikiano wa wajumbe wa 'Kongamano' na wataalamu wake;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha maudhuhi ya ***Bima ya Afya na Utumiaji wa Kadi za Afya*** na utoaji wa maamuzi; ili tafiti za ziada zifanyike hususan katika kudhibiti lugha na masharti yake; na hatimae ziwasilishwe kwenye kikao kijacho *inshaallah*.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 125 (7/13)

Yanayohusiana na ‘Matukio ya Palestina na Kwengineko’

Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), katika kikao chake cha kumi na tatu (13) kilichofanyika nchini Kuwait 7 - 12 Shawwal (Mfungo Mosi), 1422, sawa na 22 - 27 Disemba, 2001, linafuatilia kwa karibu sana hali wanayopitia Umma wa Kiislamu katika zama hizi pamoja na kutathmini na kuchambua njama za maadui zinazoelekezwa dhidi ya Uislamu na Waislamu zinazokusudia kufikia mambo mawili:

- Kuchafua ukweli wa Uislamu kupitia kuichafua akida (imanni) yake na kutilia shaka hukmu za sharia ya kiislamu.
- Kuvuruga heshima za waislamu, kuzitawala nchi zao, kumwaga damu zao, kunyakua utajiri wa nchi zao na kuharibu uchumi wao.

Wanazuoni na Wanafiqihi wa ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ wana wajibu kisharia na dhimma ya kubainisha hukmu zinazohusiana na hali za waislamu, na hawapaswi kabisa kuficha kile wanachokijua katika yale ambayo yanalazimu kubainishwa, hii ndi ahadi aloichukua Allah kwa ‘wenye ilmu’ (wanazuzoni) juu ya ulazima wa kubainisha ukweli, haki na hukmu za sharia, na uharamu wa kuuficha ukweli, bali amekemea wale wanaoficha ukweli pale aliposema:

> “*Na ni nani mwenye kudhulumu zaidi kuliko yule aliye ficha ushahidi alio nao utokao kwa Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na hayo myafanyayo*” .[1]

Wanazuoni wa Kibanii-Israil (*mayahudi*) wa zamani walistahiki laana na kukoseshwa rahma za Allah kwa kosa la kuficha *ilmu* (elimu), kama alivyosema Allah:

[1] Surat al-Baqarah: 140.

"*Hakika wale wanao ficha tuliyo yateremsha nazo ni hoja zilizo wazi na uwongofu baada ya Sisi kuzibainisha kwa watu Kitabuni -- hao anawalaani Mwenyezi Mungu, na wanawalaani kila wenye kulaani*".[1]

Hukmu ya ayah ii imekuja kukusanya kila anaeficha ilmu inayolazimu kutolewa, ndio Mtume SAW akasema:

"ما من رجل يحفظ علمًا فكتمه، إلا أُتى به يوم القيامة ملجما بلجام من نار"

"*Hakuna mtu yeyote atakaepewa ilmu na akaificha ila mtu huyu ataletwa siku ya Qiyama (malipo) akiwa amefungwa kwa koleo za moto wa Jahannam*"[2]

Aidha haijuzu kuchelewesha ubainifi wa ilmu nje ya wakati wake unaohitajika, na miongoni mwa kadhia nyeti kabisa kwa umma leo hii ambazo zinahitajika kuelezewa na kuwekwa wazi na bayana ni '*Kadhia ya Palestina*' na kadhia nyengine zinazofanana na hio katika baadhi ya nchi za kiislamu.

Hivyo basi; imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Nchi ya Palestina ni ardhi ya Masjid al-Aqsa; kibla cha kwanza cha uislamu na msikiti wa tatu kwa utukufu zaidi (baada ya ule wa Makkah na Madina) inayokusudiwa kwa ziara na ibada, na ni kituo cha safari ya kimiujiza ya Mtume SAW usiku wa *israa* kwenda *mi'raaj* (safari ya kimiujiza ya kwenda mbinguni usiku wa *israa*), pia ni ardhi ya mitume (manabii) waliotangulia na ni haki ya waislamu wote. Haki hii inamlazimu kila muislamu kuilinda na kuinusuru kwa nguvu zote zinazowezekana, licha ya kuwepo kwa baadhi ya waislamu watakaozembea na kusalimu amri kwa kuitelekeza ardhi hii lakini hoja itabaki palepale kua hii ni haki yenye watu wake; dhulma na madhalimu hawatokua na nafasi katika ardhi hii.

Katika *ijma'* (makubaliano) ya wanazuoni imepitisha uharamu wa mvamizi wa ardhi kuendelea kuikalia ardhi hio au sehemu yoyote ya ardhi ya waislamu; kumuacha mvamizi kuendelea kukalia ardhi aliyoivamia na kama kumpa rukhsa na uhalali wa uvamizi wake na kushajiisha kuendelea na

[1] Surat al-Baqarah: 159.

[2] Imepokewa na Imam ibn Majah kwa sanad (riwaya) iliyo sahihi.

uvamizi wake na uadui wake, hivyo basi uislamu umepitisha kua aliedhulumiwa ana wajibu na haki kupambana na mvamizi aliedhulumu na kupigana nae vita hadi pale mvamizi atakapoachia ardhi aliyoivamia akiwa mnyonge (dhalili) kabisa.

Mbili: Serikali za kiislamu pamoja waislamu wote kwa jumla wana wajibu wa kuirudisha ardhi (nchi) ya kiislamu yoyote inayokaliwa kimabavu kuwarudishia watu wake wa halali, na kuulinda Masjid al-Aqsa dhidi ya uchafuzi wa walowezi wa kizayuni (mayahudi) wanaowafanyia uadui uislamu na waislamu tangu uislamu ulipodhihiri, nab ado wanaendelea na ukiritimba wao kila uchao; leo hii wamekua na nguvu na ukakamavu.

Tatu: Waislamu wote duniani; kila mmoja kwa uweza wake, wana wajibu wa kuwasaidia Wapalestina kwa nafsi zao na kwa mali yao ili kuwawezesha kuendelea kulinda ardhi yao na sehemu takatifu na kupambana na *ujabari wa kizayuni* ambao hawasiti kumwaga damu na kuua wasiokua na hatia mioingoni mwa watoto na wanawake, kuwabomolea nyumba zao kwa kutumia silaha kali sana na hatari za makombora na vifaru na helikopta na ndege za kivita, mbali na kutumia vita vya kiuchumi katika kuwaharibia mashamba yao na kilimo chao na kusumua miti na mimea na kuzuia misaada ya chakula isiwafikie walengwa waliofungiziwa.

Usaidizi huu ni wajib kwa umma wa kiislamu wote raia na serikali zao, kwani waislamu ni kama mkono mmoja dhidi ya adui yao, na muislamu kwa muislamu ni kama mjengo ulioshikana kila tofali linatilia nguvu tofali lingine.

Nne: Jukumu la serikali za nchi za kiislamu kuongeza juhudi kupitia mashirika ya kimataifa na mahusiano yao ya kisiasa na kiuchumi na mengineo, na kufanya juu chini kuzuia misaada ya kigeni ya kisiasa na kijeshi inayokwenda kwa adui.

Tano: Ni haki ya Wapalestina kusimamisha dola yao iliyo huru juu ya ardhi yao yote na Quds ikiwa ndio mji mkuu wa dola hio, aidha ni haki ya Mpalestina kujilinda nafsi yake na kupigana na adui yake kwa njia zote zinazokubaliwa, bali ni heshima ya muislamu kutetea haki yake na akifa

atakua ni *shahidi* mbele ya Mwenyezi Mungu.

Hivyo basi; 'Kongamano' linausia Umma wa Kiislamu viongozi na raia; yafuatayo:

Moja: Kujilazimisha kushikamana na Uislamu; akida na sharia:

Ni wazi kwamba masaibu na matatizo ya ndani na ya nje yanayowafika umma wa kiislamu yametokana na kua waislamu wamejieka mbali na *aqeeda* na *sharia* za kiislamu ambazo ni miongozo ya Allah kwetu sisi, kama alivyosema:

> "*Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki*".[1]

Ijulikane kwamba kila mda unapozidi wa kuitenga sharia ya kiislamu na maisha mianya ya mipasuko inaongezeka baina serikali na raia zao na kuzidisha ukosefu wa elimu sahihi inayopelekea upotoshaji wa kifikra na silka za watu na jamii kwa jumla.

'Kongamano' linapenda kusisitiza wosia wake uliotolewa kwenye kikao cha saba (7) wa kuzitaka serikali katika nchi za kiislamu kulinda *aqeeda* ya kiislamu, na kuipatia nafasi na kuilinda dhidi ya vichafuzi ambavyo vinapelekea kuitilia shaka au kuibomoa na kupasua umoja wa waislamu na kuwafanya waingie kwenye *ikhtilaf* na malumbano. Aidha, 'Kongamano' linapenda kuweka msisitizo juu ya wosia huu kwa kuzitaka serikali katika nchi za kiislamu: "*Kufanya wawezavyo kutekeleza (kuifanyia kazi) sharia ya kiislamu na kuifanya iwe ni muongozo na nyenzo za kutengeneza mahusiano yao ya kisiasa ya ndani na nje*".

Mbili: Kuwanusuru waislamu:

Waislamu popote walipo ni umma mmoja unaounganishwa na *aqeeda* ya *tauheed* (kumpwekesha Allah), aidha unaunganishwa na sharia ya kiislamu na *Qibla* kimoja; wamekua kama mwili mmoja kinapougua kiungo kimoja basi mwili mzima unaumia kama alivyotufananisha Mtume SAW, hivyo basi

[1] Surat Ta-Ha: 124.

ni *wajib* wa kila muislamu kuwanusuru waislamu wanapokua kwenye dhiki, shida, uvamizi wa ardhi yao au wanapofikwa na majanga, Allah amesema:

"*Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi. Huamrisha mema na hukataza maovu...*".[1]

Na Mtume SAW akasema:

"المسلم أخو المسلم لا يظلمه ولا يسلمه، ومن كان في حاجة أخيه كان الله في حاجته، ومن فرج عن مسلم كربه فرج الله عنه بها كربة من كرب يوم القيامة"

"*Muislamu ni nduguye Muislamu, asimdhulumu wala asimsalimishe kwa adui yao, yeyote atakaemsaidia nduguye basi Allah nae atamsaidia kwenye shida zake, na yeyote atakaemuondoshea Muislamu dhiki hapa duniani, basi Allah Atamuondoshwa dhiki za Qiyama*"[2]

Kunusuru Waislamu kunafanyika ima kwa nafsi au kwa mali au kuunga mkono *kimaanawi* na kisiasa na mfano wake kwa kadri ya hali na mazingira zinavyoruhusu.

Aidha, 'Kongamano' linapenda kuweka msisitizo kuhusiana ya wosia wake uliotolewa kwenye kikao cha saba (7) wa kuzitaka serikali katika nchi za kiarabu na kiislamu juu ya suala la kuwanusuru waislamu wanaopitia madhila na unyanyasaji kote duniani, na kuwaunga mkono kwenye kadhia zao na kuwakinga dhidi ya hujma za maadui zao kwa njia zote zinazowezekana.

Tatu: Uharamu wa Uadui katika Uislamu:

Uislamu unaharamisha kabisa kumfanyia mtu yeyote uadui pasina haki, aidha unaharamisha kutisha na kutia khofu nyoyoni mwa watu wasuikua na hatia ambao Uislamu umeharamisha damu zao, uadui wowote utakaofanywa wa aina hii ni ugaidi ulioharamishwa.

Ijulikane kua kujiandaa vilivyo na kuandaa ngugu za kutosha za kumtishia

[1] Surat al-Tauba: 71.

[2] Imepokewa na Imam Muslim; Hadith namba 1830.

adui ni jambo linalotakikana kisharia, na hili ndilo lililokusudiwa pale Allah aliposema:

> "*Basi waandalieni nguvu kama muwezavyo, na kwa farasi walio fungwa tayari-tayari, ili kuwatishia maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu, na wengineo ambao hamwajui, lakini Mwenyezi Mungu anawajua*".[1]

Hapana shaka yoyote kua Muislamu kupambana na mvamizi wa aliavamia ardhi na kuikalia nchi yake kimabavu; kwa kutumia nguvu zote alizonazo ni jambo linalokubalika bali ni wajib kufanya hivyo, hii ndio hali ya mapambano ya wapalestina dhidi wavamizi wa kizayuni waliovamia na kuwavunja haki zao.

Ni katika dhulma inayosikitisha sana kua baadhi ya mataifa makubwa wanatumia vipimo viwili tofauti kuhusiana na kadhia ya Palestina, kwa upande mmoja mataifa haya yanamtizama alienyan'ganywa ardhi yake na anaepambana kwa ajili ya kuikomboa anaonekana kua gaidi, kwa upande mwingine yule dhalimu alievamia ardhi na anaevunja haki na maadili ya kibinadamu kwa kutumia silaha kali na hatari, anaendelea kunwaga damu na anaeendelea kukataa desturi na maamuzi ya Umoja wa Mataifa; anaenekana kua yeye ndie mdhulumiwa anaejitetea.

Aidha, ni katika aina ya dhulma mbaya zaidi na ugaidi hatarishi kuusingizia Uislamu na kuupatia jina la ugaidi; Uislamu ni dini ya uadilifu na msimamo wa kati na kati, ni dhulma kubwa kabisa kuzipiga taasisi za kheri na da'wa na taasisi za fedha za kiislamu kwa kisingizio cha ugaidi bila ya kuwepo ushahidi wowote wa hilo.

Nne: Maadili (akhlaq) ya Kiislamu:

Hakika ya ulimwengu wa leo unahitajia zaidi akhlaq (maadili) za kiislamu katika mazingira ya Amani n ahata yale ya vita, ili irudi mizani ya uadilifu ambayo mbingu zote na ardhi zimesimama juu ya mizani hio, na kuachana na kile kinachoendelea leo duniani cha dhulma, jeuri na uharibifu (ufisadi). Kinachopelekea migogoro na fitna duniani ni haya mataifa makubwa

[1] Surat al-Anfal: 60

kutaka kuigawa dunia kwenye matabaka na wao kuendelea kufaidika na rasilimali za dunia kwa kutumia nguvu, mabavu na elimu ya teknologia waliyonayo ambayo kimsingi, Allah aliwajibisha elimu hio itumike kwa ajili ya kusimamisha haki na uadilifu kama alivyosema:

> "*Kwa hakika tuliwatuma Mitume wetu kwa dalili waziwazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na Mizani, ili watu wasimamie uadilifu, na tumeteremsha chuma chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu, na ili Mwenyezi Mungu amjue anaye mnusuru Yeye na Mitume wake kwa ghaibu*".[1]

Tano: 'Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu' linathamini kwa heshima hotuba muhimu iliyo na ufafanuzi ya Mstahiki 'Katibu Mkuu' wa 'Shirika la Nchi za Kiislamu' (OIC) iliyowasilishwa kwa niaba yake na Mstahiki 'Naibu Katibu Mkuu Msaidizi' wa mambo ya kisiasa na jamii za kiislamu zinazoishi nje ya nchi za kiislamu (Muslim minorities), iliyosema sehemu ya hotuba hio:

"*Hakika ya kikao chenu hiki kitukufu kinafanyika katika mazingira magumu na tete, changamoto zinazotukabili zinazidi kua kubwa kuliko wakati mwengine wowote, uvamizi na uadui unaoendelea leo dhidi ya umma unahatarisha uwepo wetu na unatuweka kwenye hali ya kiza, jambo ambalo inatulazimu kuungana na kua kitu kimoja na kuunganisha safu zetu na kuazimia kusimama kidete serikali na raia kulinda ardhi zetu tukufu na rasilimali zetu.*

Nyinyi ni mashuhuda wa kiwango cha kiburi na jeuri kilichopo kwa huyu adui wa kizayuni na utashi wa kiwazimu wa kutenda maovu na kuzidisha uadui unaongezeka kwake yeye, adui huyu (Israel) analiweka eneo lote (la mashariki ya kati) kwenye ukingo wa kulipuka na kuibuka vita hatarishi za kuua halaiki ya watu zinazoelekezwa dhidi ya mashujaa wa Kipalestina, yote hayo kwa ajili ya kushibisha utashi wao wa dhulma na kiburi huku wakiendelea kupata usaidizi kutoka mataifa makubwa (Amerika na Ulaya) wa kijeshi, kiuchumi na kisiasa bila masharti yoyote.

Tukiachana na Palestina, kuna vita vingine vikali kabisa na vya mda mrefu vinavyoendelea sasa katika nchi nyingine ya Kiislamu ya Afghanistan iliyosibiwa vyenye malengo yasiyoeleweka, wamekufa maelfu na malukuki ya wasiokua na hatia

[1] Surat al-Hadid: 25

miongoni mwa wanawake, watoto na watu wazima.

Hivyo basi; ni katika majukumu yenu kiusomi na kitaaluma kuuhami utu wa kiislamu dhidi ya changamoto za kigeni zinazochangiwa na miondoko ya kisiasa ya kimataifa, kazi zenu hizi mnazozifanya zinasaidia kwa kiwango kikubwa katika kutengeneza maoni ya umma (public opinion) na kuwajengea umma uwezo wa kifikra na kudhatiti ujinasibishaji wao juu ya utamaduni (ustaarabu) wa kiislamu wa asili ambao mizizi yake ni imara kabisa na katu haiwezi kusumuliwa licha ya ukali wa vichapo vinavyowashukia umma wa kiislamu, hii ni kwa sababu kumuongoza binadamu kiaqeeda na kielimu ni jambo la msingi kuliko mambo mengine; na msingi huu ndio unaoleta mshikamano wa umma na mustakbala wake. Kwa kulizingatia hili, inapaswa jambo hili lipewe nafasi ya juu inayostahiki na kazi zinazoibuka hapa zizae matumaini kivitendo, kulisimamia jambo hili ni mojawapo ya mafanikio makubwa kwa ustaarabu wa kiislamu na kupelekea waislamu kuamka upya".

Wabillah al-Taufiq

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 126 (8/13)

Yanayohusiana na 'Haki za Binadamu Katika Uislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tatu (13) kilichofanyika nchini Kuwait 7 - 12 Shawwal (Mfungo Mosi), 1422, sawa na 22 - 27 Disemba, 2001.

Kutokana na imani kua Allah SWT ndie aliempatia binadamu heshima na utukufu ambao ndio msingi wa haki na uwajibikaji, aidha Amemuekea binadamu haki ambazo ni za mola wake na haki nyingine ambazo ni za zake yeye binafsi na haki nyingine ni za binadamu wenzake na nyingine ni za mazingira yanayomzunguka, kwa mtazamo mpana wa kina na huru wa sharia ya kiislamu utamfanya mtu ajiyakinishe juu ya suala la ubora wa uislamu na ufaaji wake kwa jamii ya kibinadamu yote na kwamba uislamu unaendana na kuwiana vizuri na maumbile ya binadamu na dunia, na ni kwa maana hii ndio uislamu unaitwa: "*Dini ya Maumbile*", kama inavyoshadidia Qur'an:

> "*Basi uelekeze uso wako katika dini iliyo sawasawa — ndilo umbile Mwenyezi Mungu Alilowaumbia watu; (yaani dini hii ya Kiislamu inawafikiana barabara na umbo la binadamu)*".[1]

Hivyo basi; haki za binadamu katika uislamu ni *takrima* zilizotokana na heshima ya Allah aliyomtunuku binadamu na akawalazimisha binadamu wote kuziheshimu kwa mujibu wa vigezo na masharti ya kisharia.

Ni kutokana na imani kua *ijma* (itifaki) ya umma wa kiislamu kwamba sharia ya kiislamu ni yenye kufaa zama zote na sehemu zote, na kuamini kua watu wana haki ya kulinda nyenzo zao za kitamaduni (ustaarabu) na kidini zinazowahusu, aidha ni haki ya kila jamii na kila umma kujitawala kwa nidhamu na mifumo wanayoiridhia wao, kutokana na yote hayo

[1] Surat al-Rum: 30

yaliyotangulia; ‘Kongamano’ linapenda kuweka msisitizo juu ya yale yaliyoazimiwa kwenye ‘*Tamko la Cairo*’ linalohusiana na ‘haki za binadamu katika uislamu’ lililotolewa na ‘Kongamano la Mawaziri wa Mambo ya Nje Wa Nchi za Kiislamu’ tarehe 14 Muharram (Mfungo Nne), 1411 Hijria, sawa na 5 Agosti, 1990, na ilani iliyotolewa na ‘Warsha ya Haki za Binadamu’ iliyofanyika chini ya mwavuli wa ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu’ Jeddah 8 – 10 Muharram (Mfungo Nne), 1417 Hijria, sawa na 25 – 27 Mei, 1996.

Kwa kua jamii za kiislamu zimekubali na kujilazimisha nazo kwa utiifu na mapenzi kutekeleza na kufuata nidhamu na sharia ya kiislamu katika mambo binafsi, mambo ya wanawake, mahusiano ya kifamilia na mengineo miongoni mwa nyanja za kijamii na kiuchumi. ‘Ilani ya Kimataifa ya Haki za Binadamu’ ya Umoja wa Mataifa mwaka 1948 inakubaliana (inawafikiana) kwenye sehemu nyingi za ilani ya haki za binadamu katika uislamu, inawafikiana kwenye madhumuni yake na malengo yake, lakini pia inakhtalifiana katika sehemu nyengine hususan kwenye mas’ala ya akhlaq (maadili) na nidhamu (mfumo) ya kijamii inayojiegemeza na dini ya kiislamu.

Kwa kua sharia ya kiislamu imepitisha hukmu zinazolinda na kuhifadhi malengo makuu kwa binadamu, muhimu katika hayo ni yale yanayojulikana kama ‘*Malengo makuu matano*’ ambayo yamelinda haki za kimsingi za binadamu katika kulinda nafsi yake, dini (imani) yake, mali yake, heshima yake na akili yake. Aidha, sharia ya kiislamu inatibu aina zote za miporomoko na mapindo kwa kuweka taratibu kabambe za kinga na kukemea kwa kusudio la kuihifadhi jamii na kurekebisha upotoshaji, ijulikane kua ‘taratibu za kinga na kukemea’ zipo na zinapatikana katika kila sheria na kanuni zama zote na sehemu zote, taasisi nyingi na makongamano ya kimataifa yamekiri ubora wa sharia ya kiislamu na uwezo wake mkuu katika kutatua na kurekebisha matatizo ya binadamu; jambo ambalo linawalazimu wenye akili, hekima na busara kulitilia maanani na kufaidika na yaliyomo kwenye sharia.

Kwa kua ‘Mkataba wa Umoja wa Mataifa’ umeainisha bayana; haki ya kila nchi kujitawala ndani ya mipaka yake ya kijiografia na kuzuia nchi kuingilia

mambo ya ndani ya nchi nyengine, na kwa kua sheria mahsusi za nchi huru hazikubali mifumo au sheria za kigeni;

Hivyo basi; imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Mashirika ya Kimataifa mbalimbali yanayojihusisha na haki za binadamu duniani yanatakiwa kutoingilia nyanja zinazohusu 'Sharia ya Kiislamu' zinazotawala maisha ya waislamu, na ijulikane kua mashirika haya hayana haki ya kulazimisha waislamu kufuata nidhamu na maadili ya mashirika hayo zinazokhtalifiana na sharia za waislamu na maadili yao, na kamwe haijuzu kuwahukumu waislamu kwa kanuni ambazo waislamu wenyewe hawaridhiki nazo.

Mbili: Kuanzishwe 'Kituo cha Haki za Binadamu' chini ya mwavuli wa 'Kongamano' na ziwekwe taratibu zote stahiki za uanzishwaji huo pamoja na kuweka nidhamu na kanuni za uendeshaji.

Aidha, Kongamano linausia yafuatayo:

Moja: 'Kongamano' linazitaka nchi na mashirika ya kimataifa na ya kibinadamu kujizatiti katika kuheshimu haki za wachache (jamii za kiislamu nchi nyengine) katika nchi mbalimbali na kuwatendea haki hasahasa katika nyakati hizi ngumu ili kufikia malengo ya uadilifu na kumpatia kila mwenye haki, haki yake.

Mbili: 'Kongamano' linaweka bayana, utayari wake wa kuwasiliana wataalamu wa mambo ya sheria (kanuni), mashirika na taasisi za kielimu za kimataifa, taasisi rasmi na za binafsi katika nyanja zote na mirengo yote ili kudurusu na kuangazia njia muafaka za maelewano na mashirikiano juu ya nyanja za haki za binadamu kwa namna ambayo italeta usalama, uadilifu, mshikamano na maisha bora, aidha kuondoa ufisadi na kusimamisha upendo na uwiano wa kijamii kwa mujibu wa misingi iliyotangulia kutajwa. Iwe nembo yetu katika hili ni neon la Allah aliposema:

"*Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani (wema), na kuwapa jamaa; na anakataza uchafu, na uovu, na dhulma. Anakuwaidhini ili*

mpate kukumbuka".[1]

Aidha, tujikumbushe na tamko lake Mtume Muhammad SAW alilolitowa siku ya Hijja yake ya mwisho akiwa Makkah (*Hijjat al-Wadaa'*) pale aliposema:

"إنّ دماءكم وأموالكم وأعراضكم حرام عليكم كحرمة يومكم هذا في شهركم هذا في بلدكم هذا"

"*Hakika ya mali yenu, heshima zenu, zimepewa utukufu wa kulindwa kama vile ilivyotukuka siku yenu yenu hii katika mwezi huu ndani ya mji huu*"

Wabillah al-Taufiq

[1] Surat al-Nahl: 90

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Kumi na Nne (14) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Doha, Dola ya Qatar

8 - 13 Dhul-Qa'ada (Mfungo Pili), 1423

11 - 16 Januari, 2003

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 127 (1/14)

Yanayohusiana na 'Kadi za Mashindano'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nne (14) kilichofanyika Doha, Qatar 8 - 13 Dhul-Qa'ada (Mfungo Pili), 1423, sawa na 11 - 16 Januari, 2003.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kadi za Mashindano,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Fasili ya Mashindano: Mashindano mi muamala wa ushindani baina ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kufikia jambo fulani; ima kuwepo zawadi kwa mshindi au bila zawadi.

Mbili: Uhalali wa Mashindano:

1) Mashindano bila ya uwepo wa zawadi kwa mshindi ni halali (yanajuzu) kwa kila jambo ambalo hakuna katazo la kuharamisha na wala halina athari ya mtu kuwacha jambo la wajibu au kuangukia kufanya jambo la haramu.
2) Mashindano yanayowekewa zawadi kwa mshindi yanajuzu kwa masharti (vidhibiti) yafuatayo:

    a) Yawe malengo, njia na nyanja za mashindano husika ni halali.
    b) Isiwe zawadi imechangiwa na washiriki wa mashindano yenyewe.
    c) Mashindano yasaidie kufikia lengo miongoni mwa malengo yanayokubalika kisharia.
    d) Mashindano husika yasipelekee kuwachwa jambo la wajibu au kuangukia kufanywa jambo la haramu.

Tatu: Haijuzu kwa kadi (kuponi) za mashindano ambazo kima chake au sehemu ya kima chake kinaingia kwenye kutengeneza zawadi, hii itakua ni aina ya Kamari.

Nne: Kubeti baina ya pande mbili au zaidi kwa matokeo ya mashindano yanayotendwa na wengine katika mambo ya *madia* (material) au *maanawia* (immaterial) ni haramu kwa ushahidi wa aya na ahadith mbalimbali zilizokuja kuharamisha Kamari.

Tano: Kulipia mazungumzo ya simu ili kuingia kwenye mashindano si halali kisharia ikiwa sehemu ya malipo hayo au malipo yote yanakwenda kwenye kima cha zawadi, ili kuzuia ulaji wa mali ya wengine kwa dhulma (batili).

Sita: Hamna katazo kwa wanaotoa zawadi kwa minajili ya kutangazia bidhaa zao tu – bila kufaidika kifedha na zoezi hilo – kwa kufanya mashindano yanayoruhusiwa, ila kwa sharti isiwe kima cha zawadi hizo au sehemu yake kimetokana na washindanaji, aidha kusiwepo ghushi (hadaa) au khiana ya aina yoyote katika utangazaji huo wa bidhaa kwa watumiaji (wanunuzi).

Saba: Haijuzu kisharia; kupandisha kiwango cha zawadi au kuteremsha kwa hasara inayojitokeza kwa aliefuzu (alieshinda).

Nane: Inajuzu kwa kadi za mahoteli, mashirika ya ndege na mashirika mengine zinayowapatia wateja wake nukta (points) zinazowawezesha kuchuma faida (manufaa) yalio halali kisharia, kwa sharti ya nukta hizo ziwe zinatokewa bila malipo, ikiwa kuna malipo ya kupata nukta hizo basi haijuzi, kwani itakua ni udanganyifu.

Inausiwa yafuatayo:

‘Kongamano’ linapenda kuwausia waislamu wote kusisitiza halali katika miamala yao na shughuli zao za kifikra au za kimapumziko, na kujiepusha kabisa na israfu na ubadhirifu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 128 (2/14)

Yanayohusiana na 'Haki za Binadamu na Unyanyasaji wa Kimataifa'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nne (14) kilichofanyika Doha, Qatar 8 - 13 Dhul-Qa'ada (Mfungo Pili), 1423, sawa na 11 - 16 Januari, 2003.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Haki za Binadamu na Unyanyasaji wa Kimataifa,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Uislamu unamuheshimu (unamtukuza) binadamu kwa ubinadamu wake, na unajihusisha sana kumlindia haki zake na kuchunga utukufu wake, Fiqh ya kiislamu ni fiqhi (kanuni) ya kwanza duniani iliyokuja na sheria za ndani na za kimataifa zinazolinda mahusiano ya binadamu kwenye mazingira ya Amani na hata yale ya vita.
2) Ugaidi: ni kufanya uadui au kutia khofu au kutishia watu *madia* (material) au *maanawia* (immaterial), nisawa jambo hili lifanywe na dola au vikundi au mtu binafsi, kumfanyia binadamu kwenye dini yake au nafsi yake au heshima yake au akili yake au mali yake pasina haki; kwa njia yoyote miongoni mwa aina za ufisidifu katika ardhi (dunia).
3) 'Kongamano' linapenda kuweka msisitizo kua kupigania kwa njia ya *jihad* na kufa *shahidi* kwa ajili ya kulinda na kueneza *aqeeda* ya uislamu na kulinda heshima na nchi za kiislamu sio ugaidi bali ni kutetea na kulinda haki za msingi, kwa hio ni haki ya watu waliodhulumiwa haki zaoau waliovamiwa ardhi (nchi) zao kutafuta njia zozote na mbinu zozote zinazowezekana kupigania uhuru wao.
4) Kuainisha ufahamu halisi wa misamiati maalum kama vile: *jihad*, *ugaidi* na *vurugu* (violence) ambayo imezoeleka kutumika kwenye

vyombo vya mawasiliano-habari mbalimbali, ijulikane kua hii ni misamiati ya kielimu, haifai kuyatumia vibaya au kwa malengo mabaya na kutoa taswira isiyokua halisi.

5) Ama hukmu ya mtu kujizamisha ndani ya safu ya maadui – akiwa amevaa mikanda ya kujilipua – ‘Baraza limeonelea kuakhirisha hadi kikao kijacho *inshaallah* ili tafiti za ziada zifanyike.

Linausia yafuatayo:

1) ‘Kongamano’ linausia juu ya ulazima wa kuandaa saiklopidia ya kiislamu juu ya kanuni ya kimataifa ya kibinadamu sambamba na saiklopidia nyengine zijulikanazo katika kanuni, alafu saiklopidia hii itafsiriwe kwenye lugha kuu mbalimbali duniani, na iwekwe kwenye maktaba (library) za vyuo vikuu duniani na katika mashirika ya Umoja wa Mataifa, kufanya hivi kutasaidia kukubwa sana kuliko kuendelea kupiga kelele kua: *uislamu hautambui ugaidi*, ili wapate kufahamu wasiokua waislamu kwa uwazi usiokua na utata nafasi halisi ya uislamu juu ya suala hili.
2) Aidha, ‘Kongamano’ linausia kuundwe kamati maalum ya wataalamu ili waandae ‘Katiba ya Kiislamu’ itakayobainisha kwa uwazi mtazamo wa kiislamu juu mahusiano na wasiokua waislamu, katiba hii baadae itafsiriwe katika lugha za kimataifa zijulikanazo na isambazwe kupitia vyombo vya habari mbalimbali, hii itakua ni mojawapo ya njia za kukanusha uongo mwingi unaosambazwa dhidi ya uislamu halikadhalika kuweka wazi ukweli wa kiislamu kwa wasiokua waislamu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 129 (3/14)

Yanayohusiana na 'Mikataba ya Ukandarasi na Ujenzi: Uhalisia wake, Kukubalika kwake na Aina zake'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nne (14) kilichofanyika Doha, Qatar 8 - 13 Dhul-Qa'ada (Mfungo Pili), 1423, sawa na 11 - 16 Januari, 2003.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Mikataba ya Ukandarasi na Ujenzi: Uhalisia wake, Kukubalika kwake na Aina zake,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na kuzingatia dalili za kisharia na misingi yake na makusudio yake, na kuzingatia maslahi mapana ya jamii kwenye mikataba na miamala, na kwa kutizama umuhimu wa 'Mikataba ya Ukandarasi' na nafasi kubwa katika kutanashati viwanda na kufungua nyanja pana za ugharamiaji na kukuza uchumi wa kiislamu;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Mkataba wa Ukandarasi: Ni mkataba ambao, kwa mujibu wake, moja wa pande mbili anakubali (kuahidi) kutengeneza kitu au kutekeleza kazi fulani kwa malipo ambayo upande wa pili umekubali (umeahidi), mkataba huu unajuzu; nisawa awe mkandarasi ametekeleza kazi na vifaa, mkataba huu aidha unajulikana kwa wanafiqihi: *istisnaa'*, au awe mkandarasi ametekeleza kazi; mkataba huu unajulikana kwa wanafiqihi: *ijara (malipo) ya kazi*.
2) Iwapo mkandarasi anatekeleza kazi pamoja na vifaa (mali ghafi), basi 'Maamuzi ya Kongamano' namba 65 (3/7) yanayohusiana na *istisnaa'* yatatumika.
3) Ama ikiwa mkandarasi atatekeleza kazi pekee, basi malipo ya *ijara* ni lazima yajulikane.
4) Inajuzu kukubaliana kwa kuainisha thamani ya malipo kwa njia

zifuatazo:

a) Kukubalina thamani ya malipo kiujumla kwa misingi ya nyaraka za uzabuni, michoro ya ramani na maelezo-ainishi kwa uwazi kabisa.
b) Kukubalina kuainisha thamani ya malipo kwa misingi ya vipande vipande, kila kipande kinakua na thamani watakayokubaliana kwa idadi ya vipande vyote kwa mujibu wa michoro, ramani na dizaini.
c) Kukubalina kuainisha thamani ya malipo kwa misingi ya bei ya gharama halisi, na kuongezea kiwango cha faida kwa asilimia (%), katika hali hii itamlazimu mkandarasi aweke maelezo yake bayana na aambatanishe mifumo ya kifedha na kazi iliyoainishwa pamoja na gharama zote na malipo yake, ziwasilishwe kwa mhusika wa mkataba, hapo atastahiki malipo ya gharama pamoja na kiwango chake cha faida walichokubaliana.

5) Inajuzu kuweka sharti la adhabu (faini) kwenye mkataba wa ukanadarasi, kwa mujibu wa walivyokubaliana pande zote mbili iwapo hakutakua na sababu za nje ya uwezo wao, katika hali hii ‘Maamuzi ya Kongamano’ namba 109 (3/12) yanayohusiana na sharti la adhabu (faini); yatatumika.
6) Inajuzu kwenye mkataba wa ukanadarasi, kuchelewesha malipo au kulipa polepole kwa awamu zilizoainishwa au kwa mujibu wa ukamilishaji wa kila awamu walivyokubaliana.
7) Inajuzu kukubaliana kufanya marekebisho au nyongeza kwenye mikataba.
8) Iwapo mkandarasi amefanya marekebisho au nyongeza kwa idhini ya ‘*mwenyekazi*’ bila ya kukubaliana malipo; ni haki ya mkandarasi kupewa malipo yanayolingana (yanayowiana) na nyongeza hizo.
9) Iwapo mkandarasi amefanya marekebisho au nyongeza bila ya makubaliano kufanya hivyo; basi hatostahiki malipo ya ziada wal hatostahiki malipo ya marekebisho hayo na nyongeza alizozifanya.
10) Mkandarasi atawajibika kulipa kasoro na makossa alizosababisha iwapo amechupa au amezembea au amekhalifu masharti ya mkataba, lakini hatowajibika kwa kasoro zitakazosababishwa na *mwenyekazi* au zitakazotokea kwa sababu za nje ya uwezo wake (*force majeure*).

11) Iwapo *mwenyekazi* amemshurutisha mkandarasi aifanye kazi yeye binafsi, basi haijuzu kwa mkandarasi huyu kukubaliana na mkandarasi mwengine (*sub-contractor*).
12) Iwapo mwenyekazi hakumshurutisha mkandarasi kuifanya kazi yeye binafsi, basi inajuzu kwa mkandarasi huyu kukubaliana na mkandarasi mwengine (sub-contractor), ila ikiwa kazi husika ni lazima itekelezwe na mkandarasi wa asili kwa sifa alizonazo, ubora wa kazi hio ungeshuka lau itafanywa na mtu mwengine.
13) Mkandarasi wa asili atawajibika kwa kazi za wakandarasi (sub-contractors) wake, aidha atawajibika mbele ya *mwenyekazi* kwa mujibu wa mkataba.
14) Haikubaliki kwenye mkataba wa ukandarasi kuweka sharti la kumuondoshea mkandarasi; uwajibikaji.
15) Inajuzu kuweka sharti la uwajibikaji kwa kipindi-ainishwa fulani.
16) Haikubaliki kwenye mkataba wa ukandarasi kuweka sharti la kutowajibika kwa kasoro zitakazojitokeza ndani ya kipindi cha *dhamana* kilichoainishwa kwenye mkataba.

Inausiwa yafuatayo:

‘Kongamano’ linausia kudurusu baadhi ya *lugha* na *misamiati* ya ‘mikataba ya ukandarasi’ kama ile inayoitwa (B.O.T) yaani: Jenga, Miliki, Tawala na Hamisha umiliki (J.M.T.H).

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≃≃≃

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 130 (4/14)

Yanayohusiana na 'Makampuni ya Kisasa: Kampuni za 'Holding' na Nyenginezo na Hukmu zake Kisharia'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nne (14) kilichofanyika Doha, Qatar 8 - 13 Dhul-Qa'ada (Mfungo Pili), 1423, sawa na 11 - 16 Januari, 2003.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Makampuni ya Kisasa: Kampuni za 'Holding' na Nyenginezo na Hukmu zake Kisharia,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Fasili ya 'Kampuni za Kisasa':

1) Kampuni za Fedha: Ni mashirika (kampuni) yanayotegemea kuasisiwa kwake na uundwaji wake kwa '*rasilimali za washirika*' bila kujali utu unaojitegemea wa mwenyehisa, hisa za kampuni hizi zinakubali mzunguko, kampuni hizi zinagawika aina zifuatazo:

    a) 'Kampuni ya Ushirikiano wa Hisa' (*joint stock company*): Nayo ni kampuni ambayo rasilimali zake zinagawanywa kwenye hisa sawa zinazokubali mzunguko, na kila mshirika anawajibika kwa kiwango cha hisa zake kwenye rasilimali.
    b) 'Kampuni yenye Ukomo wa Ushirikiano wa Hisa' (*company limited by shares*): Nayo ni kampuni ambayo rasilimali zake zimetokana na hisa zinazokubali mzunguko, na washirika wa kampuni hii wako aina mbili: (1) washirika walioshikamana pamoja na wanawajibika kwa pamoja juu ya dhamana na madeni ya kampuni (2) washirika-bubu (*silent partners*) ambao mas'uli yao ni kwa kadiri ya hisa zao.

c) ‘Kampuni ya Dhima Ndogo’ (Kampuni ambayo wamiliki wake hawawajibiki kama watu binafsi kulipa deni la kampuni - *limited liability company*): Nayo ni kampuni ambayo rasilimali zake zinamilikiwa na idadi ndogo ya watu (idadi inategemea na sheria za kila nchi), uwajibikaji wa kila mshirika unategemea kiwango cha hisa za kila mtu kwenye rasilimali, na hisa za kampuni hii hazikubali mzunguko.

2) ‘Kampuni ya Ushirika Binafsi’ (*Personal association company*): Nazo ni kampuni ambazo uwepo wake ni watu-washirika wake wanaojuana na wanaoaminiana; kampuni hizi ziko aina tatu:

a) ‘Kampuni ya Dhima ya Pamoja’ (*joint liability company*): Nayo ni kampuni inayoanzishwa na watu wawili au zaidi kwa lengo la kufanya biashara, kila mshirika atatoa kiwango kiwango chake cha rasilimali, kwa pamoja watakua mas’uli kwenye mali yao na madeni wanaodaiwa, kampuni hii huanzishwa kimsingi kwa kujuana miongoni mwa washirika.
b) ‘Kampuni ya Ushirika Mdogo’ (*limited partnership company*): Nayo ni kampuni ambayo muasisi wake anakua na mshirika mmoja au zaidi, na kwa pamoja wanakua mas’uli, na baina ya mshirika mmoja au zaidi, kwa pamoja wanakua ‘*wenyehisa*’ walio nje ya uongozi, wanaitwa *washirika waliousia*, mas’uli yao yanaendana na kiwango cha hisa zao kwenye rasilimali.
c) ‘Kampuni ya Ushirika Maalum’ (*particular partnership company*): Nayo ni kampuni isiyoonekana; isiyo na utu wa kikanuni, inakua baina ya watu wawili au zaidi; kila mmoja anakua na hisa zake zinazojulikana kwenye rasilimali, wanakubaliana miongoni mwao kugawana faida na hasara zinazotokana na shughuli za kibiashara; moja au zaidi zinazoendeshwa na washirika hao au mmoja wao kwa niaba yake binafsi, Uwajibikaji unakua wa kadiri kwa yule anaesimamia au anaeendesha shughuli.

3) ‘Kampuni Milikishi’ (*holding company*): Nayo ni kampuni ambayo inamiliki hisa katika rasilimali za kampuni au kampuni nyengine zinazojitegemea; kwa kiwango kinachoiwezesha kisharia (kikanuni)

kudhibiti uongozi wa kampuni hizo na kuziwekea mipango-kazi.

4) ‘Kampuni ya Kimataifa’ (*multinational company*): Nayo ni kampuni inayomiliki makampuni kadha chini yake kama matawi, makao yake makuu yanapatikana katika nchi fulani lakini makampuni-matawi yake yanapatikana katika nchi mbalimbali, na kila kampuni-tawi inakua ni nchi ile iliyopo. Kampuni kuu inaungana na makampuni-matawi kupitia mikakati kamili ya kiuchumi inayolenga kufikia malengo-ainishwa ya kiuwekezaji.

Mbili: Kimsingi, inajuzu kuunda (kuasisi) makampuni bora tu yasiwe na mambo ya *muharramaat* (yalioharimishwa) na makatazo ya kisharia katika shughuli zake, iwapo asili ya shughuli zenyewe ni haramu kama vile benki za riba au makampuni yanayoamiliana na *muharramaat* kama biashara za *mihadarati*, biashara ya ngono na nguruwe; nisawa iwe miamala hii ndio biashara za msingi au ni sehemu ya biashara, basi kampuni zinakua ni haramu na haijuzu kabisa kumiliki au kufanya biashara ya hisa ndani yake. Aidha, ni lazima kuhakikisha kua kampuni hizi hazina miamala ya *gharar* (udanganyifu) au kutofahamika kunakopelekea migogoro, au uwepo wa sababu zozote zile zinazopelekea kubatilisha kampuni au kufisidisha kisharia.

Tatu: Ni haramu kwa kampuni kutoa hisa za starehe au hisa za upendeleo au hati za mikopo.

Nne: Endapo kumetokea hasara kwenye rasilimali basi italazimu kila mshirika kubeba mzigo wa hasara hio kwa mujibu wa hisa za kila mmoja wao kwenye rasilimali.

Tano: Mmiliki wa hisa kwenye kampuni anamiliki hisa zilizowazi katika milki za kampuni kwa kadiri na kiwango cha umiliki wake wa hisa. Umiliki wake huu unabaki kwake hadi pale utakapohamia kwa mwengine kupitia mojawapo wa sababu kama kujiondoa au kuhamisha umilikaji kwa mwengine.

Sita: Kuhusiana namna za kimahesabu ya zaka za hisa kwa washirika kwenye ‘*makampuni ya kupokea*’ (holding company) na makampuni ya

kimataifa (multi-national company), tunaomba kurejea ‘Maamuzi ya Kongamano’ namba 28 (3/4) ya kikao cha nne na maamuzi namba 121 (3/13) ya kikao cha kumi na tatu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 131 (5/14)

Yanayohusiana na 'Jukumu la Dereva wa Usafiri wa Umma katika Kuua Kimakosa na Fidia-Mchanganyiko'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nne (14) kilichofanyika Doha, Qatar 8 - 13 Dhul-Qa'ada (Mfungo Pili), 1423, sawa na 11 - 16 Januari, 2003.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Jukumu la Dereva wa Usafiri wa Umma katika Kuua Kimakosa na Fidia-Mchanganyiko,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha maamuzi juu ya maudhui haya ili kudurusu zaidi mas'ala ya kisharia yafuatayo na kuandaa tafiti kwa kila mas'ala:

1) Kuongezeka fidia kwa kuongezeka kuua.
2) Fidia-mbadala wanapokosekana familia ya muuaji au wanaposhindwa kulipa fidia.
3) Kumnyima mirathi; muuaji kimakosa.

Wabillah al-Taufiq

≃≃≃

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 132 (6/14)

Yanayohusiana na 'Mikataba ya Utekelezaji (*Adhesion contracts*)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nne (14) kilichofanyika Doha, Qatar 8 - 13 Dhul-Qa'ada (Mfungo Pili), 1423, sawa na 11 - 16 Januari, 2003.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Mikataba ya Utekelezaji (*Adhesion contracts*),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) 'Mikataba ya Utekelezaji' (*Adhesion contracts*); ni msamiati wa kikanuni mpya wa kimagharibi unaohusika na mikataba ambayo inadhibitiwa na vigezo nan a masharti yafuatayo:

    a) Ufungamano wa mkataba na bidhaa au manufaa (huduma) za msingi wanazozihitajia watu wote na hawana budi nazo (hawawezi kuzikusoa) kama vile maji, umeme (stima), gesi, simu, posta, usafiri wa umma na kadhalika.
    b) Kuhodhi hizo bidhaa au huduma au vitendea kazi kunakokubalika kisheria, au tuseme kuzidhibiti kwa namna ambayo inapunguza ushindani wa kibiashara.
    c) Kubaki upande wa utoaji huduma-tajwa kua ni wa pekee nay eye ndie awekae masharti na vipengele vya mkataba, bila ya kutoa nafasi kwa upande wa pili kuhoji au kupunguza masharti au kurekebisha.
    d) Ofa ya mauzo inatoka upande mmoja ikielekezwa kwa raia; masharti na vigezo ni hayohayo kwa wote na kwa njia endelevu.

2) 'Mkataba wa Utekelezaji' unafungwa kwa kupatana pande mbili za

mtoa huduma na mteja kwa namna inayojulikana kikawaida yaani ridhaa ya pande mbili kuingia kwenye mkataba huo kwa mujibu wa masharti na vigezo yaliyowekwa na mtoa huduma bila ya kushurutisha kutamka au kuandika au mfano wake.

3) Kwa uwepo wa uwezekano wa upande unaohodhi (kikanuni) bidhaa/huduma hizi kua na umiliki (udhibiti) wa bei na masharti anayoyaweka kwenye mikataba ya utekelezaji kwa namna ambayo inaweza kupelekea kuwabana (kuwabinya) watu na kuwadhuru, basi inalazimika kwa 'Mkataba wa Utekelezaji' ipitishwe (iidhinishwe) na serikali kabla haijateremshwa kwa watu kuikubali ili serikali iidhinishe kile kilichokua ni haki na uadilifu, na ikibidi irekebishe kile ambacho ni dhulma kwa '*Mtekelezaji*' kwa mujibu wa matakwa ya uadilifu kisharia.

4) 'Mikataba wa Utekelezaji' - kwa mtazamo wa kifiqihi - iko aina mbili:

Ya Kwanza: Ni ile ambayo thamani ya malipo ni ya uadilifu, na hamna masharti-kandamizi kwa mtekelezaji, mkataba aina hii ni sahihi kisharia na inalazimu pande zote mbili, na si ruhusa kwa serikali au mahkama kuiingilia katika mkataba huu kivyovyote vile kama kuufuta au kuurekebisha kwa kukosekana sababu ya kisharia kufanya hivyo, kwa kua upande unaohodhi bidhaa au huduma unazitoa na wala haujakataa kuuza kwa anaetaka kwa thamani inayolazimu kisharia ambayo inawiana na bidhaa/huduma yenyewe (Utata mdogo usioepukika na uliozoeleka kwa watu kusameheana kwenye vitu kama hivi, unasamehewa kisharia), na kwa kua kumuuzia upande mnyonge kwa bei ya uadilifu ni sahihi kwa itifaki ya wanazuoni.

Ya pili: Ni ile mikataba inayobeba vifungu-kandamizi (dhulma) kwa mtekelezaji, kwa kua thamani ya mauzo si ya uadilifu (kuna utata mwingi) au kuna masharti kandamizi yenye kuumiza (kudhuru), basi kwenye mkataba aina hii; serikali (mtawala) inatakiwa kuigilia mapema kabla mkataba huu kuidhinishwa, kwa kuweka bei-elekezi ya lazima ambayo itaondosha dhulma na dhara kwa watumiaji

(wanunuzi) ambao hawana budi na bidhaa/huduma hizo, na kushusha bei iliyo juu mpaka ifike mahali inapowiana na mfano wa bidhaa/huduma hizo, au kufuta au kurekebisha masharti kandamizi yaliyopo ili kuleta haki na uadilifu baina ya pande mbili; kufanya hivi ni kutokana na:

a) Serikali ina wajibu wa kisharia kuondosha madhara yanayotokana na mtu au kampuni kuhodhi bidhaa au huduma za msingi kwa watu, iwapo amekataa kuuzia raia kwa bei-adilifu (inayowiana na bidhaa/huduma), basi hapo serikali inawajibika kuweka bei-elekezi ya lazima ambayo italinda haki za pande zote mbili; haki ya watu (raia) kwa kuwaondeshea dhara (dhulma) inayotokana na *muhodhi* kuweka bei-kandamizi, lakini pia kulinda haki ya *muhodhi* kwa kumpatia bei mbadala adilifu.

b) Katika kuweka hii bei-elekezi ni kulinda maslahi ya umma - nayo ni maaslahi ya watu wasiokua na budi kuhitajia bidhaa/huduma hizo kwa thamani adilifu - juu ya maslahi ya wachache, yaani maslahi ya anaehodhi bidhaa/huduma za dharura anaedhulumu kwa kuwauzia wahitaji wa bidhaa/huduma hizo kwa bei kandamizi au kwa kuweka masharti dhalimu, inajulikana vyema katika misingi ya fiqihi kua: “Maslahi ya umma yanatangulizwa juu ya maslahi binafsi”, aidha, inajulikana kua: “Linabebwa dhara la wachache kuzuia dhara la umma”.

5) Inatofautishwa kwa hawa ‘Mawakala wa kipekee wa uagizaji’ (sole import agents) kwenye hali tatu:

Hali ya kwanza: Iwapo hakuna ulazima au dharura ya umma au ya watu wachache kuhitajia bidhaa/bidhaa ambayo inaagizwa tu na ‘*wakala wa kipekee*’ kwa kua bidhaa/huduma husika ni miongoni mwa bidhaa/huduma za kistarehe na si za kimsingi, inawezekana kuishi bila ya bidhaa/huduma hizo, au uko ulazima na dharura lakini si wa bidhaa/huduma- fulani kwa lazima kwa kua kunapatikana mbadala au zinazofanana sokoni kwa bei adilifu, basi kwa mazingira haya ni haki ya ‘wakala muagizaji’ auze kwa bei ambayo yeye na

mnunuzi wataridhika (watakubaliana) nayo, hapa serikali au mahkama hawana haki ya kuingilia au kuweka bei-elekezi, kwani msingi wa kusihi mikataba ni maridhiano baina ya pande mbili husika, na ulazima wa mikataba ni kile walichokubalina wawili kwa hiari yao, na kuhusika mwenye uwakala wa uagizaji wa bidhaa/huduma na kua na haki ya kuhodhi (kwa maana yake ya kilugha) inajuzu kisharia, kwani ni haki yake kuuza anachomiliki kwa bei inayomridhi, iwapo hakuna dhulma au dhara kwa umma, na kwa hali hii haifai kumuekea bei-elekezi.

Hali ya pili: Uwepo wa ulazima au haja ya umma au ya watu wachache ya bidhaa/huduma inayotaalikiana na '*wakala wa kipekee*' na akawa wakala huyu yuko tayari kuuza bidhaa/huduma hio kwa bei adilifu, hamna utata ndani yake wala udhibiti kandamizi, basi katika hali kama hii haifai kwa serikali kumuekea bei-elekezi, kwa sababu kuhusika kwake na kuhodhi bidhaa/huduma hio ni kazi halali katika anachomiliki, hajamdhulumu yeyote wala hajaleta dhara kwa watu wahitaji wa bidhaa/huduma hio, kwa hio asisumbuliwe.

Hali ya tatu: Uwepo wa ulazima au haja ya umma au ya watu wachache ya bidhaa/huduma inayotaalikiana na '*wakala wa kipekee*' na wakala huyu anauza bidhaa/huduma husika kwa bei-danganyifu au kwa masharti-kandammizi, basi katika hali kama hii ni wajibu wa serikali kuingilia na kuondosha dhulma kwa raia wahitaji wa bidhaa/huduma hizo kwa kumuekea wakala huyu bei-elekezi ya lazima.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≃≃≃

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 133 (7/14)

Yanayohusiana na 'Malimbikizo Kwenye Taasisi za Fedha za Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nne (14) kilichofanyika Doha, Qatar 8 - 13 Dhul-Qa'ada (Mfungo Pili), 1423, sawa na 11 - 16 Januari, 2003.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Malimbikizo Kwenye Taasisi za Fedha za Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Taratibu zinazotumika kwenye '*taasisi za fedha za kiislamu*' za kutatua tatizo la '*malimbukizi*' ni tofauti na zile zinazotumika kwenye taasisi na benki za kawaida, benki za kawaida zinaamiliana kwa misingi ya faida (riba) iliyoharamishwa, kwa hio ni vyema kusisitiza uharamu wa faida za benki kwa mujibu wa yanayofuata:

a) **Kazi za benki za kawaida:** Ijulikane kua kanuni na sheria zanazosimamia shughuli za benki; zinaizuia benki kuingia nyanja za uwekezaji kwa misingi ya 'faida na hasara'. Benki zinachukua akiba (*deposits*) za wateja wake kwa msingi kua ni deni, na kujihusisha kazi zake – kama wanavyosema wanasheria na wanauchumi – kukopa na kukopesha kwa faida (riba), na kuandaa mazingira ya kuzikopesha akiba hizo kwa faida (riba).

b) **Uhusiano baina ya benki za kawaida na waweka akiba:** Muundo wa kisharia na ule wa kikanuni wa uhusiano baina waweka akiba na benki ni uhusiano wa kukopa ni sio uhusiano wa uwakala, na jambo hili ndilo linaloshikiliwa na kanuni na mifumo ya benki, hii ni kwa kua '*uwakala wa uwekezaji*' ni mkataba wa kufawidhi ambao unamfawidhi mtu mwingine

kuwekeza kiwango kadhaa cha fedha zinazomilikiwa muwakilishaji kwa malipo ya kazi yatakayoainishwa au kwa kiwango cha asilimia (%) cha mali (faida) ya uwekezaji, kwa hali hii wamekubaliana wanazuoni kwa *ijmaa* (kauli moja) kua muwakilishi hapa (mwenyemali) ndie mmiliki wa mali yaliyowekezwa, na faida ipatikanayo ni yak wake, kadhalika na hasara ataibeba yeye, ama wakala aliefawidhiwa kuwekeza atapata ujira (malipo) ulioainishwa kwenye 'mkataba wa uwakala' ikiwa ni uwakala wa malipo. Kwa maana hio haziwezi benki hapa kua ni '*mawakala wa wawekaji akiba*' kwenye kuwekeza mali yao, kwa kua waweka akiba hawa pindi wanapoweka mali kwenye benki za kawaida na wakahakikishiwa dhamana ya mali yao basi pesa hizo zinakua ni mkopo kwa benki ambapo benki ataruhusiwa (huru) kuwekeza pesa zile kwa njia yoyote anayotaka, kubwa kwake ni kuhakikisha kurejesha pesa hizo kwa mmiliki wake, ilivyo (kisharia) deni linarudishwa kama lilivyokua bila ya kushurutisha nyongeza (riba).

c) **Faida za benki za kawaida ni riba iliyoharamishwa kisharia:** Faida (nyongeza) za benki juu ya mali ya akiba ni riba iliyoharamishwa kisharia kwa mujibu wa *Qur'an* na *Sunnah*, na juu ya msimamo huu yameshikilia maamuzi na fatwa mbalimbali tangu '*Mkutaano wa Kiislamu wa Pili*' wa 'Taasisi ya Tafiti za Kiislamu' uliofanyika jijini Cairo (Misri) mwezi wa Muharram (Mfungo nne) 1385 Hijria (Mei 1965), mkutano ambao ulihudhuriwa na zaidi wanazuoni thamanini na tano (85) miongoni mwa wanazuoni wakubwa duniani, aidha, kwenye mkutano huu walikuwepo wawakilishi wa nchi za kiislamu thalathini na tano (35), iliamuliwa kwenye maamuzi namba moja kua:

"*Faida za aina zote za mikopo ni riba iliyoharamishwa*"

Baada ya hapo yakafuatia maamuzi na maazimio ya mikutano mbalimbali, ikiwemo:

- 'Mkutano wa kimataifa wa kwanza wa uchumi wa kiislamu' iliofanyika Makkah al-Mukarramah mwaka 1396 Hijria (1976), uliohudhuriwa na zaidi wanazuoni mia tatu (300) wakiwemo miongoni mwao wanafiqihi na wataalamu wa mambo ya uchumi na mabenki,

mkutano huu ulisisitiza uharamu wa faida (riba) za benki.

- ‘Mkutano wa pili wa benki za kiislamu’ uliofanyika Kuwait 1403 Hijria (1983) nao ukasisitiza jambo hilohilo.
- ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), katika kikao chake cha pili kilicofanyika jijini Jeddah (Saudi Arabia) Rabiul-Thani (Mfungo saba) 1406 Hijria (Disemba, 1985) katika maamuzi yake namba 10 (10/2) yaliyosema:

> “*Nyongeza yoyote au ziada juu ya deni lililofika wakati wake wa kulipwa lakini mdaiwa akashindwa kulipa hio nyongeza, au nyongeza yoyote juu ya mkopo inayotakiwa kulipwa mwanzo wa ‘Mkataba wa Mkopo’ basi aina mbili hizi tajwa ni ‘Riba’ iliyoharamishwa ki-sharia*”.

- ‘Kongamano la Fiqhi ya Kiislamu’ lilio chini ya ‘Muungano wa Ulimwengu wa Kiislamu’ (Muslim World League) Makkah al-Mukarramah, lilisisitiza kwenye kikao chake cha tisa (9) kilichofanyika mwaka 1406 Hijria (1986) kua: “*Kila kinachopatikana kwa njia ya faida za riba ni mali ya haramu kisharia*”.
- ‘Kamati ya Fatwa ya al-Azhar’ nayo: “*ilisisitiza uharamu wa faida za hati za uwekezaji (a,b) kwa kua huo ni mlango kukopesha kwa faida, na kukopesha kwa faida ni riba, na riba ni haramu*”.
- Fatwa ya Mstahiki Mufti – wa wakati huo – Sheikh Dr. Muhammad Sayid Tantawi ya mwezi wa Rajab, 1409 Hijria (Februari, 1989), ikishadidia kua: “*Kuweka pesa benki au kuwakopesha au kukopa kutoka kwao kwa namna yoyote ile ambayo itavutia faida iliyoainishwa mwanzoni, ni haramu*”.

Ukiongeza juu ya yote hayo yaliyotangulia; bado zipo fatwa nyingi tu kutoka taasisi za kielimu mbalimbali, kama vile: ‘Makongamano ya Kifiqhi’ katika nchi mbalimbali za kiislamu, ‘kamati za fatwa’, warsha za kielimu, mikutano ya kielimu, fatwa za wanazuoni wabobezi wenye *tahasusi* ya uchumi na shughuli za mabenki katika ulimwengu wa kiislamu; fatwa zote hizo zimesisitiza juu ya suala hili kwa namna ambayo imepatikana *ijmaa* ya zama hizi ya kuharamisha faida (riba) za benki na haijuzu kuikhalifu *ijmaa* hii.

d) Kuainisha faida ya uwekezaji kwa kiwango cha pesa fulani au kwa asilimia ya rasilimali mwanzoni: Ilivyo ni kwamba: ‘mkataba wa kukopesha kwa faida’ ni tofauti na ule wa ‘mkataba wa mudharaba wa kisharia’, ya kwanza: faida na hasara ni za mkopaji, ama kwenye mudharaba ni kushirikiana kwenye faida na hasara itokeapo, hii ni kwa mujibu wa alivyosema Mtume SAW:

"الخراج بالضمان"

"*Faida iendane na kudhamini mambo-hatarishi (ujasiri)*"[1]

Yaani kinachopatikana miongoni mwa faida, nyongeza na ziada, inakua ni halali kwa yule aliekua tayari (jasiri) kubeba hasara, kutilifika na kubovuka, lau zingetokea, na hapa ndipo wanazuoni walipotohoa ile qaida (msingi) yao ya kifiqhi iliyo mashuhuri inayosema: "*Faida kwa aliegharimika*" (الغُنم بالغُرم), aidha Mtume SAW "Amekataza faida isiyodhaminiwa hasara".[2]

Ipo *ijmaa* ya wanazuoni wa madhehebu yote kwa karne zote zilizotangulia ya kua: "haijuzu kuainisha kiwango cha faida za uwekezaji kwenye mudharaba au miamal mingine kwa pesa fulani au kwa asilimia ya mali yanayowekezwa (rasilimiali), kufanya hivyo ni kujihakikishia faida ndani ya rasilimali na hii ni kinyume na maelekezo ya sharia na dalili zilizo sahihi, na inaweza kupelekea kuvunja ushirikiano wa faida na hasara ambao ni msingi wa miamala ya ushirikiano na mudharaba. *Ijmaa* hii imethubutu na kuungwa mkono bila ya kupingwa na yeyote anayejulikana, na juu ya hili anasema ‘Ibn Qudama’ kwenye kitabu chake cha al-Mughni (3/43): "*Wanazuoni wanaojulikana wote wamekubaliana (ijmaa) juu ya kubatilisha muamala wa mudharaba anaposhurutisha mmoja wao au wote wawili pesa maalum*". *Ijmaa* hii ni dalili inayojitosheleza.

‘Kongamano’ hili linapenda kushadidia ijmaa hii na kuwausia waislamu kote duniani kukubali chumo la halali pekee na wajiepushe na chumo la

[1] Imepokewa na Imam Ahmad na Maimamu wengine kwa sanad iliyo sahihi.
[2] Imepokewa na Maimamu wa *Sunan* (Abudaud, Nasaai, Tirmidhi na Ibn Majah).

haramu, ishara ya utiifu wao kwa Allah SWT na Mtume wake SAW.

Mbili: Madeni yanayochelewa kulipwa:

i) Kuhusiana na ‘sharti la adhabu (faini) kwenye mikataba: ‘Kongamano’ linapenda kuweka msisitizo juu ya maamuzi yake yanayohusiana na ‘sharti la adhabu (faini) yanayopatikana kwenye maamuzi juu ya miamala ya ‘*Salam*’ namba 85 (2/9) yanayosema hivi

> “*Haijuzu kuweka sharti la adhabu kwa kuchelewa kukabidhi bidhaa, aidha haijuzu kudai (kushurutisha) ziada juu ya deni*”.

Kadhalika maamuzi yake namba 109 (3/12) yanayohusiana na ‘sharti la adhabu’ yanayosema:

> “*Inajuzu kwa Sharti la Adhabu (faini) kuingizwa kwenye mikataba yote ya fedha isipokua tu ile mikataba ambayo makubaliano ya msingi ni ukopeshaji; kwa sababu hapa pataingia riba iliyowazi kabisa. Kwa maana hio, haijuzu kuweka sharti hili – kwa mfano – katika mikataba ya ‘Biashara malipo-polepole’ kwa sababu ya mdaiwa kuchelewa kufanya malipo ya awamu ziliobakia, nisawa iwe kuchelewa huku ni kwa sababu ya kulemewa au kuzembea, wala haijuzu katika mikataba ya istisnaa’ kwa mtengenezewa bidhaa akichelewa kulipa*”.

j) ‘Kongamano’ linaweka msisitizo juu ya maamuzi yake namba 51 (2/6) katika vipengele vifuatavyo:

> “***Tatu:*** *Anapochelewa mnunuzi wa kulipa polepole kulipa deni la ke kwa wakati, haijuzu kumuongezea malipo ya ziada, kufanya hivyo ni riba.*
>
> ***Nne:*** *Ni haramu kwa mdaiwa anaelipa polepole kuchelewesha kulipa kwenye mda waliokubaliana, lakini hats hivyo haijuzu kumuwekea malipo ya zaida kwa ajili ya kuchelewa.*
>
> ***Tano:*** *Inajuzu Kisharia kwa muuzaji anaelipwa polepole kuweka sharti la kumaliza kulipwa pesa za awamu zote kabla ya mda waliokubaliana endapo mnunuzi amechelewesha kufanya malipo ya awamu za mwanzo, na pia iwapo walikubaliana hivyo hapo*

mwanzo.

Sita: *Si haki kwa muuzaji kuendelea kumiliki kile alichokuiza baada ya biashara kukamilika, lakini inajuzu kwa muuzaji kudai rahani fulani kama dhamana kuhakikisha malipo ya pesa zake*".

k) Ni muhimu sana kwa benki za kiislamu kujishughulisha kutatua changamoto za ucheleweshaji wa kulipa madeni, kama vile kujishughulisha na miamala ya murabaha (kutia faida) na mikataba ya mda mrefu, kutochukua njia za kiufundi za kugharamia (kama vile: upembuzi yakinifu) na kutochukua dhamana za kutosha.

Tatu: Baraza' linausia yafuatayo:

a) Benki za kiislamu zijilazimishe kwenye sera zake kufuata kikamilifu mfumo wa uchumi wa kiislamu na vidhibiti vyake, na wasimamie marekebisho ya kiufundi na kiutawala yanayolazimu ili kufikia maendeleo ya ukuaji kupitia rasilimali za uwekezaji za moja kwa moja au kupitia ushirika mpana ili kufiikia malengo ya ukuaji wa kiuchumi na kijamii ambayo hayo ni miongoni mwa malengo makuu ya benki na taasisi za fedha za kiislamu.
b) Juhudi zifanyike za kutafuta mbinu mbadala za utatuzi wa tatizo la ucheleweshaji madeni katika taasisi za fedha za kiislamu, na kuandaa tafiti juu ya suala hili ili ziwasilishwe kwenye kikao kijacho inshaallah.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≋≋≋

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 134 (8/14)

Yanayohusiana na 'Mfumo Mpya wa Ulimwengu, Utandawazi na Miungano ya Kikanda na Athari zake'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nne (14) kilichofanyika Doha, Qatar 8 - 13 Dhul-Qa'ada (Mfungo Pili), 1423, sawa na 11 - 16 Januari, 2003.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Mfumo Mpya wa Ulimwengu, Utandawazi na Miungano ya Kikanda na Athari zake,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeafikiwa yafuatayo:

Moja: Kinachokusudiwa kwa: Utandawazi na Mfumo Mpya wa Ulimwengu:

Utandawazi, kwa muonekano wake wa nje na shakli yake ni kuwepesisha uhamishaji wa bidhaa na fikra, na kuondoa vizuizi baina ya watu na mataifa, kiasi ya kwamba ulimwengu wote ufanane na kijiji kidogo cha kimataifa kutokana na maendeleo ya kiteknolojia ya zama hizi, na mbinu za kisasa za maingiliano ya kimataifa yakiwemo: miungano ya kikanda ya kimataifa, Shirika la Biashara la Kimataifa (WTO) na makampuni ya kimataifa. Mataifa makubwa na ushawishi walionao wa utamaduni wa kimagharibi yameweza kuutumia '*utandawazi*' na kufaidi kutokana na nafasi zilizopo, kupitia utandawazi huu wameweza kutawala na kudhibiti nyanja nyingi za maisha ya binadamu, isitoshe, mataifa haya makubwa yamekua mstari wa mbele kuongoza maendeleo ya kiteknolojia kuzidi kujiongezea nafasi na uwezo wa kuyadhibiti mataifa mengine na maisha ya kibinadamu kwa upande mwengine.

Maendeleo haya yamefungamana na kile kinachoitwa: ‘Mfumo Mpya wa Ulimwengu’ (NWO) uliojengeka kwenye mashirika ya kimataifa na mikutano ya kimataifa ambayo imekua mstari wa mbele kujihusisha na mifumo ya kielimu, kiuchumi, kijamii, kimakaazi na kimazingira yote hayo kwa mitazamo ya kulinda maslahi ya mataifa makubwa ya kimagharibi na hivyo kupelekea kueneza na kusambaza fikra na mifumo ya kitamaduni ya kimagharibi ya kisasa.

Utandawazi kwa picha hii ni ‘*mradi hatarishi*’ kwa umma wa kiislamu na risala wanayoibeba, aidha ni hatarishi kwa utamaduni wa kibinadamu waliouasisi na ulioweza kuwaletea binadamu kheri na furaha katika nyanja zote za maisha. Kwa hali hii imewajibika kwa wanazuoni wa umma na wanasiasa wao, wanafikra wao na viongozi wao katika nyanja za siasa, utamaduni, elimu-malezi, uchumi, mawasiliano-habari na nyenginezo, wana wajibu mkubwa sana kuhakikisha ‘muamko-jumuishi wa kiislamu unasimama ili kuupatia umma msukumo katika nyanja za ustawi na maendeleo.

Juhudi za kuuamsha umma zipitie kwenye maeneo mawili:

Eneo la kwanza: Kuvikinga vizazi vya umma na watoto wao dhidi ya changamoto zinazosakamishwa na matendo ya *utandawazi* ulioshehenikasumba za kimagharibi, juhudi kubwa zinahitajika kuujenga ‘*utu wa kiislamu wa kisasa*’ unaoweza kupambana na changamoto hizi kwa uelewa na uoni na kwa misingi ya ufahamu mpana na wa kina wa uislamu; kwa ufahamu wa *ukatinakati*, uliolingana na usiolemea upande mmoja, ufahamu uliokusanya elimu (sayansi) na imani, uasili na usasa, kushikilia misingi na kuwa wazi na mafanikio ya kisasa. Kufikia hapo inalazimu kupiga jicho kwa karibu sana kwenye mitaala ya elimu na malezi; hususan kutilia nguvu masomo ya dini na kukataa kuingiliwa na mataifa ya kigeni.

Eneo la pili: Kushikilia hatamu za uongozi wakati wa kuamiliana na mifumo na mbinu za utandawazi kwa kua na mipangilio-kazi jumuishi yenye uelewa mpana inayoweza kuzungumza na jamii za kisasa za binadamu kwa njia na lugha wanazozifahamu; mbali na kurupuka au mipangilio duni, mipangilio-kazi hii ilenge nyanja za fikra, utamaduni na

mawasiliano-habari na ilenge kua na ubunifu na uvumbuzi wa kisayansi na kimaendeleo-uchumi ambayo yataleta maisha bora yenye heshima kwa kila mtu kwenye jamii.

‘Kongamano’ linausia:

Katika kuliendea suala la mipangilio-kazi jumuishi iliyoashiriwa hapo juu, na kwa kutokana na ufahamu ya kwamba: Uislamu ni dini ya kimataifa iliyokuja kumletea binadamu kheri na furaha za hapa duniani na za kesho akhera, na uislamu ndio dini ya mwisho ambayo hakuna dini nyengine yoyote itakayokubaliwa mbele ya Allah; yatekelezwe yafuatayo:

1) Kuujulisha umma wa kibinadamu kua uislamu ni dini ya kimataifa (ulimwengu mzima) na una uwezo wa kuyatatua matatizo yote ya binadamu kupitia *manhaj* ya kielimu (mfumo wa kisayansi) maalum na unatumia njia zote zilizopo kufikia lengo hilo.
2) Kuiongezea nguvu ‘Jumuia ya Nchi za Kiislamu’ (OIC) na mashirika yake yaliyo chini yake na taasisi nyengine za kiislamu za kimataifa, aidha, kuhamasisha nafasi zao kwa lengo la kuutilia nguvu muungano wa kimataifa wa kiislamu hususan kwenye nyanja za uchumi.
3) Ulazima wa kulifanyia kazi – kiukamavu – suala la ‘uanzishwaji wa soko la pamoja la kiislamu’ na kushajiisha miradi na uwekezaji shirikishi ya kiuchumi miongoni mwa nchi za kiarabu na za kiislamu.
4) Kubuni upya uhusiano baina ya ‘Ulimwengu wa Kiislamu’ (MW) na ‘Mfumo Mpya wa Ulimwengu’ (NWO) kwa namna itakayolinda uhuru wa nchi za kiislamu na heshima zake turathi zake, kwa lengo la kulinda na kuhifadhi utambulisho wa kiislamu kwa watu wake wote.
5) Kuongeza juhudi katika kuinua na kujenga uwezo wa kisayansi na kiteknolojia katika nchi za kiislamu na kuiingiza teknolojia ya kisasa mashinani mwa nchi za kiislamu.
6) Kuongeza juhudi katika kuboresha mahusiano mema baina ya raia wa nchi za kiislamu na kuiunganisha safu ya kiislamu ili iweze kupambana na changamoto.
7) Kuongeza msisitizo juu ya suala la ‘*uasili na usasa*’ katika maongezi (mahubiri) ya kiislamu na kuyaongezea uwezo ili yaweze kutoa

muongozo-elekezi halisi kwa waislamu, na kuzifikisha jumbe za kiislamu kwa jamii ya kibinadamu wote kua msingi wa dini hii ni kuwaletea binadamu kheri na furaha katika nyanja zote za maisha ya hapa duniani na ya kesho akhera, ujumbe huu ufikishwe mbali na nyongeza za tashdidi kwa upande mmoja, au punguzo-legevu kwa upande wa pili.

8) Kuifanyia kazi fikra ya '*ijtihad*' katika taasisi za kielimu na vyuo vikuu na mbaraza ya fatwa na makongamano ya kifiqhi, ili umma huu ujijengee uwezo wa kupambana na kadhia mpya za kisiku hizi zinazoibuka na matatizo mapya, kwa mtazamo mpana na wa kina wa kifiqhi na kutoa suluhisho makini ya matatizo hayo.
9) Kufaidi na nafasi zilizopo zinazotolewa na teknolojia ya mawasiliano-habari za kisasa kwa kuufikisha ujumbe wa kiislamu na kuidhihirisha picha ya uislamu inayon'gara hasahasa kupitia kwenye chaneli za satalaiti (vin'gamuzi) na mitandao ya intaneti.
10) Ulazima wa kuunganisha juhudi za nchi za kiislamu na jumuia za misaada wanaposhiriki kwenye jumuia za kimataifa na mikutano ya kimataifa, ili kudhihirisha ubora na uhalisia wa mafundisho ya kiislamu katika kusukuma maendelea ya binadamu na kuyalinda dhidi ya mipango-hatarishi.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Tamko (ujumbe) la Kongamano la Fiqhi ya Kiislamu kwa Umma wa Kiislamu Kuhusiana na Palestina na Iraq

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote.

Baada ya kudurusu na kupitia hali halisi na hatarishi inazopitia nchi za kiislamu hususan Palestina na Iraq, kwa kile kinachoendelea kufanywa na Dola ya Kizayuni “Israel” inayoikalia kimabavu Palestina, kuwafanyia wapalestina ugaidi kwa kuwaua watoto, wanawake, watu wazima na raia wa kawaida wasiokua na silaha ya kujilinda, aidha kuwakamata kiholela na kuua viongozi wao na kuvamia nyumba zao na kuwabomolea watu wakiwa wamo ndani, uchafuzi wa ardhi zao za kilimo na kuwawekea vizuizi vya kijeshi vinavyoendelea kwa mda mrefu sasa kwenye vijiji vyao na kambini mwao. Kubwa ya yote hayo ni uvamizi wa Mji wa Quds mji wa *Israa* na *Mi’raj* ambao ni sehemu nyeti ya *aqeeda* na imani ya waislamu, na kuwazuia wapalestina kwenda kutekeleza ibada ya sala katika Masjid al-Aqsa uliobarikiwa.

Licha ya ugaidi wote huu unaotekelezwa na wazayuni; bado wana ujasiri wa kudai eti wao ni watu wa “amani” na yule katili wao mkubwa; jambazi (Sharon) eti ni mtu wa “amani”, na wale wapalestina wanaojitetea na kujaribu kulinda hadhi ya nchi yao na heshima zao na nafsi zao; wanaambiwa eti wao ni “magaidi”.

Hapana shaka yoyote kua vitendo hivi vya kinyama na kikatili vya “Dola ya Israel” ndio ugaidi-nchi wenyewe, ni ukiukaji wa wazi wa haki za binadamu na mikataba ya kimataifa, yote haya yanafanyika chini ya macho na masikio ya watu wote duniani, hasahasa mbele ya nchi zinazodai kua wao ni walinzi na watetezi wa uhuru, demokrasia, usawa wa watu wote, na kulinda haki za binadamu.

Ama kile kinachotishia Iraq kutokana na uvamizi (uadui) wa Amerika wakishirikiana na Uingereza ni kule kulenga kwao kwa kuwamaliza waislamu wa Iraq na kuichafua nchi yao na kuiba rasilimali zao bila kujali vilio vya waislamu kuachana na uadui huu, na kutupilia mbali maamuzi ya mashirika ya kiarabu na ya kiislamu rasmi na yasiokua rasmi, na kutupilia

mbali maombi ya nchi na watu wapenda mani kote duniani, misimamo hii ya Amerika na Uingereza ni dhihirisho la wazi la kukataa maadili na mikataba ya kimataifa inayohusiana na uvunjaji wa heshima za nchi nyingine na watu wake.

Juu ya hayo yote, 'Kongamano' linawaita umma wa kiislamu na serikali zao na kuwakumbusha wajibu wao wa kusimama na kuwanusuru wanyonge na waliodhulumiwa; ili kulinda damu zao na nafsi zao ambazo Allah SWT ameziharamisha kuchafuliwa kama alivyosema:

"*Hakika Waumini ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mrehemewe*".[1]

Akasema tena:

"*Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi. Huamrisha mema na hukataza maovu*".[2]

Nae Mtume SAW akasema:

"المؤمن للمؤمن كالبنيان، يشد بعضه بعضًا"

"*Mu'min (Muislamu) kwa Mu'min mwenzake ni kama mjengo mmoja, unashikana na kusaidiana*"[3]

Akasema tena SAW:

"المسلم أخو المسلم لا يظلمه، ولا يخذله، ولا يسلمه"

"*Muislamu ni nduguye Muislamu mwenzake, asimdhulumu wala asimkhini wala asimsalimishe (kwa adui)*"[4].

Kwa mujibu wa aya na hadith zilizotangulia; na kuongezea kwa yaliyotangulia kutajwa; 'Kongamano' linapenda kuweka msisitizo juu ya yanayofuata:

---

[1] Surat al-Hujurat, 49:10.
[2] Surat al-Tauba, 9: 71.
[3] Muttafaq Alayh (Imekubaliwa na Ulamaa wa Hadith).
[4] Muttafaq Alayh (Imekubaliwa na Ulamaa wa Hadith).

Moja: Haijuzu kisharia kuwaunga mkono wavamizi wala kuwasaidia katika kutimiza malengo yao ya uadui na kumwaga damu za wasiokua na hatia ambazo zinalindwa.

Mbili: Uvamizi wa nchi yoyote miongoni mwa nchi za kiislamu ni sawa na kuvamia umma wa kiislamu wote.

Tatu: Viongozi (watawala) wote wa kiislamu wanatakiwa kisharia, kuwajibika na kubeba dhamana (dhimma) walionayo katika kunusuru na kulinda dini yao, umma wao na nchi zao.

Wal-Hamdu Lillah Rabbil-Aalameen

≋≋≋

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Kumi na Tano (15) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Muscat, Oman

14 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1425

6 - 11 Machi, 2004

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 135 (1/15)

Yanayohusiana na 'Hotuba za Kiislamu: Nafasi zake na Changamoto Zinazozikabili'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tano (15) kilichofanyika Muscat, Oman 14 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1425, sawa na 6 - 11 Machi, 2004.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Hotuba za Kiislamu: Nafasi zake na Changamoto Zinazozikabili,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na baada ya kujikumbusha yalitajwa kwenye Qur'an Tukufu juu ya suala la kutumia hikma na mawaidha yaliyokua mazuri katika ulinganizi (kufikisha da'wa) katika njia ya Allah, na uwepo wa *nusuusi* (dalili) nyingi sana katika Sunnah za Mtume SAW na mafundisho ya kivitendo ya Bwana Mtume SAW katika kuchunga hali za unaozungumza nao (unaowalingania), na kuchagua mbinu muwafaka kulingana na zama na sehemu, na kwa kua hotuba ya kiislamu ni ile yenye ulingano unaoendana na anaelinganiwa (mlengwa wa da'wa);

Imeamuliwa yafuatayo:

a) Inakusudiwa kwa '*hotuba ya kiislamu*': mbinu za uwasilishaji zinazobainisha ukweli wa uislamu na sharia zake katika nyanja zote za maisha ya umma na ya watu binafsi.
b) Kile kinachoenezwa nyakati hizi kuhusiana na maudhui haya inalazimu kuweka wazi mambo ya kipekee na yaliyo mazuri juu ya '*hotuba ya kiislamu*' na kufutilia mbali kasumba mbaya na hujma zinazoendelezwa dhidi ya uislamu, na kupambana na 'uvamizi wa kimawasiliano-habari (media)' uliolenga kuchafua ukweli wa uislamu.
c) Katika kuliendea suala la urekebishaji wa '*hotuba ya kiislamu*' isije ikapelekea urekebishaji huu, kwa kisingizio cha kuendana na wakati,

ikapelekea kubadilisha, kuvuruga au kuachana na misingi iliyo thabiti ya uislamu au hukmu zake za kisharia zinazojulikana, hio haijuzu.

Aidha, inausiwa yafuatayo:

a) Kuunganisha juhudi za walinganizi (*madu'aat*) na wanafikra wanaojihusisha na suala la '*hotuba ya kiislamu*', sawa katika jamii za kiislamu au zisizokua za waislamu, ili kuchunga muktadha wa mfumo (*manhaj*) wa Qur'an na Sunnah katika ufikishaji wa *da;wah* kwa njia ya hikma na mawaidha yaliyokua mazuri, na kujiepusha lugha zinazowafanya walinganiwaji kutoukubali ulinganizi wa haki.
b) Ulazima wa kufaidi na vyombo vyote vya mawasiliano na teknolojia ya kisasa kuwepesisha shughuli za uwasilishaji wa '*hotuba ya kiislamu*' kwa watu wote kulingana na matabaka yao.
c) Kuzitaka serikali za kiislamu na wenye uwezo, kujitolea mali na juhudi za kakusudi katika kuifikisha '*hotuba ya kiislamu*' kupitia vyombo vya habari na mawasiliano mbalimbali hususan chaneli za satelaiti (vin'gamuzi) ni mitandao ya intaneti, katika kuweka wazi ukweli (uhalisia) wa uislamu, na kufutilia mbali kasumba na tuhuma za uwongo zinazoenezwa dhidi yake, aidha, kuvisafisha vyombo hivi na kila kinachokinzana na uislamu.
d) Kuifanyia kazi *'Ijtihad*' na '*ubunifu*' katika *uslubi* (lugha) ya '*hotuba ya kiislamu*' pamoja na kuzingatia '*Uasili na Usasa*', yaani kuchunga misingi iliyo thabiti na kutizama mabadiliko ya kila zama katika kulinda maslahi yanazuka na desturi ambazo hazigongani na misingi ya sharia.

Wabillah al-Taufiq

≃≃≃

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 136 (2/15)

Yanayohusiana na 'Musharaka Unaopunguka (*Diminishing Musharaka*) na Vidhibiti vyake vya Kisharia'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tano (15) kilichofanyika Muscat, Oman 14 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1425, sawa na 6 - 11 Machi, 2004.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Musharaka Unaopunguka (*Diminishing Musharaka*) na Vidhibiti vyake vya Kisharia,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Musharaka Unaopunguka (Diminishing Musharaka): Ni aina mpya ya miamala inayohusiana na ushirika baina ya pande mbili kwenye mradi wenye faida, upande mmoja unaahidi na kujilazimisha kununua hisa za upande wa pili (mshirika wake) kidogo kidogo, ima ununzi huu wa hisa ufanyike kupitia faida inayopatikana au kutoka sehemu nyengine.

2) Msingi wa 'Musharaka Unaopunguka (Diminishing Musharaka)': Ni ule mkataba unaokubaliwa na pande mbili na kila upande unachangia hisa zake kwenye rasilimali ya kampuni, nisawa uwe mchango wake wa hisa ni kwa pesa taslimu au vitu vinavoweza kutathminiwa, na kubainisha jinsi ugavi wa faida utakavyokua na kwa makubaliano ya kila upande kuwajibika hasara – itokeapo – kwa kiwango cha hisa za kila mmoja wao.

3) 'Musharaka unaopunguka (Diminishing Musharaka)' unajikita zaidi kwa uwepo wa wa ahadi inayolazimu kutoka moja ya pande mbili ili

amiliki hisa za upande wa pili, lakini upande mwengine utakua na hiari ya kukubali au kukataa, iwapo wamekubaliana basi watafunga mkataba wa mauziano wa hisa kila zinapomilikiwa japo kwa ishara ya kusema: nimekuuzia, na mwengine kusema: nimekubali.

4) Inajuzu kwa moja ya pande za ‘Musharaka’ kukodi hisa za mshirika wake kwa malipo maalum na kwa mda ulioainishwa, kila mshirika taendelea kuwajibika na gharama za msingi kwa kiwango cha hisa zake.

5) ‘Musharaka unaopunguka (Diminishing Musharaka)’ unajuzu iwapo pande husika watajilazimisha na hukmu za ushirika na kuchunga vigezo vifuatvyo:

    a. Kutoekeana ahadi ya upande mmoja kununua hisa za mshirika wake kwa thamani ileile ya walipoanzisha ushirika, kufanya hivyo ni sawa na kutoa dhamana ya hakikisho la kununua hisa za mshirika, inachotakiwa ni kukubaliana kwa thamani ya hisa kwa mujibu wa bei halisi ilivyo sokoni wakati wa manunuzi au kile watakachokubalina wakati wa kuuziana.
    b. Kutoshurutisha moja ya pande mbili kuwajibika gharama za bima, matengenezo na gharama nyenginezo, lakini inatakiwa gharama hizo zote ziwe kwenye chombo kimoja kila mmoja achangie kwa kadiri ya hisa zake.
    c. Kiwango cha faida kiainishwe kwa asilimia (%), haijuzu kushurutisha kiwango fulani cha pesa akatiwe mmoja wao kutokana na faida au na rasilimili ili uwe mgao wake.
    d. Kutofautisha baina ya mikataba na ahadi zihusuzo *Musharaka*.
    e. Kuzuia uwepo wa haki ya mmoja wa pande mbili kurejeshewa pesa zake alizozitoa kama hisa (kugharamia).

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 137 (3/15)

Yanayohusiana na 'Hati za *Ijara*'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tano (15) kilichofanyika Muscat, Oman 14 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1425, sawa na 6 - 11 Machi, 2004.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Hati za *Ijara*,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Fikra ya 'hati (*sukook*) za *ijara*' imejengeka kwenye msingi wa ulinzi-dhamana, ambayo inakusudiwa utowaji wa hati za fedha zilizodhaminiwa na mali (assets), kwa msingi wa mradi wa uwekezaji utakaoleta faida. Lengo la 'hati za *ijara*' ni kuhaulisha vitu na manufaa vinavyohusiana na 'mkataba wa *ijara*' viwe 'hati za fedha' (*sukook*) zinazoweza kutumika kama fedha kwa minajili ya manunuzi kwenye soko nyingine, ndio kwa maana hii zinajulikana hati hizi kua ni: 'hati zenye thamani sawiya zinazowakilisha hisa za pamoja kwenye umiliki wa vitu au manufaa yenye kuleta faida.

2) 'hati za *ijara*' haziwakilishi kiwango fulani cha pesa, wala sio kwamba ni deni linalomilikiwa na sehemu fulani – iwe ni mtu wa kawaida au mtu wa kimaanawi – lakini ni 'hati ya fedha' inayowakilisha sehemu ya pamoja ya (hisa) kutokana na umiliki wa kitu kinachotumika; kama vile nyumba au ndege au meli au kundi la vitu vinavotumika – iwe vinafanana au vinatofautiana – ikiwa vitu hivyo vinakodishwa na vinaingiza faida-ainishwa kwenye mkataba wa ijara.

3) Inawezekana kwa '*hati za ijara*' kubeba jina la mmiliki wa hati hizo na

kusajiliwa kwenye tarjis maalum ya umiliki au kuandika jina la mmiliki mpya kila inapobadilika umiliki, aidha inawezekana ziwe ni hati kwa mbebaji wake kwa namna ambayo umiliki wake unahamishwa kwa kukabidhiwa.

4) Inajuzu kutoa hati (sukook) zinazowakilisha umiliki wa vitu vilivyokodishwa na mizunguko (kubadili mikono) yake; yanapopatikana masharti ya vitu vinavyosihi kufungiwa mkataba wa ijara; kama vile nyumba au ndege au meli na mfano wake, madamu (madhali) hati hio inawakilisha vitu vya uhakika vilivyokodishwa; kikawaida vitu hivyo vinaingiza kipato (faida) kinachojulikana.

5) Inajuzu kwa wa mmiliki wa hati za *sukook* kuziuza sokoni kwa mnunuzi yeyote na kwa thamani watakayokubaliana, sawa iwe ni thamani inayolingana au ya ziada au ya chini ya bei iliyonunuliwa, hii ni kwa sababu vitu vinabadilika thamani kulingana na kanuni ya ‘kuuza na kutaka’ (supply & demand).

6) Mmiliki wa hati anastahiki mgao wake wa faida – ambao ni ujira (malipo) – kwa mida ilioainishwa kwenye masharti ya utoaji wa hati, baada ya makato ya gharama za matengenezo kwa mujibu wa hukmu za mkataba wa ijara.

7) Inajuzu kwa mkodishwaji alienahaki ya kukodisha (sub-leasing) kutoa hati za ijara zinazowakilisha hisa za pamoja katika manufaa anayomiliki kwa njia ya kukodi kwa lengo la kukodisha, hata hivyo inashurutishwa kusihi kwake ziwe hati hizo zimetolewa kabla ya kufunga mikataba na wakodishwaji (wakodishwajai wadogo – sub-lease), nisawa ukodishwaji uwe ni kwa ujira kama ijara ya kwanza (ya asili) au chini ya hapo au juu ya hapo. Iwapo mikataba na wakodishwaji wadogo imeshasainiwa basi haijuzu kutoa hati za sukook, kwa sababu hapa zitawakilisha deni kwa mtoaji juu wa wakodishwaji.

8) Haijuzu kwa mtoaji wa sukook au msimamizi wake kudhamini rasilimali ya hati au faida zake, na iwapo kutatokea hasara ya kuharibika kwa

vitu vilivyokodishwa vyote au baadi yake basi hasara hio ni ya wabeba sukook.

‘Kongamano’ linausia yafuatayo:

Kuandaa ‘warsha mahsusi’ kudurusu hukmu zaa aina mbalimbali za utekelezaji zilizoelezewa kwenye baadhi ya tafiti, lakini maamuzi haya hayakugusia hukmu hizo, ifanywe hivyo kwa ushirikiano na taasisi za fedha husika, ili ‘Kongamano’ liweze kutoa maamuzi yake kwa mujibu wa matokeo ya warsha hio; aina muhimu za hukmu ni kama zifuatazo:

1) Hukmu ya kutoa sukook ya umiliki wa vitu vilivyokodishwa kwa kodi inayoishia kumiliki kwa yule ambae vitu hivyo vimenunuliwa kwake.

2) Hukmu ya kutoa sukook na kubadilisha mikono (umiliki) kwenye ijara ya vitu (nyumba) ambavyo bado havijajengwa (*mawsufah bi al-dhimmah*).

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 138 (4/15)

Yanayohusiana na 'Kuisilimisha Mitaala (*Manahij*) ya Elimu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tano (15) kilichofanyika Muscat, Oman 14 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1425, sawa na 6 - 11 Machi, 2004.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kuisilimisha Mitaala (*Manahij*) ya Elimu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Mchakato wa '*Kuisilimisha Mitaala ya Elimu*' unatakiwa kuandaa mitaala (*manahij*) ya elimu itakayozingatia - kwenye malengo yake, hadidu zake, mbinu zake na njia za upimaji (utahini) wake - itazingatia 'mtazamo kamili wa uislamu' wa binadamu, dunia na maisha, kwa lengo la kumtayarisha binadamu alie mwema, anaejilazimisha na kufuata maadili ya dini yake na alie na uwezo wa kusimamia na kusimamisha uongozi (khilafa) bora juu ya ardhi (ulimwengu) na kuiamirisha dunia kwa mujibu wa ufahamu wa mfumo (*manhaj*) wa kiislamu.

2) Mchakato wa kielimu na kimalezi ulenge kwenye kupanda mbegu za maadili mema ya kiislamu kwa kizazi kipya na kuwawezesha kuyatumia maadili hayo kivitendo kwenye maiasha yao ya kawaida ya kila siku.

3) Kuisuka mikarara (matini) ya kielemu ndani ya 'mtazamo kamili wa uislamu' na kujitahidi kudhihirisha maono ya kiislamu (*Aqeedah*, Sharia na Mfumo wa Maisha) ndani ya mikarara.

4) Mbinu na njia za kielimu na kimalezi zijikite kwenye 'mfumo wa

kiislamu' pamoja na kufaidi na mbinu za kielimu za kisasa na teknolojia ya ufundishaji wa kisasa, na kutekeleza mipango inayofikisha kwenye kwa malengo ya kiislamu kwa taratibu zinazotakikana, kama kuwaekea zawadi wabunifu na wavumbuzi.

5) Kujilazimisha na maadili ya kiislamu wakati wa upimaji (utahini) wa mchakato mzima wa kielimu na kmalezi pamoja na kufaidi na mbinu za upimaji za kisasa, na kuhakikisha ushirikiano na kubadilishana taarifa miongoni mwa nchi za kiislamu.

6) Kuipiga msasa mitaala ya kielimu na kimalezi iliyopo sasa katika ulimwengu wa kiislamu (nchi za kiislamu), na kuiboresha kwa namna ambayo itakusanya baina ya uasili wa kiislamu na usasa, kwa juhudi za ndani kwa ndani bila ya shinikizo za kutoka nje.

7) Kuifanya 'Lugha ya Kiarabu' itumike kwenye awamu zote za masomo na masomo yawe yanasomeshwa kwa lugha hio ya Qur'an na Sunnah, ili kuulinda utu (utambulisho) wa kiislamu na kuunganisha na turathi yake ya kielimu ambayo imesajiliwa kwa kiarabu.

8) Kuzitakasa elimu za sayansi katika nyanja mbalimbali kutokana na ufahamu mbovu ulioingizwa kwenye misingi ya kiislamu.

9) Kutilia nguvu roho ya uvumbuzi, ubunifu, ukosoaji wenye kujenga (constructive criticism) na ukatinakati katika mchakato mzima wa kielimu na kimalezi.

10) Kujihusisha na kumuandaa mwalimu maandalizi ya kisilka, kimaarifa na kimalezi, aidha, kuandaa vitabu vinavyowiana na misingi na maadili ya kiislamu.

11) Kuifanya elimu-msingi iwe ni ya lazima na ya bure (bila malipo) katika nchi zote za kiislamu ili kuweza kupambana na ujinga na kukiandaa kizazi kipya kwenye misingi ya uislamu na utamaduni wa kisasa.

12) Kufanya kwa bidi kuondosha mkanganyiko katika mifumo ya elimu iliyopo kwa sasa, ili mchakato wa elimu uanzie kwenye misingi ya

kiislamu bila ya kuvuruga mahitajio ya kisasa ya zama hizi, na kuwawezesha wanafunzi kupambana na changamoto za sasa na za baadae (mustakbali).

13) Kujihusisha na maono na misingi ya malezi ya kiislamu, ili iwe ni muelekezaji mkuu wa mchakato mzima wa kielimu na kuyapatia malezi ya kimaadili nafasi kubwa inayostahiki ili mwanafunzi aweze kuandaliwa kisilka na kimaadili ya kiislamu.

14) Kupalilia kwenye mitaala ya kielimu mambo ya kutilia nguvu suala la umoja wa kiislamu na utamaduni wa kuishi pamoja kwa amani na watu wote duniani.

15) Kuitaka ‘Sekreterieti Kuu ya Kongamano la Fiqh’ kwa kushirikiana na ‘Shirika la Kiislamu la Elimu, Sayansi, na Utamaduni (ISESCO) na mashirika mengine yanayojihusisha na mambo haya, kuandaa ‘Warsha Maalum’ yenye maudhui ya: “**Kuisilimisha Mitaala (*Manahij*) ya Elimu”** pamoja na kufaidi na juhudi zilizotangulia katika eneo hili ili kuweza kuweka ‘ufahamu jumuishi’ na mpango-mkakati wa kuboresha na kusilimisha mifumo (mitaala) ya elimu katika ulimwengu wa kiislamu (MW), natija zitakazopatikana ziwasilishwe kwa ‘Jumuia ya Nchi za Kiislamu (OIC) ili ziwafikie mawaziri wa elimu na malezi katika nchi zote za kiislamu.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 139 (5/15)

Yanayohusiana na ‘Kadi za Mikopo’

Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), katika kikao chake cha kumi na tano (15) kilichofanyika Muscat, Oman 14 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1425, sawa na 6 - 11 Machi, 2004.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye ‘Kongamano’ kuhusiana na maudhui ya **Kadi za Mikopo,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na baada ya kujikumbusha ‘Maamuzi’ yaliyowahi kutolewa na ‘Kongamano’ juu ya suala hili, ‘Maamuzi namba 63 (1/7) yaliyojumuisha: fasili ya kadi za mikopo na aina zake. Aidha, Maamuzi namba108 (2/12) yaliyojumuisha: kubainisha hukmu ya kutoa kadi za mikopo zisizolindwa na akiba na jinsi ya kuamiliana nazo, malipo yanayoambatana nazo, makato kwa wafanya-biashara na watoaji huduma wanaozikubali kadi hizo, utoaji wa pesa taslimu, kununua dhahabu, fedha au sarafu kwa kutumia kadi hizo;

Imeamuliwa yafuatayo:

a) Inajuzu kutoa ‘kadi za mikopo’ zinazolindwa na akiba na kuamiliana nazo, iwapo hazikushurutisha malipo ya ziada kwa ajili ya kuchelewa kulipa deni.

b) Kuhusisana na malipo, makato kwa wafanya-biashara na watoaji huduma wanaozikubali kadi hizo na utoaji wa pesa taslimu kwa kutumia‘kadi za mikopo’ zinazolindwa; hukmu yake ni ile iliyoainishwa kwenye ‘Maamuzi namba 108 (2/12) pamoja na kuzingatia vigezo vilivyotajwa kwenye maamuzi hayo.

c) Inajuzu kununua dhahabu na fedha kwa kutumia ‘kadi za mikopo’ zinazolindwa (zenye akiba).

d) Haijuzu kwa taasisi za utoaji kadi za mikopo kumpatia mbebaji kadi inayomruhusu huduma za kuingia mwenye miamala iliyoharamishwa; kama vile: bima ya biashara au kuingia sehemu zilizoharamishwa, lakini hamna katazo la kisharia kumpatia huduma zisizoharamishwa kama nafasi ya kipaumbele kwenye huduma au punguzo la bei.

e) Taasisi za Fedha za Kiislamu zinazotoa huduma mbadala ya ‘Kadi za Mikopo zisizolindwa na akiba’ zinatakiwa wakati wa utoaji wa kadi hizo kujilazimisha na masharti na vigezo vya kisharia, aidha, wanatakiwa kujiepusha na mkamganyiko wa riba au visingizio ambavyo vinaweza kupelekea kunako riba kama vile: kufuta deni kwa deni.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≃≃≃

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 140 (6/15)

Yanayohusiana na 'Uwekezaji wa Mali ya Waqfu na Faida zake'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tano (15) kilichofanyika Muscat, Oman 14 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1425, sawa na 6 - 11 Machi, 2004.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Uwekezaji wa Mali ya Waqfu na Faida zake,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na baada ya kujikumbusha 'Maamuzi' yaliyowahi kutolewa na 'Kongamano' na mapendekezo ya warsha na mikutano juu ya suala hili;

Imeamuliwa yafuatayo

Moja: Uwekezaji wa Mali ya Waqfu:

1) Inakusudiwa kwa uwekezaji wa mali ya waqfu, kuyazalisha na kuyakuza, sawa iwe na mali ya asili au faida (ghila) zake kwa kutumia njia za uwekezaji zinazoruhusiwa kisharia.
2) Ni wajibu kuyahifadhi mali ya waqfu kwa namna ambayo asili yake itaendelea kubaki na manufaa yake kudumu.
3) Inalazimu kuwekeza mali ya waqfu ya asili sawa mali hizo ziwe ni nyumba, ardhi au vitu vinavyohamishika ikiwa hazikukusudiwa kwa matumizi ya mojamoja ya vitu venyewe.
4) Sharuti la muweka waqfu lizingatiwe iwapo ameshurutisha kua waqfu ya asili ikuzwe kwa kutumia sehemu ya faida inayopatikana kwenye waqfu yenyewe, na hii haitokinzana na malengo (multadha) ya waqfu, aidha, sharti lake lifanyiwe kazi iwapo amushurutisha kua faida inayopatikana kwenye waqfu yenyewe itumike yote kwenye maeneo yaliyoainishwa wala isitumike kwenye kukuza usuli ya waqfu.
5) Kimsingi, ni kutojuzu kuwekeza sehemu ya faida iwapo muweka waqfu

hakuainisha kitu na hakushurutisha uwekezaji wake ila kwa muwafaka wa wastahiki wa waqfu ya kifamilia, ama waqfu ya umma inajuzu kuwekeza sehemu ya faida yake kwa minajili ya kukuza usuli ya waqfu ikiwa kuna maslahi makubwa kufanya hivyo, lakini kwa vigezo vitakavyoelezewa baadae.

6) Inajuzu kuwekeza kinachozidi katika faida ya waqfu kwa ajili ya kukuza usuli au kuimarisha faida, hii ni baada ya kugawiwa wastahiki kima chao na kutoa gharama na makato, aidha, inajuzu kuwekeza pesa za faida zilizorundikana ambazo zimechelewa kusarifiwa.
7) inajuzu kuwekeza pesa za faida zilizorundikana kwenye matengenezo na kuboresha waqfu na shughuli nyenginezo zinazoruhusiwa.
8) Hakuna katazo la kisharia kuwekeza mali ya nyakfu mbalimbali kwenye ‘Mfuko Mmoja wa Kiuwekezaji’ kwa namna ambayo haitopingana na sharti la muweka waqfu, lakini dhimma za wastahiki wa nyakfu hizo zilindwe.
9) Wakati wa kuwekeza mali ya waqfu ni lazima kuzingatia vigezo vifuatavyo:

    a. Vyombo na nyanja za uwekezaji ziwe ni halali.
    b. Ni vyema kutofautisha nyanja za uwekezaji ili kupunguza hatari za hasara, aidha, kupata dhamana, ahadi na mikataba, na kufanya upembuzi yakinifu wa kiuchumi unaofaa kwa miradi ya kiuwekezaji.
    c. Kuchagua mbinu za uwekezaji salama na kujiepusha uwekezaji hatarishi kwa mujibu wa inavyofahamika katika biashara za kiuwekezaji.
    d. Uwekezaji wa mali ya waqfu unatakiwa uwiane kati ya nyanja za uwekezaji na aina ya mali ya waqfu yenyewe ili kuhakikisha maslahi mapana ya waqfu yamepatikana kwa namna ambayo italinda usuli na maslahi ya walengwa wa waqfu hio. Kwa mana hio, iwapo usuli za waqfu ni vitu basi uwekezaji wake unatakiwa usiwe ni wenye kupoteza hadhi au umiliki wa kitu hicho, ama zikiwa usuli za waqfu ni sarafu basi inawezekana kuwekezwa katika njia zote za uwekezaji zinazokubalika kama vile; *mudharaba*, *murabaha*, *istisnaa* na kadhalika.

e. Inatakiwa kutoa ripoti ya kila kipindi fulani kuhusu shughuli za uwekezaji zinazoendeleaa kwa mujibu wa desturi zinazojulikana katika jambo hili.

Mbili: Waqfu ya Sarafu (*Cash Waqf*):

1) 'Waqfu ya Sarafu' inajuzu kisharia, kwa sababu kusudio la waqfu kisharia ambalo ni kufungia usuli ya waqfu na kuendelea kufaidika na manufaa (faida) yake; linapatikana hapa.
2) Inajuzu kwa pesa za waqfu ya sarafu kutumika kama '*qard hasan*' mkopo bila riba na kuziwekeza kwa njia mubashara au kwa kushirikiana na waweka nyakfu wengine kwenye mfuko mmoja, au kupitia utoaji wa hisa za kisarafu na kiwaqfu ili kuzidi kushajiisha waqfu na kuleta ushirikiano wa pamoja.
3) Waqfu-sarafu inapowekezwa kwenye vitu kama kununua nyumba au ardhi au kuingia mikataba ya istisnaa, basi vitu hivyo vyovyo havitakua ni waqfu kushikilia nafasi ya sarafu, bali inajuzu kuviuza ili kuendeleza uwekezaji, waqfu itabaki ni ile usuli ya mwanzo ya sarafu.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kuzitaka nchi wanachama wa 'Jumuia ya Nchi za Kiislamu' (OIC), na jamii za kiislamu katika nchi zisizokua za kiislamu kuendelea kuhifadhi, kulinda na kuchunga '*taasisi ya waqfu*' na kuhuisha aina nyingine za waqfu kama: '*waqfu ya kifamilia*' amabyo imefutwa katika baadhi ya nchi za kiarabu na kiislamu.
2) Kuzitaka nchi za kiarabu na za kiislamu na mashirika na taasisi zinazohusika na mambo ya nyakfu, na mashirika ya kimataifa husika kuwajibika mbele ya kulinda 'Nyakfu za Palestina' kwa ujumla lakini pia kulinda nyakfu za al-Quds kwa njia ya kipekee na kuongeza juhudi kuzihifadhi na kuhifadhi athari zake, aidha, kutoa mwito wa kuzikuza ili ziendelee kutimiza malengo yake na risala zake.
3) Kuzitaka serikali za kiislamu kuwajibika kugharamia 'idara ya waqfu' kadri iwezekenavyo kwa kulinda maslahi ya umma, ni wajibu wa serikali kulinda maslahi ya raia na nchi.
4) Kuzitaka taasisi husika kuweka vigezi vya kisharia na vya kiuhasibu

vya ukaguzi wa kisharia, kifedha na kiutawala juu ya kazi za msimamizi wa waqfu; sawa msimamizi awe ni mtu au kundi la watu au taasisi au wizara, aidha, idara hii ya waqfu inatakiwa kua chini ya darubini ya udhibiti wa kisharia, kiutawala, kifedha na kiuhasibu.

5) Ulazima wa kuweka vidhibiti-vigezo vya matumizi ya idara za waqfu, nisawa yawe matumizi hayo kugharamia matangazo ya biashara, utawala, malipo au zawadi, ili iwe ni ‘rejea’ wakati wa ukaguzi na kutathmini utenda-kazi.
6) Kutoa wito wa kuhuisha ‘mfumo wa waqfu’ wa aina zake zote ambazo zilikua na nafasi adhimu katika kujenga na kukuza ‘Ustaarabu wa Kiislamu’ na maendeleo ya kibinadamu, kielimu, kijamii na kiuchumi.
7) Kufaidi na ‘tajriba zinazoongoza’ katika suala la usimamizi wa waqfu na kuikuza katika baadhi ya nchi za kiarabu na za kiislamu.
8) Ulazima wa kupanga vipaumbele katika uwekezaji wa nyakfu katika nchi za nchi za kiislamu.

Wabillah al-Taufiq

≃≃≃

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 141 (7/15)

Yanayohusiana na 'Dhana ya Maslahi Mursala (*huria*) na Utekelezaji wake wa Kisasa'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tano (15) kilichofanyika Muscat, Oman 14 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1425, sawa na 6 - 11 Machi, 2004.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Dhana ya Maslahi Mursala (*huria*) na Utekelezaji wake wa Kisasa,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na kwa kuzingatia uwepo wa *ijma* ya waislamu kua: hukmu za kisharia zimejikita kwenye misingi ya kuleta maslahi na kuepusha madhara;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Maana ya maslahi: Ni kulinda kusudio kuu la sharia nalo ni kuhifadhi dini, nafsi (roho), akili, kizazi (heshima ya binadamu) na mali. 'Maslaha Mursala' (huria): Ni maslahi ambayo hayajainishwa na sharia uwepo wake au aina zake, aidha, sharia haijaelekeza utupiliaji wa maslahi hayo, na yanaingia kwenye makusudio makuu ya sharia.
2) Mwanafiqihi anawajibika – kwa msisitizo – ahakikishe uwepo wa vigezo vya maslahi, navyo ni:

    - Yawe maslahi hayo ni ya uhakika si ya kudhania tu.
    - Yawe ni maslahi mapana sio finyu.
    - Yawe na maslahi ya wengi si ya binafsi.
    - Yasipingane na maslahi mengine kama hayo au mazuri kuliko hayo.
    - Yawiane na makusudio ya sharia.

Wanazuoni wameweka vigezo madhubuti vinavyopambanua aina za maslahi na msingi wa kuchagua ni maslahi yepi yanayozingatiwa; wameyagawa kulingana na mafungamano yake na maisha ya watu kwenye aina tatu kwa mpangilio wa kipaumbele nazo ni:

- Mambo ya msingi (lazima).
- Mahitajio.
- Vikamilishi.

3) Ilivyo katika maelekezo ya kifiqhi, ni kwamba shughuli za mtawala (serikali) ni ngao ya maslahi kwa raia, kwa hio anatakiwa kuchunga maslahi wakati anasimamia mambo ya raia, na ni juu ya raia (umma) kumtii mtawala wao kwa hilo.
4) 'Maslahi Mursala' (*huria*) yana aina nyingi na pana za utekelezaji katika mambo ya jamii na katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kimalezi, kiutawala, kimahkama na nyenginezo. Ni kwa vipengele hivi sharia ya kiislamu inajidhihirisha umakini wake na utayari wake wa kuendana na wakati nyakati zote katika kutumikia mahitajio ya binadamu, tafiti zilizowasilishwa kwenye kikao hiki zimeweka bayana jambo hili.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≃≃≃

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 142 (8/15)

Yanayohusiana na 'Uwajibikaji wa Daktari'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tano (15) kilichofanyika Muscat, Oman 14 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1425, sawa na 6 - 11 Machi, 2004.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Uwajibikaji wa Daktari,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Uwajibikaji wa Daktari:

1) Utabibu (Udaktari) ni elimu na fani inayoendelea kwa ajili ya kumnufaisha binadamu, inatakiwa kwa tabibu (daktari) wakati wote anapokua kazini kua na khofu (uchamungu) ya allah na kuifanya kazi yake hio kwa *ikhlasi* (imani na uaminifu) kulingana na misingi ya kitaaluma na kielimu.
2) Daktari atabeba dhamana (atawajibika) linapotokea dhara lolote kwa mgonjwa wake katika hali zifuatazo:

    a. Anapokusudia kumdhuru.
    b. Akiwa si mweledi wa elimu ya tiba, au tanzu ya tiba anayoifanyia kazi.
    c. Akiwa hana kibali (leseni) kutoka sehemu husika serikalini inayomruhusu kufanya kazi ya tiba.
    d. Anapoiendea kazi hio ya kutibu bila ya ruhusa ya mgonjwa mwenyewe au msimamizi wake (kama ilivyopitishwa kwenye 'Maamuzi ya Kongamano' namba 67 (5/7).
    e. Anapomghuri (danganya) mgonjwa.

f. Anapotenda kosa ambalo kwa kawaida madaktari hawatendi kosa kama hilo, aidha misingi ya taaluma hio haikubali kosa hilo, au akawa amezembea au kutokua muangalifu.
g. Anapotoa siri ya mgonjwa wake bila ya sababu inayokubalika (kwa mujibu wa 'Maamuzi ya Kongamano' namba 79 (10/8)).
h. Anapokataa kutekeleza wajibu wake wa kiudaktari katika hali za dhdarura (huduma ya kwanza).

3) Daktari - na anaebeba dhima kama yeye – atawajibika kimalipo katika hali-tajwa hapo juu iwapo masharti ya uwajibikaji kimalipo yamepatikana isipokua kwenye hali ya kimakosa (kipengele: 'f') basi hatowajibika kimalipo ila ikiwa kosa lenyewe ni kubwa.
4) Iwapo shughuli ya kiutabibu inasimamiwa na kundi la madaktari; basi kila mmoja wao atawajibika na kosa lake, hii ni kwa mujibu wa msingi unaosema: "*Inapokutana mtendaji kosa na msababishaji, basi muwajibikaji ni yule alietenda iwapo msababishaji ila ikionekana kua msababishaji ana dhimmi kuu katika kosa hilo*". Ama kiongozi wa kundi hilo atawajibika kama kiongozi juu ya wenzake wanaofanya chini yake iwapo alikosea kuwaelekeza au hakua na usimamizi mzuri juu yao.
5) Taasisi ya Afya (ya Umma au ya Binafsi) itwajibika na madhara yoyote yatakayojitokeza ikithubutu kua taasisi hio imezembea au imetoa maelekezo yaliopelekea kuwadhuru wagonjwa bila sababu ya kuridhisha.

Aidha, Kongamano linausia yafuatayo:

1) Kuandaa tafiti-elekezi mahsusi juu ya changamoto za utekelezaji wa kisasa wa mfumo wa '*Aaqilah*' (familia kuu inayosimamia fidia ya mmoja wao) na kuweka mfumo mbadala unaokubalika kisharia.
2) Kuandaa tafiti-elekezi mahsusi juu ya mas'ala 'madhara ya kimaanawi na fidia yake' katika kadhia za uwajibikaji kwa ujumla.
3) Kuzitaka serikali za kiislamu kulinganisha (sawazisha) sheria zao zinazohusiana na 'mipangilio ya kazi za kiutabibu' kama vile suala la utoaji mimba, kufa kwa ubongo, upasuaji na kadhalika.

4) Kuvitaka vyuo vikuu katika nchi za kiislamu kuasisi kitengo maalum cha ‘maadili na fiqhi ya utabibu’ kwa wanafunzi wa vitengo vya tiba na uuguzaji.
5) Kuzitaka serikali za nchi za kiislamu kuweka mpangilio wa ‘shughuli za tiba mbadala’ na ‘tiba ya asili’ pamoja na kutoa usimamizi na kuweka vigezo na vidhibiti vitakavyoilinda jamii dhidi ya madhara (yanayotarajiwa).
6) Kuvisisitiza vyombo vya habari kuelekeza risala ya mawasiliano kwenye nyanja za afya na tiba.
7) Kushajiisha matabibu (madaktari) waislamu kuendeleza tafiti na majaribio mbalimbali ya kisayansi na kifiqhi.

Wabillah al-Taufiq

≋≋≋

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Tamko Kuhusiana na Kadhia ya Palestina

‘Kongamano la Fiqhi ya Kiislamu’ likiwa linaendelea kufuatilia matukio yanayojiri katika ardhi ya Palestina inayokaliwa kimabavu na wavamizi wa kizayuni, linatoa mwito kwa ulimwengu mzima kuwajibika ktika kusimamisha ugaidi unaoendelezwa na ‘serikali ya kizayuni’ ya kuua kikatili wasiokua na hatia miongoni mwao watoto, wanawake na watu wazima takriban imekua ni kazi ya kila siku, achilia mauaji ya halaiki yanayofanywa mara kwa mara, mbali na bomoa-bomoa ya nyumba za wapalestina, kuwaharibia mashamba yao, kuharibu mazao yao, kunyakua ardhi zao, kuwafukuza wakaazi wa kipalestina na kusumua hata miti inayomsabihi Mwenye-Ezi mungu (Allah).

Kama yote hayo hayatoshi, sasa wamejenga kuta la kiubaguzi linalokata na kula kwa zaidi ya asilimia 25% ya ardhi za wapalestina baada ya kuwavunjia nyumba zao kwa kisingizio cha kulipitishas kuta hilo la kiubaguzi bila kujali mafundisho ya kidini, desturi za kibinadamu na sheria na kanuni za kimataifa. Juu ya yote hayo ‘serikali ya kizayuni’ inatumia makundi ya kigaidi na kihuni na ya kijambazi kwenda kuvamia benki za wapalestina na kuiba akiba na fedha za wapalestina.

Matendo (maovu) haya ya kijinai na ya kinyama kwa pamoja hayajawahi kutokea katika historia ya kibinadamu hata katika nyakati ngumu za dhulma na kiza, lakini haya yote ndio yanayofanywa leo na ‘serikali ya kizayuni’ chini ya pazia ya ‘kujilinda’ na kwa kisingizio kua ‘taasisi za kipalestina’ ni za kigaidi!!, vipi wapalestina ni magaidi wakati wanalinda ardhi zao, heshima zao na mali yao dhidi ya mvamizi kandamizi asiejali ubinadamu??, lau madai yao haya yangekua ni kweli basi harakati za ukombozi na kupigania uhuru wa nchi zao kote duniani zingekua ni za kigaidi.

Wanazuoni wa‘Kongamano la Fiqhi ya Kiislamu’ wanashangazwa sana na msimamo huu wa ulimwengu wa kuunyamazia ugaidi huu unaoendelezwa

kila siku, wakati huohuo tunazitaka taasisi za kimataifa kuwajibika na kubeba majukumu yao katika kuondosha dhulma inayoendelea na kuhakikisha kua misingi ya uhuru, uadilifu na usawa wanayoipigia kelele wanaisimamia.

Aidha, ‘Kongamano la Fiqhi ya Kiislamu’ linatoa wito kwa nchi za kiarabu wakiwa wanajitayarisha na kikao chao cha kilele kitakachofanyika hapo Tunis mwisho wa mwezi huu, waliangazi suala ‘serikali ya kizayuni’ kuendelea kuchimba chini ya msikiti wa Masjid al-Aqsa na pembezoni mwake. Pia tunazitaka nchi za kiislamu kubeba majukumu yao mbele ya Allah na mbele ya raia wao na mbele ya historia itakayoandikwa; kukemea kwa mdomo tu haitoshi, lazima ifuatiwe na vitendo kwa kadri ya wanavyoweza, na wanaweza kufanya mengi na makubwa kwa ajili ya Palestina iliyobarikiwa pamoja na watu wake waliopiga kambi kuilinda nchi hio, wapelekewe misaada ya kifedha na ya kibinadamu na kuwasaidia kwa njia zote ambazo zitapelekea kuukomoa uvamizi huu wa kizayuni na kuukomboa msikiti wa Masjid al-Aqsa na sehemu takatifu.

Ni juu ya ulimwengu wa kiislamu serikali na raia kuwajibika na kubeba majukumu yao ya kihistoria ya kusimamisha uvunjifu huu na kuwasaidia wapalestina katika mapambano yao dhidi ya janga hili hatarishi lililowafika. Kunusuriwa kwa Wapalestina si jambo zito kwa Allah, na Yeye Allah Ndie Mshindi wa mambo Yake lakini walio wengi hawalijui hilo.

Wabillah al-Taufiq

≋≋≋

≋≋≋

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Tamko Kuhusiana na Iraq

‘Kongamano la Fiqhi ya Kiislamu’ katika kikao chake cha kumi na tano (15) likiwa linaendelea kufuatilia matukio mazito yanayojiri hapo nchini Iraq, na njama hatarishi zinazosukwa zinazolenga umoja wake, na kile kinachotakikana cha kuleta na kupalilia fitna za kimadhehebu na za kikabila zitazoweza kuvunja umoja na mshikamano wa watu wa Iraq, fitna hizi zikifanikiwa zitaiangamiza nchi nzima na kuwasha moto wa maangamizi na mgawanyiko na kufungua milango iwe wazi kwa maadui wanaoisubiria fursa hii kwa umma.

‘Kongamano la Fiqhi ya Kiislamu’ na kutokana na nafasi yake katika ulimwengu wa kiislamu na kwa kutambua nafasi ya wanazuoni; linakemea kwa nguvu kabisa njama zote hizi zinazosukwa dhidi ya nchi ya Iraq.

Aidha, linatangaza kusimama pamoja na watu wa Iraq na kuwaunga mkono katika juhudi zao za kuzuia fitna hizi na kuendelea kupigani umoja wa watu wa Iraq na watokane na athari mbaya za uvamizi dhalimu (wa Marekani na Uingereza), na kuwarudishia heshima yao na utawala wao ndani ya mda mfupi unaowezekana pamoja na kulinda haki zote kwa misingi ya uadilifu na undugu.

Hakika ya ‘Kongamano’ linawataka Wairaq wote; waarabu, wakurdi, waturkumani, masunni, mashia na makundi mengine yote ya kisiasa na kikabila wasimame kitu kimoja safu moja ili kuiepusha nchi na hatari zinazoizunguka, na kuwataka warudi katika safu ya umma wa kiislamu na kusimamia majukumu yao katika ngazi zote za kikanda na kimataifa.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Kumi na Sita (16) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Dubai, Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE)

30 Swafar (Mfungo Tano) - 5 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1425,

sawa na 9 – 14 Aprili, 2005

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 143 (1/16)

Yanayohusiana na 'Zaka kwa Akaunti Zilizobanwa (*Restricted Accounts*), Kampuni za Bima za Kiislamu, Bima za Fedha na Malipo ya Mwisho wa Kazi (Kustaafu)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Dubai, Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE), 30 Swafar (Mfungo Tano) - 5 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1425, sawa na 9 – 14 Aprili, 2005.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Zaka kwa Akaunti Zilizobanwa, Kampuni za Bima za Kiislamu, Bima za Fedha na Malipo ya Mwisho wa Kazi (Kustaafu),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Zaka za akaunti za awekezaji:

a) Ni wajibu kutolewa zaka kwenye akaunti za uwekezaji na kwenye faida zake, wamiliki wa akaunti hizi watizame iwapo masharti ya utoaji zaka yametimia nisawa akaunti zenyewe ziwe ni za mda mrefu au mda mfupi, hata kama pesa haziwezi kutolewa kwa kua akaunti yenyewe imebanwa na chombo cha uwekezaji au na mwenye akaunti.
b) Aidha, ni wajibu kutolewa zaka kwenye akaunti za hundi (*current accounts*), haijalishi pesa hizo zimekusudiwa mahitajio ya mwenye akaunti au zimekusudiwa kuingizwa kwenye miradi ya uwekezaji, ila ikiwa zimekusudiwa kulipia madeni yaliofika wakati wake.

Mbili: Zaka za akaunti zilizodhibitiwa kama dhamana ya miamala:

a) Pesa za *Hamish al-Jidiyyah* (ni pesa zinazowekwa kuthibitisha utayari wa kutimiza ahadi inayolazimu na kutumia pesa hizo iwapo ahadi haikutimizwa), iwapo pesa hizi hazikuwekwa kwenye akaunti ya

uwekezaji, au dhamana ya mwanzo ya kuingia kwenye uzabuni, basi zitakua na makato ya zaka kwa ile sehemu zilikowekwa pesa hizi, na mmiliki wake atazitolea zaka pamoja na pesa zake nyingine, ikiwa imepita miaka kadha; zinatolewa zaka za mwaka mmoja wakati pesa hizo zimerudishiwa wenyewe, ama pesa hizi zikiwa kwenye akaunti ya uwekezaji basi hukmu ya (Moja: a) itafanya kazi.

b) Pesa zilizotolewa kama dhamana ya uzabuni (*security for tenders*), pesa zinazochukuliwa kutoka kwa watu au taasisi kama dhamana ya huduma za simu, umeme, kukodi sehemu au vifaa, pesa hizi zitatolewa zaka za mwaka mmoja pale zinaporudishiwa wenyewe.
c) Pesa za '*Urbuni*'; muuzaji hatakiwi kuzikata kutoka kwenye mali yake ya zaka, bali inamlazimu azitie hesabuni wakati wa kuhesabu zaka kwa kua pesa hizo ni milki yake; sawa mnunuzi amefuta mkataba au ameendelea nao.

Tatu: Akiba ya Kikanuni (*legal Deposit*):

Nazo ni pesa zinazoshurutishwa na taasisi rasmi husika ziwekwe kwenye benki kwa minajili ya kampuni fulani kuruhusiwa/kupewa leseni, iwapo pesa hizi zitawekwa kwa kipindi fulani tu basi kampuni husika wataziingiza kwenye hesabu ya zaka pamoja na pesa zao nyingine, ama ikiwa pesa hizi zitakaa siku zote basi zitatolewa zaka zake pale zitakaporejeshwa.

Nne: Pesa za Akiba na za Faida Zinazohamishiwa (*zinazowekwa au zinazozungushwa kwenye uwekezaji)*:

Zinatolewa zaka pamoja na pesa nyingine za kampuni, ikiwa patatumika njia ya kuhesabu mali ya usuli yaliyopo kwenye mzunguko kwenye hesabu za zaka za makampuni.

Tano: Zaka za Makampuni ya Bima ya Kiislamu:

a) Pesa za malipolgharama za kiufundi, pesa za akiba zinazodaiwa na 'Bima-Jumuishi, pesa za kuwalipa wateja-wastahiki na pesa za akiba zinazosubiri madai ya wateja; pes azote hizi hazitolewi zaka kwa kua ni madeni ya wengine.
b) Pesa za akiba na zilizowekwa kwa minajili ya hali za dharura, akiba za

‘bima ya maisha’ na pesa zilizowekwa kwenye ‘Bima-Jumuishi zinatolewa zaka kwa kua ni milki ya kampuni.

Sita: Posho za mwisho wa kazi (kustaafu):

Posho za mwisho wa kazi kwa muajiriwa na mfanyakazi:

a) **Posho za mwisho wa kazi:** Ni stahiki za kifedha zilizowekwa kisheria au na mkataba wa kazi kwa masharti waliyokubaliana, pesa hizi zinakadiriwa kwa idadi ya miaka ya kazi ni kiwango cha mshahara wa muajiriwa/mfanyakazi, pesa hizi zinalipwa wakati wa kustaafu, analipwa muajiriwa/mfanyakazi au familia yake. Muajiriwa au mfanyakazi hawajibiki kuzilipia pesa hizo zaka wakati bado yupo kazini, kwa kua bado hajazimiliki, lakini pale tu yanapotoka maamuzi ya kuainishwa na kukabidhiwa pesa hizo zote kwa wakati mmoja au kwa awamu mbalimbali basi pesa hizo zinakua sasa ni milki yake na ataanza kuhesabu zaka zake pamoja na pesa zake nyingine.

b) Pensheni ya Kustaafu (Mafao): Ni pesa za kila mwezi anazostahiki muajiriwa au mfanyakazi kutoka serikalini au taasisi husikabaada ya kumaliza mda wa kazi yake kwa mujibu wa sheria na kanuni na mikataba ya kazi, pesa hizi zinatolewa zaka kwa namna ilivyoelezewa kwenye kipengele cha: (Sita: a) kuhusiana na ‘*Posho za mwisho wa kazi*’.

c) Zawadi za Kustaafu: Ni pesa zinazolipwa mara moja na serikali au taasisi husika kwa muajiriwa/mfanyakazi kwa mujibu wa kanuni za ‘mfuko wa bima ya kijamii’ iwapo ametimiza masharti na vigezo vya kustahiki ‘pemsheni ya kustaafu’, pesa hizi zinatolewa zaka kwa namna ilivyoelezewa kwenye kipengele cha: (Sita: a).

d) Malipo Yaliyotokana na Akiba: Hiki ni kiwango fulani cha pesa ambacho muajiriwa/mfanyakazi alikua akikatwa kwenye mshahara wake na serikali/kampuni ikiongeza kiwango fulani, pesa hizi zinawekezwa ambapo muajiriwa/mfanyakazi anapewa kwa wakati mmoja pale anapomaliza kazi au kulingana na sheria zinazotumika.

Hapa pana khilafu kuhusu hukmu ya utoaji wa zaka kulingana na aina ya akaunti ambayo pesa hizo ziliwekwa; ikiwa ziliwekwa kwenye akaunti mahususi ya ‘muajiriwa/mfanyakazi’ na alikua na hiari ya kuchagua kuwekeza basi pesa hizo zitaingia kwenye hesabu ya utoaji zaka kwa vigezo viwili; mzunguko wa mwaka na kufikia *nisab* (kiwango cha kutoa zaka), ama iwapo hakua na hiari ya kuchagua basi hawajibiki kutoa zaka juu ya pesa hizo kwa kukosekana umiliki juu yake, lakini wakati anapokabidhiwa pesa hizo; atazitolea zaka za mwaka mmoja.

Zaka za mwisho wa kazi kwa taasisi na makampuni:

Posho za mwisho wa kazi, Pensheni ya Kustaafu (Mafao), Zawadi za Kustaafu zilizopo kwenye taasisi binafsi na makampuni, na Malipo Yanayotokana na Akiba yaliyopo kwenye akaunti za taasisi binafsi au makampuni hayatoki nje ya umiliki wa taasisi/kampuni hizo, kwa hio zinaingizwa pamoja na pesa zao nyingine kwenye hesabu ya utoaji zaka. Ama pesa hizi zikiwa kwenye mashirika ya umma ya kiserikali basi hazitolewi zaka, kwa kua ni sehemu ya mali ya umma.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 144 (2/16)

Yanayohusiana na 'Mzozo baina ya Mume na Mke Muajiriwa'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Dubai, Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE), 30 Swafar (Mfungo Tano) - 5 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1425, sawa na 9 – 14 Aprili, 2005.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Mzozo baina ya Mume na Mke Muajiriwa,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kutandukana kwa Dhimma ya Kifedha baina ya Mume na Mke:

Ijulikane kua mke ana dhimma yake ya kifedha iliyo huru kikamilifu, aidha, ana haki kamili kwa mujibu wa sharia juu ya kile anachokichuma kutokana na kazi yake, pia anamiliki mali yake mwenyewe, na kwa hili ana haki kutumia na kusarifu kile anachomiliki, mume hapa hatakua na usimamizi juu ya mali yake na wala hahitaji idhini au rukhsa ya kumiliki na kusarifu mali yake.

Mbili: Matumizi ya Mke (*Nafaqah*):

Mke anastahiki kupewa matumizi yake kamili kama mke kwa kadri ya uwezo wa mume na kwa mujibu wa mila na desturi za kijamii zinazotumika na zinazokubalika kisharia, malipo haya hayafutiki ila itokeapo mke ameasi *nushooz*.

Tatu: Kazi ya mke nje ya nyumba:

a) Miongoni mwa majukumu-msingi ya mke ni kusimamia familia yake na kulea watoto wake na kuandaa kizazi cha baadae, ni haki yake – panapotokea dharura – kufanya kazi nje ya nyumba yake; kazi

ambazo zitawafikiana na maumbile yake kama mwanamke na kwa mujibu wa desturi zinazokubalika kisharia na kwa masharti ya kujisitiri na kufuata hukmu za kisharia na adabu zake juu suala hilo; yote hayo bila ya kuharibu kazi yake ya msingi nyumbani.

b) Kutoka kwa mwanamke nje ya nyumba yake kwa ajili ya kufanya kazi hakumpotezei haki yake ya *nafaqah* (matumizi ya mke) aliowajibika nayo mume kisharia kwa mujibu wa vigezo vya kisharia, ila ikiwa kutoka kwake huko kunapakana na kuasi *nusooz* ambayo inamuangushia haki ya *nafaqah*.

Nne: Kushirikiana na mke kwenye matumizi ya familia:

a) Mke hawajibiki kushiriki kwenye matumizi (*nafaqah*) ya familia kisharia; hili ni jukumu la mume kimsingi na haijuzu kumlazimisha mke kwa hilo.
b) Anapojisikia mke kwa hiari yake kuchangia kwenye matumizi ya familia basi hilo ni jambo zuri; kwani litaonyesha maana halisi ya kusaidianam kushirikiana na uwiano baina ya mume na mke.
c) Inajuzu kwa mume na mke kukubaliana kwa ridhaa juu ya matumizi ya mashahara au malipo ya mke.
d) Iwapo kutoka kwake mke kwa ajili ya kufanya kazi kuna gharama za ziada basi atalipa yeye mke.

Tano: Kuweka sharti ya kufanya kazi:

a) Inajuzu kwa mke wakati wa kufunga ndoa kuweka ‘sharti ya kufanya kazi’ nje ya nyumba, iwapo mume ameridhia hilo basi atalazimika nalo, na ushurutishaji huu wakati wa ndoa unatakiwa ufanyike kwa uwazi.
b) Inajuzu kwa mume kumtaka mkewe kuacha kazi ya nje licha ya kua aliidhinisha mwanzo, ikiwa kwenye kuacha huko kuna maslahi ya familia na watoto.
c) Haijuzu kisharia kufungamanisha idhini (au ushurutishaji) kwa mke kufanya kazi nje ya nyumba na kushiriki kwake kwenye matumizi (*nafaqah*) ya familia ambayo ni jukumu la mume kimsingi, au mume kumtaka mkewe amgawie sehemu ya mshahara wake au chumo lake.
d) Haifai kwa mume kumlazimisha mke wake kufanya kazi nje ya nyumba.

Sita: Kushiriki kwa mke katika umiliki:

Iwapo mke amechangia kutoka mali yake au chumo la kazi yake katika kumuliki nyumba wanayoishi, nyumba ya biashara au mradi wa biashara; basi atakua na haki ya umiliki wa nyumba hio au mradi huo kwa kiwango (asilimia) cha mali ya ushiriki wake.

Saba: Utumiaji mbaya wa haki ya kufanya kazi:

a) Maisha ya ndoa ni haki na majukumu ya pande mbili baina ya mume na mke, haki hizi na majukumu haya yameainishwa na sharia, na uhusiano baina ya mume na mke unatakiwa ukae kwenye misingi ya uadilifu, kushirikiana, kunusuriana na kuoneana huruma, ni haramu kisharia kuharibu misingi hio.
b) Haijuzu kwa mume kuitumia vibaya haki yake kwa kumnyima mke kufanya kazi nje au kumtaka aiache kazi yake, ikiwa ana lengo la kumdhuru, ila ikiwa kufanya kazi kwake nje kuna ufisadi na madhara makubwa kuliko maslahi yanayotarajiwa na kazi hio.
c) Hukmu hii pia inatumika kwa mke iwapo anakusudia kwa kazi yake nje kumdhuru mumewe au familia yake au kufanya kazi kwake nje kuna madhara makubwa kuliko maslahi yanayotarajiwa na kazi hio.

Inausiwa yafuatayo:

- ‘Kongamano’ linausia kuandawe tafiti za kijamii, kiuchumi na kiutabibu juu ya athari zinazoweza kujitokeza za mke kufanya kazi nje ya nyumba kwa familia yake na kwake yeye binafsi, tafiti hizi zitasaidia sana kuweka bayana suala hili, sampuli za tafiti zichukuliwe kutoka jamii mbalimbali.
- ‘Kongamano’ linaweka msisitizo juu ya ulazima wa kupalilia mbegu za ‘dhana ya ukamilishanaji’ naina ya mume na mke na kwamba uislamu unapigania uwepo wa mahusiano baina yao kwa misingi ya mapenzi na huruma.
- Kuandawe ‘Warsha mahsusi’ itakayoangazia mambo ya mwanamke wa kiislamu kiujumla na nafasi yake katika kuikuza na kuiendeleza jamii ya kiislamu, kwa namna ambayo inawiana na mwenendo mzima

wa maendeleo ya kiustsaarabu kwa mujibu wa vigezo vya kisharia, yatoke mapendekezo yatakayowasilishwa ili yaw ni 'Maamuzi ya Kongamano' yatakayowasilishwa kwenye serikali na taasisi za kiislamu na hatimae kufikishwa kwenye mikutano ya kimataifa kuhusiana na kadhia ya 'mwanamke na wakaazi wa dunia'.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 145 (3/16)

Yanayohusiana na 'Utekelezaji wa kisasa wa mfumo wa '*Aaqilah*' na uwajibikaji wa fidia (*familia kuu inayosimamia fidia ya mmoja wao*)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Dubai, Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE), 30 Swafar (Mfungo Tano) - 5 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1425, sawa na 9 – 14 Aprili, 2005.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Utekelezaji wa kisasa wa mfumo wa '*Aaqilah*' na uwajibikaji wa fidia (*familia kuu inayosimamia fidia ya mmoja wao*),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Fasili ya *'Aaqilah*': *Aaqilah*: Ni sehemu (taasisi) au kundi la watu (ukoo) wanaobeba jukumu la kulipa fidia kwa niaba ya alietenda kosa la jinai la kuua bila kukusudia, bila ya kua na haki ya kumrudia mkosaji na kumtaka alipe fidia hio. Kisharia hili ni jopo la wanafamilia na walio wa karibu miongoni mwa watu wake katika kunusuriana na kusaidiana.

Mbili: Wasichowajibika nacho *Aaqilah*: *Aaqilah* hawawajibiki kulipa fidia ya mauaji ya makusudi wala makubaliano ya suluhu wala kukiri makossa.

Tatu: Utekelezaji wa kisasa: Katika mazingira ya kukosekana kwa ukoo au jopo la kabila watakaobeba jukumu la fidia, kwa kua msingi wa *Aaqilah* ni kunusuriana na kusaidiana basi inajuzu jukumu hili kubebwa kwa niaba yao, wakati wa dharua na wafuatao:

a) Bima ya Kiislamu (shirikishi au saidizi) ambayo inasema kwenye sheria yake kua: itabeba fidia kwa wanachama wake.
b) Vyama na miungano ya wafanyakazi iwapo imeelezewa kwa uwazi kwenye katiba zao kua wanalenga kusaidiana na kubeba gharama za mmoja wao.
c) Mifuko maalum inayoasisiwa na wafanyakazi wa sekta ya umma na ya binafsi kwa lengo la ushirikiano na kusaidiana miongoni mwa wanachama.

Nne: Nyasia:

- ‘Kongamano’ linausia serikali na nchi za kiislamu mbalimbali kuweka kwenye sheria zao vifungu maalum vitakavyolinda haki ya fidia na kwamba hakuna damu itakayopotea bila ya fidia katika uislamu.
- Kuzitaka taasisi husika kufanya wawezavyo kuhamasisha roho ya ushirikiano na kusaidiana katika wanajamii mbalimbali na vikundi vyenye mafungamano ya kijamii, jambo hili linaweza kufanyika kwa njia zifuatazo:

    a) Kuweka ‘Dhana ya kubeba fidia’ kwenye kanuni na katiba za vikundi na vyama mbalimbali.
    b) Kampuni za ‘Bima ya Kiislamu’ katika nchi za kiislamu mbalimbali zisimamie uingizwaji wa ‘fidia’ kwenye malipo ajali kwa masharti mepesi na awamu zamalipo muwafaka.
    c) Nchi za kiislamu zichukua hatua ya ‘kuibebesha hazina ya umma’ jukumu la fidia panapokosekana *Aaqilah*, ikiwa ni sehemu ya malengo ya hazina hio kwa jamii, miongoni mwayo ni kubeba jukumu la fidia mbali na nafasi yake ya kiuchumi.
    d) Jamii za waislamu (*Muslim minorities*) wanaoishi katika nchi zisizokua za kiislamu kote duniani zinatakiwa waanzishe taasisi za kusaidiana na kushirikiana miongoni mwao zitakazosema kwa

uwazi kua zitasimamia malipo ya mauaji ya kimakosa kwa mujibu wa mfumo wa sharia.

e) Kuelekeza ujumbe kwa serikali, mashirika, jumuia na taasisi za kijamii kuzifanyia kazi shughuli za wema wa kibinadamu kama vile: zaka, waqfu, Nyasia na michango ili zisaidie kwenye mzigo wa ulipaji wa fidia itokeapo mauaji ya kimakosa.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 146 (4/16)

Yanayohusiana na 'Tafsiri Mpya za Qur'an na za Maandiko Mengine ya Kidini'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Dubai, Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE), 30 Swafar (Mfungo Tano) - 5 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1425, sawa na 9 – 14 Aprili, 2005.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Tafsiri Mpya za Qur'an na za Maandiko Mengine ya Kidini,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Hiki kinachoitwa: 'Tafsiri mpya ya maandiko ya kidini' ikiwa itapelekea kupotosha maana halisi ya makusudio ya maandiko matakatifu hata kama ni kwa kutegemea kauli zilizo hafifu zinazopotosha na kile kilichokubaliwa kwa *ijma* na wanazuoni, na ikawa inapingana na uhalisia wa kisharia basi jambo hili uzushi (*bid'ah*) mchafu na hatarishi kwa jamii za kiislamu na utamaduni wao na maadili yao, ijulikane kua baadhi ya walioingia kwenye mkumbo huu unaoitwa: '*tajdeed*' (kufanya upya) wameangukia hapo kwa kutojua vigezo vinavyokubalika vya tafsiri kisharia.

Hali hii hatarishi imeanza kudhihiri pale baadhi ya vyuo vikuu vilipopitisha mitaala ya tafsiri aina hizi na kueneza machapisho na vitabu na kushajiisha wanafunzi wao wa degree ya kwanza, ya pili (uzamili) na hata ya tatu (uzamivu) waandae tafiti zihusuzo kadhia hii ya 'tafsiri mpya ya Qur'an' na kuwaalika vinara wa kasumba hii kwenye mihadhara na kuchangia kwenye warsha tatanishi na kuzisambaza kazi zao hizi kwa lugha mbalimbali na uwepo wa baadhi ya taasisi zinazochangia usambazaji wa kasumba hizi na vitabu vyao vilivyosheheni sumu.

Mbili: Kulingana na hayo sasa imekua kupambana na kasumba hizi na wimbi hili ni jambo la '*faradhi ya kifaya*', ni lazima lipatikane jopo litakalosimama kidete kuondosha hatari hii, wanaweza kufanya kaziz hii kupitia njia hizi:

- Kuzitaka serikali za kiislamu kupambana na janga hili hatarishi na kutofaotisha baina uhuru wa mawazo wa unaolenga kujenga na kuheshimu misingi ya dini na ule uhuru legevu unaobomoa, aidha, kuzita serikali za kiislamu kuchukua hatua muafaka na kuzipiga darubini taasisi za uchapishaji, utamaduni na mawasiliano-habari ili zijihusishe zaidi kutoa taarifa sahihi na kuelimisha umma juu ya mafundisho ya uislamu hususan kwa kizazi kipya na wanafunzi wa vyuo vikuu, kadhalika kuelimisha umma juu ya taratibu za kisharia za suala zima la '*ijtihad*' na tafsiri ya Qur'an iliyo sahihi na sherhe sahihi za Hadith za Mtume SAW.
- Kutumia mbinu stahiki (kama vile: warsha za hoja) kuongoza watu katika uzamivu wa kusoma elimu za sharia na misamiati yake, na kushajiisha '*ijtihad*' iliyodhibitiwa kwa vigezo vya kisharia na misingi ya lugha ya kiarabu inayojulikana.
- Kupanua wigo wa majadiliano na kundi hili liliothirika na kasumba hizi.
- Kushajiisha wataalamu wabobezi wa fani 'masomo ya kiislamu' kuandaa *radd* za kielimu na kuhoji fikra hizo katika nyanja mbalimbali hususan kwenye mitaala ya elimu.
- Kuelekeza wanafunzi ngazi za uzamili kwenye fani za aqeeda, hadith na sharia kuchagua maudhui za tafiti zao kubainisha ukweli wa mambo juu ya suala hili na kuweka *radd* stahiki kwa madai yao na mawazo yao potofu.
- Kuunda vikosi-kazi chini ya mwavuli wa 'Kongamano la Fiqhi ya Kiislamu' Jeddah na kuanzishwa kwa maktaba jumuishi ya vitabu na machapisho yanayohusiana na maudhui haya ikifuatilia na ku*radd*, ikiwa ni sehemu ya kuandaa tafiti bobezi na za uhakika, na kuwaunganisha watafiti wengine kupitia taasisi za kiutafiti mbalimbali za ndani na nje ya ulimwengu wa kiislamu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 147 (5/16)

Yanayohusiana na 'Bidhaa za Kimataifa na Vigezo vya Kuamiliana Nazo'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Dubai, Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE), 30 Swafar (Mfungo Tano) - 5 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1425, sawa na 9 – 14 Aprili, 2005.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Bidhaa za Kimataifa na Vigezo vya Kuamiliana Nazo,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ta Maamuzi ya Kongamanho namba 63 (1/7) yanayohusiana na 'Masoko ya Pesa' ambapo ilielezewa kua:

"Miamala ya bidhaa kwenye masoko yanayosimamia inafanyika kupitia mojawapo ya njia nne zifuatazo:

Njia ya kwanza: *Uwepo wa kifungu kwenye mkataba wa mauzo kinachohakikisha haki ya mnunuzi kukabidhiwa bidhaa aliyoinunua na haki ya muuzaji kukabidhiwa thamani ya bidhaa aliyoiuza; bidhaa husika iwepo wakati wa muamala au risiti inayowakilisha umilikaji wa hio bidhaa kwa mnunuzi. Mkataba huu unajuzu Kisharia kwa masharti ya mauziano yanayojulikana.*

Njia ya pili: *Uwepo wa kifungu kwenye mkataba wa mauzo kinachohakikisha haki ya mnunuzi kukabidhiwa bidhaa aliyoinunua na haki ya muuzaji kukabidhiwa thamani ya bidhaa aliyoiuza papohapo chini ya dhamana ya menegimenti ya soko. Mkataba huu unajuzu Kisharia kwa masharti ya mauziano yanayojulikana.*

Njia ya tatu: *Mkataba unaahidi kukabidhi bidhaa iliyoainishwa hivi sasa lakini itakabidhiwa baadae na malipo yafanyike wakati huo wa kukabidhiwa bidhaa,*

na kuweka sharuti kua muamala utakua umekamilika yanapofanyika makabidhiano ya bidhaa na thamani yake. Mkataba huu haufai kwa kua vyote viwili vinacheleweshwa, lakini badala yake wanaweza kuurekebisha mkataba huu ukawa ni mkataba wa 'Salam' kwa masharti yake yanayojulikana, ikifanyika hivyo basi inajuzu, aidha haijuzu kuuza bidhaa iliyonunuliwa kwa njia ya 'salam' kabla haijakabidhiwa.

Njia ya nne: *Mkataba unaahidi kukabidhi bidhaa iliyoainishwa hivi sasa lakini itakabidhiwa baadae na malipo yafanyike wakati huo wa kukabidhiwa bidhaa, lakini bila ya kuweka sharuti kua muamala utakua umekamilika yanapofanyika makabidhiano ya bidhaa na thamani yake, bali inawezekana kubadilisha mkataba kwa mkataba mwengine. Aina hii ya mikataba ndio inayotumika sana katika masoko ya bidhaa, lakini mikataba aina hii haijuzu.*"

Mbili: 'Baraza' limehoji, kwa mujibu wa tafiti zilizowasilishwa, aina mbalimbali ya miamala inayoendelea kwenye 'taasisi za fedha za kiislamu' na ikabainika kupitia mijadala hio kwamba kuna aina nyingi za utekelezaji na nyanja mbalimbali, aidha kunako tafsili nyingi zinazohitaji kubainishwa ili kufukia hukmu ya kisharia inayohusu: 'bidhaa za kimataifa na Vigezo vya Kuamiliana Nazo', kwa hio 'Baraza la Kongamano' linausia 'Sekreterieti Kuu' iandae 'warsha mahsusi' itakayoangazia yafuatayo:

1) Kubaini utekelezaji wa kiuhalisia wa miamala ya 'taasisi za fedha za kiislamu' katika masoko ya bidhaa ya kimataifa.
2) Utimizwaji wa vigezo vinavohitajika na vinavopaswa kuchungwa kupitia 'taasisi za fedha za kiislamu' katika miamala ya 'masoko ya pesa'.
3) Kuandaa tafiti za ziada katika nyanja mbalimbali za miamala hii ili kukamilisha mtazamo wa 'mas'ala ya bidhaa za kimataifa'.

Tatu: 'Baraza' linathamini 'Azma ya Serikali ya Dubai' ya kuanzisha 'soko la bidha la kimataifa' lenye makao yake makuu Dubai, ni matarajio yetu kua mradi huu utaziwezesha 'taasisi za fedha za kiislamu' kuepuka 'makatazo yanayopatikana kwenye masoko ya kimataifa' yaliyoangaziwa kwenye tafiti zilizowasilishwa, aidha, 'Baraza' linawausia wasimamizi wa mradi huu kujihusisha na nyanja za kisharia wakati wa kuandaa kanuni na taratibu za 'kazi za soko' na kutia bidi katika kuweka vitendea kazi vitakavofanya

shughuli zote za soko zinawiana na kuwafikiana na hukmu za sharia za kiislamu na misingi yake.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 148 (6/16)

Yanayohusiana na 'Udhamini wa Kibiashara'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Dubai, Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE), 30 Swafar (Mfungo Tano) - 5 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1425, sawa na 9 – 14 Aprili, 2005.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Udhamini wa Kibiashara,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Maana ya 'Udhamini wa Kibiashara':

Udhamini kisharia: ni kushikanisha dhimma ya mdhamini na dhimma ya mdhaminiwa (mdaiwa) kwenye madai ya madeni au vitu au kesi, udhamini huu sio ule udhamini wa kibiashara ambapo kunakua na makubaliano ya raia wa nchi kumuwezesha asiekua raia (mgeni) kutumia leseni ya kufanya kazi au kuanzisha miradi.

Mbili: Aina muhimu za Udhamini wa Kibiashara:

1) Raia alie na leseni ya biashara anakubaliana na mgeni (asiekua raia) afanye biashara kwa kutumia leseni hio lakini kwa gharama zote za rasilimali za mgeni pamoja na usimamizi wa kazi, raia hana jukumu lolote ispokua yale mambo rasmi ya kiserikali kama mmiliki wa leseni, raia anakua kama kwamba ndie mmiliki wa biashara hio.

2) Raia na mgeni wanashirikiana katika hali zinazoruhusiwa na kanuni, na raia anapokea malipo fulani ima mara moja au kwa awamu mbalimbali, wanakubaliana hivyo mkabala wa mgeni kutumia leseni ya biashara au mradi wa pamoja.

Tatu: Hukmu ya Udhamini wa Kibiashara:

1) Aina ya kwanza (kumtumia mgeni kwa leseni) hii ni aina mpya iliyozuka, si katika aina za 'udhamini' zinazojulikana kifiqhi wala si katika aina ya 'kampuni ya washirika', lakini hii ni haki ya *kimaanawi* anayoimiliki raia kwa mujibu wa kanuni ya nchi yake ambayo anampatia haki hio mwengine kwa malipo au bila ya malipo kwa njia ya biashara au *ijara* (kukodisha).

Muamala huu hauna katazo la kisharia iwapo hakuna *gharar* (udanganyifu), utatanishi na uvunjaji wa sheria.

2) Aina ya pili (kushirikiana katika utumiaji wa leseni) unafanyika kupitia mchango wa kifedha unaotolewa na raia pamoja na leseni, au atoe leseni pekee baada ya kuitia thamani kiuadilifu gharama zote na juhudi alizotumia kuipata leseni hio ili ziwe msingi wa kukadiria hisa zake anapoitoa leseni hio, na zitakua hisa za upande wa pili (mgeni, asiekua raia) ni mchango wa pesa atakazotoa kugharamia mradi husika; kiwango cha faida kuainishwa kwa mujibu wa mchango huu.

Muamala huu wa *Udhamini wa Kibiashara* unajuzu iwapo wamekubaliana kuanisha viwango vya faida vya kila mmoja wao na kubeba hasara (itokeapo) kila mmoja kwa mujibu wa hisa zake.

Inausiwa:

'Baraza la Kongamano' linausia na kuitaka 'Jumuia ya Nchi za Kiislamu' (OIC) kupitia taasisi zake za kiuchumi kubuni 'Soko la kiislamu la pamoja' na uhuru wa kutembea kwa biashara, fedha na watu kati ya nchi za kiislamu, jambo hili litasaidia pakubwa kuleta umoja wa kiislamu unaotamaniwa na kuleta manufaa makubwa kwa waislamu kama inavofanyika kwenye masoko ya kimataifa.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 149 (7/16)

Yanayohusiana na 'Bima ya Afya'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Dubai, Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE), 30 Swafar (Mfungo Tano) - 5 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1425, sawa na 9 – 14 Aprili, 2005.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Bima ya Afya,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) **Fasili ya Bima ya Afya:** Mkataba wa Bima ya Afya: Ni makubaliano ambayo, kwa mujibu wake, mtu au taasisi wanajilazimisha kulipia kwango fulani mara moja au awamu mbalimbali kwa taasisi husika ili taasisi hio isimamie gharama za matibabu au kulipia gharama ndani ya kipindi fulani.

2) **Njia za Bima ya Afya:** Bima ya Afya ima inafanyika kupitia taasisi ya tiba (Hospitali) au kupitia kampuni ya bima amabyo inakua kama mtu wa kati baina ya mteja wa bima na taasisi ya tiba.

3) **Hukmu ya Bima ya Afya:**

   a. Ikiwa bima ya afya inafanyika mubashara na taasisi ya tiba; basi inajuzu kisharia kwa vigezo ambavyo vinaifanya *gharar* kua chache

sana na inayosameheka ikilinganishwa na dharura iliopo ambayo ni ya kuokoa nafsi, akili, kizazi (heshima) amabvyo nivi ni miongoni mwa makusudio makuu yanayolindwa na sharia. Vigezo vinavokusudiwa ni kama vifuatavyo:

- Yawekwe maelezo bainifu yanayotaja majukumu ya kila upande.
- Kuidurusu hali ya kiafya ya mteja wa bima na uwezekano wa afya yake kuzorota.
- Madai ya malipo ya taasisi ya tiba kwa taasisi ya bima yawe ni kwa mujibu wa huduma halisi na sio madai hewa kama inavyofanyika kwenye makampuni ya bima za biashara.

b. Ikiwa bima ya afya ni kupitia kampuni ya bima ya kiislamu (shirikishi au saidizi) inayofanya shughuli zake kwa mujibu wa vigezo vya kisharia vilivopitishwa kwenye 'Maamuzi ya Kongamano' namba 9 (9/2) yanayohusiana na bima na bima-jumuishi; basi inajuzu.

c. Ikiwa bima ya afya ni kupitia kampuni ya bima ya kibiashara; basi haijuzu kama ilivobainishwa kwenye 'maamuzi' yaliyoashiriwa hapo juu.

Nne: Usimamizi na udhibiti: Ni juu ya taasisi husika kusimamia na kudhibiti shughuli za 'bima ya afya' kwa taratibu za kiuadilifu na kuondosha utatanishi na kulinda watumiaji (wateja) wa bima dhidi ya uporwaji.

'Baraza la Kongamano' linausia yafuatayo:

1) Kuzitaka serikali za kiislamu, jumuia za misaada na taasisi za nyakfu kuchangia mfuko wa 'bima ya afya' ili wasio na uwezo wapate huduma za afya ima bure aua kwa bei nafuu kwa kuwawezesha kupata bima ya afya kutoka sekta binafsi.
2) Kutotumia kadi za afya ispokua wamiliki wa kadi hizo waliosajiliwa; kinyume chake ni kukhalifu masharti ya mkataba na kufanya ghushi na udanganyifu.
3) Kutahadharisha utumiaji mbaya wa bima ya afya kama kudai ugonjwa au kuuficha au kutoa taarifa zisizokua sahihi.
4) Kuingiza maudhui ya 'Bima ya kiislamu (shirikishi au saidizi) kwenye

vikao vya ‘Kongamano’ vinavyokuja inshallah kwa mujibu wa natija na matokeo ya mikutano na warsha za mwisho na aina-tekelezi mbalimbali zilizodhihiri baada ya kutolewa ‘Maamuzi ya Kongamano’ yaliyotangulia.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 150 (8/16)

Yanayohusiana na 'Sisi na Wao'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Dubai, Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE), 30 Swafar (Mfungo Tano) - 5 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1425, sawa na 9 – 14 Aprili, 2005.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Sisi na Wao,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Kuchukua hatua zifaazo zitakazohakikisha umoja wa safu ya waislamu unapatikana pamoja na nchi zao ili tuweze kua na umma mmoja katika zama hizi, kufikialengo hili ni wajibu kuchukua hatua za makusudi za kuondosha tofauti zilizopo na kutanashati ushirikiano wa kiuchumi, kiutamaduni, kielimu na kisiasa miongoni mwa nchi za kiisalmu, na kutekeleza maamuzi ya jumuia ya nchi za kiislamu (OIC) mbalimbali yanayohusiana na jambo hili.

2) Ulazima wa kuratibu miongoni mwa nchi na mashirika ya kiislamu katika kutengeneza 'risala ya mawasiliano' iliyo wazi kabisa kuhusu uislamu, risala hii iw ndio msingi wa majadiliano na wengine (wasiokua waislamu), aidha, ipo haja ya kuandaa kizazi kipya cha wanahabari (wanamawasiliano) waislamu watakoifahamu risala hii vizuri na watakao kua na uwezo wa kuifikisha na kuielezea vizuri kwa lugha mbalimbali za dunia ili kuweza kupambana na mawimbi makali yanayoelekezwa dhidi ya uislamu na waislamu nyakati hizi.

3) Ni lazima kuwe na miradi ya pamoja sio kutoa na kupokea ruzuku, miradi ya kimaendeleo ya pamoja itakayoleta maslahi kwa wote,

kuelekeza ushirikia miongoni mwa nchi za kiislamu na nchi nyenginezo katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, kijamii, miutamaduni na kisiasa.

Mapendekezo:

1) ‘Kongamano’ linatoa wito kwa nchi wanachama, mashirika, vyuo vikuu na vituo vya kiislamu husika kuandaa mipango-mikakati ya kutoa machapisho na tafiti kwa lugha mbalimbali za dunia na katika maudhui mbalimbali zinazohusiana na kudhihirisha ukweli wa uislamu kama dini ya ulimwengu mzima na maisha na kujiepusha lugha za ‘u*chukivu*’ kwa wengine na kuweka msisitizo juu ya maadili ya uislamu, amani na ushirikiano katika kupambana na ufukara, njaa na maradhi, na kusaidiana kwenye maendeleo ya kukuza rasilimali na uwekezaji na miradi ya pamoja ambayo inaleta tija na manufaa kwa binadamu, na kuratibu juhudi hizo na ‘Kongamano’ kwenye machapisho.

2) Kuzitaka taasisi husika na masuala ya ‘mahusiano ya kimataifa’ katika ngazi za kiserikali au kiraia kuipatia ‘jamii ya kimataifa’ mazuri yanayopatikana katika uislamu kwa binadamu yakiwemo: maadili na misingi ya ushirikiano na ngome za amani duniani; kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za mashirika ya kimataifa kama vile: Umoja wa Mataifa (UM), Shirika la Kimataifa la Elimu na Utamaduni (UNESCO), na mashirika mengine ya kimataifa ya kiuchumi na kiviwanda. Kufanya kunahitajika mambo mawili:

   a. Kuwashirikisha wataalamu wabobezi kutoka vyuo vikuu na taasisi za kiislamu na nyenginezo wawe wajumbe wanaowakilisha nchi zao katika mashirika haya ya kimataifa, na kuandaa vizazi venye ufahamu kina na mpana ulio mzuri wa uislamu na misingi yake ya amani.
   b. Kuelekeza juhudi katika kutatua migogoro ya dunia kupitia mashirika ya kimataifa kwa njia ya uadilifu na kukataa kutoka nje ya uadilifu, kuendeleza ushirikiano ulioamrishwa na sharia ya kiislamu na mkundi mbalimbali duniani kwa lengo la kuinua ‘neno la haki na misingi ya amani na ushirikiano’; mambo yanayohimizwa na sharia ya kiislamu na pia misingi ya uadilifu na kanuni za kimataifa

zinashikiliwa na nchi za kimagharibi.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 151 (9/16)

Yanayohusiana na 'Kuchunga Waislamu Wachache (*Minoroties*) katika Nchi Zisizokua za Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Dubai, Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE), 30 Swafar (Mfungo Tano) - 5 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1425, sawa na 9 – 14 Aprili, 2005.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kuchunga Waislamu Wachache (*Minoroties*) katika Nchi Zisizokua za Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Inatakiwa kuaha kuwaita waislamu walioko nje ya ulimwengu wa kiislamu kua ni: "Wachache" (minorities) au "Wahamiaji" (immigrants), hii ni misamiati ya kikanuni na haielezei uwepo halisi wa waislamu; uislamu ambao ni unawakilisha ujumuishi, uasili, utulivu na uwiano wa kimaisha na jamii nyengine. Misamiati sahihi ya kuwaita waislamu ni kama: 'Waislamu waliopo nchi za magharibi (ulaya)', au 'Waislamu waliopo nje ya ulimwenngu wa kiislamu'.
2) Ni wajibu kuchukua hatua zote zifaazo kulinda na kuhifadhi uwepo wa waislamu nje ya nchi za kiislamu na kutetea mambo yao mahsusi ya kidini, kiustaarabu na kiutamaduni.
3) Ubebaji wa uraia wa nchi zaa kimagharibi haupingani na kuulinda utu wa kiislamu na kujilazimisha na maadili ya kiislamu.

Mapendekezo:

1) Kuanzishwa kwa kituo cha utafiti wa kisayansi kinachojihusisha na hali za waislamu waishio nje ya ulimwengu wa kiislamu, na kusahihisha uhalisia wa kiislamu kwa wasiokua waislamu.

2) Kuuda ‘kamati ya kifiqhi’ ndani ya ‘Kongamano’ itakayofuatilia kadhia mbalimbali za kifiqhi zinazowakabili waislamu nje ya ulimwengu wa kiislamu na kuzipatia suluhisho.
3) ‘Kongamano’ likishirikana na taasisi husika za ndani na nje ya nchi za kiislamu kuandaa semina-elekezi maalum kwa maimam na walinganiaji na wakurugenzi wa vituo vya kiislamu katika nchi zisizokua za kiislamu.
4) Kuwataka waislamu waishio nje ya nchi za kiislamu kuenndelea kuhifadhi misingi na mafundisho ya dini yao ya kiisslamu, na kuachana na tofauti za kimadhehebu, na badala yake kushikamana na umoja katika ibada zao.
5) Waislamu nje ya ulimwengu wa kiislamu wanatakiwa wawe mfano mwema wa ustaarabu wa kiislamu kupitia silka zao na waavyoamiliana na wengine.
6) Kuitaka ‘Jumuia ya Nchi za Kiislamu’ (OIC) kusaidia taasisi zinazojihusisha na mambo ya waislamu katika nchi zisizokua wanachama katika jumuia, na kuyafanyia kazi maamuzi yaliyotolewa na ‘Jumuia’ yanayohusiana na jambo hili.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Tamko Kuhusu *al-Quds* na *al-Aqsa*

Makundi ya kizayuni zaidi ya thelathinni (30) yenye mirengo mikali huko Palestina, baada yakutambua kua wana nguvu kiasi fulani na kwamba wanaweza kufanya chochote katika kuendeleza uadui na uvamizi na njama zao dhidi ya Masjid al-Aqsa uliobarikiwa; qibla cha mwanzo namsikiti wa tatu kwa utukufu, wanaendeleza hujma zao na kujaribu kuubomoa na kusigizia kua wanataka kujenga hekalu lao la “Sulaiman” linalodaiwa eti liko chini ya Masjid al-Aqsa. Makundi haya yamekua yakitafuta visingizio mbalimbali vya kutaka kuubomoa Masjid al-Aqsa na kua na majaribio ya mara kwa mara ya kutaka kuingia msikitini humo na kutekeleza ibada zao potofu ikiwaw ni ishara ya uvamizi wa msikiti huo na utekelezaji wa njama zao za kiuadui.

Baada ya utangulizi huo; ‘Kongamano la Fiqhi la Kiislamu’ katika kikao chake kilichofanyika ‘Dola ya Imaaraat za Kiarabu Zilizoungana (UAE) 30 Swafar (Mfungo Tano) - 5 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1425, sawa na 9 – 14 Aprili, 2005, na baada ya kupitia matangazo ya kiuadui na njama hatarishi za dhulma zinazotoka kwa viongozzi wa kizayuni wenye siasa kali dhidi ya mji wa al-Quds kwa ujumla na hasahasa Masjid al-Aqsa;

Hivyo basi imeamuliwa yafuatayo:

1) Mji wa al-Quds na Masjid al-Aqsa ni sehemu takatifu kwa waislamu wote ulimwenguni; kwa kua sehemu hizo zimefngamana na tukio la kimuujiza ya *israa* na *mi’raj* liloelezewa kwenye Qur’an.
2) Mji huu Msikiti wake ulioarikiwa ni milki za kiislamu kwa mujiu wa Quran tukufu na Sunnah za Bwana Mtume SAW, na kwamba jambo hili halikubali kupanguliwa au kubadilishwa au kupunguzwa, aidha, hakuna nafasi ya kuyagawa maeneo haya. Wanazuoni wa kiislamu wote walishakubaliana uharamu wa kumuachia adui mvamizi hata shubiri moja ya ardhi ya waislamu aliyoivamia adui huyu; hususan ardhi tukatifu.
3) Masjid al-Aqsa uliobarikiwa ni milki ya waislamu pekee, mayahudi hawahusiki katu na msikiti huo, na ni lazima watahadharishwe dhidi ya kuugusa au kuchafua utukufu wa msikiti huo, serikali ya uvamizi ya

kiyahudi na nchi zinaowasaidia watabeba jukumu kamili dhidi ya uchafuzi wa aina yoyote juu ya Masjid al-Aqsa. Msikiti huu haupo kwenye meza ya mazungumzo au kuwaachia mayahudi hata chembe moja ya msikiti huo, na hakuna yeyote anaemiliki kufanya hivyo, msikiti huu uko juu ya yote hayo.

4) Haiwezekani kupatikana kwa amani-adilifu na utulivu kwenye maeneo haya (Mashariki ya Kati) ila baada ya kuumaliza uvamizi wa kiyahudi juu ya Mji wa al-Quds na Masjid al-Aqsa na Wapalestia waliotolewa kurudi kwenye miji yao.
5) Ni haki ya Wapalestina kusimamisha dola yao huru juu ya ardhi yao na mji wao mkuu ukiwa ni al-Quds, ni haki yao vilevile kujilinda nafsi zao na kupambana na adui kwa njia (nguvu) zote zinazokubalika walizonazo hadi pale wliofukuzwa nchini mwao waweze kurudi katika nchi yao.

Aidha, ‘Kongamano’ linawataka viongozi wote na raia wa ulimwengu wa kiarabu na kiislamu wawajibike kidini, kitaifa na kihistoria katika kuutetea na kuulinda mji huu uliotekwa na kuvamiwa, na kusimama na watu wake wanaoendeleza mapambano hapo na kusaidia taasisi zao za kiafya, kielimu, kijamii na nyenginezo ili kuzuia uyahdishaji na utaifishaji wa mji wa al-Quds; uyahdishaji na utaifishaji ni jambo linalokataliwa na kamwe haliwezi kukubalika. Kazi ifanyike kwa nguvu zote kuondosha uvamizi wa kiyahudi juu ya ardhi ya *israa* na *mi’raj*.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Tamko Kuhusu Iraq

Katika kulifanyia kazi neno la Bwana Mtume SAW pale aliposema:

"من لم يهتم بأمر المسلمين فليس منهم"

"*Yeyote yule asiejihusisha na mambo ya waislamu basi si miongoni mwao*";

'Kongamano la Fiqhi la Kiislamu' katika kikao chake kilichofanyika 'Dola ya Imaaraat za Kiarabu Zilizoungana (UAE) 30 Swafar (Mfungo Tano) - 5 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1425, sawa na 9 – 14 Aprili, 2005, linafuatilia yale yanayojiri katika nchi ya Iraq iliovamiwa na masaibu yaliyowafaya Wairaq wote kua wahanga. Wairaq hawa walishaumia vya kutosha walipokua wakipambana na dhulma na udikteta, sasa wanajikuta wanasagika chini ya dhulma nyingine na uvamizi, na sasa imebainika kua vile visingizio viliyotumiwa kwa kuanzisha vita na kuivamia Iraq kumbe ni uongo mtupu, na wala hakujapatikana chochote katika kile kilichokua kinadaiwa cha eti kuwaokoa Wairaq dhidi ya udikteta.

Huu ukiwa ni mwaka wa pili tangu vita na uvamizi wa Iraq; Wairaq hawajaona ndani ya kipidi hiki ispokua maangamizi kwa nchi yao, kuuawa kwa wanasayansi wao, kumaliza nguvu zao na kupalilia fitna zza kimadhehebu na kiukabila zinazougawanya umma wa wairaq. Na jambo linazidi kumuhamasisha mvamizi kendelea na njama zake hatarishi za kuigawa nchi ya Iraq iwe vipande vipande na kuzidi kuuvunja umoja wa wairaq.

Sisi, wanazuoni tunaokutana hapa Dubai katika kikao cha 'Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu' tunawasihi ndugu zetu wote wa Iraq iliyojeruhiwa na iliyovamiwa; waamke na washikamane na Kamba ya Mwenyezi Mungu (ya Umoja) na wasimame kwa nguvu wakiwa kwenye safu moja iliyoungana dhidi ya mikakati na njama zinazosukwa dhidi yao, aidha, tunawataka washike njia itakayomaliza uvamizi huo na kuirudishia Iraq heshima yake na utawala wake na kuijenga nchi ya Iraq ikiwa imeungana na huru yenye amani na nguvu, na katu wasiweke nafasi ya

udikteta. Tunaitaka Iraq ibaki kwenye mfumo wa kiislamu na uadilifu wake; mbali na ukakasi wa kimadhehebu unaochukiza.

Tukiwa tunalaani na kuchukizwa na ufisadi wowote katika mgongo wa ardhi; tunakataa aina zote za uadui, dhulma na ufisadi, tunayataka mashirika ya kikanda na Umoja wa Mataifa na wapenda amani, uhuru na uadilifu kote duniani waweke ukomo wa hiki kinachoendelea na masaibu wanayoyapitia Wairaq ambayo yameifanya nchi nzima kuchafuka na kuhatarisha amani ya eneo lote.

Na wakati huohuo tunafuatilia juhudi zinazoendelea hapo Iraq za kuweka taasisi za kikatiba, tuna imani kubwa kua hakuna Muiraq yoyote ila ana shauku ya kutaka kuiona Iraq ikiwa imeungana na huru na inajitawala yenyewe. Tunamuomba Allah SWT Awape Wairaq kheri nyingi na taufik ya kujikomboa na athari zote za uamizi na wajichagulia mustakbala wao na katiba yao na taasisi za kikatiba, na waweze kusimamia uchumi wao ulioporomoka na waimarishe mahusiano yao na nchi jirani na wachukue nafasi yao katika nyanja za mshikamano wa kiislamu na kimataifa na kufukia malengi makuu ya umma wa kiislamu ya amani ulimwenguni kote.

Wabillah al-Taufiq

≋≋≋

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Kumi na Saba (17) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Amman, Falme ya Kihashimi ya Jordan (HKJ)

28 Jumada al-Uula (Mfungo Nane) - 2 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1427,

sawa na 24 – 28 Juni, 2006

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 152 (1/17)

Yanayohusiana na 'Uislamu: Umma Mmoja Madhehebu Mbalimbali ya Kiitikadi, Kifiqhi na Kielimu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Amman, Falme ya Kihashimi ya Jordan (HKJ) 28 Jumada al-Uula (Mfungo Nane) - 2 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1427, sawa na 24 – 28 Juni, 2006.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Uislamu: Umma Mmoja Madhehebu Mbalimbali ya Kiitikadi, Kifiqhi na Kielimu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na kujikumbusha 'maamuzi ya mkutano wa kiislamu wa kimataifa' uliofanyika mwaka 1425 Hijria (2005), ambao ulitoa wito wa kudurusu na kufanyia kazi maelekezo yaliyotolewa kwenye 'Risala ya Amman'; risala ambayo tayari ilishabebwa na 'Jopo la wanazuoni na wanafikra' lililokutana Makkah al-Mukarramah kuandaa kikao-kilele cha dharura cha 'Jumuia ya Nchi za Kiislamu (OIC) cha tatu;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Tafiti zote zilizoandaliwa kuhusiana na maudhui haya zinakubaliana juu ya misingi mikuu ya uislamu, na kuchukulia kua madhehebu ya Kiitikadi, Kifiqhi na Kielimu; ni matunda ya *ijtihadi* za wanazuoni wa kiislamu kwa kusudio la kuwepesisha utendaji kazi, lengo kuu la ijtihada zote hizi na madhehebu haya ni kutilia nguvu umoja wa kiislamu na kuukwasisha kifikra na kuhakikisha uendelevu wa risala ya uislamu. Tafiti zilizowasilishwa kwenye maudhui haya pamoja na zile za '*Risala ya Amman*' zinashikana pamoja kwenye maelekezo yao ya kubainisha na kuweka wazi ukweli wa uislamu na nafasi yake katika jamii zza kisasa, kwa mnasaba huu tunapenda kutoa shukrani na kutathmini juhudi za Mstahiki Mfalme Abdalla Bin al-Hassan (II) wa pili, Allah Amuhifadhi; Mfalme wa

Falme ya Kihashimi ya Jordan, kwa kuibeba risala hio ya Amman na kuisambaza duniani kote.

Mbili: Kuweka msisitizo juu ya ‘maamuzi ya mkutano wa kiislamu wa kimataifa’ uliofanyika Amman, Jordan chini ya anwani: “Ukweli wa Uislamu na Nafasi yake katika Jamii ya Kisasa” na kuowanisha baina ya maazimio ya mkutano huu na yaliyopatikana kwenye tafiti na hoja juu ya maudhui haya. Ikimbukwe kua utangulizi wa maamuzi haya uliangazia fatwa na maazimio mbalimali ya taasisi za fatwa na ‘majopo ya maulamaa wakubwa’ wa madhehebu mbalimbali waliounga mkono maamuzi hayo; nayo ni:

1) Yeyote anaefuata mojawapo wa madhehebu manne ya *Ahl al-Sunnah Wal Jama’ah* (Hanafi, Maliki, Shaafi’I na Hanbali), madh’hab ya Ja’fari, madh’hab ya Zaydi, madh’hab ya Ibadhi na madh’hab ya Dhaahiri basi huyo ni muislamu na haijuzu kumkufurisha, na ni haramu kudhuru damu yake, heshima yake na mali yake. Aidha, na kwa mujibu wa fatwa ya Shaikh al-Azhar (Sheikh Mkuu wa Azhar): haijuzu kuwakufurisha wenye itikadi ya Kiash’ari na wanaojishughulisha na usufi wa ukweli, kadhalika haijuzu kwakufurisha wanaofuata fikra ya Salafi iliyo sahihi. Kiujmla haijuzu kukufurisha kundi lolote la waislamu wanaomuamini Allah SWT na Mtume wake SAW, na kuamini nguzo za imani na nguzo za uislamu, na hawakanushi mambo ya msingi ya kiislamu yanayojulikana.
2) Kinachounganisha baina ya madhehebu ni kingi na kikubwa kuliko kinachofarakanisha, waasisi wa madhehebu yote manane wanakubaliana juu ya misingi mikuu ya uislamu; wote wanamuamini Allah SWT kua Mmoja wa Pekee, na kuamini kua Qur’an tukufu ni maneno ya Allah Aliyoyateremsha na yaliyohifadhiwa na Allah na kulindwa dhidi ya uharibifu wa aina yoyote, na kumuamini Mtume Muhammad SAW kua ni Mtume wa Allah kwa binadamu wote. Pia wanakubaliana juu ya nguzo tano za uislamu: shahada mbili, swala, zaka, saum ya ramadhan na hajj, kadhalika wanakubaliana juu ya nguzo za imani: kumuamini Allah, malaika wake, vitabu vyake, mitume wake, siku ya mwisho na qadari ya kheri na ya shari. Tofauti zilizopo miongoni mwa wanazuoni na wafuasi wa madhehebu ni tofauti tanzu na baadhi ya misingi; na kutofaotiana huko ni rahma kwa umma, ndio

zamani wasomi walinena: “Kutofautiana kwa wanazuoni kimawazo ni rehema pana”.

3) Kuyatambua madhehebu katika uislamu inamaanisha kujilazimisha na manhaj maalum ya fatwa; hivyo basi haifai kwa mtu yeyote kutoa fatwa bila ya kua na taaluma ya kielimu inayomuwezesha kufanya hivyo, aidha hijuzu kufutu (kutoa fatwa) bila ya kufuata manhaj inayokubalika kimadh’hab, na haijuzu kwa yeyote kudai kua yeye amefikia kiwango (daraja) ya *ijtihad* na kuzua rai mpya au kutoa fatwa zisizokubalika zinazowatoa waislamu kwenye misingi ya sharia inayojulikana kwenye madhehebu husika.
4) Kiini cha maudhui ya ‘*Risala ya Amman*’ iliyotoka usiku wa tarehe 27 ya mwezi wa Ramadhan, 1425 Hijria (November 9, 2004), na iliyosomwa hapo ‘*Masjid al-Hashimiyin*’ ni kuyakubali madhehebu pamoja na *manahij* zinazokubalika na madhehebu hayo; utambulikano wa madhehebu na kusisitiza uwepo wa *hiwar* (mawasiliano/mdahalo) na mikutano ya pamoja yatasaidia kuleta uwiano na kusameheana na kuoneana huruma.
5) Tunatoa wito kwa waislamu wote kutupilia mbali tofauti zao na badala yake kuunganisha neno lao na safu yao, na kuheshimiana miongoni mwao, na kutilia nguvu umoja na mshikamano wa nchi zao na watu wao, na kuimarisha viunganishi vya undugu vinavyowaleta kwenye kupendana kwa ajili ya Allah, na wasiziachie fitna nafasi yoyote baina yao. Allah SWT amesema:

   “*Hakika Waumini ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mrehemewe*” (Surat al-Hujuraat: 10).

6) Washiriki wa ‘Mkutano wa Kiislamu wa Kimataifa’ - wakiwa wanakutana Amman, Jordan karibu kabisa na Masjid al-Aqsa na Ardhi za Palestina zilizokaliwa kimabavu – wanapenda kuweka msisitizo juu ya ulazima wa kuzidisha juhudi katika kuulinda Masjid al-Aqsa - qibla cha mwanzo na msikiti wa tatu kwa utukufu – dhidi ya uadui hatarishi, kwa kuondosha uvamizi na kuzikomboa sehemu takatifu, aidha, ulazima wa kuyahifadhi maeneo matakatifu ya Iraq na kwengineko.
7) Washiriki wanapenda kuweka msisitizo juu ya ulazima wa kuyafanyia

kazi maadili ya: uhuru, kuheshimu rai na mawazo ya wengine katika ulimwengu wa kiislamu... wal-Hamdulillah.

Tatu: Kuweka msisitizo juu a 'Maamuzi ya Kogamano' namba 98 (1/11) yanayohusiana na 'Umoja wa Kiislamu' na mapendekezo yaliyotolewa kuhakikisha umoja wa kiislamu unapatikana, kikao kilikhatimishwa kwa kuitaka 'Sekreterieti ya Kongamano' kuunda kamati kutokana na wanachama wake na wataalamu wake; kamati ambayo itakubaliwa na 'Jumuia ya Nchi za Kiislamu' (OIC) na shughuli zake ile iweke mpango-tekelezi, visaidizi na programu zitakazoleta umoja wa kiislamu katika nyanja za kiutamaduni, kijamii na kiuchumi.

Nne: Kuweka misingi mikuu ya kadhia zilizowafikiwa na kuzidhihirisha, ama kadhia ambazo bado kuna khilafu juu yake zitizamwe tena kwa misingi ya kisharia, wakati wa kuelezea kuhusu madhehebu kuwe na insafu na uaminifu bila upendeleo, kwa lengo la kuyakuza yanayotuunganisha na kuheshimiana kwa yale tunayokhitalifiana. Wakati wa kupima uzito wa madh'hab tunaangalia uzito wa dalili na anaekua karibu zaidi na makusudio makuu ya sharia, bila ya kulitanguliza dhehebu analolifuata au dhehebu lililoenea zaidi katika eneo husika au jamii fulani.

Tano: Kuwekwe kwenye vyuo vikuu na shule za sekondari (Thanawi) somo la '*Fiqh al-Wahda al-Islamia*' (Fiqh ya Umoja wa Kiislamu) na somo la 'Adabu za kukhtalifiana na mdahalo wenye kujenga' kwenye mitaal yao, aidha, wanafunzi wafundishwe kuheshimu rai na mawazo ya wengine.

Sita: Kukuza na kuhuisha madhehebu ya kielimu-malezi yanayofungamana na Kitab na Sunnah kama njia muafaka ya kupunguza makali mihemko ya *kimadia* (kidunia) iliyoenea zama hizi na kuvilinda vizazi vya sasa dhidi mifumo ya kimaadili inayokinzana na misingi ya kiislamu.

Saba: wanazuoni wa madhehebu mbalimbali wanatakiwa kuelimisha wafuasi wao juu ya 'mfumo wa uadilifu na ukatinakati' kwa kutumia mbinu mbalimbali zikiwemo: vikao vya pamoja, warsha za kielimu za tahasusi, mikutano ya umma pamoja na kufaidi kutokana na taasisi husika za

kujenga mahusiano mema (kukaribiana) ya kimadhehebu kwa lengo la kusahihisha mtazamo wa madhehebu ya kiitikadi, kifiqhi na kielimu, kwa mantiki ya kua hii ni mifumo mbalimbali ya utekelezaji wa misingi ya kiislamu na hukmu zake, na tuchukulie utofauti uliopo baina ya madhehebu ni tofauti za kukamilishana na sio za kupingana, aidha, kuwe na ulazima wa kuwaelemisha watu juu ya misingi na mazuri yanayopatikana kwenye kila dhehebu.

Nane: Ijulikane kua kuheshimu madhehebu isiziwie ukosoaji wenye kuujenga unaolenga kutilia nguvu mshikamano na ukaribu na kubana mianya ya ikhtilafu. Hapa haina budi kutoa nafasi ya midahalo yenye kujenga miongoni mwa madhehebu ya kiislamu kwa mujibu wa maelekezo ya Qur'an na Sunnah na kuimarisha umoja wa kiislamu.

Tisa: Ni wajibu kuzuia na kupambana na madhehebu na mirengo ya kifikra za kisasa inaopingana na maelekezo ya Qur'an na Sunnah, kama vile hatutakiwi kukanyagia upande mmoja kadhalika hatutakiwi kulegeza upande wa pili kwa kukubali kila ulinganio unaokuja hata kama ni tatanishi, ni lazima kuweka vigezo vya wazi vya kulinda uhalisia wa uislamu.

Kumi: Kuendelea kusisitiza kua madhehebu ya kiitikadi, kifiqhi na kielimu-malezi hayatowajibika kwa makosa yanayotendwa na wafuasi wa dhehebu husika dhidi ya wasiokua na hatia kama kuua, kuvunja heshima, na kuharibu mali ya wengine.

Mapendekezo:

1) 'Baraza' linaitaka 'Sekreterieti ya Kongamano' iandae warsha na vikao mbalimbali kwa lengo la kurekebisha sababu zinazoyafanya madhehebu mbalimali kua na mivutano/migogoro miongoni mwa wafuasi wake, migogoro hii huenda ikapelekea hali ya mtafaruku kwa umma mzima; ipo haja ya kuweka ufahamu sahihi wa baadhi ya *nususi* (maandiko) ambazo labda huenda zikawa zinafahamika vibaya au zinatekelezwa vibaya au zinalingania pasipo na uhalisia, miongoni mwa nususi kama hizo ni hizi:

   a. Mas'ala ya *walaa* na *baraa* (kuungana na kujivua).

b. Hadith ya *al-Firqat al-Naajiyah* (kundi lililookoka).
c. Vidhibiti (vigezo) vya kukufurisha, kufasikisha na kubida'isha bila tashdidi wala kulegeza.
d. Hukmu ya kuritadi na masharti ya utekelezaji wa *hadd* (adhabu) yake.
e. Kutanua wigo wa *kabaair* (madhambi makubwa) na athari zake kwa mwenye kuangukia kutenda madhambi hayo.
f. Ukufurishaji kwa kutotekeleza kikamilifu hukmu za sharia kiujumla bila kufafanua hali za mazingira.

2) 'Baraza' linausia taasisi husika katika nchi za kiislamu kuchukua hatua zifaazo kudhibiti na kuzuia uchapishaji au usambazaji wa vitabu au Makala ambayo yanaweza zidisha mgawanyiko wa kimadhehebu au kukufurisha waislamu au kuwaita kua ni wapotevu bila uwepo wa sababu inayokubalika kisharia.
3) Baraza' linausia taasisi husika kuendelea kusimamia vyanzo jumuishi vya sharia ya kiislamu katika kanuni zote na matendo ya watu kama ilivyobainishwa na 'Kongamano' kwenye maamuzi yake na mapendekezo ya kikao kilichopita.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 153 (2/17)

Yanayohusiana na 'Utoaji Fatwa: Masharti yake na Maadili yake'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Amman, Falme ya Kihashimi ya Jordan (HKJ) 28 Jumada al-Uula (Mfungo Nane) - 2 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1427, sawa na 24 – 28 Juni, 2006.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Utoaji Fatwa: Masharti yake na Maadili yake,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Fasili ya kufutu, Mufti na umuhimu wa kufutu:

Kufutu; ni kubainisha hukmu ya kisharia wakati inapoulizwa, na inaweza kutolewa hata bila ya kuulizwa kunapokua kumetokea jambo au janga linalohitaji ubainishaji wa hukmu ya kisharia na kusahihisha au kurekebisha mambo ya watu.

Mufti; ni mwanachuoni anaezifahamu vizuri hukmu za sharia na kadhia na mambo yanayotuka, pia ni mtu alieruzukiwa elimu na uwezo wa kuchokonoa hukmu za sharia kutokana na dalili zake na kuzitumia kwenye mambo mapya yaliyozuka.

Ama Fatwa; ni jambo adhimu kwa kua ni ubainishaji wa sharia ya Allah, Mufti hapa anakua kama msemaji wa Allah katika hukmu zake, na anafuata nyayo za Bwana Mtume SAW katika kazi ya kubainisha hukmu za Allah.

Mbili: Masharti ya Mufti:

Haijuzu kwa mtu yeyote kusimamia suala la *iftaa* (kufutu) ila yule ambae kwake yeye kunapatikana masharti yaliokubaliwa; yakiwemo:

a) Uelewa mpana wa Kitabu cha Allah (Qur'an) na Sunnah za Bwana Mtume SAW na elimu nyingine zinazohusiana na Qur'an na Sunnah.
b) Uelewa mpana wa maeneo yanayopatikana *ijmaa* ya wanazuoni na ikhtilafu zao na uelewa wa madhehebu na rai mbalimbali za kifiqhi.
c) Ufahamu bobezi wa elimu ya *Usool al-Fiqh*, misingi yake na makusudio makuu ya sharia pamoja na elimu-saidizi kama vile: *Nahau*, *Swarf*, *Balagha*, *Lugha ya Kiarabu*, *Mantik* na nyenginezo.
d) Uelewa mzuri wa hali za watu na mila zao, aidha, awe na ufahamu muafaka wa mambo ya kisasa na mapya yanayozuka, na kutizama mabadiliko yanayojitokeza juu ya mila na desturi zinazozingatiwa ambazo hazipingani na uislamu.
e) Awe na uwezo wa kuchokonoa (*istinbati*) hukmu za kisharia kutokana na *nususi* (dalili za Qur'an na Sunnah).
f) Atake ushauri kutoka kwa wajuzi na wataalamu wa kila fani husika katika mas'ala yanayotakikana kutolewa fatwa; kama vile mas'ala ya kiafya, kitiba, kiuchumi na mengenie.

Tatu: Fatwa za Pamoja:

Kwa kua kadhia nyingi za kisasa zimepandiana; kufikia uelewa sahihi na hukmu zake unahitaji juhudi shirikishi na fatwa za pamoja, ili jambo hili liwezekane basi hakuna budi kua na taasisi za fatwa, mabaraza na makongamano ya kifiqhi.

Nne: Kimsingi, fatwa si lazimishi kiutekelezaji wa kikanuni, lakini ni lazimishi kidini, hivyo haifai kwa muislamu yeyote kujua uwepo wa fatwa sahihi juu ya jambo fulani akaenda kinyume chake. Kwa taasisi za fedha za kiislamu zinawajibika kufuata maelekezo ya bodi zake za kisharia sambamba na maamuzi ya makongamano ya kifiqhi.

Tano: Ambao fatwa zao hazikubaliki:

a) Hazikubaliki fatwa zitokazo kwa wasiokua wataalamu ya *tahasusi* na wasiotimiza masharti yaliyotajwa hapo juu.
b) Fatwa zinazorushwa hewani kupitiia vyombo vya habari mbalimbali, nyingi miongoni mwa fatwa hizo hazifai kwa asiekua muulizaji wake, ila

ikiwa mtoaji fatwa yuko kwenye mazingira hayohayo ya muulizaji.

c) Hazizingatiwi fatwa zinazokinzana na *nususi* zilizowazi au zinazogongana na *ijmaa* inayojulikana.

Sita: Maadili ya *Iftaa*:

Inatakiwa kwa Mufti awe na *ikhlasi*, utuvu na utulivu katika utoaji wake wa fatwa, awe ni muelewa wa mazingira yanayomzunguka, ana kinai na uchamungu, anatekeleza yale anayoyafutu yeye mwenyewe ya kutendwa au kuachwa, anajieka mbali na sehemu tatanishi, hana haraka katika kujibu; anatizama nyanja zote zinazofanana na mas'ala yaliyopo mbele yake na mas'ala yenye utata, anashauriana na wanazuoni wenzake, anasoma sana na kupekua vitabu, muaminifu wa siri za watu, daima anamuomba Allah Amuafikie katika utoaji wake wa fatwa, mas'ala asiyoyajua hakurupuki; anazidi kuendelea kutafiti na kupitia rejea mbalimbali na kuhakikisha.

Mapendekezo:

1) 'Kongamano' linapenda kuusia mwendelezo wa mawasiliano na uratibu baina ya taasisi za fatwa katika ulimwengu wa kiislamu na kupeana taarifa juu ya mas'ala mapya yanayozuka na matukio makuu.
2) Suala la iftaa iwe ni elimu inayojitegema, na isomeshwe kwenye vyuo vya elimu ya kisharia na vyuo vya kuandaa makadhi, maimamu na makhatibu.
3) Kuandaliwe warsha maalum za kila wakati zitakazoangazia umuhimu wa fatwa na haja ya watu kupata fatwa hizo ili kutatua mapya yanayoibuka.
4) Aidha, 'Kongamano' linausia kufaidi na 'Maamuzi ya Kongamano' namba 104 (7/11) yanayohusiana na njia za kufaidika na fatwa; hususan kwenye mapendekezo yafuatayo:

    a. **"*Moja:*** *Kua na tahadhari juu ya fatwa amabazo haziegemezwi kwenye misingi ya kisharia wala ambazo hazikutegemea dalili inayokubalika kisharia, lakini zinategemea maslahi yanayodhaniwa; ambayo yanakataliwa kisharia kwa kua yametokana na utashi wa nafsi au yametokana na kuathirika na mazingira-kinzani ya misingi ya sharia na*

makusudio yake makuu.

b. ***Mbili:*** *Kuwataka wanaosimamia mambo ya fatwa miongoni mwa wanazuoni au taasisi na kamati kutumia na kuyachukulia kwa uzito 'Maamuzi na Maazimio' ya Makongamano ya Fiqhi', ili kudhibiti utoaji wa fatwa na mipangilio yake katika ulimwengu wa kiislamu*".

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 154 (3/17)

Yanayohusiana na 'Msimamo wa Uislamu juu ya Suala la *Ghuluw* (Uchupaji mipaka), *Tatarruf* (Misimamo mikali) na *Irhab* (Ugaidi)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Amman, Falme ya Kihashimi ya Jordan (HKJ) 28 Jumada al-Uula (Mfungo Nane) - 2 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1427, sawa na 24 – 28 Juni, 2006.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Msimamo wa Uislamu juu ya Suala la *Ghuluw* (Uchupaji mipaka), *Tatarruf* (Misimamo mikali) na *Irhab* (Ugaidi),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya.

Na baada ya kupitia 'Maamuzi ya Kongamano' namba 128 (2/14) yanayohusiana na '*Haki za Binadamu na Unyanyasaji wa Kimataifa*', ambapo ugaidi ulifasiliwa kua ni: "*Kufanya uadui au kutia khofu au kutishia watu madia (material) au maanawia (immaterial), nisawa jambo hili lifanywe na dola au vikundi au mtu binafsi, kumfanyia binadamu kwenye dini yake au nafsi yake au heshima yake au akili yake au mali yake pasina haki; kwa njia yoyote miongoni mwa aina za ufisidifu katika ardhi (dunia)*".

Na baada ya kupitia machapisho maalum yaliyotolewa kwenye mikutano

rasmi na isiokua rasmi ya nchi za kiarabu na za kiislamu yaliyogusia suala la ‘kupambana na ugaidi’ kwa kutibu sababu zake na kuwakatia njia magaidi, pamoja na kuendelea na sera ya kuwapatia walionyan’ganywa nchi zao; haki ya mapambano ya kivita na kutumia silaha. Na kwa kuzingatia yaliyotajwa kwenye ‘Risala (ujumbe) ya Amman’ ya 27 Ramadha, 1425 Hijria (9 Novemba, 2004);

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Uharamu wa matendo yote ya kigaidi na aina zake zote na kwamba ugaidi ni makosa makubwa ya jinai yanayoingia kwenye kundi la makosa ya ‘*Hiraba*’ (ufisadi katika ardhi) popote yanapofanyika na yeyote awe mtendaji wake. Aidha, inachukuliwa kua ni ugaidi kila alieshiriki kwenye matendo ya kigaidi ima mubashara au kwa wakala, au kusababisha, au kulipia gharama zake au kuunga mkono; sawa iwe ni mtu binafsi au kundi au nchi, pia inawezekana ugaidi ukatendwa na nchi dhidi ya nchi nyingine.

2) Kutofautisha baina ya makosa ya kijinai ya ugaidi na mapambano halali ya kupigania uhuru kwa njia zinazokubalika kisharia ili kuondosha dhulma na kurejesha haki zilizotwaliwa, hii ni haki inayokubalika kisharia na kiakili, mikataba ya kimataifa pia inakiri jambo hili.

3) Ulazima wa kutibu sababu zinazopelekea kufanya ugaidi zikiwemo: *Ghuluw* (Uchupaji mipaka), *Tatarruf* (Misimamo mikali), Ta’assub (Ukabila, Udini, Umadhehebu), kutoelewa hukmu za sharia ya kiislamu, uvunjaji wa haki za binadamu na uhuru wa kisiasa na kifikra, kupanguka kwa hali za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

4) Kuweka msisitizo juu ya ‘Mmamuzi’ yaliyoashiriwa hapo juu kua: kupigana (jihad) kwa ajili ya kulinda Aqeeda ya Kiislamu na kulinda mipaka ya nchi au kuzikomboa iwapo zimetawalia na wavamizi; haya si katika ugaidi kabisa, bora tu vita hivi vya jihad viendeshwe kwa mujibu wa maadili ya kiislamu.

Aidha, inausiwa yafuatayo:

1. Kuongezea nguvu nafasi za wanazuoni, walinganiaji na taasisi za kielimu za umma na za binafsi ili ziweze kutoa elimu sahihi ya jinsi ya kupambana na ugaidi na kutibu sababu zake.
2. Kuvitaka vyombo vyote vya mawasiliano-habari kua makini, waangalifu na wakweli wanapotoa habari zao na ripoti zao hususan kwenye kadhia zihusuzo mambo ya ugaidi na kujiepusha kuyafungamanisha na uislamu, kwani ugaidi unapatikana pia kwa waumini wa dini na tamaduni nyengine.
3. Kuzitaka taasisi za kielimu na vyuo vikuu waudhihirishe uislamu katika uhalisia wake unaovutia na unaolingania kwenye maadili huruma, mapenzi, kusameheana na kuishi na wengine kwa kusaidiana kwenye kheri.
4. Kuitaka ‘Sekreterieti Kuu’ kuongeza juhudi zao maradufu juu ya suala hili kwa kuandaa warsha tahasusi na mihadhara mizito na vikao vya kielimu vya wasomi yote hayo ili kubainisha upeo wa hukmu za sharia ya kiislamu katika kuzuia ugaidi na kuumaliza, aidha, juhudi za makusudi zichukuliwe kuandaa mwavuli wa kisharia utakaokusanya janibu zote za mas’ala haya.
5. Kulitaka Shirika la Umoja wa Mataifa (UM) kuongeza juhudi katika kuzuia ugaidi na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika kupambana nao na kuweka misingi imara na vigezo vya kuainisha na kufasili ugaidi kwa kipimo kimoja.
6. Kuzitaka nchi zote duniani na serikali zao kuweka kwenye vipaumbele vyao namna ya ‘kuishi kwa amani’ na waachane na sera za kuvamia nchi nyengine na kuwanyima watu wengine haki zao za kujitawala, aidha, nchi hizi zinatakiwa kuboresha mahusiano yao yawe mazuri kwa misingi ya kuheshimiana, usawa, amani na uadilifu.
7. Kuzitaka nchi za magharibi kupitia tena (upya) mitaala yao ya elimu na vile vilivyomo ndani vya mtazamo hasi juu ya dini ya kiislamu na kuzuia matendo yanayochafua au kuukosea uislamu kwenye vyombo vyao vya mawasiliano mablimbali ili kuonyesha nia njema ya kutaka kuishi kwa amani na maingiliano na kuzuia utamaduni wa chuki na uadui.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 155 (4/17)

Yanayohusiana na 'Kuowanisha Baina ya Kushikilia ya Asili na Matakwa ya Uraia wa Waislamu Nje ya Nchi za Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Amman, Falme ya Kihashimi ya Jordan (HKJ) 28 Jumada al-Uula (Mfungo Nane) - 2 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1427, sawa na 24 – 28 Juni, 2006.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kuowanisha Baina ya Kushikilia ya Asili na Matakwa ya Uraia wa Waislamu Nje ya Nchi za Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: '*Uraia*' ni hali ya mtu kujinasibisha na nchi fulani kiardhi na kiuhalisia na akabeba uraia wa nchi hio. '*Asili za Kiislamu*' ni zile hukmu za kisharia, za kiitikadi, kivitendo na kimaadili zinazopatikana kwenye *nususi* za kisharia zilizowazi au zile zinazopatikana kwa hukmu ya *ijmaa* ya wanazuoni wa kiislamu. Kuhifadhi mambo matano ya msingi kama vile: kuhifadhi dini, nafsi, akili, kizazi (heshima) na mali ni miongoni mwa '*Asili za Kiislamu*'.

Mbili: Hakuna katazo la kisharia kwa muislamu kutoa mchango wake katika nchi zisizokua za kiislamu kwenye shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi ambazo hazigongani na '*Asili za Kiislamu*' zilizotangulia kuelezewa hususan ikiwa michango kama hio ni sehemu ya uraia alimradi yasiharibu utu na utambulisho wa kiislamu.

Tatu: Hakuna katazo kisharia kwa waislamu wanaoishi nchi za magharibi kupeleka kesi zao kwenye mahakama za nchi hizo ikiwajibika kupata haki

zao au kuondosha dhulma. Ama katika kadhia za mambo binafsi ni lazima kufuata hukmu za sharia ya kiislamu ima kupitia kuhukkumiwa kiislamu au kutekeleza fatwa ya kisharia.

Nne: Hakuna haja ya kua na fatwa mahsusi kwa waislamu waishio nchi zisizokua za kiislamu ila iwapo kuna dharura ya kufanya hivyo au ipo haja ya lazima ambayo itapelekea kwenye '*uzito au muhali*' basi hapo kila dharura au haja itakadiriwa kwa nafasi yake pamoja na kuzingatia masharti ya kisharia ya kufanya hivyo.

Imeusiwa:

1) 'Kongamano' linaweka msisitizo juu ya umuhimu wa kua na mawasiliano baina ya waislamu, waishio nchi zisizokua za kiislamu, na nchi na jamii za kiislamu.
2) 'Kongamano' linausia nchi za kiislamu kuwasaidia waislamu waishio nchi zisizokua za kiislamu kwa kadiri ya kitakachowawezesha kuimarisha uwepo wao katika sehemu waishizo kupitia kuwasaidia kuasisi shule na taasisi za kufundishia dini ya kiislamu na lugha ya kiarabu, na kuanzisha koleji (college) za kuandaa maimamu na walinganiaji ili waendelee na kazi ya kulinda vizazi vya waislamu na utambulisho wao wakiwa nje ya nchi za kiislamu.
3) Kuanzishwe 'kituo cha tafiti na ukusanyaji wa taarifa' kuhusu hali za waislamu katika nchi zisizokua wanachama wa 'Jumuia ya Nchi za Kiislamu' (OIC); kukusanya taarifa za kidemografia (ukaazi), historia na nafasi zao katika nchi zao, pamoja na kukusanya taarifa za shughuli za jumuia za kiislamu mbalimbali zinazofanya kazi huko kupitia mpamngo mzima wa kujua hali za waislamu nje ya nchi za kiislamu.
4) Kujihusisha na kazi ya uandaaji wa 'walinganiaji mahiri wenye uweledi' wa kuweza kuamiliana na waislamu waishio nchi zisizokua za kiislamu na jamii nyengine kwa kufahamu lugha itumikayo, ada, desturi, mila na mazingira ya kisiasa, kiuchumi, na kijamii ya jamii hizo.
5) Kuzitaka vituo vya kiislamu vinavuojihusisha na mambo ya waislamu waishio nchi zisizokua za kiislamu kuendelea kushirikiana na makongamano na mabaraza ya kifiqhi yaliyopo maeneo yao ambayo

yana uanachama wa watu waishio maeneo hayo au yanayojihusisha na kadhia zao; ili kuongeza juhudi za kupata haki zao za kidini na kupata suluhisho za kisharia muafaka kwa mazingira yao.

6) Kuyataka makongamano na mabaraza ya kifiqhi yaliyopo nje ya nchi za kiislamu kushirikiana na kuratibu na ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ kwa kua hiki ni chombo-rejea cha kielimu na kifiqhi kwa umma wa kiislamu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 156 (5/17)

Yanayohusiana na 'Kukamilisha Maamuzi juu ya Hati (Sukuk) za Musharaka: Mihimili ya Mali'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Amman, Falme ya Kihashimi ya Jordan (HKJ) 28 Jumada al-Uula (Mfungo Nane) - 2 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1427, sawa na 24 – 28 Juni, 2006.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kukamilisha Maamuzi juu ya Hati (Sukuk) za Musharaka: Mihimili ya Mali,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya.

Na baada ya kupitia 'Maamuzi ya Kongamano' namba 30 (5/4) yanayohusiana na '*Hati-fungani (Sukuk) za Mudaraba*' zilizokusanya misingi mikuu inayotumika kwenye hati (sukuk) zote, pamoja na kuzingatia tofauti zilizopo baina ya sukuk na 'Maamuzi ya Kongamano' namba 137 (3/15) yanayohusiana na '*Hati za Ijara*', na 'Maamuzi ya Kongamano' namba 60 (11/6) ya kuzuia 'hati za deni' iliyoashiriwa kwenye ibara: (Moja: kipengele cha tatu).

Na baada ya kujua uwepo wa idadi kubwa ya warsha na vikao vikiwemo: semina ya 'al-Baraka' ya ishirini (20), warsha ya kwanza (1) ya 'Kampuni ya al-Rajihi', jopo-kazi loililoundwa na 'Mamlaka ya Uhasibu na Udhibiti' ya Taasisi za Fedha za Kiislamu' (*Accounting and Auditing Organization for Islamic Financial Institutions* (AAOIFI)), 'kipimo cha kisharia kuhusiana na sarafu' na 'kipimo cha kisharia kuhusiana na hati za uwekezaji', vipimo vyote viwili hivyo vimetolewa na 'Bodi ya Sharia ya Mamlaka'.

Na kwa kua 'Kongamano' bado halijatoa 'kanuni na sheria' za ile iliyoashiriwa kwenye maamuzi yake yanayohusiana na 'hati za mudharaba'

ikiwa hati hizi (sukuk) zinawakilisha machanganyiko wa mali; vitu, manufaa, pesa na madeni, na kwa kua pesa za taasisi nyingi za kiislamu za fedha zinakua kwenye vitu na manufaa lakini kwa uchache ikilinganishwa na madeni na pesa taslimu;

Hivyo basi; Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha utoaji wa maamuzi juu ya maudhui haya ili kutoa nafasi za tafiti za ziada, pamoja na kuusia kuandaliwe ‘warsha mahsusi’ ya kutengeneza ‘kanuni na sheria’ zilizoahidiwa kutolewa kwenye ‘Maamuzi yake’ namba 30 (5/4).

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 157 (6/17)

Yanayohusiana na 'Kuahidiana na Kushirikiana katika Mikataba'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Amman, Falme ya Kihashimi ya Jordan (HKJ) 28 Jumada al-Uula (Mfungo Nane) - 2 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1427, sawa na 24 – 28 Juni, 2006.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kuahidiana na Kushirikiana katika Mikataba,** na baada ya kujikumbusha 'Maamuzi' namba 40 & 41 (2/5 & 3/5), na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kimsingi, panapokua na maahidiano ya pande mbili basi inalazimu kuyatekeleza kidini, lakini sio lazma kimahkama.

Mbili: Maahidiano ya pande mbili juu mkataba fulani kama ujanja (kificho) wa kula riba kama vile; kukubaliana biashara ya '*Inah*' (ni riba inayojificha kwenye biashara), au kuahidiana 'kuuza na kukopesha' ambayo imekatazwa kisharia.

Tatu: Katika mazingira ambayo haimkini kukamilisha mkataba wa mauziano kwa kukosekana uwepo wa kinachouzwa kwenye milki (dhimma) wa muuzaji, lakini ipo haja kubwa ya kuwalazimisha pande zote mbili kukamilisha mkataba wa mauziano kwa mustakbali ima kwa hukumu ya kanuni au nyengineo, au kwa mujibu wa taratibu za kibiashara za kimataifa, kama kufungua '*waraka wa mkopo*' wa kuagiza bidhaa kutoka nje (*n'gambo*), kwa mazingira haya; inajuzu kuweka maahidiano-lazimishi ima kwa kutunga sheria ya kiserikali au kwa kuweka kifungu maalum kwenye mkataba wao kinachofanya maahidiano baina yao kua lazimishi kwa pande

zote mbili.

Nne: Maahidiano-lazimishi kwenye mazingira yaliyotajwa hapo kipengele cha: ‘Tatu’ hayabebi hukmu ya ‘biashara inayosubiria mustakbali’, kwa maana hio umiliki wa kinachouzwa hauhamishiki kutoka kwa muuzaji kwenda kwa mnunuzi, wala thamani yake haichukuliwi kua ni deni juu yake, na hakuna mkataba wa biashara utakaofungika ila kwa miadi waliowafikiana ifikapo tarehe hio na kwa kuwepo kwa ridhaa ya kuuza na kukubali kununua.

Tano: Atakapokhalifu (kuchelewa) moja ya pande mbili za maahidiano kwenye mazingira yaliyotajwa hapo kipengele cha: ‘Tatu’; kinyume na alivyoahidi, basi mahakama itamlazimisha ima kukamilisha mkataba au kulipa fidia dhidi ya dhara lolote latakalomfikia mwenzake wa mkataba kwa kukhalifu kwake ahadi yake.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 158 (7/17)

Yanayohusiana na 'Kuuza Deni'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Amman, Falme ya Kihashimi ya Jordan (HKJ) 28 Jumada al-Uula (Mfungo Nane) - 2 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1427, sawa na 24 – 28 Juni, 2006.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kuuza Deni,** na baada ya kujikumbusha 'Maamuzi' namba 40 & 41 (2/5 & 3/5), na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya.

Na baada ya kupitia 'Maamuzi ya Kongamano' namba 101 (4/11) yanayohusiana na **'***Kuuza Deni na Hati za Mikopo*', yanayosema: "*Haijuzu kuuza deni la baadae kwa asiedaiwa kwa malipo ya sasahivi ya jinsi ya deni hilo au isiokua jinsi hio* …".

Na baada ya kupitia 'Maamuzi ya Kongamano' namba 139 (5/15) yanayohusiana na 'Kadi za Mikopo' yanayosema: "*Taasisi za Fedha za Kiislamu zinatakiwa kujiepusha na mkamganyiko wa riba au visingizio ambavyo vinaweza kupelekea kunako riba kama vile: kufuta deni kwa deni*";

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kunahesabiwa ni kufuta deni kwa deni ambayo imekatazwa kisharia; kila jambo liatakalopelekea nyongeza ya deni kwa mdaiwa mkabala wa kuongeza mda wa deni (*maturity*); mfano wa hilo ni kufuta deni kwa deni kwa njia ya muamala baina ya mdai na mdaiwa; kwenye muamala huu panaibuka mkataba mpya wa deni jipya kwa mdaiwa ili ionekane amelipa deni lake la kwanza lote au baadhi yake, sawa awe mdaiwa ni muweza au

amelemewa, ni kama tuseme: mdaiwa ananunua bidhaa kwa mdai kwa thamani ya kulipwa baadae kisha anaiuza bidhaa hiohio kwa thamani ya sasa ili alipe deni la kwanza lote au baadhi yake.

Mbili: Aina za kuuza deni zinazoruhusiwa:

1) Mdai kuuza deni lake kwa asiekua mdaiwa wake kwenye mojawapo ya aina hizi:

    a. Kuuza deni liliopo kwenye dhimma kwa sarafu nyengine hivi sasa isiokua sarafu ya asili ya deni ya siku hio.
    b. Kuuza deni kwa bidhaa fulani.
    c. Kuuza deni kwa manufaa ya kitu fulani.

2) Kuuza deni ndani ya mchanganyiko wa mali; aghalabu yake yakiwa: vitu na manufaa ambayo ndio lengwa ya mauzo.

Aidha, inausiwa kuandaa tafiti za kina ili kukamilisha mas'ala yaliyosalia yanayohusiana na maudhui haya na utekelezaji wake wa kisasa.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 159 (8/17)

Yanayohusiana na 'Hali ya Mwanamke na Nafasi yake ya Kijamii kwa Mtazamo wa Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Amman, Falme ya Kihashimi ya Jordan (HKJ) 28 Jumada al-Uula (Mfungo Nane) - 2 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1427, sawa na 24 – 28 Juni, 2006.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Hali ya Mwanamke na Nafasi yake ya Kijamii kwa Mtazamo wa Kiislamu,** na baada ya kujikumbusha 'Maamuzi' namba 40 & 41 (2/5 & 3/5), na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya.

Na baada ya kupitia 'Maamuzi ya Kongamano' namba 114 (8/12) yanayohusiana na **'***Tamko la Kiislamu juu ya Nafasi ya Mwanamke katika Maendeleo ya Jamii ya Kiislamu*', ambayo yalibainisha nafasi za kukamilishana baina baina ya mwanamume na mwanamke katika kuunda jamii bora iliyolingana ya kiislamu, wote mume na mke wana nafasi muhimu, ikizingatiwa kua familia ndio jiwe la msingi katika mjengo huu, na kukataa aina nyengine zote za 'familia' zinazodaiwa.

Aidha imeelezewa kua umama ni miongoni mwa nafasi nyeti na za kawaida kwa mwanamke kwenye maisha yake, na kwamba mwanamume na mwanamke wako sawa katika heshima ya kibinadamu, na kama alivyo mwanamke ana haki pia ana na majukumu yanayoendana na maumbile yake na uwezo wake na alivyo mwenyewe.

Pia imetiliwa nguvu suala la kumuheshimu mwanamke katika nyanja zote na kukataa yale yanayoenezwa dhidi yake ya kudunisha utu wake na kudharau heshima yake. Na imekemewa vikali sana kwa baadhi ya serikali

kumkataza mwanamke wa kiislamu kutekeleza maagizo ya dini yake;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Hakika ya mikutano ya kimataifa inayoandaliwa kuhusiana na suala la 'Haki za mwanamke kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiuraia na kiutamaduni (mikutano ya maendeleo na ukaazi) imetokana na fikra (kasumba) ya kutenganisha maisha – katika nyanja zake zote – na dini, bali wanachukulia kua baadhi ya misingi ya kiislamu na hukmu zake ni aina fulani ya ubaguzi dhidi ya mwanamke.

Mbili: Ni lazima kuchukua tahadhari dhidi ya nembo za "usawa" baina ya mume na mke kwa visingizio na matendo yanayopingana na uislamu.

Tatu: Ulazima wa kumhami (kumlinda) mwanamke wa kiislamu dhidi ya matendo, mila na desturi dhalimu zinazomvunjia haki yake katika kuhifadhi dini yake, utu wake, heshima yake, mali yake na haki nyenginezo ambazo zinakubalika kwenye misingi ya haki za binadamu kama ilivyo kwenye misingi ya sharia ya kiislamu.

Nne: Hakika ya mikutano ya maendeleo na ukaazi na makubaliano yaliyoibuka kwenye mikutano hiyo imejihusisha tu na nyanja za *kimadia* (materialistic) bila kuzingatia maleng ya kiroho, yametupilia mbali kabisa nafasi asilia na ya kimaumbile ya mwanamke ambayo ni kusimamia familia yake na kujenga kizazi cha mustakbali kwa njia salama, lakini badala yake wanamuita kwenye kujiachia (kujiporomosha kimaadili), hii isimaanishe kua kwenye makubaliano hayo hakuna mengine yaliokua ni mazuri na chanya.

Tano: Mikutano hii imetupilia mbali kabisa na kuiweka pembeni nafasi ya familia katika kuijenga jamii na kuruhusu mahusiano yasiokua ya kawaida (kijinsia) ya aina zote.

Sita: Kulingana na utitiri wa mambo mapya yanayoibuka kimataifa; 'Kongamano' linaonelea ulazima wa kwenda na wakati lakini kufuatana na hukmu za kiislamu, na kufuatilia maazimio ya mikutano hii inayohusiana na kadhia za mwanamke, na ipo haja ya kuunganisha juhudi za nchi na mashirika ya kiislamu ili maazimio yanapotolewa yasigomgane na misingi

ya sharia za kiislamu na hukmu zake.

Aidha, ‘Kongamano’ linausia yafuatayo:

1) Ushiriki wa kikamilifu kwenye mikutano ya kimataifa inayohusiana na mambo ya wanawake, na kuweka mbadala wa kiislamu wa masuala ya kijamii.
2) Ulazima wa kuitaarifu dunia ‘msimamo wa uislamu kwa mwanamke’ hasahasa kwenye mambo yahusuyo haki na majukumu kwa mtazamo wa kiislamu, taarifa hizi zisambazwe kwa lugha mbalimbali duniani kote.
3) Kuitaka ‘Sekreterieti Kuu ya Kongamano’ kuandaa majopo-kazi au warsha kudurusu:

    a. Makubaliano na mikataba ya kimataifa yanayohusiana na ‘maendeleo na ukaazi na kadhia za wanawake’ kwa lengo la kufikia msimamo wa kiislamu wa pamoja katika yote yanayoazimiwa.
    b. Suala la ‘Ushiriki wa kisiasa na mipaka yake na vidhibiti vyake’ kwa mujibu wa misingi na maelekezo ya hukmu za kisharia,

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 160 (9/17)

Yanayohusiana na 'Mahusiano na Miafaka ya Kimataifa kati ya nchi za Kiislamu na Nyenginezo'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na sita (16) kilichofanyika Amman, Falme ya Kihashimi ya Jordan (HKJ) 28 Jumada al-Uula (Mfungo Nane) - 2 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1427, sawa na 24 – 28 Juni, 2006.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Mahusiano na Miafaka ya Kimataifa kati ya nchi za Kiislamu na Nyenginezo,** na baada ya kujikumbusha 'Maamuzi' namba 40 & 41 (2/5 & 3/5), na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Mahusiano kati ya nchi za kiislamu na zile zisizokua za kiislamu katika jamii ya kimataifa; yanatakiwa yejengeke kwenye misingi ya amani na kukataa vita, na misingi ya kuheshimiana na kusaidiana kwa lengo la kufukia maslahi ya pamoja ya binadamu wote kwa mujibu wa misingi ya hukmu za kisharia.

Mbili: Dola ya kiislamu haiwezi kuifanyia uadui dola nyingine isiyokua ya kiislamu eti kwa kutofautiana kidini, lakini iwapo dola hio isiyokua ya kiislamu itaanza uadui au kuchafua sehemu takatifu na alama za kidini basi hapo dola ya kiislamu itarudisha uadui, hii ni kwa sababu vita katika uislamu ni njia ya mwisho kabisa inayotumika kwa ajili ya kujilinda au kurudisha uadui.

Tatu: Ulazima wa kusaidiana na kukamilishana baina ya nchi za kiislamu katika nyanja zote; kama vile: Soko la kiislamu la pamoja na maeneo-huru

ya kiuchumi (*free trade zones*) na kufunga mikataba ya ushirikiano katika nyanja mbalimbali za kimataifa.

Nne: Hakuna katazo la kisharia la kufunga mikataba ya kimataifa ambayo haigongani na misingi ya uislamu na sharia zake, na haipelekei kuzifanya dola fulani kua na ubabe dhidi ya dola nyengine; mikataba hii inaweza kufungwa kwenye nyanja zote kwa maslahi ya waislamu.

Inausiwa yafuatayo:

1) ‘Kongamano’ linausia vyuo vikuu na vituo vya utafiti vya pembe zote za ulimwengu wa kiarabu na kiislamu kutilia umuhimu zaidi tafiti zinazohusiana na kubainisha misingi ya kiislamu kwenye mahusiano ya kimataifa na kuheshimu haki za wasiokua waislamu waishio ndani ya nchi na jamii za kiislamu.
2) ‘Kongamano’ linazisihi nchi za kiislamu wakati watumapo wajumbe wao kushiriki kwenye mikutano ya kimataifa ya kifikra, na kiutamaduni; waweke wataalamu wa tahasusi wa mas’ala ya utamaduni wa kiislamu ili wachangie kwenye maudhui za mikutano hii.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 161 (10/17)

Yanayohusiana na 'Vigezo vya Kisharia juu ya Tafiti za Tiba-Baiolojia (*Bio-Medical Research*) kwa Binadamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na saba (17) kilichofanyika Amman, Falme ya Kihashimi ya Jordan (HKJ) 28 Jumada al-Uula (Mfungo Nane) - 2 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1427, sawa na 24 – 28 Juni, 2006.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Vigezo vya Kisharia juu ya Tafiti za Tiba-Baiolojia (*Bio-Medical Research*) kwa Binadamu,** na baada ya kuupitia 'waraka' uliotolewa na 'warsha' iliyoandaliwa na 'Jumuia ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' iliyofanyika Cairo (Misri) katika kipindi kuanzia 29 Shawal (Mfungo mosi), 1425 Hijria (11 – 14 Disemba, 2004) iliyohusiana na: (Misingi-Elekezi ya Kimaadili ya Kimataifa ya Tafiti za Tiba-Baiolojia Zinazohusiana na Janibu za Kibinadamu: Mtazamo wa Kiislamu), na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuitambua misingi mikuu ya waraka huo:

'Konganabo' linapenda kusisitiza kua linaitambua misingi mikuu iliyokuja kwenye waraka na ambayo kwa misingi hiyo; vigezo-ratibishi vya maadili ya tafiti za tiba-baiolojia vimejengeka juu yake, kama ifuatavyo:

1) Kuheshimu watu na kumtukuza binadamu ni msingi uliothubutu na sharia ya kiislamu inakiri msingi huo kwa mujibu wa neno lake Allah SWT:

   "*Na hakika tumewatukuza wanaadamu, na tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na*

tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tulio waumba”.[1]

Hivyo basi; ni lazima kuheshimu uhuru wa binadamu alie na utu na ubinadamu kamili muweza kiakili na aliejitolea kwa ajili ya kufanywa utafiti wa tiba awe na uhuru wa kujiamulia na kuchukua maamuzi maridhawa kwa ridhaa yake timamu na matakwa yake huria bila ya kutenzwa nguvu au kudanganywa au kufanyiwa ghilba, kama ilivyo kisharia:

”حق الآدمي لا يجوز لغيره التصرف فيه بغير إذنه“

“*Haki ya Kibinadamu inaheshimiwa na haijuzu kwa yeyote kuigusa pasina ridhaa yake*”.

Ama ikiwa mtu si muweza kiakili au ana mapungufu (ulemavu wa akili au ni mtoto mdogo) katika utu wake basi nzazi wake au msimamizi wake (walii) ana wajibu wa kumlinda na kumhami dhidi ya kutumiwa vibaya. Juu ya hili misingi mikuu ya fiqhi inasisitiza kua:

”من لا يصح تصرفه لا قول له“

“*Asiekua na maamuzi sahihi (huru) hana kauli*”

Kwa maana hio sharia imemuekea mtu kama huyu msimamizi anaesimamia mambo yake na kumchungia maslahi yake kwa namna ambayo yatalindwa na kuhifadhika bila ya kudhurika au kuharibika.

2) Kuhakikisha upatikanaji wa maslahi ni katika misingi ya sharia ya kiislamu kupitia kaida inayosema: ‘*kuwaletea waja maslahi na kuwaepushia madhara*’, ama katika mazingira ambayo madhara hayaepukiki basi pataangaliwa dhara dogo ili kuepusha dhara kubwa; yaani kutenda dhara dogo (liso budi hutendwa).
3) Kuhakikisha uadilifu; yaani kujilazimisha kimaadili kwa kuamiliana na kila mtu kwa mujibu wa usawa na usahihi kimaadili, na kumpatia kila mwenye haki; haki yake sawa awe mume au mke, huu ndio msingi uliosimamishwa na sharia ya kiislamu, aidha, msingi huu ni miongoni mwa njia tekelezi za msingi wa uadilifu na inswafu ambao uislamu

[1] Surat al-Israa: 70.

umeukita na kuufanya kua chimbuko la matengenezo na mafanikio ya maisha.

4) Kufanya wema (ihsani); juu ya msingi huu pameshuka aya adhimu sana katika Qur'an ya kuhimiza kutenda wema kikamilifu na kujiepusha na madhara kiukamilifu; nayo ni neno lake allah SWT:

> "*Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani, na kuwapa jamaa; na anakataza uchafu, na uovu, na dhulma*...".[1]

Mbili: Vidhibiti vya Tafiti za Tiba-Baiolojia kwa Binadamu:

'Kongamano' linaweka msisitizo kua linatambua 'Vidhibiti vya tafiti za tiba-baiolojia kwa binadamu' vilivyoainishwa kwenye 'waraka' tajwa katika utangulizi wa maamuzi haya kwa kua vidhibiti hivi vinaratibu vizuri mchakato wa kufanya tafiti za tiba-baiolojia ndani ya mfumo-elekezi wa hukm za sharia za kiislamu. Aidha, kuitaka 'Jumuia ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' kuandaa kikao kipana na kizito kitakachojumuisha madaktari na wanafiqihi kwa minajili ya kuvipatia nguvu vidhibiti hivyo.

Mapedekezo:

1. 'Kongamano' linausia viongozi wa nchi za kiislamu kutilia umuhimu suala la kusaidia utafiti na watafiti; kwa kuweka bajeti-toshelezi na kuandaa mazingira rafiki kwa watafiti na kuwatimizia mahitajio yao yote ya kielimu, kisayansi na kimaslahi ili waweze kutenga mda wao na kutimiza wajbu wao kwa mataifa yao.
2. Kongamano' linausia nchi za kiislamu kufaidi na elimu ya wansayansi wa kiislamu waishio ughaibuni – wao ni chumo (akiba) kubwa kwa umma – na kufungua mianya ya mawasiliano na kuwashajiisha washirikiane na wenzao walioko nchi za kiislamu katika kweka misingi imara ya mbinu za utafiti.
3. Kongamano' linausia 'Jumuia ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' Kuwait, na wizara za afya katika nchi za kiislamu kuandaa semina za mafundisho kwa wafayakazi kwenye sekta ya afya na tiba; juu ya 'Fiqhi ya tiba na afya' na 'Maadili ya kazi za tiba' hususan maadili ya utafiti wa kisayansi

[1] Surat al-Nahl: Aya 90.

na mamo yanayohusiana na vidhibiti vilivyoashiriwa kwenye maamuzi haya.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≋≋≋

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 162 (11/17)

Yanayohusiana na 'Maradhi ya Kisukari na Funga (saum) ya Mwezi wa Ramadhan'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na saba (17) kilichofanyika Amman, Falme ya Kihashimi ya Jordan (HKJ) 28 Jumada al-Uula (Mfungo Nane) - 2 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1427, sawa na 24 – 28 Juni, 2006.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Maradhi ya Kisukari na Funga (saum) ya Mwezi wa Ramadhan,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha utoaji wa maamuzi juu ya maudhui haya ili kutoa nafasi ya tafiti za ziada, na kuiusia 'Jumuia ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' Kuwait; kuunda kamati ya madaktari na wanafiqihi ili kudurusu na kutafiti 'Maradhi ya Kisukari na husiano wake na Funga (saum) ya Mwezi wa Ramadhan'.

Wabillah al-Taufiq

≅≅≅

Tamko la Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu' juu ya Palestina, Masjid al-Aqsa, Iraq na Somalia

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote.

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na saba (17) kilichofanyika Amman, Falme ya Kihashimi ya Jordan (HKJ) 28 Jumada al-Uula (Mfungo Nane) - 2 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1427, sawa na 24 – 28 Juni, 2006.

Kwa nafasi ya 'Kongamano' kama muakilishi wa nchi zote za kiislamu na umma wa kiislamu, na kwa kujihusisha kwake na kadhia za waislamu; linatoa tamko hili kuhusiana na '**Palestina, Masjid al-Aqsa, Iraq na Somalia**'.

Palestina na Masjid al-Aqsa:

'Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu' likiwa linaendelea kufuatilia kwa uchungu hali ngumu wanayopitia watu wa Palestina iliyokaliwa kimabavu wakiwa kwenye uvamizi na kuzingirwa (*siege*). Wapalestina wamefanyiwa *hisar* (kuzingirwa) ya kikatili ikiwa ni kuadhibiwa kwa kutekeleza haki yao ya kuchagua serikali yao na bunge lao kwa hiari yao.

'Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu' linazitaka nchi zote za ulimwengu wa kiislamu na ulimwengu mzima kwa jumla kusimamia jukumu lao na wajibu wao wa kibinadamu na wa kiustaarabu katika kuiondosha dhulma na nyenginezo na mateso yaliyowakumba wapalestina na nchi yao iliyokaliwa.

Aidha, 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu' likiwa linaendelea kufuatilia yanayojiri katika nchi ya Palestina iiyokaliwa; linaitaka dunia yote kuusimamisha ugaidi unaoendelezwa na serikali haramu ya kizayuni, ikiwa ni utekelezaji wa mauaji ya wasiokua na hatia miongoni mwa watoto, wanawake na watu wazima kila uchao, na kutekeleza mauaji ya halaiki (*massacre*) mtawalia, pamoja na kuwabomolea nyumba zao na

kuwafukuza kwenye ardhi zao na kuzinyakua ardhi hizo, kuharibu mimea na mazao na kusumua miti ya matunda, yote hayo bado hawajatosheka sasa wanaweka (wanajenga) kuta la kibaguzi na uvamizi linalogawa maeneo na kunyakua ardhi za wapalestina zipatao asilimia 25% baada ya kubomoa nyumba za wapalestina na kuwafukuza kutoka kwenye ardhi hizo. Kuta hili la kibaguzi linapingana na sharia za dini zote zinazojulikana na mila na desturi za kibinadamu na sheria za kimataifa na maamuzi ya ‘mahkama ya kimataifa ya uadilifu’.

‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ linapenda kuashiria *hisar* (siege) hio na maovu ya kijinai yanayotendwa na ‘waisraeli’ hayajawahi kutokea mfano wake katika historia ya binadamu, hata katika hali mbaya zaidi na za dhulma; hazijafikia yanayotendwa na ‘waisraeli’. Yote haya yanafanywa kwa kisingizio cha ‘eti kujilinda’, na kuwaita wale wapalestina wanaotetea haki yao na kupambana na uvamizi ‘eti ni magaidi na maadui’.

‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ linapenda kuweka msisitizo juu ya ‘Matamko yake’ yaliyotangulia kuhusiana na al-Quds, na kuongeza msisitizo kwenye kikao hiki baada ya kupitia matamshi ya kiuadui na mikakati dhalimu kutoka kwa walowezi wa kizayuni kuhusiana na mji wa al-Quds na hasahasa Masjid al-Aqsa; linasisitiza yafuatayo:

1) Mji wa al-Quds na Masjid al-Aqsa ni sehemu takatifu kwa waislamu wote ulimwenguni; kwa kua sehemu hizo zimefngamana na tukio la kimuujiza ya *israa* na *mi'raj* liloelezewa kwenye Qur'an, na kwa kua Masjid al-Aqsa ndio iliokua Qibla cha kwanza cha waislamu.

2) Masjid al-Aqsa uliobarikiwa ni milki ya waislamu pekee, mayahudi hawahusiki katu na msikiti huo, na ni lazima watahadharishwe dhidi ya kuugusa au kuchafua utukufu wa msikiti huo, serikali ya uvamizi ya kiyahudi na nchi zinaowasaidia watabeba jukumu kamili dhidi ya uchafuzi wa aina yoyote juu ya Masjid al-Aqsa. Msikiti huu haupo kwenye meza ya mazungumzo au kuwaachia mayahudi hata chembe moja ya msikiti huo, na hakuna yeyote anaemiliki kufanya hivyo, msikiti huu uko juu ya yote hayo.

3) Haiwezekani kupatikana kwa amani-adilifu na utulivu kwenye maeneo haya (Mashariki ya Kati) ila baada ya kuumaliza uvamizi wa kiyahudi juu ya Mji wa al-Quds na Masjid al-Aqsa na Wapalestia waliotolewa kurudi kwenye miji yao.

4) Ni haki ya Wapalestina kusimamisha dola yao huru juu ya ardhi yao na mji wao mkuu ukiwa ni al-Quds, ni haki yao vilevile kujilinda nafsi zao na kupambana na adui kwa njia (nguvu) zote zinazokubalika walizonazo hadi pale wliofukuzwa nchini mwao waweze kurudi katika nchi yao.

5) Kutahmini na kupongeza juhudi kubwa zinazofanywa na serikali ya Falme ya Kihashimi ya Jordan katika kuusimamia Masjid al-Aqsa na kuhifadhi utambulisho wa kiarabu na wa kiislamu wa Mji wa al-Quds, hasahasa 'kitengo cha awqaf na sehemu takatifu' kilichopo chini ya wizara ya 'awqaf, sehemu takatifu mambo ya kiislamu' ya Jordan, aidha tunathamini kazi zinazofanywa na 'Wakala wa Baitulmaal' ya al-Quds iliyo chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), bila ya kusahau juhudi nyengine mbalimbali zinazotekelezwa na nchi na mashirika ya kiarabu na ya kiislamu mengine.

6) Aidha, ‘Kongamano’ linawataka viongozi wote na raia wa ulimwengu wa kiarabu na kiislamu wawajibike kidini, kitaifa na kihistoria katika kuutetea na kuulinda mji huu uliotekwa na kuvamiwa, na kusimama na watu wake wanaoendeleza mapambano hapo na kusaidia taasisi zao za kiafya, kielimu, kijamii na nyenginezo ili kuzuia uyahdishaji na utaifishaji wa mji wa al-Quds; uyahudishaji na utaifishaji ni jambo linalokataliwa na kamwe haliwezi kukubalika. Kazi ifanyike kwa nguvu zote kuondosha uvamizi wa kiyahudi juu ya ardhi ya *israa* na *mi’raj*.

Iraq:

Nchi ya Iraq iliyojeruhiwa; leo inapitia mikasa hatarishi inayotishia uwepo wake na umoja wake na uhuru wake, kwani ukiachia uvamizi unaoendelea na masaibu yaliyowafika; bado kuna makundi kadhaa yanayoendeleza machafuko na ugaidi yanaendelea kuua wasiokua na hatia miongoni mwa wanawake, watoto na watu wazima, na kwenda kulipua misikiti, nyumba za ibada na masoko ya biashara, na kueneza ufisadi katika ardhi.

Kama haya yote hayatoshi; pamezuka umadhehebu unaoua kimadhehebu na kusambaza khofu kwa watu wa Iraq, jiji la Baghdad linalojulikana kama kitovu cha ustaarabu wa kibinadamu, Baghdad ya Harun al-Rashid na al-Amin, Baghdad iliyojulikana kwa jina la Dar–us–Salam (mji wa amani), leo Baghdad imegeuka na kua jiji la maharibiko na ufisadi na ukatwaji vichwa vya watu, mto maarufu wa ‘Dejla’ (Tigris) kila asubuhi panaokotwa vichwa vya watu bila ya miili yao; na miili isiyokua na vichwa, mbali na milipuko ya kiholela kwenye sehemu wanazoishi watu; misikitini, nyumba za ibada, masokoni, kwenye mabasi ya umma na maofisini, seuzi yanayoendelea kwenye majela na maangamizi yake.

Juu ya masaibu yote haya; ‘Kongamano’ lina matumaini kupitia uchaguzi wa mwisho uliofanyika ambapo Wairaq waliweza kusimamisha taasisi rasmi kama vile; bunge, serikali na uongozi wa nchi.

‘Kongamano la Fiqh la Kiislamu’ linatoa wito wa kuukomesha uvamizi na kulaani mauaji na ugaidi na majaribio ya kuingiza fitna za kimadhehebu na utesi wa kidini, aidha, ‘Kongamano’ linazitaka taasisi za kidini; za kishia na

kisunni kuingilia kati na kufanya wawezalo kukomesha umwagikaji wa damu na ugomvi hatarishi ambapo hatapatikana mshindi hata siku moja; lakini patapatikana fitna kubwa na hatarishi itakayotafuna kila kitu, kuondosha mizizi hii ya fitna za kimadhehebu na utesi wa kidini ndio msingi na hatua muhimu ya kufanikisha sulhu ya kisiasa na utulivu na maendeleo ya Iraq.

Kwa mnasaba huu; 'Kongamano' linawataka watu wa Iraq wote washirikiane pamoja kisiasa na kufanya kazi kwa bidi na kujiingiza kwenye taasisi za dola mbalimbali hususan wizara za ulinzi na mambo ya ndani ili kuleta uwiano miongoni mwa makundi mbalimbali ya Wairaq, na kusaidia kuufanikisha mpango wa serikali wa kutaka kuyafumua makundi na 'milishia' ya kivyama ili kuleta uwiano wa kitaifa kwa misingi ya kusameheana na haki-adilifu kwa wote. Yafanyike yote haya ili Iraq ijirudishie uhuru wake kamili na kuhakikisha umoja wake, na kutowapa sababu wavamizi (wa kimarekani) kuendelea kuwepo na kubaki Iraq, na ili Iraq ipate kurudi kwenye nafasi yake kama kiungo muhimu kwenye umma na safu ya kiarabu na ya kiislamu.

Aidha, 'Kongamano' linazitaka nchi za kiislamu na nchi rafiki kuisaidia Iraq iweze kutoka kwenye majanga haya na kurudia nafasi yake inayotarajiwa, misaada ya dharura inatakiwa kwa haraka kwenye maeneo yaliyokumbwa na machafuko Iraq. Pia 'Kongamano' linathamini juhudi za upatanishi zinazoendeshwa na nchi mbalimbali na kuondosha hali ngumu ya kimaisha wanayoipitia Wairaq; hususan juhudi za serikali ya Falme ya Kihashimi ya Jordan katika upande wa kuwakusanya viongozi wa kidini wa Iraq kufikia suluhisho la kidini jumuishi ambalo limekua msingi wa suluhisho la kisiasa.

Somalia:

Ama kuhusiana na yanayojiri Somalia hivi sasa, 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC); linatoa wito kwa ndugu wenye akili Somalia; rais, serikali, mahkama za kiislamu na raia wote kwa ujumla na kuwataka wote wakae kwenye meza ya kutafuta sulhu ya uhakika na waachane na kupigana na kuuana, waweke maslahi mapana ya watu wa Somalia juu maslahi yao binafsi,

aidha, linawataka wasiipoteze fursa hii ya upatanishi na kuunganisha juhudi za kuleta amani na utulivu nchini na kuanza kuijenga upya nchi iliyobomolewa na vita.

Aidha, ‘Baraza la Kongamano’ linaunga mkono juhudi adhimu zinazochukuliwa ‘Muungano wa Nchi za Kiarabu’ (*Arab League*) Somalia, na kuweka msisitizo juu ya nafasi ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), kwa msaada wa ‘Katibu Mkuu’ wa *Arab League* na ‘Katibu Mkuu’ wa OIC na ‘Kamati ya Ufuatiliaji ya Mambo ya Somalia’, matarajio yetu ni makubwa juu ya kuongezeka juhudi hizi maradufu na ziendelee kwenye nyanja zote mwenginezitakazoisaidia Somalia kiuchumi, kisiasa na kiusalama ili Somalia irudi katika hali yake iliyokua imeungana kwenye familia ya kimataifa na irudi katika nafasi yake kwenye mashirika ya kiarabu, kiislamu na kimataifa.

Na wakati huohuo ‘Baraza la Kongamano’ linawataka umma wa kiislamu; serikali kwa raia kuinusuru Somalia na kuipelekea misaada inayohitajika katika nyanja zote hususan misaada ya dharura kwa sababu ya vita vya mda mrefu, kadhalika kuwasaidia waliokumbwa na njaa kwa sababu ya ukame, ikumbukwe kua: ‘muislamu ni nduguye muislamu mwengine, asimdhulumu wala asimkhini wala asimsalimishe kwa adui’ na ‘Allah anamsaidia mja wake ambae anamsaidia nduguye’.

Wabillah al-Taufiq

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Kumi na Nane (18) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Putrajaya, Malaysia

24 - 29 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1428,

sawa na 9 – 14 Julai, 2007

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 163 (1/18)

Yanayohusiana na ‘Ramani ya Kuurudia Mfumo wa Kiustaarabu wa Uislamu’

Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), katika kikao chake cha kumi na nane (18) kilichofanyika Putrajaya, (Malaysia) 24 - 29 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1428, sawa na 9 – 14 Julai, 2007.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye ‘Kongamano’ kuhusiana na maudhui ya **Ramani ya Kuurudia Mfumo wa Kiustaarabu wa Uislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya.

Na baada ya kujikumbusha kua uislamu ulitangulia wengine katika kubuni ‘*Dola-adilifu*’ ambapo Mtume Muhammad SAW aliweka katiba ya kwanza duniani ijulikanayo kama: ‘*Katiba ya Madina*’ iliyoweka na kuanisha mahusiano ya kila mmoja kwenye jamii ya kwanza ya kiislamu na ‘tamko la kimataifa la kwanza la haki za binadamu’ lililotolewa hapo Makkah kwenye Khutba ya Mtume SAW ya kuaga.

Na kwa mujibu wa *nususi* za Qur’an na Sunnah ambazo kwa pamoja ndio katiba ya kiislamu ni kama pale Allah SWT aliponena: “*Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani, na kuwapa jamaa; na anakataza uchafu, na uovu, na dhulma*..” (Surat al-Nahl: 90).

Pia akanena tena: “*Enyi mlio amini! Mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi*” (Surat al-Nisaa: 59);

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kwa hakika; kufuata *manhaj* (mfumo) wa kiustaarabu wa kiislamu kunatoa tena fursa kwa waislamu kuirudia nafasi yao na kutoa muelekeo wa kibinadamu kwa wote na kutoa mchango katika juhudi za kuikomboa dunia kutokana na dhulma kandamizi za *kimadia* (materialistic).

Mbili: Njia ya pekee ya kutibu gonjwa la ujinga na kuachwa nyuma kwa umma wa kiislamu ni kurudi kiukweli kwenye mafundisho ya dini sahihi; hali za kuhuzunisha wanazopitia waislamu zama hizi imetokana na kua mbali na mafundisho ya uislamu na badala yake kuiga mifumo ya kibinadamu ya kimagharibi.

Tatu: *Manhaj* (mfumo) wa kiustaarabu wa kiislamu uliojikita kwenye mpango thabiti, unaweza kuzikomboa jamii za kiislami na nchi zao kutokana na kutawaliwa, kufuata na kubaki nyuma (kushika mkia).

Nne: Ufahamu sahihi wa uislamu na ukweli katika kuzitekeleza hukmu zake kikamilifu ni msingi imara wa kufanikisha harakati za muamko wa kiislamu.

Tano: Kuimarisha msingi wa '*Shura*' (consultation) kinadharia na kivitendo kwa mujibu wa maelekezo ya Allah aliponena: "*na shauriana nao katika mambo*" (Surat Aal-Imran: 159), pia akanena tena: "*na mambo yao yakawa ni kwa kushauriana baina yao*" (Surat al-Shura: 38). Hii ni kwa sababu, 'Shura' ni msingi imara katika kuisimamisha dola ya kiislamu.

Sita: Inaruhusiwa kisharia kutenganisha mihimili ya dola: mhimili wa serikali (utekelezi), mhimili wa utungaji sheria na mhimili wa mahkama, kama ikivyokua wakati wa utawala wa kiislamu; enzi za makhalifa, jambo hili limetokana na utendaji wa Mtume SAW mwenyewe katika ufikishaji wake wa risala na uongozi wa kidini na kuhukumu.

Saba: Kukiri haki ya uraia kwa wote; waislamu na wasiokua waislamu kwa mujibu wa vigezo vya kisharia vya haki na wajibu.

Nane: Kumshirikisha mwanamke katika shughuli za kawaida bila kuharibu hukmu za kisharia zinazomhusu, amesema Allah SWT: "*Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi. Huamrisha mema na hukataza maovu*" (al-Tauba: 71).

Tisa: Ulazima wa kuharakisha kuachana na tabia hasi miongon mwa waislamu ili kuweza kuzishinda changamoto zinazowakanili, kama vile:

a) Mivutano ya kimadhehebu amabyo imekua vikwazo kwa maendeleo ya kinidhamu.
b) Ukakasi wa kifikra na kisilka unaoletea jamii matatizo mengi na kuamsha harakati potofu.
c) Ukanushaji uwepo wa Mwenyezi Mungu (Allah) au ukataaji wa dini kupitia kasumba ya kuitenga dini na maisha.
d) Upweke wa maarifa (elimu finyu): kunakomfanya mtu kutoona mambo kwa uhalisia wake.
e) Kutoifahamu thamani ya wakati na athari yake katika kufeli kwa waislamu na kubaki nyuma.

Na inausiwa yafuatayo:

a) Kuimarisha imani na amali njema; kwa kua mawili haya ndio hatua ya kwanza katika mchakato wa kimalezi unaolenga kumtengeneza muislamu barabara atakaeweza kurudisha ustaarabu wa kiislamu na kuchangia kwenye ustaarabu wa kibinadamu.
b) Kusisitiza kua ‘mfumo wa kiustaarabu wa kiislamu’ kusimika maadili mema ya kiislamu katika jamii.
c) Kuipongeza Malaysia kwa muelekeo wake wa kuingiza ‘mfumo wa uislamu wa kiustaarabu’ pamoja na kuitaka (Malaysia) iandae mkutano wa kielimu wa kimataifa utakaobainisha ukweli wa uislamu na madhumuni ya risala yake; natija na matokeo ya mkutano huu wa kielimu yawasilishwe kwa wanafikra na viongozi katika nchi za kiislamu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 164 (2/18)

Yanayohusiana na 'Kukuza Rasilimali-Watu katika Ulimwengu wa Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nane (18) kilichofanyika Putrajaya, (Malaysia) 24 - 29 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1428, sawa na 9 – 14 Julai, 2007.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kukuza Rasilimali-Watu katika Ulimwengu wa Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Rasilimali-watu; ni uwezo wa binadamu na ujuzi wake, kwa kuzingatia kua ndio kiini cha mchakato mzima wa maendeleo, na kwa kua binadamu huyu nu mwenye kusimamia mas'uli yake ya msingi ya kiimarisha hii dunia kama khalifa wa Allah juu ya dunia, kama alivyosema Allah SWT:

"*Na kina Thamud tuliwapelekea ndugu yao Saleh. Akasema: Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo*".[1]

Akasema tena:

"*Na pale Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika: Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa (mfwatizi)*".[2]

Mbili: 'Ufahamu (mtazamo) wa kiislamu' wa kukuza rasilimali-watu umejikita kwenye msingi unaosema kua: 'Kuiamirisha hii dunia na kusimamia kazi za ukhalifa hazitofanyika kwa ufanisi ila anapoandaliwa

[1] Surat Hud: 61.

[2] Surat al-Baqara: 30.

binadamu muweza wa kutekeleza majukumu kwa uweledi na umahiri, aidha, kumuandaa ba kuibua vipaji vyake na uwezo wake katika janibu mbalimbali za kiwiliwili, kiakili, kisaikolojia na kiroho.

Tatu: Kumkuza (kumuendeleza) binadamu kwa minajili ya kuhakikisha malengo ya maendeleo jumuishi kwa mtazamo wa kiislamu; hautimii ila kupitia malezi, elimu na maandalizi, na juu ya hili; 'Kongamano' linaonelea kuweka msisitizo juu ya maamuzi yake namba 138 (4/15) yaliyohusiana na 'kuisilimisha mitaala ya elimu' ambapo kuliusiwa mambo kadhaa yakiwemo:

- Kuisuka mikarara (matini) ya kielemu ndani ya 'mtazamo kamili wa uislamu' na kujitahidi kudhihirisha maono ya kiislamu (*Aqeedah*, Sharia na Mfumo wa Maisha) ndani ya mikarara.
- Kuipiga msasa mitaala ya kielimu na kimalezi iliyopo sasa katika ulimwengu wa kiislamu (nchi za kiislamu), na kuiboresha kwa namna ambayo itakusanya baina ya uasili wa kiislamu na usasa, kwa juhudi za ndani kwa ndani bila ya shinikizo za kutoka nje.
- Kuzitakasa elimu za sayansi katika nyanja mbalimbali kutokana na ufahamu mbovu ulioingizwa kwenye misingi ya kiislamu.
- Kuifanya elimu-msingi iwe ni ya lazima na ya bure (bila malipo) katika nchi zote za kiislamu ili kuweza kupambana na ujinga na kukiandaa kizazi kipya kwenye misingi ya uislamu na utamaduni wa kisasa.
- Kufanya kwa bidi kuondosha mkanganyiko katika mifumo ya elimu iliyopo kwa sasa, ili mchakato wa elimu uanzie kwenye misingi ya kiislamu bila ya kuvuruga mahitajio ya kisasa ya zama hizi, na kuwawezesha wanafunzi kupambana na changamoto za sasa na za baadae (mustakbali).
- Kuitaka 'Sekreterieti Kuu ya Kongamano la Fiqh' kwa kushirikiana na 'Shirika la Kiislamu la Elimu, Sayansi, na Utamaduni (ISESCO) na mashirika mengine yanayojihusisha na mambo haya, kuandaa 'Warsha Maalum' yenye maudhui ya: "**Kuisilimisha Mitaala (*Manahij*) ya Elimu"** pamoja na kufaidi na juhudi zilizotangulia katika eneo hili ili kuweza kuweka 'ufahamu jumuishi' na mpango-mkakati wa kuboresha na kusilimisha mifumo (mitaala) ya elimu katika ulimwengu wa kiislamu

(MW), natija zitakazopatikana ziwasilishwe kwa ‘Jumuia ya Nchi za Kiislamu (OIC) ili ziwafikie mawaziri wa elimu na malezi katika nchi zote za kiislamu.

Nne: ‘Ufahamu wa elimu zenye manufaa’ usiishie kwenye ‘elimu za dini’ pakee, lakini unatakiwa uwe ni uafahamu unaokusanya: ‘elimu za kidini za zile za kidunia zinazowanufaish umma na binadamu, na kwamba elimu hizo zinakua ni wajibu wa ‘*fardh al-kifaya*’ kwa kiasi cha manufaa kuweza kupatikana kwa umma.

Tano: Mifumo (mitaala) ya elimu inayolenga uandaaji wa nguvu-kazi za kibinadamu inatakiwa isheheni maadili na misingi ya kiustaarabu inayotokana na akida (imani) ya umma na mambo-msingi yanayomjenga binadamu kua na pupa (shauku) ya kutenda amali njema na kumoatia matumaini, misingi iliyo muhimu zaidi ni: maadili ya kiislamu yanayomfanya mtu kua na hima ya hali ya juu, kua na hisia ya uwajibikaji, uharakishaji wa kiutendaji, kulelewa kwenye misingi ya shura, kufanya kazi kwa pamoja, kuheshimu wakati, kujiamini, mawasiliano yenye kujenga, kuheshimu rai na mawazo ya wengine, ukosoaji wenye kujenga, kuheshimu tahasusi, kuthamini maarifa (ujuzi), kushajiisha *ijtihad* na kuibua vipaji, uhuru wenye kuwajibika, uadilifu, uaminifu, kuendana na wakati, kutizamia mustakbali na kuheshimu maadili ya kazi.

Sita: Taasisi zisimamiazo elimu zijuhusishe na kupangilia michakato ya kielimu na kuielekeza mitaala kwenye haja halisi za jamii za kiislamu kwa mujibu wa maono ya mustakbali ili kuweze kupatikana ulingano kamilifu wa binadamu atakaeweza kuhakikisha malengo ya maendeleo jumuishi kulingana na mtazamo wa kiislamu.

Saba: Ulazima wa kua makini kwenye kuandaa safu ya viongozi watendaji watakaoweza kuziendeleza kwa viwango vya juu taasisi za elimu na mafunzo katika nyanja mbalimbali zinazohitajika kwa ajili ya umma; huku wakiwa wamejikita kwenye nguzo mbili adhimu za uongozi, nazo ni: nguvu (uwezo) na uaminifu, kama alivosema Allah SWT:

“*Akasema mmoja katika wale wanawake: Ewe baba yetu! Muajiri huyu. Hakika*

mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu”.[1]

Akasema tena:

“*Yusuf akasema: Nifanye mshika khazina za nchi. Kwani hakika mimi ni mlinzi mjuzi*”.[2]

Na siku moja; Mtume SAW aliwahi kumuambia swahaba wake Abudharr al-Ghifaari RA:

”إنك ضعيف وإنها أمانة وإنها يوم القيامة خزي وندامة إلا من أخذها بحقها وأدى الذي عليه فيها“

“*Hakika ya wewe (Abudharr) ni dhaifu, na jambo hili (la uongozi) ni amana kubwa (mzito), na siku ya qiyama ni hizaya na majuto ispokua yule alielibeba jukumu hili kwa haki yake na akatekeleza wajibu wake juu yake*”.[3]

Nane: Kusukuma mbele tafiti za kisayansi na kushajiisha uwekezaji na kusaidia kwenye nyanja hizi muhimu za kumuamsha binadamu mwenye manufaa kwa umma na mwenye kuwatimizia haja zao.

Tisa: Kutokana na kua ‘*ummiya*’ (hali ya kutojua kusoma na kuandika) umeenea zaidi miongoni mwa wanawake katika maeneo memgi ya ulimwengu wa kiislamu; ‘Kongamano’ limapenda kusisitiza kwa namna mahsusi juu ya ulazima wa kujihusisha na kumuelimisha mwanamke na kumuandaa ipasavyo ili nae aweze kutoa mchango wake katika maendeleo ya jamii ya kiislamu, na hapa ‘Kongamano’ linapenda kuongeza msisitizo juu ya maamuzi yake namba 114 (8/12) yaliyohusiana na ‘*Tamko la Kiislamu juu ya Nafasi ya Mwanamke katika Maendeleo ya Jamii ya Kiislamu*’ na maamuzi mengine yanayohusiana na maudhui haya.

Kumi: Katika mbinu fanisi zaidi za kumuamsha binadamu ili kumrahisishia kufikia malengo ya elimu na kufikia maendeleo jumuishi; ni kua na pupa wa kuufanya muamko uwe unakamilishana na mambo mengine ya kimsingi, muhimu, katika hayo:

---

[1] Surat al-Qasas: 26.

[2] Surat Yusuf: 55.

[3] Imepokewa na Imam Muslim kwenye kitabu chake cha ‘Sahih’.

a) Utekelezaji wa sharia ya kiislamu katika nyanja mbalimbali, na juu ya hili; 'Kongamano' linaweka msisitizo juu ya maamuzi yake namba 48 (14/5) yanayohusiana na '*utekelezaji wa sharia ya kiislamu*'.
b) Kusambaza maadili ya uhuru wenye kuwajibika, uadilifu, amani kwa ufahamu wake mpana na jumuishi, kuachana na udikteta, utekelezaji wa misingi ya haki za binadamu kwa mujibu wa sharia ya kiislamu na misingi yake ambayo imekua chimbuko la 'kanuni ya kiislamu ya haki za binadamu'; kanuni iliyopitishwa na 'Kongamano'.

Kumi na moja: Kushajiisha na kuthamini juhudi za Malaysia na baadhi ya nchi za kiislamu katika kuibua 'muamko wa kiustaarabu' na kuandaa mazingira ya ufanikishaji wa viwango vya kukuza rasilimali-watu katika nchi nyingi za kiislamu.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kuandaa tafiti-tahasusi na warsha maalum kuangazia tatizo la kugura kuhama) kwa akili za kiislamu (*brain migration*) kutoka nchi za kiislamu kwenda nchi nyengine, na kubaini nini chanzo cha tatizo hili na kupendekeza njia muafaka za kutibu tatizo hili au kupunguza athari zake.
2) Ulazima wa kuratibu na kusaidiana miongoni mwa nchi za kiislamu katika nyanja za kimalezi, kielimu, kiutamaduni, kimafunzo na kubadilishana ujuzi faidifu kwa mujibu wa alivyosema Allah SWT:

   > "*Na saidianeni katika wema na uchamngu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui*".[1]

   hii ikiwa ni kuweka msisitizo juu 'Maamuzi ya Kongamano' namba 98 (1/11) yanayohusiana na '*umoja wa kiislamu*'.
3) Kushajiisha uanzishwaji wa vyuo tahasusi na vituo vya utafiti wa kisayansi vitakavujihusisha na kumuendeleza na kumkuza binadamu na jinsi ya kuibua vipaji vyao na ubunifu wao.
4) Kuandaa warsha tahasusi juu ya maudhui ya 'kuihamisha tekolojia na kuitaifisha katika nchi za kiislamu na kujihusisha na ufundishaji wa

[1] Surat al-Maaida: 2.

kielektroniki.

5) Kufaidi kutokana na ujuzi wa baadhi ya nchi za kiislamu na nyenginezo katika mbinu za kupambana na *ummiya* na kushajiisha mafunzo ya kiufundi na kiteknolojia.
6) Kujenga madaraja ya mawasiliano na ushirikiano baina ya ulimwengu wa kiislamu na wanasayansi waislamu waishio ughaibuni.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 165 (3/18)

Yanayohusiana na 'Kutanashati Mfumo wa Zaka katika Kupambana na Ufukara na Kuweka Nidhamu ya Ukusanyaji na Ugawanyaji kwa Kufaidika na Jitihada za Kifiqihi'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nane (18) kilichofanyika Putrajaya, (Malaysia) 24 - 29 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1428, sawa na 9 – 14 Julai, 2007.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kutanashati Mfumo wa Zaka katika Kupambbana na Ufukara na Kuweka Nidhamu ya Ukusanyaji na Ugawanyaji kwa Kufaidika na Jitihada za Kifiqihi,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Pesa ambazo hazikuainishwa kwenye Qur'an utoaji wake wa zaka; wanazuoni wanahitajika kufanya jitihada iwapo pesa hizo zinatoewa zaka au la, iwapo masharti na vigezo vya *ijtihad* yamepatikana.

Mbili: Sio lazma kwa mtoaji zaka kutoa zaka zake kwa aina zote nane (8) zilizotajwa katika Qur'an, lakini iwapo mtawala (serikali) au naibu yake (taasisi ya kiserikali) atasimamia ugwanyaji wa zaka basi watawajibika kutoa kwa aina zote nane iwapo mali yenyewe yanatosheleza kufanya hivyo na iwapo iko haja ya kufanya hivyo na inawezekana kuwafikia wote.

Tatu: Kimsingi, mali ya zaka anatakiwa kutolewa pale yanapostahiki au pale yanapopatikana, lakini inajuzu kuccchelesha utoaji wake; iwapo kuna maslahi kufanya hivyo au kumsubiria fukara wa karibu (ukoo) au kujiwekea mda maalum wa kutoa ambao ni muwafaka zaidi katika kuwatimizia mafukara na wahitaji; haja zao za kimaisha.

Nne: Fungu la mafukara na maskini:

- Mafuakara na maskini wagawiwe kiasi ya kinachokimu maisha yao na kuwatosheleza wao na wale waliopo chini yao ikiwezekana, kwa mujibu wa watakavyoonelea taasisi husika za kugawa zaka.
- Iwapo fukara ana ujuzi wa kazi fulani asi agawiwe kiasi atakachoweza kununulia vitendea (ala) kazi yake, na ikiwa ni mjuzi wa biashara apewe rasilimali ya kuanzishia biashara, akiwa ana ujuzi wa kilimo apewe shamba linalomtosheleza mavuno yake. Aidha anaweza kupewa rasilimali anayoweza kuanzishia kwenye miradi midogo ya ujasiriamali kama kituo cha ushonaji warsha za kazi za kiufundi ndogondogo ambazo zinamilikiwa na mafukara.
- Pia inajuzu kuweka miradi ya uzalishaji na ya kutoa huduma kwa kutumia pesa za zaka; kwa mujibu wa 'Maamuzi ya Kongamano' namba 15 (3/3).

Tano: Mafungu mengine ya wapokeaji zaka:

1) **Wafanyikazi ya ukusanyaji zaka:**

   a. Wafanyikazi ya ukusanyaji zaka kwa utekelezaji wa kisasa zinaingia taasisi, idara na washirika wanaotumikia zoezi la ukasanyaji zaka kutoka kwa matajiri na kuzigawa kwa mafukara kupitia vigezo kya kisharia.
   b. Taasisi za kusimamia mambo ya zaka zinatakiwa ziwe huru kwenye maamuzi yake ya kifedha na kiutawala na zisiwekwe chini ya vyombo vya dola vingine; hata hivyo zitabaki chini ya uangalizi na darubini ya kiserikali ili kulinda uwazi na ukweli wa shughuli zao na utekelezaji wa maelekezo ya kiutawala.
   c. Taasisi zilizofawidhiwa kusimamia ukasanyaji na ugavi wa zaka, ni zenye kuaminika kusimamia amana, hawatowajibika na maharibiko upotevu wa mali ila ikibainika kusudio hilo au kuzembea; ama mtoaji zaka hatokua na dhimma tena baada ya kukabidhi zaka zake kwa taasisi husika.

2) **'*Muallafat Quloob*' (kulainisha nyoyo):**

a. Fungu la '*Muallafat Quloob*' (kulainisha nyoyo) litaendelea kubaki milele, na linakua kulingana na haja na maslahi; wakati wowote ikionekana kua ipo haja au kuna maslahi ya kufanya hivyo basi fungu hilo litatolewa.

b. Inajuzu kutoa fungu la '*Muallafat Quloob*' kuwapatia waliosilimu wapya kama njia ya kuwathibitisha kwenye imani yao mpya na kufidia kile ambacho wantakua wamekikosa kwa kusilimu kwao, aidha, inafaa kumpatia asiekua muislamu ikiwa anatarajiwa kusilimu au kuepusha shari (dhara) ambayo angeifanya kwa waislamu.

c. Inajuzu kupeleka misaada kutumia mali ya zaka kwa waliofikwa na majanga miongoni mwa waislamu katika maeneo ya majanga, mitetemeko, mafuriko na njaa ili kuzilainisha nyoyo zao.

3) **Watumwa:**

a. Fungu la watumwa pia linaweza kutumika kwa mateka wa vita waislamu kama fidia ya kuachiliwa.

b. Inajuzu kutumia pesa za zaka kuwakomboa waislamu waliotekwa nyara na maharamia.

4) **Wenye madeni:** Fungu la wanaodaiwa ima ni wale wenye madeni ya binafsi au madeni kwa ajili ya kupatanisha walioteta kwa vigezo vya kisharia, aidha inaingia pia kugharimia fidia inayotokana na kuua kimakosa kwa wale wasiokua na familia (ukoo) ya kuwalipia, deni la maiti ambae hakuacha pesa za kulipia deni lake; yote haya ikiwa hazina ya umma (dola) haijawalipia.

5) **Waliojitolea Fiy-sabilillah:** Hili ni fungu la 'Mujahidina' kwa njia ya allah na wapiganaji wanaolinda nchi zao kwa njia za halali.

6) **'*Ibn al-Sabeel*' (msafiri aliofikwa na matatizo):**

a. '*Ibn al-Sabeel*' ni msafiri safari isiokua ya maasia na akafikwa na matatizo kiasi cha kukosa gharama (nauli) ya kurudi mjini mwake, hata kama yeye nia tajiri huko mjini mwake

b. Kutoa misaada ya kifedha kupitia uanzishwaji wa sanduku maalum ya kusaidia wakimbizi ima wawe ndani au nje ya nchi; ima kwa

sababu ya vita au mafuriko au njaa au mitetemeko na sababu nyenginezo.

c. Kusaidia wanafunzi mafukara ambao hawana wenye kuwapatia ufadhili (scholarship) kwenda kusoma nje ya nchi zao kulingana na taratibu zinazotumika.
d. Wahamiaji wanaoishi kwa njia isiokua halali kwenye nchi za kigeni, na ambao wamekatikiwa na mbinu za usafiri; wanapewa kutokana na pesa za zaka zitakazowawezesha kurudi nyumbani.
e. Kuwatimizia wanafunzi na wasafiri walioishiwa na pesa za kujikimu.

Mapendekezo:

Kulingana na haja iliopo kwa umma wa kiislamu ya kupangilia mfumo wa zaka na kuiweka kwenye misingi ya kitaasisi kuanzia ukusanyaji hadi ugawanyaji wa zaka kwa njia za kisasa na kufuata taratibu zote za kisharia; ‘Baraza la Kongamano’ linazitaka taasisi husika za zaka za ulimwengu wa kiislamu kuan a ushirikiano wa karibu na kuratibu juhudi zao kufikia uanzishwaji wa miradi ya pamoja ya kusaidia maskini na mafukara.

Aidha, inausiwa yafuatayo:

1) Kuwataka watoaji zaka walipe zaka zao kupitia taasisi husika zilizosajiliwa na kupata leseni za kiserikali ili kuhakikisha kua zaka hizo zinawafikia walengwa wastahiki, na kuhamasisha nafasi zao (taasisi) kidini, kimaendeleo, kijamii na kiuchumi.
2) Kushikilia upande wa kiutangazaji wa zaka kupitia vyombo vyote vya habari-mawasiliano za kuonekana na kusikizwa na nyenginezo ili kuihamasisha jamii juu ya nafasi ya zaka na umuhimu wake katika kujenga jamii na uchumi.
3) Kuweka taratibu muwafaka za kisharia na kiuhasibu za mifuko ya zaka.
4) Kuweka mifumo-elekezi ya kiuhasibu ya zaka kama miongozo ya kudhibiti kila mfuko wa zaka itakayosaidia utekelezaji wa kivitendo wa taratibu-tajwa kisharia.
5) Kufaidi kutokana na teknolojia ya habari na mitandao ya mawasiliano na chaneli za vin’gamuzi katika kuelimisha waislamu juu ya kadhia za kisasa za zakana nafasi yake katika kuleta maendeleo ya kijamii na

kiuchumi kwa umma mzima wa kiislamu.

6) Kuzisihi nchi za kiislamu kupunguza kodi kwa watoaji zaka kwa kuzingatia zaka watowazo kua ni sehemu ya kodi juu yao, ili kuhamasisha waislamu wengine watoe zaka za mali yao.
7) Kuingiza na kusomesha somo la Fiqhi na Uhasibu-zaka kwenye taasisi na vyuo vikuu, ikichukuliwa kua zaka ni nguzo ya tatu katika uislamu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 166 (4/18)

Yanayohusiana na 'Tatizo la Kuwaogopesha Watu Dhidi ya Uislamu (*Islamophobia*): Changamoto na Mapambano'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nane (18) kilichofanyika Putrajaya, (Malaysia) 24 - 29 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1428, sawa na 9 – 14 Julai, 2007.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Tatizo la Kuwaogopesha Watu Dhidi ya Uislamu (*Islamophobia*): Changamoto na Mapambano,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya.

Na baada ya kujikumbusha athari mbaya zitokanazo na '*Tatizo la Kuwaogopesha Watu Dhidi ya Uislamu (Islamophobia)*, ambazo zimeibua hisia na wimbi kali la chuki dhidi ya uislamu na kushinikiza waislamu katika nchi nyingi duniani, huenda ikawa haya ni kwa sababu za chuki za kihistoria na uchafuzi wa uhalisia wa uislamu, pia huenda ikawa ni mapungufu ya waislamu wenyewe kutoifahamisha dunia vizuri maana halisi ya uislamu.

'Kongamano' likiwa linatambua vyema athari mbaya zitokanzo na tatizo hili;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Ulazima wa kupambana na tatizo hili kupitia mpango-mkakati maalum utakaoandaliwa na nchi na mashirika ya kiislamu ya kimataifa, na mashirika yanayowakilisha waislamu nje ya nchi za kiislamu; mikakati hii ionyeshe taratibu-jumuishi muwafaka zitakazozingatia nyanja za kimawasiliano, kisiasa, kiuchumi na kijamii. Aidha, ipo haja ya kuandaa 'risala ya kimawasiliano iliyo wazi' ya kelezea uhalisia wa dini ya kiislamu na kubainisha ukweli wake, misingi na maadili ya hali ya juu ya uislamu, na kuzisambaza jumbe hizi kupitia vyombo mbalimbali vya habari-mawasiliano, mitandao ya kimataifa ya intaneti na ushiriki wa vyombo vya habari vyenye ushawishi wa kimataifa.

Mbili: Ulazima wa kushauriana na kuratibu miongoni mwa nchi za kiislamu na mashirika a kimataifa ya kiislamu wakati wa kuchukua maamuzi na hatua zifaazo katika kuraddi juhudi za uchafuzi na udhalilishaji zinazoelekezwa dhidi ya umma wa kiislamu na alama zake nyeti.

Tatu: Kuitaka jamii ya kimataifa kushirikiana na kusimama pamoja na nchi, mashirika ya kiislamu na waislamu kwa ujumla kwnye mapambano haya dhidi hujma kali zinazoelekezwa kwa uislamu na waislamu wenyewe, aidha, jamii ya kimataifa inaombwa kueneza utamaduni wa upendo na ushirikiano mingoni mwa binadamu na kukemea uchukivu na ukatili, na kusimamia ushirikiano utakaoleta kheri kwa binadamu wote.

Nne: Kuwataka waislamu waishio nje ya ulimwengu wa kiislamu wawe ni mabalozi wa amani na usalama, na wabebe risala ya uislamu iliyo safi kabisa na kuifikisha kwa nchi na kwa wasiokua waislamu, aidha, wanatakiwa kujiepusha na matendo yoyote ambayo yatatoa picha mbaya ya uislamu katika nchi hizo, wawe mfano mzuri katika kushikamana na maadili na misingi ya kiislamu.

Aidha, 'Kongamano' linaziomba nchi za kiislamu kuwasaidia waislamu hawa ili waweze kuusoma na kuufahamu uislamu vizuri na kuwapa taarifa wajue nini kinachoendelea katika ulimwengu wa kiislamu, na waanzishe taasisi zitakazowasaidia kukuza mahusiano yao na umma wa kiislamu.

Tano: Kutambua vitabu na machapisho yaayohusiana na tatizo hili la (islamophobia), na kuwasisitiza wanafikra wa kiislamu wenye uweledi wa lugha nyengine wawasiliane na wasaidiane kwenye kusahihisha na kurekebisha picha ya uislamu na waislamu waliioko ndani na nje.

Sita: Kuandaa *madu'at* (walinganizi) wanaokwenda nchi zisizokua za kiislamu, na kua na ufahamu mzuri wa lugha za nchi hizo na kushajiisha taasisi zinazosimamia program za kuandaa *madu'at* kama zipo; na kuunda taasisi kama hizo ikiwa hazipo, ili waandaliwaji wawe kielelezo kizuri katika uwasilishaji wa uislamu kisilka, kielimu na kimuamala na wengine.

Saba: Kujenga mahusiano mazuri na wengine kwa misingi ya kuheshimiana na uwasilishaji wa risala ya uislamu iliyo safi, kwa minajili ya kufahamiana na kupalilia suala hili kwenye mitaala ya elimu.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kukifanyia kazi kifungu cha nne, ibara ya sita (6) ya sheria-msingi ya 'Kongamano' inayohusiana na: (*uanzishwaji wa vituo na taasisi za masomo ya kiislamu katika maeneo muhimu nje ya ulimwengu wa kiislamu, na kushirikiana na vituo vilivyopo ili kufikia malengo ya Kongamano, na kufatilia machapisho yanayosambazwa kuhusu uislamu katika maeneo yaliyopo chini ya duara ya kazi zake na kusahihisha kasumba mbaya dhidi ya uislamu*), vituo hivi vinavyokusudiwa kuanishwa vitaandaa tafiti za kina juu ya 'Umagharibi' na kupendekeza mpango-mkakati muwafaka utakaotoa dira ya muelekeo wa nchi za kiislamu na watu wake namna ya kuamiliana na nchi za kimagharibi, na pia kuamiliana na wadau wengine wenye ushawishi juu ya serikali za kimagharibi na jamii zao.

2) Ipo haja ya kuratibu juhudi na kituo-msingi kilichoanzishwa na 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC) kwa minajili ya ufuatiliaji wa kadhia za uislamu kwenye vyombo vya habari vya kimagharibi, na kusaidia kusahihisha picha ya uislamu kwenye mitaala ya kielimu ya kimagharibi, kadhalika kuraddi kasumba mbaya kwa kuweka taswira halisi ya uislamu wa ukweli kwa kuhirikiana na 'Kongamano'.

3) Kuandaa warsha za kielimu, kisayansi na kifikra baina ya wasomi wa kiislamu na wasiokua waislamu kwa minajili ya kujenga madaraja ya mawasiliano na kufahamiana.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 167 (5/18)

Yanayohusiana na 'Makusudio Makuu ya Sharia na Nafasi yake katika Kutohoa (*istinbati*) Hukumu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nane (18) kilichofanyika Putrajaya, (Malaysia) 24 - 29 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1428, sawa na 9 – 14 Julai, 2007.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Makusudio Makuu ya Sharia na Nafasi yake katika Kutohoa (istinbati) Hukumu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: 'Malengo makuu ya shari'a' ni maana, busara na malengo makuu ambayo sharia ya kiislamu inakusudia kuyafikia kupitia hukumu mbalimbali zinazowaletea waja maslahi ya duniani na ya akhera.

Mbili: Uzingatiaji wa 'makusudio makuu' kwenye kufanya '*ijtihad* ya kisharia' unasaidia kutekeleza mambo mengi yakiwemo:

1) 'Mtazamo-jumuishi' wa *nususi* (maandiko) za sharia na hukmu zake.
2) Kuchukulia 'makusudio makuu' ya sharia kua na uzito wa kuamua wakati wanapokhitalifiana wanazuoni.
3) Kutambua matokeo ya mwisho ya matendo ya waja na kuteremsha hukmu za sharia juu yake.

Tatu: Kuyazingatia 'makusudio makuu' ya sharia kwa ngazi zake mbalimbali kua ndio kalibu-msingi (framework) mnasibu (muwafaka) ya haki za binadamu.

Nne: Umuhimu wa kuzingatia 'makusudio makuu' ya sharia wakati wa

‘*ijtihad*’ (mchakato wa kutohoa hukmu).

Tano: Utekelezaji mizuri wa ‘makusudio makuu’ ya sharia hakupingani na ‘*dalili za nususi za kisharia*’ wala na ‘*ijmaa*’ sahihi.

Sita: Umuhimu wa kudurusu vipimo mbalimbali vya ‘makusudio makuu’ ya sharia kwenye nyanja za kijamii, kiuchumi, kimalezi, kielimu, kisiasa na nyenginezo.

Saba: Umuhimu wa kujikumbusha ‘makusudio makuu’ ya sharia katika kuufahamu ujumbe wa sharia vizuri.

Nane: Umuhimu wa kuyafanyisha kazi ‘makusudio makuu’ ya sharia katika ufafanuzi wa hukmu za sharia kwenye matukio mapya kwenye ‘miamala ya kifedha ya kisasa’ na mengineo ili kufikia kiwango cha ubora katika lugha (misamiati) na taratibu za kiislamu, ili ziangatike juu ya zile taratibu za kawaida.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kuitaka ‘Sekreterieti Kuu ya Kongamano’ iagize wataalamu waandae tafiti za ziada zitakazofasili na kufafanua kwa uwazi zaidi na ufasaha: ‘Makusudio makuu ya sharia’ na juhudi za wanazuoni na watafiti juu ya jambo hili.
2) Kuzitaka taasisi na vituo vya kielimu kulifundisha somo la ‘makusudio makuu’ ya sharia kwenye mitaal yao ya kielimu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 168 (6/18)

Yanayohusiana na 'Kuainisha Umri wa Kubalighi na Athari yake katika Uwajibikaji (*Taklif*)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nane (18) kilichofanyika Putrajaya, (Malaysia) 24 - 29 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1428, sawa na 9 – 14 Julai, 2007.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kuainisha Umri wa Kubalighi na Athari yake katika Uwajibikaji (*Taklif*),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya.

Na baada ya kujikumbusha kua 'akili' ndio sababu ya ukalifishwaji (*taklif*), mtoto mdogo hakalifishwi kisharia ila afikapo umri fulani unaoashiria kukomaa kiakili na kutimia utambuzi, zipo alama za kimwili zinazoashiria hayo, ama kuainisha umri maalum iwapo alama za kimwili hazitoshelezi kubaini iwapo mtoto huyu sasa amealighi inawafikiana na misingi ya sharia na makusudio yake makuu, sharia inataka kujieka mbali na kuadhibu kisharia kadri inavyowezekana;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Umri wa utambuzi (*tamyiiz*) unaokuja kabla kubalighi ni umri wa mika saba; hapa matendo ya mtoto huyu hayana athari kisharia (batili), lakini matendo ya mtoto huyu mtambuzi (*mumayyaz*) ya kifedha yamegawika sehemu mbili: matendo yenye kumfaa na kumnufaisha, yanakua ni sahihi na ni yenye kutekelezwa, matendo yanayoingia kwenye kumnufaisha na kumdhuru; hapa itasubiriwa idhini ya mmiliki wa matendo hayo. Ama matendo yenye kumdhuru tu basi hayazingatiwi.

Mbili: Kwa kua kubalighi kumefungamana na ukuaji kimwili na kufikia umri

fulani ambapo mtoto sasa anakua ‘mtambuzi’ hivyo basi; ‘bulughi’ ya kawaida inazingatiwa kwa zile alama zinazoashiri hivyo, ama ‘bulughi’ ya kiumri (kufikia miaka kumi na tano) inazingatiwa kwenye mambo ya kiibada, lakini mambo ya kifedha na kijinai anaachiwa ‘Mtawala’ (serikali) kuamua na kuainisha ni umri upi muawafaka kwa vigezo vya maslahi kulingana na mazingira ya sehemu husika.

Tatu: Haijuzu kuhukumiwa asiebalighi kwa adhabu ya ‘*Haddi*’ au ‘*Kisasi*’, adhabu yake inaishia kwenye ‘*Taazir*’ kuaziriwa na kuadabishwa atakayofawidhiwa msimamizi (serikali) wake, itakayonasibiana na umri wake.

Nne: Majukumu ya kifedha yanayotokana na maharibifu au kutahamali fidia hayapomoki kwa asiekua balighi kama ilivyo kisharia.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 169 (7/18)

Yanayohusiana na 'Haki na Majukumu ya Mwanamke wa Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nane (18) kilichofanyika Putrajaya, (Malaysia) 24 - 29 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1428, sawa na 9 – 14 Julai, 2007.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Haki na Majukumu ya Mwanamke wa Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya.

Na baada ya kujikumbusha kua uislamu umemuweka mwanamke kwenye nafasi yake stahiki na kumfanya kua ndio nguzo ya familia pamoja na kumuachia nafasi ya kufanya kazi na kumuandalia nafasi ya kuchangia, aidha, imempatia fursa ya kushiriki na kubuni, na umejihusisha nae kwa namna ya kipekee katika kumuelekeza, kumchunga na kumtimizia haki zake kamili. Uislamu umeusia kipekee akiwa kama mama, dada, binti na mke na kumueka sawa na mwanamume kwenye heshima ya kibinadamu na kwenye mambo ya aqeeda, faradhi za ibada, kuamrishana mema, kukatazana maovu, matendo mema, majukumu na malipo yake, haki ya kielimu na matendo ya kifedha; na ukaweka vigezo vya kisharia vinavyozingatiwa, na msingi mkuu ni kua maagizo yote ya 't*aklif*' (maamrisho ya kisharia) yanajumuisha wanaume na wanawake kisawasawa ila anapohusishwa fulani kwa agizo maalum;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Ni haki yake (rukhsa) mwanamke kumiliki anachotaka; iwe mali yanayohamishika na yasiyohamishika (real estate) kwa misingi na vigezo vya kisharia vya umiliki.

Mbili: Kazi ya mwanamke inadhibitiwa na vigezo vya kisharia, na

inamshajiisha mwanamke kufanya kazi kwenye nyanja ambazo ana uwezo na ufanisi mkubwa kulingana na maumbile yake; kama vile: malezi, kufundisha, kutibu wanawake na watoto (*gynecology and pediatrics*), na shughuli za kijamii.

Tatu: Inafaa kwa mwanamke kuchangia kwenye shughuli za kijamii, kiutamaduni, na kimalezi kwa namna ambayo haitogongana na misingi na mafundisho ya kisharia kulingana na vigezo vilivyowekwa.

Nne: 'Kongamano' linapenda kuweka msisitizo juu ya maamuzi yake namba 114 (8/12) na 159 (8/17).

Aidha, Kongamano linausia yafuatayo:

1) Kuanzishwa kwa 'Taasisi ya kiislamu ya kimataifa' itakayohusika na mambo ya wanawake, kazi ya taasisi hii iwe ni kufuatilia kadhia za wanawake na mikutano ya kimataifa inayohusiana na mambo ya wanawake pamoja na kushiriki kwenye mikutano kama hio.
2) Kushirikiana na taasisi za kimataifa kwa minajili ya kulinda familia na watoto dhidi ya harakati hatarishi zinazowatishia.
3) Kuzitaka nchi wanachama kupinga vifungu vya miafaka ya kimataifa vinavyobeba mikhalafa ya kishaaria.
4) 'Kongamano' linausia kufanywe tafiti za ziada kuhusu: 'haki za mwanamke za kisiasa, ukadhi na uongozi wa juu (urais).

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 170 (8/18)

Yanayohusiana na 'Mikataba ya Kushirikiana Kiwakati (*Time Sharing*)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nane (18) kilichofanyika Putrajaya, (Malaysia) 24 - 29 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1428, sawa na 9 – 14 Julai, 2007.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Mikataba ya Kushirikiana Kiwakati (*Time Sharing*),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Fasili ya 'Kushirikiana Kiwakati': Ni mkataba wa kumiliki hisa kwa pamoja, ima kwa kununua kitu maalum au kukodi kwa pamoja kwa manufaa ya kitu kila mmoja kwa wakati wake, au kukodi manufaa ya kitu kwa kipindi fulani kwa namna ambayo kila mmoja atanufaika na kitu kilichomilikiwa au manufaa yaliyokodiwa kwa kugawiana wakati au sehemu pamoja na uwepo wa hiari ya kuainisha kwa kuhusisha kila mmoja wakati maalum.

Mbili: Aina za 'Kushirikiana Kiwakati': Kushirikiana Kiwakati' iko namna mbili:

a) Umiliki kamilifu (wa kitu na manufaa) kwa kununua hisa ya pamoja kupitia mkataba wa kuuziana kwa manufaa ya pamoja ndani ya mida inayofuatana.
b) Umiliki pungufu (wa manufaa pekee) kwa kukodi hisa ya pamoja ya manufaa kupitia mkataba wa *ijara* kwa manufaa ya pamoja ndani ya mida inayofuatana.

Tatu: Hukmu ya kisharia ya 'Kushirikiana Kiwakati':

a) Inajuzu kisharia kununua hisa ya pomoja ya kitu (mali) au kukodi hisa ya pamoja ya manufaa ainishwa kwa mda maalum pamoja na kuafikiana na mmiliki wa kitu (mali) au manufaa yake kwa matumizi kwa njia ya kugawiana mda au sehemu, nisawa maafikiano haya yawe yamefanyika na mmiliki mubashara au kupitia kwa wakala wake anaesimamia umiliki wa pamoja, hamna tatizo kuizungusha hisa ya pamoja ima kwa kuiuza au kuinunua au kutoa zawadi au kurithiwa au kuwekwa rehani na yasiokua hayo katika matendo ya kisharia anayoruhusiwa mmiliki wa kitu (mali) juu ya anachomiliki; hakuna katazo la kisharia juu ya hili.
b) Vigezo vya kisharia vya mkataba; kuuza au kukodisha vinatumika kwenye muamala huu wa ‘kushirikiana kiwakati’.
c) Kwenye muamala wa *ijara* inamlazimu mkodishaji gharama za matengenezo ya kimsingi ambayo bila matengenezo hayo hakuna maana ya kukodisha. Ama matengenezo madogo madogo ya kila siku inajuzu kumshurutisha mkodishwaji, na iwapo mkodishaji amegharamikia basi mkodishwaji atalipa mfano wa gharama hizo au kwa mujibu wa wakuvyokubaliana.

   Ama kwenye muamala wa kuuziana basi mmiliki ndie atakaegharamika kwa kua ni sehemu ya umiliki kwa kiwango cha hisa yake ya kiwakati au sehemu katika ‘umiliki wa pamoja’.
d) Hakuna katazo la kubadilishana hisa katika umiliki wa kiwakati wa pamoja kati ya wamiliki wa kitu (mali) au manufaa ya pamoja, nisawa mabadilishano haya yanafanyika mubashara baina ya wamiliki au kupitia kampuni (wakala) maalum za kazi hizo za kubadilishana.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 171 (9/18)

Yanayohusiana na 'Haki za Uwepesishaji na Utejelezaji wake wa Kisasa Kwenye Umiliki wa Pamoja'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nane (18) kilichofanyika Putrajaya, (Malaysia) 24 - 29 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1428, sawa na 9 – 14 Julai, 2007.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Haki za Uwepesishaji na Utejelezaji wake wa Kisasa Kwenye Umiliki wa Pamoja,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Fasili ya Haki za Uwepesishaji: Haki za Uwepesishaji ni zile zinazothubutu kwenye nyumba (au mali) juu ya nyumba nyengine miongoni mwa mambo ya manufaa kwa wote na yanayokubali ushirikiano.

Mbili: Uwepesishaji uko aina nyingi na unaendelea kuzuka aina mpya kila wakati. Kilichoelezewa na wanazuoni zamani ni:

1) Haki ya maji: nayo ni mzunguko wa wa kunufaika na maji kwa kunyoshea mimea au kuwapatia wanyama au kupitisha maji kutoka nyumba hadi nyingine.
2) Haki ya kupitisha maji (mtaro): nayo ni kupitisha maji yasiyohitajika au yasiyofaa kunywa kutoka ardhi iliyoangatika kwenda kwenye ardhi inayotakiwa ipate maji hayo, au kuyapitisha yaende kwenye mtaro mkuu (wa maji taka).
3) Haki ya kupita (njia): nayo ni haki ya mtu kupita kwenda kwenye ardhi yake kupitia ardhi jirani na ardhi yake.
4) Haki ya kupanda juu (kuangatika): nayo ni sehemu ya juu ya mjengo

(nyumba) yenye ghorofa mbili au zaidi, ambapo nyumba ya chini inamilikiwa na mwengine.

Tatu: Haki za uwepesishaji zinapatikana kwa sababu zifuatazo:

1) Idhini ya mmiliki wa mali binafsi ima kwa njia ya kuuza au kuchangia.
2) Dharura.
3) Kuhuisha ardhi maiti (isiyotumika kwa mda mrefu).
4) Ujirani na milki za pamoja.
5) Sababu nyengine zozote za uwepesishaji za kisasa ambazo zitakua ni zenye kizingatiwa kisharia iwapo hazitogongana na *nususi* za sharia na misingi yake mikuu; mithili ya nyaya za umeme au paipu (mabomba) za maji taka.

Nne: Hukumu:

1) Msingi mkuu unaotumika kwenye ‘haki za uwepesishaji’ ni uhalali iwapo kuna manufaa, na iwapo kuna madhara basi ni haramu. Ama maji mahsusi yanayomilikiwa si haki ya wengine il wakati wa dharura na kwa thamani ya mfano wake.
2) ‘Haki za uwepesishaji’ ya maji na kuyapitisha imethubutu kwa nyumba na mashamba na mfano wake, kwa mujibu wa desturi zilizopo. Kwa mfano: ‘uwepesishaji kwa kupitisha paipu (mabomba) ya uendeshaji viwanda au kupitisha maji-taka, kwa sharti ya kutodhuru wengine.
3) Haki ya kupanda juu (kuangatika) imethubutu kwa mmiliki na ana uhuru wa kufanya anachotaka ima kwa malipo au bila ya malipo kwa mujbu wa sheria zilizopo.

Tano: Uwepesishaji wa kisasa:

Desturi za kisasa zinakubali kua miongoni mwa ‘Haki za uwepesishaji’ ni kupitisha huduma za umma kama vile: umeme, mabomba ya maji, mabomba ya gesi, mabomba ya maji-taka na kiyoyozi (air-condition) kikuu.

Sita: Hukmu za Uwepesishaji wa kisasa:

Maegesho ya magari iwapo ni mahsusi kwa majumba, masoko na sehemu

za biashara; yanakua ni sehemu ya kitu (mali) ambayo imeruhusiwa kuegesha kwa ajili ya mali yoyo.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 172 (10/18)

Yanayohusiana na 'Idhini Kwenye 'Amalia (*Operesheni*) za Upasuaji za Haraka'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nane (18) kilichofanyika Putrajaya, (Malaysia) 24 - 29 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1428, sawa na 9 – 14 Julai, 2007.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Idhini Kwenye 'Amalia (Operesheni) za Upasuaji za Haraka,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Inajuzu kuchukua tahadhari na taratibu za kitiba za lazima katika hali za dharura (*Emergency*) bila ya haja ya kupata rukhsa ya mgonjwa au msimamizi wake katika hali zifuatazo:

a) Afikapo mgonjwa akiwa kwenye hali ya kupoteza fahamu au hali ambayo ni vigumu (muhali) kupata idhini yake.
b) Awe mgonjwa yuko katika hali ya hatari kiafya inayoweza kumpelekea kifo, panahitajika uharaka wa daktari kumshighulikia kabla ya kupata rukhsa.
c) Iwapo mgonjwa hana msimamizi au mtu wake wa karibu mwenye haki ya kutoa rukhsa, na wakati ukawa finyu.

Mbili: Uharakishaji wa daktari (bila ya idhini ya mgonjwa) kwenye hali kama hizo unakubalika kwa masharti yafuatayo:

a) Aina ya tiba anayopewa iwe ni ile inayokubalika na taasisi za kiafya husika.
b) Ulazima wa uwepo wa daktari bingwa pamoja na timu yake isiyopungua angalau madaktari watatu watakaokubaliana kutambua ugonjwa na

tiba-pendekezi, pamoja na kusajiliwa nukta zote za mchakato huo na kusainiwa na timu hio.

c) Hakikisho la kua faida za kumtibu zinazotarajiwa ni kubwa ikilinganishwa na hasara za kutomtibu, na kujaribu kupunguza tena madhara kadri inavyowezekana.
d) Anapozinduka mgonjwa ni wajibu wa daktari kumfafanulia yote yaliyojiri kiukamilifu.
e) Matibabu anayofanyiwa yawe ni ya bure; na iwapo kuna gharama (malipo) basi iwepo taasisi nyengine huru ya kuatathmini gharama.

Tatu: Kuakhirisha utoaji wa maamuzi juu ya hali zifuatazo hadi kikao kijacho:

1) Operesheni za dharura (haraka) mithili ya: 'Uvimbe wa kidole-tumbo' (*Inflammatory Appendix*) iwapo mgonjwa amekataa kutoa idhini.
2) '*Janin*' (Mjusi) ambae amezungukwa shingoni mwake na kamba ya kitovu, na hakujapatikana idhini ya kufanyiwa upasuaji wa sizeria (*cesarean*) wa kumuokoa mtoto.
3) Inapohitajika kwa mtoto mgonjwa kufanyiwa upasuaji wa dharura kama vile operesheni ya kidole-tumbo au kusafishwa figo na kupewa damu, na msimamizi wake akakataa mtoto huyu afanyiwe matibabu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 173 (11/18)

Yanayohusiana na 'Operesheni ya Kujirembesha (*Plastic Surgery*) na Hukmu Zake'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nane (18) kilichofanyika Putrajaya, (Malaysia) 24 - 29 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1428, sawa na 9 – 14 Julai, 2007.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Operesheni ya Kujirembesha (*Plastic Surgery*) na Hukmu Zake,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Fasili ya 'Operesheni ya Kujirembesha': Operesheni ya Kujirembesha inahusika na kuboresha (na kubadilisha shakli) sehemu ya au za mwili wa binadamu za Dhahiri (nje), au kuzifanya zirudie kufanya kazi yake iwapo ziliathirika.

Mbili: Vigezo na masharti ya kufanya Operesheni ya Kujirembesha:

1) Uwe upasuaji huu unaleta maslahi yanayokubalika kisharia, kama kurudishia kazi au kusilihisha (kurekebisha) kasoro na kulirudisha umbile kama lilivyokua.
2) Usiwe upasuaji huu unaleta madhara zaidi ya maslahi yanayotarajiwa kwenye opersheni hii, wataalamu bingwa na wabobezi wa suala hili walio waaminifu watashauri.
3) Asimamie zoezi zima; daktari bingwa aliesomea, kinyume chake atawajibika na athari yoyote itakayojitokeza kwa mujibu wa 'Maamuzi ya Kongamano' namba 142 (8/15).
4) Zoezi la upasuaji (operesheni) lifanyike kwa idhini mgonjwa (anaetaka

upasuaji).

5) Daktari muhtasi amfahamishe mgonjwa wake atakaefanyiwa upasuaji, hatari zozote zinazotarajiwa au matatizo yatakayotokana na upasuaji huo.
6) Iwe hakuna njia nyingine ya matibabu yenye athari ndogo na isioharibu mwili kwa upasuaji.
7) Pasijitokeze mkhalafa wowote wa *nususi* za sharia kama alivyosema Mtume SAW kwenye hadith anayoipokea ‘Abdullah bin Mas’oud:

"لعن الله الواشمات والمستوشمات والنامصات والمتنمصات والمتفلجات للحسن المغيرات خلق الله"

“*Allah Amewalaani wanawake wanaochora miili yao kwa tatoo na wale wanaowachora, na Amelaani wanawake wanaotoa nywele za usoni mwao na wale wanaowatoa, na Amelaani wanawake wanatengeneza mianya kwenye meno yao wakitafuta urembo huku wakiharibu umbile la Allah*”[1]

Akasema tena Mtume SAW kwenye hadith ya Ibn Abbas:

"لعنت الواصلة والمستوصلة والنامصة والمتنمصة والواشمة والمستوشمة من غير داء"

“*Amelaaniwa mwanamke anaeunganisha nywele na yule anaemuunganisha, amelaaniwa mwanamke aneotoa nywele za usoni mwake na yule anaemtoa, amelaaniwa mwanamke anaechora mwili wake kwa tatoo na yule anaemchora pasina uwepo wa ugonjwa*”.[2]

Aidha, amekataza Mtume SAW wanawake kujifananisha na wanaume, na wanaume kujifananisha na wanawake, kadhalika zipo *nususi* (hadith) nyengine zinazokataza kujifananisha na watu wengine (wasiokua waislamu) au watu wa uchafu na maasia.

8) Misingi (maadili) ya utabibu izingatiwe kama vile kutokaa faragha baina ya mwanamume na mwanamke, kutodhihirisha *aura* (utupu) na mengineo ila itokeapo dharura isioepukika.

[1] Imepokewa na Imam al-Bukhari.
[2] Imepokewa na Imam Abudaud.

Tatu: Hukmu za sharia:

1) Inajuzu kufanya upasuaji (operesheni) wa kujirembesha wa dharura na wa lazima kwa lengo la:

   a. Kurudisha shakli ya viungo vya mwili kama vilivyokua kwenye umbile lake la asili, kama alivyosema Allah: "*Bila ya shaka tumemuumba mtu kwa umbo lilio bora kabisa*" (Surat al-Tin: 4).
   b. Kuvirudishia viungo kazi zake za asili.
   c. Kurekebisha kasoro za kimaumbile kama vile: mdomo uliopasuka, pua iliopinda vibaya sana, alama ya kuzaliwa nayo, kilichozidi kwenye vidole au meno, vidole vilivyoshikana ambavyo kubaki hivyo kunamletea adha na maumivu.
   d. Kurekebisha kasoro zilizojitokeza zilizosababishwa na kuungua kwa moto, ajali za barabarani, maradhi na nyenginezo; zinazohitajia mathalan: kupandikizwa kwa ngozi, na kuweka kiraka, kurudisha shakli ya titi lote ikiwa limekatwa au baadhi yake likiwa ni kubwa au dogo na ingemsababishia maradhi ikibaki hivyo, na kupandikiza nywele ambazo zimedondoka khasa kwa mwanamke.
   e. Kuondosha ubovu wa kimwili ambao unamsababishia mtu adha ya kisaikolojia na ya kimwili. (Maamuzi ya Kongamano namba 26 (1/4).

2) Haijuzu kufanya operesheni (upasuaji) wa kujirembesha kwa ajili ya kutafuta tu uzuri, na si kwa lengo la tiba, bali kwa kusudio la kubadilishe umbile sahihi la binadamu kwa kufuata utashi wa nafsi na kuiga wengine; kama vile: operesheni za kubadilisha shakli ya uso ili uwe na muonekano fulani, au kubabaisha watu na kudanganya vyombo vya sheria, au kubadilisha shakli ya pua kwa kuifanya kubwa zaidi au ndogo zaidi, au kudogosha midomo na kubadilisha shakli ya macho na kukuza zaidi mashavu.
3) Inajuzu operesheni ya kupunguza mwili (kukonda) kwa taratibu za kisayansi zinazokubalika kama vile operesheni ya kufyonza mafuta, ikiwa (uzito wa) mwili unamsababishia maradhi na hakuna njia nyengine ya kukata mwili ispokua upasuaji; kwa sharti ya kutosababisha madhara.
4) Haijuzu kuondosha mikunjo ya ngozi kwa operesheni au au kwa

sindano; ila ikiwa hali hio ni ya ugonjwa na kwa sharti ya kutosababisha madhara.

5) Inajuzu kuunganisha ubikira (kizinda) uliochanika ima kwa ajali au ubakaji au kutenzwa nguvu; lakini haijuzu kisharia kuunganisha ubikira uliochanika kwa ajili kutenda tendo chafu ili kutotoa nafasi ya udanganyifu na ufisadi, jambo ni bora likasimamiwa na madaktari wa kike.
6) Ni wajibu wa daktari muhtasi (bingwa) kufuata maadili ya kisharia kwenye kazi zake za tiba, na ni juu yake kuwapa wagonjwa wake wa 'Operesheni ya kujirembesha' ushauri-nasaha mzuri, (*Dini ni kunasihiana*).

Aidha, inausiwa yafuatayo:

1) Siptali na kliniki mahsusi na madaktari; wanatakiwa kumcha Allah SWT, na wasijiingize kwenye operesheni zilizoharamishwa.
2) Ni juu ya madaktari na wapasuaji kujielimisha elimu ya fiqhi inayohusiana na hukmu za shughuli za kimatibabu hususan zile za 'Operesheni ya kujirembesha', wasifuate tamaa ya chumo la pesa bila ya kujiridhisha kwamba wanafuata hukmu za kisharia kisawasawa, na wasijiingize kwenye mkumbo wa matangazo ya kibiashara yanayokhalifu ukweli wa mambo.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 174 (12/18)

Yanayohusiana na 'Ukamilishaji wa Kuangazia Mambo Yanayofunguza Saumu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na nane (18) kilichofanyika Putrajaya, (Malaysia) 24 - 29 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1428, sawa na 9 – 14 Julai, 2007.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Ukamilishaji wa Kuangazia Mambo Yanayofunguza Saumu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na kwa kuiambatanisha na maamuzi namba 93 (1/10) yanayohusiana na '*Mambo Yanayofunguza Saumu Kwenye Matibabu*';

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha kuangazia maudhui haya hadi kikao kijacho; ili kutoa nafasi ya tafiti za ziada.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Kumi na Tisa (19) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Sharjah, UAE

1 - 5 Jumada al-Uula (Mfungo Nane), 1430,

sawa na 26 – 30 Aprili, 2009

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 175 (1/19)

Yanayohusiana na 'Uhuru wa Kidini (Kuabudu) Katika Sharia ya Kiislamu: Upeo wake na Vigezo vyake'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tisa (19) kilichofanyika Sharjah, (UAE) 1 - 5 Jumada al-Uula (Mfungo Nane), 1430, sawa na 26 – 30 Aprili, 2009.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Uhuru wa Kidini (Kuabudu) Katika Sharia ya Kiislamu: Upeo wake na Vigezo vyake,** na kutambua umuhimu wa kujadili maudhui haya ya 'uhuru wa kidini' kwenye 'Kongamano' kukidhi mahitajio ya mada hii ndani na nje ya nchi za ulimwengu wa kiislamu, na kujua ni upi msimamo wa 'Kongamano' juu yake kwa kuzingatia kua: Kongamano ndio rejea kuu ya kiislamu ya kifiqhi, na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Uhuru wa kidini (ibada) ni msingi unaokubalika na sharia ya kiislamu na umetokana na maumbile halisi ya binadamu unaombatana na uwajibikaji, kwa vigezo vilivyowekwa, lengo lake ni kuhakikisha upatikanaji wa heshima ya binadamu.

Mbili: Uhuru wa kuabudu umedhaminiwa na jamii na ni wajibu kuulinda dhidi ya fikra potofu na hatarishi zinazotoka nje na dhidi ya kila aina ya uvamizi wa kifikra unaolenga kuuyeyusha (kuuchafua) utambulisho wa kiislamu wa umma.

Tatu: Waislamu wanautekeleza msingi huu wa Qur'an: "*Hakuna kulazimishana katika dini*" (Surat al-Baqara: 256), na wameonyesha kwa vitendo katika historia yao jinsi ya kusameheana na kuishi na wengine ndani ya dola ya kiislamu, hivyo ni lazima kwa wasiokua waislamu

kuheshimu mila za kiislamu na kusitisha mazingira ya kashfa dhidi Mtume Muhammad SAW na matakatifu ya uislamu.

Nne: Tafauti za kiamadhehebu na kifiqhi ni jambo la kawaida, na waislamu kusaidiana ni wajib kisharia kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah licha ya tofauti zao za kimadhehebu. Uislamu unalingania kwenye '*aqeeda ya tauheed*' na kuunganisha neno la waislamu kwa msingi wa ushirikiano ni jambo lililohimizwa, na tunatakiwa kupeana nyudhuru kwa yale tunayokhitalifiana.

Tano: Kuweka mipaka ya uchafuzi dhidi ya mambo ya msingi ya uislamu na kutilia shaka yale yanayojulikana wazi katika uislamu ndani ya jamii ya kiislamu; kuendelea hivyo ni kuhatarisha uwiano wa jamii na dini. Wanaoeneza kashfa hizi wanajificha nyuma ya kisingizio cha 'uhuru wa kidini', kwa hio ipo haja ya kuzuia upotoshaji huu na kuilinda jamii kwenye misingi yake ya kidini na kifikra na kuzuia wasiokua waislamu kuendeleza kashfa zao.

Sita: Utoaji wa fatwa ya kuritadisha au kukufurisha; wahusika wake ni wanazuoni wanaokubalika, na mahkama ya kadhi inatakiwa kutekeleza agizo la wanafiqihi la kua: mkufurishwaji anapewa fursa ya kufanya toba na kufafanuliwa shaka alizonazo ndani ya mda wa kutosha kufanya hivyo kwa lengo la kulinda maslahi mapana ya sharia.

Saba: Kudhihirisha *ridda* (kuritadi) ni jambo hatarishi kwa umoja na mshikamano wa jamii ya kiislamu na aqeeda yao, aidha, inashajiisha wasiokua waislamu au wanafiki kuitumia kama silaha ya kueneza shaka, kwa maana hio mdhihirishaji *ridda* anastahiki adhabu kutoka mahkamani ili iwe funzo kwa wengine na kuilinda jamii na amani yake, hukmu hii haipinganni na msingi wa 'uhuru wa kidini' unaolindwa na uislamu kwa yule anaeheshimu hisia za kidini, maadili ya jamii na amani ya nchi.

Inausiwa yafuatayo:

Kuwataka viongozi (watawala) wa kiislamu kutoa nafasi kwa mahitajio ya msingi kwa jamii zao ikiwemo: 'uhuru wenye kuwajibika', chakula, makazi (nyumba), matibabu, elimu, fursa za ajira na mahitajio mengine

yatakayosaidia kuvilinda vizazi vipya dhidi ushawishi potofu unaoeneza fikra hatarishi kwa maadili ya uislamu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 176 (2/19)

Yanayohusiana na 'Uhuru wa Kutoa Maoni (Rai): Vigezo Vyake na Hukmu Zake'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tisa (19) kilichofanyika Sharjah, (UAE) 1 - 5 Jumada al-Uula (Mfungo Nane), 1430, sawa na 26 – 30 Aprili, 2009.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Uhuru wa Kutoa Maoni (Rai): Vigezo Vyake na Hukmu Zake,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Uhuru wa Kutoa Maoni (Rai) inakusudiwa pale binadamu anapokua na uwezo kwa uhuru wake na hiari yake kutoa maoni au rai kwa lile analoamini kua ni sawa na ni lenye kuleta manufaa kwake yeye na kwa jamii nzima. Nisawa yawe yanataalikiana na mambo binafsi au kadhia za jamii.

Mbili: Uhuru wa kutoa maoni ni haki inayolindwa katika uislamu ndani ya vigezo vya kisharia.

Tatu: Miongoni mwa vigezo vya msingi vya uhuru wa kutoa maoni:

a) Kutowakosea wengine kwenye maisha yao au heshima zao au utu wao au nafasi zao kama vile kuwadogosha, kuwadharau na kuwakejeli kwa njia zozote.
b) Kua na uangalifu, kujilazimisha na ukweli na uadilifu na kujieka mbali na utashi wa nafsi.
c) Kua na uwajibikaji na kulinda maslahi na maadili ya jamii.
d) Kutumia njia sahihi na halali za kutoa maoni (rai), haijuzu kutoa maoni kwa njia fisidifu au njia za ukosefu wa '*haya*' au ukiukaji wa maadili japo

maoni yenyewe ni sawa (sahihi), uhalali wa jambo usipelekee kutumia njia haribifu.

e) Iwe lengo la kutoa maoni ni kumridhisha Allah SWT na kutumikia maslahi ya jamii ya kiislamu ya binafsi na ya umma.
f) Izingatiwe matokeo ya mwisho na natija ya utoaji maoni, iendane sambamba na msingi usemao: '*pima baina ya maslahi na madhara; ni yepi mazito kuliko mengine*'.
g) Maoni yanayotolewa yawe yamejikita kwenye taarifa za ukweli na kuaminika, na iepukwe uvumi kama alivyosema Allah SWT: "*Enyi mlio amini! Akikujieni mpotovu na khabari yoyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kuto jua, na mkawa tena wenye kujuta kwa mliyo yatenda*" (Surat al-Hujurat: 6).
h) Uhuru wa kutoa maoni usiwe ni kisingizio cha kuhujumu dini au ibada zake au sharia zake au matakatifu yake.
i) Uhuru wa kutoa maoni usipelekee uvunjifu wa amani kwenye jamii au kutia mtafaruku miongoni mwa waislamu.

Inausiwa yafuatayo:

a) Kuweka uhakikisho wa kutosha wa kulinda uhuru wa kutoa maoni kwwa mujibu wa vigezo vya kisharia na kuzingatia uwajibikaji kwa kutengeneza kanuni maalum za kulinda uhuru huo na kuweka sheria na huumu adilifu ya kusimamia.
b) Kuchukua njia zote ziwekanazo kuzuia 'uhuru wa maoni' utumike kama kifaa cha ukosefu na uchafuzi wa maadili na matakatifu ya kiislamu au kueneza fitna miongoni mwa waislamu.
c) Kuhakikisha utekelezaji wa yaliyokubaliwa kwenye miafaka ya kimataifa ya pingamizi dhidi ya kuzikosea heshima dini na alama zake, na kujiepusha na 'unafiki (*double standard*) wa jamii ya kimataifa' wa kutizama kadhia za waislamu tofauti na kadhia nyengine.
d) Nchi za kiislamu zinatakiwa kubuni sheria ya kimataifa itakayolinda ibada na matakatifu ya kidini kwa ujumla dhidi ya hujma, kejeli na uchafuzi nyuma ya pazia ya 'sanaa' au 'uhuru wa maoni' na mfano wake.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 177 (3/19)

Yanayohusiana na 'Nafasi ya Usimamizi wa Kisharia Katika Kudhibiti Shughuli za Mabenki ya Kiislamu: Umuhimu wake, Masharti yake na Namna ya Utendakazi wake'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tisa (19) kilichofanyika Sharjah, (UAE) 1 - 5 Jumada al-Uula (Mfungo Nane), 1430, sawa na 26 – 30 Aprili, 2009.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Nafasi ya Usimamizi wa Kisharia Katika Kudhibiti Shughuli za Mabenki ya Kiislamu: Umuhimu wake, Masharti yake na Namna ya Utendakazi wake,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Usimamizi wa Kisharia inakusudiwa: utoaji fatwa na hukmu za kisharia zinazotaalikiana shughuli za taasisi ya kifedha pamoja na kufuatilia utekelezaji wake na kuhakikisha kua utejelezaji wake ni salama.

Mbili: Usimamizi wa kisharia umejengeka kwenye nguzo tatu:

1) **Bodi ya Usimamizi wa Kisharia:** Wajumbe wa bodi hii ni wanazuoni wa tahasusi waliobobea kwenye Fiqh hususan *Fiqhul Muamalaat*. Idadi yao isipungue watatu (3), wanatakiwa pia wawe ni waelewa wa hali halisi wa shughuli za kibenki, kazi yao ya msingi ni kutoa fatwa na kuhakikisha kua miamala yote inayoendelea kwenye benki husika inawafikiana na hukmu na misingi ya sharia ya kiislamu, na hatimae kuandaa ripoti ya maamuzi yao itakayowasilishwa kwa wenyehisa, maamuzi ya ripoti hii ni lazima yatekelezwe.

   1.1 - Bodi ya Usimamizi wa Kisharia inatakiwa iwe huru;

kulifanikisha hili yazingatiwe yafuatayo:

a) Kikao Kikuu cha Taasisi ndio kiwe chombo cha kuajiri, kufuta kazi na kuainisha viwango vya malipo (mishahara) wajumbe wa Bodi za sharia, maamuzi yao yapitishwe na 'Usimamizi Mkuu wa Kisharia' au wafawidhiwa.
b) Mjumbe wa Bodi ya sharia asiwe ni mkurugenzi mtendaji au mfanyakazi wa taasisi husika, au anahusika na kazi fulani tofauti na kazi yake ndani ya Bodi.
c) Asiwe ni 'Mwenyehisa' wa benki au taasisi husika.

1.2 – Vigezo vya ijtihadi na fatwa kwenye bodi za kisharia:

a) Kujilazimisha na maamuzi ya 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' pamoja na kuzingatia maamuzi mengine ya makongamano mengine lakini bila ya kugongana na maamuzi ya 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh'.
b) Kujiepusha na maoni yaliyojitenga, na ufuatiliaji wa rukhsa kiholela kwa mujibu wa 'Maamuzi ya Kongamano' namba 70 (1/8).
c) Kuyazingatia makusudio makuu ya sharia na hatima ya matendo wakati wa kutaka kubainisha hukmu ya sharia.
d) Kuyazingatia maamuzi ya 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' namba 153 (2/17) yanayohusiana na vigezo vya fatwa.

2) Kitengo cha udhibiti wa kisharia wa ndani: Hiki ni kitengo cha utekelezaji wa taratibu zote zifaazo za kuhakikisha kua 'maamuzi ya bodi ya sharia' yanatekelezwa vilivyo na taasisi husika kwenye miamala yote, taratibu hizi ziko kwenye vifungu vitatu vifuatavyo:

a. Kupitia madaftari na taratibu zote kuhakikisha kua shughuli zote zinaendeshwa kwa mujibu wa fatwa za 'Bodi ya Udhibiti wa Kisharia'.
b. Kuwaandaa wafanyakazi wa taasisi kwa namna itakayowawezesha kutekeleza kazi zao kwa njia sahihi kisharia na kiuweledi.
c. Kutengeneza timu ya 'ukaguzi wa kisharia wa ndani' *(internal shari'ah audit*), wajumbe wa timu hii wawe na taaluma na ujuzi na wawe huru, timu hii iwe chini ya 'kamati ya ukaguzi' au 'Bodi ya

Wadhamini', kuandikwa kwao kazi na kufutwa iratibiwe na 'Bodi ya Udhibiti wa Kisharia'.

3) **Udhibiti Mkuu wa Kisharia:** Hii ni bodi ya udhibiti wa kisharia kwa ngazi ya mamlaka za usimamizi za kiserikali, zinasimamia mambo makuu mawili:

   a. Usimamizi juu ya 'bodi za usimamizi' zilizo chini yake.
   b. Kuhakikisha ukakamavu wa udhibiti wa kisharia kwa ngazi za kitaasisi; kupitia ukaguzi wa shughuli za 'bodi za udhibiti wa kisharia' na udhibiti wa ndani wa kisharia, pamoja na kuweka vigezo na taratibu za uendeshaji wa kazi udhibiti wa kisharia zikiwemo utaratibu mzima wa kuajiri wajumbe na kuwafuta, kutambua uwezo wao na idadi yao na pia kazi zao katika taasisi ambazo wao ni wajumbe wa bodi hapo.

Inausiwa yafuatayo:

a) 'Bodi za Usimamizi' za kila nchi ziweke sheria na kanuni za kuratibisha kazi za udhibiti wa kisharia, na kuchukua hatua za lazima za uwepo wa chombo huru cha kudhibibti.
b) Aidha, wakala za kislamu za viwango zinausiwa kutoorodhesha bidhaa ambazo 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' limezikataa kupitia maamuzi yake.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 178 (4/19)

Yanayohusiana na 'Sukook za Kiislamu (Tawarruq): Utekelezaji wake wa Kisasa na Matumizi yake'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tisa (19) kilichofanyika Sharjah, (UAE) 1 - 5 Jumada al-Uula (Mfungo Nane), 1430, sawa na 26 – 30 Aprili, 2009.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Sukook za Kiislamu (Tawarruq): Utekelezaji wake wa Kisasa na Matumizi yake,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Maana ya *Tawreeq* na *Taskeek*:

***Taureeq* ya kawaida:** Ni kulihaulisha deni kwenye hati za kifedha zinazolingana na kima cha deni hilo na zinazowezekana kuamiliana kibiashara, hati hizi zinawakilisha deni na faida kwa mbebaji kwa dhimma ya mtoaji wake; haijuzu kisharia utoaji wa hati kama hizi wala kuamiliana nazo.

***Taskeek* (Taureeq ya Kiislamu):** Ni utoaji wa hati za kifedha zenye kima sawia zinazowakilisha hisa za pamoja kwenye umiliki wa mali (Vitu au manufaa au haki au mchanganyiko wa vitu, manufaa, pesa na madeni) yaliyopo au yatakayoasisiwa kwa kwa kila mmoja kuchangia hisa yake, hati hizi zinatolewa kwa mujibu wa mkataba wa kisharia chini ya hukmu zake.

Mbili: Sifa za Sukook:

1) Sukook inawakilisha hisa ya pamoja kwenye umiliki halisi.
2) Sukook inatolewa kwa msingi wa mkataba wa kisharia chini ya hukmu

zake.

3) Kutokuwepo kwa dhamana ya msimamizi (mudharib au wakala au mshirika msimamizi).
4) Sukook zinashirikiana kwenye faida kwa kiwango kilichoainishwa, aidha zinashirikiana kwenye hasara kwa kiwango cha kila hisa inayowakilishwa na sukook, wamiliki wa sukook hawaruhusiwi kupewa mgao wao wa faida ulioainishwa awali au kiwango fulani cha pesa.
5) Mbebaji wa sukook kutahamali hatari zote za uwekezaji.
6) Kutahamali gharama na malipo yanayoambatana na umiliki wa mali yanayowakilishwa kwenye sukook, nisawa gharama hizo ziwe ni matumizi ya kiuwekezaji au kushuka kwa kima cha pesa au matumizi ya matengenezo au malipo ya bima.

Tatu: Hukmu za Sukook:

1) Haijuzu kwa msimamizi wa sukook kuahidi kuwakopesha wabebabji wa sukook au kuchangia endapo faida iliyopatikana ni chini ya ile iliyotarajiwa, lakini ataruhusiwa kufanya hivyo, baada ya kujulikana matokeo ya uwekezaji, kuchangia tofauti iliyopo au kukopesha, ikiendelea kua ada yake kufanya hivyo basi inakua ni ahadi.
2) Msimamizi wa sukook ni muaminifu; hivyo habebi dhamana ya sukook ila iwapo kazembea au kachupa mipaka au kakhalifu masharti ya mudharaba au musharaka au uwakala kwenye uwekezaji.
3) Haijuzu kulipia sukook kwa thamani yake mwanzo, bali zinalipiwa kwa thamani ya bei yake sokoni au kwa thamani watakayokubaliana wakati wa malipo.
4) Kuhusiana na miamala ya sukook; izingatiwe vigezo vilivyotajwa kwenye ‘Maamuzi ya Kongamano’ namba 30 (5/4) ikiwemo yafuatayo:

    a) *Iwapo mali zilizokusanywa kwa minajili ya Mudaraba baada ya kusainiwa mikataba lakini kabla ya kuanza mradi husika kwa kutumia pesa hizo basi ijulikane kua mzumguko wowote katika kipindi hiki wa ‘Hati-fungani ni sawa na kubadilishana pesa kwa pesa, kwa maana hio: ‘hukmu zote za ubadilishanaji wa pesa’ zitatumika.*
    b) *Iwapo pesa hizi za Mudaraba ni deni, basi hukumu zote zinazohusiana na madeni zitatumika.*

c) *Iwapo ‘Pesa za Mudaraba’ ni mkusanyiko wa pesa taslimu na madeni na ankari na huduma basi inafaa kuuziana ‘Hati-fungani za Mudaraba’ kulingana na bei watakayoridhiana ikiwa ankari na huduma ndio kiwango kikubwa, ama ikiwa pesa taslimu au madeni ndio kiwango kikubwa basi hukumu za Sharia zitakazozingatiwa ni zile zitakazobainishwa na kupitishwa kwenye kikao kijacho. Katika hali zote miamala hii ya kuuziana Hati-fungani ni lazima isajiliwe na sehemu husika.*

Nne: Rukhsa ya kuamiliana kwenye sukook isifanywe ni kisingizio cha dhamana ya deni kama vile kulifanya sanduku la sukook linaamiliana kwenye madeni yaliyotokana na bidhaa, na kujaalia sehemu ya bidhaa hiyo kwenye sanduku kama ujanja fulani wa kuendelea na muamala.

Tano: Utekelezaji wa kisasa wa sukook:

Kutokana na ukweli kua sharia ya kiislamu ina uwezo wa kuendana na mapya yanayoibuka, ikiwemo kutoa suluhisho la kila jambo jipya na kulipatia hukmu ya kisharia, na kutokana na ukweli kua sukook za kiislamu ni ubunifu wa kisharia wa kua na kifaa halali cha ugharamiaji chenye uwezo mkubwa wa kiuchumi; hivyo basi pamekua na nyanja nyingi za utekelezaji wa sukook ikiwemo utumiaji wake kama kifaa-tekelezi katika vifaa vya sera ya kifedha, au kugharamia rasilimali za benki za kiislamu au uwekezaji wa pesa za ziada (*Investing its surplus liquidity*). Aidha, Kuyazalisha mali ya waqfu, kugharamia miradi ya kiserikali na uwezekano wa kuzitumia sukook hizi kwenye ubinafsishaji wa mpito ni miongoni mwa matumizi ya sukook; lakini kwa sharti faida zote zipatikanazo za sukook ziwe zimetokana na miradi inayozalisha na kutia faida.

‘Kongamano’ linausia yafuatayo:

1) Ulazima wa benki za kiislamu kuendelea kutafuta suluhisho zinazokidhi mahitajio ya kiuchumi pamoja na kushikamana na hukmu za kisharia.
2) Kwa kua matakwa (mipaka) ya kisheria (kanuni) ya udhamini wa sukook ni mojawapo wa hatua-msingi zinazochangia katika ufanikishaji wa mchakato mzima wa sukook; ili kulifanikisha hili taasisi za utungaji sheria (bunge) za nchi wanachama wa OIC zinatakiwa kuandaa mipaka na mazingira ya kikanuni munasaba itakayodhibiti mchakato wa utoaji

wa sukook kwa kutunga sheria muawafaka zitakazosimamia mchakato mzima wa utoaji sukook katika nyanja zake mbalimbali kwa lengo la kujenga uwezo wa kiuchumi na uhalali wa kisharia kivitendo.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 179 (5/19)

Yanayohusiana na 'Tawarruq: Uhalisia wake na Aina zake (Inavyojulikana kifiqhi na inavyotumika kibenki)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tisa (19) kilichofanyika Sharjah, (UAE) 1 - 5 Jumada al-Uula (Mfungo Nane), 1430, sawa na 26 – 30 Aprili, 2009.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Tawarruq: Uhalisia wake na Aina zake (Inavyojulikana kifiqhi na inavyotumika kibenki),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na baada ya kupitia 'Maamuzi ya Kongamano la Fiqh ya Kiislamu' liliopo chini ya *Rabitat al-Aalam al-Islami* (Muslim World League) Makkah kuhusiana na kadhia hii;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Aina za Tawarruq na hukmu zake:

1) Tawarruq kwa istilahi ya wanafiqihi: ni kitendo cha mtu (*Mustauriq*) kununua bidhaa kwa malipo ya baadae ili aende akauze bidhaa hio kwa mtu mwengine kwa malipo ya papohapo lakini kwa thamani chini (duni) ya ile alionunulia kwa lengo la kupata pesa taslimu. Twarruq aina hii inajuzu kisharia iwapo masharti ya kuuziana yamekamilika.
2) Tawarruq-mpangilio kwenye istilahi ya kisasa: ni pale *mustauriq* anaponunua bidhaa kwenye soko la ndani au la kimataifa au mfano wake kwa malipo ya baadae ambapo muuzaji (mgharamiaji) anasimamia utaratibu wa kuuza bidhaa hio ima yeye mwenyewe au kupitia wakala wake au kwa makubaliano baina ya *mustauriq* na muuzaji kwa malipo ya papohapo; lakini aghlabu hua ni duni.
3) Tawarruq-kinyumenyume: hii ni sawa na Tawarruq-mpangilio isipokua tu hapa *mustauriq* ni taasisi na mgharamiaji ni mteja.

Mbili: Tawarruq aina hizi mbili; (mpangilio na kinyumenyume) haijuzu, kwa kua hapa kuna aina fulani ya ujanja baina ya mgharamiaji na mustauriq ima wa wazi au fiche au desturi kwa lengo la kupata faida juu ya pesa zinazolipwa sasa kwa malipo ya baadae; hii ni riba.

Inausiwa yafuatayo:

a) Kuweka msisitizo juu ya benki na taasisi za fedha za kiislamu kutumia mifumo ya uwekezaji (investment modes) na ugharamiaji inayokubalika kisharia katika shughuli zao zote, na kujiepusha mifumo ilioharamishwa au yenye tashwishi fulani; hivi ni kutimiza vigezo vya kisharia kwa lengo la kuyafikia makusudio makuu ya sharia, na kudhihirisha ubora wa mfumo wa uchumi wa kiislamu kwa dunia nzima ambayo inapitia mikasa na mitikiso ya kiuchumi wakati baada ya mwengine.
b) Kushajiisha utoaji wa '*Qard hasan*' ili kuwakinga wenye shida wasiingie kwenye tawarruq, aidha, taasisi za fedha za kiislamu zinatakiwa ziwe na mifuko maalum ya '*Qard hasan*'.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 180 (6/19)

Yanayohusiana na 'Unyanyasaji wa Kifamilia'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tisa (19) kilichofanyika Sharjah, (UAE) 1 - 5 Jumada al-Uula (Mfungo Nane), 1430, sawa na 26 – 30 Aprili, 2009.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Unyanyasaji wa Kifamilia,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na baada ya kujikumbusha kua uislamu umetilia maanani sana suala la familia na kuliekea misingi madhubuti iliyojikita kwenye: mapenzi na huruma, mbali na kuweka hukmu za kuleta utulivu na uwiano wa kifamilia, kukaa mbali na mfumo huu ni kufungua milango ya unyanyasaji ndani ya familia;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Maana ya unyanyasaji wa kifamilia:

Unyanyasaji wa kifamilia ni matendo au matamko yatokayo mmoja wa wanafamilia juu ya mwengine yenye sifa ya ukali unaoumiza mwili au hisia ya mwanafamilia au family nzima, ni tabia haramu kwa kua inapingana na makusudio makuu ya sharia katika kuhifadhi nafsi (roho) na akili, aidha, inakinzana na mfumo wa wa Allah SWT unaosisitiza familia kuishi kwa upendo na uwiano.

Mbili: Haya si katika unyanyasaji au ubaguzi kwa mtazamo wa kiislamu:

a) Kulazimiana na hukmu za kisharia zinazoratibu suala la maisha ya ndoa na kukataa aina zote za mume na mke kuishi pamoja kinyume na sharia (bila ya ndoa).
b) Dawa au mbinu za kuziwia mimba zisipeanwe kwa wasiokua wanandoa

halali.

c) Kuzuia utoaji mimba ila kwa ushauri wa daktari bingwa kutokana na mazingira ya kiafya ya mama.
d) Kuharamisha ubaradhuli.
e) Mume kumzuia mke wake asisafiri peke yake ila kwa idhini yake na kwa kufuata matakwa ya kisharia.
f) Haki ya kisharia ya kila mwanandoa kutimiziwa mahitajio yake ya kijinsia hata iwapo mwenzake hana raghba ya tendo hilo.
g) Mwanamke anatakiwa kusimamia majukumu yake ya kimsingi kama mama na mke kwenye nyumba yake, hali kadhalika mume nae anatakiwa asimamie majukumu yake kama '*Qawwam*' msimamizi wa mahitajio ya nyumba yake na familia yake.
h) Walii (msimamizi wa kiume) kumsimamia binti yake mambo yake yote ya ndoa kama vile kutoa idhini.
i) Mafungu ya mirathi yaliopangwa na sharia au kwenye wasia.
j) Talaka; itokeapo, ifanyike ndani ya mipaka na vigezo vya kisharia.
k) Ukewenza ufanyike kwa misingi ya uadilifu.

Tatu: Mfumo wa uislamu katika kutatua migogoro ya kifamilia:

Katika kutatua migogoro ya kifamilia; hususan ile inayotaalikiana na suala la nashiza na mke kutoka nje ya utiifu, vigezo vya kisharia vifuatvyo vizingatiwe:

1. Kujiepusha na matusi, matukano na kejeli.
2. Kulazimiana na mfumo wa kisharia wakatia wa kumrekebisha mke anaetoka nje ya utiifu; kwa kuanzia na kumpa mawaidha kisha kumhama kitandani na mwisho kabisa kipigo kisichoumiza kama ishara ya kutaka kumpiga lakini haifikii kitendo chenyewe cha kupiga, kupiga mwenyewe ni kinyume na pendekezo la Mtume Muhammad SAW aliposema: "ولن يضرب خياركم" "*Waungwana wenu hawapigi*", lakini pia kumuiga Mtume SAW kivitendo kwani yeye katu hakuwahi kumpiga mwanamke.
3. Kutafuta wapatanishaji wawili iwapo mgogoro unazidi kukua.
4. Zikishindikana njnia zote; sasa hapa wataanza mchakato wa '*talaka*' kwa kufuata taratibu zilizowekwa na sharia, yaani talaka-mpangilio

inayoanza na '*talaka raj'ii*' (wanaweza kurejeana), kisha '*talaka bain*' kubwa au ndogo pamoja na kuzingatia nyakati za kuitukisha (kuitoa) talaka, aidha, kutambua kua: '*halali inayochukiza zaidi mbele ya Allah ni talaka*'.

Nne: 'Kongamano' linasisitiza yafuatayo:

1) Kwa ngazi ya kifamilia:

a. Kuweka msisitizo juu ya malezi ya kiimani kama njia ya makuzi ya kijamii.
b. Kuweka msisitizo juu ya misingi ya kisharia inayotaalikiana mjengo wa kifamilia uliojikita kwenye ushirikiano, mapenzi, huruma, utulivu, kufanyiana wema na kuishi kwa upendo baina ya wanandoa.
c. Kutumia njia ya mazungumzo kutatua masuala ya ndani ya familia.

2) Kwa ngazi ya taasisi rasmi:

a. Kuandaa warsha maalum na semina za uhamasishaji juu ya madhara ya unyanyasaji na kushajiisha uwepo wa mazungumzo kwa wanafamilia.
b. Kuzitaka taasisi za kimalezi na kielimu kuingiza somo linaloangazia masuala ya unyanyasaji wa kifamilia wa aina zote.
c. Kuratibu baina ya wizara na idara husika kwa minajili ya kua na sera ya pamoja itakayolinda turathi za umma na kuuwezesha kupambana na wimbi hatarishi la umagharibi dhidi ya familia.
d. Kuvielekeza vyombo vya mawasiliano kubeba majukumu yao katika suala la kukikuza kizazi kipya kinachojielewa.

3) Kwa ngazi ya nchi za kiislamu:

a. Ulazima wa kuchukua ushauri kutoka kwa wanazuoni wa sharia na kanuni juu ya miafaka ya kimataifa inayohusiana na masuala ya mwanamke na mtoto na miswada ya sheria mengine inayohusiana nayo ili ikosolewe na iwekwe sawa kwa mizani ya kisharia kabla haijasainiwa, na kukataa kila kinachopingana na na hukmu za sharia za kiislamu na makusudio yake makuu. Aidha, kuzitaka serikali za

kiislamu zifanye mapitio upya juu ya miafaka iliyokwisha kusainiwa ili kubaini kama kuna vifungu vyovyote vinavyogongana na sharia ya kiislamu na kuvikataa vifungu hivyo, bila ya kuvuruga mambo mengine yaliyopo humo ambayo ni mazuri na yanayowiana na sharia ya kiislamu.

b. Kukataa vifungu vinavyokhalifu *nususi* (maandiko) za sharia ya kiislamu kwenye miafaka ya kimataifa ambayo inanadi kutupilia mbali mbali tofauti za kimaumbile baina ya mwanamume na mwanamke katika jamii, na kudai usawa kamili baina ya mume na mke katika mafungu ya mirathi, kuichafua nidhamu ya talaka ya kiislamu, na kutaka kuondoa nafasi ya mume kama '*Qawwam*' (msimamizi) juu ya familia, na mengineo katika mambo yaliyothubutu kwenye sharia ya kiislamu.
c. Kukataa vifungu vyote kwenye miafaka vinavyohalalisha mambo kinyume na sharia na maumbile kama vile kuhalalisha ndoa za jinsia moja, mahusiano ya kijinsia nje ya ndoa halali, mchanganyiko wa jinsi za kiume na za kike kwa namna iliyokatazwa na vifungu venginevyo vinavyogongana na hukmu za sharia za kiislamu.
d. Kuzitaka taasisi za utungaji sheria (bunge) watunge sheria zinazoharamisha aina zote za unyanyasaji miongoni mwa wanafamilia kwa kua sharia ya kiislamu imeharamisha jambo hilo.
e. Kuuwezesha muhimili husika wa utoaji hukmu kusimamia utekelezaji wa sheria.
f. Kuweka msisitizo juu ya kulazimiana na utamaduni wa kiislamu, hukmu za sharia na kuheshimu mawazo ya nchi za kiislamu yanayotolewa kukataa baadhi ya vifungu kwenye miafak ya kimataifa vinavyogongana na sharia ya kiislamu katika masuala ya kifamilia.
g. Kuunda kamati maalum ya kuandaa muongozo wa haki na nyajibu za wanafamilia, kupitia muongozo huu utaibuka mswada wa sheria (kanuni) itakayowafikiana na sharia ya kiislamu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 181 (7/19)

Yanayohusiana na 'Waqfu ya Hisa, Sukook, Haki za *Kimaanawi* (Moral Rights) na Manufaa'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tisa (19) kilichofanyika Sharjah, (UAE) 1 - 5 Jumada al-Uula (Mfungo Nane), 1430, sawa na 26 – 30 Aprili, 2009.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Waqfu ya Hisa, Sukook, Haki za *Kimaanawi* (Moral Rights) na Manufaa,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Waqfu ni miongoni mwa milango mipana ya Fiqh iliyojikita kwenye '*ijtihad*', ambayo ni mchakato wa kiakili uliofungamana na makusudio ya sharia, lengo likiwa ni kulinda maslahi ya waqfu kwa muwekaji na wakusudiwa wa waqfu hio.

Mbili: Waqfu ya hisa, sukook, haki za *kimaanawi* (moral rights), manufaa na sanduku za uwekezaji:

1) *Nususi* (maandiko) za kisharia zilizokuja kwenye mas'ala ya waqfu; zimekuja kiujumla lakini zinaelezea aina nyingi za nyakfu: ya milele, ikikabiliana na ya mda, ya mahsusi ikikabiliana na ya pamoja, ya mali na manufaa ikikabiliana na pesa, ya isiohamishika ikikabiliana na inayohamishika, kwa kua waqf ni miongoni mwa michango; ni mlango mpana na kila mmoja anashajiishwa kuweka waqf.
2) Inajuzu kuweka waqfu ya hisa za kampuni inayoruhusiwa kumilikiwa kisharia, aidha inajuzu waqfu za sukook, haki za *kimaanawi* (moral rights), manufaa na sanduku za uwekezaji kwa hayo ni mali yanayokubalika kisharia.

3) Waqf za sukook, haki za *kimaanawi* (moral rights) na manufaa na nyenginezo zinadhibitiwa na hukmu mbalimbali zikiwemo:

a. Kimsingi, hisa za waqf zinatakiwa zibaki rasilimali zake, lakini zitumike faida zake kwenye malengo ya waqf yaliyokusudiwa na sio kuzifanyia biashara kwenye masoko ya fedha, msimamizi wa waqf hatakiwi kutumia mali ya waqf ila penye maslahi ya uhakika au kwa kutekeleza masharti ya muekaji waqf, nyakfu zinasimamiwa na hukmu za sharia zijulikanazo za '*istibdal*' (kubadili kiti kwa kitu).
b. Iwapo kampuni imeuzwa au thamani ya sukook zimelipwa basi inajuzu kubadilisha mali mengine kama kununua majumba, au hisa au sukook nyengine lakini kwa masharti ya muweka waqf au kwa kuthubutu maslahi ya uhakika ya waqf.
c. Iwapo muweka waqf ameweka waqf kwa mda basi mda uliowekwa ukiisha hesabu ya waqf hio ifungwe kama alivyoshurutisha.
d. Iwapo pesa za 'waqf ya sarafu' zimetumika kuwekeza kwenye ununuzi wa hisa au sukook, basi hisa hizo au sukook hizo hazitohesabiwa zenyewe kua ni waqf kama pesa taslimu, ila ikiwa muweka waqf ameainisha hivyo, aidha, inajuzu kuziuza ili kuwekeza kunako faida Zaidi kwa maslahi ya waqfu, na pesa taslimu za asili ndizo zitakua waqfu iliyofungiwa.
e. Inajuzu kuweka waqfu ya manufaa, huduma na sarafu kwenye huduma za mahospitali, vyuo vikuu, taasisi za kielimu, huduma za simu, umeme, manufaa ya nyumba, madaraja na njia.
f. Waqf ya manufaa ya mda fulani haimzuii mmiliki wa mali yenyewe kufaidika na mali yake kwani kisharia anaruhusiwa kufanya atakalo kwa mali yake kwa sharti tu alinde haki ya waqf ya manufaa hapo.
g. Haki za *kimaanawi* zinafika ukomo pale mda wa kikanuni uliopangwa ukiisha.
h. Uwekaji mda wa waqfu maana yake ni kua waqgfu una mda fulani ukipitamda huo nayo wafu inaisha, inajuzu kuwekea mda aina zote za waqfu.
i. Inajuzu kwa aliepata mali yenye wasiwasi au mali ya haramu na wenye mali hayo hawajulikani na akawa anataka kujiepusha na uharamu huo basi inajuzu kwake yeye kuyaweka mali hayo kwenye

waqfu ya matumizi ya umma ya kawaida lakini sio kukusudia matendo ya ibada kama vile kujenga misikiti au kuchapisha misahafu, na ijulikane wakati wote uharamu wa kumiliki hisa kwenye benki za riba na kwenye kampuni za bima za kawaida.

j. Inajuzu kwa aliepata mali yenye kuingiza faida ya haramu kuweka waqfu rasilimali yake kwenye mali hayo, na faida itakayopatikana ielekezwe kwenye mambo ya kheri, wastahiki wa faida hizi na mali haya ni mafukara, maskini na njia za manufaa kwa umma iwapo imeshindikana kurudishiwa pesa hizi wenyewe, na ni juu ya msimamizi wa waqfu kuhaarakisha kuyabadilisha mali haya kwa mali yaliyokua halali kisharia hata kama inakwenda kinyume na matakwa ya muweka waqfu, masharti ya muweka waqfu hayazingatiwi iwapo yanagongana na msingi wa sharia.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kuzitaka serikali na mabunge katika nchi za kiislamu zifanyie marekebisho ya sharia na kanuni za waqfu kwenye nchi zao kwa namna itakavyowafikiana na ‘Maamuzi ya ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’.
2) Kuzitaka wizara za elimu katika nchi za kiislamu kuweka mitaala ya masomo inayodurusu elimu ya waqfu kwa kina na ustadi.
3) ‘Kongamano’ linaitisha tafiti zaidi juu ya: Usimamizi (utawala) wa waqfu, misingi yake, mipangilio yake, vigezo vyake na vipimo vya kuchagua na kuendeleza usimamizi wa waqfu, tafiti hizi ziwasilishwe kwenye vikao vinavyokuja inshaallah, ni matarajio yetu kua maudhua haya yatapewa nafasi stahiki ya kipaombele kwa kua ni chachu ya mafanikio nyakfu na fursa za uwekezaji.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 182 (8/19)

Yanayohusiana na 'Utekelezaji wa Mfumo wa Jenga, Endesha na Hamisha Umiliki kwenye Uwekezaji wa Waqfu na Makazi ya Umma'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tisa (19) kilichofanyika Sharjah, (UAE) 1 - 5 Jumada al-Uula (Mfungo Nane), 1430, sawa na 26 – 30 Aprili, 2009.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Utekelezaji wa Mfumo wa Jenga, Endesha na Hamisha Umiliki kwenye Uwekezaji wa Waqfu na Makazi ya Umma,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Maana ya '*Jenga, Endesha na Hamisha Umiliki*' ni makubaliano baina ya mmiliki (wa ardhi) au muwakilishi wake na mgharamiaji (kampuni ya mradi) juu ya kuwezeka mradi fulani, kuusimamia na kupokea malipo (ya kodi) ima kamili au kama walivyokubaliana, ndani ya mda waliokubaliana kiasi ya kurejesha rasilimali iliyowekezwa pamoja na faida inayokubalika, kisha baada ya hapo mradi huu anakabidhiwa mmiliki (wa ardhi).
2) Mkataba wa '*Jenga, Endesha na Hamisha Umiliki*' ni aina ya mikataba mipya iliyoibuka siku hizi, nayo licha ya kufanana baadhi ya aina zake na mikataba ya kawaida na zana za uwekezaji zinazojulikana lakini huenda ikawa haiwafikiani na mikataba inayojulikana.
3) Inajuzu kuingia mkataba wa '*Jenga, Endesha na Hamisha Umiliki*' kwenye Uwekezaji wa Waqfu na Makazi ya Umma.

Inausiwa yafuatayo:

Kuongeza tafiti za kifiqhi juu aina zote za mikataba ya '*Jenga, Endesha na Hamisha Umiliki*' kwa lengo la kudhibiti hukmu zake mbalimbali na

kuzitunga kwenye vifungu vya wazi na vyepesi ili iwe rahisi wakati wa kuamiliana miamala kama hii.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 183 (9/19)

Yanayohusiana na 'Ugonjwa wa Kisukari na Swaum (*Funga*)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tisa (19) kilichofanyika Sharjah, (UAE) 1 - 5 Jumada al-Uula (Mfungo Nane), 1430, sawa na 26 – 30 Aprili, 2009.

Kwa mujibu wa 'Waraka wa Ushirikiano' uliopo baina ya 'Jumuiya ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' na 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu', uliotokana na makubaliano yaliyosainiwa na pande zote mbili, na baada ya 'Kongamano' kuitaka rasmi 'Jumuiya ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' waandae tafiti zihusuzo: **'Ugonjwa wa Kisukari na Swaum (*Funga*)'**, na baada ya kupata matokeo ya warsha mbili zilizoandaliwa na 'Jumuiya' tarehe 2 Rabiu al-Thani (Mfungo saba), 1429 Hijriya (3 Novemba, 2007) na tarehe 8 Aprili, 2008.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na ukamilishaji wa tafiti juu ya maudhui ya **Ugonjwa wa Kisukari na Swaum (*Funga*),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na baada ya kuzipitia nyanja za kitiba na kifiqhi juu ya athari ya Swaum (funga) kwa wagonjwa wa kisukari;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Fasili fupi ya ugonjwa wa kisukari: Ni mlegolego na upangukaji wa kiwango cha sukari kwenye damu, hususan pale kiwango cha sukari kinapopanda juu ya kiwango cha kawaida, ugonjwa wa kisukari hutokana na ukosekanaji wa hormoni za insulini (*insulin hormone*) zinazozalishwa na seli hasa seli (b) kwenye kongosho (*pancreas*) ima kwa uhaba (uchache) wa insulini au seli za mwili zinashindwa kuwiana nazo (insulini) baadhi ya nyakati.

Mbili: Aina ya maradhi ya kisukari: Zipo aina nyingi za maradhi ya

kisukari na zinatafautiana kwa kiasi kikubwa baina yao kwenye sababu na njia za kutibu; wanataaluma na Taasisi ya Tiba ya Kimataifa (*International Medical Organization*) inayojihusisha na maradhi ya kisukari wanakubaliana juu ya aina zifuatazo:

1) Kisukari aina ya kwanza (*Diabetes Mellitus Type I*), inayotegemea dozi kadha za insulini kwa siku.
2) Kisukari aina ya pili (*Diabetes Type II*), Haitegemei insulini.
3) Kisukari kipindi cha mimba (*Gestational Diabetes*).
4) Aina nyingine, nazo:
   a. Kisukari utokanao na a baadhi ya magonjwa ya kongosho (*pancreas*).
   b. Kisukari utokanao na upangukaji wa hormoni hususan katika tezi za pituitary na adrenal na seli katika kongosho.
   c. Kisukari utokanao na utumiaji wa baadhi ya madawa.

Tatu: Upangaji (tasnifu) wa wagonjwa wa kisukari kitiba: Wagonjwa wa kisukari wanapangwa kwenye makundi manne kwa namna ifuatayo:

Kundi la kwanza:

Wagonjwa wenye uwezekano mkubwa wa hali yao kuzorota zaidi, wagonjwa kwenye kundi hili wanafikiwa na hali moja au zaidi kama ifuatavyo:

- Kushuka kwa sukari kwa kiwango kikubwa miezi mitatu kabla ya Ramadhani.
- Wagonjwa ambao viwango vyao vya sukari kwenye damu hupanda na kushuka mara kwa mara.
- Wagonjwa wenye waliokosa hisia juu ya ushukaji wa kiwango cha sukari, hali hii inawafika baadhi ya wagonjwa wa kisukari; hususan wale *aina ya kwanza* ambao wanakua na tatizo la kushuka kwa kiwango cha sukari yao sana na kwa mda mrefu.
- Wagonjwa wanaojulikana kua na shida ya kudhibiti kisukari kwa mda mrefu.
- Uibukaji wa matatizo ya hamidhi ya kisukari (*Acidosis Diabetic Ketoacidosis*) au matatizo ya upoteaji fahamu wa kisukari ndani ya

miezi mitatu kabla ya mwezi wa Ramadhani.

- Kisukari ya aina ya kwanza.
- Magonjwa mengine makali yanayofuatana na kisukari.
- Wagonjwa wa kisukari ambao hawana budi na kufanya kazi ngumu.
- Wagonjwa wa kisukari ambao wanaofanyiwa usafishaji wa figo.
- Mwanamke aliepata kisukari kipindi cha mimba.

Kundi la pili:

Hili ni kundi la wagonjwa wenye uwezekano mkubwa wa kuzidi ugonjwa wao kutokana na saumu (funga) kwa mujibu wa ushauri wa madaktari, ugonjwa huu unaingia kwenye hali moja au zaidi kama zifuatavyo:

- Wagonjwa ambao kiwango cha sukari yao kinapanda kwenye 180 – 300 mg/dcl (milimita 10 – 16.5) na kiwango cha hemoglobin iliopandiana (yenye kisukari) kinapita asilimia 10 %.
- Wagonjwa wenye upungufu wa nguvu za figo na kibofu cha mkojo.
- Wagonjwa wenye udhaifu wa mishipa mikuu (kama magonjwa ya moyo na mishipa).
- Wagonjwa wanaokaa peke yao na wanaotibiwa kupitia sindano za insulini au tembe za kuteremsha viwango vya sukari kupitia kuzihamasisha seli zinazozalisha insulini kwenye Kongosho (pancreas).
- Wagonjwa wenye maradhi mengine yanayowaongezea hatari ya ziada.
- Watu wazima wenye maradhi mengine.
- Wagonjwa wanaopokea matibabu lakini yanawaathiri kwenye akili zao.

Hukmu ya makundi mawili; la kwanza na la pili:

Ni wazi kua hali ya makundi mawili haya ni yenye kupata madhara makubwa au uwezekano wa kupata madhara makubwa kwa mujibu wa ushauri wa madaktari bingwa waaminifu, hivyo basi inatakiwa kisharia kwa mgonjwa yeyote mwenye kupitia hali hizi zilizotajwa asifunge saumu ya Ramadhani ili kuepusha madhara juu ya nafsi yake, kama alivyosema Allah

SWT:

"*Wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo*".[1]

Akasema tena:

"*Wala msijiuwe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwarehemuni*".[2]

Kwa hio daktari anaetibu anatakiwa kuwabainishia wagonjwa wake hawa uhatari wa kufunga juu ya afya zao na uwezekano wa wao kuzidiwa na hivyo kuhatarisha afya zao au maisha yao. Aidha, Daktari anatakiwa atumie taratibu zote muwafaka zitakazomuwezesha mgonjwa wake kufunga bila ya kujiingiza kwenye madhara.

Hukmu za kutofunga ndani ya mwezi wa ramadhani kwa udhuru wa ugonjwa zitatumika kwa makundi haya mawili la kwanza na la pili kwa kigezo cha neon lake Allah pale aliposema: "*Na atakaye kuwa miongoni mwenu mgonjwa au yumo safarini basi atimize hisabu katika siku nyengine.*" (Surat al-Baqarah: 184). Ama yule mgonjwa atakaefunga na akadhurika kwa sababu ya swaumu hio basi atapata madhambi, lakini swaumu yake ni sahihi.

Kundi la tatu:

Wagonjwa wenye uwezekano wastani wa kuzidiwa na ugonjwa wao kwa sababu ya swaumu wakiwemo pia wagonjwa wa kisukari wenye hali zilizotulia na zinazodhibitika kwa kutumia dawa mnasibu za kushusha sukari ambazo zinahamasisha seli za Kongosho (pancreas) zinazozalisha insulini.

Kundi la nne:

Wagonjwa wenye uwezekano wa chini wa kuzidiwa na ugonjwa wao kwa sababu ya swaumu wakiwemo pia wagonjwa wa kisukari wenye hali zilizotulia na zinazodhibitika kwa kutumia chakula muwafaka (*diet*) au kutumia dawa za kushusha sukari ambazo hazihamasishi seli za Kongosho lakini zinazidisha uwezo wa insulini iliopo kwao.

---

[1] Surat al-Baqarah: 195.

[2] Surat al-Nisaa: 29.

Hukmu ya makundi mawili; la tatu na la nne:

Haijuzu kwa makundi mawili haya kutofunga ramadhani, kwa sababu hali zao za kitiba haziashirii uwezekano wa kuzidiwa na kudhuru afya zao na maisha yao, bali inawezekana swaumu ikawa ni dawa kwao. Daktari anaetibu anatakiwa kujilazimisha na hukmu hii na akadirie dawa muwafaka kwa kila hali ya mgonjwa.

Inausiwa yafuatayo:

1) Madaktari wanatakiwa wawe na uwelewa wa hukmu za kisharia zinazohusiana na maudhui haya kwa kiwango kinachokubalika, kulifanikisha hili taasisi husika zinatakiwa kuandaa dondoo mahsusi na kuzifikisha kwa wahusika.
2) Wanafiqihi na walinganizi (wana-da'wa) wanatakiwa kuwaelimisha wagonjwa wanaowafika kwao na wanaotaka kujua hukmu za sharia na kuwaelekeza waende kwa madaktari wao wanaofahamu mambo ya swaumu kitiba na kidini na ambao wanamuogopa Allah wakati wa kutoa ushauri kwa kila hali ya mgonjwa.
3) Kutokana na hali hatarishi za uhakika zitokanazo na ugonjwa wa kisukari juu ya afya na maisha ya wagonjwa hawa; ni wajibu kuchukua tahadhari zote zinazowezekana za kufahamisha na kuelimisha zikiwemo kupitia khutba za misikitini na vyombo vya habari mbalimbali ili kuufahamisha umma na wagonjwa wa kisukari juu ya hukmu zilizotangulia, hii ni kwa sababu ongezeko la kiwango cha ufahamu wa ugonjwa huu na namna ya kuamiliana nao utapunguza sana athari zake na kurahisisha upokeaji wa hukmu za kishaaria na nasaha za matabibu kwa minajili ya kutibu gonjwa hili.
4) 'Jumuiya ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' kwa kushirikiana na 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu' wanatakiwa waandae kitabu-muongozo juu ya maudhui haya kwa lugha za kiarabu na nyenginezo na wakisambaze miongoni mwa madaktari na wanafiqihi na pia kukisambaza kwenye mitandao ya intaneti ili na wagonjwa nao wapate kufaidika na miongozo hio.
5) Kuzitaka wizara za afya katika nchi za kiislamu kuandaa programu za kitaifa katika Nyanja za kinga, tiba na kuelimisha juu ya ugonjwa wa

kisukari na hukmu zake za kisharia.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 184 (10/19)

Yanayohusiana na 'Idhini juu ya Operesheni za Kitiba za Dharura'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tisa (19) kilichofanyika Sharjah, (UAE) 1 - 5 Jumada al-Uula (Mfungo Nane), 1430, sawa na 26 – 30 Aprili, 2009.

'Kongamano' liliwahi kuchukua maamuzi namba 67 (5/7) kwenye kikao chake cha saba (7) kilichofanyika Jeddah, Saudi Arabia kuanzia tarehe 7 – 12 Dhul-Qa'adah (Mfungo pili), 1412 Hijriya (9 – 14 Mei, 1992) yaliyohusiana na 'Hukmu za Matibabu', aidha likachukua maamuzi namba 172 (10/18) kwenye kikao chake cha kumi na nane (18) kilichofanyika Putrajaya, Malaysia, yaliyohusiana na 'Kujuzu kuchukua tahadhari na taratibu za kitiba za lazima katika hali za dharura (*Emergency*)', sasa; kukamilisha kile kilichoonekana wakati huo kizungumziwe baadae katika hali za ugonjwa za haraka (dharura);

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na ukamilishaji wa tafiti juu ya maudhui ya **Idhini juu ya Operesheni za Kitiba za Dharura,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Hali za dharura: Ni zile hali za ugonjwa zinazohitaji kufanyiwa upasuaji (operesheni) kwa haraka bila kucheleshwa, kutokana na hali hatarishi anayopitia mgonjwa ili kuokoa maisha yake au kuzuia maharibiko ya mojawapo ya viungo vyake kama vile:

    a) Mazingira yanayohitaji uzalishaji wa kisizeria ili kuokoa maisha ya mama au maisha ya mtoto au wote wawili, kama mwenye mazingira ya mzunguko wa kamba ya kitovu, au kuchanika kwa uzao wakati wa mazazi.

b) Mazingira yanayohitaji upasuaji wa dharura kama vile upatikanaji wa uvimbe wa kidole-tumbo.
c) Mazingira yanayohitaji tiba maalum kama vile usafishaji wa figo au kuhamisha damu.

2) Iwapo mgonjwa yuko kwenye uwezo wake wa kiakili na fahamu zake kamili na anaelewa maamuzi anayoyachukua kwa hiari yake bila ya kutenzwa nguvu, na iwapo madaktari wameamua kua hali ya ugonjwa wake ni ya dharura na anahitaji tiba ya upasuaji kwa haraka; basi ni wajibu kisharia kwa mgonjwa huyu kutoa idhini ya kutibiwa na akikataa atapata madhambi. Inajuzu kwa daktari anaemtibu kutumia njia za lazima za tiba ili kuokoa maisha ya mgonjwa kwa mujibu wa hukmu za dharura zijulikanazo kwenye sharia.
3) Iwapo mgonjwa ana punguani ya akili na msimamizi wake akakataa kutoa idhini ya kutibiwa kwenye hali za dharura basi kata yake haizingatiwi na haki ya kumsimamia mgonjwa huyu itahamia kwa mtawala (serikali) au taasisi husika ya kiserikali.
4) Iwapo inalazimu upasuaji wa kisizeria kwa ajili ya kuokoa maisha ya mtoto au ya mama au wote wawili na wakakataa mume na mke au mmoja wao kufanya hivyo, basi kata hio haitozingatiwa na haki ya kutoa idhini itahamia kwa mtawala (serikali) au atakaewakilishwa kusimamia upasuaji.
5) Kuingilia kimatibabu kwenye hali za dharura kunashurutishwa yafuatayo:

a) Daktari anatakiwa amfafanulie mgonjwa au msimamizi wake umuhimu wa matibabu na uhatari wa hali ya mgonjwa na athari zinazoweza kujitokeza iwapo atakataa, endapo ameshikilia kukataa basi daktari anatakiwa kurikodi mazungumzo yanayojiri baina yao.
b) Aidha, daktari anatakiwa kutumia juhudi kubwa za kumkinaisha mgonjwa na msimamizi wake kuacha kata hio na badala yake atoe idhini ili kuepusha kuzorota kwa hali yake.
c) Kundi la madaktari washauri wasiopungua watatu, anaemtibu akiwa miongoni mwao, kundi hili lihakikishe kua mgonjwa amefanyiwa ukaguzi barabara na kuandikiwa dawa muwafaka

yote hayo yakiwa yamerikodiwa na kusainiwa na timu hii ya madaktari na uongozi wa hospitali ujulishwe juu ya hayo.

d) Matibabu yawe ni bila ya malipo (bure), au ziwepo taasisi huru za kukadiria gharama.

Inausiwa yafuatayo:

- Serikali za nchi za kiislamu zinatakiwa zitunge sheria maalum zinazoratibu utekelezaji wa kazi za tiba katika hali zote za kiugonjwa wa dharura na haraka kwa namna ambayo 'Maamuzi ya Kongamano' yataweza kutekelezwa kwenye mambo ya kitiba.
- Kuendelea kuwaelimisha wagonjwa elimu za afya ili kuwaepushia hali tatanishi kama hizi na kulinda maisha yao.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≋≋≋

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 185 (11/19)

Yanayohusiana na 'Kulinda Mazingira kwa Mtazamo wa Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha kumi na tisa (19) kilichofanyika Sharjah, (UAE) 1 - 5 Jumada al-Uula (Mfungo Nane), 1430, sawa na 26 – 30 Aprili, 2009.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na ukamilishaji wa tafiti juu ya maudhui ya **Kulinda Mazingira kwa Mtazamo wa Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Kuharamisha utupaji wa taka (za sumu) zinazodhuru sehemu yoyote duniani, nchi zinazozalisha taka hizo (za sumu) zinatakiwa kwa lazima wazitokomeze taka hizo kwenye nchi zao na kwa namna ambayo haitadhuru mazingira, aidha kuzitaka nchi za kiislamu kutoruhusu kutumika kwa nchi zao kama jaa la kumwaga taka hizo (za sumu) au kuzizika kwenye nchi zao.
2) Kuharamisha matendo yote ambayo yatapelekea kudhurika au uchafuzi kwa mazingira kama vile matendo yatakayosababisha mpanguko wa uwiano wa kimazingira au utumizi mbaya wa mali ghafi usiozingatia maslahi ya vizazi vijazo; kwa mujibu wa maelekezo ya sharia ya 'kuondosha madhara'.
3) Ulazima wa kuzitokomeza 'silaha za maangamizi makuu' (WMD) katika nchi zote, na kupiga marufuku kila kinachopelekea uvujaji wa gesi unaosababisha utoboaji wa tabaka la ozoni (Ozone layer) na uchafuzi wa mazingira; kwa mujibu wa maelekezo ya sharia ya 'kuondosha madhara'.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kushajiisha uwekaji wa waqfu wa kulinda mazingira ya ardhini, majini na angani.
2) Uanzishwaji wa ‘kamati-tafiti’ chini ya ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqhi ya Kiislamu’ ya kudurusu suala zima la mazingira kwa mtazamo wa kiislamu itakayojihusisha kukusanya tafiti zote na mikataba na matatizo zinazohusiana na mazingira.
3) Kushirikiana na ‘jamii ya kimataifa’ kwenye Nyanja mbalimbali kwa lengo la kulinda mazingira na kuzuia uchafuzi wake, aidha, kujiunga na mikataba na miafaka ya kimataifa inayolenga kuzuia uchafuzi na kudhuhru mazingira kwa sharti mikataba hio iskhalifiane na misingi ya sharia ya kiislamu au kudhuru nchi za kiislamu.
4) Kuzitaka nchi za kiislamu kuzihamasisha taasisi za kimazingira zilizoanzishwa na ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC) au mashirika yake, na kuendeleza ushirikiano wa karibu na ‘Baraza la Ushirikiano la Kiarabu’ linalohusiana na mazingira, halikadhalika na Baraza la Ushirikiano la Nchi za Ghuba’ linalojihusisha nayo.
5) Kukithirisha viwanda (rafiki kwa mazingira) na kuvishajiisha kwa njia zote zinazowezekana.
6) Kuzitaka nchi wanachama wa ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), kuendelea kutunga sheria na kanuni zinazoratibu mazingira na kuzuia uchafuzi wake na kushirikiana na vyombo vingine vya dola vinavyosimamia makossa ya jinai na kuweka adhabu maalum kwa anaedhuru mazingira, aidha vyombo hivyo vinatakiwa kua makini na waangalifu dhidi ya matendo yoyote ambayo yanaweza yakadhuru mazingira sehemu zote zile: majini au angani au ardhini.
7) Kuzitaka taasisi husika kwenye mambo ya kidini katika nchi za kiislamu kuwawezesha maimamu na madu’ati (walinganizi) kwa taarifa sahihi za mazingira na kusambaza tafiti zinazohusiana na mazingira na namna ya kuyalinda.
8) Kueneza elimu ya mazingira kupitia njia mbalimbali ili kupelekea kua na usafi (nadhifu) wa mazingira na kuyalinda dhidi ya mambo hatarishi kupitia:

    a. Matangazo endelevu ya kuelimisha juu ya mambo hatarishi kwa mazingira kupitia vyombo vya habari.

b. Malezi bora na mazuri kupitia majumbani au kwenye mitaala ya elimu awamu mbalimbali.
c. Kuanzisha somo la ‘Fiqh ya Mazingira’ kwenye taasisi za kielimu ya sharia na fiqhi.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Tamko la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’

Kuhusiana na:

Matukio yanayoendelea Palestina hususan uadui dhidi ya Masjid al-Aqsa, na matukio ya Iraq, Somalia na Sudan

Tamko hili limetolewa kwa mnasaba wa kufanyika kwa kikao cha kumi na tisa (19) cha ‘Baraza la Kongamano’ Sharjah 26 – 30 Aprili, 2009.

‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), katika kikao chake cha kumi na tisa (19) kilichofanyika Sharjah, (UAE) 1 - 5 Jumada al-Uula (Mfungo Nane), 1430, sawa na 26 – 30 Aprili, 2009, kwa kuzingatia kua ‘Kongamano’ hili ni rejea muhimu ya kifiqhi kwa umma wa kiislamu, na kwa kutambua majukumu makubwa yaliyopo juu ya ‘Kongamano’ hili, na kwa kutokana na wajibu wake kwa umma juu ya changamoto na mambo hatarishi zinazowakabili waislamu hususan mambo yanayojiri Palestina, Iraq, Somali na Sudan; ‘Kongamano’ linaweka msisitizo juu ya yafuatayo:

Moja: Palestina na Masjid al-Aqsa:

‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ linafuatilia kwa kukemea na kulaani maovu yote wanayoyapitia Wapalestina wakakamavu wakiwa wanapambana na adui wa kizayuni dhalimu na jeuri ambae hajali kamwe uvunjifu wa haki za kibinadamu za msingi hususan kwa yale yanayojiri kwenye uvamizi wao wa hivi karibuni dhidi ya Ghaza, na yanayofanyika huko yakiwemo: mauaji ya kikatili yasiyobagua wazee au watoto au

wanawake au walemavu, kuwafurusha wapalestina na kuzingira miji yao, kuwaweka na njaa na kuwapotezea Amani, na kukatisha njia zote za kuwafikishia mahitaji ya msingi kama vile: misaada ya dharura au chakula au madawa. Mbele ya ukatili huu wa kishenzi ‘Kongamano’ linazitaka nchi za kiislamu nan chi zote duniani wasimamie majukumu yao ya kisharia, kiundugu na kiubinadamu katika kuwaondeshea wapalestina madhila na mateso wanayopitia na kwa kuwafikishia misaada ya dharura inayohitajika.

Aidha, ‘Kongamano’ linapenda kuwasihi makundi yote ya kipalestina na asasi za kiraia kuungana na kua na mshikamano miongoni mwao ili kuepusha madhara zaidi na kulinda haki zao na kuukomesha uvamizi kwa njia zote ziwezekanazo, kadhalika kuitaka jamii ya kimataifa kufanya juu chini na kwa nguvu zote kuwazuia wavamizi kutoendelea na matendo yao ya kishenzi na ukandamizi na kuzuia ugaidi wanaoufanya.

Halikadhalika ‘Kongamano’ linapenda kuelezea wasiwasi wake na hofu zake juu ya yale yanayojiri katika ‘Mji Mtukufu wa Quds’ miongoni mwa matendo ya ‘uyahudishaji’ ili kufuta athari za kiarabu na za kiislamu za mji huu, majaribio ya kila aina ya kuubomoa Masjid al-Aqsa al-Mubarak, kuwabana wakaazi wa asili wa mji huu waislamu na wakristo, ‘Kongamano’ linapenda kuweka msisitizo kua ‘Mji Mtukufu wa al-Quds’ na ‘Masjid al-Aqsa al-Mubarak’ ni miongoni mwa maeneo matakatifu kwa waislamu duniani kote.

Ijulikane kwamba Masjid al-Aqsa ndio Qibla cha kwanza kwa waislamu na ni sehemu ya safari ya kimiujiza ya Bwana Mtume Muhammad SAW ya Israa na Mi’raaj; kuanzia hapo ndipo ilipoanza safari yake kwenda mbinguni, na ijulikane kua Masjid al-Aqsa ni wa waislamu pekee na hauna uhusiano wowote na mayahudi, na hapa ni lazima kuwatahadharisha waisraili dhidi ya uchafuzi wa heshima ya msikiti huu na kwamba serikali ya kivamizi na nchi zinazowaunga mkono kua watawajibika moja kwa moja dhidi ya maharibiko yoyote juu ya ‘Masjid al-Aqsa’ na ‘Mji Mtukufu wa Quds’, pia ieleweke kwamba sehemu mbili hizi hazipo kwenye mazungumzo yoyote wala hazitoachiwa yeyote na hakuna anaeweza kufanya hivyo; heshima ya sehemu mbili hizi iko juu ya kila mtu.

‘Kongamano’ linawataka na kuwasihi viongozi na raia wote wa nchi za kiarabu na za kiislamu kuwasaidia wapelestina wanaoedelea kukandamizwa, na kuwataka vilevile wabebe majukumu yao ya kidini, ya kitaifa nay a kihistoria katika kulinda na kutetea Mji wa Quds uliokaliwa kimabavu na Msikiti wake uliobarikiwa, na kusimama kidete pamoja na watu wake wanaojitolea na kuwasapoti ili kuzuia ‘Uyahudishaji’ au ‘Utaifishaji’ wa mji huu mtakatifu; yote mawili hayo hayakubaliki kwa namna yoyote ile.

Mbili: Jamhuri ya Iraq:

‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ linawataka na kuwasihi watu wa Iraq kushiriki kikamilifu na kwa roho safi katika kuulinda umoja na mshikamano wan chi yao; Iraq, na kuleta uwiano wa uhakika miongoni mwa matabaka yote ya watu wa Iraq na kusimamia upatanishi wa kitaifa kwa misingi ya kusameheana, haki na uadilifu kwa wote, aidha kukomesha uwepo wa majeshi ya kigeni na kuirudisha Iraq kwenye nafasi yake katika safu ya umma wa kiarabu na wa kiislamu.

Tatu: Somalia:

Ama kuhusu yanayojiri Somalia hiviv sasa; ‘Kongamano’ linapenda kutoa mwito kwa ndugu wote wa Somalia kuanzia raisi, serikali na raia wote na kuwataka wasuluhiane kiukweli na kuachana na migawanyiko, vurugu na vita na badala yake kuyaweka juu maslahi mapana ya watu wa Somalia dhidi ya maslahi ya kibinafsi, aidha, linawataka wasiipoteze fursa hii waliyonayo ya upatanishi chini ya serikali halali iliyopo na kamwe kutoitikia milinganio utetanishi na kurarua umoja wao au kuparagua juhudi za dhati na halisi zinazohitajika katika kipindi hiki kigumu cha historia ya Somalia, linawataka Wasomali wawe na mshikamano na umoja utakaowawezesha kujenga na sio kubomoa, kuunganisha na sio kufarakanisha, kuiendeleza nchi na sio kuidumaza, ili wafikie hali ya amani na utulivu nchini na ili waweze kuijenga upya nchi iliyoangamizwa na vita vya mda mrefu.

Na katika kuyaendea malengo haya; ‘Kongamano’ linashangazwa na kukemea vikali matendo ya kiharamia na kigaidi yanayofanywa na

‘Maharamia’ kwenye fukwe (fuo) za Somalia yanayohatarisha usalama wa safari na biashara za baharini na kuhatarisha amani eneo zima la ‘Bahari Nyekundu’. ‘Kongamano’ linasisitiza kua matendo ya kiharamia haya ni matendo ya kigaidi na ya kijinai aina ya ‘*Hiraba*’ kwa mujibu wa ‘Fiqhi ya Kiislamu’.

Nne: Jamhuri ya Sudan:

‘Kongamano’ linashangazwa na kukemea tuhuma zisizo na msingi zinazoelekezwa kwa Rais wa Sudan Omar al-Bashir kutoka ‘Mahkama ya Kimataifa ya Jinai’ katika kipindi ambacho rasi huyu anatumia juhudi kubwa kuleta amani na utulivu katika nchi ya Sudan, wakati dunia nzima imefumbia jicho maovu na maangamizi ya kidhulma yanayozidi kutekelezwa Ghaza, Ukingo wa Magharibi nam aeneo mengine duniani, jambo hili linaonyesha na kudhihirisha kwa uwazi kabisa unafiki wa kimataifa unaosimamiwa na kile kinachoitwa: “Jamii ya Kimataifa”, ‘Kongamano’ linaitaka “Jamii ya Kimataifa” kusitisha unafiki huu.

‘Kongamano’ linasisitiza kua tatizo la Darfur litatuliwe kwa msingi wa mshikamano na umoja wan chi ya Sudan. Aidha, ‘Kongamano’ linaweka msimamo wake bayana na kuunga mkono juhudi halisi zinazosimamiwa na ‘Jumuia ya Nchi za Kiislamu (OIC) chini ya uongozi wake Mstahiki Katibu Mkuu wa OIC Profesa Dkt. Akmaludin Ihsan Oglu katika kadhia zote hizi na nyenginezo kwenye nyanja za kiuchumi, kisiasa na kiusalama, halikadhalika ‘Kongamano’ linaunga mkono juhudi zinazochukuliwa na nchi za kiislamu zote katika maeneo haya huku tukiwa na matumaini wa kuongeza kasi ya juhudi hizo.

Tunamuomba Allah Ahifadhi umma wa kiislamu dhidi ya kila ovu na baya na kuwaongoza njia ya sawa kupitia viongozi wao. Yeye ndie mwenye kutuwafikia.

≅≅≅

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Ishirini (20) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Wohran, Algeria

25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa'da (Mfungo Pili),

1433,

sawa na 13 – 18 Septemba, 2012

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 186 (1/20)

Yanayohusiana na 'Hukmu ya Kulemewa na kufilisika katika Sharia ya Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini (20) kilichofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa'da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Hukmu ya Kulemewa na kufilisika katika Sharia ya Kiislamu na Mifumo ya Kisasa,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Fasili ya Mlemewa na Mdaiwa alielemewa:

1) Kwa kuzingatia ibara ya saba ya 'Maamuzi ya Kongamano' namba 64 (2/7) inayohusiana na: "Kidhibiti cha 'Kulemewa' ambacho kinaruhusu kumuongezea mda wa kulipa"; ijulikane kua kulemewa ni: sifa ya mpito inayomfika mtu inayomfanya awe amelemewa na majukumu yake ya msingi na kushindwa kulipa madeni anayodaiwa, ama mlemewa ni yule anaesifika na sifa hii.
2) 'Kidhibiti cha kufilisika' ni pale ambapo mali anayomiliki mdaiwa hayatoshi kulipia deni lake, ama aliefilisika ni yule anaesifika na sifa hii.

Mbili: Tofauti za wazi baina ya kulemewa na kufilisika kwa mujibu wa wanafiqihi:

1) Kulemewa ni hali ambayo ima mtu alikua kwenye wepesi au la, tofauti na kufilisika ambayo ni hali inayotanguliwa na wepesi tu.
2) Aliefilisika baada tu ya kutangazwa kufilisika kwake mali zake zinazuiliwa, ama alielemewa kwa mujibu wa vigezo vinavyozingatiwa kisharia kama alivyosema Allah: "*Na akiwa (mdaiwa) ana shida, basi (mdai)*

angoje mpaka afarijike” (Surat al-Baqarah: 280), basi anapewa mda wa ziada huenda akawepesika.

3) Kadhi (Jaji) hatakiwi kumuhukumu alielemewa kufungwa ikithubutu kulemewa kwake, ama aliefilisika anapewa adhabu ya kifungo iwapo imethubutu kua kufilisika kwake kumetokana na ima udanganyifu au khiana au kuzembea au dharau.
4) Kulemewa kunatokana ima na deni au jukumu la kisharia kama nafaqa (matumizi ya familia), tofauti na kufilisika ambako kunatokana na deni tu.

Tatu: Hukmu za ufilisi kwa mujibu wa fiqhi ya kiislamu:

1) Kumzuia aliefilisika kua na uhuru juu ya mali zake ili wadai wake wasidhurike kwa namna yoyote ile, ni kadhi (jaji) tu ndie anaetoa hukmu ya kuzuiliwa aliefilisika kusarifu mali zake na ni yeye kadhi ti ndie atakaeiondoa hukmu hio.
2) Inajuzu pia kumzuia aliefilisika asisafiri, iwapo safari yake hio itawadhuru wadai wake.
3) Mida ya madeni ya baadae inaanguka kwa aliefilisika.
4) Kadhi (Jaji) anaehusika kuuza mali za aliefilisika, anatakiwa kulinda maslahi ya wote mdai na mdaiwa na kugawa thamani yake, ikidhihiri kwa aliefilisika kua ana mali mengine basi inajuzu kwa wadai kuendelea kumtaka awalipe kilichosalia kwenye madeni yao.
5) Ni haki ya mdai kurejeshewa asili ya mali yake iliyopo kwenye mali za aliefilisika, ikiwa bado ipo katika hali yake na hajalipwa thamani yake kamili.

Nne: Kumbebesha gharama (faini) mdaiwa mwenye uwezo anaechelewesha kulipa:

‘Kongamano’ linaweka msisitizo juu maamuzi yake yaliyotangulia namba 51 (2/6) kwenye ibara ya tatu na ibara ya nne; inayohusiana na biashara ya malipo ya polepole na uharamu wa kumuwekea gharama (faini) au malipo fulani kwa mdaiwa mwenye uwezo anaechelesha kulipa, lakini inajuzu kumbebesha gharama za malipo ya mahkama.

Tano: ‘Kongamano’ linaonelea kuakhirisha maamuzi juu ya kadhia zifuatazo katika maudhui ya kulemewa na kufilisika hadi kikao kijacho:

1) Mas’ala ya kifiqhi yanayohusiana na kuzilinda taasisi za fedha za kiislamu, yakiwemo mas’ala ya ‘bima ya madeni’ na ‘ahadi ya kuchangia’.
2) Hukmu zinazohusiana na tasarufi za aliefilisika na alielemewa kwenye kipindi cha shaka.
3) Hukmu za ufilisi wa makampuni na taasisi za fedha kwa mtazamo wa mifumo ya kisasa.
4) Maudhhui inayohusiana na msamiati wa ‘Kulemewa’ kwani inaonekana kua msamiati huu kwenye kanuni (sheria) za kisasa ukimaanisha kufilisika na kulemewa katika fiqhi ya kiislamu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 187 (2/20)

Yanayohusiana na 'Bima Shirikishi: Hukmu na Vigezo vya Kisharia'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini (20) kilichofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa'da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Bima Shirikishi: Hukmu na Vigezo vya Kisharia,** kwenye kikao hiki na vikao vilivyotangulia, na baada ya kupitia mapendekezo yaliyoibuka kutokana na mkutano wa "*Bima Shirikishi: Nyanja zake na Upeo wake na Msimamo wa Sharia ya Kiislamu juu yake*" ulioandaliwa na 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu' uliofanyika hapo Amman, Jordan, na kwa kushirikiana na 'Chuo Kikuu cha Jordan', 'Jumuia ya Kiislamu ya Elimu-Malezi, Sayansi na Utamaduni (ISESCO) na 'Taasisi ya Kiislamu ya Mafunzo na Tafiti' iliyo chini ya 'Benki ya Kiislamu ya Maendeleo' katika kipindi kati ya 26 – 28 Rabii al-Thani, 1431Hijria (11 – 13 Aprili, 2010), na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya yale yaliyoamuliwa kwenye maamuzi namba 9 (9/2) yanayohusiana na 'Bima' na 'Bima-Jumuishi' ya kwamba:

> **"*Moja**: Mikataba ya bima ya biashara yenye malipo maalum (premium) ambayo ndio utaratibu unaotumiwa na makampuni ya bima; kua ni 'Mikataba yenye 'gharar' (udanganyifu) kubwa hali inayopelekea mkataba huu kufisidika kwa maana hio 'Mkataba aina hii ni Haramu'.*
> ***Mbili:** Mkataba mbadala wa bima unaoheshimu misingi ya miamala ya kiislamu ni 'Mkataba wa Bima ya Ushirikiano' uliojikita kwenye misingi ya kuchangia na kusaidia, na ndio hivyo hivyo pia kuhusiana na 'Bima Jumuishi' iliyokaa juu ya msingi wa 'Bima-Shirikishi*".

Mbili: Kulingana na matatizo mbalimbali ya kiutekelezaji yaliyojitokeza kwenye makampuni ya bima za kiislamu, na vikwazo vya kikanuni na vya kiuchunguzaji vinavyoyakabili makampuni haya; ipo haja ya kua na ufahamu kamili wa 'Bima-shirikishi'.

Hivyo basi; inausiwa yafuatayo:

Moja: Kuitaka 'Sekreterieti Kuu ya Kongamano' iunde kamati ya jopo la Mafuqahaa (Wanafiqihi) na Wataalamu wakishirikiana na vituo vya utafiti vinavyohusika na mada hii ili kufikia muongozo kamili utakaoratibu hukmu na vigezo vya kisharia vilivyojikita kwenye misingi ya 'bima-shirikishi', aidha, muongozo huu uelekeze taratibu zinazokubalika kisharia kwa namna itakayorahisisha utekelezaji wake; na miongoni mwa hukmu na vigezo:

1) Ufahamu wa 'Bima-shirikishi' na uhalisia wake kwa mtazamo wa sharia ya kiislamu.
2) Ulinganisho baina ya bima-shirikishi na bima ya kibiashara:
    a) Ulinganisho baina ya bima-shirikishi inayokubalika kisharia na baina ya misingi ya kimataifa ya ushirikiano.
    b) Ulinganisho baina ya bima-shirikishi inayokubalika kisharia na baina ya misingi ya bima ya kibiashara.
3) Mahusiano na utambulisho baina ya pande za bima-shirikishi hususan utambuliso wa uhusiano baina ya washiriki wa mfuko na uhusiano wa mfuko na wasimamizi wake.
4) Hukmu za malipo ya wasimamizi na vigezo vya kuainisha malipo hayo.
5) Hukmu za masalio (faida) ya bima na hasara zake zitokeapo.
6) Kushiriki na kujiondoa kwenye mfuko wa bima-shirikishi na vigezo vyake vya kisharia.
7) Hukmu za kisharia za kufunga hesabu za mfuko wa bima-shirikishi.
8) Hukmu na vigezo vya kisharia vya 'bima-mtawanyo' (reinsurance).
9) Msingi wa kushirikiana kwenye faida na hasara.
10) Msingi wa ubadilishanaji na mambo yanayotaalikiana nayo.
11) Msingi wa uwajibikaji na mambo yanayotaalikiana nayo.

Mbili: Pendekezo la mswada liwasilishwe na kamati hii kwenye kikao kijacho cha 'Kongamano' ili 'Maamuzi' yaweze juchukuliwa kwa mujibu

vipengele-tajwa kwenye ibara: ‘Mbili’ hapo juu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 188 (3/20)

Yanayohusiana na 'Kukamilisha Maudhui ya Sukook za Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini (20) kilichofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa'da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya; na baada ya kupitia mapendekezo yaliyotokana na warsha ya: 'Sukook za Kiislamu: Maelezo na Tathmini' iliyofanyika Jeddah, kwenye ukumbi wa 'Taasisi ya Tafiti za Uchumi wa Kiislamu' (Chuo Kikuu cha Mfalme Abdulaziz) na kwa kushirikiana na 'Taasisi ya Kiislamu ya Utafiti na Mafunzo (iliopo chini ya Benki ya Kiislamu ya Maendeleo) katika kipindi cha 10 -11 Jumada al-Thani, 1431 Hijria sawa na 24 – 25 May, 2010, na kwa kuzingatia pia 'Maamuzi ya Kongamano' namba 178 (4/19) yanayohusiana na 'Sukook za Kiislamu (Tawarruq) na utekelezajij wake wa kisasa yaliyopitishwa kwenye kikao cha kumi na tisa (19) na maamuzi mengine mbalimbali, na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Vigezo vikuu:

1) Sukook za Kiislamu zinatakiwa zifikie makusudio makuu ya sharia ya kutanashati maendeleo, kusaidia shughuli za uhakika na kusimamia haki baina ya pande mbili.
2) Mikataba ya Sukook inatakiwa ithibitishe muktadha wake kwa kuthubutu umiliki kisharia na kikanuni na mambo yanayoambatana nayo ya kua na uwezo wa kusarifu na kuwajibika, aidha, mikataba hio ni lazima iwe na uwazi na kusiwepo udanganyifu na mfano wake, na kuhakikisha usalama wa mambo yatakavyokua kisharia.

3) Hati za Sukook zinatakiwa ziweke bayana taratibu zote za kudhibiti utekelezaji wake na kuhakikisha kua hakuna udanganyifu, lakini kuwepo kwa utaratibu wa kurekebisha kasoro zozote zitakazojitokeza, aidha, kuwepo na uhakiki wa mara kwa mara ili kujihakikishia usalama wa matumizi wa sukook kwenye malengo yaliyokusudiwa, na kujiridhisha kua utekelezaji wa vifungu vyote vya mikataba unaendana na namna iliyokusudiwa kisharia.
4) Sukook za Kiislamu zinatakiwa kuakisi tofauti za msingi zilizopo baina yake na baina ya hati za riba kwenye muundo wake na zionekane athari zake kwenye utaratibu wa uuzaji wake uwekaji bei.

Mbili: Ahadi ya dhamana:

1) Haijuzu kwa Mudharib au Mshirika au Wakala kuahidi chochote katika yafuatayo:
   a) Kununua sukook au maliasili ya sukook kwa thamani ya sokoni au kwa kima kilichoainishwa mapema kwa namna ambayo itapelekea kubeba dhima ya rasilimali au kupokea pesa taslimu mda wa sasa mkabala wa pesa nyingi zaidi ambazo zingelipwa baabdae, ama kesi za kuchupa au kuzembea zinaamiliwa tofauti kwani hapa haki za wabeba sukook zinalindwa.
   b) Kuwakopesha wabeba sukook kunako mapungufu ya faida iliyotarajiwa kwa namna ambayo itapelekea mazingira ya mkopo na mauzo au mkopo kwa faida, lakini inajuzu kuweka akiba ya faida kufidia mapungufu yanayotarajiwa.
2) Inajuzu kujipanga na kuchukua tahadhari dhidi ya mambo hatarishi kwa rasilimali kwenye sukook na kwengineko kwa kuingia kwenye bima-shirikishi au takaful inayodhibitiwa kwa misingi ya sharia tukufu.

Tatu: Kumkodisha muuzaji maliasili aliyoiuza:

Haijuzu kuuza asilimali kwa malipo ya hivi sasa lakini kwa sharti muzaji yule akodi asilimali ile kwa ijara iliyofungamanishwa na ahadi ya kumiliki ambapo thamani ya baadae itapita ile thamani ya sasa hivi, nisawa sharti hili liwe wazi au fiche, muamala aina hii ni biashara ya '*al-'Inah*' ambayo imeharamishwa kisharia, kwa hio haijuzu kutoa sukook kwa muamala

kama huu.

Nne: Ukodishaji wa mali isiyokuwepo lakini ijulikanayo kwa malipo ya baadae:

1) Inajuzu kukodisha mali yasiyokuwepo lakini yajulikanayo kwa namna ambayo haitokhalifu misingi ya miamala ya kisharia, aidha, inajuzu kutoa sukook kwa msingi huo.
2) Tatizo la muamala huu lipo kwenye mambo mawili:
   a) Hukmu ya kucheleweshaji malipo baada ya kikao cha makubaliano.
   b) Hukmu ya kuuza sukook za ijara za mali yasiyokuwepo na kabla ya kuainisha mahali pa ijara.

'Kongamano' linaielekeza 'Sekreterieti Kuu' kuunda jopo la wanazuoni na wataalamu kwa minajili ya kudurusu muamala wa aina hii na kuwasilisha matokeo ya utafiti wao kabla ya kikao kinachofuata.

Tano: Uuzaji wa hati za fedha; sukook au hisa au mikoba ya uwekezaji:

1) Iwapo hati za fedha zilizopo ni pesa au madeni basi uuzaji wake unafuata hukmu za ubadilishanaji sarafu au kuuza deni.
2) Iwapo hati za fedha zilizopo ni asilimali au manufaa au haki basi inajuzu kuziuza kwa bei watakayokubaliana.
3) Ama Iwapo hati za fedha zilizopo ni mchanganyiko wa pesa, madeni, asilimali, manufaa na haki basi hapo kutakua na hali mbili:

   a) Hali ya kwanza ni pale ambapo pesa na madeni zinafuata kinachosihi kufuatwa (asilimali, manufaa, shughuli za kiuchumi na kadhalika), na ikawa hati za fedha zimebeba umiliki wa kile kinachofuatwa, basi hapo inajuzu uuzaji wa hati za fedha bila ya kuzingatia kiwango (cha asilimia) cha pesa na madeni mkabala wa mali yaliyopo.
   b) Hali ya pili ni pale ambapo pesa na madeni hazifuati mali yoyote au kutokuwepo kwa hati-miliki, basi uuzaji utafuata hukmu za anaeshinda.

4) Iwapo kampuni au mradi unaowakilishwa kwenye hati ya fedha bado kuanza kazi au iko chini ya kufunga hesabu (kufilisika) basi uuzaji wake utafuata hukmu za anaeshinda.

5) Imedhihiri kupitia kwenye tafiti zilizowasilishwa kua ufuasi unathubutu kupitia umiliki wa kituo au shughuli au sehemu ya biashara, aidha, imedhihiri pia utanuzi wa kigezo cha ‘anaeshinda’. Kutokana na uwepo wa haja ya kuainisha vigezo vya ufuasi na utambulisho wa hali zake na kuainisha vigezo vya anaeshinda na utambulisho wa hali zake; ‘Kongamano’ linaielekeza ‘Sekreterieti Kuu’ kuunda jopo la wanazuoni na wataalamu kwa minajili ya kudurusu vigezo hivi kwa mujibu wa yaliyotangulia na kuwasilisha matokeo ya utafiti wao kabla ya kikao kinachofuata.

Sita: Athari ya ‘Maamuzi’ juu ya mikataba iliyotangulia:

1) ‘Maamuzi’ yanayochukuliwa na ‘Kongamano’ yanaanza kufanya kazi pale yanapoamuliwa, na hayatoathiri mikataba iliyotangulia kufungwa kabla ya hapo ikiwemo sukook zilizotolewa kutokana na ijtihad au fatwa inayozingatiwa kisharia.
2) Ni wajibu kwa waislamu kufuata sharia tukufu katika maisha yao na shughuli zao kadri ya uwezo wao kama alivyosema Allah: “*Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama muwezavyo*”,[1] na neon lakae tena: “*Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya iwezavyho*”,[2] zaidi ya hapo Allah Anasamehe wale wasiokua na uwezo, lakini waislamu wanatakiwa kuongeza bidii na juhudi za makusudi kutekeleza maagizo ya sharia ya kiislamu ili hikma ya sharia ya kutengeneza jamii ya kiislamu iliyo bora ipatikane.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

[1] Surat al-Taghabun: 16.
[2] Surat al-Baqarah: 286.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 189 (4/20)

Yanayohusiana na 'Kukamilisha Maudhui ya Mikataba ya Utengenezaji (Ukarabati)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini (20) kilichofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa'da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na **Kukamilisha Maudhui ya Mikataba ya Utengenezaji (Ukarabati),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya pamoja na kuzingatia 'Maamuzi ya Kongamano' namba 103 (6/11) yanayohusiana na 'Mikataba ya Matengenezo' kwenye kikao cha kumi na moja (11);

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya maamuzi-tajwa namba 103 (6/11) ya kua mkataba wa matengenezo unalazimisha upande fulani kukagua na kutengeneza kinachohitajika kutengenezwa ima mara kwa mara au itokeapo dharura kwa kipindi maalum na kwa malipo maalum, mtengenezaji anaweza kujilazimisha ima kushughulikia kazi ya matengenezo pekee au kazi na vifaa (vipuri).

Mbili: Kuhusu aina ya mikataba ya utengenezaji ambazo ziliakhirishwa utowaji wa hukmu kwenye maamuzi-tajwa; 'Kongamano' linapendekeza kuakhirisha tena ili aina hizo ziwe wazi zaidi kuweza kutoa hukmu, utafiti wa ziada uendelee na matokeo yake kuwasilishwa kwenye kikao kijacho.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 190 (5/20)

Yanayohusiana na 'Nafasi ya Makongamano ya Kifiqhi katika Kuongoza Taratibu za Taasisi za Kifedha za Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini (20) kilichofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa'da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na **Nafasi ya Makongamano ya Kifiqhi katika Kuongoza Taratibu za Taasisi za Kifedha za Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya; 'Kongamano' linapenda kusisitiza kua uwepo wa makongamano ya kifiqhi na taasisi za kifedha na benki za kiislamu ni miongoni mwa mafanikio makubwa ya zama hizi, aidha, 'Kongamano' linathamini kazi zinazofanywa za na bodi za udhibiti wa kisharia na taasisi za kifedha za kiislamu leo kwa mchango mkubwa wanaotowa katika kuhuisha mifumo ya kifedha ya kiislamu ya kisasa na kujenga Imani ya watu juu yake.

Hivyo basi linaonelea:

1) Upo ulazima wa ushirikiano baina ya vyombo vya udhibiti katika taasisi za kifedha za kiislamu na makongamano ya kifiqhi kwa lengo la kuratibu, kusaidiana na kubadilishana mawazo.
2) Ulazima wa kuratibu miongoni mwa vyombo vya udhibiti katika taasisi za kifedha za kiislamu.
3) 'Kongamano' liandae tafiti faidifu zenye kunufaisha zitakazowezesha kuimarisha nafasi za taasisi za kifedha za kiislamu katika utekelezaji wa sharia ya kiislamu na kupendekeza suluhisho muwafaka ya matatizo na mitikisiko.

4) ‘Kongamano’ liandae ‘sheria-jumuishi’ katika miamala ya kifedha ya kiislamu ili iwe ni muongozo utakaotumika kwenye miamala hii.
5) ‘Kongamano’ linakumbushia ibara ya sita (6) kifungu cha kwanza (1) katika maamuzi yaliyotangulia namba 188 (3/20) kuhusiana na maudhhui ya sukook za kiislamu, kua:

   “*6(1) Maamuzi yanayochukuliwa na ‘Kongamano’ yanaanza kufanya kazi pale yanapoamuliwa, na hayatoathiri mikataba iliyotangulia kufungwa kabla ya hapo ikiwemo sukook zilizotolewa kutokana na ijtihad au fatwa inayozingatiwa kisharia*”.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kuendeleza mdahalao na benki kuu na vyombo vya usimamizi katika nchi za kiislamu ili kuziwezesha taasisi za kifedha za kiislamu kutekeleza majukumu yake katika nyanja za kiuchumi na maendeleo ya kitaifa ndani ya udhibiti maalum unaowiana na kazi za kifdha za kiislamu.
2) Kuyawasilisha ‘Maamuzi ya Kongamano’ kwenye taasisi zote za kifedha na benki za kiislamu na taasisi za kielimu na vituo vya utafiti vya ndani na vya kimataifa, na yaenezwe ‘Maamuzi’ hayo pia kupitia vyombo vya habari na mitandao ya mawasiliano ya kijamii (social media).
3) Kuzitaka taasisi za kifedha za kiislamu kuyafanyia kazi maamuzi ya ‘makongamano ya kifiqhi’.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 191 (6/20)

Yanayohusiana na 'Haki za Wafungwa (Mahabusu) katika Fiqhi ya Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini (20) kilichofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa'da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na **Haki za Wafungwa (Mahabusu) katika Fiqhi ya Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

'Baraza la Kongamano' linausia yafuatayo:

1) 'Sekreterieti Kuu' isimamie kuandaa waraka wa haki za wafungwa kwa kushirikiana na wataalamu kutoka nchi wanachama.
2) Kuwepo na chombo huru cha kusimami majela na kulinda haki za wafungwa na kupiga darubini kwa yanayojiri kwenye jela na kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wanaovunja haki hizo.
3) Nchi za kiislamu zinatakiwa zianzishe (zijenge) jela kwa viwango vitakavyolinda haki za binadamu na heshima yake, aidha, miundo ya jela inatakiwa iwe rafiki na masuala ya usalama na haki zao.
4) Kutoubana uhuru wa watu ila kwa kwa mujibu hukmu ya mahkama iliyotolewa kwa kufuata vigezo vya kimahkama vinavyolinda haki na kuepusha dhulma na mabavu.
5) Kuwawezesha wafungwa kiuchumi kwa kuwaanda na kuwafunza stadi za kuwanufaisha watakazo faidika nazo wakiwa vifungoni na hata baada kumaliza mida yao ya vifungo pamoja na kuwalindia ajira na malipo yao kwa kazi wanazozifanya.
6) Kulinda haki za wafungwa za kijamii kwa kukutana na familia zao na marafiki zao wanaojulikana kwa tabia zao, na pia kuruhusu kukutana mtu na mkewe pamoja na kulinda usiri (privacy) wao.
7) Kulinda haki zote za wafungwa zilizoidhinishwa na sharia, ikiwemo

haki yao ya chakula cha heshima, mavazi laiki, na huduma za vyoo vyenye maji safi pamoja na kuwapatia mazingira ya utwahara (usafi).

8) Kuwawezesha wafungwa kutekeleza ibada zao za kidini kwa uhuru pamoja na kuwafundisha kwa ujumla hususan elimu ya dini na kuwarahisishia wakutane na walimu na masheikh.
9) Kupunguza adhabu hasi zinazobana uhuru kadri inavyowezekana kwa kuweka ima adhabu ya kimwili au adhabu nyengine mbadala isiokua jela, ili kuwaepushia natija hasi za kubana uhuru.
10) Kutotanua suala la vifungo vya dharura (akiba), kukamata na mfano wake ambavyo baadhi ya nchi wanatumia pasipo na hukmu ya mahkama; badala yake ziwepo sheria za kutosha zinazolinda haki za wanaotakiwa kukamatwa na kuwe na mda maalum usiozidi hapo wa mtu kua kwenye kifungo cha dharura.
11) Kutungwe sheria katika nchi za kiislamu mbalimbali za kulipa fidia wafungwa ambao itathubutu kua walikua hawana hatia, na pia fidia kwa wafungwa walioteswa pamoja na kuwawajibisha wahusika na ubabe huo.
12) Kuandaa warsha za kila mara za kuwaelimisha maofisaa wa jela na wahusika wengine juu haki na nyajibu za kila mtu, na kukumbushia kwa kila atakaekiuka au kukhalifu maadili ya jela anaweza kuwajibishwa kwa kuzembea kwenye majukumu yake.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 192 (7/20)

Yanayohusiana na 'Adhabu ya Kifo kwa Mtazamo wa Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini (20) kilichofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa'da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na **Adhabu ya Kifo kwa Mtazamo wa Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na baada ya kusisitiza kua Uislamu kupitia misingi yake ya kimaadili inayolinda haki za binadamu, umwkua na nafasi nzuri na ya kihistoria na yenye athari kubwa katika kupunguza hali za vifo hasahasa katika nyakati ngumu za utanuzi wa uislamu duniani, hilo lilifanyika kupitia misingi imara ya kuzuia umwagikaji wa damu kama ile inayosema: 'Msingi wa Uharamu wa Damu' na 'Msingi wa Kutotekeleza Adhabu ya Hudood Panapokua na Utatanishi' na 'Msingi wa Uangalifu kwenye Damu';

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Adhabu ya kifo ni miongoni kwa sehemu ya mfumo wa adhabu inayosimamia maslahi mapana na makuu ya jamii za kibinadamu, adhabu hii inatakiwa inasibiane na uzito wa kosa la jinai lililotendwa na mkosaji kwa mujibu wa misingi ya kisharia, kwa maana hii kelele zinazoelezewa na wapinga hukmu hii bila mantiki sahihi hazikubaliki kisharia wala kiakili.
2) Adhabu ya kifo ni kumyima mkosaji haki ya kuishi kwa hukmu ya mahkama.
3) Hahukumiwi mtu adhabu ya kifo ila baada ya kuthibiti kua mkosaji ametenda kosa la jinai linalowajibisha hukmu hio kupitia misingi na taratibu za ithbati za kimahkama.
4) Hukmu ya kosa la jinai inayowajibisha adhabu ya kifo ni lazima iwe na

tegemeo la wazi kutoka sharia ya kiislamu.

5) Lazima kuwepo dhamana za uhakika dhidi ya ukurupukaji wa kutekeleza adhabu hii au kukosea kutoa hukmu.
6) Lazima tahadhari zote zichukuliwe za kuzuia utendadaji wa makossa ya jinai yanayopelekea adhabu ya kifo, ili mkosaji asiwe na udhuru wakati wa kutekelezwa adhabu hii juu yake.
7) Sheria za nchi za kiislamu zipewe nafasi ya kuchagua mbinu ya utekelezaji wa adhabu ya kifo ndani ya misingi mikuu ya sharia ya kiislamu na makusudio yake.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 193 (8/20)

Yanayohusiana na 'Uhandisi wa Maumbile na Jinomu ya Binadamu ya Maumbile kwa Mtazamo wa Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini (20) kilichofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa'da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na **Uhandisi wa Maumbile na Jinomu ya Binadamu ya Maumbile kwa Mtazamo wa Kiislamu,** na kwa mapendekezo yaliyotokana na kikao cha kumi na moja (11) cha 'warsha ya ya tiba na fiqhi' iliyofanyika Kuwait kwa kushirikiana baina ya 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu' na 'Jumuia ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' ya Kuwait juu ya maudhui ya **Uhandisi wa Maumbile na Tiba ya Kimaumbile kwa Mtazamo wa Kiislamu,** mwaka 1419 Hijria sawa na 1998, na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya,

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Kuakhirisha uchukuliwaji wa maamuzi hadi kwenye kikao kijacho cha 'Kongamano'.
2) Kuitaka 'Sekreterieti Kuu' kuandaa warsha mahsusi itakayoangazia kwa kina juu ya maudhui haya na kuwasilisha mapendekezo katika kikao kijacho cha 'Kongamano'.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 194 (9/20)

Yanayohusiana na 'Ushahidi wa kisheria kwa Kutumia Dokezo (*Qarina*) na Dalili (Mapya yaliyoibuka)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini (20) kilichofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa'da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na **Ushahidi wa kisheria kwa Kutumia Dokezo (*Qarina*) na Dalili (Mapya yaliyoibuka),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya,

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Fasili ya *Qarina* (Dokezo): Qarina (Dokezo) ni jambo la dhahiri linalotoa utambulisho wa kujua lisilojulikana.

Mbili: Aina za *Qarina* (dokezo): Qarina ina ufahamu mpana unaojumuisha anwai mbalimbali kwa kuzingatia vitu mbalimbali, kwa nyakati za sasa pameibuka aina mpya za *qarina* kutokana na maendeleo kisayansi na ya kiteknolojia kama vile; alama za vidole, picha, sauti zilorikodiwa, saini ya lielektroniki, barua-pepe na kadhalika.

Tatu: Kuzifanyia kazi *qarina*: Kimsingi, hakutolewi hukmu yoyote ila kuwepo hoja ya kisharia inayobainisha ukweli kama vile; kukiri au ushahidi, au kiapo, pasipopatikana mojawapo ya yaliyotajwa basi inajuzu kuzifanyia kazi *qarina* za uhakika ima ziwe za kimaandiko au kimahkama, kwa hio:

1) Inajuzu kuzitegemea *qarina* za kisasa za uhakika katika kuthibitisha haki zinazoambatana na mali na mkosa ya jinai mbalimbali isipokua kwenye kuthibitisha kesi za kisasi na zile za hududi.
2) Inajuzu kuzitegemea *qarina* katika kuthibitisha mikataba iwapo hakuna

kiashiria cha kuibatilisha.

3) *Qarina* zisizokua za uhakika ziaweza kutumika kuthibitishia haki na mfano wako iwapo kuna dalili nyengine za kutilia nguvu na mahkama ikawa ni yenye kuridhika na hilo.

Nne: Alama ya urithi (DNA): Kisayansi, alama ya urithi (DNA) ni mojawapo ya njia za uhakika zinazokaribia kutokosea katika kuthibitisha ubaba kibaiolojia, na kuthibitisha utambulisho wa mtu hasahasa katika nyanja za tiba, na alama hizi za urithi zinaweza kua ni *qarina* za uhakika zinazokubalika na wanafiqihi katika kuthibitisha kesi mbalimbali zisizokua zile za hududi, uvumbuzi huu wa 'alama za urithi' ni katika mafanikio makubwa ya zama hizi kwenye sanaa ya '*Qayyafa*' (elimu ya nasaba na usuli) ambayo inakukabilikana wanazuoni wa fiqhi wengi kua inaweza kuthibitisha nasaba inayotetaniwa, lakini ni vyema *Qarina* hii ichukuliwe kwenye maabara mbalimbali.

Inawezekana kutumia 'alama za urithi' kwenye nyanja za kuthibitisha nasaba kama vile inavyokubalika kutumia elimu ya *Qayyafa* katika mazingira yafuatayo:

1) Mazingira ya utatanishi ya kutojua nasaba; utatanishi wa aina yoyote miongoni mwa yaliyotajwa na wanafiqihi.
2) Mazingira ya kuchanganyikana watoto waliozaliwa mahospitalini na vituo vya watoto na mfano wake, halikadhalika mkanganyiko wa watoto wa chupa (baby tubes).
3) Mazingira ya kupotea kwa watoto au kuchanganyikana kwa sababu ya ajali au majanga au inaposhindikana kuwajua watu (wazazi) wao, halikadhalika kunapopatikana maiti zisizoweza kujukikana utambulisho wao ima kwa sababu ya vita au sababu nyengine.

Tano: Haijuzu kutegemea 'alama za urithi' katika kukana nasaba, aidha haitumiki kwenye kesi za '*Li'an*' (mchakato wa mume kukana mimba ya mkewe).

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

Tamko la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’

Kuhusiana na:

‘Utengenezaji wa Filamu ya Kashfa Inayovunja Heshima ya Bwana Mtume Muhammad SAW Nchini Marekani’

Bismillah al-Rahman al-Raheem

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ likiwa kwenye kikao chake cha ishirini (20) kinachofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa’da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012; linafuatilia kwa wasiwasi mkubwa mienendo ya baadhi ya wachukivu wa Uislamu kufika kutengeneza filamu ya kashfa kwa minajili ya kuvunja heshima ya Bwana Mtume Muhammad SAW nchini Marekani.

Jambo hili, ambalo linakwenda kinyume kabisa na sharia za dini zote na pia kupingana na sheria za kimataifa na maadili ya kibinadamu, linachochea na kuchokoza mamilioni ya waislamu katika matakatifu yao makuu kabisa nayo ni Mtume Muhammad SAW, ambae alitumilizwa kama rehma ya Mwenyezi Mungu kwa ulimwengu mzima, aidha jambo hili lichochea na kuchokoza wenye dhamira hai, na wala halisaidii katika kuleta amani na atu kuishi kwa pamoja, bali linapelekea machafuzi na machafuko yasiyojulikana yatakwisha vipi.

Wakati ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ likiwa linalaani vikali kitendo hiki cha kuumbua na cha kishenzi kinachofanywa na watu wenye mirengo miovu, linapenda kubainisha yafuatayo:

Moja: Uhuru sio kua hauna mipaka, lakini unaambatana na uwajibikaji, na sharti la uhuru ni kua usiguse na kuwaudhi au kuwakera wengine kwenye haki zao nyeti, inakuaje watu wakawa na ujasiri wa kuchafua na kukashifu matakatifu ya dini za wengine na wafuasi wao??, hata ‘baraza kuu la umoja wa mataifa’ limesisitiza mara kwa mara juu ya jambo hili. Katika kikao cha

hamsini na tisa (59) cha ‘baraza kuu’ kilichofanyika tarehe 11/11/2004 kulipitishwa ‘maamuzi’ ya kushajiisha midahalao miongoni mwa dini mbalimbali, na wakati huohuo kukemea uchafuzi wa matakatifu ya dini, na kususutiza kua kunasihiana na midahalo miongoni mwa dini mbalimbali ni mojawapo ya nguzo muhimu za uwiano wa kiustaarabu na kujenga utamaduni wa amani.

Katika kikao cha sitini na moja (61) cha ‘Kamati ya Haki za Binadamu’ paligusiwa madhila yanayowakabili jamii za kiislamu katika nchi zisizokua za kiislamu, na mtazamo hasi wa uislamu unaokaririwa kwenye vyombo vya habari-mawasiliano vya nchi hizo, na kupitisha kanuni za kibaguzi dhidi ya waislamu. ‘Kamati ya Haki za Binadamu’ ilipitisha maamuzi kadhaa ya kupinga uchafuzi wa matakatifu ya dini, aidha ‘Kamati’ imezitaka nchi zote wanachama waweke sheria kali za kupiga marufuku shughuli zozote za kifikra na kimaandiko zilizojikita kwenye ubaguzi na uchukivu zinazoelekezwa dhidi ya dini yoyote au wafuasi wa dini yoyote kua ni vitendo vya kiubaguzi au uadui au kuleta vurugu.

Mambo muhimu yanayopatikana kwenye maamuzi haya: ni msisitizo kwamba uchafuzi wa dini yoyote ile ni miongoni mwa sababu zinazopelekea ‘Mgawanyiko wa kijamii’ na kupelekea uvunjwaji wa haki za binadamu na kuathiri vibaya uwiano wa kijamii wa kuishi kwa pamoja kwa amani na kuheshimiana miongoni mwa wafuasi wa dini mbalimbali.

Mbili: ‘Baraza la Kongamano’ linakataa ‘unafiki’ wa baadhi ya nchi katika kuamiliana na kadhia za uislamu na waislamu, na kuzitaka nchi kama hizi kunakofanyika matendo haya ya kashfa na kuumbua wayakomeshe kivitendo na wasitosheke kukemea kwa mdomo lakini hakuna athari yoyote, na pia kuwataka wawajibishe wahusika wa kashfa kama hizi.

Tatu: ‘Baraza la Kongamano’ linawataka viongozi wa nchi za kiislamu kuchukua misimamo thabiti dhidi ya matendo ya kashfa yanayofanyika nchi nyengine na wawatahadharishe dhidi ya kuharibika kwa maslahi ya nchi hizo na mustakbali wa mahusiano yao miongoni mwa watu na tamaduni.

Nne: ‘Baraza la Kongamano’ linaziomba ‘asasi za kiraia’ za nchi za

kimagharibi na watu wenye utu na dhamira wakatae tabia hizi mbovu za kukera, na washikamane na maadili ya kiustaarabu yanayolinda nakuheshimu imani za wafuasi wa dini na kuheshimu matakatifu yao, aidha, linalitaka ‘baraza la umoja wa mataifa’ litoe maamuzi ya kulazimisha na kuwatia hatiani kijinai kila anaejihusisha na matendo ya chuki na uchochezi dhidi ya uislamu na matakatifu yake.

Tano: ‘Baraza la Kongamano’ linawataka waislamu wote kupitia taasisi zao mbalimbali kusimama kidete na kukemea matendo haya ya kashfa na wasimame ili kumnusuru Mtume Muhammad SAW, na wafanye hivyo kwa njia ya ustaarabu na amani kwa mujibu wa misingi ya sharia bila kuharibu mali na roho za watu au kuchafua ofisi za kibalozi za kigeni zilizopo nchini mwao; haya ndio mafundisho na maadili ya dini yetu ya kulinda ahadi na mikataba.

Sita: ‘Baraza la Kongamano’ linawasihi waislamu kushikamana na mwenendo wa Bwana Mtume Muhammad SAW na kumuiga kwenye maisha yetu na kumfanya awe ni kielelezo (kigezo) chetu na kuusambaza ujumbe wake ambao ni huruma (rehma) kwa binadamu wote na ulimwengu mzima, tuwajulishe binadamu uhalisia wa ujumbe huu na kurekebisha makosa tuliyonayo ambayo maadui wa uislamu na waislamu wanayatumia kama mwanya wa uchafuzi. Ni wazi kwamba waislamu hawana hata chembe ya shaka kwenye nyoyo zao kua dini hii ya uislamu ni ya haki na kwamba Allah SWT ni Mwenye kuihifadhi na kuilinda na kwamba uislamu, hatimae ndio utakaoshinda, na kwamba Yeye (Allah SWT) ni mwenye muliinua neno lake na kumnusuru Mtume wake na kuidhihirisha dini yake kwa walimwengu wote na mwenye kuwanyamazisha wachafuzi na wanaomkashifu Mtume SAW, kama alivyosema: “*Hakika Sisi tunatosha kukukinga na wanao kejeli*” (Surat al-Hijr: 95), akasema tena: “*Hakika anaye kuchukia ndiye aliye mpungufu*” (Surat al-Kauthar: 3).

Mwisho wa maombi yetu ni kumhimidi Allah SWT Mola wa walimwengu wote, na kuomba sala na salamu zimfikie Mtume wetu na aali zake na maswahaba wake wote.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≈≅

Tamko la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’

Kuhusiana na:

‘Mji Mtukufu wa al-Quds na Masjid al-Aqsa al-Mubarak’

Bismillah al-Rahman al-Raheem

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ likiwa kwenye kikao chake cha ishirini (20) kinachofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa’da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012; linafuatilia kwa karibu kile kinachoendelezwa na serikali ya kimabavu ya Israeli cha kuuyahudisha mji mtukufu wa al-Quds na majaribio ya makusudi ya kutaka kuubomoa Masjid al-Aqsa al-Mubarak kupitia unyakuzi-endelevu wa ardhi na maeneo mapana yanayouzunguka Masjid al-Aqsa al-Mubarak, ili kujenga majumba marefu yatakayotenganisha mtaa wa ‘Selwan’ na Masjid al-Aqsa upande wa kusini, na kuutenganisha ‘mji mkongwe’ na Masjid al-Aqsa upande wa magharibi, aidha, kuendelea na kazi ya kuchimba maeneo mbalimbali ya ardhi inayopakana na upande wa kusini na kuendelea kuchimba maeneo yanayouzunguka Masjid al-Aqsa na chini yakeupande wa mbele; jambo ambalo ni hatarishi kwa msikiti huo na huenda ikapelekea kuporomoka.

‘Kongamano’ linafuatilia mambo haya kwa wasiwasi mkubwa na kukemea vikali sana muendelezo wa matendo haya ya kijinai, aidha, linakemea uvamizi mtawalia wa viongozi wa serikali ya kimabavu ya Israeli na makundi ya kiyahudi yenye mirengo mikali kuingia sebule za Masjid al-Aqsa mara kwa mara ili kuandaa mazingira mapya ya kuugawa mskiti huo kiwakati na kimahali.

Wakati ‘Kongamano’ linakemea yote haya kwenye kikao kikao chake cha ishirini (20) kinachofanyika Wohran, (Algeria); linasisitiza yafuatayo:

Masjid al-Aqsa al-Mubarak na maeneo yake yote na sebule zake na

viwanja vyake ni mali ya waislamu pekee na hakuna haki mtu mwengine yeyote kusarifu sehemu yoyote ya msikiti huo, aidha, linaibebesha serikali ya kimabavu ya Israeli majukumu na uwajibikaji wa haribiko lolote litakalousibu Masjid al-Aqsa al-Mubarak, na kuwataka waislamu wote kote duniani raia na serikali kubeba majukumu yao na kuwajibika kidini kwenye kuuhami Masjid al-Aqsa na Mji Mtukufu wa al-Quds.

Mwisho wa maombi yetu ni kumhimidi Allah SWT Mola wa walimwengu wote, na kuomba sala na salamu zimfikie Mtume wetu na aali zake na maswahaba wake wote.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Tamko la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’

Kuhusiana na:

‘Matukio Yanayojiri katika Nchi ya Syria’

Bismillah al-Rahman al-Raheem

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ likiwa kwenye kikao chake cha ishirini (20) kinachofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa’da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012; limekua likifuatilia matukio yanayojiri nchini Syria kwa zaidi ya miezi kumi na nane (18) sasa na matakwa ya raia wan chi hio ya kua na uhuru, heshima na kundoshewa dhulma na unyanyasaji, ilianza kama maandamano ya amani lakini serikali kupitia vyombo vyake wakahusika na mauaji na uchafuzi wa mali na roho za raia na kuwabomolea myumba zao, wakati ‘Kongamano’ linakemea matukio hayo ya kinyama (kikatili) linatangaza yafuatayo:

Moja: Kuwaunga mkono raia wa Syria kwenye matakwa yao ya kudai uhuru, heshima na fahari.

Mbili: Linasisitiza uwepo wa Syria kama nchi moja iliyoungana, na kukataa madai yoyote ya kuigawa nchi hio kwa misingi yoyote ile.

Tatu: Linakemea uadui wa kinyama (kikatili) dhidi ya raia wanaoandamana kwa amani na kuwaua kikatili kwa kuikatakata miili yao, aidha, linakemea vikali ubomoaji wa majumba na miji na kuangamiza mashamba na vizazi.

Nne: Linaitaka serikali ya Syria kusitisha maramoja matendo yote ya mauaji, uadui na umwagaji wa damu na kuondosha ishara zote za matumizi ya silaha za kijeshi kwa raia.

Tano: Linaitaka serikali kuachilia huru wafungwa wote wa kisiasa kwa haraka iwezekanavyo.

Sita: Linaitaka serikali ya Syria kuruhusu mashirika ya misaada kwa minajili ya kutibu majeruhi na kuwasilisha misaada ya dharura ya chakula na dawa kwa waliojeruhiwa na wanyonge.

Saba: Linaitaka 'Jamii ya kimataifa' na nchi zote duniani kusimama safu moja na raia wa Syria, na kuzitaka nchi zote kuwasaidia raia wa Syria na kutetea maslahi yao.

Nane: linazitaka nchi na raia wote duniani kuharakisha kuwasaidia watu wa Syria kwa misaada ya kibanadamu na kuwalinda raia waliopo nchini na wale waliokimbili nchi nyengine.

Mwisho wa maombi yetu ni kumhimidi Allah SWT Mola wa walimwengu wote, na kuomba sala na salamu zimfikie Mtume wetu na aali zake na maswahaba wake wote.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Ishirini na Moja (21) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Riyadh, Saudi Arabia

15 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1435 Hijri

sawa na 18 – 22 Novemba, 2013

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 195 (1/21)

Yanayohusiana na 'Uangalifu kwenye Miamala ya Kifedha'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na moja (21) kilichofanyika Riyadh, (Saudi Arabia) 15 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1435 Hijri, sawa na 18 – 22 Novemba, 2013.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Uangalifu kwenye Miamala ya Kifedha,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha uchukuaji wa maamuzi juu ya maudhui ili kutoa nafasi ya utafiti wa ziada, tafiti zitakazowasilishwa ziangazie uangalifu wa taasisi za kifedha za kiislamu na taratibu mbadala za kisharia za uangalifu katika miamala ya kawaida.

Allah Ndie Mwenye Kutuafikia

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 196 (2/21)

Yanayohusiana na 'Kukamilisha Maudhui ya Sukook za Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na moja (21) kilichofanyika Riyadh, (Saudi Arabia) 15 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1435 Hijri, sawa na 18 – 22 Novemba, 2013.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kukamilisha Maudhui ya Sukook za Kiislamu,** hususan katika maudhui ya:

- Kuchelewesha malipo ya ijara ya mali yanayojulikana lakini yasiyokuwepo.
- Hukmu ya uuzaji wa sukook za ijara za baadae kabla ya kuainisha mali yatakayofungiwa mkataba.
- Vigezo vya ushindi na ufuasi na hali zake zote.

na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuchelewesha malipo ya ijara ya mali yanayojulikana lakini yasiyokuwepo:

1) Katika ijara ya ya manufaa ya mali yanayojulikana; inajuzu kutanguliza malipo, kuyagawa kwa awamu na kuchelewesha.
2) Katika ijara ya ya manufaa ya mali yanayojulikana; malipo hayastahiki ila kwa kumuwezesha mkodishwaji kunufaika na alichokodi, asiponufaika na alicholipia kodi ndani ya mda waliokubaliana basi haistahiki malipo.
3) Katika ijara ya huduma (ambapo kuna kazi inafanyika); inajuzu kutanguliza malipo, kuyagawa kwa awamu na kuchelewesha.
4) Kwa yaliyotangulia haitakiwiw ipelekee kwenye kuuza deni kwa deni, au kufaidika pasipo na kudhamini hasara, au kuuza asichomiliki

muuzaji; jambo ambalo limekatazwa kisharia.

Mbili: Hukmu ya uuzaji wa sukook za ijara za baadae kabla ya kuainisha mali yatakayofungiwa mkataba:

1) ‘Kongamano’ linakazia ‘Maamuzi’ yake namba 188 (3/20).
2) Haijuzu kuuza sukook za umiliki wa manufaa ya mali yanayojulikana lakini yasiyokuwepo kabla ya kuainisha mali yenyewe ambayo manufaa husika yatapatikana.
3) Haijuzu kuuza sukook za umiliki wa huduma zijulikanazo ambazo zitapatikana kutoka sehemu fulani (mtoa huduma) kabla ya kuainishwa mtoaji huduma, ila kwa kuzingatia vigezo vya kusarifu katika madeni, lakini akijulikana mtoaji huduma basi inajuzu kuuza sukook.
4) Haijuzu kuuza sukook ambazo zinawakilisha mali yatakayotengenezwa alafu ndio yakodishwe kwa ijara inayojulikana lakini isiyokuwepo na kabla ya utengenezaji wa mali hio.

Tatu: Mazingira ya utoaji wa sukook:

1) ‘Kongamano’ linakazia ‘Maamuzi’ yake namba 188 (3/20).
2) Iwapo sukook zinawakilisha mali ya mradi au shughuli fulani ya kiuwekezaji, panachanganyikana pesa, madeni, mali na manufaa; basi kifungu cha sita, ibara ya 3a) itatumika, kama ifuatavyo:
   a) Iwapo madeni na pesa ziko kando na mali, manufaa, chombo cha kiutawala na shughuli za kiuchumi zinazofuatwa, basi haijuzu kutoa sukook au mikoba ya uwekezaji ila ikiwa asilimali na manufaa ni yenye kughilibu.
   b) Iwapo umiliki wa wabeba sukook au mikoba ya uwekezaji umekusanya chombo cha kiutawala na shughuli za kiuchumi zinazozalisha pesa na madeni, na ikawa umiliki huo ni ‘taasisi huru ya kisharia na ya kikanuni’ basi inajuzu kwa hali hii kutoa na kuuza sukook au mikoba ya uwekezaji kwa msingi wa ufuasi.
   c) ‘Shughuli za kiuchumi’ zilizotajwa hapo juu inamaanisha kazi ambazo zinazalisha madeni na pesa kwa njia iliyo halali kisharia.
3) ‘Kongamano’ linaweka msisitizo tena juu ya ‘maamuzi yaliashiriwa, kipengele cha sita:1’ kinachosema: “‘*Maamuzi’ yanayochukuliwa na*

‘Kongamano’ yanaanza kufanya kazi pale yanapoamuliwa, na hayatoathiri mikataba iliyotangulia kufungwa kabla ya hapo ikiwemo sukook zilizotolewa kutokana na ijtihad au fatwa inayozingatiwa kisharia”.

4) Kuhusiana na vigezo vya ‘ushindi’ na ‘ufuasi’; ‘Kongamano’ linaonelea kuakhirisha utoaji wa maamuzi juu masuala hayo, lakini inausia muendelezo wa tafiti juu yake.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 197 (3/21)

Yanayohusiana na 'Uwajibikaji wa Kijinai kwa Madereva wa Vyombo Kutokana na Uendeshaji wa kasi na Kutojali'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na moja (21) kilichofanyika Riyadh, (Saudi Arabia) 15 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1435 Hijri, sawa na 18 – 22 Novemba, 2013.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Uwajibikaji wa Kijinai kwa Madereva wa Vyombo Kutokana na Uendeshaji wa kasi na Kutojali,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na kutambua umuhimu wa kuliangazia suala hili hasa baada ya ongezeko la ajali za barabarani na athari zake mbaya kwa watu na jamii nzima;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kushadidia juu ya 'Maamuzi ya Kongamano' namba 71 (2/8) kwenye kikao chake cha nane (8) kilichofanyika mji wa Bandar Siriy Bejwan, Falme ya Brunei, Darussalam 1 – 7 Mfungo Nne (Muharram), 1414, sawa na 21 – 27 Juni, 1993, kuhusiana na 'ajali za Barabarani'.

Mbili: Ni lazima kutii sheria za barabarani kwa usalama na maslahi ya wote.

Tatu: Ni haramu kwa dereva wa chombo kujihusisha na matendo ambayo aghlabu yatapelekea kujidhuru au kudhuru wengine, atawajibika kwa matendo yake hayo itokeapo dhara kwa yeyote, kwa mfano:

a) Kupita wakati taa nyekundu inawaka.
b) Kuendesha kasi ya ziada ya kuchupa mipaka.
c) Kuonyesha stadi za uendeshaji kama vile 'skidding' au kufukuzana na wengine pasipo na sababu.

d) Kuzembea kwa kutokisimamia chombo kimatengenezo au kiukarabati, au kuendesha kiholela ikasababisha madhara.

Itokeapo kua kwa ajili ya uzembe kama huu na ikasababisha ajali ya mtu ima kufa au kudhurika kimwili basi dereva huyu atawajibika kijinai kwa kosa la ima makusudi au mfanano wa makusudi au kukosea kulingana na mazingira halisi yatakayojitokeza, na hakimu atatoa hukmu muwafaka kwa kosa hilo.

Nne: ‘Kongamano’ linausia taasisi zote husika katika nchi za kiislamu kueneza elimu juu ya umuhimu wa kufuata (kutii) sheria za barabarani na athari zake mbaya za kutofanya hivyo kwa watu na jamii.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 198 (4/21)

Yanayohusiana na 'Kugeuza na Kutumia Kemikali za Kuhifadhia Chakula na Dawa'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na moja (21) kilichofanyika Riyadh, (Saudi Arabia) 15 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1435 Hijri, sawa na 18 – 22 Novemba, 2013.

Baada ya kupitia mapendekezo 'Warsha ya Fiqhi ya Tiba' iliyoandaliwa na 'Jumuia ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' Kuwait, kwa kushirikiana na 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu', na kwa ushiriki wa 'Taasisi ya al-Hassan al-Thani (II) ya Tafiti za Sayansi na Tiba' na 'Shirika la Kiislamu la Elimu-Malezi, Sayansi na Utamaduni' (ISESCO), na Ofisi ya Kanda ya 'Shirika la Afya Duniani' (WHO); juu ya 'Mtazamo wa kiislamu kwa baadhi ya matatizo ya kiafya', kuanzia tarehe 8 – 11 Swafar (Mfungo Tano), 1418 Hijria, sawa na 14 – 17 Juni, 1997, mjini Dar al-Baydhaa (Cassablanca), Morocco; na baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kugeuza na Kutumia Kemikali za Kuhifadhia Chakula na Dawa,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Ni wajibu kwa kila muislamu kufuata sharia za kiislamu, hususan katika mpango mzima wa chakula na dawa, ili kufikia uzuri wa chakula, kinywaji na dawa, huruma za Mwenyezi mungu kwa waja wake ni kua amewapesishia njia za kuifuata sharia yake kwa kuweka misingi ya dharura; kama ile: '*Dharura inahalalisha iliyoharamishwa*', '*Shida inapewa daraja ya dharura, sawa iwe shida hio ni ya binafsi au ya wengi*', '*Kila lenye manufaa ni halali ila ikiwepo dalili ya kuharamisha, kama vile kila kitu ni tahara ila ikiwepo dalili ya kuthibitisha unajisi wake*'. Ijulikane kua uharamu wa chakula au kinywaji hakumaanishi unajisi wa chakula hicho au kinywaji

hicho kisharia.

Mbili: Vitu vilivyoharamishwa au ambavyo vyenyewe ni najisi vinapochanganywa na chakula au dawa vinageuka na kua halali kwa mojawapo wa njia mbili:

1) **Kugeuza (*istihala – transmutation*):** 'Kugeuza' kwa istilahi ya kifiqhi; ni kugeuka kwa uhalisia wa kitu ambacho ni najisi au kilichoharamishwa utumiaji wake, kitu hicho kinageuka kutoka hali yake na kua hali nyingine au kitu kingine kabisa chenye jina na sifa tofauti, jambo hili kwa istilahi ya kisayansi linajulikana kua ni: '*Kila muingiliano kamili wa kikemikali (chemical reaction) kama vile kugeuza mafuta na shahamu (grisi), kutoka vyanzo mbalimbali, na kua sabuni*'. Venginevyo; ni kuchanika (kuoza) kwa dutu (material) na kua vitu vingine tofauti, kama kuyafumua mafuta na shahamu na kuyafanya yawe hamidhi (asidi) na glisirini (*glycerin*) ya mafuta. Muingiliano huu kamili wa kikemikali unaweza ukafanywa kwa makusudi kupitia taratibu za kisayansi na kiufundi, lakini pia unaweza ukafanyika bila ya kukusudiwa (kuonekana) kwa aina ambazo wanafiqihi wamezielezea; kwa mfano: ugeukaji wa siki, ngozi na kuungua, ama ikiwa muingiliano wa kikemikali sio kamili basi haitozingatiwa kua ni kugeuka, na ikiwa dutu ni najisi itabaki hivyo hivyo na haijuzu kuitumia. Kwa mujibu wa yaliyotangulia:

   a) Michanganyiko ya kikemikali ya kuongezea yenye usuli ya wanyama walioharamishwa au najisi lakini ikapatikana ugeukaji kwa msingi uliotangulia basi inazingatiwa kua ni tahara na utumiaji wake kwenye chakula na dawa ni halali.
   b) Michanganyiko ya kikemikali iliyotokana na usuli zilizo najisi au zilizoharamishwa kama vile: damu iliyomwagika ai majitaka ambayo hayakupata sifa ya kugeuka kwa namna iliyoelezewa, basi inakua haijuzu utumiaji wake kwenye chakula na dawa; mifano ya hizo ni: vyakula vinavyoongezewa damu iliyomwagika kama soseji inayojalizwa damu, uji wa damu (*Pudini nyeusi - Black Puding*), ham'baga (*blooded hamburger*) ya damu, vyakula vya watoto vilivyochanganywa na damu, unga uliokandwa kwa kutia damu,

supu yenye damu, na mifano kama hio, yote hayo inazingatiwa kua ni vyakula najisi (vichafu) haviruhusiwa kuliwa kwa kua vina damu iliyomwagiliwa ambayo haikupitia mchakato wa kugeuka kikemikali.

Kuhusu plasma (nyevunyevu) ya damu - ambayo inachukuliwa kuwa mbadala wa bei rahisi ikilinganishwa na ute wa yai - na inaweza kutumika katika mikate (*pies*), supu, soseji, ham'baga (*hamburger*), keki, biskuti, pudini, mikate, bidhaa za maziwa, dawa za watoto na chakula chao, ambazo zinaweza kuongezwa kwa unga; hivyo vyote ni halali, kwani ni tofauti na damu kwa jina na sifa, kwa maana hio; havina hukmu ya damu.

2) **Kuhusu utumiaji wake;** 'Kongamano' linaonelea kuakhirisha ili utafiti wa ziada ufanyike.

Inausiwa yafuatayo:

1) Umuhimu wa kufaidika na ngozi na mifupa ya wanyama waliochinjwa kwa kutoa dutu ya jelatini (*gelatin*) inayotumika kwenye chakula na dawa, kufanya hivyo ni kufaidi na mali ya kitaifa na kujiepusha na utata wa kutumia dutu za jelatini kutoka sehemu zisizojulikana au kukubalika kisharia.
2) Kuwataka watendaji katika nchi za kiislamu wawe makini kwenye viwanda vya dawa na vyakula kua masharti na vigezo vya kisharia vinazingatiwa katika malighafi na mchakato wa utayarishaji.
3) Watendaji wan chi za kiislamu wawalazimishe kampuni zinazozalisha au kuagiza bidhaa za vyakula vilivyohifadhiwa wabainishe kwa uwazi na kwa lugha nyepesi michanganyiko iliyotumika kwenye vyakula hivyo; taarifa hizo ziwekwe kwenye kila kifungashio.
4) Kuitaka 'Jumuia ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' Kuwait, kufuatilia kwa karibu mambo mapya yanayoibuka kwenye sanaa ya chakula na dawa, na kuandaa warsha kwa ushirikiano na 'Kongamano' kujadili mapya hayo na kubainisha hukmu ya sharia.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≈≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 199 (5/21)

Yanayohusiana na 'Kuwafananisha na watu; Mitume na Maswahaba kwenye Kazi za Sanaa'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na moja (21) kilichofanyika Riyadh, (Saudi Arabia) 15 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1435 Hijri, sawa na 18 – 22 Novemba, 2013.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kuwafananisha na watu; Mitume na Maswahaba kwenye Kazi za Sanaa,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

'Kongamano' linaonelea kuakhirisha maudhui haya hadi kwenye kikao kijacho ili kutoa nafasi ya ziada ya utafiti.

Allah Ndie Mwenye Kutuafikia

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 200 (6/21)

Yanayohusiana na 'Hukmu na Vigezo vya Kisharia vya Misingi ya Bima Shirikishi'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na moja (21) kilichofanyika Riyadh, (Saudi Arabia) 15 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1435 Hijri, sawa na 18 – 22 Novemba, 2013.

Baada ya kupitia mapendekezo ya 'Warsha ya Kielimu ya Hukmu na Vigezo vya Kisharia vya Misingi ya Bima ya Ushirikiano' iliyofanyika chini ya usimamizi wa 'Kongamano' kuanzia 20 – 21 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1434 Hijria, sawa na 30 Aprili – 1 Mei, 2013, Jeddah, warsha hii iliandaliwa kufuatia 'Maamuzi ya Baraza la Kogamano' namba 187 (2/20) yaliyopitishwa kwenye kikao cha ishirini (20) kilichofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa'da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Hukmu na Vigezo vya Kisharia vya Misingi ya Bima Shirikishi,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Bima-shirikishi ni aina ya mikataba mipya iliyojikita kwenye misingi ya kusaidiana inayodhibitiwa na vigezo vya kisharia vitokanavyo na Qur'an Tukufu na Sunnah za Bwana Mtume SAW.

Kimsingi, bima ziko aina mbili:

Ya kwanza: Bima ya kibiashara yenye lengo la kupata faida kupitia muundo wa kibima waw kupokea malipo dhidi ya kukabiliana na hatari, ama kwa upande wa uendeshaji kikampuni; inalenga kupata faida.

Ya pili: Bima isiokua ya kibiashara na isiyolenga kupata faida, lakini inakusudia kulinda maslahi ya washirika wake kwa kushirikiana kwao (malipo sawa) endapo kutatokea dhara au hatari kwa mmoja wao.

Aina hii ya pili ina majina mengi kama vile: 'Bima-shirikishi', 'Bima ya kusaidiana' (*takaful*), 'Bima ya kubadilishana' 'Bima ya kiislamu'. Zipo tofauti za kimsingi baina ya 'Bima-shirikishi' na 'Bima ya kibiashara'; zikiwemo:

1) Bima-shirikishi ya kiislamu ni kusaidiana miongoni mwa wanakundi au miongoni mwa makundi kadhaa katika jamii kupitia kushiriki kwenye kubebeana madhara na hatari inayyomfika mmoja wao pasipo na lengo la kupata faida, kwa maana hio mkataba si miongoni mwa mikataba ya mauziano, na lau kutatokea utata basi unasameheka. Kinyume chake; bima ya kibiashara ni mkataba wa mauziano kwa lengo la kutengeneza faida kwenye mauziano hayo kupitia kuhamishia hatari a kupata hasara kutoka kwa muweka (mteja wa) bima kwenda kwa kampuni ya bima, hapa hukmu za biashara zote zinafanya kazi ambapo utata (*gharar*) ni dosari kwenye mkataba huo.
2) Pande husika za bima-shirikishi ni washirika wote kwenye mfuko wa bima-shirikishi, pamoja na upande wa usimamizi (utawala – kampuni); ama bima ya kibiashara ni kampuni ya bima na wabeba hati za bima (policyholders).
3) Mfuko wa bima-shirikishi unajengeka kutokana na ada za wabeba hati za bima, faida za uwekezaji na akiba zilizokubaliwa; ama kwenye bima ya kibiashara hakuna mfuko kama huu.
4) Kampuni inayosimamia bima-shirikishi inaendesha shughuli za bima kupitia kufanya malipo ya madhara, shughuli za bbima na uwekezaji wa mali ya mfuko; ama kwenye bima ya kibiashara kampuni ndio yenye bima na inamiliki malipo ya bima yanayolipwa kwa awamu na pia kumiliki faida na ziada zipatikanazo.
5) Kiuhalisia, kwenye bima-shirikishi anebeba hati ya bima na mwenye bima ni huyohuyo mtu mmoja kwa nafasi zote mbili; lakini kwenye bima ya kibiashara ni watu wawili tofauti; kwani anaebeba hati ya

bima ni mteja wa bima na bima yenyewe inamilikiwa na kampuni ya bima.

6) Usimamizi wa bima-shirikishi sawa iwe ni jopo lililochaguliwa kutokana na washirika au iwe ni kampuni maalum au iwe ni taasisi ya umma inakua ni wakala wa kusimamia mikataba kwa niaba ya ‘mfuko wa washirika’ (wabeba hati za bima), na jopo hili au kampuni hii watakua na haki ya kupata malipo (ujira) kwa kazi yao; wakati kwenye bima ya kibiashara kampuni mhusika asilia na wanafunga mikataba kwa niaba ya kampuni yenyewe.

7) Usimamizi wa bima-shirikishi haumiliki awamu za malipo ya bima lakini awamu hizi zinamilikiwa na ‘mfuko wa washirika’ (wabeba hati za bima); lakini kampuni ya bima ya kibiashara inamiliki awamu zote za malipo dhidi ya wao kulipia gharama za baadhi ya wateja wakati wa madhara (ajali).

8) Pesa zitakazosalia na faida zake – baada ya kukata matumizi na malipo – zinabaki kua ni milki ya ‘mfuko wa washirika’ kanuni za ‘mfuko’ ndizo zitakazoamua namna ya kusarifu pesa hizo, jambo hili halip kabisa kwenye bima za kibiashara, kwa kua awamu za malipo zote ni milki ya kampuni kwa mkataba na kwa kukabidhiwa, pesa hizo zinakua ni faida ya kampuni pekee kwenye bima za kibiashara.

9) Faida zitokanao na uwekezaji wa usuli ya pesa za bima baada ya kutoa gharama za uendeshaji wa kampuni inayosimamia bima-shirikishi zinarudi kwa washirika wote wabeba hati za bima-shirikishi, ambapo faida kama hizi zinarudi kwa kampuni kwenye bima ya kibiashara.

10) Mali ya ‘mfuko’ wakati wa kufunga hesabu za ‘Mfuko wa Bima-Shirikishi’ ima yanatumiwa kwenye njia za kheir (misaada ya kibinadamu) au wanapewa washirika (kama ilivoelezewa kwenye kifungu cha kumi na tatu (13) cha misingi ya bima-shirikishi), ambapo kwenye bima ya kibiashara mali haya yanarudi kwa wanahisa wa kampuni.

11) Kampuni ya Bima-shirikishi inawajibika kufuata hukmu za sharia ya kiislamu na fatwa za bodi ya sharia, ama bima ya kibiashara ni kinyume na hayo.

12) Bima-shirikishi na bima ya kibiashara zinaongozwa na ‘kanuni za

msingi' za bima, nazo ni:

a) Msingi wa maslahi ya kibima: hii ni haki ya kikanuni kwenye bima inayotokana na uhusiano wa kifedha unaotambulika kikanuni baina ya mteja wa bima na kitu kinachokusudiwa kusimamiwa na bima.
b) Msingi wa nia njema: Ni wajibu chanya wa kujitolea kuweka wazi kikamilifu ukweli wote kuhusiana na uhatari wa kitu kinachotakiwa kuekewa bima, nisawa ziwe taarifa hizi zimeombwa au la.
c) Msingi wa sababu ya karibu na mubashara: Ni sababu kuu toshelezi ya kusababisha msururu wa ajali ambazo zitakua ni sababu ya natija itakayopatikana bila ya kuwepo kitu chochote kingine kinachoingilia na kukatisha muendelezo huo wa ajali.
d) Msingi wa fidia.
e) Msingi wa ushiriki.
f) Msingi wa ubadilishaji na haki.

Bima-shirikishi, ina misingi mingine mahsusi kwa bima hii:

a) Kujilazimisha kufuata hukmu za sharia za kiislamu katika miamala na mikataba yote.
b) Kutosimamia bima ya vitu vilivyoharamishwa.
c) Kutofungamana na mikataba aina yoyote ya riba; kupokea na kutoa.

Yafuatayo ni maelezo juu ya misingi na kanuni za bima-shirikishi ya kiislamu:

Kifungu cha (1): Ufafanuzi

Bima-shirikishi: Ni kundi la watu wanaotarajia kukabiliana na mambo hatarishi kwa mali yao, watu hawa wanashiriki kwa pamoja kulipa kiwango fulani cha pesa kila mmoja kwa 'mfuko maalum' kama njia ya kusaidiana pasipo na kutarajia kutengeneza faida kwa zoezi hili, lakini itokeapo mmoja wao amesibiwa na madhara kwa mali yake basi pesa hizo zitumike kufidia dhara hilo kwa mujibu wa makubaliano na mikataba na sheria elekezi.

Kifungu cha (2): Aina za usimamizi wa mfuko wa bima-shirikishi:

Bima-shirikishi inasimamiwa kiutawala na chombo huru chenye leseni kinachofanya kazi kwa kufuata sheria za Shari'ah ya Kiislamu, na inaweza kuchukua moja ya aina kadhaa zijulikanazo, zikiwemo:

a) Jopo lililochaguliwa la wabeba hati za bima.
b) Kampuni maalum ya usimamizi wa bima.
c) Taasisi ya Umma iliyoanzishwa ima na serikali au mkusanyiko wa nchi mbalimbali, na yaasisi hii inakua chini yao.

Kifungu cha (3): Uhusiano kati ya 'mfuko' na 'usimamizi':

Uhusiano baina ya mfuko wa bima-shirikishi na jopo la usimamizi unakua kama ifuatavyo:

a) Kuhusu usimamizi wa biashara ya bima: uhusiano ni kulingana na mkataba wa uwakala, kwa malipo au bila malipo.
b) Kuhusu uwekezaji: uhusiano unakua ima kwa mujibu wa uwakala au mkataba wa mudaraba. Katika mazingira ya mkataba wa uwakala; ima unakua kwa malipo au bila malipo. Ama kwenye mazingira ya mudaraba; basi chombo kinachosimamia kina haki ya kushiriki katika ya asilimia faida kulingana na makubaliano, wakati hasara hubebwa na mmiliki wa mtaji, isipokuwa ikiwa kuna uzembe au ukiukwaji wa masharti au uvunjaji wa kanuni.

Kifungu cha (4): Malipo kwa wasimamizi:

Malipo kwa wasimamizi yanakua kwenye hali mbili:

a) Katika hali ambapo usimamizi wa shughuli za bima-shirikishiunaenda kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wa uwakala, basi inajuzu kwa wasimamizi kupokea malipo ya kazi yao ima pesa fulani au kiwango cha asilimia watakachokubaliana kutokana na pesa za washirika.
b) Ama iwapo usimamizi wa mali za uwekezaji wa mfuko wa washirika kwa mkataba wa mudaraba, basi wasimamizi (mudarib) wana haki ya asilimia fulani ya faida, ama ikiwa uwekezaji ni kulingana na mkataba wa uwakala, basi malipo yanaweza kuwa kima fulani, au asilimia fulani ya

kiasi kilichowekezwa.

Kifungu cha (5): Umiliki wa pesa zilizochangwa na faida za uwekezaji wake:

Pesa zote zilizochangwa na washirika pamoja na faida zipatikanazo kutokana na uwekezaje wake zinakua ni za ‘mfuko wa bima-shirikishi’. Haki za wabeba hati za bima zitaainishwa kwa mujibu wa nidhamu za bima, mashrti ya kustahiki fidia na masalio ya ziada baada ya malipo yote kufanywa.

Kifungu cha (6): Hadudi-rejea za kukadiria malipo ya wasimamizi wa shughuli za bima:

Tathmini ya fidia au mshahara kwa wale wanaosimamia mchakato wa bima itakuwa kwa mujibu wa viwango-adilifu vilivyowekwa na chombo huru cha idara ya bima, kama vile: ‘Mamlaka ya Usimamizi wa Bima’, au kupitia mazungumzo kati ya wawakilishi wa mfuko, au chombo chochote kilichoundwa kwa kuzingatia maslahi yao nay ale ya wasimamizi.

Kifungu cha (7): Wajibu wa Mfuko:

Mfuko wa Ushirika utabeba hasara yoyote ya kifedha, iwe katika uwekezaji au katika shughuli za bima, ila iwapo hasara kama hizo zitatokana na ukiukwaji, au kuzembea au uvunjaji wa masharti au kanuni za chombo kinachosimamia, basi wasimamizi ndio watakaowajibika.

Kifungu cha (8): Mali-ziada ya mfuko wa bima:

Mali-ziada ya mfuko wa bima ni salio la kifedha lililobaki la jumla ya michango iliyokusanywa, mapato kwenye uwekezaji wao, na mapato mengine yoyote baada ya malipo ya fidia, malipo ya wasimamizi na akiba muhimu, na kuweka kando gharama na majukumu yote yanayotokana na mfuko. Mali-ziada haya ya mfuko wa bima yanaweza kuhifadhiwa kwa mfuko, au kugawiwa yote au baadhi yake kwa wamiliki wa hati kwa njia ambayo ni ya uadilifu na kwa mujibu wa kanuni za mfuko.

Kifungu cha (9): Upungufu (hasara) katika Mfuko wa Bima-shirikishi na hali zake:

Iwapo mfuko wa bima-shirikishi umeshindwa kulipia majukumu stahiki, kampuni inayosimamia inaweza kutumia mojawapo ya njia zifuatazo:

a) Kukopa kutoka kwa mtu (upande) wa tatu.
b) Utoaji wa *qardh hasan* (mkopo wa ukarimu) kutoka kwa chombo kinachosimamia.
c) Kuongeza kiwango cha mchango kwa idhini ya washirika.
d) Makubaliano na wanufaika wa fidia ili kupunguza kiasi cha fidia au kuwalipa kwa awamu.
e) Aidha, inajuzu kutafuta njia nyengine zinazoonekana kua ni sawa na iwapo zitakubaliwa na ‘mamlaka ya udhibiti wa kisharia’.

Kifungu cha (10): Bima-Mtawanyo (*reinsurance*):

1) Inajuzu kwa kampuni ya bima-shirikishi kufunga mikataba ya bima-mtawanyo, kwa masharti kwamba shughuli za bima-mtawanyo zinaendeshwa na zinaambatana na hukmu za Shari'ah ya Kiislamu na kanuni za msingi za bima-shirikishi kama ilivyoamuliwa na Bodi yake ya Udhibiti wa Shari'ah.
2) Kampuni za bima-shirikishi zinawajibika kuamiliana na kampuni za bima-mtawanyo za kiislamu, ikishindikana kufanya hivyo kwa sababu zinazokubalika, basi zitaruhusiwa kuamiliana na bima-mtawanyo za kawaida; zisizokua za kiislamu kwa kadri ya haja iliopo na kwa kufuata vigezo vitakavyowekwa na Bodi ya Udhibiti wa Shari'ah na vigezo vingine vinavyoonekana muwafaka, ikiwemo:

    a) Kupunguza kuamiliana na kampuni za bima-mtawanyo za kawaida kwa kiwango cha chini kabisa kwa kadri iwezekanavyo.
    b) Wasimamizi wa mfuko bima-shirikishi wasielekeze uwekezaji wao kwenye bima-mtawanyo ila kwa kadri ya inavyowafikiana na hukmu ya sharia ya kiislamu, aidha, haijuzu kudai faida ya uwekezaji kutoka kampuni hio iwapo inakhalifiana na misingi ya sharia ya kiislamu, halikadhalika hawatawajibika na hasara yoyote itakayopatikana kwenye kampuni hio.
    c) Kampuni za bima-shirikishi haziruhusiwi kulipa faida za riba kwa pesa zilizopo kwenye kampuni za bima-mtawanyo za kawaida,

wala wao hawaruhusiwi kuchukua faida za riba kwa pesa zilizopo kwenye bima-mtawanyo za kawaida, lakini inatakiwa pesa zao zihifadhiwe na kampuni za bima-shirikishi na sio kampuni za bima-mtawanyo za kawaida.

d) Mkataba na kampuni za bima-mtawanyo za kawaida, ifungwe kwa mda fupi kabisa iwezekanavyo.

Kifungu cha (11): Ulazima wa kufuata sharia ya kiislamu:

Ni wajibu kwa wasimamizi wa bima-shirikishi kufuata hukmu za sharia ya kiislamu katika shughuli zote za bima na miamala na uwekezaji.

Kifungu cha (12): Udhibiti wa Kisharia:

Ni wajibu wa kampuni ya bima-shirikishi kuunda ‘jopo la udhibiti wa kisharia’ na ‘chombo cha ukaguzi wa kisharia’ kwa mujibu wa ‘Maamuzi ya Kongamano’ namba 177 (3/19) yanayohusiana na: “*Nafasi ya Usimamizi wa Kisharia Katika Kudhibiti Shughuli za Mabenki ya Kiislamu: Umuhimu wake, Masharti yake na Namna ya Utendakazi wake*”, jopo hili linapaswa kuidhinishwa uundwaji wake na kazi zake na ‘Mamlaka Kuu ya Udhibiti wa Kisharia’; ikiwepo.

Kifungu cha (13): Ufungaji wa Hesabu za Mfuko:

Katika mazingira ya kufunga mahesabu ya mfuko wa bima-shirikishi, mali ya mfuko ima yanapelekwa kwenye taasisi za misaada au yagawiwe kwa washirika kwa misingi ya uadilifu, lakini yoye hayo iwe ni baada ya kulipa gharama zote za kiutendaji na kikanuni kwa mujibu wa sheria ya mfuko na chini ya usimamizi wa ‘Bodi Kuu ya Udhibiti wa Kisharia’, haijuzu kwa wasimamizi wa mfuko kuchukua chochote katika pesa hizo.

Kifungu cha (14): Kutatua migogoro:

Iwapo kuna mgogoro wowote baina ya ‘Kampuni ya Bima-shirikishi’ na ‘Wabeba hati za biba’, basi mgogoro huo utatuliwe kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo, ni vizuri mgogoro ukatatuliwa kwa njia ya sulhu (upatanishi) na maamuzi, lakini ikishindikana hivyo basi wafikishe kesi yao kwenye taasisi husika za kimahkama.

Kifungu cha (15): Uhusiano wa Washirika kwenye Bima-shirikishi:

Uhusiano wa Washirika kwenye Bima-shirikishi ni uhusiano wa kusaidiana baina ya watu miongoni mwao kwa kila mtu kutoa (kuchangia) kiwango fulani-ainishwa kwa lengo la kufidia au kupunguza hasara kwa mmoja wao pindi anapotokewa na janga, ni kusaidiana kwa misingi ya kusameheana na kufarijiana na kuhalalishiana haki zao miongoni mwao, kusaidiana huku hauko kwenye misingi ya kulipana au ubakhili au kutafuta faida, na kwa mazingira kama haya utata utakaojitokeza hua unasamehewa na wala hapaingii riba; pana ushahidi wa kutosha, ikiwemo:

Moja: Amri ya kusaidiana katika mambo ya kheri na uchamungu:

Hapa Anasema Allah SWT: "*Na saidianeni katika wema na uchamngu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui*".[1]

Mbili: Hadith ya kina al-Ash'ary:

Imepokewa kutoka kwa Abumusa al-Ash'ary kutoka kwa Mtume SAW, amesema: "*Kundi hili la kina al-Ash'ary (wa-Yemen) wanapokufavitani na kuacha wajane au wanapokua katika hali ngumu za kimaisha basi wanakusanya (chakula) walichonacho sehemu moja kisha wanagawiana baina yao wote sawa kwa sawa, watu hawa ni miongoni nami, na mimi ni miongoni mwao*".[2]

Katika maelezo yake al-Imam al-Nawawi RA juu ya hadith hii, anasema: "*Hadith hii inadhihirisha fadhila za kina al-Ash'ary, na fadhila za kusaidiana na kutakiana mema, na fadhila ya kuchanganya chakula pamoja watu wanapokua safarini, na fadhila ya kukikusanya chakula hicho pale kinapokua ni kichache wakiwa mjini kisha kugawiana; hapa hapakusudiwi suala la kugawiana linalojulikana kwenye vitabu vya fiqh na masharti yake na kuzuia riba na kushurutisha kufarijiana na mengineo, kalla, bali kinachokusudiwa hapa ni kile kitendo cha kuhalalashiana miongoni mwao na kufarijiana kwa kile kilichopo hata kama ni kichache*".[3]

---

[1] Surat al-Maaida: 2.
[2] *Muttafaq 'alayh* – imekubaliwa
[3] Kitabu cha Sherehe ya al-Nawawi juu ya kitabu cha Sahih Muslim: 16/62

Tatu: *Nahd* au *Munahadah* (Kushirikiana):

Imam al-Bukhari RA ameandika kwenye kitabu chake anwani ndefu akifafanua dhana ya *nahd* (kushirikiana):

> "*Mlango wa Shirka (Kushirikiana), Sura ya Kushirikiana kwenye chakula, nahd, mali, na vipi namna ya kugawa vinavyopimwa kwa mizani au kwa makisio au mafungu; kwa kua waislamu hawajaona kama kuna tatizo la kufanya nahd (kushirikiana) huyu anakula kidogo cha mwenziwe na yule nae anakula kidogo na kadhalika katika kupimiana kwa makisio wanapouziana dhahabu kwa fedha au wanapouziana aina mbili tofauti za tende*".

Anachokusudia hapa ni kile kitendo cha kundi la wasafiri wanashirikiana kwa pamoja gharama za safari na kugawiana kila mtu kima fulani. Akasema Imam Ibn-Hajar al-Asqalani kwamba:

> "*Nahd au pia hutamkwa nihd; ni kitendo cha watu kuchanga kima fulani sawia ili pesa hizo zitumike kugharamia safari yao*".

Akaendelea kufafanua kua:

> "*Aghalabu watu hushirikiana kwenye mali, chakula vikiwemo vyakula vinavyoweza kuingiwa na chembe za riba, lakini hapa inasamehewa ikiwa kwa mtindo wa nahd (kushirikiana) kwa uwepo wa dalili inayojuzisha hilo*".[1]

Kifungu cha (16): Mfuko ulio huru:

Mfuko wa Bima-shirikishi unatakiwa uwe huru unaojengeka kutokana na michango ya washirika au wengineo, ili kuhakikisha uhuru wa mfuko huu unatakiwa uwe na '*utu wa kikanuni*' au akaunti yake iwe ni tofauti kabisa na akaunti ya wasimamizi, aidha inawezekana kuasisi 'waqfu ya sarafu ya misaada' kwa misingi ya 'waqfu ya sarafu'.

Kifungu cha (17): Kujitoa kwenye mfuko:

Sheria za Bima-shirikishi zinatakiwa kuelezea taratibu za kujitoa kwa mujibu wa nidhamu, masharti na vigezo zilizoidhinishwa na 'Bodi ya

[1] Kitabu cha Fath al-Bari: 5/128.

Udhibiti', na iwe ni kwa namna ambayo haitoleta madhara kwa wengine.

Kifungu cha (18): Kuchangia kwenye Bima:

1) Inawezekana kuainisha kiwango cha kuchangia kulingana na kanuni za uhalisia (*actuarial principles*) na kwa kuzingatia misingi ya kitakwimu pamoja na kutambua uwepo wa hatari ima ya mara kwa mara au ya mara moja moja, na pia kuzingatia msingi wa uwiano baina ya kima cha kuchangia na hatari-tarajiwa, aina yake mda wake na kiwango cha bima.
2) Inashurutishwa kwa jambo linalotakiwa kulindwa na bima liwe na uwezekano wa kutukia, isitaalakiane (isifungamane) na utashi wa mchangiaji na pia isitaalakiane na yaliyoharamishwa.

Kifungu cha (19): Kuchukua Nafasi:

'Idara ya Usimamizi wa Mfuko' inachukua nafasi ya mshirika, alielipiwa fidya kutokana na madhara aliyoyapata, katika kesi zote za madai na kutaka malipo kutoka kwa aliesababisha dhara (ajali), na pesa zitakazopatikana zinaingia kwenye 'Mfuko'.

Kifungu cha (20): Kuwajibika:

Inajuzu kuweka sharti kwenye hati ya bima kua: mteja wa bima atawajibika kwa asilimia fulani ya malipo ya fidya kutokana na madhara yaliyomsibu au yale aliyosababisha.

Kifungu cha (21): Umiliki wa Malipo:

Inawezekana kwa 'Mfuko' kua mmiliki wa malipo ya michango, ikiwa hivi basi umiliki wa wabeba hati unaishia pale wanapofanya malipo, na kwa msingi huu itakua kila mmoja miongoni mwa wabeba hati wameachia umiliki wao wa pesa walizochangia, hili linatakiwa lielezewe kwa uwazi kabisa kwenye kanuni ya bima.

Inausiwa yafuatayo:

1) Hukmu hizi, misingi na masharti ziwasilishwe kwa taasisi husika zote katika nchi za kiislamu hususan zile taasisi zinazohusika na utoaji na

usimamizi wa sheria na kanuni na makampuni ya bima-shirikishi na wahusika wote wa jambo hili.

2) Kulifanyisha kazi ‘Azimio la Kongamano’ namba 177 (3/19) linalohusiana na kuzitaka nchi za kiislamu waanzishe ‘Mamlaka Kuu ya Udhibiti wa Kisharia’ itakayosimamia ‘Bodi za Kisharia’ Katika Taasisi za Kifedha za Kiislamu na Bima-shirikishi.
3) Kuanzishwe ‘Baraza la Kisharia la Kimataifa’ chini ya usimamizi wa ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’, Baraza hili liundwe na taasisi msingi za kifedha za kiislamu kama vile:

   - ‘Mamlaka ya Uhasibu na Ukaguzi wa Taasisi za Fedha za Kiislamu’ (AAOIFI) ya Bahrain.
   - Benki ya Kiislamu ya Maendeleo (IsDB).
   - ‘Baraza la Huduma za Kifedha la Kiislamu’ (IFSB), Malaysia.
   - ‘Baraza Kuu la Mabenki na Taasisi za Kifedha za Kiislamu’ (GCIBFI), Bahrain.

   Miongoni mwa majukumu ya msingi ya ‘Baraza’ ilnalopendekezwa; ni utoaji wa vigezo vya kisharia vinavyosimamia bima-shirikishi na shughuli za benki za kiislamu, na kufanya vigezo hivyo viidhinishwe na ‘Kongamano’ na kufanyiwa kazi na vyombo vya usimamizi na udhibiti kwa namna ambavyo vitatumika kama sheria zinazosimamia kazi za taasisi za kifedha za kiislamu. ‘Benki ya Kiislamu ya Maendeleo’ na ‘Sekreterieti ya Kongamano’ kuratibu utayarishaji wa mpango mzima wa kazi za Baraza hili:

4) ‘Sekreterieti ya Kongamano’ iendelee na tafiti za ziada kuhusuana na baadhi ya kadhia za Bima-shirikishi, zikiwemo:

   - Kufaidi na tajriba za kimataifa katika suala la Bima-shirikishi na kubaini ni kwa kiwango gani zinaambatana na misingi iliyopitishwa kwenye maamuzi haya.
   - Kutafiti uwezekano wa kujaalia malipo wanayolipwa wasimamizi wa mfuko wa bima yawe ima ni mshahara au asilimia fulani ya ‘masalio ya ziada’ lakini bila ya kukata kwenye michango yenyewe kulipia gharama za uendeshaji.

- Kutafiti uwezekano wa kuchanganya malipo ya wasimamizi wa mfuko, kiwango fulani kutokana na michango na asilimia fulani kutokana na ‘masalio ya ziada’ ili iwe ni kama kuwahamasisha zaidi kuendeleza ufanisi wa kazi.
- Kudurusu pande zote za ‘msingi wa kiwakfu wa bima ya kiislamu’.

Allah Ndie Mwenye Kutuafikia

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 201 (7/21)

Yanayohusiana na 'Kuchinja Baada ya Kumtia Mnyama Kisunzi kwa Miale ya Umeme: Mapya yaliyoibuka'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na moja (21) kilichofanyika Riyadh, (Saudi Arabia) 15 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1435 Hijri, sawa na 18 – 22 Novemba, 2013.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kuchinja Baada ya Kumtia Mnyama Kisunzi kwa Miale ya Umeme: Mapya yaliyoibuka,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya 'Maamuzi ya Kongamano' namba 95 (3/10) kuhusiana na kuchinja.

Mbili: Ama kuhusiana na mambo mapya yaliyoibuka 'Kongamano' linaitaka 'Sekreterieti Kuu' kuunda jopo la 'baadhi wajumbe na wataalamu wa kongamano' wakatembelee nchi zinazozalisha nyama aina hio zinazouzwa katika nchi za kiislamu; majukumu ya msingi ya jopo hili yawe ni:

1. Kuweka vigezo na taratibu muwafaka zitakazohakikisha kua uchinjaji unafanyika kwa mujibu wa vigezo vya kisharia.
2. Kuyakinisha kua uchinja ndani ya viwanda vya kuzalisha nyama unaendana na hukmu za kisharia kwa wa maamuzi-tajwa hapo juu.
3. Kuitaka 'Taasisi ya Viwango na Ubora' ya nchi za kiislamu' (SMIIC) kuhakikisha ukweli wa vyeti vinavyotolewa na taasisi husika juu ya suala hili.

Allah Ndie Mwenye Kutuafikia

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 202 (8/21)

Yanayohusiana na 'Mazungumzo (Midahalao) Baina ya Wafuasi wa Madhehebu ya Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na moja (21) kilichofanyika Riyadh, (Saudi Arabia) 15 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1435 Hijri, sawa na 18 – 22 Novemba, 2013.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Mazungumzo (Midahalao) Baina ya Wafuasi wa Madhehebu ya Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Kuweka msisitizo juu ya 'Maamuzi ya Kongamano' namba 98 (1/11) kuhusiana na 'Umoja wa Kiislamu' na 'Maamuzi' namba 152 (1/17) kuhusiana na: 'Uislamu: Umma Mmoja Madhehebu Mbalimbali ya Kiitikadi, Kifiqhi na Kielimu'.
2) Mazungumzo (midahalao) baina ya wafuasi wa madhehebu ya kiislamu, ni kubadilishana mawazo juu ya maudhui fulani miongoni wafuasi wa madhehebu ya kiislamu mbalimbali lakini ya *ta'assub* (ushabiki wa kimadhehebu) kwa lengo la kufikia ufahamu wa pamoja au wa karibu au wa kushirikiana.
3) Mazungumzo (midahalao) yanakua ni muhimu kijamii ili kuendeleza mtiririko wa maisha, ama miongoni mwa wafuasi wa dini moja basi inakua ni muhimu zaidi hasa katika ulimwengu huu uliokithiri vikundi na mijumuiko.
4) Mazungumzo (midahalao) yana adabu zake ambazo zinapaswa kutumika zikiwemo: nia njema, kumuheshimu mpinzani, kuachana na ushabiki (*ta'assub*) kujieka mbali na kutaka kujionyesha na ushindi, kuchgua mbinu bora za kukinaisha na kunakishiana kwa wema.

5) Mazungumzo-mdahalo yana misingi yake inayodhibiti uendeshaji wake na kulinda ufanisi wake, miongoni mwa misingi hio ni:

   a) Kukubaliana juu ya hadudi-rejea zilizo wazi ambazo ni usuli za dalili na ushahidi unaokubalika miongoni mwa wanazuoni (ulamaa) na kuhakikisha kua usuli hizo zinafuatwa.
   b) Kuainisha maeneo wanayokubaliana na yale wanayokhitalifiana, na kufanya yale wanayokubaliana kua ndio msingi wa kutabhithi (kutafiti) yale wanayokhitalifiana, ili kulinda uwiano wa kimaisha, na kila upande uheshimu mawazo ya upande mwengine ila iwapo hoja zitolewazo zinakinzana moja kwa moja na Qur'an na Sunna na kile kilichokubaliwa kwa pamoja (ijmaa) na umma.
   c) Eneo la mazungumzo-mdahalo liwe ni masaail (masuala) ya kiijtihadi yanayoweza kufahamika kwa namna nyingi, ama masuala yaliyo wazi yasiingizwe kwenye meza ya mdahalo ila kwa njia ya kuusiana na kukubaliana namna ya utekelezaji wake.

6) Kuukubali Mpango-kazi ulioandaliwa na 'Sekreterieti Kuu ya Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya kiislamu', ambao ni sehemu ya utekelezaji wa mpango maalum wenye mambo kumi juu ya maudhui haya, mpango ambao ulipitishwa kwenye Mkutano wa Kilele wa Dharura wa Tatu uliofanyika Makkah al-Mukarramah kwa mualiko rasmi wa '*Khadim al-Haramain al-Sharifain*' Mfalme wa Saudi Arabia tarehe 5 – 6 Dhul-Qa'ada, 1426 Hijria, sawa na 7 – 8 Disemba, 2005. Mpango-kazi huu ambao uliwasilishwa kwa 'Jumuia ya Ushirikiano ya Kiislamu' (OIC) ulikubaliwa na wanazuoni wakubwa wamadhehebu mbalimbali waliohudhuria kikao hicho cha tarehe 28 Julai, 2008 kwa mualiko wa 'Katibu Mkuu', tayari Mpango-kazi huu umeshasambazwa kwa wahusika na utendaji.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kuweka msisitizo juu ya suala zima la kuheshimu wakeze Mtume SAW; mama wa waumini (*Ummahaat al-Mu'minin*), maswahaba zake na Aali zake kutoka kwa wafuasi wa madhehebu ya kiislamu, na kutowakosea heshima au kuwakejeli au kuwatusi.

2) Kuharamisha ukufurishaji wa kundi lolote miongoni mwa makundi ya kiislamu ambao wanamuamini Allah SWT na Mtume wake SAW, na wanaamini nguzo za uislamu, na nguzo za Imani na hawakanushi jambo lililowazi katika dini.
3) Uharamu wa kumwaga damu ya waislamu bila kujali ni wa kundi gani, aidha, kuharamisha vita miongoni mwao kivyovyote.
4) Katazo la dhehebu fulani kwenda kulingania wafuasi wa dhehebu lingine; hii inaweza kupalilia fitna na kuamsha hisia za chuki na kurarua safu ya waislamu.
5) Kuyaeneza maazimio yaliyotangulia kwa nchi wanachama wote ili yafanyiwe kazi na yaingizwe kwenye mitaal ya elimu, vyombo vya habari-mawasiliano na pia kuingizwa kwenye misimamo ya kisiasa mbalimbali.
6) 'Kongaman' liandae warsha na semina kwa lengo la kuimarisha mazungumzo kati ya wafuasi wa madhehebu ya kiislamu, kuondoa vikwazo vinavyozuia, kusisitiza juu mambo-misingi na maadili pamoja, na kueneza utamaduni wa uvumilivu, ukatinakati (*wasatiya*) na ulingano.

Allah Ndie Mwenye Kutuafikia

≋≋≋

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 203 (9/21)

Yanayohusiana na 'Maumbile, Uhandisi-Maumbile na Jenomu ya Binadamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na moja (21) kilichofanyika Riyadh, (Saudi Arabia) 15 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1435 Hijri, sawa na 18 – 22 Novemba, 2013.

Baada ya kupitia mapendekezo ya '*Warsha ya Fiqhi ya Tiba*' iliyoandaliwa na 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' kwa kushirikiana na 'Jumuia ya Kiislamu ya Sayansi za Tiba' Kuwait, juu ya maudhui ya '*Maumbile, Uhandisi-Maumbile na Jenomu ya Binadamu*', na iliyofanyika Jeddah (Saudi Arabia), kuanzia 13 – 15 Rabii al-Thani (Mfungo saba), 1434 Hijria sawa na 23 – 25 Februari, 2013, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa 'Maamuzi ya Kongamano' namba 193 (8/20) yaliyopitishwa kwenye kikao cha ishirini (20) kilichofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa'da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Maumbile, Uhandisi-Maumbile na Jenomu ya Binadamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Jenomu ya Binadamu:

Kuisoma jenomu ya binadamu ambayo ni: kuchora ramani kamili ya jeni (*genetic map*) za binadamu, ni sehemu ya binadamu kujielewa mwenyewe, na kuyafichua maumbile ya Allah kwa viumbe vyake kama alivyoashiria hilo pale aliposema:

"*Tutawaonyesha Ishara zetu katika upeo wa mbali na katika nafsi zao wenyewe*

mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli",[1] na mfano wa aya kama hizi.

Kwa kua kuisoma jenomu ni njia ya kutambua baadhi ya maradhi ya kurithishana au uwezekano wa kupata maradhi hayo, basi bila shaka itakua ni nyongeza yenye thamani kwa elimu ya sayansi ya afya na tiba katika harakati za kutafuta kinga au tiba za magonjwa hayo, kwa hivyo hii itaingia kwenye hukmu ya '*Fardh al-Kifaya*' yaani faradhi ya lazima angalau atokee mmoja aifanye basi wengine watasameheka bila hivyo waislamu wote wataingia kwenye hatia na madhambi, hata hivyo utumiaji wa jenomu uzingatia hukmu zifuatazo:

1) Inajuzu kutumia jenomu ya binadamu au sehemu yake katika nyanja za kunufaisha, kwani kufanya hivyo ni kuleta maslahi yaliyohimizwa na sharia kama vile kujikinga na kujitibu dhidi ya maradhi.
2) Haijuzu kutumia jenomu ya binadamu kwa matumizi ya kudhuru kwa namna yoyote ile ambayo inapingana na sharia ya kiislamu
3) Haijuzu kufanya utafiti wowote au kutibu au kufanya ukaguzi wowote unaohusiana na (jenomu) ya mtu yeyote isipokuwa baada ya tathmini yakinifu ya hatari na faida zinazoweza kujitokeza zinazohusiana na shughuli hizi kwa kuzingatia masharti ya sharia ya kiisilamu katika suala hili.
4) Ulazima wa kuapata idhini sahihi na inayokubalika kisharia kutoka mhusika mwenewe au msimamizi wake wa kisharia ili ramani yake jenomu ifanyiwe uchambuzi na kuzingatia maslahi mtu mhusika mwenyewe.
5) Kila mtu ana haki ya kuamua mweyewe ikiwa anapendelea kujulishwa natija ya uchambuzi wa kiurathi au matokeo yake au la.
6) Natija za uchambuzi wa kijenomu zilizohifadhiwa au zinaoandaliwa kufanyiwa utafiti wa kisayansi au shughuli nyengine yoyote ni lazima zilindwe kwa usiri mkubwa, siri hio isifichuliwe ila kwenye maingira yaliyobaiishwa kwenye 'Maamui ya Kongamano' namba 79 (10/8) yanayohusiana na: '*Usiri kwenye Kazi za Udaktari*', na 'Maamuzi' namba 142 (8/15) yanayohusiana na: '*Uwajibikaji wa Daktari*'. Ni juu ya Daktari kupata rukhsa ya ya kutoa siri ya mgonjwa wake kwa

[1] Surat Fussilat: 53.

wanafamilia wake iwapo ana ugonjwa wa hatari, iwapo mgonjwa hatowafiki jambo hilo, basi ni juu ya Daktari kuendelea kumuomba na kumkinaisha akubali kwa minajili ya kulinda afya ya wengine katika familia yake.

7) Kusisitiza juu ya vigezo vya kisharia - vinavyohusiana na Jenomu ya binadamu – vilivyopendekezwa kwenye Warsha ya '*Maumbile, Uhandisi-Maumbile na Jenomu ya Binadamu* na *Tiba ya Kijeomu*' iliyoadaliwa na 'Jumuia ya Kiislamu ya Sayansi za Tiba' Kuwait, na kwa kushirikiana na 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' mwaka 1419 Hijria.
8) Haijuzi kwa mtu yeyote kubaguliwa kwa sababu ya sifa zake za urithi ikiwa lengo ni kukiuka haki zake na uhuru wake wa msingi na kudhuru heshima yake.
9) Haijuzu kufanya tafiti za kliniki zinazohusiana na jeni za binadamu au matumizi yake yoyote ambazo zinakiuka sharia za kiislamu au ambazo haziheshimu haki za binadamu zinazotambuliwa na uislamu, hasa katika uga wa biolojia, maumbile na tiba.

Matibabu ya jeni:

Inamaanisha kuhamisha sehemu ya asidi ya *nucleic* (DNA), au kuhamisha jeni yenye afya, au kubadilisha jeni yenye afya mahali pa jeni gonjwa ndani ya seli ya mgonjwa ili kuirejeshea kazi ambayo jeni hii inafanya kwa kazi inayotarajiwa kutoka kwake. Na matibabu ya jeni yanagawika kulingana na seli inayotibiwa katika aina mbili:

Aina ya kwanza: Tiba ya Jeni kwa seli za mwili:

Hizi ni seli zote za mwili; na hukmu zake zinatofautiana kulingana na madhumuni yake, ikiwa madhumuni ni tiba, basi inaruhusiwa kwa masharti; yakiwemo:

a) Isiwe inasababisha madhara makubwa zaidi ya madhara ya awali.
b) Idhihirike kiaghalabu kuwa tiba hii inafikia lengo la kuponesha au kupunguza maumivu.
c) Iwe imeshindikana kupata tiba mbadala.

d) Kuzingatiwe masharti ya uhamishaji wa viungo kwa mtoaji na mpokeaji kama ilivyobainishwa na ‘Baraza la Kongamano’ katika maamuzi yake namba: 57 (8/6). Zaidi ya hayo; utaratibu wa uhamishaji wa jeni ufanywe na wataalamu wenye uzoefu na ujuzi mzuri na uaminifu.

Kuhusu matumizi ya tiba ya jeni katika kupata sifa maalum kama umbo, haijuzu, kwa sababu inahusisha kubadilisha maumbile; jambo ambalo limekatazwa kisharia, na kwa kua kufanya hivyo pia ni upuuzi na uvunjaji wa heshima ya binadamu, pamoja na kutokuwepo kwa hitajio au dharura inayokubalika kisharia.

Aina ya pili: Matibabu ya jeni kwa seli za uzazi:

Hii ni matibabu ya jeni kwa seli za uzazi (jinsia) na hukumu yake ni kuwa inaruhusiwa kufanya uchunguzi wa jeni kwa seli za uzazi ili kujua ikiwa zina ugonjwa wa jeni au la. Ama kuhusu matibabu ya jeni kwa seli za uzazi katika hali yake ya sasa ambayo haizingatii sharia za kiislamu na hasa kutokuchanganyika kwa nasaba; basi haijuzu, kwa sababu ya hatari na madhara ya aina hii ya matibabu.

Mbili: Uhandisi wa Jeni:

1) Haijuzu kutumia uhandisi wa jeni kwa lengo la kubadilisha muundo wa jeni katika kinachoitwa ‘*kuboresha spishi ya kibinadamu*’ (*Enhancement of Human Progeny*), na kila jaribio la kuingilia jeni za kibinadamu au kuingilia uwezo wake wa kuwajibika ni haramu kisharia.
2) Kimsingi, ni halali na inajuzu kutumia uhandisi wa jeni katika mimea na wanyama; hata hivyo, rukhsa hii izingatie vigezo vifuatavyo:
    a) Matumizi haya yasisababishe madhara ya hivi sasa (haraka) au ya baadae (muda mrefu).
    b) Matumizi haya yafanywe kwa lengo sahihi lililo halali, bila kucheza-cheza au kupoteza rasilimali (israfu).
    c) Utekelezaji wake usimamiwe na wenye uzoefu na uaminifu.
3) Haijuzi kutumia uhandisi wa jeni kwa malengo yenye kudhuru.

Tatu: Ushauri wa Jenetiki (Ushauri wa Jeni):

Ushauri wa Jeni (*genetic counseling*) unalenga kutoa taarifa sahihi, matokeo yanatotarajiwa na takwimu zake. Uchukuaji wa maamuzi ufanyike baina ya wahusika na daktari anaetibu, bila ya kuwepo kwa shinikizo yoyote ya kutaka kuathiri mwelekeo fulani, maeneo muhimu ya ushauri ni kama tafuatayo:

a) Huduma za ushauri wa jenetiki kwa familia au wale wanaotarajia kuoa au kuolewa zinapaswa kuandaliwa na kutolewa na wataalamu wenye ujuzi, huku wakijenga uelewa na kuelimisha umma kwa njia mbalimbali kwa manufaa ya wote.
b) Ushauri wa jenetiki unapaswa kufanywa kulingana na kipengele cha uchunguzi wa jenetiki-kinga na matokeo yake yasipelekee kulazimisha maamuzi.
c) Matokeo ya ushauri wa jenetiki yalindwe kwa usiri kamili.
d) Kukuza ufahamu wa ushauri wa jenetiki katika taasisi za matibabu, afya, shule, vyombo vya habari, na nyumba za ibada; baada ya mafunzo ya kutosha kwa wale wanaoshughulika na hilo.
e) Katika familia ambazo zinakabiliwa na uwepo wa ugonjwa wa kurithi kwa baadhi ya wanafamilia, wanapaswa kushauriana na madaktari ili kujua uwezekano wa kuenea kwa ugonjwa juo.

Hukmu za tiba ya jenetiki:

Hukmu za tiba ya jenetiki zinatofautiana kwa namna ifuatayo:

a) **Hukmu ya ‘ukaguzi wa jenetiki-kinga’:** Inajuzu kufanya ukaguzi wa aina hii lakini kwa sharti ya kua njia zinazotumiwa ziwe ni halali na salama na hazidhuru binadamu. Ili kufikia lengo la kuzuia madhara kwa umma, mamlaka ya kitaifa yenye uwezo yana haki ya kuwalazimisha raia kutumia njia hizi iwapo kuna ugonjwa ulioenea sehemu (mji) fulani, kuna ugonjwa wa mlipuko unaoenea nchini au iwapo nchi imeathirika na mionzi au miale ya sumu inayoathiri jeni. Walakin, matokeo ya ukaguzi huo yanapaswa kubaki kuwa siri ili kulinda faragha ya masuala ya kibinafsi na kudumisha heshima ya binadamu, kama inavyosisitizwa katika makusudio makuu na misingi

ya shari'a ya kiislamu.

b) **Hukmu ya ukaguzi wa jenetiki kabla ya ndoa**: Inaruhusiwa kufanya ukaguzi wa jenetiki kabla ya ndoa, kwani husaidia kufikia malengo ya Shari'a ya kiislamu ya kulinda familia dhidi ya magonjwa ya jenetiki, ikiwa njia iliyotumika ni halali na salama. Mamlaka yenye uwezo yanaweza kulazimisha jambo hili kwa ajili ya kulinda maslahi ya umma yanayotambulika kisharia.

c) **Hukmu ya ukaguzi wa jenetiki kabla ya kupandikiza tone la manii:** Inaruhusiwa kufanya ukaguzi wa jenetiki kabla ya kupandikiza tone la manii, baada ya kuyarutubisha nje ya ufuko wa uzazi (vitro fertilization), kwa sharti kwamba hatua za tahadhari zinachukuliwa kuhakikisha kutokuwepo mchanganyiko wa sampuli na kuzilinda.

d) **Hukmu ya ukaguzi wa jenetiki kipindi cha mimba:** Ukaguzi huu una njia kadhaa za kimatibabu, na zinaweza kufanywa katika nyakati tofauti za mimba; mwanzoni, katikati na mwishoni, ikithibitika kua kuna ugonjwa wa kijenetiki basi inajuzu kwa mwanamke kuitoa mimba, hii ni kwa mujibu wa ‘Maamuzi ya Kongamano’ namba 56 (6/7) yanayohusiana na ‘utoaji mimba’.

e) **Hukmu ya ukaguzi baada kuzaa:** Ni wajibu kufanya ukaguzi wa kijenetiki kwa watoto wapya wanaozaliwa ili kuweza kuingilia mapema hali ambazo zinawezekana kutibika.

Inausiwa yafuatayo:

1) Uhamasishaji juu magonjwa ya kijenetiki na jitihada za kupunguza kuenea kwake.
2) Kuhamasisha upimaji wa kijenetiki kabla ya ndoa, kwa kueneza ufahamu kupitia vyombo vya habari mbalimbali, semina, na nyumba za ibada.
3) Kuzitaka mamlaka za afya za kitaifa kuongeza idadi ya vitengo vya jenetiki ya binadamu ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za washauri wa jenetiki na kupanua wigo wa huduma za afya katika eneo la uchunguzi na matibabu ya jenetiki ili kuimarisha afya ya

uzazi.

4) Kuitaka ‘Jumuia ya Kiislamu ya Sayansi za Tiba (IOMS) na taasisi nyinginezo maalum kufuatilia maendeleo mapya katika eneo la uhandisi wa jenetiki.
5) Kuzitaka nchi za kiislamu kujihusisha zaidi katika uhandisi wa kijenetiki kwenye nyanja zake mablimbali na utekelezaji wake unaokubalika kisharia. Wafanye hivyo kupitia:

   - Kuanzisha vituo vya utafiti katika eneo hili kwa mujibu wa misingi na hukmu za sharia ya kiislamu na kuwe na uwiano baina yake.
   - Kuandaa nguvu-kazi na rasilimali-watu kufanya kazi kwenye vituo hivi.
   - Kuingiza taaluma hii kwenye mitaala ya kielimu.
   - Kuiwepesisha ufahamu wake kwa umma kupitia vyombo vya habari mbalimbali.

6) Nchi za kiislamu zisimamie utoaji wa huduma kwa raia wake wanaozihitaji huduma hizo, hii ni kwa sababu huduma hizo ni ghali sana.
7) Kampuni zinazozalisha bidhaa zitokanazo na chimbuko la wanyama au mimea zinapaswa kubainisha wazi ikiwa bidhaa zao zinazalishwa kwa kutumia njia za uhandisi wa jeni au la ili kuwawezesha watumiaji kufanya maamuzi yao ya kununua bidhaa hizo au la kwa msingi wa taarifa hizo.
8) Kuzitaka nchi za kiislamu kutunga sheria na kanuni stahiki za kuwalinda raia wao dhidi ya kutumiwa kama sampuli za majaribio.
9) Kuziwezesha taasisi za kulinda wanunzi na watumiaji (consumers) na kuwahamasisha katika nchi za kiislamu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 204 (10/21)

Yanayohusiana na 'Waislamu Kupigana Vita Wao kwa Wao kwa Jina la Jihad'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na moja (21) kilichofanyika Riyadh, (Saudi Arabia) 15 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1435 Hijri, sawa na 18 – 22 Novemba, 2013.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Waislamu Kupigana Vita Wao kwa Wao kwa Jina la Jihad,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha utoaji wa maamuzi hadi kikao kijacho ili kutoa nafasi ya ziada ya utafiti.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Tamko la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’

Kuhusiana na:

‘Yanayojiri Katika Baadhi ya Nchi za Kiarabu na za Kiislamu’

Bismillah al-Rahman al-Raheem

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), katika kikao chake cha ishirini na moja (21) kilichofanyika Riyadh, (Saudi Arabia) 15 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1435 Hijri, sawa na 18 – 22 Novemba, 2013; kwa nafasi yake kama taasisi-rejea ya Umma kwa mas’ala ya Fiqh, na kwa kutambua uwajibikaji wake na kutekeleza jukumu lake kwa umma dhidi ya changamoto na mambo hatarishi wanayopitia; hususan yale yanayoendelea katika baadhi ya nchi za kiarabu na za kiislamu;

likiwa linafuatilia matukio yanayojiri katika sehemu nyingi za nchi za kiarabu na kiislamu yakiwemo; vita, migogoro, fitna na machafuko yanayokaribia kuuangamiza umma na kutishia uwepo wake, umoja wake, mshikamano wake, usalama wake na uchumi wake na hivyo kupelekea umma kuingia kwenye giza la dhulma, njaa, khofu, mtafaruku, kudhoofika kwa serikali na kuitikisa nchi na kuyumbisha usalama wake.

Kuambatana na kuwajibika mbele ya Umma wa Kiislamu, na kwa mujibu ‘Maamuzi na Maazimio Mbalimbali ya Kongamano’ hususan ‘Maamuzi’ ya kikao cha ishirini (20) kilichofanyika Wohran, (Algeria) 25 Shawal (Mfungo Mosi - 2 Dhul Qa’da (Mfungo Pili), 1433, sawa na 13 – 18 Septemba, 2012, kuhusiana na ‘Kadhia ya Syria’; tunapenda kuelekeza mwito wetu kwa umma mzima na viongozi wao, ‘*ulamaa*’ (wanazuoni) wao na watawala wao hususan katika zile nchi na jamii zilizokumbwa na fitna hizi na machafuko haya kwamba:

Moja: Kuweka msisitizo juu uharamu wa kumwaga damu ya muislamu, na

ulazima wa kulinda heshima ya muislamu na kutokua na ujasiri wa kudhulumu watu, kwa mujibu wa maelekezo yake Allah pale aliposema: *"…Kwa sababu ya hayo tuliwaandikia Wana wa Israili ya kwamba aliye muuwa mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewauwa watu wote, na ikiwa mtu yeyote ameokoa maisha, itakuwa ni kana kwamba ameokoa maisha ya watu wote …*" (Surat al-Maida: 32), na kwa neno la Bwana Mtume Muhammad SAW aliposema: "*Ni haramu kwa muislamu juu ya muislamu mwenzie damu yake, mali yake na heshima yake*". (Imepokewa na Imam Bukhari na Imam Muslim).

Mbili: Kuweka msisitizo juu suala la 'umoja wa umma wa kiislamu' na usalama wa nchi zao, na kutoruhusiwa kusaidia au kuchangia kwenye kupasua umoja wa nchi hizi na jamii zao, aidha, kuweka msisitizo juu 'umoja wa kitaifa' ambao ndio ngao ya mshikamano wa nchi unaozuia mgogoro wa ndani.

Tatu: Ulazima wa kuinua viwango vya ufahamu kwa tabaka zote za jamii za nchi a kiarabu na za kiislamu ili kuwanyima maadui wa umma fursa na kuifelisha mipango yao ya kuugawa umma na kuushughulisha na mambo madogo madogo dhidi ya kadhia kuu za umma.

Nne: Kuweka msisitizo juu kutumia mbinu za *hiwar* (mazungumzo) kama ilivyobainishwa kwenye 'Maamuzi' namba 152 (1/17) kama njia ya kutatua tofauti na migogoro ya kisiasa na kujenga mahusiano baina ya watawala na raia na vyama mbalimali, na katu kutotumia mabavu na nguvu za silaha miongoni mwa ndugu wa nchi moja na kujieka mbali kabisa na *ta'assub* (ushabiki), umadhehebu na uchama.

Tano: Kuweka msisitizo juu haki ya raia kupata insafu, uadilifu, kutakwa ushauri, kushirikiana na kupata maisha yenye heshima miongoni mwa tabaka zote ili kuhakikisha upatikanaji wa malengo makuu ya umma.

Sita: Wajibu wa kusimama na raia wanyonge wanaopitia madhila, dhulma, vita, vurugu na ukosefu wa amani; kwani waumini (waislamu) wote ni ndugu moja kama alivyosema Allah SWT: "*Hakika ya waumini (waislamu) wote ni ndugu*" (Surat al-Hujurat: 10).

Saba: Kuweka msisitizo juu haki ya raia kua na uhuru na kuondosha *munkar* (maovu) na kuamrisha mema kwa njia (mbinu) za amani zilizodhibitiwa kwa vigezo vya kisharia.

‘Kongamano’ linawataka umma wote; viongozi, raia, makundi ya kisiasa, wasomi, wanazuoni na wanafikra, wote wasimame safu moja katika kuepusha majanga yanayowakabili umma huu, ili nchi zao zifanikiwe kwenye majukumu waliyobeba kwa umma. Aidha, kwa kua ‘Kongamano’ ni ‘Taasisi ya Kimataifa’ iliyotokana na: ‘Jumuia ya Nchi za Kiislamu’ (OIC); linawataka viongozi wa nchi zote za kiislamu wawe na ushirikiano katika kuziba mipasuko na kuongeza juhudi katika kuondoa dhulma na kuleta amani katika jamii zao ambazo zimeikosa hio amani.

Tunamuomba Allah SWT auhifadhi umma wetu na kila baya, na awafungulie milango ya uongofu.

Allah Ndie Mwenye Kutuafikia

≅≅≅

Tamko la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’

Kuhusiana na:

‘Yanayojiri Katika Mji Mtukufu wa al-Quds na Masjid al-Aqsa al-Mubarak Chini ya Uadui na Uvamizi wa Kiyahudi (Israeli)’

Bismillah al-Rahman al-Raheem

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), katika kikao chake cha ishirini na moja (21) kilichofanyika Riyadh, (Saudi Arabia) 15 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1435 Hijri, sawa na 18 – 22 Novemba, 2013; kwa nafasi yake kama taasisi-rejea ya Umma kwa mas’ala ya Fiqh, na kwa kutambua uwajibikaji wake na kutekeleza jukumu lake kwa umma dhidi ya changamoto na mambo hatarishi wanayopitia; hususana yale yanayoendelea katika Mji Mtukufu wa al-Quds na Masjid al-Aqsa al-Mubarak Chini ya Uadui na Uvamizi wa Kiyahudi (Israeli); ‘Kongamano’ linasisitiza yafuatayo:

Moja: Masjid al-Aqsa ni kitulizo cha nyoyo za waislamu na ni kito kinachopamba paji la uso la mji wa al-Quds na Palestina, ni *Qibla* cha kwanza kati ya vibla viwili (mwelekeo wa sala ya waislamu) na cha tatu kati ya misikiti mitatu mitukufu ambayo; yaani al-Aqsa, na Masjid al-Haram wa Makkah na Masjid al-Nabawi wa Madina; misikiti mitatu ambayo haifungiwi safari kwa lengo la kusali (ibada) isipokuwa hio. Aidha, Masjid al-Aqsa ndipo ilipokua safari ya Mtume SAW ya kimiujiza ya *Israa* na *Mi’raaj* kuelekea mbinguni kama ilivyosimuliwa kwenye Qur’an pale Allah SWT aliposema: “*SUBHANA, Ametakasika aliye mchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao tumevibariki vilivyo uzunguka, ili tumuonyeshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona*” (Surat al-Israa: 1). Ni wazi kwa aya hii mafungamano ya kudumu (milele) baina ya misikiti miwili hii; Msikiti Mtukufu wa Makkah na Msikiti Mtukufu wa al-Aqsa, jambo ambalo linawalazimu waislamu kushikamana nayo.

Mbili: Msikiti Mtukufu huu wa al-Aqsa pamoja na Mji Mtukufu wa al-Quds hivi sasa inapitia uvamizi wa mda mrefu na Dola ya Kivamizi ya Wazayuni (Israeli) wanaoendelea kwa bidii sana kuuyahudisha mji huu na kuzidi kuukalia pamoja na msikiti wake kupitia matendo yao ya kiuadui, unyakuzi wa ardhi, uvunjaji wa nyumba za wapalestina (wakaazi wa al-Quds) na machimbo wanayoyaendeleza chini ya msikiti wa al-Aqsa yaliyofikia misingi ya msikiti chini kwa chini; jambo ambalo linahatarisha kuporomoka kwa msikiti wenyewe na kuchafua athari za kiislamu mbalimbali, sambamba na hayo wanaendelea kujenga mahekalu ya kiyahudi katika mji huu mtukufu ambapo walowezi wa kiyahudi huyatumia mahekalu hayo kama sehemu ya kuanzia uvamizi wao wa mara kwa mara dhidi ya msikiti wa al-Aqsa na wakaazi wa al-Quds. Hivi sasa mayahudi wamefikia kuugawa msikiti kiwakati na kimahali baina ya waislamu na mayahudi kupitia taarifa rasmi zinazotolewa na viongozi na kuandaa mswada wa kanuni utakaopelekwa bungeni kwao; ikiwa ni hatua-palilizi ya kujenga hekalu lao linalodaiwa juu ya msikiti wa al-Aqsa.

Tatu: Kutambua matukio hatarishi kwa al-Quds na Masjid al-Aqsa na matakatifu mengine ya mji huu; ‘Kongamano’ linawataka waislamu wote kupitia serikali zao na raia kusimama kidete na kupambana na mambo haya hatarishi na kufanya liwezekanalo kuyaepusha maeneo haya na hatari hizi kupitia mchakato wa kisiasa na wa kikanuni katika mikao (majukwaa) ya kikanda na ya kimataifa, hali kadhalika kuwasaidia wakaazi wa al-Quds kwa hali na mali ili kuwaimaarisha kwenye mapambano yao katika nyanja zote za kimaisha zikiwemo; nyanja za kiafya, kielimu, kijamii na kiuchumi, hususan katiak sekta makaazi (nyumba) na kuzitaka serikali za kiarabu kutimiza ahadi zao za kifedha walizochukua kwenye vikao vya ‘Muungano wa Nchi za Kiarabu’ (Arab League), na wafanye hivyo kwa haraka ili kuwapunguzia wakaazi wa al-Quds badhi ya masaibu wanayopitia.

Nne: ‘Kongamano’ linathamini juhudi kubwa zinazochukuliwa na wakaazi wa al-Quds katika kuulinda Masjid al-Aqsa dhidi ya hujma za mara kwa mara zinazolenga kuchafua hadhi na heshima ya msikiti huo. Aidha, ‘Kongamano’ linapenda kutoa shukran za dhati kwa nchi wanachama wa

OIC na nchi wanachama wa '*Arab League*' na 'Kamati ya al-Quds' kwa kazi wanazozifanya za kuyalinda matakatifu ya al-Quds.

Kwa aina ya kipekee, 'Kongamano' linatanguliza shukrani kwa Falme ya Saudi Arabia kwa juhudi zao kubwa na katika kusaidia kadhia ya Palestina kiujumla, lakini kwa tahasusi misaada yao kwa Mji wa al-Quds na Masjid al-Aqsa, aidha, tunathamini msimamo wao wa kukataa nafasi katika 'Baraza la Usalama' (Security Council) la Umoja wa Mataifa kama njia ya kudhihirisha unafiki wa kimataifa juu ya kadhia hii ya haki ya Palestina, Mji wa al-Quds na Masjid al-Aqsa, hatua hii ni muhimu katika kuashiria mabadiliko kwenye 'Baraza la Usalama wa Kimataifa'.

Shukrani za dhati ziwafikie Falme ya Urdun (Jordan); kuanzia mfalme mwenyewe na serikali yake na raia wake kwa kazi wanayoifanya ya usimamizi, utunzaji na usaidizi wa 'Matakatifu ya Kiislamu ya Mji wa al-Quds'.

Kuhitimisha; 'Kongamano' linapenda kuwasilisha shukrani kwa taasisi, jumuia, kamati na makundi mbalimbali yanayofanya kazi za kusaidia Mji Mtukufu na wakaazi wake kwenye mapambano yao hadi pale uvamizi huu utakapokomolewa: "*Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu humsaidia (humnusuru) yule anaye msaidia (anaemnusuru) Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mtukufu*".[1]

[1] Surat al-Hajj: 40.

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Ishirini na Mbili (22) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Dola ya Kuwait

2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri

sawa na 22 – 25 Machi, 2015

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 205 (1/22)

Yanayohusiana na 'Shura na Demokrasia kwa Mtazamo wa Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na mbili (22) kilichofanyika Dola ya Kuwait 2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri, sawa na 22 – 25 Machi, 2015.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Shura na Demokrasia kwa Mtazamo wa Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) 'Shura' ni mojawapo ya misingi ya maisha ya kiislamu, aidha, ni mojawapo ya misingi ya utawala katika uislamu kama alivyoelekeza Allah SWT pale aliposema: *"…na mambo yao yakawa ni kwa kushauriana baina yao*" (Surat al-Shura: 38), aidha akamwambia Mtume wake, ambae analindwa na kukosea kwa *wahy*: *"… na shauriana nao katika mambo. Na ukisha kata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao mtegemea*" (Surat Aal Imran: 159). Mtume SAW, kwa vitendo, alitekeleza agizo hilo la Allah SWT kama anavyosimulia Swahaba mtukufu Abuhuraira RA: "*Sijaona mtu anaechukua ushauri kwa wingi kutoka kwa watu (maswahaba) wake kama Mtume SAW*".
2) Hakuna katazo la kisharia la kufaidi kutokana na utaratibu wa mfumo wa demokrasia katika yale yanayoleta maslahi kwa watu na jamii lakini baada ya kuutenganisha mfumo huo na misingi yake ya kifalsafa inayokazia kwenye utawala wa watu bila ya vidhibiti (vigezo) vya sharia ya kiislamu kwa namna inavyotumika katika jamii zisizokua za kiislamu. Utumiaji wa taratibu za kidemokrasia ni lazima uendane na vidhibiti vya kisharia, na kila nchi ya kiislamu itizame wapi wanaweza kufaidi kutokana na mfumo huo kwa kuzingatia zaidi kipengele cha

maslahi ya jamii ambayo yanakubalika katika hukmu za sharia ya kiislamu.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kujihusisha zaidi katika uhamasishaji wa utamaduni wa shura katika uislamu kwa kuitolea elimu na kuitekeleza kupitia mihadhara, semina, mitaala ya elimu, vyombo vya habari-mawasiliano na mawasiliano ya kisasa.
2) Wenye tahasusi hii wajihusishe zaidi na kufanya tafiti za ni jinsi gani msingi huu wa shura unaweza kutekelezeka katika mazingira ya zama hizi pamoja na kuzingatia vigezo vya kisharia kwa hilo.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 206 (2/22)

Yanayohusiana na 'Masuali ya Taasisi ya Viwango na Ubora ya Nchi za Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na mbili (22) kilichofanyika Dola ya Kuwait 2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri, sawa na 22 – 25 Machi, 2015.

Baada ya kupitia **Masuali ya Taasisi ya Viwango na Ubora ya Nchi za Kiislamu** yaliyowasilishwa kwenye 'Kongamano' na majawabu yaliyoandaliwa na 'warsha maalum' kwa kazi hio na baada ya kuyajadili majawabu hayo haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kwa kua kuna maoni mbalimbali ya kifiqhi na yanayotofautiana juu ya majawabu hayo, na maoni yaliyotolewa na wajumbe wa 'Kongamano'; imeamuliwa kua 'Sekreterieti Kuu' iandae majawabu ya masuali hayo kwa mujibu wa majadiliano alafu yawasilishwe tena kwenye 'Kikao cha Kongamano'.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 207 (3/22)

Yanayohusiana na 'Jihad ya Kushambulia na Jihad ya Kujilinda'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na mbili (22) kilichofanyika Dola ya Kuwait 2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri, sawa na 22 – 25 Machi, 2015.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Jihad ya Kushambulia na Jihad ya Kujilinda,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na baada ya kuhudhurisha dhana halisi ya jihad na malengo yake, na kwamba kimsingi, uhusiano wa Umma wa Kiislamu na wasiokua waislamu ni: 'amani', na kwamba sababu ya vita (vya jihad) katika uislamu ni uadui (uvamizi) na sio kutofautiana katika imani (dini), na kwa kuzingatia mapya yanayojiri kwenye nyanja za da'wa (ulinganizi) na mabadiliko ya mbinu za mawasiliano miongoni mwa binadamu katika nchi mbalimbali;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) **Maana ya Jihad kiujumla:** Ni juhudi yoyote inayokubalika kisharia ya kutaka kuliunua 'Neno' la Allah na kufikisha ujumbe wa uislamu kwa njia zozote za hali na mali, na kueneza uadilifu, amani na huruma kwa jamii zote za kibinadamu.

2) **Jihad ni aina mbili:**

   a) **Jihad ya Kutaka (Kushambulia):** Hii ni jihad inayolenga kulinda uhuru wa kusambaza dini na kuondosha vikwazo vyovyote mbele yake, aidha, inalenga kuwalinda wanyonge na wanaodhulumiwa katika sehemu mbalimbali kwa kufuata vigezo na vidhibiti vya kisharia vilivyoainishwa na *fuqahaa* (wanafiqihi) kuhakikisha upatikanaji wa maslahi na uepushwaji wa *mafsada* (madhara), kama alivyosema Allah SWT: "*Na piganeni nao mpaka pasiwepo fitina,*

na Dini iwe ya Mwenyezi Mungu tu. Na kama wakiacha basi usiweko uadui ila kwa wenye kudhulumu" (Surat al-Baqara: 193), akasema tena: "*Na mna nini msipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu na ya wale wanao onewa, wanaume na wanawake na watoto, ambao husema: Mola Mlezi wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhaalimu*".[1]

Kusudio kuu la jihad ya kutaka (kushambulia) ni kufikisha ujumbe (risala) wa uislamu, lakini bila ya kutenza nguvu (kuwalazimisha) watu kama alivyosema Allah SWT: "*Hapana kulazimisha katika Dini*",[2] akasema tena: "*Na hapana juu ya Mtume ila kufikisha Ujumbe wazi wazi*",[3] na pia akasema: "*Si juu yako ila kufikisha Ujumbe tu*".[4] Aina hii ya jihad, na kwa mazingira ya zama hizi za sasa; ni juu ya walinganiaji (*Du'at*) leo kufaidi na mikataba na miafaka ya kimataifa ambayo imeifanya dunia kua ni sehemu ya maridhiano ambapo watu wanaruhusiwa kutembelea nchi mbalimbali na kua na uhuru wa kufikisha ujumbe (*Da'wa*) kwa kutumia mbinu za kisasa mbalimbali zikiwemo vyombo vya mawasiliano ya kisasa (kulingania) na kufikisha risala ya uislamu kupitia lugha mbalimbali kwa jamii mbalimbali.

'Kongamano' linapenda kusisitiza hapa juu ya mambo-msingi yaliyowahi kuamuliwa na kupendekezwa kuhusiana na: ulazima wa kuandaa maandalizi kabambe na kuyapa nguvu majeshi ya ulimwengu wa kiislamu kwa kuyawezesha kisilaha na kuwamilikisha zana za kuwawezesha kulinda umma.

b) **Jihad ya kujilinda:** Hii ni jihad ya faradhi (lazima) iliyolazimishwa na sharia, nayo ni pale panapokua na uvamizi au uadui dhidi ya umma au jamii au dini au nchi au raia, ulazima wa jihad hii utaondoka tu pale zinapoondoka sababu zake kama vile kukomeshwa kwa uadui au uvamizi au anapotoka adui na kuiacha nchi ya kiislamu aliyoivamia, kama alivyosema allah SWT: "*Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanao kupigeni, wala*

[1] Surat al-Nisaa: 75.
[2] Surat al-Baqara: 256.
[3] Surat al-Noor: 54.
[4] Surat al-Shura: 48.

msianze uadui. Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi waanzao uadui".[1]

Inausiwa yafuatayo:

1) Kuhamasisha uanzishwaji wa 'Mahkama ya Kiislamu ya Uadilifu' (*Islamic Court of Justice*) itakayosimamia usuluhishaji wa migogoro miongoni mwa nchi na jamii za kiislamu, na kuyawezesha maamuzi yake kupitia kikosi maalum cha pamoja kitakachoundwa na nchi za kiislamu.
1) Kuweka msisitizo juu ya 'Maamuzi ya Kongamano' ya kikao cha saba; namba 68 (6/7) yaliyohusiana na 'Kuandaa Mswada wa Haki za Kimataifa katika Uislamu', na 'Maamuzi' namba 128 (2/14) yaliyohusiana na 'Uandaaji wa saiklopidia ya kiislamu juu ya kanuni ya kimataifa ya kibinadamu'.
2) Kukalifisha jopo la Ulamaa na Wataalamu ili waandae mitaala na mikarara ya masomo itakayolenga kubainisha mafundisho ya uislamu katika nyanja za mahusiano ya kimataifa nyakati za amani na nyakati za vita, mitaala hio isikose kuashiria mapya yaliyoibuka katika nyanja hizi lakini pia kukazia misingi na usuli ya uislamu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

[1] Surat al-Baqara: 190.

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 208 (4/22)

Yanayohusiana na 'Kumkufurisha Muislamu: Sababu zake, Athari zake na Suluhisho lake'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na mbili (22) kilichofanyika Dola ya Kuwait 2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri, sawa na 22 – 25 Machi, 2015.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kumkufurisha Muislamu: Sababu zake, Athari zake na Suluhisho lake,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na kwa kutizama ujasiri uliodhihiri zama hizi za baadhi ya waislamu kuharakisha kuwakufurisha waislamu wenzao kwa kuwarushia 'hukmu ya *ridda*' (kuwaritadisha), watu, jamii, nchi na serikali pasipo na kuzingatia misingi, vigezo na makusudio makuu ya sharia, na kwa kua jambo hili ni hatarishi kutokana na athari zake ambazo zinafikia watu (waislamu) kuuana, kubomoa nchi zao na kufurusha raia kutoka miji na majumba yao. Baada ya kujikumbusha mafundisho ya sharia ya kiislamu na tahadhari ambazo zinaweza kulinda umma na jamii za kiislamu dhidi ya janga hili la ukufurishaji;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya 'Maamuzi ya Kongamano' namba 152 (1/17) ya kikao cha kumi na saba (17) yaliyohusiana na 'Uislamu: Umma Mmoja Madhehebu Mbalimbali ya Kiitikadi, Kifiqhi na Kielimu' na yaliyojikita kwenye dhana ya kua 'Kutojuzu kukufurisha kundi lolote la waislamu wanaomuamini Allah SWT na Mtume wake SAW, na kuamini nguzo za imani na nguzo za uislamu, na hawakanushi mambo ya msingi ya kiislamu yanayojulikana'.

Mbili: Kuweka msisitizo juu ya 'Maamuzi ya Kongamano' namba 175

(1/19) yaliyohusiana na ‘Uhuru wa Kidini (Kuabudu) Katika Sharia ya Kiislamu: Upeo wake na Vigezo vyake’, na yaliyojikita kwenye: ‘Utoaji wa fatwa ya kuritadisha au kukufurisha; wahusika wake ni wanazuoni wanaokubalika, na mahkama ya kadhi inatakiwa kutekeleza agizo la wanafiqihi na kuondosha utata wowote uliopo’. Aidha, linatahadharisha dhidi ya ubaya wa kubambikiza tuhma ya ‘*takfir*’ (ukufurishaji) kwa kundi miongoni mwa makundi ya kiislamu au kukufurisha baadhi ya maswahaba na wakeze Mtume SAW au kudogosha nafasi zao na heshima zao.

Inausiwa yafuatayo:

‘Sekreterieti ya Kongamano’ ikamilishe utekelezaji wa mapendekezo yaliyatangulia kuusiwa na ‘Kongamano’ yaliyotaka kuandaliwe ‘Semina na vikao’ kuangazia zaidi maudhui yafuatayo:

a) Mas’ala ya walaa na baraa (kuungana na kujivua).
b) Hadith ya al-Firqat al-Naajiyah (kundi lililookoka), na natija ya ufahamu wa hadithi hii.
c) Ukufurishaji kwa kutotekeleza kikamilifu hukmu za sharia kiujumla.

Aidha, ‘Kongamano’ linapenda kuwausia wafuatao:

1) Vijana (*Mashabab*) wa umma; na kuwatahadharisha dhidi ya kuwafuata watu wenye fikra potofu zilizopinda na watu wa *ghuluw* (waliochupa mipaka), na badala yake linawaelekezaa kunako ilimu sahihi yenye manufaa na inayoambatana na manhaj ya *wasatiy*a (katinakati), na kuiga yale yaliopokewa kutoka kwa salaf (wema waliotangulia) wa umma huu wakiwemo maswahaba na tabiun na tabi-tabiun na waliowafuata wao kwa wema.
2) Linausia wanazuoni wa umma na walinganiaji (*Du’at*) kua na mawasiliano mazuri na vijana na kusimamia majukumu yao ya *Da’wah* ipasavyo, na kuamrisha mema na kukataza maovu kwa mujibu wa manhaj ya *wasatiy*a (katinakati).
3) Aidha, linaziusia serikali na nchi za kiislamu kurahisisha njia na kuondoa vikwazo vya mawasiliano mazuri na vijana na kuwaelekeza njia sahihi kupitia wanazuoni wa umma na viongozi wa fikra mahiri.
4) Kufaidi kutokana na tajriba zilizofanikiwa katika baadhi ya nchi katika

kujadiliana kimazungumzo na wenye fikra potofu, kwa mfano tajriba ya ‘Kunasihiana’ iliyotumika Saudi Arabia.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 209 (5/22)

Yanayohusiana na 'Haki na Wajibu wa Raia Wasiokua Waislamu Katika Nchi za Kiislamu, na Kiwango cha Utekelezaji wa Sharia ya Kiislamu Juu Yao'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na mbili (22) kilichofanyika Dola ya Kuwait 2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri, sawa na 22 – 25 Machi, 2015.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Haki na Wajibu wa Raia Wasiokua Waislamu Katika Nchi za Kiislamu, na Kiwango cha Utekelezaji wa Sharia ya Kiislamu Juu Yao,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Sharia ya Kiislamu inalinda haki za raia wasiokua waislamu waishio katika nchi za kiislamu kwa pamoja na kwa kila mmoja kama ambavyo inalinda haki hizo kwa waislamu, haki zao ni sawa na zile za waislamu, halikadhalika wajibu wao pia ni sawa na waislamu, kwa maana hio wako sawa kwenye haki na nyajibu.

Mbili: Wana haki ya kutumia sheria zao kwenye ibada zao na sheria za mambo ya binafsi (*Personal Law*), aidha, wanaruhusiwa kua jaji (kadhi) wao wa kuhukumu kesi zao na serikali kutekeleza hukmu wanazozitoa, kwa mamo mengineo sheria ya nchi ndio itakayofanya kazi

Tatu: Yanawajibikia wasiokua waislamu waishio katika nchi za kiislamu yale yaayowajibikia waislamu ya kufuata nidhamu na kutii sheria za nchi, na kutotenda mikhalafa, na iwe utiifu wao ni wa nchi wanayoishi na kujinasibisha nayo

Nne: vyombo vya habari-mawasiliano vyote vinatakiwa vijihusishe katika kubainisha haki za wasiokua waislamu katika nchi ya kiislamu ambazo zinalindwa na sharia ya kiislamu, ili kudhihirisha *thaqafa* (utamaduni) wa kiislamu wa usamehevu na uadilifu, mitaala ya elimu nayo pia iangazie mambo hayo.

Tano: vyombo vya habari-mawasiliano vyote vinatakiwa kujiepusha na kupalilia fitna nembo za udini na umadhehebu miongoni mwa jamii kwa minajili ya kuendelea kulida amani ya nchi

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 210 (6/22)

Yanayohusiana na 'Kugeuza na Kutumia Kemikali za Kuhifadhia Chakula na Dawa'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na mbili (22) kilichofanyika Dola ya Kuwait 2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri, sawa na 22 – 25 Machi, 2015.

Baada ya agizo la 'Konamano' la kuitaka 'Sekreteriti Kuu' kuandaa warsha maalum kutizama masuala ya **'Ugeuzaji na utumiaji';**

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuhusu fasili ya *istihala* (ugeuzaji); inasisitizwa kutumia fasili iliyotumiwa kwenye 'Maamuzi' namba 198 (4/21) na kuongezea kidogo ambayo itakua hivi: *istihala* (ugeuzaji) kwa istilahi ya kifiqhi; ni kugeuka kwa uhalisia wa kitu ambacho ni najisi au kilichoharamishwa utumiaji wake, kitu hicho kinageuka kutoka hali yake na kua hali nyingine au kitu kingine kabisa chenye jina na sifa tofauti, jambo hili kwa istilahi ya kisayansi linajulikana kua ni: 'Kila muingiliano kamili wa kikemikali (*chemical reaction*) kama vile kugeuza mafuta na shahamu (*grisi*), kutoka vyanzo mbalimbali, na kua sabuni', aidha, ni kuchanika (kuoza) kwa dutu (material) na kua vitu vingine tofauti, na kama kwamba muingiliano huu wa kikemikali unaweza ukafanywa kwa makusudi kupitia taratibu za kisayansi na kiufundi, lakini pia unaweza ukafanyika bila ya kukusudiwa (kuonekana), kwa aina ambazo wanafiqihi wamezielezea; kwa mfano: ugeukaji wa siki, ngozi na kuungua, ama ikiwa muingiliano wa kikemikali sio kamili basi haitozingatiwa kua ni kugeuka, na ikiwa dutu ni najisi itabaki hivyo hivyo na haijuzu kuitumia. Ama utumiaji wake: Ni kuzamishwa dutu ndani ya dutu nyengine kiasi ya kwamba dutu iliyozamishwa inapoteza sifa zake zote na inakua haiwezekani tena kuzibagua kwa namna yoyote ile, hii ni pamoja na kuzingatia misingi na vigezo vilivyokubaliwa na wenye tahasusi katika yote

yaliyotangulia.

Mbili: Kuhusu plasma (nyevunyevu) ya damu ambayo imetajwa kwenye maamuzi-tajwa; ‘Kongamano’ linaoelea kua ipo haja ya kurudia tena kutafiti kwani kuna mambo mapya yaliyoibuka kwenye hilo, ‘Sekreterieti Kuu’ iunde kamati ya wataalamu kuliangazia suala hili.

Tatu: Kwa mujibu wa ‘Maamuzi ya Kongamano’ yaliyotajwa hapo juu kuhusiana na ‘utumiaji’ ilisema hivi: ‘*Kongamano’ linaonelea kuakhirisha ili utafiti wa ziada ufanyike*’.

Nne: Kuhusiana na alkoholi na jelatini na kugeuka kwazo: Wajumbe walikualiana kwa kauli moja kutumia ‘Fatwa na mapendekezo yaliyotolewa na ‘Jumuia ya Kiislamu ya Sayansi za Tiba’ kwenye warsha maalum ya: ‘Dutu zilizoharamisha na najisi katika chcakula na dawa’ iliyofanika Kuwait tarehe 22 – 24 Dhul-Hijja (Mfungo tatu), 1415 Hijria, sawa na 22 – 24 Mei, 1995, katika makao makuu ya ‘Jumuia ya Kiislamu ya Sayansi za Tiba’, Kuwait. Fatwa yenyewe inasema hivi:

Misingi mikuu:

1) Ni wajibu kwa kila Muislamu kuzingatia maagizo ya Shari'a, hasa katika eneo la chakula na dawa, ili kuhakikisha usafi wa chakula chake, kinywaji na nguo zake. Miongoni mwa aina zisizohesabika za rehema za Mungu na mapenzi yake ya kuwezesha kufuata maagizo yake kwa urahisi, ni kwamba Shari'a inatambua kabisa hali za dharura na mahitaji na ikaziwekea kanuni muwafaka kabisa kama vile:
   - *‘Dharura huhalalisha iliyoharamishwa*’
   - ‘*Mahitaji, yanapewa hukmu ya dharura ikiwa yameainika’*.
   - ‘*Kimsingi, vitu vyote ni halali ila isimamapo dalili ya kuharamisha*’. Vivyo hivyo,
   - ‘*Vitu vyote ni twahara (safi) ila isimamapo dalili ya kuthibitisha kua ni najisi.’*

   Uharamu (umarufuku) wa kula kitu fulani au kunywa kitu fulani sio dalili ya unajisi wake kulingana na Shari'a.

2) Dutu ya alkoholi kisharia sio najisi, kulingana na taarifa iliyotangulia kua:*’Asili ya vitu vyote ni utwahara*’ hapa nisawa alkoholi iwe peke

yake au iwe imehafifishwa kwa kutiwa maji, kwa maana hio hakuna kosa kisharia kutumia alkoholi kimatibabu kama kusafishia ngozi, majeraha, vifaa, kuulia wadudu au kuitumia kama harufu ya manukato (maji ya kolonia) ambayo inatumia alkoholi kwa kuyeyusha dutu za kimanukato zinazoruka, au utumiaji wa krimu (cream) iliyochanganyishwa na alkoholi. Hukmu hii haitumiki kwenye pombe kwa kua yenyewe ni haramu.

3) Kwa kua alkoholi ni dutu inayolewesha kwa maana hio ni haramu kuitumia (kunywa), kwa dharura iliyopo sasa kwamba alkoholi inahitajika kwenye utengenezaji wa dawa hasa dawa za watoto na wajawazito, hakuna katazo la kisharia kutumia dawa kama hizo iwapo kiwango cha alkoholi kilichotumika ni cha chini (kidogo) sana kwa lengo la kuhifadhi au kuyeyusha baadhi ya dutu za dawa ambazo haziyeyuki kwa maji iwapo haikutumika alkoholi ni vyema kuzingatia kwamba haijuzu kutumia alkoholi kama kiungo cha kutuliza. Uhalali wa utumiaji alkoholi kwenye dawa ni kutokana na kutokuwepo kwa mbadala mwingine. Semina ilipendekeza kuhusiana na hilo kuwa mamlaka za afya zinazohusika kuainisha kiwango cha alkoholi kinachohitajika kutumika kwenye dawa kulingana na kanuni za kisayansi husika na sheria za udhibiti.
4) Haijuzu kutumia chakula ambacho kunapatikana kiwango cha pombe ndani yake hata iwe ni kwa kiwango kidogo sana, hususan vile vilwaji vilivyoenea katika nchi za kimagharibi kama kama vile aina fulani ya chokoleti, aiskirimu, jelati, buza, pamoja na aina fulani za maji yenye gesi; hii ni kwa mujibu wa msingi wa sharia unaosema: ‘Kilevi kinacholewesha kwa wingi, hata uchache wake ni haramu’, na kwa kua hakuna sababu ya kisharia inayoruhusu utumiaji wa vitu kama hivyo vilivyotajwa.
5) Inajuzu ulaji wa vyakula vinavyotumia kiwango kidogo sana cha alkoholi katika utayarishaji wake kwa lengo la kuyeyusha vipengele visivyoyayuka kwa maji kama vile rangi, vihifadhishi na mfano wake; hii ni kutokana na kwamba sehemu kubwa ya alkoholi hio inakua moshi na kupotea hewani, haya ni kwa mujibu wa maelekezi na ushauri wa taasisi za afya na vyakula, hata hivyo ni bora zaidi kutumia mibadala isiyokua na haja ya alkoholi kabisa.

6) Utayarishaji wa vyakula unaotumia mafuta (shahamu) ya nguruwe kama vile baadhi ya jibini (*cheese*) na baadhi ya aina ya mafuta, samli na siagi, na baadhi ya aina za biskuti, chokoleti na aiskirimu; hivi vyote ni haramu kuliwa, hii ni kwa mujibu wa *ijmaa* ya wanazuoni kua nguruwe ni najisi, na ni haramu nyama yake na kwamba hakuna dharura hapa ya kula vitu kama hivi.
7) Jelatini: kuhusu hii, 'Kongamano' linaikalifisha 'Sekreterieti Kuu' kuandaa tafiti za ziada juu ya maudhui haya.

Homoni (Hormones) na Enzymes:

Hormone: ni dutu ya kemikali ambayo hukamuliwa kwenye damu na tezi za mwili ili kudhibiti michakato mingi ya kibaiolojia ya kujitegemea na ya kujenga. *Hormone* ina athiri mwili mzima.

Enzyme: ni molekuli ya protini inayotolewa na seli za mwili na ina athari ya maeneo ambayo huongeza muingiliano wa kemikali katika viumbe hai bila kumalizika.

Heparin iliyotolewa kutoka kwa nguruwe: haijuzu kutumika isipokuwa kwenye mazingira ya 'dharura', Ukarabati wa heparini ili kupata heparini yenye uzito mdogo wa molekuli, hauzingatiwi kua ni ugeuzaji wa kikemikali ambao unaweza kujenga msingi wa hukmu huru. Hakuna katazo la kutumia heparini iliyosindikwa kupitia uhandisi wa jeni bila viungo vyovyote vya nguruwe.

Haijuzu kutumia insulini inayotokana na nguruwe isipokuwa kwenye mazingira ya 'dharura' kwa inapatikana mbadala iliyo halali, lakini inajuzu kutumia insulin ya kibinadamu na inayofanana na hio iwapo imetayarishwa kupitia uhandisi wa jeni.

Vizibo (vali) vya moyo: inajuzu kutumia vizibo mbadala vya moyo ambavyo vinakua ima ni madini (metallic) au vya kibaiolojia (kibinadamu au kihayawani), ama vizibo vinavyotokana na nguruwe haijuzu kuvitumia ila iwapo kuna hali ya 'dharura'.

Juu ya yaliyotangulia; imeamuliwa yafuatayo:

Jibini (*cheese*) iliyotegenezwa kwa kutumia reneti *(rennet)*:

a) Reneti ya nguruwe ni najisi na ni haramu.

b) Reneti ya mnyama mwengine annaeliwa na aliyechinjwa kihalali inakua ni twahara na halali.
c) Ikiwa reneti ni mnyama anaeliwa lakini hakuchinjwa kihalali au aliekufa; maoni ya walio wengi ni kutokua twahara na halali, baadhi ya wajumbe wanaonelea kua ni twahara.
d) Inajuzu kutumia reneti iliyosindikwa kupitia uhandisi wa jenetiki kutokana na jeni inayozalisha reneti.

Maji-taka yaliyotibiwa: Ni maji ambayo watu tayari wameyatumia kwa mahitaji yao ya kuishi, nyumbani, huduma na mahitaji ya utengenezaji, na ambayo yanabeba aina mbalimbali za taka za kibinadamu na za viwandani.

Matumizi ya Maji-taka yaliyotibiwa:

‘Baraza la Kongamano’ limepitisha kujuzisha utumiaji wa Maji-taka yaliyotibiwa katika mambo ya kawaida kama vile: kufulia nguo, kusafishia nyumba na kwenye umwagiliaji wa kilimo kisicholiwa iwapo hapatakua na madhara, ama ikiwa kutakua na madhara basi haijuzu kuyatumia ili kuepusha madhara. Aidha, inajuzu kuyatumia kwenye chakula na kunywa iwapo hapatakua na madhara, lakini haijuzu kuyatumia kwa ajili ya ibada ila baada ya kuhakikisha utwahara wake.

Mapendekezo:

1) Kufanya kazi ya kuyasafish maji-taka ni wajibu kisharia hata kama hakuna nia ya kuyatumia, ili kuondoa hatari za kibinadamu na mazingira zinazoweza kutokea kutokana na mkusanyiko wake. Ni wajibu kuyasafish, kando na kuzingatia faida za kiuchumi zinazoweza kupatikana, hata kama maji-taka hayo baada ya kusafishwa kwake yataelekezwa tu katika mito na bahari, hii ni kwa mujibu wa msingi wa shari'a unaosema: "*kuepusha madhara itangulizwe kabla ya kuleta maslahi*".
2) Kuongeza ufahamu juu ya matumizi ya busara ya maji kwa madhumuni yote ikiwa ni pamoja na kaya, huduma, na umwagiliaji, kwa sababu shari'a ya kiislamu inahimiza watu kufanya hivyo.

3) Kuendelea na utafiti wa kisayansi juu ya njia za kusafisha maji taka zenye gharama nafuu zaidi na zinazotumia nishati kidogo, ili kuepuka matokeo mabaya ya kuhifadhi maji taka.
4) Kuendelea na utafiti wa kisayansi na majaribio ambayo yanahakikisha matumizi ya maji yaliyotibiwa ya maji-taka kwa malengo yanayofaa na yanayoruhusiwa kwa mujibu wa sharia.
5) Udhibiti mkali juu ya vituo na watu wanaohusika na usafishaji wa maji-taka.
6) Ufuatiliaji endelevu wa usalama wa mazao ya chakula na yasiyo ya chakula yanayolimwa kwa kutumia maji-taka yaliyotibiwa.
7) Muuzaji anapaswa kuwafahamisha watu kuhusu bidhaa ambazo zinategemea umwagiliaji wa maji-taka ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa kama hiyo kabla ya kufanya maamuzi ya kununua.
8) Kutumia taka katika maji-taka katika uzalishaji wa nishati kwa ajili ya kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Matumizi ya malisho yanayojumuisha viungo vilivyoharamishwa

‘Baraza la Kongamano’ limeamua kupiga marufuku malisho yanayojumuisha taka za wanyama waliokufa, damu, nguruwe, homoni na antibiotiki, kwa sababu viungo hivi husababisha madhara makubwa kwa afya ya binadamu.

Na linapendekeza yafuatayo:

Nchi za Kiislamu zinapaswa kufanya uchunguzi wa kina wakati wa kuagiza malisho kutoka nchi za kigeni, ili kuhakikisha kuwa malisho yaliyoagizwa hayana viungo vilivyotajwa hapo juu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 211 (7/22)

Yanayohusiana na 'Mwanamke na Uongozi wa Juu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na mbili (22) kilichofanyika Dola ya Kuwait 2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri, sawa na 22 – 25 Machi, 2015.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Mwanamke na Uongozi wa Juu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: "Kongamano' linasisitiza kua Uislamu umemlindia mwanamke haki zake zote kiukamilifu na kumuweka maweko anayostahili pamoja na kuchunga nafasi yake ya kijamii na umbile lake na kazi zake za msingi kama mama, binti, mke na mtu anaewajiika.

Mbili: "Kongamano' linachukua rai wanafiqihi walio wengi ya kwamba: 'Mwanamke hapaswi kuchukua nafasi za juu za uongozi (rais wa nchi).

Tatu: Uongozi wa mwanamke kwa nyadhifa kama kua kadhi (jaji), waziri na mfano wake; wanazuoni wamekhitalifiana juu ya hili, na wanafiqihi wa kila nchi wana fatwa wanayoitumia na kuikubali.

Nne: Katika mazingira ambapo mwanamke amechukua nafasi za uongozi zilizotajwa, basi anatakiwa kulazimiana na heshima na adabu zilizowekwa na sharia ya kiislamu, hususan katika mas'ala ya mavazi na mengineo, aidha anatakiwa asiharibu majukumu yake ya msingi kwa familia yake kwa sababu ya nafasi yake ya uongozi wa ngazi za juu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 212 (8/22)

Yanayohusiana na 'Dhamana ya Benki kwa Mambo Hatarishi Yanayotokana na Uwekezaji Mbovu wa Pesa za Wateja na Kufidia Hasara Zitakazojitokeza'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na mbili (22) kilichofanyika Dola ya Kuwait 2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri, sawa na 22 – 25 Machi, 2015.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Dhamana ya benki kwa mambo hatarishi yanayotokana na uwekezaji mbovu wa pesa za wateja na kufidia hasara zitakazojitokeza,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: 'Dhamana' ya benki ni ule uwajibikaji wa kuwalipa waweka akiba au wenye akaunti za uwekezaji iwapo kumetokea hasara iwe ni kamili au baadhi.

Mbili: Nafasi za benki kushikilia pesa zilizohifadhiwa kama akiba ziko aina mbili:

1) Hali ya kwanza ni kushikilia kama 'dhamana': nayo ni kushikilia fedha kama mmiliki au kwa maslahi ya mshikiliaji kama vile: mnunuzi alieshikilia fedha na mpokeaji (wa bidhaa) kwa thamani aliyolipia, kushikilia mali ya rehani, mnyakuzi, mmiliki na mkopaji. Halikadhalika, inaingia kwenye kundi hilo la 'dhamana' katika akaunti za kibenki pesa akiba zilizowekwa na ambazo zinaweza kuombwa wakati wowote (Akaunti za Biashara), juu ya jambo hili; 'Kongamano' linapenda kusisitiza 'Maamuzi' yake namba 86 (3/9) yaliyohusiana na: 'akiba' kwenye kifungu cha kwanza (moja) kwamba:

"*Moja:* *Akiba zinazoweza kuombwa wakati wowote (akaunti za biashara au current account) ni sawa ziwe kwenye benki za Kiislamu au zile za riba, zinabeba hukmu ya deni (mkopo) kwa mtazamo wa kifiqhi, hii ni kwa kua benki inayopokea akiba hizi wanabeba dhamana ya kulinda mali haya na wanatakiwa kua tayari wakati wowote kurudisha dhamana hio inapohitajika*".

2) Hali ya pili ni kushikilia kama 'amana': nayo ni kushikilia fedha kwa niaba, na sio kumiliki, ya mwenye fedha hizo kama vile: kushikilia akiba, kuazima, kukodi, mshirika, mfanyia kazi mudharaba, msimamizi wa waqf na wasia na nyenginezo. Halikadhalika, inaingia kwenye kundi hilo la 'amana' katika akaunti za benki ya kiislamu; akaunti za uwekezaji kwenye benki ya kiislamu. Juu ya jambo hili; 'Kongamano' linapenda kusisitiza 'Maamuzi' yake namba 86 (3/9) yaliyohusiana na: 'akiba' kwenye kifungu cha pili (mbili) kwamba:

"Mbili: *Akiba zinazowekwa kwenye benki zinazofuata mfumo wa Sharia ya Kiislamu zinaingia kwenye mkataba wa uwekezaji wa akiba hizo ambazo zinachukuliwa kua ni rasilimali ya mudaraba na faida ipatikaayo itagawiwa kwa mujibu wa hukmu za mudaraba zijulikanazo kwenye fiqhi ya Kiislamu ambazo miongoni mwazo ni kutobebeshwa mudarib (benki) dhamana ya rasilimali za mudaraba*".

Tatu: Haijuzu kwa benki inayofanya mudharaba kudhamini (kuwajibika) hasara ima kamili au baadhi ya akaunti za uwekezaji, ila ikithubutu kuzembea au kukhalifu masharti yanayokubalika kisharia, miongoni mwa hali za kuzembea:

1) Ni benki kutojilazimisha kufuata vigezo vya kisharia vinavyohusiana na mikataba au miafaka mahsusi ya kufungua akaunti za uwekezaji za aina mbalimbali.
2) Kukhalifu nidhamu, kanuni na desturi za kibenki na za kibiashara zinazotolewa na mamlaka za usimamizi wa kuratibu shughuli za kibenki, iwapo hazigongani na hukmu za sharia za kiislamu.
3) Kutofanya upembuzi yakinifu na wa kutosha juu ya shughuli za kiuwekezaji.
4) Utumiaji wa njia na mifumo mibaya ya uendeshaji.
5) Ukiukaji wa maagizo ya ndani na udhibiti wa uendeshaji.

6) Kushindwa kupata dhamana za kutosha, kama ilivyo kawaida katika tasnia hii.

Nne: Haijuzu kuishurutisha benki kama mudharib kuweka sharti la ‘dhamana’, kufanya hivyo ni kinyume na maana ya mkataba wa mudharaba. Kwa hiyo, ‘Baraza la Kongamano’ linathibitisha tena yale yaliyosemwa katika Azimio lake Namba 86 na Azimio lake Namba 30 (5/4) kifungu cha kwanza ibara ya nne (Moja:4) juu ya Sukuk za Mudaraba, ambayo inaonyesha kuwa:

> “*4) Haijuzu kwa ‘Waraka wa Makubaliano’ au ‘Hati-fungani ya Mudaraba’ kuwepo kifungu cha kumshurutisha ‘Mudarib’ kubeba dhamana ya ‘Rasilimali’ au dhamana ya faida inayonasibishwa na rasilimali, na lau patakuwepo kifungu kama hicho ima kwa uwazi au kwa upenyezi basi sharuti ya dhamana inabatilika na itakua ni haki ya Mudarib kupokea mgao wa faida kwa taratibu zinazojulikana*”.

Tano: Jukumu la kuthibitisha madai ya upatikanaji wa hasara lipo kwa benki, tofauti na ilivyo kwa kawaida, lakini ni kwa sharti kupatikane vidokezo (*qarina*) vinavyokinzana na msingi wa madai yake ya kutozembea, linalotilia nguvu kulifanyia kazi jambo hili ni

a) Ikiwa ni desturi ya watu kutokubali madai ya mudharib (benki) mpaka athibitishe ukweli wa madai yake ya kutozembea au kuchupa mipaka.
b) Kuthibiti kwa tuhuma dhidi ya alieaminiwa: hapa inakusudiwa kughilibu dhana ya kutokua mkweli (mudharib) kwenye madai yake ya kutozembea au kuchupa mipaka. Kwani kilichotarajiwa kwa mudharib ni kulinda rasilimali zilizowekezwa dhidi ya hasara, na badala yake zipate chumo na faida.
c) Ithubutupo kua ni maslahi kuhamisha jukumu la uthibitishaji wa madai kwa mudharib (benki), kwa minajili ya kulinda rasilimali za wawekezaji dhidi ya hasara pindipo mudhari anapodai kua kumepatikana hasara au mali ya wawekezaji yameangamia.

Sita: Inajuzu kwa benki (mudharib) kutoa mchango wa gawio lake la faida bila ya kweka sharti kwenye mkataba wa mudharaba.

Saba: Zipo taasisi kadhaa zilizofawidhiwa kuainisha uwajibikaji wa uendeshaji mbovu wa benki katika uwekezaji wa mali ya wenye akaunti za

uwekezaji, nazo ni:

1) Taasisi za usimamizi kama vile; Benki Kuu, ni iwe ni taasisi ya kifedha ya kiislamu au ni taasisi ya kawaida lakini ina kamati maalum zinazohusika na shughuli za kibenki za kiislamu.
2) Vituo vya usuluhishaji na utatuzi wa migogoro, kama vile; 'Kituo cha Kimataifa cha Kiislamu cha Usuluhishaji na Upatanishaji', (*Islamic International Center for Reconciliation and Arbitration*) Dubai.
3) Wakaguzi wa Mahesabu kwa mujibu wa inayojulikana kwenye 'tasnia ya ukaguzi'. Kwa mujibu wa 'Msingi namba 5' ya misingi ya uhasibu iliyotolewa na: 'Mamlaka ya Uhasibu na Ukaguzi ya Taasisi za Kifedha za Kiislamu' (*Accounting and Auditing Organization for Islamic Financial Institutions (AAOIFI)*) Bahrain; msingi huo umeainisha kua: jukumu hili kwa kawaida ni jukumu la 'Mkaguzi wa Nje', na inawezekana lisimamiwe na: 'Bodi za Udhibiti wa Kisharia'.

Nane: Ufidiaji wa hasara katika akaunti za uwekezaji uabaki tu kwenye dhara lenyewe, nisawa hasara iwe kwa mali yote au baadhi, na bila kdhamini faida iliyopita (fursa mbadala), kwa kua ilikua ni matarajio tu yasiyokuwepo.

Inausiwa yafuatayo:

1) Benki za kiislamu zinatakiwa ziwe na uangalifu kwenye uwekezaji wa mali ya waweka akiba kwa kufuata mbinu na taratibu zifaazo kulinda mali ya wateja wao na kuyakinga dhidi ya madhara, kupitia kuanzisha mikoba na kutengeneza msingi wa akiba mahsusi kwa hilo.
2) Kuzitaka nchi za kiislamu zitunge kanuni za uanzishwaji wa taasisi za kudhamini mali ya waweka akiba, au wazifanyie marekebisho kanuni zilizopo kwa msingi wa 'Bima ya kusaidiana' ambapo taasisi za kifedha za kiislamu zinashirikishwa. Mikoba hii isimamiwe kwa mujibu wa 'Azimio la Kongamano' namba 200 (6/21) linalohusiana na 'Hukmu na Vigezo vya Kisharia vya Misingi ya Bima Shirikishi'.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 213 (9/22)

Yanayohusiana na 'Haki za Walemavu kwa Mtazamo wa Fiqh ya Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na mbili (22) kilichofanyika Dola ya Kuwait 2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri, sawa na 22 – 25 Machi, 2015.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Haki za walemavu kwa mtazamo wa fiqh ya kiislamu,** na kutokana na umuhimu mkubwa ambao sharia ya kiislamu umeupatia suala hili, na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Mlemavu: ni mtu alielemewa (kiakili, kihisia na kimwili) na kushindwa kujisimamia mambo ambayo anayahitajia; tofauti na mtu aliesalimika.
2) Haki za walemavu: ni mambo maalum ambayo sharia au kanuni imewawekea ili waishi maisha ya heshima.
3) Sharia ya kiislamu imejihusisha sana na haki za walemavu kwa kuwafanya wahisi ni sehemu ya jamii iliyoshikana na hawatenganishiki, wana haki sawa na wengine, halikadhalika wanawajiika kama wengine isipokua pale sharia inapowaekea hukmu maalum.
4) Mlemavu ana haki juu ya familia yake, haki yake inaanzia kwenye uchukuaji wa tahadhari kuzuia ulemavu mapema, aidha, familia inawajibika kumsimamia mlemavu kwa mahitaji yake, na kwa malezi sahihi yaliyojikita kwenye misingi ya mapenzi na heshima, na kumtimizia mahitajio yake ya msingi kama ndoa na maskani na mffano wake.
5) Mlemavu ana haki juu ya jamii yake zikiwemo: kuchanganyikana na

wanajamii wenzake, kumpatia urafiki (swahiba) mwema, kumuheshimu, kutomdharau kwa namna yoyote ile, kuwekeza nguvu zake na uwezo wake kwa faida yake na kwa faida ya jamii yake.

6) Mlemavu ana haki juu ya nchi yake, zikiwemo:

- Huduma za afya kupitia kuanzishwa kwa taasisi za matibabu maalum kwa ajili ya huduma na utunzaji wa watu wenye ulemavu na kuwapatia mafunzo walezi wao juu ya jinsi ya kuwatunza.
- Elimu sahihi, ikiwa ni pamoja na kutoa njia na mbinu za elimu za kisasa zaidi, na mafunzo kwa walimu na wafundishaji wenye tahasusi ya elimu na ulezi kwao.
- Wapewe kazi zinazozingatia uwezo wa watu wenye ulemavu, ikiwa ni pamoja na mafunzo ya kujiandaa kuingia kwenye soko la ajira.
- Kuwatosheleza kifedha watu wenye ulemavu wenye mahitajio kupitia pesa za zakat, awqaf, misaada, na fedha za umma.
- Kuwawezesha usafiri kwa njia sahihi, ikiwa ni pamoja na kutoa njia sahihi za usafiri na kuanzisha viwango sahihi kwenye majengo ya umma na miundombinu ili kurahisisha harakati zao.
- Kutunga sheria na kanuni ambazo zinalinda haki zao na kufuatilia utekelezaji wake.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kueneza uhamasishaji kwa familia na jamii kwa jumla juu ya suala zima la ‘haki za walemavu’ kwa njia zote zinazowezekana, kupitia program za kihabari-mawasiliano, kielimu, kiutamaduni na kijamii.
2) Kuzisaidia taasisi za kiserikali na asasi za kiraia zinazojihusisha na ‘mambo ya walemavu’ na kuimarisha mazingira yatakayosaidia taasisi hizo.
3) Kuanda mikutano, semina na warsha kuhusiana na ‘mambo ya walemavu’.
4) Kuanzisha vituo vya utafiti vya ‘mambo ya walemavu’, na kufaidi kupitia vituo hivyo na program-elekezi kwa wenye ulemavu.
5) Kutanua wigo wa mawasiliano wa pande mbili baina ya jamii na watu wenye ulemavu, ikiwemo kuanzisha na kusaidia jumuia zinazojihusisha na haki zao na mambo yao katika ngazi za kikanda

na kimataifa.

6) ‘Kongamano’ linaweka msisitizo juu ya ulazima wa kufanya liwezekanalo kupunguza au kuzuia sababu zinazopelekea ulemavu, zikiwemo; ukaguzi wa kiafya kabla ya ndoa na chanjo dhidi ya ya ugonjwa wa kupooza na aina nyingine za magonjwa.
7) Kuidhinisha mikataba ya kimataifa kuhusu haki za watu wenye ulemavu bila kukiuka sharia za kiislamu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 214 (10/22)

Yanayohusiana na 'Ushindi (*Majority*) na Ufuasi (*Subordination*) katika Miamala ya Kifedha: Hali zake, Vigezo vyake na Masharti ya Upatikanaji wake'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na mbili (22) kilichofanyika Dola ya Kuwait 2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri, sawa na 22 – 25 Machi, 2015.

Baada ya kupitia mapendekezo ya 'warsha ya kielimu' kuhusiana na maudhui ya **Ushindi (*Majority*) na ufuasi (*Subordination*) katika miamala ya kifedha: hali zake, vigezo vyake na masharti ya upatikanaji wake,** iliyofanyika tarehe 25 – 26 Swafar (Mfungo tano), 1436 Hijri, sawa na 17 – 18 Disemba, 2014; na baada ya kudurusu undani wa mapendekezo hayo na kulinganisha na 'Maazimio ya Kongamano' yanayohusiana na maudhui haya, nayo ni 'Azimio' namba (30), 'Azimio' namba (188) na 'Azimio' namba (196); ikabainika kwa 'Kongamano' kua ipo haja kuyaratibu 'Maazimio ya Kongamano' mbalimbali kwenye mada hii ili yasukwe upya pamoja na mapendekezo ya 'warsha ya kielimu'; hivyo basi imeamuliwa kuikalifisha 'Sekreterieti Kuu' kuunda kamati ya kielimu ya wanatahasusi, ili wawasilishe watakayoyafikia kwenye kikao kijacho.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 215 (11/22)

Yanayohusiana na ‘Ukamilishaji wa Tafiti juu ya Suala la Bima-Shirikishi’

Katika utekelezaji wa ‘Azimio’ namba 200 (6/21) la ‘Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ kuhusiana na ‘Hukumu na Vigezo vya Kisharia vya Misingi ya Bima-Shirikishi’, ililotolewa katika kikao chake cha ishirini na moja (21) katika Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Imam Muhammad bin Saud huko Riyadh (Falme ya Saudi Arabia), tarehe 15 -19 Muharam (Mfungo nne), 1435, sawa na tarehe 18 - 22 Novemba 2013, iliomba kuandaa semina maalum kujadili masuala kadhaa yanayohusiana na bima-shirikishi kama maandalizi kwa ‘Baraza la Kongamano’ kutoa maazimio na mapendekezo sahihi kuhusu somo hilo.

Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), katika kikao chake cha ishirini na mbili (22) kilichofanyika Dola ya Kuwait 2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri, sawa na 22 – 25 Machi, 2015.

Baada ya kupitia mapendekezo ya semina iliyofanyika Jeddah, Saudi Arabia chini ya anuani hii, tarehe 15 -19 Muharam (Mfungo nne), 1435, sawa na tarehe 18 - 22 Novemba 2013, semina ambayo ililenga kunakishi mas’ala yafuatayo:

- Uandaaji wa masharti na vigezo vya kisharia na kikanuni vya kutengeneza ‘utu wa kikanuni’ (legal person) wa kusimamia akaunnti za wabeba hati za bima.
- Kuainisha uhusiano wa kimafungamano unaoratibu mkataba wa bima-shirikishi kwenye:

  - Uhalisia wa uhusiano unaowaleta pamoja baina ya ‘wabeba hati’ na ‘mfuko’ ili kuweza kuainisha wapi mkataba wa kulazimu kuchangia; ili kuepuka mkanganyiko wa kurudi kwenye ‘zawadi’ wakati wa kugawa faida.

- Uhalisia wa uhusiano baina ya ‘wenyehisa’ na ‘wabeba hati’ kwenye mazingira ya akaunti ya washirika imelemewa kutekeleza majukumu yake (Qardh Hasan – Mkopo bila riba).

- Kudurusu masalio ya ziada (*surplus*) ya bima kwa upande wa:

  - ✓ Uwezekano wa kukata sehemu ya masalio hayo ya ziada ya uhakika na kuyaweka akiba ya baadae kupambana na hatari za kulemewa (*defecits*) kwenye mfuko wa bima-shirikishi.
  - ✓ Uwezekano wa kukata kiwago fulani cha masalio ya ziada ya uhakika na kuyaweka akiba ya baadae kupambana na majanga yaayotarajiwa.
  - ✓ Uwezekano wa kujaalia fidia wanayopewa wasimamizi wa shughuli za bima iwe ni sehemu au kiwango fulani katika masalio ya ziada ya bima, na iwe malipo hayo ni mkabala wa kazi zao zote bila ya kukatiwa malipo mengine kutokana na pesa za washiriki.
  - ✓ Uwezekano wa kuchaganya baina ya kiwango fulani kutoka pesa za washiriki na kiwango fulani kutoka masalio ya ziada ili iwe ni malipo kwa chombo cha usimamizi wa bima; malipo haya ni mkabala wa usimamizi wao wa shughuli za bima na pia iwe ni kuwashajiisha ili waboreshe utenda kazi wao.

- Kudurusu misingi ya kiwaqfu ya bima ya kiislamu kwenye pande zote, pamoja na kubainisha msukumo wa tajriba inavyotekelezwa kwenye makampuni yanayohusiana na tasnia hii, na pia kubaini iwapo makampuni haya yamekidhi masharti na vigezo vya kisharia.
- Kuwasilisha ‘tajriba’ za kimataifa kwenye tasnia ya bima-shirikishi, na kujua iwapo misingi iliyopitishwa kwenye ‘Azimio la Kongamano’ namba 200 (6/21) linalohusiana na ‘Hukumu na vigezo vya kisharia vya misingi ya bima-shirikishi’; limefayiwa kazi.

Baada ya kuyadurusu na kujadiliana juu yake’ ‘Kongamano’ limefikia kuchukua maamuzi na maazimio yafuatayo:

Moja: Maazimio ambayo yamegawika kwenye sehemu kuu tatu:

Sehemu ya kwanza: Salio la ziada (*surplus*) la bima:

- Uwezekano wa kukata sehemu ya masalio hayo ya ziada ya uhakika na kuyaweka akiba ya baadae kupambana na hatari za kulemewa (*defecits*) kwenye mfuko wa bima-shirikishi.
- Uwezekano wa kukata kiwago fulani cha masalio ya ziada ya uhakika na kuyaweka akiba ya baadae kupambana na majanga yaayotarajiwa.
- Uwezekano wa kujaalia fidia wanayopewa wasimamizi wa shughuli za bima iwe ni sehemu au kiwango fulani katika masalio ya ziada ya bima, na iwe malipo hayo ni mkabala wa kazi zao zote bila ya kukatiwa malipo mengine kutokana na pesa za washiriki.
- Uwezekano wa kuchaganya baina ya kiwango fulani kutoka pesa za washiriki na kiwango fulani kutoka masalio ya ziada ili iwe ni malipo kwa chombo cha usimamizi wa bima; malipo haya ni mkabala wa usimamizi wao wa shughuli za bima na pia iwe ni kuwashajiisha ili waboreshe utenda kazi wao.

Baada ya kupitia mapendekezo ya semina; ‘Baraza la Kongamano’ linapenda kuweka msisitizo juu ya vifungu viwili; kifungu cha (4) na kifungu cha (6) kwenye ‘Azimio’ lake namba 200 (6/21), aidha, linaonelea kua kujaalia fidia iwe ni kiwango fulani kutoka masalio ya ziada au kujaalia kiwango fulani cha salio la ziada ni cha uhamisishaji kwa chombo cha usimamizi; jambo hili halipaswi kutekelezwa kwani litazua matatizo ya kifiqhi na ya kiutekelezaji.

Sehemu ya pili: misingi ya kiwaqfu ya bima ya kiislamu kwenye pande zote:

Kwa mujibu wa kifungu namba (16) cha ‘Azimio la Kongamano’ namba 200 (6/21) linalohusiana na ‘Hukumu na vigezo vya kisharia vya misingi ya bima-shirikishi’; ilisema hivi: “… *inawezekana kuasisi ‘waqfu ya sarafu ya misaada’ kwa misingi ya ‘waqfu ya sarafu*’”; ‘Kongamano’ linaonelea kua inawezekana kufaidi na waqfu kwa kutekeleza ‘azimio’ hilo-tajwa kupitia yafuatayo:

1) Inajuzu kuanzisha ‘Mikoba ya kiwaqfu ya kusaidiana’ itakayosaidia kufidia baadhi ya hasara zitakazopatikana kutokana na faida (mapato) ya nyaqfu hizo, aidha, inajuzu kwa mikoba hii kupokea

malipo ya awamu (hatua kwa hatua) kwa aina mbalimbali za bima, pia, inajuzu kwa mikoba hii kupokea michango, na hakuna katazo la kisharia kutumia pesa zitokanazo na faida (mapato) ya waqfu, malipo ya polepole na michango iliyopokewa kwa minajili ya kufidia hasara, taasisi husika za waqf za nchi mbalimbali zisimamie kuratibu zoezi hili kwa mujibu wa wanavyoona inaleta maslahi na inalazimiana na misingi ya uadilifu.

2) Inajuzu kukata sehemu ya 'salio la ziada' la bima na kuifanya iwe ni waqf ya sarafu (*Waqf al-Nuquud*) kwa minajili ya kuimarisha kulemewa kwa mfuko na kuuwezesha kupambana na hasara kwa mambo yaliyowekewa bima tayari.
3) Inajuzu kwa 'kampuni za bima za kiislamu' kuanzisha 'mikoba ya waqfu' kwa michango ya fedha inayokatwa kutokana na 'masalio ya bima' ili zitumike faida zake kwenye mazingira ya kulemewa au wakati kampuni hizi zinapitia hali ngumu.

Kwa maana hio inawezekana kufaidi na waqfu katika nyanja za bima-shirikishi, lakini isiwe ni mbadala taratibu zilizokwisha bainishwa kwenye 'Azimio la Kongamano'.

Sehemu ya tatu: Kuwasilisha 'tajriba' za kimataifa kwenye tasnia ya bima-shirikishi, na kujua iwapo misingi iliyopitishwa kwenye 'Azimio la Kongamano' namba 200 (6/21) linalohusiana na 'Hukumu na vigezo vya kisharia vya misingi ya bima-shirikishi'; limefayiwa kazi:

Imetambulikana kulingana na tafiti zihusuzo 'tajriba' za kimataifa' kua: Tajriba za kimataifa nyingi kwenye utekelezaji wa bima-shirikishi zinawafikiana na 'Azimio la Kongamano' namba 200 (6/21) kwenye maeneo mengi ya utekelezaji wake, ila imebainika uwepo wa baadhi ya kasoro na mikhalafa kama ifuatavyo:

- **Moja:** Baadhi ya kampuni za bima-shirikishi hazina 'Bodi za udhibiti wa kisharia'.
- **Mbili:** Kukilazimisha chombo cha usimamizi kulipa *Qardh Hasan* (mkopo bila riba) au wachukue ahadi ya kufanya hivyo mapema, jambo hili linapingana na 'Azimio la Kongamano' namba 200 (6/21) kwenye kifungu namba (9).

- **Tatu:** Kutoweka wazi mifumo na taratibu za bima-shirikishi kwa washiriki wakati wa kufunga mikataba.
- **Nne:** Kugawana ‘salio la ziada’ la bima kati ya kampuni ya usimamizi na wanachama, kwani kampuni tayari imepokea haki yake ya malipo au asilimia ya faida kulingana na kilichoidhinishwa kwa mkataba wa wakala au mkataba wa mudharaba.
- **Tano:** Mmiliki wa hati ya bima kuachana na faida ya mudharaba ikiwa faida itashuka chini ya kiasi kilichotajwa.

Mbili: Mapendekezo:

- **Moja:** Kufanyia kazi na kusambaza yale yaliyopitishwa kwenye ‘Azimio la Kongamano’ namba 200 (621) na ‘Azimio’ la kikao hiki; maazimio yote mawili yanatengeneza ‘rejea-jumuishi’ ya misingi na taratibu zinazosimamia shughuli zote za bima-shirikishi kwa upande wa sharia kwa upana zaidi, aidha, maazimio haya yatafsiriwe kwenye lugha mbalimbali na yasambazwe zaidi kwenye makampuni ya bima-shirikishi yanayofanya kazi na pia kwenye ‘bodi za udhibiti wa kisharia’.

- **Mbili:** Inapendekezwa kwa vyombo vya kutunga sheria vinavyofanya kazi kwenye nyanja za bima-shirikishi katika nchi za kiarabu na za kiislamu waingize ‘Maazimoi ya Kongamano’-tajwa kwenye kanuni zao na waashirie ‘Kongamano’ kama rejea muhimu inayotegemewa.

- **Tatu:** Inapendekezwa kwa vyombo vya kutunga sheria inayoratibu bima-shirikishi; waweke wazi kwamba watakipatia ‘chombo cha bima’ (Mfuko wa wabeba hati, Akaunti huru ya bima isiyoshikana na akaunti ya kampuni), ‘Utu wa kikanuni’ utakaokusanya washirika wote kwenye akaunti ya bima-shirikishi, pamoja na kuzingatia yaliyotajwa kwenye ‘Azimio la Kongamano’ namba 200 (621), kwa namna ambayo sheria hizo zitataja anaewakilisha ‘Utu wa kikanuni’ kwa namna ambayo haitopelekea mgongano wa maslahi.

- **Nne:** Kutoa vigezo na taratibu za kusimamia taasisi na kampuni za bima za kiislamu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa kwenye ‘Azimio la

Kongamano’ namba 200 (621), ‘Azimio’ hili linalinda haki za pande zote husika; hususan mahusiano baina ya ‘chombo cha usimamizi’ na ‘mfuko wa bima’ kwa namna ambayo inazuia mgongano wa maslahi na kuhakikisha uadilifu wa pande zote mbili.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 216 (12/22)

Yanayohusiana na 'Ziara ya (Kutembelea) Mji wa al-Quds: Malengo na Hukmu za Kisharia'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na mbili (22) kilichofanyika Dola ya Kuwait 2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri, sawa na 22 – 25 Machi, 2015.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Ziara ya (Kutembelea) Mji wa al-Quds: Malengo na Hukmu za Kisharia,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Baada ya kusikiliza majadiliano marefu juu ya suala hilo, 'Kongamano' limefikia uamuzi kua: ziara ya Msikiti wa Al-Aqsa ni tendo la ibada na kupendekezwa, lakini majadiliano yalilenga maslahi na mafsada za ziara hii.

Baraza linaonelea kwamba ukadiriaji wa maslahi haya unafanywa na wataalamu wenye ujuzi kama vile watawala (serikali) na viongozi katika nchi za Kiislamu.

Ni muhimu kukumbusha Waislamu wote kwamba suala la al-Quds al-Sharif ni suala la Umma mzima na kwamba ni wajibu kusaidia na kunusuru al-Quds al-Sharif, wakazi wake, na watu wote wa Palestina.

Al-Quds Al-Sharif sio tu suala la watu wa Palestina bali la Waislamu wote. Uhifadhi wa Msikiti wa Al-Aqsa ni sehemu ya imani ya Kiislamu na ni miongoni mwa majukumu ya Waislamu.

Allah Ndie Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Ishirini na Tatu (23) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Madina al-Munawarah, Saudi Arabia

19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri

sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 217 (1/23)

Yanayohusiana na 'Ndoa ya Wasichana Wadogo Baina ya Haki ya *Walii* (Msimamizi) na Maslahi ya Binti na Upeo wa Nguvu za Mtawala (Serikali) Kulizuia Hilo au Kuliekea Nidhamu: Mtazamu wa Kisharia'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Ndoa ya wasichana wadogo baina ya haki ya walii (msimamizi) na maslahi ya binti na upeo wa nguvu za mtawala (serikali) kulizuia hilo au kuliekea nidhamu: mtazamu wa kisharia,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Msichana mdogo ni yule ambae hajabalighi, kipimo cha kuainisha umri wa kuolewa kwa msichana ni kubalighi; kwa kua ni jambo linalodhibitika, kwa mujibu wa wanafiqihi.
2) Sharia ya kiislamu haukuainisha umri fulani kua ni umri wa kufunga *nikah* (ndoa), ama umri wa kumuingilia (*dukhla*) mke, ni katika mambo ambayo yanaendana kulingana na zama na sehemu, na kulingana na utayari (uhalali) wa pande zote mbili kuingia kwenye ndoa na kuanzishsa familia.
3) Baba mzazi wa binti mwenye kite na huruma juu ya binti yake na anaewajibika kulinda maslahi ya bintiye; ana haki ya kumuozesha binti yake baada ya kuchukua idhini ya Kadhi, na ikithubutu kua baba kumuozesha binti yake kutamletea binti madhara basi baba atazuiliwa kumuozesha, ama kwa asiekua baba haruhusiwi kuozesha binti mdogo.
4) Kuainisha umri wa kuozesha wasichana wadogo ni jambo la Kadhi

lakini anaweza kumuakilisha msimamizi, kila nchi itafanya kulingana na mazingira ya zama na mahala na umri (mwaka) kwa kuzingatia maslahi ya jamii.

5) Ni wajibu kuzingatia maslahi ya binti wakati wa kuozeshwa.
6) Usimamizi (walii) wa baba au mwengineo juu ya binti unashurutishwa kulinda maslahi yake (binti).
7) Idhni ya binti wakati wa kuozeshwa ni lazma ipatikane, haijuzu kumuozesha binti pasina idhni yake na ridhaa yake, kama alivyosema Mtume SAW: “Mke mkuu (aiewahi kuolewa) ana haki ya kujiamulia mwenyewe binafsi yake, ama mwari (mwanamwali) anaombwa idhni, na idhni yake ni kunyamaza”.[1] Lau itatokea kua binti ameozeshwa bila ya ridhaa yake basi ndoa hio ni batili na ni haki yake kuifusakhi (kuifuta).
8) Kila nchi ina haki ya kuainisha umri mnasaba wa kuowa/kuolewa kwa mujibu wa inavyoonekana ni maslahi kwa binti, familia na jamii, aidha, kila nchi ina haki ya kuweka adhabu mnasaba kwa kila atakaemuozesha binti mdogo pasina idhni ya Kadhi.
9) Inalazimika kuweka vigezo vya kiafya vya kuozesha wasichana wadogo, haijuzu kumuozesha binti yoyote bila ya kutimiza vigezo hizo, madaktari waaminifu ndio watakaokadiria vigezo hizo.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

[1] Imepokewa na Imam Muslim

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 218 (2/23)

Yanayohusiana na 'Hukmu za Kulemewa na Kufilisika Baina ya Sharia ya Kiislamu na Mifumo ya Kisasa (Kukamilisha Yaliyotangulia)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018.

Baada ya kupitia mapendekezo yaliyowasilishwa kutokana na 'warsha ya kielimu' kuhusiana na 'Hukmu za Kulemewa na Kufilisika Baina ya Sharia ya Kiislamu na Mifumo ya Kisasa' iliyoandaliwa na 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu' kwa kushirikiana na 'Taasisi ya Kiislamu ya Utafiti na Mafunzo' (mwanachama wa Kundi la Benki ya Kiislamu ya Maendeleo – IsDB), tarehe 31 Novemba – 1 Disemba, 2017, na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya 'Azimio la Kongamano' namba 186 (1/20) kifungu (1) cha 'Fasili ya Mlemewa na Mdaiwa alielemewa' mazowea ya watu na desturi zao kwenye utekelezaji wa 'alielemewa' yanazingatiwa.

Mbili: Kuweka msisitizo kwenye kifungu (2) cha Azimio-tajwa kuhusiana na 'Kidhibiti cha kufilisika', pamoja na kuzingatia yafuatayo:

1) Ufilisikaji hautambuliwi ila kwa hukmu ya mahkama.
2) Hukmu za ufilisi zinafanya kazi sawa kwa mtu wa kawaida na 'mtu wa kikanuni'

Tatu: Kuweka msisitizo kwenye vifungu: (Mbili, Tatu na Nne) vya azimio-tajwa.

Nne: Miongoni mwa mas'ala ya kulemewa na kufilisika katika taasisi za kifedha za kiislamu ni kama yafuatayo:

1) Kushindwa kulipa ni kulemewa, na sio kufilisika kwa mtazamo wa kisharia iwapo usuli zinazomilikiwa na na kampuni au taasisi zinatosheleza kulipa madeni, mdai ana haki ya kwenda mahkamani ili kutolewe hukmu ya ufilisi, aidha kampuni au taasisi wana haki ya kwenda mahkamani kutaka wadai walazimishwe kusubiri.
2) Miongoni mwa suluhisho-pendekezi ya kutatua tatizo la ulemevu (ucheleweshaji wa kulipa) katika taasisi za kifedha za kiislamu ni kama zifuatazo:

    a) Kutoa usuli ya mali fulani au manufaa ya mali fulani kugharamia (kulipia) deni.
    b) Kulihaulisha deni kua hisa (kutengeneza rasilimali) kupitia kuongeza rasilimali ya kambuni inayodaiwa kwa kutoa hisa za kawaida ambapo mdai nae atapata hisa kwa deni lake juu ya kampuni, hivyo atakua ni mmiliki wa hisa kwenye kampuni husika na milki zake kwa kiwango cha deni lake alilonalo juu ya kampuni-daiwa.

3) Kampuni au taasisi inayodaiwa waafikiane na mdai kuweka mda wa kusubiri kulingana na ushauri wa wataalamu wanaoweza kukadiria mazingira ya kampuni au taasisi na kuainisha masharti ya kusubiri ikilazimu kufanya hivyo.

Inausiwa yafuatayo:

1) ‘Kongamano’ Inausia kufanyike tiafiti pana na za kina na kuja na suluhisho linalofanyika kazi la tatizo la ‘kulemewa’ (kushindwa kulipa deni) katika taasisi za kifedha kwa namna ambayo italinda haki ya pande zote.
2) ‘Kongamano’ Inausia juu ya umuhimu wa kutunga sheria na kanuni zitakazolinda wanaoamiliana na kampuni miongoni mwa wadai na wadaiwa, pamoja na kulinda haki za pande zote husika kwa minajili ya kuweka sawa (kusahihisha) miamala yao ya kifedha.
3) ‘Kongamano’ Inausia taasisi husika; hususan taasisi za mahkama kujihusisha na misingi ya kimahkama ili kuendana na wakati katika kadhia za ‘ulemevu’ na ‘ufilisi’.

4) ‘Kongamano’ Inausia ‘sekreterieti Kuu’ kukamilisha kudurusu maudhui ya ‘athari ya kulemewa na kufilisika’ juu ya makampuni yenye dhima ndogo, ikiwemo hali za kulemewa au kufilisika kwa kampuni ya dhima ndogo; licha ya kua mmiliki wake mkuu ni muweza.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 219 (3/23)

Yanayohusiana na 'Mambo Yanayofunguza Saumu Kwenye Matibabu (Kukamilisha Yaliyotangulia)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018.

Ikiwa ni kukamilisha 'Azimio la Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu' namba 93 (1/10) kuhusiana na: **Mambo Yanayofunguza Saumu Kwenye Matibabu,** na ambapo mas'ala kadha yaliainishwa kua yalihitaji utafiti wa ziada kwenye kikao hicho, nayo ni:

1) Vibomba vya pumu na kuvuta pumzi zenye nyoshi za dawa.
2) Kuumika (hijama) na kutoa damu (safd).
3) Kuchukua sampuli ya damu kwenye maabara kwa ajili ya uchunguzi, au kutoa damu kutoka kwa mchangiaji, au kuingizwa damu kutoka kwa mtu mwingine.
4) Sindano zinazotumika kutibu figo kupitia kwenye tumbo au kwenye figo bandia.
5) Sindano za dawa zinazopitia kwenye utupu wa nyuma au darubini au kidole kwa minajili ya uchunguzi wa kimatibabu.
6) Amalia za upasuaji (Operesheni) kwa kumpoteza fahamu (ganzi) mgonjwa ikiwa mgonjwa huyu alishatia nia ya kufunga na hakuna kitu cha majimaji au chakula kinachoingia ndani.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui haya, na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Vifunguzaji, ni kukusudia kula na kunywa na kufanya jimai (tendo la

ndoa) na mfano wake, na kutapika.

2) Saumu (funga) inafisidika kwa kila kitu kinachoingia ndani na kuvuka koo kuelekea kwenye mfumo wa usagaji chakula (*digestion system*) na kufika kwenye maeda (utumbo) ni sawa kitu hicho kiwe ni lishe (chakula) au la, na ni kwa njia ya kawaida au la.

3) Visivyofisidi saumu (funga):

    a) Vibomba vya pumu haviharibu usahihi wa saumu, kwa kua dawa hio inaelekea kwenye mfumo wa pumzi (*respiratory system*), kinachofika kwenye maeda ni kitu kichache sana na kisichokusudiwa, kinasameheka, ni kichache mno kuliko masalio ya kupiga msuwaki au kusukutuwa yanayofika kwenye maeda.
    b) Kutoa damu kwa minajiil ya uchunguzi wa kimaabara au kuchangia.
    c) Kila kinachoingia kupitia utupu wa nyuma, kama sindano, mafuta, darubini na marhamu (cream), isipokua sindano ya lishe (virutubishi)
    d) Plasta (gundi) ya kuondoa hamu (hisia) ya njaa.
    e) Utoaji (unyonyaji) wa mafuta lakini bila ya kutumia majimaji yenye lishe.
    f) Kuingiza darubini au kidole cha ukaguzi wa kimatibabu kwenye utupu wa nyuma.
    g) Kuumika na utoaji taka kwenye damu (*faswad*).
    h) Kupoteza fahamu kwa sababu ya ganzi, kwa mda mfupi wa mchana, hata kama kupotea fahamu Kwame kutaendelea siku mzima, bora tu iwe ganzi ilianza akiwa yuko kwenye saumu tayari, na kwa sharti pasitumike majimaji ya lishe.

4) Yanayofisidi saumu:

    a) kila kitu kinachoingia ndani na kuvuka koo kuelekea kwenye mfumo wa usagaji chakula (*digestion system*) na kufika kwenye maeda na tumbo nyembamba.
    b) Kila ambacho ni lishe kwa mwili wa mfungaji saumu, kupitia njia

yoyote ile ya kawaida, inahesabiwa ni kula na kupingana na makusudio ya saumu, kama vile sindano zenye lishe.

c) Mashine ya kuvuta gesi kwenye mapafu (*nebuilizer*) inayotumiwa kutibu pumu, inafunguza, kwa kua kiwango kinachoingia kwenye maeda ni kikubwa sana kuliko kile kiwango kinachosameheka.
d) Kuingiza damu, kwa kua ina kiwango kikubwa cha maji.
e) Usafishaji wa figo wa damu na peritonili (*peritoneal*), kwa kua unaingiza kiwango kikubwa cha maji, chumvi na sukari.
f) Kapsosi (capsules) zinazotumika kwenye vibomba vya pumu ambavyo vina poda kavu, kiwango cha poda hio kinaingia na kufika kwenye maeda.

Inausiwa yafuatayo:

1) Nafasi ya daktari anaetibu ni muhimu sana katika kuainisha ulazima au haja ya kufanya matibabu au uchunguzi ambao huenda yakafisidi saumu, ikiwa hakuna ulazima wa kufanya hivyo, na inawezekana kuchelewesha matibabu mpaka wakati wa kufutari, basi daktari anawajibika kumshauri mgonjwa hivyo.
2) Kueneza elimu kwa wagonjwa kwa yale yanayohusiana na ibada zao ili wazitekeleza kwa njia iliyokua sahihi na toshelezi kisharia, na kuwahimiza watake ushauri wa maulamaa na wenye ilimu kwa kila jambo wanalohisi linawatatiza katika mas'ala ya saumu.
3) Kumjulisha mgonjwa wa figo iliyofeli asitarajiwa kupona, kutofunga ili kulinda maisha yake, mtu huyu ni *ma'adhur* anaruhusiwa kula (kutofunga) na kutoa fidia ya chakula kwa maskini kwa kila siku ya saumu.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 220 (4/23)

Yanayohusiana na 'Kutahiri (kupasha tohara) kwa Watoto wa Kike: Mtazamo wa Sharia ya Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kutahiri (kupasha tohara) kwa Watoto wa Kike: Mtazamo wa Sharia ya Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Kutahiri watoto wa kike; ni kukata kiasi kidogo ya ugozi wa juu ya utupu wa mbele lakini bila ya kugusa kinyama chenyewe, ukataji huu unaitwa 'kupunguza uzibo' au 'kupunguza ugozi' (*clitoropexy*).
2) Ukataji huu ni ada ya kijamii ya zamani, lakini Mtume SAW alielekeza kua mkato wenyewe uwe hafifu mno na kwa namna ambayo itamlinda mtoto wa kike.
3) Tohara ya watoto wa kike iliyoelezewa kwenye kifungu (1) ina khilafu miongoni mwa wanazuoni, na tohara haifanyiwi kazi kwenye nchi nyingi za kiislamu, wapo wanafiqihi kadhaa walioihalalisha ikifanyika ndani ya vigezo na masharti amabayo lazima yapatikane na uwepo wa usimamizi wa wataalamu wa tiba.
4) Haijuzu kugusu sehemu yoyote ya mfumo wa uzazi wa mwanamke; kwani kufanya hivyo ni kudhuru wanawake na kuwavurugia maisha yao ya ndoa. kitendo hiki kimeharamishwa na sharia ya kiislamu, na mtendaji wake atakua ameatenda kosala jinai kisharia, 'Kongamano' linaunga mkono juhudi na taratibu za nchi za kiislamu za kumaliza tatizo hili.

5) Tohara ya watoto wa kike kwa namna ilivyoratibiwa hapa haingii kwenye msamiati wa ‘uchafuzi au ukataji wa viuongo vya uzazi wa wanawake’ ambao umekatazwa na kutahadharishwa na taasisi za afya za kimataifa, hususan ‘Shirika la Afya Duniani’ (WHO).

Inausiwa yafuatayo:

‘Baraza la Kongamano’ linalitaka ‘Shirika la afya Duniani’ (WHO) kurudia na kudurusu suala la: ‘uchafuzi au ukataji wa viuongo vya uzazi wa wanawake’ kwa kuwashirikisha viongozi wa kidini, wa kijamii na sekta ya afya, ili kuboresha ufahamu wa shirika hilo juu ya suala hili na kujua hukmu yake na na kuweka upya elimu ya kidini juu ya suala hili.

Watendaji wa kisasa wa sekta ya afya kwenye mahospitali; watakwe ushauri wakati wanawake wanapohitajia huduma hii ya kutahiri, na kutofautisha baina ya kutahiri na mikato aina nyingine iliyokubalika uharamu wake.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 221 (5/23)

Yanayohusiana na 'Taratibu za Kifikra na za Kivitendo za Kupambana na *Ghuluw* (Uchupaji Mipaka), Siasa Kali na Kinachoitwa Ugaidi Siku hizi Kwenye Nyanja Mbalimbali'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Taratibu za Kifikra na za Kivitendo za Kupambana na *Ghuluw* (Uchupaji Mipaka), Siasa Kali na Kinachoitwa Ugaidi Siku hizi Kwenye Nyanja Mbalimbali,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Siasa kali (*Tatwarruf*) za aina zote ni haramu kwa mujibu wa maandiko ya Qur'an na Sunnah, na inazidi uharanu wake pale inapompelekea mhusika wake kwenye kufanya uadui dhidi ya roho za watu, heshima zo, mali yao akili zao na dini zao.

Inausiwa yafuatayo:

Moja: Kuboresha mbinu na madhumuni ya mahubiri ya kidini misikitini, kwa kuyafungamanisha na hali halisi ya jamii na na matukio yanayoiathiri.

Mbili: Kuboresha nafasi na hadhi ya 'imamu' na 'muadhini' kwa kuwaongezea kipato cha kimaisha (mishahara), na kwa kuwaandaa ipasavyo kupitia semina na warsha maalum katika nyanja za kuhubiri na kuwaidhi kwa kila mfanyakazi wa msikiti.

Tatu: Kuanzisha vituo vya kusomesha na kuhifadhisha Qur'an katika kila

nchi, na visimamiwe na wataalamu wabobezi kwenye fani za Qira'at na Uloom al-Qur'an, na kuviandaa vituo hivi kwa mbinu za ufundishaji za kisasa ili kuziwezesha kupambana na fikra potofu (*tatwarruf*).

Nne: Kuchagua mamufti wenye maarifa sahihi waliokamilisha masharti ya kufutu (kutoa fatwa), na waajiriwe kazi katika miji na mikoa mbalimbali ya kila nchi, na kuzitaka nchi zakiislamu kuchukua fatwa za pamoja kwenye mas'ala ya majanga (*nawazil*) makuu, hii ni kuhuisha 'Fiqh ya ijtihad ya pamoja', na pia kuweka sheria za kuwazuia wasiostahiki kufikia daraja ya umufti na kuweka adhabu kali kwa watu kama hawa.

Tano: Kurekebisha na kuendeleza mikarara (matini) ya masomo kwenye taasisi za kielimu kwa kuongeza madhumuni ya utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu, na kuachana na vurugu, *tatwarruf*, ugaidi na uzindiki, na badala yake kutambua haki ya mwengine yaa kutofautiana na kua na mawazo pacha.

Sita: Kutengeneza mitaala ya kielimu inayowafikiana na misingi ya aqeeda kwa namna ambayo inajumuisha uasili na usasa, na kufanya mapitio ya madhumuni yenye kasumba potofu dhidi ya uislamu na kuyarekebisha.

Saba: Kuzitaka taasisi za habari-mawasiliano kukumbatia msimamo wa *wasatiya* (ukatinakati) na ulingano wakati wanapoandaa vipindi vyao na wajilazimishe na ukweli na wajiepushe na uvumi.

Nane: Kusahihisha kasumba potofu zinazoenezwa za misamiati ya kisharia kama vile: suala la 'jihad', 'khilafa', '*walaa*' (utiifu kwa waumini), '*baraa*' (kuwakataa makafiri), 'haakimiya' (kuitawalisha sharia ya Allah) na masuala mengine ambayo vijana wanayafahamu vibaya na kuyatumia sipo kwenye migogoro na magomvi.

Tisa: Kuingiza mikarara (matini) ya masomo kwenye taasisi za kielimu na vyuo vikuu inayolenga kutupilia mbali vurugu, jinai na ubaguzi wa kimadhehebu, na badala yake kuimarisha ufahamu juu ya uharamu wa kumwaga damu, kuharibu mali na kuvunja heshima za watu.

Kumi: Kuandaa programu-jumuishi za kuelimisha za aina yake

zitakaosimamiwa na serikali kwa lengo la kusahihisha ufahamu wa watu juu ya uislamu na mafundisho yake, na kutilia mkazo misingi yake ya kisharia ambayo watu wengi wameghafilika nayo; na walinganizi na wanafikra wameitupilia mbali.

Kumi na moja: Kupitisha sera za kielimu zilizojikita kwenye misingi ya kusameheana na uzalendo na fikra-tunduizi na kuhehimu mawazo (fikra au rai) ya mwengine.

Kumi na mbili: Kizitaka nchi na jamii mbalimbali kufaidi kutokana na tajriba zilizofanikiwa katika kupambana na *tatwarruf* na ugaidi.

Kumi na tatu: Kufungua milango ya mazugumzo (kujadiliana kwa wema) na wenye fikra potofu na kujaribu kuziangusha hoja zao tatanishi na kuwarudhisha kwenye njia ya haki (sawa) na maisha ya kijamii ya *wasatiya*, na kuishi vizuri pamoja na jamii ili kpatikane amani, utulivu na maendeleo.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 222 (6/23)

Yanayohusiana na 'Huduma Maalum (Zawadi) Wanazopata Wateja wa Akaunti ya Hundi (Biashara): Mtazamo wa Kisharia'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Huduma Maalum (Zawadi) Wanazopata Wateja wa Akaunti ya Hundi (Biashara): Mtazamo wa Kisharia,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Maana ya 'Akaunti ya Hundi' (current): Ni rejista ya pesa za mteja anazoziweka kwenye benki, ima ya kiislamu au ya kawaida, akiwa na haki ya kuzichukua (withdraw) pesa hizo wakati wowote anapotaka, kwa taratibu zinazojulikana; zikiwemo kuandika hundi (cheki), uhaulishaji na utowaji wa moja kwa moja, pesa hizi zilizowekwa benki zinakua chini ya dhamana ya benki lakini benki wana haki ya kuzisarifu vile wanavyotaka kwa faida yao kwa mujibu wa kanuni.

Mbili: Hukmu ya Kisharia: 'Kongamano' limepitia maweko kadhaa ya kisharia juu ya pesa hizi zinazowekwa kwenye akaunti ya hundi kama vile: 'pesa hizi ni amana iliyodhaminiwa matumizi' au ni: 'mkataba mpya unaojitegemea' au ni: 'mfumo wa mafungamano wenye mikataba kadhaa', 'Kongamano' liliishia kuweka msisitizo wa 'Azimio' lake namba 86 (3/9) lilihosiana na 'Akiba za Kibenki (Akaunti za Benki)' likisema:

> "***Moja:*** *Akiba zinazoweza kuombwa wakati wowote (akaunti za biashara au current account) ni sawa ziwe kwenye benki za Kiislamu au zile za riba, zinabeba hukmu ya deni (mkopo) kwa mtazamo wa kifiqhi*".

Tatu: Hukmu ya Sharia juu ya huduma maalum (zawadi) kwa wateja wa akaunti ya hundi:

Maana ya huduma maalum (zawadi):

Huduma maalum za kibenki ni zile haki za nyongeza ambazo benki inawapatia wateja wa akaunti za hundi (akiba zinazoweza kuombwa wakati wowote), kwa lengo la kuwashajiisha kufungua akaunti na kuziendeleza. huduma hizi maalum (zawadi) kwa mujibu wa manufaa yake na malengo yake ziko aina mbili:

a) Ya kwanza: Ni ile ambayo manufaa yake yanamrudia mteja pekee.
b) Ya pili: Ni ile ambayo wote; mteja na benki wananufaika.

Aina ya kwanza: Manufaa ambayo yanamrudia mteja pekee: Huduma maalum (Zawadi) ambazo faida yake inamrudia mteja pekee zimegawanyika sehemu mbili: faida za ki-*maanawi* (moral) na faida za ki-*maadi* (material).

1) **Faida za ki-*maanawi* (moral):** Ni manufaa na huduma anazopewa mteja na benki yake, hakuna ishara ya kuonyesha faida hizi ni nyongeza ya pesa zake alizoziweka akiba (amana); mfano wa faida hizi ni kama: ubora wa huduma anazopewa kwenye matawi ya benki, kupewa vipeperushi vyenye miongozo kila wakati, statementi ya mara kwa mara, cheti cha uwezo wa kifedha (kutolemewa) na kadi ya kimataifa ya kutolea pesa kwenye mashine (ATM) na mfano wake.
   Hukmu ya kisharia: Inajuzu kupokea huduma maalum aina hizi; kwa sababu hizi si katika nyongeza za pesa ambazo zingekua ni riba ambazo benki wanajilazimisha kuwalipa wateja wake, ikiwa ni ziada ya pesa mkopo alizoziweka, lakini huduma hizi ni msaada kutoka kwa mkopeshwaji (benki) kwenda kwa mkopeshaji (mteja) ili aweze kufaidika na haki ya fedha zake, kwa kua hakuna katazo juu ya hili basi itabaki kua ni halali (*mubah*).

2) **Faida za ki-*maadi* (material):** Hizi ni nyongeza ya vitu, manufaa na pesa za ziada juu ya pesa zilizowekwa akiba (amana) kwenye akaunti ya hundi; nyongeza hizi zinafanana na ziada ya pesa

kutokana na mkopo; kwa mfano mteja kupewa zawadi za mashine za elektroniki (TV, simu, mashine ya kufukia nguo na kadhalika) na tikiti ya ndege na mfano wake.

Hukmu ya kisharia: Haijuzu kupokea huduma (faida) kama hizi ni sawa ziwe zimeshurutishwa au la, ikiwa ni kwa sababu ya mkopo na kwa kutizama kiwango cha pesa na mda wake; hii itakua ni nyongeza ya riba ambayo benki inajilazimisha kumlipa mkopeshaji kwa mkopo wake. Ama ikiwa huduma (zawadi) zinapewa kila mteja mpya awe ni wa akaunti ya hundi au ya mudharaba au ya kugharamia na nyenginezo, basi hizi zinahesabiwa kua ni katika matumizi ya matangazo ya kibiashara na kuvutia wateja; kwa maana hio zinakua ni halali (*mubah*), kwani hazifungamani na mkopo na kiwango chake na mda wake.

Aina ya pili: Manufaa ambayo yanawarudia wote; mteja na benki: Nayo yako aina mbili: Ya kwanza; ni manufaa yanayohusiana na uwekaji na utoaji wa pesa, ama ya pili; ni yasiyohusiana na hilo.

1) Manufaa anayoyapata mteja yanayohusiana na uwekaji na utoaji wa pesa, kwenye akaunti ya hundi na amabpo manufaa yenyewe ni ya pande mbili; kama vile: huduma ya ‘kitabu cha hundi’ (*Cheque book*) na kadi ya ATM, hukmu yake; inajuzu, kwa kua hii ni mkopeshwaji (benki) anamsaidia mkopeshaji (mteja) kupata haki yake ya pesa zake, hapa manufaa ya huduma hizi hayamuendei mteja peke yake; bali na benki pia (mkopeshaji na mkopeshwaji), kila mmoja wao ananufaika bila ya kumdhuru mwengine, sharia haikatazi maslahi ambayo ndani hakuna madhara kwa mwengine, aidha, huduma hizi hazina katazo la kisharia wala hazijalazimishwa; kwa maana hio zitabaki kua ni halali (*mubah*).
2) Manufaa ya pande zote mbili; lakini hayahusiani na uwekaji na utoaji wa pesa, kwenye akaunti ya hundi; kama vile: kumpatia mteja huduma za kibenki kwa bei za upendeleo, yaani chini ya kiwango cha kawaida wanacholipa wengine, miongoni mwa miamala ubadilishaji wa sarafu, ada ya uhaulishaji, malipo ya visanduku vya kuhifadhia nyaraka nyeti, ada za kufungua akaunti za mikopo (credits), kadi za mikopo (credit cards) na hati za udhamini na mfano wa vitu kama

hivyo; vyote hivyo ni haramu, kwa kua zinaingia kwenye ‘mkopo unaoleta manufaa’.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 223 (7/23)

Yanayohusiana na ‘Uwajibikaji wa Daktari kwa Makosa ya Kimatibabu Yasiokusudiwa: Mtazamo wa Kiislamu’

Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018.

Baada ya kupitia ‘Maazimio ya Kikao cha Kielimu’ kuhusiana na **‘Uwajibikaji wa Daktari kwa Makosa ya Kimatibabu Yasiokusudiwa: Mtazamo wa Kiislamu’** yaliyotolewa na ‘Jumuia y Kiislamu ya Elimu za Tiba’ Kuwait, tarehe 5 – 7 Jumada al-Thani (Mfungo tisa), 1436 Hijri, sawa na 26 – 28 Machi, 2015. Na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Makosa ya Kimatibabu Yasiokusudiwa:

1) Imekubaliwa kutumia fasili ya ‘Kosa la Kimatibabu’ kua ni: ‘Kushindwa kukamilisha kilichopangiwa kufanywa kwa sababu ya kudharau au kuzembea na mfano wake’.
2) Imekubaliwa kutumia fasili ya ‘Ajali ya Kimatibabu’ kua ni: ‘Ajali inayotokana na shughuli za kimatibabu, haihusiani na hali za kiafya za mgonjwa’.

3) Imekubaliwa kutumia fasili ya ‘Ajali za Kitaasisi’ kua ni: ‘Ajali kadhaa zinazotokea kwa nyakati za karibu zinazosababisha ukoseaji kwenye ngazi mbalimbali, pamoja na uwepo wa mfumo mbovu wa kiafya ambao kupitia ajali hizo kunapelekea kutokea mambo hatarishi kadhaa’.
4) Imekubaliwa kutumia fasili ya ‘Misingi ya Kazi za Kiafya’ kua ni: ‘Misingi iliyo thabiti inayojulikana kisayansi na kiutendaji’.
5) Uandaaji wa programu za kisayansi zilizotokana na tafiti pana za kisayansi kuhusiana na sababu na viashiria vya vya makossa, ili kuweza kuweka suluhisho muwafaka la kupunguza makossa kadri iwezekanavyo.
6) Ulazima wa kuandaa mazingira muwafaka ya ndani na ya nje yanayofungamana na huduma za afya na kuhakikisha ufanisi wake.
7) Usalama wa wagonjwa unatakiwa uwe lengo la msingi katika sera zote za kiafya.
8) Ulazima wa kuandaa warsha kwa wafanyakazi wote wa sekta ya huduma za afya na kuimarisha dhamira yao ya kidini na uchamunugu ili kuwawezesha kuepukana na makossa mengi yanapojitokeza, kwa kuzingatia kua warsha hizi ni sehemu ya majukmu-msingi ya huduma za afya.
9) Kuwapatia mahitajio ya lazima; kama vile: vifaa, maabara, taarifa (data), na ulazima wa kufuata taratibu (protocols) za kazi za kimataifa ili kuchagia katika ukaguzi na utambuzi sahihi wa ugonjwa.
10) Ulazima wa kufuata misingi na kanuni za kazi za kimataifa, hususan kwenye suala la kutozidisha masaa ya kazi ya jopo la madaktari kwa zaidi ya masaa manane (8) kwa siku, hasahasa siku za kubadilishana zamu, ili kulinda ufanisi wa daktari nae aweze kulinda afya ya mgonjwa.
11) Ulazima wa kupunguza idadi ya wagonjwa wa kila daktari kadri inavyowezekana, ili kumpatia mgonjwa fursa ya kutosha ya kujielezea tatizo lake la kiafya.
12) Ulazima wa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya kanuni na maazimio yanayohusiana na mahakikisho ya usalama wa wagonjwa na jinsi ya kuwalinda dhidi ya ‘makosa ya kimatibabu’.
13) Kuweka msisitizo juu ya suala la ukarabati (maintainance) wa vifaa

vvya kiafya mara kwa mara na wataalamu wa vifaa hivyo, ili kuhakikisha usalama wake na ufanisi wake.

14) Ipo haja ya kuannzisha ‘chombo chca juu’ cha kusimamia ‘makosa ya kimatibabu’, chombo hiki kijumuishe wenye tahasusi mbalimbali na wenye uzoefu na wanaojulikana kwa uaminifu na ukweli, chombo hiki kiwe chini ya usimamizi wa waziri husika, na iwe miongoni mwa majukumu yake ni kufanya uchunguzi kila kutokeapo ‘ajali ya kimatibabu’, sawasawa iw ajali hio imesababisha madhara au la, na ufanyike uchunguzi huo kwa haraka iwezekanavyo, kabla ya ushahidi wake na athari hazijapotea, uchunguzi huu unatakiwa uwe jumuishi utakaoainisha sababu na athari za kutokea kosa hilo iwapo kuna madhara, ripoti kamili iwasilishwe kwa wahusika wa ngazi za juu pamoja na mapendekezo ya kuzuia kosa kama hilo na mengineo mustakbala.

15) Kuwashajiisha madaktari waliokosea kufunguka na kuelezea makossa yao na wadhihirishe ukweli na uwazi ili isaidie mustakbala wa kazi ya tiba na mafanikio yake, na kutafuta njia za kikanuni za kuwapunguzia lawama.

16) Kuwashajiisha wanaogundua makossa kufikisha taarifa sehemu husika na wapewe ulinzi dhidi ya kudhalilishwa au kudhuriwa.

17) Ulazima wa kuanzisha ‘kituo maalum cha ukusanyaji taarifa (data)’ kitakachosimamiwa na jopo la wataalamu; madaktari, wanafiqihi na wanasheria, na kutungwe kanuni lazimishi kwa taasisi zote zinazofanya kwenye wizara ya afya kuwasilisha taarifa za ‘makosa’ kwenye kituo-tajwa ili kubaini sababu na yanayosababisha makossa hayo.

18) ‘Mamlaka maalum’ isimamie kufanya tathmini ya utendakazi wa wa ‘wahudumu wa afya’ iwapo kumetokea makoa makubwa yaliyoababisha madhara, ili kubaini mazingira ya kazi na uwezo wake.

19) Kuzitaka taasisi husika kurekodi na kufuatilia dawa, ili kuhakikisha utaratibu wake ni sahihi, aidha, kufuatilia mwenendo mzima wa dawa, hasa zile ambazo ni za hatari, baada ya matumizi yake, na kurekodi athari zozote za pembeni (side effects) za dawa hizo pamoja na dawa nyengine, au kiwango cha madhara iwapo yamepatikana, na

hatimae kchukua hatua zifaazo.

20) Kuihamasisha jamii kukubali dhana ya kua upo uwezekano wa makossa kufanyika kwenye shughuli za kimatibabu.
21) Kuingizia mfumo wa kadi za kielektroniki kwa kutumia nidhamu ya utambulisho ya 'bakodi' (*Barcode*) kwa kila mtu kila nchi, kadi hizi zitumike kwenye miamala yote ya kimatibabu, pamoja na kusisitiza juu ya ulazima wa kuukagua mfumo huo wa bakodi mara kwa mara ili kuhakikisha ufaaji wake.
22) Kuandaa machapisho ya tafiti na mifumo (*protocols*) na miongozo ya kazi ili kuimarisha kituo-taarifa (*database*) kinachorikodi hali za wagonjwa, mazizngira yao na historia yao ya kiafya.
23) 'Makosa ya Kimatibabu' ni lazima ya yarikkodiwe, yakusanywe na yapangwe kwa nidhamu fulani, ili iwe rahisi kufanya rejea yoyote ya kutengeneza rippoti ya kisayansi na kuitumia katika uchambuzi wa anwai zote za 'makosa'.
24) Kutofautisha baina ya 'Makosa ya Kimatibabu' yanayotokana na uzembe wa madaktari, na yale 'Makosa' yanayotokana na taasisi za afya zenyewe kwa ajili ubovu au kutoendana na wakati wa vifaa vyao vya matibabu.
25) Kutofautisha baina ya 'Makosa ya Kimatibabu' na ajali zisizotarajiwa, ambazo ziko nje ya uwezo wa daktari, aidha, Kutofautisha baina ya 'Makosa ya Kimatibabu' na mzoroto wa afya uliotarajiwa kutokana na shughuli za kimatibabu.
26) Daktari atawajibika katika mazingira ya uzembe na kutojali[1] na kukiuka misingi ya kimatibabu iliyokubalika miongoni mwa wataalamu wa tiba, aidha, aendapo daktari kumtibu mgonjwa bila ya idhini yake au idhini ya msimamizi wake au serikali katika hali ambazo idhini ni lazima.
27) Kwa mazingira ya uzembe au kutojali, daktari atawajibishwa na sharia au kanuni kulipa fidia.
28) Kuandaa mkarara (matini) wa masomo utakaozingatia suala la maadili kwenye kazi za tiba, na kutambua 'makosa ya kimatibabu' kwenye kila tahasusi, na jinsi gani ya kujikinga na makossa hayo,

[1] Uzembe: ni kutofanya la wajibu, kutojali: ni kufanya lisilofaa.

aidha, somo hili liwe ni somo la lazima kwa wanafunzi wanaosomea elimu ya tiba.

29) Ni wajibu wa daktari kufahamu vilivyo maradhi ya mgonjwa wake, na athari zinazoweza kujitokeza kwa matibabu anayompatia, na awe na pupa la kusimamia maslahi ya mgonjwa kwa mujibu wa mazingira na utamaduni uliopo.
30) Daktari anatakiwa awe na pupa la kumhudumia mgonjwa na ajitahidi uwezo wake.
31) Uharamu wa daktari kufichua siri za mgonjwa wake, na atawajibika iwapo amekiuka maadili haya kwa madhara yoyote yatakayomfika mgonjwa wake, 'Azimio la Kongamano' namba 79 (10/8) lirejelewe; pamoja na mapendekezo ya warsha ya 'Jumuia ya Kiislamu ya Elimu za Tiba' iliyofanyika Kuwait, tarehe Aprili, 1987.

Mbili: Idhini ya Kutibu:

1) Kimsingi, hakuna matibabu yatakayofanyika bila ya idhini ya muhusika mwenyewe ispokua kwenye baadhi ya hali zifuatazo:

    a) Hali za dharura ambazo ni hatarishi kwa maisha (uhai) ya mgonjwa au kwa baadhi ya viungo vyake muhimu, ishindikanapo kupata idhini ya mgonjwa au msimamizi wake.
    b) Hali ambazo ni lazima zitibiwe kwa haraka kwa minajili ya kulinda maslahi ya umma, kama vile magonjwa ya miripuko na ya kuambukiza ambayo ni hatarishi kwa afya ya jamii nzima.
    c) Iwapo mgonjwa ana maradhi ya kisaikolojia au ya kiakili yanayotishia maisha yake au maisha yaw engine, basi atachukuliwa ili akatibiwe kwa kulazimishwa, lakini baada ya kufuata taratibu zinazohitajika.

2) Kutokuwepo ulazima wa idhini:

    a) Iwapo msimamizi amekataa kutoa idhini, usimamizi wa idhini unahamia kwa anaesimamia maslahi ya umma (serikali).
    b) Katika hali tete, lakini mgonjwa aliebalighi na mwenye akili timamu bado anakataa kutoa idhini, hapa ni lazima aelezewe hatari iliyopo

ya yeye kukataa kutoa idhini, daktari atarekodi maelezo yake rasmi, kwa hali hii, idhini ya mgonjwa itaendelea kuzingatiwa madamu fahamu zake ni sahihi.

c) Ipo haja ya utafiti wa ziada wa hali zinazohitajia ‘uzalishaji (upasuaji) wa sizeria’ ili kuokoa maisha ya mama au mtoto au wote wawili pamoja, kama vile hali ya kamba ya kitovu inapomtatia mtoto shingoni mwake, iwapo mama kwa hali kama hii, amekataa kutoa idhini kwa ‘upasuaji wa sizeria’.

Inausiwa yafuatayo:

1) ‘Jumuia ya Kiislamu ya Elimu za Tiba’ Kuwait, inaombwa kufanya tafiti linganishi baina ya: ‘misingi ya sharia ya kiislamu kwenye nyanja za kazi za kimatibabu na uwajibikaji juu ya makosa yanayojitokeza kwenye kazi hii’, walinganishe na: ‘sheria, kanuni na misingi ya kimahkama inayokubalika katika suala hili’. Tafiti hii linganishi ifanyike katika nchi za kiarabu na za kiislamu, na baadae wapendekeze kinacholazimu kufanywa kuleta uwiano kamili baina ya mifumo miwili hii.
2) Kuratibu baina ‘Jumuia’ na ‘Muungano wa Nchi za Kiarabau’ (*Arab League*) na jumuia zinazofanana katika nchi za ulimwengu wa kiislamu, ili kudurusu uwezekano wa kua mswada wa kanuni-elekezi ya pamoja inayohusiana na ‘Hukmu za matendo ya kimatibabu na uwajibikaji kutokana na makosa yanayojitokeza’, kanuni-elekezi hii iwe ni muongozo kwa nchi za kiarabu na za kiislamu wanapotaka kutunga sheria zinazohusiana na ‘matendo ya kimatibabu na makosa yanayotokana nayo’.
3) Uanzishwaji wa chombo huru na chenye tahasusi katika kila nchi ya kiarabu na ya kiislamu; kitakachosimamia uandaaji wa ripoti ya kitaalamu juu ya masuala ya kesi za kimahkama na migogoro inayopelekwa kusawazishwa na jopo la majaji, hii kwa minajili ya ‘makosa yanayotokana na matendo ya kimatibabu’.
4) Kutumia mfumo wa ‘usuluhishaji’ kwenye kesi za jinai zinazohusiana na ‘makosa yanayotokana na matendo ya kimatibabu’, katika kiwango chochote cha kesi hio, kwa namna ambayo lau suluhu

itapatikana; madai ya kesi ya jinai yafutwe na kusitisha utekelezaji wa adhabu yoyote iwapo hukumu ishatolewa.

5) Kujitanua katika kutafuta usuluhishaji wa migogoro, na kwenda kutafuta upatanishi juu ya 'uwajibikaji wa kiraia' unaotokana na 'makosa yanayotokana na matendo ya kimatibabu'.
6) Kuunda kamati maalum za kutizama kesi zisizokua za jinai na zile za kiraia dhidi ya makosa ya madaktari na wasidizi wao, kamati hizi ziwezeshwe kutoa maamuzi.
7) Inalazimu kukuza ufahamu wa masuala haya yote na taratibu zinazohusiana na misingi ya kazi za pamoja, na kuziimarisha taratibu hizo kupitia mafunzo maalum yatakayotolewa mapema kwenye vyuo vikuu na taasisi za afya.
8) Madaktari wanatakiwa kupokea mafunzo juu ya matendo yao kimatibabu na namna ya kupambana na matatizo mbalimbali na kuendeleza ustadi wao wa kufanya kazi kwa pamoja ili kuboresha uwezo wao; wanatakiwa wapate mafunzo haya wakiwa vyuo vikuu na taasisi za elimu.
9) Madaktari wanatakiwa kupokea mafunzo wakiwa kazini juu ya umuhimu wa kufanya kazi kwa pamoja katika huduma za afya, yatasaidia kujenga utamaduni wa usalama.
10) Sekta ya huduma ya afya inatakiwa kuimarisha mafunzo yaliyopatikana kwenye programu-andalizi za juu.
11) Umahiri wa madaktari kuhusiana na suala la kufanya kazi kwa pamoja unatakiwa uthaminiwe kwa kupewa vyeti maalum vya kuwaruhusu kufanya kazi.
12) Madaktari wapya kabla ya kuidhinishwa na kupewa leseni ya kazi wanatakiwa wafanyiwe tathmini ya uwezo wao wa kufanya kazi kwa pamoja na matarajio ya kazi ya pamoja.
13) Kudurusu uanzishwaji wa mifumo ya bima kwa 'makosa yatokanayo na matendo ya kimatibabu', kama njia ya kuwashajiisha madaktari kuongeza juhudi kutibu wagonjwa.
14) Vyombo vya habari-mawasiliano na vyombo vingingine vya kueneza uhamasishaji vitumie nafasi zao kwa shauku kutoa taarifa juu ya magonjwa ya kisaikolojia ili waweze kutiibwa mapema na kwa ufanisi, aidha, watoe elimu kwa wagonjwa wa kisaikolojia ili wajue

haki zao.

15) Ushirikiano baina ya nchi za kiarabu na za kiislamu katika kutoa kanuni-elekezi ya pamoja ya ‘matibabbu ya kisaikolojia’, iliyojikita kwenye misingi mikuu ya sharia ya kiislamu na misingi na miafaka ya kimataifa husika.
16) ‘Jumuia ya Kiislamu ya Elimu za Tiba’ Kuwait, inaombwa ishirikiane na nchi za kiarabu na za kiislamu katika kutunga ‘kanuni ya pamoja ya matibabu ya wagonjwa wa akili’ itakayojikita kwenye misingi mikuu ya sharia ya kiislamu na misingi na miafaka ya kimataifa husika.
17) Kuandaa warsha maalum ya matibabu ya kisaikkoljia na kiakili na kujadili masuala ya kimaadili na kisharia yanayohusiana na siha ya kisaikoljia, na hatimae kupatikane mapendekezo ya uhakika juu ya suala hili.
18) Taasisi za tiba zinatakiwa ziwe na vikao vyva mara kwa mara baina yao na madaktari au wasaidizi wao ili kudurusu masuala mapya yanayoibuka kwenye sekta ya ‘matendo ya kiutabibu’, na kubadilishana mawazo ju ya matatizo yanayowakwaza kwenye kazi zao, aidha kuelimishana juu ya ‘makosa ya kimatibabu’ na kupendekeza njia za kuyapunguza au kuyazuia.
19) Kukuza stadi za mawasiliano kwa madaktari ili waweze kuwasiliana vizuri na wagonjwa wao na familia zao, ili waweze kua karibu zaidi na maedeleo ya kiafya ya mgonjwa, na kutambua kwa haraka iwapo kuna tatizo lolote katika matendo yao ya kiutaibu.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 224 (8/23)

Yanayohusiana na 'Kua na Tahadhari (*Tahawwut*) Katika Miamala ya Kifedha: Vigezo na Hukmu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018.

Baada ya kupitia 'Maazimio ya Warsha ya Kielimu' kuhusiana na '**Kua na Tahadhari (*Tahawwut*) Katika Miamala ya Kifedha: Vigezo na Hukmu**' iliyoandaliwa na 'Kongamano' Dubai, tarehe 2 – 27 Aprili, 2016, na kwa kushirikiana na 'Idara ya Mambo ya Kiislamu na Kazi za Kheri' kupitia 'Semina ya Fiqhi ya Uchumi wa Kiislamu' kwenye kikao chake cha pili. Na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Maana ya Misamiati (Dhana) ya Kimsingi:

1) **Maana ya Tahadhari (*Tahawwut*):**

   a) Tahadhari (*Tahawwut*); maana yake kiujumla ni: kujikinga, kujilinda au kujihami kama wanavyoelezea wanafiqihi.
   b) Tahadhari (*Tahawwut*) katika istilahi ya kifedha ni: Taratibu za makusudi na za mpangilio za kusimamia uepushaji, upungzaji na uzuiaji wa mambo hatarishi kwa njia ya kuyahamisha kwa upande mwingine.
   c) Tahadhari (*Tahawwut*) kwa maana ya kiistilahi: ni kujihami dhidi ya mambo hatarishi na kupunguza athari zake, bila ya kubana kwenye dhana iliyoenea katika miamala ya masoko ya kifedha, ambayo aghalabu yake imejikita kwenye misingi ya riba na fidia juu ya mambo hatarishi (*risks*). Dhana hii ya tahadhari inabeba ndani yake misamiati ya: 'vitu vya baadae (*mustakbali*)', 'chaguzi (*options*)' na

miamala ya kubadilishana (*swaps*) ya mda, baadhi ya miamala hii tayari ‘Kongamano’ lilishatoa ‘Maamuzi’ ya kutojuzu kwa mujibu wa ‘Azimio’ kama vile chaguzi na mengi ya mambo ya baadae na ubadilishanaji wa mda kwenye ‘Azimio’ lililohusiana na masoko ya fedha.

2) **Dhana ya ‘Mambo hatarishi (risks)’:**
Maana ya kilugha ya ‘mambo hatarishi’; ni uwezekano wa kuhiliki (kupotea kwa mali). Ama maana yake ya kiistilahi ni: uwezekano wa kupotea kwa mali, au wa kupata hasara, au kukosa faida-tarajiwa, au kupata faida chini ya kiwango-tarajiwa.

Mambo hatarishi yanayokusudiwa kwa maana hii; yanazunguka kwenye shughuli za kiuchumi, ikumbukwe kua katika sharia ya kiislamu kuna mikataba ya uhakikisho; kama vile: mikataba ya rehani na dhamana na mengineo, kwa lengo la kulinda pande zote mbili dhidi ya mambo hatarishi na fidia, ‘uhatarishi’ ni jambo lisilotakikana; kwa kua ni kuyasogeza mali kwenye maangamizi.

3) Kuhami maana yake ni: kutumia mbinu zozote za kujikinga dhidi ya kupata hasara au kupungua kwa mali au kutilifika. Himaya kwa mana hii; ni pana zaidi kuliko kudhamini rasilimali, kwa kua kudhamini ni kujilazimisha kutoka upande fulani kubeba dhimma ya kitu chochote kitakachokifikia rasilimali kama hasara au kupungua au kutilifika, lakini himaya ni kulinda rasilimali na kudhamini mubashara na isiyokua mubashara.

Mbili: Msimamo wa sharia ya kiislamu juu ya kujikinga (*tahawwut*) dhidi ya mambo hatarishi:

1) Tahadhari (*Tahawwut*) kiujumla ni: kuyakinga kuyahami mali dhidi ya uhatarishi, kwa maana hio hili linawafikiana na mojawapo ya makusudio makuu ya sharia ya kiislamu ya kuhifadhi mali.
2) Hukmu ya kisharia juu ya utekelezaji wa kivitendo; itategemea ni kwa kiwango gani cha makubaliano ya matumizi ya taratibu zote za *tahawwut* (tahadhari ya kinga) yamekidhi vigezo vya kisharia, kujua hilo kunahitajika tathmini ya kila muamala umelazimiana kiasi gani na

vigezo vya kisharia.

Tatu: vigezo vya kisharia na taratibu zake kwa miamala ya *tahawwut* (tahadhari ya kinga):

1) Miamala ya *tahawwut* (tahadhari ya kinga) isibebe chembe za riba au isiwe ni njia ya kuifikia riba, aidha, isibebe utata mwingi, kufanya hivyo ni sawa na kula mali yaw engine kwa batili (dhulma).
2) Muamala wenyewe uwe ni sahihi unaokubalika kisharia.
3) Miamala ya *tahawwut* (tahadhari ya kinga) isipelekee kwenye kuuza deni kwa kima kisichokua chake, na kubadilishana vilivyokatazwa kisharia, kama ilivyo kwenye masoko ya fedha ya kawaida.
4) Miamala ya *tahawwut* (tahadhari ya kinga) isipelekee kuuza haki za mhusika, kama vile kuuza chaguzi ambazo zimeharamishwa na ‘Azimio la Kongamano namba 63 (1/7) kifungu cha 2 (b). Aidha, isipelekee kuuza ahadi kama kuchukua malipo juu ya dhamana ambayo imekatazwa na ‘Kongamano’ kwenye ‘Azimio’ lake namba 12 (2/12).
5) Makusudio makuu yazingatiwe wakati wa kufunga mikataba ya *tahawwut* (tahadhari ya kinga) na pia kuzingatia hatima ya mikataba hio na athari zake katika nyanja mbalimbali, uzingatiaji wa hatima ni msingi unaohimizwa kisharia.
6) Mikataba ya *tahawwut* (tahadhari ya kinga) isipelekee kudhamini rasilimali au faida inayotarajiwa, nisawa kudhamini huko kutoke kwa Msimamizi, au Mudharib au Wakala, lakini hii ni katika mazingira ya kutokuwepo kuzembea au kutojali au kukhalifu masharti.
7) Haijuzu kuifanya hali ya uhatari kua ni bidhaa ya biashara.
8) Kusudio la kutumia vifaa vya *tahawwut* liwe ni kuhifadhi usalama wa mali, na sio kubahatisha (kamari) kwenye utofauti wa bei (*speculation*).

Inausiwa yafuatayo:

1) Kutokana na tofauti ya fomula za *tahawwut* (kinga), njia zake, na taratibu katika utekeleza wa kivitendo kwenye Taasisi za Kifedha za Kiislamu, na kwa kua mada hii ni katika mas’ala mapya yaliyozuka; basi bila shaka misingi ya ijtihadi ya Fiqhi ya Kiislamu iko imara

kulisimamia suala hili na kulipatia hukmu muwafaka, kwa maana hio; ‘Kongamano’ linapendekeza kuandaliwe warsha za kielimu kwa kushirikiana na ‘Taasisi za Kifedha za Kiislamu’ ili kudurusu fomula na miamala ya *tahawwut* (kinga) inayoedelea kutumika kwenye ‘Taasisi za Kifedha za Kiislamu’ au iliyopitishwa na ‘Bodi’ zake, ili kubaini ni kwa kiwango gani miamala hio imekidhi vigezo na na masharti yaliyopitishwa kwenye ‘Maamuzi na Maazimio ya Kongamano’.

2) Kuwasisitiza wasimamizi na wafanyakazi wa ‘Taasisi za Kifedha za Kiislamu’ kufaidi na formula na mikataba iliyoidhinishwa (iliyopitishwa) na ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’, na ‘Kongamano la Fiqhi’ lilio chini ya ‘*Rabitat al-Alam al-Islami*’ (Muslim World League) na makongamano mengineo yanayotegemewa katika kusuka mikataba ya ya *tahawwut* (kinga) na miamala, kama vile: mikataba ya *salam*, *salam*-sambamba, murabaha kwa ‘*aamir bis-shiraa*’, *istisnaa*, *istisnaa*- sambamba na hiari ya sharti, miamala yote hio kwa kufuata vigezo vya kisharia vilivyoelezewa kwenye ‘Maazimio hayo’.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 225 (9/23)

Yanayohusiana na 'Suala la '*Halali*', Kujibu Masuali ya Taasisi ya Ubora na Viwango ya Nchi za Kiislamu (SMIIC)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018.

Baada ya kupitia 'mswada wa mwisho' wa warsha ya kielimu '*Halal*', ikiwa ni kujibu **Masuali ya Taasisi ya Ubora na Viwango ya Nchi za Kiislamu (SMIIC),** iliyofanyika Jeddah, tarehe 22 – 23 Rabii al-Thani (Mfungo saba), 1436 Hijria, sawa na 11 – 12 Februari, 2015 ambapo mswada huo ulirudiwa tena na kuandikwa upya kwa mujibu wa 'Azimio la Kongamano' namba 206 (2/22) lililohusiana na 'Masuali ya Taasisi ya Ubora na Viwango ya Nchi za Kiislamu (SMIIC)', lililotolewa kwenye kikao cha ishirini na mbili (22) kilichofanyika Kuwait, kuanzia tarehe 2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri, sawa na 22 – 25 Machi, 2015. Na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuhaulisha maudhui haya kwa 'Sekreterieti Kuu' kudurusu na kufanya marekebisho wanayoyaona ni sawa na baadae kuyawasilisha kwa waulizaji (SMIIC) juu ya hayo.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 226 (10/23)

Yanayohusiana na 'Ushindi (*Majority*) na Ufuasi (*Subordination*) katika Miamala ya Kifedha: Hali zake, Vigezo vyake na Masharti ya Upatikanaji wake'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018.

Baada ya kupitia 'mswada wa mwisho' wa mapendekezo ya warsha ya kielimu kuhusiana na: '**Ushindi (*Majority*) na Ufuasi (*Subordination*) katika Miamala ya Kifedha: Hali zake, Vigezo vyake na Masharti ya Upatikanaji wake**' iliyoandaliwa na 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu' na kwa kushirikiana na 'Benki ya Kiislamu ya Maendeleo' (IsDB) iliyofanyika Jeddah, tarehe 25 – 26 Swafar (Mfungo tano), 1436 Hijria, sawa na 17 – 18 Disemba, 2014 ambapo mswada huo ulirudiwa tena na kuandikwa upya kwa mujibu wa 'Azimio la Kongamano' namba 214 (10/22) lililohusiana na '**Ushindi (*Majority*) na Ufuasi (*Subordination*) katika Miamala ya Kifedha: Hali zake, Vigezo vyake na Masharti ya Upatikanaji wake**', lililotolewa kwenye kikao cha ishirini na mbili (22) kilichofanyika Kuwait, kuanzia tarehe 2 - 5 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1436 Hijri, sawa na 22 – 25 Machi, 2015.

Baada ya kusikiliza kwa makini hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya, na kwa kuzingatia yaliyoamuliwa kwenye 'Maazimio ya Kongamano' kuhusiana na maudhui-tajwa namba 30 (5/4), 188 (3/20) na 196 (2/21); hasahasa namba 30 (5/4);

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya 'Azimio-tajwa' namba 30 kipengele cha tatu, kifungu (a) na (b) kuhusiana na '*mali zilizokusanywa kwa minajili ya Mudaraba baada ya kusainiwa mikataba lakini kabla ya kuanza mradi husika*'; basi ijulikane

kua mzunguko wowote katika kipindi hiki wa ‘Hati-fungani (hisa, sukuk, bidhaa) ni sawa na kubadilishana pesa kwa pesa kwa maana hio: ‘hukmu zote za ubadilishanaji wa pesa’ zitatumika. Aidha, iwapo pesa hizi za Mudaraba ni deni, basi hukumu zote zinazohusiana na madeni zitatumika.

Mbili: Msingi wa ufuasi (ufuasi wa mfuataji kwa anaefuatwa) unazingatiwa kisharia, na unasema: mfuasi ni mfuasi, kinachofuata kitu kinachukua hukmu ya kitu hicho, kwa maana hio inajuzu kuamiliana kwenye hati za fedha (sukuk) kwasharti ya upatikanaji wa kinachofuatwa.

Kidhibiti cha: ‘upatikanaji wa kinachofuatwa’, ni uwepo wa shughuli na kazi na taasisi inayosimamia mzunguko wa fedha, kwa hali hii inajuzu kuamiliana kwenye hatia za fedha bila ya kuzingatia viwango (asilimia) vya pesa na madeni miongoni mwa mali yaliyopo, hii ni kwa kua hati hizi za fedha ni zenye kufuata asilimali, na haziko huru (hazijitegemei), pamoja na kuzingatia kua asilimali inayofuatwa itaendelea kubaki hivyo katika awamu zote za miamala (mizinguko).

Tatu: Iwapo hati za fedha haziwakilishi shughuli ya kibiashara yenye mzunguko wa pesa, lakini ni uwepo wa umiliki wa pamoja kwenye baadhi ya ugharamiaji unaolipiwa na taasisi ya kifedha; basi ‘Kongamano’ linasisitiza yaliyoamuliwa kwenye ‘Azimio lake’ namba 30 kipengele cha tatu, kifungu (c), kua: ‘Iwapo ‘Pesa za Mudaraba’ ni mkusanyiko wa pesa taslimu na madeni na ankari na huduma basi inafaa kuuziana ‘Hati-fungani za Mudaraba’ kulingana na bei watakayoridhiana ikiwa ankari na huduma ndio kiwango kikubwa, kidhibiti cha kiwango hapa kua ankari na huduma ziwe ni zaidi ya nusu (50%).

Nne: Haijuzu kutumia kisingizio cha: ‘miamala ya hati za fedha kwa msingi wa ufuasi’ kua ni njia au ujanja wa kugeuza madeni na kuyafanya hati za fedha, na kuamiliana kwenye hati hizo kama kwamba hati hizo ni mchanganyiko wa madeni na pesa zikaongezewa ankari na manufaa ili ziwe na ushindi (majority) ili ziweze kutumika kama ‘*tawarruq*’.

Utekelezaji wa msingi wa ushindi (*majority*) na ufuasi (*subordination*) katika miamala ya kifedha:

Moja: Sukuk na mikoba ya uwekezaji:

1) Katika mpangilio wa utekelezaji wa msingi wa ushindi (*majority*) na ufuasi (*subordination*) kwenye miamala ya sukuk, ni lazima kuzingatia kua makataba ambao kwa mujibu wake sukuk zinatolewa, umekamilisha nguzo zake na masharti yake ya kisjaria, na kusiwepo sharti lolote linakinzana na mkataba wenyewe au kukhalifu hukmu zake.
2) Kuweka msisitizo juu ya yaliyoamuliwa kuhusiana na utekelezaji wa sukuk za ijara kwenye 'Azimio la Kongamano' namba 196 (2/21) lililohusiana na 'Kukamilisha maudhui ya sukuk za kiislamu' vifungu namba (2), (3) na (4).
3) Inajuzu kuamiliana (kubadilishana) kwenye sukuk ikiwa wingi wa mali yanayowakilishwa ni: ankari, au manufaa au huduma, baada ya kufunga mlango wa washiriki na kuanza kwa shughuli, ama ikiwa ni kabla ya shughuli kuanza basi vigezo vya kisharia vizingatiwe kwenye mikataba ya ubadilishanaji sarafu iwapo mali husika ni pesa, na kutekeleza hukmu za madeni iwapo mali husika ni madeni.
4) Inajuzu kuamiliana kwenye sukuk za umiliki wa ankari (mali yasiyohamishika) fulani kabla ya kurudia kuzikodisha ankari hizo, zikiingiswa kwenye kukodishwa basi sukuk zinakua ni za ijara, na zitakua kwenye dhimma ya mkodishwaji wa pili, na hapa ubadilishanaji utafanyika kwa mujibu wa hukmu na vigezo vya madeni.
5) Haijuzu kuamiliana kwenye sukuk za umiliki wa ankari zinazojulikana lakini bado hazijaainishwa ni ipi hasa ya kutumika manufaa yake, na kabla ya kukabidhishwa ila kwa kuzingatia vigezo vya madeni, lakini iwapo zimeshaainishwa; basi inajuzu kuamiliana na sukuk hizo.
6) Inajuzu kuamiliana kwenye sukuk za umiliki wa manufaa yanayopatikana kutoka sehemu fulani lakini kabla ya kukodishwa (*re-leasing*) huduma hizo mtu wa pili, zikikodishwa (*re-leasing*) mtu wa pili; basi sukuk zinwakilisha kodi, na zinakua ni deni kwenye dhimma ya ya mkodishwaji wa pili, kwa maana hio ubadilishanaji utafanyika kwa mujibu wa hukmu na vigezo vya madeni.
7) Haijuzu kuamiliana kwenye sukuk za umiliki wa huduma zinazopatikana kutoka sehemu fulani zinazojulikana lakini bado hazijaainishwa ni zipi hasa za kupatikana huduma hizo ila kwa

kuzingatia vigezo vya madeni, lakini iwapo zimeshaainishwa; basi inajuzu kuamiliana na sukuk hizo.

8) Inajuzu kuamiliana kwenye sukuk za '*istisnaa*' (makubaliano ya utengenezaji), iwapo sukuk hizo zimetolewa na mtengenezaji mwenyewe, au iwapo pesa zimehaulishwa kua ankari zinazomilikiwa na wabeba sukuk ndani ya mda wa '*istisnaa*', ama mapato ya sukuk yakilipwa kama thamani ya '*istisnaa*' sambamba au ikikabidhiwa mali yaliyotengenezewa muagizaji; kwa maana: thamani ya '*istisnaa*' imekua ni deni kwenye dhimma yake (muagizaji), kwa hali kama hii; miamala yote inabeba hukmu za madeni.
9) Haijuzu kuamiliana kwenye sukuk za '*salam*', kwa sababu kufanya hivyo itakua ni kuuza deni kwa deni; hukmu za madeni zitatumika hapa.
10) Haijuzu kuamiliana kwenye sukuk za '*murabaha*', baada ya kuuza bidhaa za *murabaha* kumuuzia mnunuzi na kukabidhiwa; kufanya hivyo itakua ni kuuza deni.
11) Inajuzu kuamiliana kwenye sukuk za *musharaka*, sukuk za *mudaraba* na sukuk za *wakala* kwa uwekezaji (uwekezaji wa sukuk kupitia kwa wakala) baada ya kufunga mlango wa makubaliano na na kukamilisha vigezo vya asili (*majority*) kwa mujibu w ilivyobainishwa kwenye kifungu cha (3) hapo juu.
12) Inajuzu kuamiliana kwenye sukuk za *ijarah* ya uendeshaji biashara na *ijarah* inayoishia kumiliki baada ya mkodishwaji kumiliki mali yaliyokusudiwa kukodishwa.

Mbili: Hisa:

Kwa kuzingatia yaliyopitishwa kwenye 'Maamuzi-tajwa' hapo juu na 'Azimio laKongamano' namba 63 (1/7) lililohusiana na 'Masoko ya Pesa' hususan kwenye vifungu namba (4), (5), (7), (8) na (13); kwa hio yanayowajibika kuzingatiwa wakati wa kutoa hisa ni yafuatayo:

1) Haijuzu kuamiliana kwenye hisa za kampuni ambayo mali yake ni madeni pekee, ila kwa kuzingatia hukmu za madeni.
2) Haijuzu kuamiliana kwenye hisa za kampuni ambayo mali yake ni pesa pekee, ni sawa iwe wakati wa kununua hisa au baada ya hapo,

kabla sehemu ya mtaji haijageuzwa kuwa mali imara kwa kiwango cha 10%.

3) Ikiwa mali ya hisa inajumuisha mali, manufaa, pesa na madeni, na isiwezekane kua na ushindi wa mali na manufaa (*majority*) juu ya madeni na pesa kwa kua mali yote hayo yamelingana, au ikawa pesa na madeni ndzo zenye ushindi (*majority*), au imeshindikana kujua; basi kwa hali kama hii kanuni ya *ufuasi* itatumika, kidhibiti chake ni kuhakikisha kuwepo kwa kinachofuatwa nacho ni: shughuli, kazi na chombo cha usimamizi cha kuyazungusha mali. Kwa mazingira haya; inajuzu kuamiliana (biashara) kwenye hisa bila ya kuzingatia kiwango cha asilimia cha pesa na madeni kukabiliana na mali mengine kwa sababu hapa yatakua ni yenye kufuata na hayajitegemei lakini kwa kuzingatia wakati wote kua asili inayofuatwa inabaki kua hivyo wakati wote wa miamala (biashara).

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 227 (11/23)

Yanayohusiana na 'Athari ya Mkataba wa Ndoa Juu ya Umiliki Binafsi wa Wanandoa'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye Kongamanao kuhusiana na **Athari ya Mkataba wa Ndoa Juu ya Umiliki Binafsi wa Wanandoa,** na baada ya kusikiliza kwa makini hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kila mmoja wao; mume na mke ana dhimma yake ya kifedha inayojitegemea (huru), na kwa mujibu wa hio kila mmoja ana haki (uhuru) ya kusarifu (kutumia) kila anachomiliki; mali na haki, kulipia au kusaidia (kutoa zawadi).

Mbili: Kinachomilikwa na mmoja wa wanandoa ima kwa sababu ya ndoa au nyengineo inakua ni milki binafsi ya anaemiliki, na mali hayo yatahamia kwa warithi wake baada yake.

Tatu: Iwapo mume na mke wameridhiana kugawana mali yao kwa moyo safi na kwa hiari, basi hapana katazo kisharia juu ya hilo, lakini haijuzu kulazimisha kufanya hivyo.

Nne: Ni haki ya mke, iwapo uhusiano wa kindoa umekatika ima kwa talaka au kwa kuachishwa au kwa kujivua kwenye ndoa (*khul'i*) na ikamsababshia madhara, basi ana haki ya kwenye mahkamani (kadhi) kudai fidia ya madhara yaliyomkuta ikiwa ni sehemu ya kuifanyisha kazi hukmu ya sharia ya kiislamu ya mke mtalaka 'haki ya *mut'a*' (masurufu) baada ya talaka.

Tano: Kutoa wito wa uanzishwaji wa taasisi za kiserikali au za kiraia

zitakazojishughulisha na huduma na mahitajio ya wanawake watalaka (waliotalikiwa).

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 228 (12/23)

Yanayohusiana na 'Mapendekezo ya Kamati Iliyoundwa na Sekreterieti ya Kongamano Kufanyia Tafiti za Ziada Juu ya Baadhi ya Mas'ala ya Sukuk'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018.

Baada ya kuwasilishwa yaliyojiri (ripoti) kwenye Kikao cha Kamati ya Kielimu ya 'Kongamano' kilichofanyika tarehe 9 Rabii al-Awwal (Mfungo sita), 1438 Hijria, sawa na 8 Disemba, 2016 kwa minajili ya kutafiti kwa kina zaidi juu ya baadhi ya ya mas'ala ya sukuk kwenye 'Maamuzi ya Kongamano';

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuandaa 'Warsha ya Kielimu' itakayohusisha wanatahasusi kwa minajili ya kuzamia na kudurusu mas'ala mawili yanayofuata, na 'Warsha' hio itoke na mapendekezo ya kielimu ili yawasilishwe kwenye kikao kijacho cha 'baraza la Kongamano', mas'ala yenyewe ni haya:

Mas'ala ya kwanza: Je kukodisha asilimali (kumkodishia) kwa alieiuza inaingia kwenye biashara ya '*al-'ina*' (kununua na kuuza papohapo) ambayo imeharamishwa kisharia, na kama ilivyoamuliwa kwenye 'Azimio la Kongamano' namba 188 (3/20).

Mas'ala ya pili: Kwa kiwango gani inawezekana kulipia sukuk za *ijara* inayoishia kumiliki kwa thamani yake ya sokoni (kawaida), na kwanini isiwe kwa thamani yake ya sokoni kwa mujibu wa kua mtoaji na mfaidi wa sukuk wameridhiana juu ya hilo wakati wa kutoa sukuk, kama ilivyopitishwa kwenye 'Azimio la Kongamano' namba 178 (4/19).

Allah Ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 229 (13/23)

Yanayohusiana na 'Ilani (Tamko) Juu ya Kuishi Pamoja kwa Kuheshimiana: Mtazamo wa Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018.

Kwa kutambua matatizo ya ndani wanayopitia Umma hivi sasa, na changamoto za nje zinazowakabili; 'Baraza la Kongamano' linapenda kutoa tamko chini ya anwani:

Tamko la Madina juu ya Kuishi Pamoja kwa Kuheshimiana: Mtazamo wa Kiislamu

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu alietumilizwa kama huruma (rehema) kwa walimwengu wote, na Aali zake na maswahaba wake wote.

Ammaa ba'ad:

Dini ya kiislamu ndio dini ya mwisho, na sharia yake ndio hitimisho ya sharia zilizoteremshwa kutoka mbinguni, ulinganizi katika kumpwekesha (*Tauhid*) Allah SWT ndio lengo lake na kusudio lake kuu kama vile ilivyo kwenye risala (jumbe) zilizotangulia la kuwatakia kheri binadamu wote ya hapa duniani na ya kesho akhera, amesema Allah SWT: "*Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote*"[1], pia akasema: "*Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinacho bainisha kila kitu, na ni uwongofu,na rehema, na bishara kwa Waislamu*"[2].

[1] Surat al-Anbiya: 107.
[2] Surat al-Nahl: 89.

Kwa imani hio tulionayo; sisi wajumbe wa ‘Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya kiislamu’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), tuliokutana katika kikao chake cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018, juu ya umuhimu wa misingi na maadili yanayosimamiwa na uislamu; hii hapa chini ni baadhi ya maadili kama hayo tumeyaweka kwenye tamko hili, tukijua fika kua binadamu na jamii zote za kibinadamu wanayahitajia maadili haya kuliko kitu chochote kingine; tunafanya hivi ikiwa ni kuiga kitendo alichokifanya Mtume SAW pale alipoguria Madina (*Yathrib*), alipoandika muongozo kwa watu wa Madina na jamii zake mbalimbali, muongozo ambao uliratibu na kusimamia mahusiano mema miongoni mwa wakaazi wa Madina; ndani ya muongozo (katiba) huo kulikuwepo misingi mikuu ya kiislamu, hapa chini tutaelezea baadhi yayo:

1) Ulinganizi (*Da’wah*) wa uislamu ni ulinganizi kwa binadamu wote, na Mtume Muhammad SAW ni ametumilizwa kwa binadamu wote kwa mujibu wa kauli ya Allah SWT aliponena: “*Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri, na mwonyaji. Lakini watu wengi hawajui*”[1]. Kwa kua risala hii ya uislamu ni ya watu wote; basi ulinganizi wake ni wajibu kuwalingania binadamu wote, na njia ya kuwafikishia ujumbe huu iwe ni ya hikma (busara) na mawaidha yaliyo mema (mazuri) na kujadiliana na watu kwa namna iliyokua bora; mbali na majivuno au ujeuri, amesema Allah SWT: “*Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hikima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora*”[2].

2) Binadamu, kwa mtazamo wa kiislamu; ni msimamizi (*khalifa*) aliechaguliwa na allah kwenye ardhi yake, Mwenyezi-Mungu amemtukuza kiroho na kimwili, na kamwe haijuzu kumuudhi au kumtweza au kumdharau akiwa hai n ahata akiwa maiti (amekufa), amesema Allah SWT: “*Na hakika tumewatukuza wanaadamu*”[3], na

[1] Surat Saba’: 28.
[2] Surat al-Nahl: 125.
[3] Surat al-Israa: 70.

akasema Mtume SAW: “Kuvunja mfupa wa binadamu akiwa maiti, ni sawa na kuuvunja akiwa hai”[1], na viumbe wengine wote wameumbwa na kuandaliwa kumtumikia huyu binadamu, amesema Allah SWT: “*Kwani hamwoni ya kwamba Mwenyezi Mungu amevifanya vikutumikieni viliomo mbinguni na kwenye ardhi, na akakujalizieni neema zake, za dhaahiri na za siri? Na miongoni mwa watu wapo wanao bishana juu ya Mwenyezi Mungu pasipo ilimu, wala uwongofu, wala Kitabu chenye nuru*”[2], akasema tena Allah SWT: “*Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanao fikiri*”[3]. Uislamu umejihusisha sana kumjenga binadamu kimwili, kiakili na kiroho, ili aweze kutekeleza majukumu ya ukhalifa (usimamizi) wa hii ardhi (dunia).

3) Allah amemkalifisha (lazimisha) binadamu kufuata sharia yake ambayo ameiteremsha kupitia kwa manabii na mitume, na kwa kadri atakavyoifanyia kazi ndio itakua hatima yake hapa duniani na kesho akhera, amesema Allah SWT: “*Akasema: Ondokeni humu nyote, hali ya kuwa ni maadui nyinyi kwa nyinyi. Na ukikufikieni uwongofu kutoka kwangu basi atakaye ufuata uwongofu wangu, hatapotea wala hatataabika*”, akaendelea kusema: “*Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu*”[4].

4) Katika kufafanua ujumuishaji wa sharia wa hali zote za kibinadamu na kuakisi mahusiano yake; wanazuoni wamezigawa hukmu za sharia katika makundi makuu matatu: la kwanza: hukmu za ki-imani (*aqeeda* na *tauhid*), la pili: hukmu za ki-akhlaaq (maadili) na la tatu: hukmu za ki-vitendo; ambazo zinajumuisha aina zote za ibada na aina zote za miamalaat (miamala).

---

[1] Hadithi hii imepokewa na imam Abudaud kwenye ‘Sunan’ yake, mlango wa ‘majeneza’: Juzuu 3, hadith namba 3207, pia imepokwa na imam Ibn Majah kwenye ‘Sunan’ yake, mlango wa ‘majeneza’, hadith namba 1616.

[2] Surat Luqman: 20.

[3] Surat al-Jaathiya: 13

[4] Surat Ta-Ha: 123, 124.

5) Hakuna kutafautisha (kubagua) miongoni mwa binadamu kwa sababu ya rangi au jinsia au lugha, binadamu wote wametokana na asili moja, baba mmoja na mama mmoja (Adam na Hawaa), amesema Allah SWT: "*Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni kutokana na nafsi moja, na akamuumba mkewe kutoka nafsi ile ile. Na akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi. Na tahadharini na Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana, na jamaa zenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaangalieni*"[1]. Akasema Mtume SAW: "Hakika Allah anasema: *Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari*"[2], akaendele kusema Mtume SAW: "*Basi mwarabu hana ubora juu ya ajemi (asiekua mwarabu), wala ajemi hana ubora juu ya mwarabu, aidha mtu mweusi hana ubora juu ya mtu mweupe, wala mtu mweupe hana ubora juu ya mtu mweusi ispokua kwa daraja ya taqwa (ucha-Mungu)*"[3].

6) Aidha, hakuna tofauti baina mwanamume na mwanamke katika heshima (utu) ya kibinadamu na misingi ya nyajibu za kisharia, amesema Allah SWT: "*Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi. Huamrisha mema na hukataza maovu, na hushika Sala, na hutoa Zaka, na humt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu, Mwenye hikima*"[4], na Mtume SAW akasema: "*Hakika ya wanawake ni sawa na wanaume*"[5], ba inapokuja ulinganio kwa mwito wa: *Ya ayyuha al-Naas* (Enyi watu) na *Ya ayyuha al-Mu'minoon* (Enyi mlioamini) basi hua inajumuisha wanaume na wanawake pamoja.

---

[1] Surat al-Nisaa: 1.

[2] Surat al-Hujuraat: 13.

[3] Imepokewa na imam al-Tabrani, mlango wa: mwenye jina la adaa, Juzuu 18, Uk. 12.

[4] Surat al-Tauba: 71.

[5] Imepokewa na imam al-Tirmidhi kwenye 'Sunan' yake; Juzuu 1, Uk. 173, hadith namba 113.

7) Miongoni mwa nguzo za imani kwa muislamu, ni kuamini mitume na manabii wote, na kuamini vitabu walivyoteremshiwa, na kuwatukuza na kuwaenzi, na kuamini kua mitume wote hao wametumilizwa na Allah kuja na ulinganizi mmoja nao ni ulinganizi wa *tauhid*; kumpwekesha Allah SWT na kumuabudu yeye pekee, na katu haijuzu kwa muislamu kubagua (kutofautisha) yeyote miongoni mwa mitume wa Allah, kama alivyosema: "*Mtume ameamini yaliyo teremshwa kwake kutoka kwa Mola Mlezi wake, na Waumini vile vile. Wote wamemuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake na Mitume wake. Hatutafautishi baina ya yeyote katika Mitume wake, na (Waumini) husema: Tumesikia na tumet'ii. Tunakutaka maghfira Mola Mlezi wetu! Na marejeo ni kwako*"[1]. Uislamu unalingania kuwe na mazungumzo (mdahalo) na *Ahlul-kitab* (waliopewa kitabu kabla ya waislamu – Mayahudi na Manaswara) na kujadiliana nao kwa wema, amesema Allah SWT: "*Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njooni kwenye neno lilio sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe na chochote; wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa Waola Walezi badala ya Mwenyezi Mungu. Na wakigeuka basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu*"[2].

8) Kuingia katika uislamu (kusilimu) kunatakiwa kufanyike kwa uhuru kamili wa mhusika bila ya utenzwaji nguvu wa aina yoyote, au ghilba au kutumia shida (haja) zake kuwashurutisha wasilimu wale wanaolinganiwa, Allah amesema: "*Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anaye mkataa Shet'ani na akamuamini Mwenyezi Mungu bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisicho vunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua*"[3], pia akasema tena: "*Angelitaka Mola wako Mlezi wangeliamini wote waliomo katika ardhi. Je, wewe utawalazimisha watu kwa nguvu mpaka wawe Waumini?*"[4].

---

[1] Surat al-Baqarah: 285.
[2] Surat Aal-Imran: 64.
[3] Surat al-Baqarah: 256.
[4] Surat Yunus: 99.

9) Nafsi (roho) ya binadamu katika uislamu inalindwa na kuhifadhiwa, kuua roho ya mtu mmoja katika uislamu ni sawa na kuua watu wote, aidha kuhuisha roho ya mtu mmoja ni sawa na kuhuisha watu wote, na hivyo hivyo ndivyo ilivyokua kwenye dini zilizoteremshwa na Allah kabla ya uislamu, amesema Allah SWT: "*Kwa sababu ya hayo tuliwaandikia Wana wa Israili ya kwamba aliye muuwa mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewauwa watu wote. Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote. Na hakika waliwajia Mitume wetu na hoja zilizo wazi. Kisha wengi katika wao baada ya haya wakawa waharibifu katika nchi*"[1].

10) Uislamu umeharamisha dhulma dhidi ya waislamu na wasiokua waislamu, na kuikemea vibaya sana, aidha uislamu umeharamisha kuwafanyia wengine uadui na kulifanya jambo hilo kua ni ufisadi (uharibifu) mkuu katika ardhi na madhambi makubwa katika uislamu, kama alivyosema Allah SWT: "*Wala msifanye uharibifu katika nchi baada ya kuwa imekwisha tengenezwa.*"[2], akaendelea kusema: "*Sema: Mola Mlezi wangu ameharimisha mambo machafu ya dhahiri na ya siri, na dhambi, na uasi bila ya haki, na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na asicho kiletea uthibitisho, na kumzulia Mwenyezi Mungu msiyo yajua*"[3], na kwa ukubwa wa dhambi la ufisadi (uharibifu) katika ardhi; adhabu iliyowekwa inanasibiana na ukubwa huo, pale Allah SWT aliposema: "*Basi malipo ya wale wanao mpiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wakawania kufanya uchafuzi katika nchi, ni kuuwawa, au kusalibiwa, au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho, au kutolewa nchi. Hii ndiyo hizaya yao katika dunia; na katika Akhera watapata adhabu kubwa*"[4], ukali wa adhabu hii uko wazi kwenye hii adhabu ya '*hiraba*' (uharibifu katika ardhi) na dhulma.

11) Familia katika uislamu ndio msingi wa kuijenga jamii, hivyo haijuzu kuivuruga familia au kuikosea; familia inajikita kwenye msingi wa

[1] Surat al-Maidah: 32.
[2] Surat al-A'raaf: 56.
[3] Surat al-A'raaf: 33.
[4] Surat al-Maaidah: 33.

ndoa yenye utulivu, mapenzi na huruma, amesema Allah SWT: "*Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao fikiri*"[1].

12) *Salam* (amani) ni nembo iliyo wazi kabisa miongoni mwa nembo za kiislamu, na ni msingi wa mahusiano (maingiliano) na wengine, ni katika mafundisho ya msingi kabisa kuwafanyia wema wale wanaoishi kwa amani, amesema Allah SWT: "*Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu*" akaendelea kusema: "*Hakika Mwenyezi Mungu anakukatazeni kufanya urafiki na wale walio kupigeni vita, na wakakutoeni makwenu, na wakasaidia katika kufukuzwa kwenu. Na wanao wafanya hao marafiki basi hao ndio madhaalimu*"[2]. Pia akasema tena: "*Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanao kupigeni, wala msianze uadui. Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi waanzao uadui*" [3], kwa maana hio sharia (amri) ya kupigana jihad imekuja kama njia ya kuzuia uadui na kulinda mipaka ya nchi na kuondosha vikwazo vyote vinavyowakwaza watu (binadamu) na kutomjua (kutomuamini) Allah na dini yake ya mwisho, aidha, jihad pia inalenga kuwanusuru wanyonge wanaodhulumiwa na wanaozuiwa kutekeleza haki yao ya kumuamini Allah na kumuabudu, amesema Allah SWT: "*Na mna nini msipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu na ya wale wanao onewa, wanaume na wanawake na watoto, ambao husema: Mola Mlezi wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhaalimu, na tujaalie tuwe na mlinzi anaye toka kwako, na tujaalie tuwe na wa kutunusuru anaye toka kwako*"[4]. Vikwazo vinatakiwa viondoshwe hadi kusumua mizizi ya fitna; isiwepo tena, na dini itakayobaki iwe ni ya Allah, amesema Allah SWT: "*Na piganeni nao mpaka isiwepo fitna na mateso, na Dini yote iwe kwa*

[1] Surat al-Rum: 21.
[2] Surat al-Mumtahanah: 8,9.
[3] Surat al-Baqarah: 190.
[4] Surat al-Nisaa: 75.

ajili ya Mwenyezi Mungu. Lakini wakiacha, basi hakika Mwenyezi Mungu anayaona wanayo yatenda"[1], kwa maana hio, jihad katika uislamu inalenga kuzuia uadui, kuondosha vikwazo vinavyowakwaza watu na kutomjua Allah SWT au kuingia katika uislamu na kuwanusuru wanyonge wanaodhulumiwa katika ardhi.

13) Haijuzu kuwafanyia wengine uadui pasina haki; iwe ni kwenye nafsi (roho) zao, heshima zao na mali zao, na kwa anaefanyiwa uadui ana haki ya kujilinda na kurudisha uadui huo dhidi ya dini, roho, heshima na mali lakini bila ya kuchupa mipaka, amesema Allah SWT: "*Anaye kushambulieni nanyi mshambulieni, kwa kadiri alivyo kushambulieni. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu yu pamoja na wachamngu*"[2], akasema tena: "*Na mkilipiza basi lipizeni sawa na vile mlivyo adhibiwa. Na ikiwa mtasubiri, basi hakika hivyo ni bora zaidi kwa wanao subiri*"[3].

14) Kushuka chini kwa minajili ya kutafuta amani-adilifu itakayohifadhi haki pamoja na maadui, ni jambo adhimu katika uislamu, Allah amesema: "*Na wakielekea amani nawe pia elekea, na mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua*"[4], uvunjaji wa ahadi na khiyana ni miongoni mwa mambo yaliyoharamishwa, kama alivyosema Allah SWT: "*Na ukichelea khiana kwa watu fulani basi watupilie ahadi yao kwa usawa. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi makhaini*"[5].

15) Katika mambo yaliyowazi kabisa katika dini hii adhimu ya uislamu ni kukemea kwa nguvu zote; aina zote za kile kinachoitwa: 'ugaidi' siku hizi, kuua wasiokua na hatia, kudhulumu wanafamilia, kulipua miji na vijiji, kuharibu mali na heshima kwa njia za kihuni na kishenzi, na pia kuufanyia uadui Masjid al-Aqsa na milipiko inayojiri ndani ya misikiti. Ikiwa uislamu wenyewe unakemea yote hayo; kuendelea kuutaja

[1] Surat al-Anfaal: 39.
[2] Surat al-Baqarah: 194.
[3] Surat al-Nahl: 126.
[4] Surat al-Anfaal: 61.
[5] Surat al-Anfaal: 58.

uislamu na kuulinganisha na ugaidi hio nayo pia ni dhulma nyingine na uadui, na kwa maana hio ipo haja kubwa ya kua na kampeni pana ya kimawasiliano ili kubainisha ukweli na uhalisia wa dini hii, aidha, kubainisha nafasi kuu ya uislamu ambayo inamimina kheri nyingi kwa binadamu wote na manufaa kwao ya hapa duniani na kesho akhera. Juhudi hizi zinatakiwa pa ziwepo kwenye mitaala ya masomo.

16) Huruma, upole, kusamehe, ukarimu na ukweli ni miongoni mwa sifa-maadili alizokua nazo Mtume Muhammad SAW na kujipamba nazo, waislamu nao wanatakiwa kumuiga Mtume wao na kujipamba na sifa njema kama hizo kwenye miamala yao iwe ni baina yao au na kati yao na wengine, amesema Allah SWT: "Na vivyo hivyo tumekufanyeni muwe Umma wa wasitani, ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe ni shahidi juu yenu"[1], pia akasema tena: "*Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungeli kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia. Basi wasamehe, na waombee maghfira, na shauriana nao katika mambo*"[2], akaendelea tena kusema: "*Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana*"[3].

17) Msimamo wa ukatinakati, ulingano na kutolemea upande mmoja; ndio njia inayowalazimu waislamu kuifuata katika mambo yao, *tatwarruf* (misimamo ya siasa kali) na *ghuluw* (kuchupa mipaka) ni madhambi yaliyoharamishwa, amesema Allah SWT: "*Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Msipite kiasi katika dini yenu bila ya haki. Wala msifuate matamanio ya watu walio kwisha potea tangu zamani, na wakawapoteza wengi, na wenyewe wakapotea njia iliyo sawa*"[4]. Katika masimulizi ya Bibi (*Sayidatna*) Aisha RA kuhusu silka za Bwana Mtume SAW, alisema: "Anapochaguzwa baina ya mambo mawili, basi huchagua jepesi lao iwapo hakuna dhambi, ima ikiwa kuna dhambi basi anakua mbali

[1] Surat al-Baqarah: 143.
[2] Surat Aal-Imran: 159.
[3] Surat al-Ahzaab: 21.
[4] Surat al-Maaidah: 77.

kabisa”[1], maadili haya ya ‘ukatinakati, ulingano na kutolemea upande mmoja’ yanadhihiri kwa uwazi kwenye hukmu mbalimbali za kisharia; kusudio la sharia liko wazi kwenye kujumuisha roho na mwili, amesema Allah SWT: “*Na nitakapo mkamilisha na kumpulizia roho inayo tokana nami, basi muangukieni kwa kumt'ii*”, aidha, inajumuisha maslahi ya umma na maslahi binafsi, na baina ya malipo ya kidunia na yale ya kiakhera, imepokelewa kutoka kwa al-Nuuman ibn Bashir RA kutoka kwa Mtume SAW akisema: “*Mfano wa yule anaesimama juu ya mipaka ya Allah na yule anaechupa mipaka hio, ni kama mfano wa watu wanaosafiri kwenye safina (meli au jahazi), baadhi yao wakawa sehemu (gorofa) ya juu na wengine wako sehemu ya chini, wale waliopo sehemu ya chini kila watakapo maji (ya kunywa) ilibidi wapande juu, basi wakasema: kwa nini tusitoboe sehemu yetu hii ya chini ili tupate maji kiurahisi na bila ya kuwaudhi wenzetu waliopo juu, sasa hapa, lau wale waliopo juu watawaachia watu waliopo chini waendelee na mpango wao huo bila shaka wataangamia wote, lakini wakiwakataza basi watasalimika (okoka) wote vilevile*”[2].

18) Ushirikiano miongoni mwa binadamu ni kiunganishi cha kivitendo na kuimarisha mahusiano mazuri baina ya wafuasi wa uislamu na wengine, lengo la ushirikiano ni kutafuta kheri kwa binadamu, utofauti wa dini, rangi na jinsia badi si sababu za watu kutoshirikiana au kupunguza viwango vya ushirikiano, amesema Allah SWT: “*Wala kuwachukia watu kwa kuwa wali- kuzuilieni kufika Msikiti mtakatifu kusikupelekeeni kuwafanyia uadui. Na saidianeni katika wema na uchamngu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu*”[3].

19) Wasiokua waislamu waishio kwenye nchi za kiislamu wana haki sawa na zile za waislamu, aidha, wana uhuru kamili wa kubaki kwenye dini zao na itikadi (imani) zao na kutekeleza ibada zao, amesema Allah

[1] Imepokewa na imam al-Bukhari kwenye ‘Sahih’ yake; juzuu 4, uk. 189, hadith namba 3560. Aidha, imepokwa na imam Muslim kwenye ‘Sahih’ yake; juzuu 4, uk. 1813, hadith namba 2327.
[2] Imepokewa na imam al-Bukhari kwenye ‘Sahih’ yake; juzuu 3, uk. 139, hadith namba 2493.
[3] Surat al-Maaidah: 2.

SWT: "*Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu*"[1], akasema tena: "*Hapana kulazimisha katika Dini*"[2]. Ahadi ya Mtume SAW au ile inayojulikana kama '*Katiba ya Madina*' iliyoharirwa kwa agizo la Bwana Mtume SAW kwa raia na jamii ya watu wa Madina; imekua ndio msingi wa kusimamia na kuratibu mahusiano ya jamii zote za Madina baada ya Mtume SAW kuhamia hapo na kuasisi jamii ya kiislamu na dola yake hapo, katiba hii imeweka msisitizo juu ya msingi huu adhimu na misingi mingine inayosimamiwa na uislamu, kwa maana hio ndio kumekua na haja na umuhimu wa mazungumzo na majadiliano kwa wema ili kujenga uwiano wa kijamii ulio madhubuti. Waislamu walipokua wakifutahi (wakifungua) miji mbalimbali waliutekeleza msingi huu kivitendo na walikua wakisema: "Haki zao sawa na zetu, nyajibu zao sawa na zetu", 'kodi ya *jizya*' waliokua wakilipa wasiokua waislamu ni mukabala wa ulinzi waliokua wakipata, ndio maan siku moja kiongozi wa kiislamu Abu-Ubaida ibn al-Jarraah alikataa kuchukua 'kodi ya *jizya*' na kuwarudishia watu wa mji wa '*Homs*' baada ya kuufungua mji huo, akiwaambia mpaka pale atakapoanza kuwalinda ndipo atakapoanza kupokea kodi hio ya '*jizya*'. Kwenye tukio lingine, waislamu waliondoa jeshi lao kutoka mji wa '*Samarkand*' waliokua wameshauchukua lakini amri ya mahkama ikawataka waondoe jeshi hilo, ilipobainika kua jeshi hilo liliuchukua mji huo kabla ya kuwalingania na kuwabainishia wakazi (wenyeji) wake uislamu na kuwapa hiari ya kuchagua na kuwapatia muhula kwa mujibu wa taratibu za jihad katika uislamu. Kwa upande mwengine uislamu umetilia nguvu suala la kuwapatia haki zao, jamii za wachache (minorities) wasioukua waislamu wanaoishi kwenye jamii (dola) ya kiislamu, na kuwaacha waendelee na imani zao na nyumba zao za ibada na kuwapatia uhuru kamili wa kutekeleza mafundisho ya dini zao pamoja na kuharamisha kuwaharibia makanisa yao, pia uislamu umejishughulisha na waislamu wachache

[1] Surat al-Mumtahanh: 8.

[2] Surat al-Baqarah: 256.

(minority) wanaoishi katika nchi zisizokua za kiislamu kwa sharti ya kua nao wataendelea kulinda dini yao na utambulisho wao.

20) Utawala wa kiislamu wa serikali ya Madina (wakati wa Mtume SAW na makhalifa wake baada yake) unatoa mfano hai kwa mkataba wa amani aliouandika Mtume SAW alipofika Madina, uliowakikishia 'Jamii ya Mayahudi wa Madina' kua watakua na amani katika dini yao na mali zao, alisema Mtume SAW: "*Mayahudi wana dini yao*"[1].

21) Uislamu, katika uhalisia wake, ni ulinganizi wa uadilifu, haki, na kuheshimu haki za wengine, bila ya kutizama dini au rangi au jinsia au lugha, dhulma ni haramu; imeharamishwa hata kuwafanyia maadui, Allah ameseme: "*Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mzirudishe amana kwa wenyewe. Na mnapo hukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu. Hakika haya anayo kuwaidhini Mwenyezi Mungu ni mazuri sana. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kuona*"[2], akasema tena: "*Enyi mlio amini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkitoa ushahidi kwa haki. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda*"[3], na imekuja katika 'Hadith Qudsiy', amesema Allah SWT: "*Enyi waja wangu; Hakika ya Mimi (Allah) nimejiharamishia dhulma juu ya nafsi yangu, na nikaifnya kua haramu baina yenu, kwa hio musidhulumiane*"[4].

22) Kushikamana na (kamba ya) Allah, umoja na ushirikiano miongoni mwa waislamu, ndio ngome thabiti (madhbuti) ya kuwaunganisha waislamu na kuwaletea furaha na kuwafurahisha hapa duniani na kesho akhera, lakini kua mbali na Allah, na kufarikiana kwa waislamu, bila shaka itakua ndio njia yao ya balaa na sababu ya mateso na dhiki kwao, amesema Allah SWT: "*Na atakaye jiepusha na mawaidha*

[1] Barua ya Mtume SAW; inayopatikana ndani ya 'Katiba ya Madina'.
[2] Surat al-Nisaa:58.
[3] Surat al-Maaidah: 8.
[4] Imepokewa na imam Muslim kwenye 'Sahih' yake, mlango wa kuharamisha dhulma, juzuu 4, uk. 1994, hadith namba 2577.

yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu"[1], akasema tena: "*Na shikamaneni kwa Kamba ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja, wala msifarikiane*"[2], akaendelea tena kusema: "Na mwenye kushikamana na Mwenyezi Mungu basi huyo ameongozwa kwenye Njia Iliyo Nyooka"[3]. Hakika ya ushirikiano na mshikamano miongoni mwa waislamu kielimu (kisayansi), kiuchumi na kijeshi ndio dhamana ya nguvu zao na njia ya kutoshelezana na kusimamisha maisha bora kwa raia wao, na ni sababu utulivu, maendeleo na amani katika nchi zao, amesema Allah SWT: "Na saidianeni katika wema na uchamngu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu"[4].

23) Uislamu pia umejihusisha sana na haki za jirani, bila ya kujali imani (dini) yake, ukahimiza kumkirimu jirani kama alivyosema Allah SWT: "*Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni wema wazazi wawili na jamaa na mayatima na masikini na jirani wa karibu na jirani wa mbali, na rafiki wa ubavuni na mpita njia, na walio milikiwa na mikono yenu ya kulia. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kiburi wanao jifakhiri*"[5], na Mtume SAW akasema juu ya suala la jirani, akishadidia kwa kuapa mara tatu (3): "*Naapa kwa Allah; hatoamini, Naapa kwa Allah; hatoamini, Naapa kwa Allah; hatoamini, wakasema (maswahaba): nani ya rasulallah; akasema: yule ambae jirani yake hana amani na vitimbi vyake*"[6].

24) Uislamu, umesisitiza na kuhimiza suala la elimu (za aina zote), amesema Allah SWT: "*Kwa hakika wanao mcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye*

[1] Surat Ta-Ha: 124.
[2] Surat Aal-Imran: 103.
[3] Surat Aal-Imran: 101.
[4] Surat al-Maaidah: 2.
[5] Surat al-Nisaa: 36.
[6] Imepokewa na imam al-Bukhari kwenye 'Sahih' yake, mlango wa madhambi kwa ambae jirani yake hana amani na vitimbi vyake, juzuu 8, uk. 10, hadith namba 6016.

nguvu, Mwenye kusamehe"[1], na kama tujuavyo, aya za kwanza kabisa zilizoteremka kwenye Qur'an zilihimiza suala la kusoma, akasema Allah SWT: "*1. Soma kwa jina la Mola wako Mlezi aliye umba, 2. Amemuumba binaadamu kwa tone la damu, 3. Soma! Na Mola wako Mlezi ni Karimu kushinda wote! 4. Ambaye amefundisha kwa kalamu, 5. Kamfundisha mtu aliyo kuwa hayajui*"[2].

25) Katika Uislamu ni wajibu kufanya kazi na kuhangaika katika ardhi kwa ajili ya kutafuta rizki, amesema Allah SWT: "*Na itakapo kwisha Sala, tawanyikeni katika nchi mtafute fadhila za Mwenyezi Mungu, na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi ili mpate kufanikiwa*"[3], akasema tena: "*Yeye ndiye aliye idhalilisha ardhi kwa faida yenu, basi tembeeni katika pande zake, na kuleni katika riziki zake. Na kwake Yeye ndio kufufuliwa*"[4]. Kwa hakika njia ya pekee kwa waislamu na nchi zao kuinuka kiuchumi na nchi kuneemeka na maishas kua mazuri ni kwa kufanya kazi yenye tija kwa bidii, hata mitume wa Allah nao pia walikua wakifanya kazi. Shwahaba mtukufu; al-Miqdam ibn Ma'ad Yakrib amepokea kutoka kwa Mtume SAW akisema: "Hakuna anaekula chakula bora na kizuri zaidi kuliko kile alichokichuma kwa jasho lake, na Nabii (Mtume) wa Allah Daud alikua akila chakula kitokanacho na jasho (kazi) lake"[5]. Zipo dalili (ushahidi wa aya) nyingi katika Qur'an na Sunnah za Bwana Mtume SAW juu ya suala hili. Amesema al-Imam al-Ghazali RA katika kitabu chake cha '*Ihyaa Uloom al-Din*': "*Lau watu wataacha shughuli za kutengeneza bidhaa na shughuli za kilimo; basi maisha yote yatachafuka, na watu wengi kuangamia, ili mambo ya watu yatiririke kwenye nidhamu ni lazima washirikiane, na kila kundi la watu washughulikie wadhifa fulani, na lau watu wote watashughulikia kazi aina moja tu; basi shughuli nyengine*

[1] Surat Faatir: 28.
[2] Surat al-'Alaq: 1 – 5.
[3] Surat al-Jumu'ah: 10.
[4] Surat al-Mulk: 15.
[5] Imepokewa na imam al-Bukhari kwenye 'Sahih' yake; 'mlango wa chumo la mtu na kazi ya mkono wake', juzuu 3, uk. 57, hadith namba 2072.

zitaharibika na watu wataangamia"[1]. Jamii ya kiislamu ni jamii inayosaidiana na kushikamana, amepokea al-Nu'man ibn Bashir RA kutoka kwa Mtume SAW akisema: "*Mfano wa waumini (waislamu) katika kupendana kwao na kuhurumiana kwao na kusaidiana kwao, ni kama mfano wa kiwiliwili kimoja kinapougua kiungo kimoja cha mwili huo basi mwili mzima unashikamana na kiungo hicho kwa homa na kukesha*"[2]. Akasema tena mtume SAW: "*Hatoamini mmoja wenu (imani ya kweli) mpaka ampendelee (mazuri) nduguye (muislamu) lile analojipendelea nafsi yake*"[3].

26) Ili kufikia maendeleo jumuishi; ni lazima kwa waislamu wafanye kazi kwa bidii na kuongeza juhudi katika kuinua hali za kimaisha na kimaendeleo za nchi zao katika nyanja zote; kilimo, kiviwanda, kijeshi na kimatibabu, ili nchi za kiislamu zishike nafasi yake ya juu kimaendeleo duniani, na njia muwafaka ya kufikia hayo ni kuchangamkia elimu za sayansi, teknolojia na elimu nyenginezo mbalimbali kwa mujibu wa alivyosema allah SWT: "*Basi waandalieni nguvu kama muwezavyo, na kwa farasi walio fungwa tayari-tayari, ili kuwatishia maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu, na wengineo ambao hamwajui, lakini Mwenyezi Mungu anawajua*"[4], na akasema tena: "*Na tukamfundisha kuunda mavazi ya vita kwa ajili yenu ili yakuhifadhini katika kupigana kwenu. Je! Mtakuwa wenye kushukuru?*"[5].

27) Kusuluhisha na kupatanisha baina ya (makundi ya) waislamu na kuzuia uasi na uadui ni katika matakwa ya kisharia, amesema Allah SWT: "*Na ikiwa makundi mawili katika Waumini yanapigana, basi*

[1] Abu Hamid al-Ghazali, Ihyaa Uloom al-Din, juzuu 2, uk. 6.
[2] Imepokewa na imam al-Bukhari kwenye 'Sahih' yake; 'mlango wa huruma za watu na wanyama', juzuu 1, uk. 12, hadith namba 6011.
[3] Imepokewa na imam al-Bukhari kwenye 'Sahih' yake; 'mlango wa ni katika imani mtukumpendelea nduguye lile analolipendelea nafsi yake', juzuu 1, uk. 12, hadith namba 13. aidha imepokewa na imam Muslim kwenye 'Sahih' yake; 'mlango wa miongoni mwa mambo ya imani ni mtu kumpendelea nduguye lile analolipendelea nafsi yake katika kheir', juzuu 1, uk. 67, hadith namba 45.
[4] Surat al-Anfaal: 60.
[5] Surat al-Anbiya: 80.

yapatanisheni. Na likiwa moja la hao linamdhulumu mwenzie, basi lipigeni linalo dhulumu mpaka lirejee kwenye amri ya Mwenyezi Mungu. Na likirudi basi yapatanisheni kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanao hukumu kwa haki"[1], na kutofanya hivyo basi kutaendeleza fitina, mivutano na migogoro katika nchi za kiislamu, fitna ni mlango wa shari nyingi na balaa ambao mlango huo ni lazima ufungwe na uwekwe mbali kwa njia yoyote ile inayowezekana, mlango huu utazidi kudhoofisha waislamu na kuwavunja nguvu zao na kuwakata mapande mapande, na kuwawezesha maadui zao wanaowavizia kupata nafasi ya kuwaingia, amesema Allah SWT: "*Na jikingeni na Fitna ambayo haitowasibu walio dhulumu peke yao kati yenu. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu*"[2], pia akasema tena: "*Na mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala msizozane mkaingiwa woga, na zikapotea nguvu zenu. Na subirini. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanao subiri*"[3].

28) Mshikamano wa kijamii (*social solidarity*) miongoni mwa waislamu ni agizo la msingi na wajibu katika dini hii, kwa wanafamilia wa akraba (*relatives*) kusaidiana wao kwa wao, kuwasaidia mafakiri na maskini kwa kuwapatia haki yao kutokana na mali ya matajiri na mali ya zaka ni miongoni mwa nyajibu za kisharia, kusaidiana kupitia sadaka mbalimbali, zawadi na kuweka waqfu na mnjia nyenginezo, yote hayo ni matakwa ya lazima kisharia, kusaidiana na kushikamana ni miongoni mwa njia za kuleta amani katika jamii na ndio siri ya utulivu wa kijamii, kamaalivyosema Allah SWT: "*Na mpe aliye jamaa yako haki yake, na masikini, na msafiri; wala usitumie ovyo kwa fujo*"[4], akasema tena: "*Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo, na uwaombee rehema. Hakika maombi yako ni utulivu kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua*"[5]. Amepokea Ibn Abbas RA kutoka kwa Mtume SAW wakati anamtuma Mu'adh RA kwenda

[1] Surat al-Hujuraat: 9.
[2] Surat al-Anfaal: 25.
[3] Surat al-Anfaal: 46.
[4] Surat al-Israa: 26.
[5] Surat al-Taubah: 103.

Yemen alimwambia hivi: "*Walinganie kwenye kushuhudia kua; hapana mola wa kuabudiwa kwa haki ispokua Allah SWT, na kwamba mimi (Mtume) ni Mtume wa Allah (Shahada mbili), wakilikubalia hilo; basi wajulishe kua Allah SWT amawafaradhishia swala tano kila siku; mchana na usiku, wakilikubalia hilo; basi wajulishe kua Allah SWT amewafaradhishia kutoa zaka; ambazo zitachukuliwa kutoka kwa matajiri wao na kugawiwa maskini wao*"[1].

29) Kuhakikisha maisha yenye heshima kwa kila mtu kwenye jamii bila ya kujali imani (dini) ni msingi wa dhati katika misingi ya dini hii adhimu. Siku moja Sayidna Umar ibn al-Khattab RA katika tembetembea zake, alimuona mtu mzima wa kiyahudi (yuko barabarani, anaomba), akamuliza; "*una shida gani?*" akasema: 'sina mali, na mimi nimekua nikilipa *jizya*, hapa Umar RA akasema: "*Hatujakutendea haki; tulikula kodi yako ya jizya (ni wazi mzee huyu alikua sio muislamu) ulipokua na afya yako, na bado tuendelee kukudai katika umri huu?*" hapohapo Umar RA akatoa agizo kwa magavana wake mikoani kote kua: "*si ruhusa kuendelea kuchuka kodi ya jizya kutoka kwa watu wazima na badala yake Baitul-Maal (hazina ya waislamu) iwatizame watu kama hawa*"[2]. Siku moja Khalifa Umar ibn Abdulaziz RA alituma ujumbe kwa gavana wake wa Basra akimwambia: "*Tizama Ahlul-Dhimma (wasiokua waislamu wanaoishi kwenye dola ya kiislamu) wa mkoa wako ambao wamekua watu wazima na wamedhoofika kiafya na hawana tena uwezo wa kuchuma (kufanya kazi); basi wapatie kutoka 'Baitul-Maal' kitakachowasaidia kujikimu*"[3]. Maendeleo-jumuishi katika nyanja zote ni katika mafundisho ya dini hii adhimu, na yote hayo yanahitaji uandaaji wa mipango na mikakati madhbuti kuyafikia malengo haya.

---

[1] Imepokewa na imam al-Bukhari kwenye 'Sahih' yake; 'mlango wa: kuwatuma Abu-Musa na Mu'adh kwenda Yemen', juzuu 5, uk. 162, hadith namba 4347.

[2] Kisa hiki kimesimuliwa na Ibn Zanjawayh kwenye kitabu chake: 'Kitab al-Amwaal' mlango wa: 'kodi ya jizya na kiwango chake' juzuu 1, uk. 162, ibara namba 165.

[3] Imesimuliwa na Ibn Zanjawayh kwenye kitabu chake: 'Kitab al-Amwaal' mlango wa: 'ukusanyaji wa jizya na kodi na kua na huruma kwa walipaji na kutowaburuza' juzuu 1, uk. 162, ibara namba 169, 179.

30) Kwa mujibu wa maelezo tuliyoyabainisha kuhusiana na dini hii adhimu, ambayo maelezo hayo ndio yamekua misingi ya 'Maamuzi na Maazimio ya Kongamano' mbalimbali katika kadhia mbalimbali zilizowasilishwa na kutolewa maamuzi yake hususan kwenye nyanja za kisharia kama vile; mambo ya aqeeda, ibada, miamala, makosa ya jinai, *akhlaaq* (maadili) na kila yanayohusiana na jamii ya kibinadamu, ambayo hayana budi yapatiwe ufumbuzi wake wa kisasa kutoka kwenye maelekezo na mafundisho ya uislamu, mambo ambayo ndio kiini cha ulinganizi (da'wah) wa kiislamu kwa ufahamu sahihi wakati wa ufafanuzi wa masuala ya kiuchumi, kimatibabu, kifamilia, kifikra na kisayansi na mengineo, amesema Allah SWT: "*Sema: Hii ndiyo Njia yangu - ninalingania kwa Mwenyezi Mungu kwa kujua - mimi na wanao nifuata. Na ametakasika Mwenyezi Mungu! Wala mimi si katika washirikina*"[1]. Kuyafikia haya; inahitajika uandaaji makini wa walinganiaji (Ma-*Du'at*) na *Ulamaa* (wanazuoni) wabobezi watakaowezana na changamoto za zama hizi, na watakaofahamu uhalisia wa kina wa dini hii na hali ilivyo ya jamii za kisasa, na watakaolingania watu kwa Allah kwa kutumia njia za hikma na busara na mawaidha yaliyokua mazuri pamoja na kujadiliana kwa taratibu mzuri kwa mujibu wa maelekezo ya Allah SWT pale aliposema: "*Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hikima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako Mlezi ndiye anaye mjua zaidi aliye ipotea Njia yake, na Yeye ndiye anaye wajua zaidi walio ongoka*"[2].

Mwisho tunapeleka swala na salamu kwa Mtume wetu Muhammad SAW na kwa Aali zake na maswahaba wake.

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kislamu

23 Swafar (Mfungo tano, 1440 Hijria, sawa na 1 Novemba, 2018

≅≅≅

[1] Surat Yusuf: 108.

[2] Surat al-Nahl: 125.

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Ishirini na Nne (24) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Dubai, UAE

7 - 9 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1441 Hijria

sawa na 4 - 6 Novemba, 2019

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 230 (1/24)

Yanayohusiana na 'Kuidurusu Mikataba-Mierevu (*Smart Contracts*) na Kwa Kiasi Gani Inafungamana na Sarafu za Kidigitali'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na nne (24) kilichofanyika Dubai (UAE) tarehe 7 - 9 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1441 Hijria, sawa na 4 - 6 Novemba, 2019.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kuidurusu Mikataba-Mierevu (*Smart Contracts*) na Kwa Kiasi Gani Inafungamana na Sarafu za Kidigitali, na namna ya kuifanyisha kazi na kuisitisha,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya 'Azimio la Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu' namba 52 (3/6) lililohusiana na: '*Hukmu ya Mikataba Kupitia Vyombo vya Mawasiliano vya Kisasa*' kikopitishwa kwenye kikao chake cha sita (6) kilichofanyika Jeddah, tarehe 1410 Hijria, sawa na 1990 kwenye vipengele vyake vyote, 'Azimio' hili lilifungamana na 'mikataba ya kielektroniki' ambayo ni tofauti na hii 'mikataba-nyerevu' (*smart contracts*).

Mbili: Maana ya 'mikataba-mierevu': Ni mkataba baina ya pande mbili unaofungika wenyewe (*automatic*) uliojikita kwenye dhana ya 'wawili wanaolingana' (bila ya kuwepo mtu wa kati) kupitia mtandao-gavi (*blockchain*) na unaojifanyisha kazi kupitia sarafu za kidigitali (zilizowekwa simbo) kama vile '*bitcoin*' na mfano wake.

Tatu: Mikataba-mierevu inafungwa kupitia majukwaa mahsusi yanayodhibitiwa, au majukwa ya umma yasiyodhibitiwa lakini yanatumia, kwa aghalabu, sarafu za kidigitali (zilizowekwa simbo).

Nne: Imeamuliwa na ‘Kongamano’ kuakhirisha uchukuaji wa ‘Maamuzi’ juu ya maudhuia haya hadi pale itakapofanyika ‘Warsha-tahasusi’ itakayoangazia ‘Mikataba-mierevu’, na baada ya kutizama kwa kina maudhui ya ‘sarafu za kidigitali (zilizowekwa simbo)’ ili kuweza kudurusu nyanja zote za ‘Mikataba-mierevu’ pamoja na kuangazia yaliyoelezewa kwenye kifungu: (mbili), itakua vizuri waalikwe wataalamu wenye tahasusi katika mas’ala ya ‘*blockchain*’ na ‘sarafu za kidigitali (zilizowekwa simbo)’ na mengineo.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 231 (2/24)

Yanayohusiana na 'Ufumukaji-Bei na Kubadilika kwa Thamani ya Sarafu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na nne (24) kilichofanyika Dubai (UAE) tarehe 7 - 9 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1441 Hijria, sawa na 4 - 6 Novemba, 2019.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Ufumukaji-Bei na Kubadilika kwa Thamani ya Sarafu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya 'Azimio la Kongamano' namba 42 (4/5) lilichokuliwa kwenye kikao chake cha tano (5), ambapo 'Kongamano' lilionelea kua linatekelezwa iwapo hakuna ufumukaji-bei au iwapo mfumuko-bei ni hafifu.

Mbili: Ama iwapo mfumuko wa bei ni mkubwa basi pande husika watakadiria vile watakavyoridhiana, ikishindikana kuridhiana basi ima watakwenda mahkamani au waangalie mpatanishi kulingana na mazingira.

Tatu: Iwapo kumepatikana mfumuko wa bei mkubwa baada ya kuingia kwenye deni; basi hamna katazo la kukubaliana mdai na mdaiwa wakati wa kulipana ima kwa kulilipa deni hilo kwa thamani au wapatane kusaidiana madhara baina ya pande mbili, aidha inajuzu kupatanishwa na mahkama au na mpatanishaji, lakini haijuzu kupatana kwa hilo wakati wa kufunga mkataba.

Nne: 'Kongamano' linaweka msisitizo kwa serikali za kiislamu juu ya mapendekezo yake yaliyoainishwa kwenye 'Azimio lake' namba 115 (912).

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 232 (3/24)

Yanayohusiana na 'Mikataba ya FIDIC (Muungano wa Kimataifa wa Wahandisi-Washauri)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na nne (24) kilichofanyika Dubai (UAE) tarehe 7 - 9 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1441 Hijria, sawa na 4 - 6 Novemba, 2019.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Mikataba ya FIDIC,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Mikataba ya FIDIC: Ni mifano na sampuli za mikataba ya kiujenzi na kihandasa inayolenga kudhibiti mahusiano baina mwenye kazi (mradi) au wakala wake, na wanaoitekeleza kazi (ujenzi) hio kwa mujibu wa mkataba, waukamilishe mradi husika ambao unakua na ncha nyingi na hatimae kukabidhi mradi ukiwa umekamilika na tayari kwa matumizi yaliyokusudiwa.

'Kongamano' linaonelea kua mkataba hii inajuzu kisharia, iwapo pande husika watalazimiana na hukmu na vigezo vya kisharia, kwa kuchukulia kipimo cha mikataba ya '*istisnaa, ijara na muqawala (ujasiriamali)*', na iwapo kutatokea mgogoro na utata basi wataenda kwa vyombo vya upatanishi kwa mujibu wa 'Azimio la Kongamano' namba 91 (8/9), aidha, inajuzu kutekeleza 'sharti la adhabu' iwapo mkandarasi amechelewa kukamilisha mradi zaidi ya mda waliokubalina, kwa mujibu wa 'Azimio la Kongamano' namba109 (3/12). Ama kile kinachoengezwa kwenye thamani kwa sababu ya mabadiliko ya mazingira ya utekelezaji au marekebisho kwenye mkataba; nyongeza hio itakua ni fidia ya madhara yaliyojitokeza.

Allah ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 233 (4/24)

Yanayohusiana na ‘Kusameheana katika Uislamu na Umuhimu wake Kijamii na Kimataifa na athari zake’

Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), katika kikao chake cha ishirini na nne (24) kilichofanyika Dubai (UAE) tarehe 7 - 9 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1441 Hijria, sawa na 4 - 6 Novemba, 2019.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye ‘Kongamano’ kuhusiana na maudhui ya **Kusameheana katika Uislamu na Umuhimu wake Kijamii na Kimataifa na athari zake,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya maamuzi, maazimio, mapendekezo na matamko mbalimbali ya Kongamano yaliyotolewa kunadi watu waishi kwa amani.

Mbili: Kusameheana ni maadili ya msingi, zipo dalili (maandiko) nyingi katika Qur’an tukufu na Sunnah za Bwana Mtume Muhammad SAW, aidha upo ushahidi wa utekeleza wa kivitendo katika sera ya Bwana Mtume Muhammad SAW na matendo ya maswahaba wake na katika historia ya kiislamu, miongoni mwa mifano hai ya utekelezaji wa maadili ya usamehevu ni yale yaliyosajiliwa kwenye ule ‘Waraka (katiba) wa Madina.

Tatu: Waislamu wameamrishwa kujipamba na tabia hii ya usamehevu miongoni mwao na baina yao (waislamu) na wengine.

Nne: Ipo haja kubwa sana ya kuyafanyia kazi maadili haya ya usamehevu na kusameheana kwenye matendo na maneno katika nyanja zote, tabia ya kusameheana ni mojawapo ya athari za watu kuishi kwa amani na mshikamano wa kijamii, aidha, maadili ya kusameheana yanalinda uwiano

na mahusiano ya kijamii, umoja wa kijamii kwa tabaka zote na umoja wa kitaifa.

Tano: ‘Kongamano’ linaunga mkono na kubariki yafuatayo:

1) Miafaka, ilani za kimataifa na juhudi mbalimbali zinazosimamiwa na nchi mbalimbali juu ya suala la kusameheana na uwiano wa kijamii.
2) Sera za dola ya Emaraat kupitia miradi mbalimbali inayolenga kujenga usamehevu na uwiano wa kijamii miongoni mwa watu (raia), jambo hili linatowa picha (taswira) halisi ya ulinganizi wa uislamu katika kusameheana.

Inausiwa yafuatayo:

- Kuingiza ‘maadili ya usamehevu na kusameheana’ kwenye mitaala ya elimu.
- Hotuba na mahubiri ya kidini yaangazie ‘maadili ya usamehevu na kusameheana’ katika nyanja zote.
- Kuyadhihirisha ‘maadili ya usamehevu na kusameheana’ kwenye vyombo vya habari-mawasiliano na vyombo vya mawasiliano ya kijamii mbalimbali.
- Kuwahimiza wanatahasusi na wanafikra mbalimbali kujishughulisha kwa kuandika na kutafsiri na kueneza ‘maadili ya usamehevu na kusameheana’ kupitia vyombo vya habari-mawasiliano.
- Kuitaka ‘Jumuia ya Umoja wa Mataifa’ na nchi wanachama kutunga sheria na kuandaa miafaka ya kimataifa itakayoharamisha ‘ubaguzi, utengaji, ukabila na urangi, na kuyafanya maovu (madhambi) haya yawe ni sehemu za katiba za nchi wanachama.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 234 (5/24)

Yanayohusiana na 'Kufikia Malengo ya Amani ya Chakula na Maji: Changamoto Kuu Zinazokabili Nchi za Kiislamu na Athari zake kwa Mustakbala wa Umma wa Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na nne (24) kilichofanyika Dubai (UAE) tarehe 7 - 9 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1441 Hijria, sawa na 4 - 6 Novemba, 2019.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kufikia Malengo ya Amani ya Chakula na Maji: Changamoto Kuu Zinazokabili Nchi za Kiislamu na Athari zake kwa Mustakbala wa Umma wa Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Amani ya Maji: Ni mazingira ya uwepo wa maji salama kwa matumizi ya binadamu na kwa kwa kiwango cha kutosheleza nchi nzima nay awe ni endelevu bila ya hofu ya kuathirika.

Mbili: Amani ya chakula: Ni mazingira ya uwepo wa chakula lishe chenye afya na salama kwa raia wote na kuhakikisha uendelevu wake kwa jamii nzima.

Inausiwa yafuatayo:

Kwa kua uislamu unalingania kulinda na kuhifadhi rasilimali za maji na chakula na unakataza kufanya israfu na ubadhirifu katika kila kitu, na kwa kila chenye kuleta madhara kwa raia na jamii; 'Baraza la Kongamano' linapendekeza yafuatayo:

1) Serikali za nchi za kiislamu zinatakiwa kulipatia suala la 'amani ya

chakula na amani ya maji' nafasi ya kipaumbele, na kutengeneza sera na programu za kuzuia israfu na kuongoza kwenye matumizi mazuri ya rasilimali hizo.

2) Waislamu wanatakiwa kisharia, kua waangalifu katika utumiaji wa rasilimali hizi za maji na chakula na kutofanya ubadhirifu.
3) Wasomi wenye tahasusi katika sayansi za maji, kilimo na mazingira, wanatakiwa kuongeza juhudi kutafuta mbinu na taratibu muwafaka zitakazosaidia kuhakikisha uwepo wa 'amani ya chakula na amani ya maji', na kufaidi kutokana na teknolojia ya mapinduzi ya kiviwanda kwenye nyanja za kusafisha maji-taka na kufaidika nayo kwa kufuata vigezo na hukmu za sharia ya kiislamu.
4) Nchi za kiislamu, zinatakiwa kuharakisha na kua na ushirikiano baina yao katika kupambana na tatizo kupungua kwa maji na chakula; kwa kuweka sera na mipango-mikakati madhbuti itakayohakikisha ukuaji wa rasilimali za maji na kuhakikisha amani ya chakula, aidha, kushirikiana na mashirika ya kikanda na ya kimataifa yanayojihusisha na harakati za maji na chakula.
5) Utumiaji wa mbinu na teknolojia za kisasa katika kuzalisha mbegu na kuboresha njia za kuendeleza kilimo ili kuinua viwango vya uzalishaji wa chakula na kufikia lengo la amani ya chakula.
6) Nchi za kiislamu, zinatakiwa kufaidi na mafundisho yaliyoletwa na sharia ya kiislamu katika kukuza na kuendeleza rasilimali za kilimo kwa kuufanyia kazi msingi wa: 'kuhuisha ardhi iliyokufa' kwa kufuata vigezo vyake vya kisharia, na kuondoa pingamizi zozote zitakazokwaza lengo la kufikia amani ya chakula.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 235 (6/24)

Yanayohusiana na 'Jinomu za Kibinadamu na Uhandisi wa Kibaiolojia wa Mustakbali

(Kutathmini Maamuzi ya Kongamano na Kubainisha Athari zake na Kutizama Changamoto Mpya)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na nne (24) kilichofanyika Dubai (UAE) tarehe 7 - 9 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1441 Hijria, sawa na 4 - 6 Novemba, 2019.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Yanayohusiana na 'Jinomu za Kibinadamu na Uhandisi wa Kibaiolojia wa Mustakbali (Kutathmini Maamuzi ya Kongamano na Kubainisha Athari zake na Kutizama Changamoto Mpya),** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya 'Azimio la Kongamano' namba 203 (9/21) lililohusiana na 'Maumbile, Uhandisi-Maumbile na Jenomu ya Binadamu' yaliyochukuliwa kwenye kikao chake cha ishirini na moja (21), kilichofanyika Riyadh, (Saudi Arabia) 15 - 19 Muharram (Mfungo Nne), 1435 Hijri, sawa na 18 – 22 Novemba, 2013.

Mbili: Teknolojia ya uhariri wa jeni kama vile (*CRISPR-CAS 9*) na nyenginezo, ni mbinu mpya za kisasa za kubadilisha na kuhariri jeni; kama vile kompyuta inavyohariri na kusahihisha makossa ya kiuchapaji na kilugha; kwa mbinu hiohio jenomu inahaririwa kwa kurekebisha vijinasaba (DNA) na kuziundaunda vile unavyotaka, na mbinu hizi za kisasa ziko barabara na makini kabisa katika kutibu na kurekebisha uhandisi-maumbile, lengo lake kuu ni kutibu magonjwa kadha wa kadha yaliyo sugu na yaliyoshindikana,

hata hivyo, mbinu hizi bado zinahitaji kufanyiwa utafiti wa ziada ili kuhakikisha na kubaini usalama wake na ufanisi wake; uhariri wa kijeni (jenomu) kwa mbinu hizi unakua ni halali yapatikanapo mashrti yanayofuata:

1) Taasisi husika za kimatibabu zihakikishe usalama na ufanisi wa utumiaji wa mbinu hizi.
2) Mbinu hizi zitumike tu kwa malengo ya kimatibabu na kutibu magonjwa ya kiurathi au kujikinga nayo, lakini inakatazwa katakata kuzitumia kwa malengo ya kiurembo na kujipendezesha.
3) Kuwepo taratibu za kinidhamu kali za kuhakikisha heshima ya wanaopitia matibabu haya inazingatiwa na kuzuia utumiaji mbovu wa teknolojia hii.

Tatu: Teknolojia (mbinu) ya kuhamisha mitokondria (*mitochondrial*): hii ni vidudu vinavyozalisha nishati kwenye seli kutoka kwenye yai la mwanamke mzima pamoja na vijinasaba (DNA) kuhamishiwa kwenda kwa mwanamke mwengine mwenye tatizo la vijinasaba vya mitokondria (tatizo hili husababisha maradhi sugu yanayoshindikana kutibika) kwa minajili ya kuweza kupata mzima, mbinu hii haijuzu; kwa sababu inapelekea kuchanganyika kwa nasaba mbalimbali.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 236 (7/24)

Yanayohusiana na 'Nafasi ya Malezi yaKidini Katika Kuimarisha Amani'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na nne (24) kilichofanyika Dubai (UAE) tarehe 7 - 9 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1441 Hijria, sawa na 4 - 6 Novemba, 2019.

Baada ya kupitia 'Mapendekezo' yaliyotolewa na 'Warsha ya Kielimu ya Kimataifa' juu ya **Nafasi ya Malezi yaKidini Katika Kuimarisha Amani,** iliyoandaliwa na 'Kongamano' hapo Rabat, (Morroco) kwa kushirikiana na 'Shirika la Kiislamu la Elimu-Malezi, Sayansi na Utamaduni' (ISESCO), na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

1) Kujishughulisha zaidi na Qur'an Tukufu; kitabu chenye uongofu kilichotoka kwa Allah Chimbuko la Hikma na Elimu, na pia kujishughulisha zaidi na Sunnah (hadith) za BwanaMtume SAW, na kuendelea kufaidika na mfumo wa kimaluezi utokanao na vyanzo viwili hivi.
2) Kuendelea kuandaa vikao, mikutano, semina na *halaqah* za kimasomo kwa ngazi za kitaifa na kikanda ndani nan je ya ulimwengu wa kiislamu juu ya suala la kuimarisha 'nafasi ya malezi ya kidini na masomo ya kidini', na pia pia kuandaa makongamano ya kimataifa na kuwashirikisha wataalamu na wanafikra ili waweze kutambulisha 'Utamaduni wa Kiislamu wa Ukatinakati'.
3) Kuzitaka nchi wanachama waunde kamati za tahasusi zitakazosimamia tafiti za kielimu fafanuzi juu ya 'mitaala ya elimu ya dini', ndani yake kuingizwe maadili ya: 'amani', 'mazungumzo-mdahalo' (*hiwaar-dialogue*) na 'uwiano wa kimaisha'.
4) Kuzitaka taasisi husika za kielimu-malezi katika nchi wanachama

waingize kwenye somo la ‘malezi ya kidini’ maadili ya amani kwenye mitaala hio ya kimasomo.

5) Kutilia mkazo kwenye mitaala ya elimu ya dini juua ya suala la utukufu aliokirimiwa nao binadamu na allah SWT, kwa kua yeye ni binadamu mwenye haki ya maisha ya heshima, haki ya elimu bora na afya nzuri na mengineo katika mahitajio-msingi ya maisha.
6) Kudhihirisha stadi na dhana ambazo zitaimarisha maadili mema ya kidini na kitaifa na muimarisha mielekeo chanya katika jamii, na kuitumikisha na kuifanyisha kazi kwenye mitaala ya malezi, mawaidha na elimu ya dini.
7) Kueneza programu za kisasa za kufundisha lugha ya kiarabu kwa wazungumzao lugha nyengine isiokua hio, kwa lengo la kuimarisha elimu ya utamaduni wa kiislamu na maadili yake.
8) Kueneza masomo ya elimu-malezi kwa kutumia vifaa vya kiteknolojia ya kisasa, ili elimu hio ienee kwa mapana zaidi na ichangie kusahihisha uhalisia wa uislamu na waislamu wenyewe.
9) Umuhimu wa kushirikiana na kufanya kazi kwa pamoja miongoni mwa wanazuoni wa dini na wanatahasusi wa elimu-malezi katika kuandaa mitaala ya elimu ya dini kwa kuowanisha taaluma za kimitaala na elimu ya dini ili kuijenga dhana ya maadili na kuisimika kwenye silka za watoto wanaoinukia.
10) Kuratibu na kushirikiana miongoni mwa vyombo vya habari-mawasiliano na taasisi za kimalezi, kida’wah, kiutamaduni na taasisi za mambo ya vijana, ili kuimarisha na kuukuza utambulisho wa kidini na kiutamaduni, aidha, kutilia nguvu uzalendo wa kitaifa na kuheshimu rai (mawazo) ya wengine.
11) Kuboresha taratibu za uandaaji wa viongozi wa kidini na wanaofanya kazi katika sekta hio.
12) Uwaandaaji mzuri kielimu na kimalezi kwa ‘walimu wa somo la dini’ katika nchi wanachama, na pia kuendelea kumtayarisha akiwa kazini kupitia miradi endelevu ya mafunzo.
13) Kuboresha mbinu na vifaa vya ufundishaji, ili ziendane na wakati na kizazi cha sasa cha utumiaji wa vifaa vya kiteknolojia vya kisasa (*multimedia*), na kutilia nguvu maadili ya maelewano (*hiwaar-dialogue*) na kujadiliana (debate), na pia kujitanua katika utumiaji wa

mbinu za harakati za kimasomo zinazonoa bongo la mwanafunzi na kumsaidia kwenye ‘ufikiri wa kimpangilio’ (*systematic thinking*) na kuutengeneza utu wa kujiamini.

14) Kuandaa na kueneza tafiti-msingi juu ya uimarishaji wa malezi ya ‘mfumo wa ukatinakati’ na ulingano; na tafiti hizo zitafsiriwe kwenye lugha hai (kuu) duniani.
15) Uanzishwaji wa vituo vya utafiti vitakavyosimamia suala zima la kuwaelekeza na kuwaongoza waislamu, na ku-*raddi* (kujibu) wale wanaoeneza fikra potofu, *ghuluw* (uchupaji mipaka) na uzindiki, waweze kujibu hoja kwa hoja kisharia na kimantiki.
16) Kuandaa semina za kimataifa katika maudhui za ‘kuzifanyisha kazi (kuwekeza) vyombo vya mawasiliano ya kijamii’ kwenye kuimarisha maadili ya amani, ukatinakati na ulingano.
17) Kuimarisha utamaduni na dhana ya amani na kujenga uwezo, stadi, maadili na misimamo ya kuleta maingiliano ya kijamii katika programu za ‘elimu ya dini’.
18) Kujihusisha zaidi na kusomesha ‘somo la fiqh’ na ‘fiqh-linganishi’ katika vyuo vikuu vya nchi wanachama kwa kufuata mfumo unaolenga kudhihirisha ‘uwepesi wa sharia’ na ‘msinigi wa kutofautiana’ na kua na ‘mawazo-tanzu’ na nafasi yake kwenye jamii yenye fikra anwai, na kua na kifua kipana cha kumkubali mwengine, na ufahamu mpana wa uwepesi wa hukmu za sharia.
19) Kuweka msisitizo juu ya elimu ya dini na kuboresha mitaala yake.
20) Kudhihirisha dhana sahihi kuhusiana na ‘mwanamke katika uislamu’, na kuingiza dhana hio kwenye mitaala ya masomo ya dini.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 237 (8/24)

Yanayohusiana na 'Sarafu za Kielektroniki (*Electronic currencies*)'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na nne (24) kilichofanyika Dubai (UAE) tarehe 7 - 9 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1441 Hijria, sawa na 4 - 6 Novemba, 2019.

Baada ya kupitia 'Mapendekezo' yaliyotolewa na 'Warsha ya Kielimu juu ya Sarafu za Kielektroniki', iliyoandaliwa na 'Kongamano', Jeddah (Saudi arabia), tarehe 10 – 11 Muharram (Mfungo nne), 1441 Hijria, sawa na 9 – 10 Septemba, 2019, na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Dhana, taratibu za kuamiliana na mambo hatarishi:

1) Kwa kua dhana ya 'sarafu za kielektroniki' ni pana; inajumuisha: kadi za mikopo (*credit cards*), kadi za malipo yaliyotangulizwa, hundi (cheki) za kielektroniki, na nyenginezo, na kwa mujibu ya hayo; mijadala ya wanazuoni ilijikita kwenye 'sarafu za kidigitali zenye simbo' *(coded*), ni miongoni mwa sarafu hizo mashuhuri zaidi ni: '*bitcoin*', '*etherium*' na '*ripple*', licha ya kua zipo tofaoti mingoni mwazo, lakini kinachozifanya sarafu hizo kua zipo tofauti na zingine, ni kua hizi ni sarafu zenye simbo (*encrypted*), lakini si aina ya sarafu inayoshikika, au yenye uwepo wa kimwili au wa kifizikia, miamala juu ya sarafu hizi hufanyika bila ya kuwepo mtu wa kati, bali hufanyika kupitia mfumo unaojulikana kama 'rika' kwa 'rika'. Sarafu hizi kwa mujibu wa tafiti zilizowasilishwa zinaweza kusanifiwa kwenye aina tatu:

   - Aina ya kwanza: 'sarafu': na hapa zinaingia '*bitcoin*'.
   - Aina ya pili: 'sarafu mbadala' '*altcoins*': na hapa zinaingia, '*lightcoin*',

‘*bitcoin-cash*’, ‘*etherium*’ na ‘*ripple*’.

- Aina ya tatu: usuli zinazoweza kubadilishika na kufanyia biashara na bidhaa na sarafu zenye simbo.

Katika sifa muhimu za aina ya kwanza ya sarafu-tajwa ni kua hazina udhibiti wa serikali kuu, yaani haziko chini ya usimamizi wa taasisi ya kiserikali inayosimamia utoaji wake, tofauti na na aina nyingine ambazo zinasimamiwa na serikali, na aghalabu ya ‘sarafu za kidigitali zenye simbo’ *(coded*); zinategemea matumizi ya teknolojia inayojulikana kama: ‘*block-chain*’, teknolojia hii ndio inayotengeneza (zalisha) sarafu husika na kuihifadhi kwenye masjala zake pamoja na miamala yote juu ya sarafu hio, na katika sifa za ‘*bitcoin*’ ni uwepo wa mjadala juu ya utu wa mtoaji sarafu hii.

2) Miamala yote ya ‘sarafu za kidigitali zenye simbo’ *(coded*); inafanyika kwenye ‘majukwaa ya kielekroniki’ (*online platforms*), iayopatikana kwenye mitandao ya intaneti ima mubashara au kupitia kwa madalali. Zipo ada zinazolipwa kwa majukwaa hayo, na kila anaeamiliana kwenye jukwaa hilo ni lazima awe na ‘mkoba wa kielektronili’ (*electronic wallet*) kwenye kompyuta yake binafsi, unaothibitisha umiliki wake wa hizo ‘sarafu za kidigitali zenye simbo’ *(coded*) anazozimiliki na uwezo wa kuzisarifu. sifa kuu ya wanaoamiliana kwenye majukwa haya na mikoba ya kielektroniki ni kutotumia majina yao halisi, na badala yake kutumia majina bandia (ya kuazima) yanayojulikana kama: ‘asiejulikana’ (*anonymity*).

3) Baadhi ya nchi kama Malaysia zimewweka sheria ya kuwalazimisha waamilianao kwenye majukwaa ya kielektroniki kabla hawajaanzisha majukwaa hayo; mwanzo wapate vibali (leseni) maalum kutoka taasisi husika za kiserikali, pamoja na kuekewa vidhibiti (vigezo) vya kuamiliana kwenye majukwaa hayo ikiwemo: kusajili kwa kuthibitisha utambulisho (identity) wa muamili.

4) Licha ya kwamba sarafu hii kwa sasa imeenea katika nchi nyingi na kwenye maelfu ya maduka ya biashara, na licha ya kua kuna wanaozibadilisha sarafu hizi kwa sarafu za kitaifa za kawaida, na kukubalika kwenye baadhi ya taasisi za kiserikali; lakini bado zipo tafiti

nyingi zinazoashiria uwepo wa mambo hatarishi (*risks*) katika matumizi ya sarafu hizi za kidigitali zenye simbo *(coded*), na hasahasa kwenye mabadiliko ya thamani.

Mbili: Hukmu ya Kisharia:

Kupitia tafiti zilizowasilishwa na majadiliano yaliyoibuka kwenye kikao, imebainika kua, ili hukmu ya kisharia iwe muwafaka; bado kuna mas'ala yanayohitaji kufahamika zaidi yakiwemo:

1) Hii 'sarafu ya kidigitali yenye simbo' hasa ni kitu gani? je, ni bidhaa? au ni manufaa? au ni asilimali ya kiuwekezaji? au ni usuli ya kidigitali?
2) Je, hii 'sarafu ya kidigitali yenye simbo' ni mali inayoweza kutiwa thamani? na kufanyiwa biashara kisharia?

Tatu: Kwa mujibu wa yaliyotangulia na uwepo au uwezekano wa mambo hatarishi makubwa na kutokuwepo utulivu wa kimuamala; 'Kongamano' linausia kufanyike tafiti za ziada juu ya mas'ala yanayoathiri utoaji wa hukmu ya kisharia.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅≅

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 238 (9/24)

Yanayohusiana na ‘Miamala ya Kujikinga Katika Taasisi za Kifedha za Kiislamu’

Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), katika kikao chake cha ishirini na nne (24) kilichofanyika Dubai (UAE) tarehe 7 - 9 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1441 Hijria, sawa na 4 - 6 Novemba, 2019.

Baada ya kupitia ‘Mapendekezo’ yaliyotolewa na ‘Warsha ya Kielimu juu ya Miamala ya Kujikinga Katika Taasisi za Kifedha za Kiislamu’, iliyoandaliwa na ‘Kongamano’, Jeddah (Saudi arabia), tarehe 24 – 25 Rajab (Rajabu), 1440 Hijria, sawa na 31 Machi – 1 Aprili, 2019, kwa kushirikiana na ‘Taasisi ya Waqf Iqra: Maendeleo na Uzalishaji’, na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya ‘Maazimio ya Kongamano’ mbalimbali kuhusiana na: ‘Kua na Tahadhari (*Tahawwut*) Katika Miamala ya Kifedha’, hususan ‘Azimio la Kongamano’ namba 224 (8/23) lililohusiana na ‘Kua na Tahadhari (*Tahawwut*) Katika Miamala ya Kifedha: Vigezo na Hukmu’ lililotolewa kwenye kikao cha ishirini na tatu (23) kilichofanyika Madina al-Munawarah, Saudi Arabia, 19 - 23 Swafar (Mfungo Tano), 1440 Hijri, sawa na 28 Oktoba – 1 Novemba, 2018, katika vipengele vyake vyote vya ‘Azimio-tajwa’ navyo ni:

1) Dhana ya (*Tahawwut*) Tahadhari.
2) Dhana ya Mambo hatarishi (risks).
3) Dhana ya Kujikinga (kujihami).
4) Msimamo wa sharia ya kiislamu juu ya kujikinga (*tahawwut*) dhidi ya mambo hatarishi.

5) vigezo vya kisharia na taratibu zake kwa miamala ya *tahawwut* (tahadhari ya kinga).

Mbili: Miamala ya *Tahawwut* (kujikinga) kwa maana ya kiujumla:

Ipo miamala kadhaa ambayo inawezekana kua ni msingi wa muamala wa *Tahawwut* na kujikinga kwa maana ya kiujumla, na hio ndio miamala inayotumika kwenye taasisi za kifedha, na hukmu yake kisharia: inajuzu, miongoni mwa miamala hio ni:

1) *Tahawwut* ya (kujihami) kiuchumi: Imejikita kwenye usuli-tanzu anwai na mikoba ya uwekezaji ni miamala anwai. Kusimamia *Tahawwut* kama hii inahimizwa kisharia kwa minajili ya utunzaji mzuri wa rasilimali.
2) *Tahawwut* Shirikishi (ya ushirikiano): Imejikita kwenye miamala ya kusaidiana kupitia kuingia kwenye mikataba ya bima-shirikishi na ya kusaidiana kwa lengo la kufidia madhara na hasara zitokeapo na ambazo huenda zikaitikisa taasisi ya kifedha ya kiislamu. Miamala hii haina tatizo kisharia kwa sababu tayari bima-shirikishi inajuzu juu ya miradi, asilimali, na mali, ‘Maazimio mawili ya Kongamano’ namba 9 (9/2) na 200 (6/21) yanasisitiza kujuzu kwa aina zote za bima-shirikishi.
3) *Tahawwut* ya kimkataba sambamba: Hi ni kwenye mkataba wa pili sambamba na ule mkataba wa asili kwa masharti yaleyale na vigezo zilezile, taasisi inajikinga na mambo hatarishi ya kwenye mkataba wa kwanza wa asili, ni kama biashara ya *salam* na ya *salam* sambamba, na mkataba wa *istisnaa* na *istisnaa* sambamba, ni kama ilivyokuja kwenye mapendekezo ya ‘Azimio la Kongamano’ namba 224 (8/23) lililohusiana na ‘Kua na Tahadhari (*Tahawwut*) Katika Miamala ya Kifedha. Katika vigezo muhimu vya kujuzisha mikataba sambamba ni kutoifungamanisha mikataba ya asili na mengine, bali ni lazima kila mkataba ujitenge na mwengine katika haki zote na nyajibu zake.
4) Mikataba ya kushikanishwa: Hii ni mikataba inayojumuishwa pamoja kwa lengo la kujikinga dhidi ya mambo hatarishi kwa yale mambo yanayojumuishika, lakini isiwe ni sharti hilo wala isiwe ni mkataba ndani ya mkataba, kama vile: kujumuisha mkataba wa mauziano na

ahadi lazimishi, mikataba ya *wakala* na *murabaha*, ifuatayo ni baadhi ya mifano ya mikataba iliyoshikanishwa:

a) Kujumuisha mikataba ya *murabaha* na *musharaka*: Hii inafanyika kwa kuugawa mkoba wa uwekezaji (*investment portfolio*) kwenye sehemu mbili; sehemu ya kwanza inahusishwa na miamala ya muarabaha na taasisi zinazoaminika kwa faida fulani-ainishwa, na sehemu ya pili inawekezwa kwenye miamala ya *musharaka*, kama biashara za hisa kwenye soko la hisa, au hisa za ankari na mfano wake, kufanya hivi kutasaidia kuilinda rasilimali kwenye *murabaha*, na uwezekano wa kupata hasara kwenye sehemu ya pili (*musharaka*).
b) Kujumuisha mikataba ya *ijara* na *musharaka*: Njia ya kujikinga hapa ni kama iliyotangulia, lakini hapa utajikinga kupitia miamala ya *ijara* badala ya *murabaha*, kama vile kuwekeza sehemu ya mkoba wa uwekezaji kwenye kununua sukuk za ijara zenye mapato yanayoweza kuilinda rasilimali, sehemu iliyosalia iwekezwe kwenye mikataba ya musharaka.
c) Kujumuisha mikataba ya *murabaha* na biashara ya *urbuni*: Nayo pia kwa kuugawa mkoba wa uwekezaji (*investment portfolio*) kwenye sehemu mbili; sehemu ya kwanza inahusishwa na miamala ya muarabaha na taasisi zinazoaminika kwa faida fulani-ainishwa, na sehemu ya pili inawekezwa kwenye miamala ya *urbuni*, kwa kununua hisa kwenye soko la hisa, thamani ya hisa ikipanda atasaini mkataba wa kununua, akisha kabidhiwa aziuze, alipe thamani ya kununua kwa muuzaji, kufanya hivi mkoba utapata faida, ama ikiwa thamani haikupanda kama ilivyotarajiwa basi ataachana na kuingia mkataba na atakua amepata hasara kwenye urbuni, lakini rasilimali itabaki imehifadhiwa (imekingwa) kwenye miamala ya murabaha. Kwa njia hii, vigezo vya kisharia vya biashara ya urbuni lazima vizingatiwe, vikiwemo: Kuiacha mali ya urbuni mahali ilipo tangu mkataba ulipofungwa hadi pale itakaposawazishwa, na kutoifanyia biashara mali ya urbuni yenyewe.

5) *Tahawwut* kwa kutumia ‘hiari ya sharti’ ili kujikinga dhidi ya mteja kuvunja ahadi yake: kama vile mikataba ya murabaha au ijara inayoishia kumiliki, ‘Maamuzi ya Kongamano’ mbalimbali yanayohusiana na maudhui ya ‘*muwa’adah*’ (kuahidiana) kwamba: inajuzu kuekeana ‘sharti la hiari’ kwa walioahidiana ima pande zote au upande mmoja, ama ikiwa hakuna hiari basi haijuzu. Hapa ni lazma ijulikane kua: ‘Maamuzi ya Kongamano’ yaliyoangazia kujuzu ahadi-lazimishi kwa upande mmoja wa pande mbili za mkataba ni kwa sababu ya kujikinga dhidi ya mteja kuvunja ahadi yake, na kuilinda taasisi dhidi ya kudhurika, basi hiari hio pia anapewa upande wa pili.
6) *Tahawwut* kwa kutumia ‘dhamana’ ili kuzikinga rasilimali kwenye uwekezaji: Hizi ni mbinu anwai miongoni mwa miamala ya *Tahawwut* (kujikinga) dhidi ya mambo hatarishi na hasara au kutopata faida kwenye miradi ya kiuwekezaji, ilisisitizwa na ‘Kongamano’ kwenye ‘Maamuzi yake’ kujuzu kwa miamala kama hio; nayo ni:

    a) Dhamana ya upande wa tatu (*Third-party guarantee*): Huyu ni mtu wa kawaida au utu wa kikanuni asiekua sehemu ya pande mbili za mkataba anajilazimisha mwenyewe kua dhamana katika mradi fulani. Dhamana kama hii ilisisitizwa kujuzu kwake na ‘Azimio la Kongamano’ namba 30 (5/4) kwa sharti mdhamini yeye binafsi na dhimma yake ya kifedha asiwe ni sehemu ya pande mbili za mkataba, na aamue kujitolea kufidia hasara kwenye mradi fulani, ahadi hii iwe inajitegemea.
    b) Kumbebesha (kumwajibisha) mudharib mzigo wa kuthibitisha madai ya hasara; ‘Azimio la Kongamano’ namba 212 (8/22) lilipitisha kuhamisha mzigo wa kuthibitisha madai ya hasara kwa benki (mudharib) tofauti na asili, kwa sharti ya uwepo wa vidokezo (*qarina*) vinavyopinga madai ya asili ya kutozembea.

Tatu: Miamala ya *Tahawwut* (Kujikinga) kwa maana ya kiujumla na inayokatazwa kisharia; ikiwemo:

1) *Tahawwut* (Kujikinga) kwa madeni ya kubadilishana kwa kutumia sarafu mbili tofauti pamoja na kuweka sharti: Muamala huu

unatumika kwa minajili ya kujikinga (*Tahawwut*) dhidi ya mabadiliko ya bei za sarafu na akaunti za wahusika kufikia mwisho wa kutoa pesa (*overdraft*). Ikiwa taasisi ya kifedha ina salio la ziada (*surplus*) la sarafu fulani, wanawakopesha sarafu hio taasisi nyengine ili taasisi hio nyengine iwakopeshe sarafu nyengine ambayo wanaihitajia kwa kuekeana sharti ima la wazi au fiche au kimazowea (desturi), muamala huu ni ukopeshaji kwa ajili ukopeshaji wenye sharti; haujuzu kisharia, na wanazuoni wa madhehebu ya kifiqhi mbalimbali wamekubaliana kutoujuzisha muamala huu kwa sababu ya kufungamanishamikopo miwili: 'nikopeshe ili nikukopeshe' ni sawa mida ya kulipana imewafikiana au imekhtalifiana.

2) *Tahawwut* (Kujikinga) ili kulinda rasilimali kwenye hisa na sukuk: Zipo aina kadhaa za ukingaji (*Tahawwut*), ushurutishaji na ahadi zinazopatikana kwenye sukuk ambazo zinakhalifu vigezo vya kisharia, na pia kukhalifu 'Azimio la Kongamano' namba 30 (5/4) 1988, lililohusiana na 'sukuk za mudaraba na sukuk za uwekezaji' na 'Azimio' namba 188 (3/20) lililohusiana na 'kukamilisha maudhui ya sukuk za kiislamu', zikiwemo:

   a) Mtoaji wa sukuk (Mudharib, Mshirika, Msimamizi, Wakala wa uwekezaji) kudhamini thamani ya sokoni.
   b) Mudharib kuahidi kuukopesha mkoba wa sukuk ili kuhakikisha (kukinga) kiwango fulani cha mgao wa faida.
   c) Kushurutisha wabebaji sukuk wasiweze kusarifu kwenye mali yaliyokodishwa katika mazingira ya kushindwa kulipa awamu (*installment payment default*) zao.
   d) Kutohamishika kwa umiliki wa usuli za sukuk kwa wawekezaji au kwa wabebaji sukuk; ikimaanisha kutowajibika lakini pia kutostahiki na faida zipatikanazo, kwa kua hawakutahamali gharama kustahiki faida, uthibitisho wa hili ni kwamba asilimali zinaendelea kubaki kwenye daftari la mtoaji.
   e) Kushurutisha kuweka kipengele kwenye mkataba wa utoaji sukuk kua: msimamizi atawakopesha wabebaji sukuk iwapo kumetokea mazingira ya faida iliyotarajiwa kupungua; kwa aghalabu kipengele hiki hua kinakabiliana na kipengele kingine

cha sharti kua: iwapo faida imevuka kiwango walichokubaliana basi ziada hiyo inachukuliwa na msimamizi kama mojawapo ya njia za uhamasishaji (*incentive*).

Nne: Vifaa mbadala vya *tahawwut* (kujikinga) vya bidhaa za kifedha na hukmu zake za kisharia

Vifaa hivi vinagawanyika kwenye aina nne:

Aina ya kwanza:

Kujikinga (*tahawwut*) dhidi ya mabadiliko ya bei za sarafu kwa mustakbali; miamala muhimu chini ya ania hii ni:

Moja: Ahadi-lazimishi baina ya pande mbili ya kuingia kwenye mkataba wa kubadilishana sarafu kwa baadae.

Inakua hivi: 'Pande zote mbili zinakubaliana na kuwekeana ahadi-lazimishi ya kuingia kwenye mkataba wa kubadilishana sarafu kwa mustakbali na kwa bei ya sarafu iliyoainishwa'.

Hukmu yake kisharia:

a) Haijuzu kutumia ahadi-lazimishi kama njia ya kujikinga (*tahawwut*) kwenye mikataba ya sarafu, 'Azimio la Kongamano' namba 102 (5/11) kuhusiana na 'Biashara za Sarafu (Kubadilisha pesa za kigeni)' yaliweka wazi kua haijuzu kisharia biashara ya sarafu kwa malipo-baadae, aidha haijuzu kuahidiana kulipana baadae, hii imetokana na kua ahadi-lazimishi inafanana na mkataba, kama ilivyobainishwa kwenye 'Azimimo la Kongamano' namba 40 (2/5) kuhusiana na 'Utekelezaji wa Ahadi na Muamala wa 'Murabaha kwa anaetoa amri ya manunuzi (Aamir Bi al-Shirai)' kua: '*Ahadi inayotolewa ima kwa anaenunua au kwa anaeuza inakua yenye kumlazimu mtoa ahadi hio*'.
b) Katika muamala huu-tajwa hazipatikani hali zisizokua za kawaida na ambazo zimeelezewa kwenye 'Azimio la Kongamano' namba 157 (6/17) lililohusiana na: 'Kuahidiana na Kushirikiana katika Mikataba'. Azimio hilo lilijuzisha maahadiano-lazimishi katika zisizokua za

kawaida, pamoja na Azimio-tajwa kuweka msisitizo kua maahadiano-lazimishi katika zisizokua za kawaida; zisikaribie riba.

Mbili: Ahadi mbili zinazokabiliana (ahadi-lazimishi kwa masharti maalum; ikikabiliana na ahadi-lazimishi kwa masharti tofauti kwa kuingia mkataba wa sarafu mustakbali).

Inakua hivi: Upande mmoja unaahidi upande wa pili ahadi-lazimishi ya kumuuzia kiwango fulani cha pesa kwa bei iliyoainishwa na wakati uliyoainishwa katika hali (mazingira) ambayo muelekeo wa bei ya sarafu hauko kwenye maslahi yake, ama ikiwa iko kwenye maslahi yake; basi haahidi chochote. Aidha, upande wa pili nao unatoa ahadi-lazimishi ya kununua pesa (sarafu) hiohio kwa bei hiohio iliyoainishwa na wakati huohuo uliyoainishwa katika hali (mazingira) ambayo muelekeo wa bei ya sarafu unakhalifiana na maslahi yake, ama ikiwa unawafikiana na maslahi yake; basi haahidi chochote.

Hukmu yake kisharia:

Haijuzu kuekeana ahadi zinazokabiliana kwa ajili ya kujikinga (*tahawwut*) na mabadiliko kwenye bei za sarafu, kwa sababu kiuhalisia wake inafanana na maahadiano-lazimishi ya kubadilishana sarafu iliyokatazwa kisharia kwa mujibu wa ‘Azimio-tajwa la Kongamano’ hapo juu.

Tatu: Ofa (aridhi) inayotolewa kwa kipindi maalum inayomlazimisha atoaye ofa hio kuingia mkataba wa ubadilishaji wa fedha.

Inakua hivi: Upande mmoja unatoa ofa itakayoendelea kwa mda maalum, ndani ya mda huu anaingia mkataba wa ubadilishaji wa fedha kwa kuuza sarafu fulani kwa bei maalum na kwa kiwango maalum; na upande wa pili nao ukatoa ahadi-lazimishi au ahadi isiyo-lazimishi kwa kukubali ofa hio ndani ya mda waliokubaliana.

Hukmu yake kisharia:

a) Haijuzu kutabikisha (kutumia) msingi wa ofa (aridhi) inayotolewa kwa kipindi maalum juu ya mkataba wa ubadilishaji fedha; kwa sababu ya uwepo wa sharti la kukabidhiana wakati wa kufunga mkataba, nisawa kuna ahadi-lazimishi inayokabiliana nayo au la, hii ndio hukmu

iliyopitishwa na ‘Azimio la Kongamano’ namba 52 (3/6) lililohusiana na: ‘Hukmu ya Mikataba Kupitia Vyombo vya Mawasiliano vya Kisasa’ kifungu cha ‘Nne’.

b) Iwapo ofa (aridhi) inayotolewa kwa kipindi maalum inayomlazimisha mtoaji ofa hio; inakabiliana na ahadi-lazimishi kutoka upande wa pili, basi inakua ni kama maahidiano-lazimishi, bali hata ni zaidi ya hivyo, kwa kupatikana moja ya nguzo mbili za mkataba ambayo ni mpendekezaji (mtoa ofa).

Nne: Kutekeleza miamala miwili ya *tawarruq* inayokabiliana.

Inakua hivi: Kutekeleza muamala wa *tawarruq* wa mpangilio (*structured tawarruq*) ambao matokeo yake ni kuthibitisha uwepo wa deni kwa kiwango kadhaa cha sarafu ya kwanza inayotakiwa kulipwa deni hilo; kisha kunatekelezwa muamala wa *tawarruq*-akisi (*reversed tawarruq*) ambao matokeo yake ni kuthibitisha uwepo wa deni kwa kiwango kadhaa cha sarafu ya pili inayotakiwa kupokelewa, hapa sasa panaibuka madeni aina mbili yanayokabiliana kwa pande zote mbili za muamala, kila muamala kwa sarafu yake.

Hukmu yake kisharia:

Kwa kua muamala huu unategemea kwenye muundo wake kwa miamala ya *tawarruq* ilitokatazwa kisharia; basi miamala yenyewe inkua haifai. Kuhusu uhalisia wa *tawarruq* na aina zake; ‘Azimio la Kongamano’ namba 179 (5/19) tayari lilishatoa hukmu ya kutojuzu kufanya *tawarruq* mbili ya mpangilio (*structured*) na ya akisi (*reversed*), kwa kua kunaficha makubaliano kati ya mgharamiaji (*financier*) na mpokea (mfaidika wa) *tawarruq* (*mustauriq*), ima ya wazi au fiche au mazowea (desturi), aina fulani ya njama ya kupata pesa taslimu kwa kulipa zaidi ya hizo; hii ni riba.

Tano: Maahidiano-lazimishi ya kuingia mkataba wa *murabaha* au biashara ya mustakbali ya hasara ambayo faida yake na hasara yake itategemea viashiria (*index*) walivyokubaliana.

Inakua hivi: Muamala huu unafanyika kupitia maahidiano-lazimishi ya pande mbili ya kuingia mkataba wa muamala wa *murabaha* au hasara kutoka upande wa kwanza kwenda upande wa pili, au kutoka upande wa

pili kwenda upande wa kwanza katika siku ya mustakbali, na iwe faida ya muamala huo au hasara yake kwa kiwango cha tofauti itakayopatikana chanya / hasi katika siku ya mustakbali waliyokubaliana kuhasibu kwa mujibu wa viashiria siku hio.

Hukmu yake kisharia:

a) Kimsingi, ni kutojuzu miamala ya maahidiano-lazimishi ya pande mbili, hii ni kwa mujibu wa 'Azimio la Kongamano' namba 40 (2/5).
b) Katika muamala huu-tajwa hazipatikani hali zisizokua za kawaida na ambazo zimejuzishwa na 'Kongamano kwenye 'Azimio lake' namba 157 (6/17) kama ilivyobainishwa kwenye ibara ya 'Nne' kifungu 1(a).

Sita: Ahadi mbili zinazokabiliana (ahadi-lazimishi kwa masharti maalum; ikikabiliana na ahadi-lazimishi kwa masharti tofauti kwa kuingia mkataba wa *murabaha* au hasara mustakbali).

Inakua hivi: Upande mmoja unaahidi upande wa pili ahadi-lazimishi ya kuingia mkataba wa *murabaha* au hasara kwenye wakati ulioainishwa katika hali (mazingira) ambayo muelekeo wa viashiria vya bei ya sarafu hauko kwenye maslahi yake, ama ikiwa viashiria vya bei ya sarafu viko kwenye maslahi yake; basi haahidi chochote. Aidha, upande wa pili nao unatoa ahadi-lazimishi ya kuingia mkataba wa *murabaha* au hasara kwenye wakati ulioainishwa katika hali (mazingira) ambayo muelekeo wa viashiria vya bei ya sarafu hauko kwenye maslahi yake, ama ikiwa viashiria vya bei ya sarafu viko kwenye maslahi yake; basi haahidi chochote. Watahasibu faida ya *murabaha* au hasara kwa mujibu wa viashiria walivyokubaliana.

Hukmu yake kisharia:

Haijuzu kuekeana ahadi zinazokabiliana, kwa sababu kiuhalisia wake inafanana na maahadiano-lazimishi yaliyokatazwa kisharia kwa mujibu wa 'Azimio-tajwa la Kongamano' hapo juu, ibara ya (4) kifungu cha (5).

Aina ya pili:

Kujikinga (*tahawwut*) dhidi ya mabadiliko ya viashiria (*index*) vya kiwango cha faida (riba) vinavyoathiri katika kuainisha viwango vya faida kwenye miamala ya kiislamu:

Moja: Maahidiano-lazimishi ya pande mbili ya kuingia mkataba wa *murabaha* au hasara mustakbali ambayo faida yake na hasara yake itategemea viashiria (*index*) walivyokubaliana:

Inakua hivi: Muamala huu unafanyika kupitia maahidiano-lazimishi ya pande mbili ya kuingia msururu mikataba ya miamala ya *murabaha* au hasara kutoka upande wa kwanza kwenda upande wa pili, au kutoka upande wa pili kwenda upande wa kwanza katika idadi kadhaa ya siku za mustakbali, na iwe faida ya kila muamala au hasara ni kwa kiwango cha tofauti itakayopatikana chanya / hasi katika kila siku za mustakbali kwa mujibu wa waliyokubaliana kuhasibu viashiria siku hio.

Hukmu yake kisharia:

a) Haijuzu kutumia Maahidiano-lazimishi kama ni muamala wa kujikinga (*tahawwut*) kwa kubadilishana viwango vya faida vilivyotulia au vinavyobadilika. Hii ni kutokana na kua Maahidiano-lazimishi yanafanana na mkataba, kama ilivyokuja kwenye ‘Azimio la Kongamano’ namba 40 (2/5) kuhusiana na ‘Utekelezaji wa Ahadi na Muamala wa ‘Murabaha kwa anaetoa amri ya manunuzi (*Aamir Bi al-Shirai*)’ kua: Maahidiano-lazimishi kwenye biashara yanafanana na biashara yenyewe.
b) Katika muamala huu-tajwa hazipatikani hali zisizokua za kawaida na ambazo zimejuzishwa na ‘Kongamano kwenye ‘Azimio lake’ namba 157 (6/17) kama ilivyobainishwa kwenye ibara ya ‘Nne’ kifungu 1(a).

Mbili: Ahadi mbili zinazokabiliana (ahadi-lazimishi kwa masharti maalum; ikikabiliana na ahadi-lazimishi kwa masharti tofauti kwa kuingia mkataba wa *murabaha* au hasara mustakbali):

Inakua hivi: Upande mmoja unaahidi upande wa pili ahadi-lazimishi ya kuingia msururu wa mikataba ya *murabaha* au hasara kwenye nyakati zilizoainishwa katika hali (mazingira) ambayo muelekeo wa viashiria vya kiwango cha faida (riba) haviko kwenye maslahi yake, ama ikiwa viashiria

vya kiwango cha faida viko kwenye maslahi yake; basi haahidi chochote. Aidha, upande wa pili nao unatoa ahadi-lazimishi ya kuingia msururu wa mikataba ya *murabaha* au hasara kwenye nyakati zilizoainishwa katika hali (mazingira) ambayo muelekeo wa viashiria vya kiwango cha faida haviko kwenye maslahi yake, ama ikiwa viashiria vya kiwango cha faida viko kwenye maslahi yake; basi haahidi chochote. Watahasibu faida ya *murabaha* au hasara kwa mujibu wa viashiria walivyokubaliana.

Hukmu yake kisharia:

Haijuzu kuekeana ahadi zinazokabiliana, kwa sababu kiuhalisia wake inafanana na maahadiano-lazimishi yaliyokatazwa kisharia kwa mujibu wa 'Azimio-tajwa la Kongamano' hapo juu, ibara ya (4) kifungu cha (5).

Tatu: Kutekeleza miamala ya *tawarruq* inayokabiliana:

Inakua hivi: Kutekeleza muamala wa *tawarruq* wa mpangilio (*structured tawarruq*) ambao matokeo yake ni kuthibitisha uwepo wa deni kwa kiwango kadhaa cha faida thabiti inayotakiwa; kisha kunatekelezwa muamala wa *tawarruq*-akisi (*reversed tawarruq*) ambao matokeo yake ni kuthibitisha uwepo wa deni kwa faida inayobadilika, kwa namna ambayo watapunguziana (watakatan) baina ya madeni aina mbili hizo kila siku katika siku za mida ya mikataba hio, mwisho wa siku fidia italipwa kujaliza tofauti tu. Faida inayobadilika kwenye miamala ya *tawarruq* inafikiwa kwa mojawapo wa njia tatu:

a) Mkataba wa *tawarruq* kwa faida inayobadilika.
b) Mkataba wa *tawarruq* kwa faida thabiti, pamoja na ahadi ya kukata/kupunguza kila kitakachozidi na kiashiria cha kiwango cha faida kila siku ya malipo ya awamu ya mustakbali.
c) *Tawarruq*-mzunguko; kutekeleza msururu wa miamala ya *tawarruq* ya mda mfupi (*short-term*); kila muamala ukiwa na kiwango cha faida thabiti, ifikapo mwisho wa siku inatengeneza deni kwa faida inayobadilika.

Hukmu yake kisharia:

Haijuzu; kwa muamala umejikita kwenye taratibu iliyokatazwa kisharia (*tawarruq*) kama ilivyokuja kwenye ibara ya (4) kifungu cha (4).

Aina ya tatu:

Ahadi-lazimishi kutoka upande mmoja ikiwa ni mbadala wa muamala wa 'hiari-chaguzi':

Inakua hivi: Kutoa ahadi-lazimishi kwa upande mmoja wa kuingia muamala wa *murabaha* kwa upande wa pili kwa kiwango cha tofauti-chanya katika siku watakayoafikiana, au ndani ya mda waliokubaliana wakati wowote anapotaka upande wa pili, ahadi hii-lazimishi inauzwa kwa thamani inayoainishwa na inalipwa mwanzo, na upande wa kwanza uliotoa ahadi-lazimishi unakua ni sawa na 'muuzaji' wa 'hiari-chaguzi'; na upande wa pili unakua ni sawa na 'mnunuzi' wa 'hiari-chaguzi'.

Hukmu yake kisharia:

Haijuzu kufidia (kulipia) ahadi-lazimishi; 'Azimio la Kongamano' namba 63 yaliyohusiana na 'Masoko ya Pesa: Hisa, Chaguzi (Hiari), Bidhaa na kadi za mkopo'; lilisema hivi:

"Mbili: Chaguzi (hiari):

c) Namna ya mikataba ya chaguzi: *Kusudio la mikataba ya chaguzi ni kujitoa katika ulazima au kujifunga kuuza au kununua kitu fulani kilichoainishwa kwa bei iliotajwa ndani ya kipindi fulani au wakati fulani-tajwa ima moja kwa moja au kupitia wakala anaesimamia haki za pande mbili.*

d) ***Hukmu yake Kisharia:*** *Mikataba ya chaguzi – kwa namna inavyofanyika leo kwenye masoko ya pesa ya kimataifa (global financial markets) – ni aina mpya ya mikataba iliyozuka, haina mifano yake katika mikataba inayojulikana Kisharia, lakini kwa kua kinachofungiwa mkataba hapa si mali wala si manufaa wala haki ya mali basi huo ni mkataba usiojuzu Kisharia, na kwa kua mkataba huu haujuzu basi vilivile haijuzu miamala inayotokana nayo*".

Aidha, 'Azimio la Kongamano' namba 224 lililohusiana na '*Tahawwut* (kujikinga)' liliangazia vigezo vya *tahawwut* inayojuzu katika sharia kwenye ibara ya (3), kifungu cha (4):

"*Miamala ya tahawwut (tahadhari ya kinga) isipelekee kuuza haki za mhusika, kama vile kuuza chaguzi ambazo zimeharamishwa na 'Azimio la Kongamano namba 63 (1/7) kifungu cha 2 (b). Aidha, isipelekee kuuza ahadi kama kuchukua malipo juu ya dhamana ambayo imekatazwa na 'Kongamano' kwenye 'Azimio' lake namba 12 (2/12)*".

Inausiwa yafuatayo:

1) 'Baraza la Kongamano' linapendaa kuusia Mabaraza ya Kisharia, Bodi za Fatwa na Udhibiti wa Kisharia, Wanazuoni na Watafiti wazingatie 'Makusudio Makuu ya Sharia ya Kiislamu' na vigezo vya kisharia wakati wanapofanya *ijtihad* ya kuowanisha mikataba na bidhaa za kifedha za kiislamu kiujumla, na namna ya kuisuka mikataba ya *tahawwut* kwa njia mahsusi, pamoja na kuzingatia hatima na athari za mikataba hio; kuzingatia hatima ya chochote ni katika misingi inayozingatiwa kisharia.
2) 'Baraza la Kongamano' linapendaa kuusia idara za uwekezaji na hazina kwa ngazi ya taasisi, na pia taasisi zinazosimamia kuandaa sera za sarafu na fedha katika ngazi za nchi (dola) kulinda uwiano baina ya nyajibu na madeni kwa upande mmoja; na baina ya utajiri na harakati za kiuchumi halisi kwa upande mwengine, ili wasizame (wasighariki) kwenye madeni yatakayoathiri harakati za kiuchumi.

Allah ni Mjuzi Zaidi

≅≅

Maamuzi na Maazimio

ya Kikao cha Ishirini na Tano (25) ya

Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu (KKFK)

Jeddah, Saudi Arabia

29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha’ban (Shaabani), 1444 Hijria

sawa na 20 - 23 Februari, 2023

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 239 (1/25)

Yanayohusiana na 'Hukmu ya Elimu ya Aina Zote Mbili; Elimu ya Dini na Elimu ya Dunia kwa Wanaume na Wanawake Katika Uislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia 'Azimio lake' namba 38 (13/4) lililohusiana na '*Mbinu za Kupambana na Miporomoko ya Maadili, Nyanja za Umoja wa Kiislamu na Namna ya Kufaidika nazo, Kusilimisha Mifumo ya Elimu katika Nchi za Kiislamu*' lililopitishwa kwenye kikako chake cha nne (4) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia), kuanzia tarehe 18 – 23 Mwezi wa Mfungo Tisa, (Jumadal-Aakhira) 1408 sawa na tarehe 6 – 11 Februari, 1988;

Na baada ya kupitia 'Azimio lake' namba 164 (2/18) lililohusiana na '*Kukuza Rasilimali-Watu katika Ulimwengu wa Kiislamu*', na 'Azimio' namba 169 (7/18) lililohusiana na '*Haki na Majukumu ya Mwanamke wa Kiislamu*' yaliyopitishwa kwenye kikako chake cha kumi na nane (18) kilichofanyika Putrajaya, (Malaysia) 24 - 29 Jumada al-Thani (Mfungo Tisa), 1428, sawa na 9 – 14 Julai, 2007;

Na baada ya kupitia 'Azimio lake' lililotangulia, namba 236 (7/24) lililohusiana na '*Nafasi ya Malezi yaKidini Katika Kuimarisha Amani*' lililopitishwa kwenye kikako chake cha ishirini nan ne (24) kilichofanyika Dubai (UAE) tarehe 7 - 9 Rabii al-Awwal (Mfungo Sita), 1441 Hijria, sawa na 4 - 6 Novemba, 2019;

Na baada ya kupitia 'Tamko la Sekreterieti Kuu ya Kongamano' kuhusiana na 'Kusitisha elimu ya wasichana na watoto wa kike kwenye maskuli na

vyuo vikuu nchini Afghanistan' lililotolewa tarehe 28 Jumada al-Ula (Mfungo nane), 1444 Hijria, sawa na 22 Disemba, 2022;

Na baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Hukmu ya Elimu ya Aina Zote Mbili; Elimu ya Dini na Elimu ya Dunia kwa Wanaume na Wanawake Katika Uislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Maana ya elimu katika uislamu: ni ule mchakato mzima wa kujifunza maadili, tabia, maarifa, fani na stadi zinazomsaidia binadamu kumuabudu Allah SWT, kuimarisha dunia, kuifikia furaha na kuyafikikia mafanikio ya hapa duniani na ya kesho akhera.

Mbili: Kuwafundisha watoto wa kike na wa kiume elimu zenye manufaa ni haki kwa familia zao, kwa jamii na kwa nchi nzima, aidha ni haki ya watoto wenyewe katika aina zote za elimu na awamu zake, kwa hili; wanazuoni hawajakhitalifiana tangu enzi za maswahaba hadi leo hii, hii ni kwa mujibu wa neno lake Allah SWT pale aliposema:

"***1.*** *Soma kwa jina la Mola wako Mlezi aliye umba,* ***2.*** *Amemuumba binaadamu kwa tone la damu,* ***3.*** *Soma! Na Mola wako Mlezi ni Karimu kushinda wote,* ***4.*** *Ambaye amefundisha kwa kalamu,* ***5.*** *Kamfundisha mtu aliyo kuwa hayajui.*"[1], na pia pale aliponena: "*Ametukuka Mwenyezi Mungu, Mfalme wa Haki. Wala usiifanyie haraka hii Qur'ani, kabla haujamalizika ufunuo wake. Na sema: Mola wangu Mlezi! Nizidishie ilimu*"[2], akanena tena: "*Na katika watu, na wanyama, na mifugo, pia rangi zao zinakhitalifiana. Kwa hakika wanao mcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kusamehe*"[3], na aya nyenginezo nyingi, lakini

[1] Surat al-'Alaq: 1 – 5.

[2] Surat Ta-Ha: 114.

[3] Surat Faatir: 28.

kuifanyia kazi hadith ya Mtume SAW pale aliposema: "*Utafutaji wa elimu ni faradhi (jambo la lazima) juu ya kila muislamu*"[1].

Tatu: Elimu iliyoamrishwa hapa inajumuisha aina yoyote ya elimu ambayo itasaidia kuhakikisha kua yale makusudio makuu matano ya sharia yanafikiwa; ambayo ni: kulinda nafsi (roho), dini, kizazi, akili na mali, aidha kila aina ya elimu ambayo inapelekea kulinda maslahi ya kimahitajio na ya kiubora wa maisha; kama vile: elimu ya dini ambayo inamuwezesha binadamu kujua yale aliyofaradhishiwa na Allah na aliyoyapendekeza miongoni mwa maneno na matendo, na pia kujua yale aliyoyakataza Allah SWT miongoni mwa maneno na matendo. elimu hizi ni kama: elimu ya aqida (tauhid), elimu ya fiqh na usul al-fiqh, elimu za Sunnah (hadith za bwana mtume SAW), elimu za tafsir na nyenginezo; pia inajumuisha elimu ya dunia inayomuwezesha kuufahamu ulimwengu, maisha, hali halisi na utumiaji uliobora wa rasilimali alizotuneemesha nazo Allah SWT, elimu hizo ni kama; elimu za tiba, elimu za handasa, elimu za uchumi, elimu za kijamii na kibinadamu na elimu za mazingira na nyenginezo.

Nne: Ni wajibu wa familia, jamii na nchi kwa jumla kuandaa bajeti maalum ya elimu za aina zote hizo; yaani za dini za dunia, kwani kufanya hivyo ni kuisimamisha dini na kuitengeneza dunia na ndani yake kunapatikana maslahi ya binadamu ya hapa duniani na ya kesho akhera.

Tano: Haijuzu kisharia kumnyima yeyote awe mume au mke kupata aina yoyote miongoni mwa aina hizi za elimu zenye manufaa kwa pande zote mbili, kwani kufanya hivyo ni kukiuka maagizo ya sharia ya kiislamu inayoamrisha kusomwa kwa elimu hizo, na pia ni kupingana na itifaki ya wanazuoni wa karne nyingi zilizopita waliokubaliana juu ya uwajibu wa kizisoma elimu aina zote mbili, kutofanya hivyo ni kueneza ufisadi na kutanua ujinga, ufukara, maradha na yanayozalikana na mambo hayo.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kuzirekebisha fatwa potofu zinazopingana na mafundisho ya Qur'an na Sunnah; fatwa ambazo zinamzuia mwanamke kujifunza na kupata

[1] Imepokewa na imam ibn Majah kutoka kwa Anas RA.

elimu.

2) Kupambana na fikra (rai) zinazoelekea kumnyima mwanamke fursa ya elimu ya aina zote mbili, kwa kutumia hoja hafifu zisizofaa, na kuziraddi hoja hizo na kubainisha makossa yake.
3) Kuziomba serikali za kiislamu kuongeza juhudi na kujihusisha zaidi katika kuwawezesha watoto wa kike na wa kiume katika suala la elimu ya pande zote mbili na awamu zake zote, hususan watoto wa kike, kuwafundisha watoto wa kike ina umuhimu wa aina yake katika kusimamia vizazi vya baadae.
4) Kuzitaka serikali na jamii kurekebisha matatizo na vikwazo amabvyo huenda vikawakwaza au kuwazuia watoto wa kike kuendelea na masomo yao ya pande zote mbili.
5) Uwepo wajibikaji wa vitengo vya kielimu kwenye vyuo vikuu, makongamano ya kifiqhi, vituo vya utafiti, majarida ya kisayansi, wanazuoni, wanafikra, maimamu, makhatibu na madu'at (walinganizi) wa kufanya kazi kubwa katika kuufahamisha umma juu ya umuhimu wa elimu kwa watoto wa kike na wa kiume, kwa kua elimu ndio msingi imara wa umma wenye afya katika nyanja zote za kiusalama, kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiafya, aidha, elimu ni sababu miongoni mwa sababu za ulingano na kuachana na *ghuluw* (uchupaji mipaka) na *tatwarruf* (kujitenga na umma).
6) Kuzitaka taasisi na vituo vya kielimu katika vyuo vikuu kuandaa mitaala na programu zenye ubora wa viwango ili ziweze kutengeneza vizazi vya baadae vyenye uwezo wa kupambana na changamoto mbalimbali na kuzigeuza changamoto hizo kua ni fursa za kujenga na maendeleo na kukazia zaidi mtaala wa somo la dini kwa kulichukulia somo hilo kua lina nafasi ya kuwawezesha vizazi kua na masuluhisho-fanisi ya matatizo ya maisha ya kisasa kwa changamote zake na fursa zake.
7) Kushajiisha utafiti wa kisayansi, kuendeleza fikra za kiubunifu na ukosoajai-chanya, kusaidia ubunifu na uvumbuzi na kujenga uwiano wa kielimu wa pande zote mbili ya kidini na ya kidunia ili kuweza kuanda kizazi kilichokamilika na kilichoiva kiroho, kimwili, kidini na kidunia.

Baada ya hayo, Baraza la Kongamano; linapenda kuthamini juhudi kubwa

zinazochukuliwa na nchi wanachama wa ‘Jumuia ya Nchi za Kiislamu’ (OIC) ambazo zimechukulia suala la elimu kwa watoto wa kike na wa kiume kua ndio msingi wa maendeleo yao na kujiimarisha.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 240 (2/25)

Yanayohusiana na 'Athari za Janga la Korona (UVIKO) Juu ya Hukmu za Ibada, Familia na Makosa ya Jinai'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Athari za Janga la Korona (UVIKO) Juu ya Hukmu za Ibada, Familia na Makosa ya Jinai;**

na baada ya kupitia mapendekezo ya 'Warsha ya Pili ya Fiqhi ya Tiba' iliyoandaliwa na 'Sekreterieti Kuu ya Kongamano' kupitia mitandao ya intaneti tarehe 23 Shaabani, 1441 Hijria, sawa na 16 Aprili, 2020, yenye anwani ya: 'Virusi vya Korona (UVIKO-19) na Mambo Yanayohusiana Nayo ya Tiba na Hukmu za Kisharia';

na baada ya mapendekezo ya 'Warsha ya Fiqhi ya Tiba' ya kubainisha hukmu ya sharia katika utumiaji wa chanjo zinazopatikana kwa ajili ya kuchanja dhidi ya COVID-19; na baada ya kupitia mapendekezo ya 'Warsha juu ya hukmu ya ununuzi wa chanjo za UVIKO-19 na kuzigawa kwa kutumia pesa za zaka' iliyoandaliwa na 'Sekreterieti Kuu ya Kongamano' kupitia mitandao ya intaneti tarehe 10 Rajab, 1442 Hijria, sawa na 22 Februari, 2021; na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: 'Janga' hapa inakusudiwa ugonjwa wa mlipuko unaoenea kwa kasi sana na kwa maeneo makubwa nchi kwa nchi huku ikiathiri watu wengi

sana. ‘Korona’ hapa inakusudiwa kijidudu cha kirusi-taji kinachosababisha muwasho katika mfumo wa kupumua, inajulikana kwa ufupi kama: UVIKO-19.

Mbili: Korona (UVIKO-19) inahesabika kua nia janga kuu kwa kua limeugubika (limeuvamia) ulimwengu mzima, kwa maana hio hukmu za majanga na magonjwa ya milipuko zitumike juu ya janga hili.

Tatu: Mongoni mwa hukmu za majanga kwa ujumla na hukmu za korona hususan, ni kama zifuatazo:

1) Inatakiwa kwa kiongozi-mtawala (serikali) kuchukua hali za tahadhari zote zitakazozuia kuenea kwa janga, kama kuzuia swala za jamaa na ijumaa misikitini, kuzuia utekelezaji wa ibada ya hijja na umrah, kuzuia watu kutembea nje, kufunga maskuli na madaris na hatua nyenginezo zinazolenga kuihifadha nafsi (roho) ya binadamu.
2) Inajuzu kutumia mali ya zaka kwa minajili ya ununuzi wa chanjo au dawa au vifaa vya kiafya ili ziwafikie mafukara, maskini na *muallafat-Quloob* (waislamu wapya wenye mahitajio); kwa kua hawa ni miongoni mwa yale makundi manane yaliyotajwa kama wapokeaji wa zaka, aidha, inakubalika kununua hizo chanjo au dawa au vifaa vya kiafya kwa kutumia pesa nyengine kama zile za sadaka au zawadi au waqfu na pesa nyenginezo zitokanazo na michango mbalimbali.
3) Inajuzu kwa muislamu kuharakisha kutoa zaka zake iwapo kuna haja ya kufanya hivyo, kama vile inavyojuzu nyakati za majanga kumpatia zaka hizo mgonjwa alieshindwa kugharamia malipo ya matibabu yake, na pia kuwapatia wafanyakazi waliokosa kazi zao kwa sababu ya janga husika iwapo hawana kinachowatosheleza kujikimu.
4) Ni wajibu kumuosha maiti aliekufa kwa sababu ya korona, kumkafini (kumvisha sanda), kumsindikiza na kumsalia na kumzika; hatua za kinga na tahadhari zichukuliwe, ikishindikana kuoshwa basi atayamamishwe, ikiwezekana.
5) Haijuzu kuuchoma mwili wa maiti aliekufa kwa sababu ya korona, lakini anazokwa pamoja na kuchukua hatua za kinga na tahadhari.

6) Kumsindikiza na kumswalia maiti aliekufa kwa sababu ya korona ifanyike kwa kadri inavyowezekana, na kwanmna ambayo haitosababisha madhara ya kiafya.
7) Kukusudia kueneza virusi vya korona kwa wenye afya; ni kosa la jinai na mkosaji huyo anapaswa kuadhibiwa kwa kiwango cha kosa lake.

Baada ya hayo, Baraza la Kongamano; linapenda kuthamini fatwa na maamuzi mbalimbali yaliyotolewa na ‘Mabaraza ya Kisharia’ na ‘Makongamano ya Kifiqhi’ mbalimbali katika nchi kadhaa wanachama wa ‘Jumuia ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), ambapo, kupitia fatwa hizo, zimechangia kwa kiasi kikubwa kuzuia ueneaji wa janga hili.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 241 (3/25)

Yanayohusiana na 'Athari za Janga la Korona (UVIKO) Juu ya Hukmu za Miamala, Mikataba na Dhimma za Kifedha'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Athari za Janga la Korona (UVIKO) Juu ya Hukmu za Miamala, Mikataba na Dhimma za Kifedha,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano; na kuunganisha na 'Azimio la Kongamano' lililotangulia hapo juu kuhusiana na '*Athari za Janga la Korona (UVIKO) Juu ya Hukmu za Ibada, Familia na Makosa ya Jinai*';

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Janga la korona ni miongoni mwa nyudhuru za dharura zinazojuzisha kuzipitia upya dhimma za kimikataba; ima kwa kuchelewesha au kufuta au kutoa baadhi ya vipengele na mfano wake, hukmu ya yote hayo ni ile hukmu iliopo kwenye milango ya miamala katika fiqh ya kiislamu nyakati za majanga na magonjwa ya milipuko.

Mbili: Kwa wahanga (walioathirika) kwenye mikataba iliyosimamishwa au iliyoshindikana kutekelezwa nyakati za majanga na ikawa waliweka urbuni watakua na haki ya kurejeshewa urbuni zao au waingie kwenye makubaliano mapya ya kuakhirisha kwa mda, utekelezaji wa makubaliano ya awali au kumpunguzia muathirika sehemu ya uwajibikaji kwa namna ambayo italinda maslahi ya pande zote.

Tatu: Kwa aliekodi nyumba ya kuishi na akawa amenufaika na matumizi ya

nyumba aliyoikodi basi hapatakua na athari yoyote ya janga la korona juu ya malipo ya kodi; kwa hio kodi itabaki kua ni deni kwenye dhimma ya mkodishwaji iwapo ameshindwa kulipa kipindi hicho.

Nne: Haijuzu kulazimisha sharti la adhabu ikiwa korona ndio sababu ya kuchelewa kutekeleza.

Tano: Inajuzu, chini ya usimamizi wa serikali, kufanya marekebisho ya malipo ya mishahara kulingana na taathira ya janga kwa maisha ya watu, aidha inajuzu kupunguza malipo ya mishahara pamoja na kupunguza masaa ya kazi kwa kadri ya kupungua kwa manufaa, ili kuwe na uwiano na uadilifu baina ya pande zote nyakati za janga (la korona).

Sita: Inajuzu kuelekea kwenye bima ya kibiashara kwa kadri ya haja kuweza kupambana na mazito ya korona, iwapo bima-shirikishi ya kiislamu haipatikani.

Saba: Dhimma na malumbukizo ya mali yaliyotokana na mikataba ya ugharamiaji mbalimbali ambayo, janga lakorona, limesababisha ucheleweshaji wa malipo ya awamu zake; inatakiwa pande husika watafute suluhu kwa namna itakayoleta uadilifu kwa wote.

Nane: Itokeapo kumekua na magonjwa ya milipuko au majanga mengine yanayofanana na janga la korona; basi hukmu zitakua ni hizi hukmu za korona.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kuzitaka serikali za kiislamu kuandaa miradi maalum na endelevu ya kibinadamu kwa ngazi za kitaifa na kimataifa ili kupunguza uzito wa athari za kifedha zilizopelekea makmpuni na taasisi nyingi kufilisika, miradi hii ilenge kuzipatia misaada nchi zenye vipato vya chini na sekta binafsi zilizoathirika, mbali na kuwapelekea misaada ya dharura wakimbizi na waliolazimika kuacha makaazi yao na wahanga wa migogoro, majanga na magonjwa ya milipuko kwa kadri itakavyowezekana.
2) Kuzitaka kampuni za kibiashara, mabenki na wasamaria wema (*ahlul kheir*) katika jamii kuendelea kuzisaidia jamii kwa njia ya ruzuku, michango,

sadaka na misaada kwa waathirika wa janga la korona, kwa njia ya kuwaanzishia miradi mbalimbali inayolenga kupunguza athari (makali) za janga hili juu yao.

Baada ya hayo, Baraza la Kongamano; linapenda kuthamini misingi na maamuzi mbalimbali yaliyotolewa na ‘Taasisi za Kimahkama’ mbalimbali katika nchi kadhaa wanachama wa ‘Jumuia ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), ambapo, kupitia maamuzi hayo, zimechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza ‘Athari za Janga la Korona (UVIKO) Juu ya Hukmu za Miamala, Mikataba na Dhimma za Kifedha’; na kuwataka watafiti kufaidi kutokana na hayo.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 242 (4/25)

Yanayohusiana na 'Suala (Tatizo) la Kutumia Lugha Isiokua ya Kiarabu Kwenye Swala'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Suala (Tatizo) la Kutumia Lugha Isiokua ya Kiarabu Kwenye Swala,** na kwa mujibu wa mawasilisho kwa 'Wajumbe wa 'Kongamano' juu ya tatizo hili jipya la baadhi ya watu kutaka swala iswaliwe kwa kutumia lugha isiokua ya kiarabu kwa kusoma tarjama (tafsiri) ya maana ya Qur'an na tarjama za maana za dua na dhikr za lazima kwenye swala ziwe mbadala wa kusoma Qur'an yenyewe na zile adhkar za lazima za swala ambazo ni kwa lugha ya kiarabu ambazo zimetajwa kwenye Qur'an. Kwa kuzingatia kua tatizo hili halihusiani na mas'ala ya kikhilafu yaliyopo kwenye fiqh juu ya 'usomaji kwa kutumia lugha isiokua ya kiarabu kwenye swala'; na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano; na kujiepusha na mafsada yanayotokana na tatizo hili hatarishi;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Utumiaji wa lugha ya kiarabu kwenye swala ni nembo-msingi miongoni mwa nembo za kiislamu na ni wajibu uliopkelewa kizazi hadi kizazi tangu wa kati wa Mtume SAW, na ndivyo hivyo hivyo ilikua hali wakati wa maswahaba zake na waliokuja baada yao hadi leo hii, kwa hio haijuzu katu kukhalifu utaratibu huu.

Mbili: Haisihi swala yoyote itakayoswaliwa kwa kutumia lugha isiokua ya kiarabu, na hapana udhuru unaokubalika kwa asiejua lugha hio ya kiarabu,

ni wajibu wa kila muislamu kujifundisha kadiri ya inayowajibika kusomwa kutoka Qur'an na adhkar za lazima kwenye swala kama vile *takbeer* (kusema: *Allah Akbar*), tasbeeh (kusema: *Subhanallah*), t*asmee'*, *tahmeed* (kusema: *Samiallah liman hamidah*), tashahud (dua ya *tashahud – al-Tahiyyaat*) na mfano wake, rukhsa ya pekee ni muislamu mpya na yule alielemewa kabisa na kushindwa kujifundisha lugha ya kiarabu.

Tatu: Tarjama (tafsiri) ya maana ya maneno ya Qur'an Tukufu sio Qur'an kwa itifaki (ijmaa) ya wanazuoni wote wa kiislamu, kwa kua Qur'an ni jina la matamshi na maneno yenyewe, nayo ni maneno ya Allah ya kimiujiza yaliyoteremshwa kwa Mtume wake (*Rasulullah*) SAW kwa lugha ya kiarabu iliyowazi (inayofahamika), inayotumika kumuabudia Allah SWT kupitia kwayo na inayopatikana kwenye magamba mawili ya '*msahafu*' na iliyonukuliwa hivyo hivyo kizaz kwa kizazi tangu wakatu huo hadi leo hii. Lakini tarjama za maana ya Qur'an sio maneno ya Allah SWT, bali ni maneno ya binadamu, na si ya kimiujiza, bali maneno yenyewe hayajalindwa dhidi ya kukosea na hayafai kutumika kuabudia.

Nne: Kuswali kwa kutumia tarjama (tafsiri) ya maana ya maneno ya Qur'an na tarjama za maana za dua na dhikr za lazima; ijulikane kua swala hio ni batili, na muhusika wakeanawajibika kuirudia swala hio, kwa kua pamekosekana nguzo muhimu miongoni mwa nguzo za swala nayo ni: kuisoma Qur'an Tukufu ile aliyoteremshiwa Mtume Muhammad SAW.

Tano: Ni wajibu wa Mtawala (serikali) kumuadhibu kila anaeswali au anaelingania watu kuswali pasina kutumia lugha ya kiarabu, kwani kitendo hicho kitapelekea watu kukaa kando na Qur'an Tukufu na kujitosheleza na tarjama za maana yake tu, na hili likiachiwa litapelekea kuufarikisha umma na kuanza kupalilia mbegu za kiukabila.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kuzitaka serikali za nchi wanachama wa 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC) na taasisi husika kwenye masuala ya jamii za kiislamu kusimama kidete na kupambana na hao wanaolingania watu kuswali kwa kutumia tarjama (tafsiri) ya maana ya maneno ya Qur'an na tarjama za maana za dua na dhikr za lazima kwenye swala zao,

jambo ambalo tayari limeshaanza kuenea katika baadhi ya nchi wanachama wa ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), na katika jamii za kiislamu kwenye nchi nyengine, ni wazi kua kampeni hii ya upotoshaji inasimamiwa na kudhaminiwa na taasisi na makundi kinzani yenye uadui dhidi ya uislamu na yenye malengo ya kupalilia fitina miongoni mwa waislamu.

2) Kuzitaka taasisi za fatwa, mamlaka za kisharia, taasisi na makongamano ya kifiqhi, maimamu, makhatibu na madu’at (walinganizi) wajizatiti katika kubainisha uhatari wa tatizo hili na athari zake mbaya dhidi ya umoja wa umma.
3) Kuzitaka taasisi, vyuo vikuu na vituo vya kielimu kurahisisha utoaji wa elimu ya lugha ya Qur’an (kiarabu) na kuliwepesisha jambo hilo ile kumuwezesha kila muislamu ajue kusoma Qur’an kwa lugha ya kiarabu, lugha ambayo allah SWT Mwenyewe ndio kaichagua ibebe maneno yake matukufu ya kimiujiza kwa lafdhi zake na muundo wake.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 243 (5/25)

Yanayohusiana na 'Kubainisha Hukmu ya Swala Kupitia Simu, Redio na Televisheni'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kubainisha Hukmu ya Swala Kupitia Simu, Redio na Televisheni,** na kwa kuzingatia kua kumekua na maendeleo makubwa kwenye nyanja za teknolojia ya mawasiliano na vikao na mikutano kupitia mitandao ya intaneti, na uwepo wa mawasiliano ya kijamii (*social media*), kadhalika hili janga la korona linahitaji kuwe na hukmu maalum zinazohusiana na swala, misikiti na 'umbali wa kijamii (*social distance*); inayosababisha uhaba wa nafasi misikitini na pia kuzuiliwa kwa watu wasitoke majumbani mwao; na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Miongoni mwa masharti ya kusihi kua maamuma ni kuungana na imam kimahali na kiwakati ima kiuhalisia au kwa kukadiria, aidha uwepo wa maamuma kumuona imam au kumuona anaemuona imam, pia awe anasikia *takbeer* za imam japo sio zote.

Mbili: Haisihi kuswali kupitia simu, redio na televisheni; nisawa maamuma awe yuko karibu na imam au mbali, kwa kua hapa pamekosekana ufuasi baina yake na imam wa kimahali na kwa kupanguka sharti ya kusihi kua maamuma kama ilivyotajwa hapo juu, na kwa kua kufanya hivyo kutapelekea mafsada mengi sana kama vile kuwafanya watu wasiende

misikitini kuswali ijumaa na swala za jamaa, na hio kupelekea shughuli zote za kimsikiti kuatilika (kuharibika).

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 244 (6/25)

Yanayohusiana na 'Hukmu za Mitandao ya Kijamii: Vidhibiti Vyake katika Usambazaji wa Taarifa na Habari Kupitia Mitandao Hio kwa Lengo la Kukemea Maovu au Kueneza Uvumi au Kudhuru'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Kwa kutegemea 'Azimio la Kongamano' namba 52 (3/6) lililohusiana na 'Hukmu ya Mikataba Kupitia Vyombo vya Mawasiliano ya Kisasa' na baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Hukmu za Mitandao ya Kijamii: Vidhibiti Vyake katika Usambazaji wa Taarifa na Habari Kupitia Mitandao Hio kwa Lengo la Kukemea Maovu au Kueneza Uvumi au Kudhuru,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Vyombo vya mawasiliano ya kijamii ni ule mpango mzima wa mitandao ya kielektroniki inayomruhusu mshiriki wake kuanzisha eneo (site) mahsusi na kulifungamanisha na mfumo wa kijamii-kielektroniki na wanachama wengine, ama habari-mawasiliano ya kijamii ni taarifa (*content*) za kimawasiliano zinazoanzishwa na mtu yeyote binafsi lakini taarifa hizo zikaenea pande zote kwenye mitandao ya kijamii kwa uhuru kamili kutoka kwa mtuma taarifa hizo lakini pia kwa mkabala wake kuna uhuru kamili wa mrejesho kutoka kwa mpokea wa taarifa hizo, mawasiliano yanajumuisha mitandao kama ile ya: *twiter*, *whatsapp*, *facebook*, *snapchat* na mengineo inayopatikana kwa sasa na itakayozuka baadae.

Mbili: Ni haramu kuwasilisha, kueneza, kusambaza na kurikodi mambo ya

munkar (yaliyoharamishwa) kupitia kwenye vyombo hivi na mitandao hii na mengineo, aidha, ni haramu kueneza habari zozote za uongo, uvumi na kila lenye kusababishia jamii madhara katika amani yao na utulivu wao na kudhuru dini yao, aqeeda yao na maadili yao.

Tatu: Kukemea *munkar* (uchafu) kupitia mitandao ya mawasiliano ya kijamii kunadhibitiwa na masharti yaliyotajwa na wanazuoni ya kukemea (kuondoa) munkar yakiwemo:

a) Yapatikane maslahi kwa kuondoa *munkar* huo.
b) Uondoshaji wa *munkar* huo usipelekee upatikanaji wa *munkar* mwengine mkubwa kuliko huo wa awali.
c) Uondoshaji wa *munkar* huo usipelekee kuikashifu serikali (mtawala).

Inausiwa yafuatayo:

a) Mitaala ya elimu na mikarara ya masomo ibebe vigezo vya kisharia vinavyopaswa kufuatwa wakati wa utumiaji wa mitandao ya mawasiliano ya kijamii mbalimbali ile kuwawezesha vijana wa kizazi cha sasa kutofautisha baina ya manufaa na ya madhara.
b) Kujiepusha kutumia mawasiliano haya wakati mtu anaendesha vyombo kama magari na mfano wake, na wakati wa kutekeleza ibada kama ibada ya *twawaf* na *sa'yi*; kwani kunapelekea kuharibu ibada hizo na pia inapelekea mtu kuingia kwenye dhambi la kujionyesha na *ria* ambavyo vinaporomosha malipo ya ibada na kuifanya isikubalike mbele ya Allah SWT.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 245 (7/25)

Yanayohusiana na 'Mtazamo wa Sharia ya Kiislamu juu ya Kutibu Tatizo la Watoto Wanaookotwa na Watoto Waliozaliwa Wasiojulikana Nasaba zao'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Mtazamo wa Sharia ya Kiislamu juu ya Kutibu Tatizo la Watoto Wanaookotwa na Watoto Waliozaliwa Wasiojulikana Nasaba zao,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Mtoto alieokotwa ni mtoto ambae hawajulikani wazazi wake; ima ametupwa (ametelekezwa) au amepotea, ama mtoto asiejulikana nasaba yake ni yule ambae wazazi wake hawajulikani ima kwa sababu ya vita au mtetemeko wa ardhi au sababu nyengineo, aidha, inakua ni mtoto anaejulikana mama yake lakini baba yake ndie ambae hajulikani, hapa anaingia pia mtoto aliezaliwa nje ya ndoa yaani baba yake si wa halali.

Mbili:

Kuwalea watoto waliookotwa na wale wasiojulikana nasaba zao kwa mtazamo wa sharia ya kiislamu; ni lazima (*fardhi-kifaya*) apatikane mwenye kuwalea watoto kama hao, na ni jukumu miongoni mwa majukumu ya serikali iwapo hakujapatikana mwenye kuwalea, kuwalea watoto hawa kunajumuisha pia kuwatunza, kuwalipia mahitajio yao, kuwapatia elimu, kuwapatia matibabu na kuwalinda dhidi ya jambo lolote linalohatarisha

maisha yao na usalama wao, lakini pia kuwapatia kila kinachokihitajika kuwafanya wawe na maisha yenye heshima.

Tatu: Mtoto asiejulikana nasaba atanasibishwa kwa yule anaedai kua yeye ni babaake ikiwa madai hayo hayakadhibiki na hayapingiki kiakili wala kimantiki, aidha atanasibishwa kwa baba iwapo imethubutu kua ni mtoto wake kupitia mojawapo ya njia za uthibitishaji wa ubaba zinazokubalika kisharia, inamlazimu yule alithubutu ubaba wake kumsimamia mtoto huyo na kumlea.

Nne: Mtoto alieokotwa na yule asiejulikana nasaba, wapewe majina mazuri na lakabu mzuri, aidha, wapewe uraia wa nchi waliokutwa.

Tano: Mtoto alieokotwa na yule asiejulikana nasaba, watakua na haki kamili za kidini na za kiraia kama watu wengine, na kamwe haijuzu kuwaazirisha au kuwadharau, na anaewafanyia hayo aadhibiwe adhabu stahiki.

Sita: Haijuzu kumsalimisha mtoto alieokotwa na yule asiejulikana nasaba, kwa taasisi zisizokua za kiislamu au kwa watu wasioaminika.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kuzitaka serikali watunge sheria na kanuni na kuchukua taratibu muwafaka kuwachunga, kuwalea na kuwalinda watoto waliookotwa na wale wasiojulikana nasaba.
2) Inatakiwa kwa yule alieokota mtoto ampatie mke wake ili amnyonyeshe au awapatie binti zake (wakubwa wenye watoto) wamnyonyeshe ili mtoto huyo akikua atambue kua ana watu wake anaojikua nao na wanaompenda na kumtakia mazuri.
3) Kushajiisha waislamu na taasisi za kheri kuwalea na kuwachunga watoto waliookotwa na wale wasiojulikana nasaba, na kuasisi vituo vya ulezi na mapenzi hususan katika nchi zilizokumbwa na majanga na vita na migogoro.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 246 (8/25)

Yanayohusiana na 'Mtazamo wa Sharia ya Kiislamu juu ya Kutibu Tatizo la Watoto wa Barabarani, Watoto-Ombaomba na Watoto Wanaofanyishwa Kazi Ngumu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Mtazamo wa Sharia ya Kiislamu juu ya Kutibu Tatizo la Watoto wa Barabarani, Watoto-Ombaomba na Watoto Wanaofanyishwa Kazi Ngumu,** na baada ya kujikumbusha 'Azimio la Kongamano' namba 113 (7/12) lililohusiana na 'Haki za Watoto na Wazee' na ulazima wa kulifanyia kazi hususan ibara ya kwanza (moja) vifungu vyake vyote 1 hadi 10 kwa kua vimefungamana moja kwa moja na maudhui haya; na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Watoto wa Barabarani; ni watoto ambao bado hawajafikia umri wa kubalighi na ambao maisha yao wanaishi barabarani au mfano wake, huko ndiko makaazi yao na kujipatia riziki zao, nisawa iwe wazazi wao (na wasimamizi wao) wanalijua hilo au hawalijui. Watoto-Ombaomba; ni watoto ambao bado hawajafikia umri wa kubalighi na ambao wanalazimishwa kufanya kazi hio ya ombaomba kwa njia isiokua sahihi, ili wapate pesa au chakula kwa ajili ya nafsi zao au hao waliowatuma, nisawa iwe inafanyika kwa maelekezo au bila maelekezo ya wasimamzi wao. Ama watoto wanaofanyishwa kazi ngumu; ni watoto ambao bado hawajafikia umri wa kubalighi na ambao wanalazimishwa kufanya kazi ngumu na hatarishi kwa

maisha yao na afya zao, pia zinawazuia kuendelea na masomo yao na yale ambayo yangewaletea maslahi katika mustakbala wao, nisawa iwe inafanyika kwa maelekezo au bila maelekezo ya wasimamzi wao.

Mbili: Haijuzu kuwaacha (kuwatelekeza) watoto wakae barabarani na kufanya iwe ndio makaazi yao ima ya kudumu ya mda, au kufanya kua ndio nyenzo ya chumo lao, aidha, haijuzu kuwatumia watoto hao na kuwafanyisha kazi za ombaomba mabarabarani au majumbani au maofisini au kwengineko, hali kadhalika, haujuzu kuwafanyisha kazi ngumu kwenye migodi, viwandani, mashambani, majumbani na kwengineko. Haifai kabisa kuuchukulia ufukara au shida au haja kua ni kisingizio ya hayo yaliyotangulia, kwani kufanya hivyo ni kukhalifu kwa mandiko ya sharia yaliyowazi yanayolinda haki za watoto za maisha (uhai), malezi, elimu, na afya, kinyume na hivyo ni kuyaingiza maisha yao kwenye hatari na kuwanyima haki zao na kuwafanya wawe viwinjo rahisi kwa makundi ya kitapeli na kuzamishwa kwenye janga la mihadarati.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kuzitaka serikali kuwahami (kuwalinda) watoto dhidi ya dhulma, unyanyapaji, maonevu na kuwatumia vibaya; zisimamie utekelezaji wa sheria na kanuni zinazokataza kuwafanyisha kazi watoto.

2) Kuwaomba wanazuoni, madu'at (walinganizi), maimamu na makhatibu kuimarisha ufahamu wa umma juu ya uharamu wa kuwatumia vibaya watoto barabarani, nisawa iwe kutafuta rizki au kuombaomba, na wafahmishwe juu ya uharamu wa kuwafanyisha watoto kazi ngumu.
3) Kuzitaka nchi ambazo hazina sheria na kanuni zinazokataza kuwafanyisha kazi watoto; ziharakishe kutunga sheria na kanuni kama hizo ambazo zitawalinda watoto na kuwaepusha kudhulumiwa na kuonewa.
4) Kuimarisha nafasi ya familia na kuhamasisha wasimamizi kuwachunga na kuwalea watoto wao, na kujilazimisha na maadili mema na tabia mzuri katika kuamiliana na watoto.

5) Kuzisisitiza vyombo vya habari-mawasiliano mbalimbali katika nchi za

kiislamu kusimamia vyema nafasi yao katika kuielimisha jamii vilivyo juu ya uhatari wa kadhia hizi: watoto wa barabarani, watoto-ombaomba na watoto wanaofanyishwa kazi ngumu, na kuunganisha juhudi zao ili kupunguza kuenea kwa tatizo hili na kulitafutia suluhisho la kudumu.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 247 (9/25)

Yanayohusiana na 'Vigezo vya Kuyafanyisha Kazi Makusudio Makuu ya Sharia Katika Kuielekeza Miamala ya Kifedha ya Kisasa kwa Mujibu wa Hukmu za Sharia ya Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kujikumbusha 'Azimio la Kongamano' namba 167 (5/18); na baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Vigezo vya Kuyafanyisha Kazi Makusudio Makuu ya Sharia Katika Kuielekeza Miamala ya Kifedha ya Kisasa kwa Mujibu wa Hukmu za Sharia ya Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Kuweka msisitizo juu ya 'Azimio la Kongamano' namba 167 (5/18) lililohusiana na 'makusudio makuu ya sharia na nafasi yake katika kutohoa (*istinbati*) hukumu'.

Mbili: 'Makusudio makuu ya sharia' katika miamala ya kifedha ni maana na

malengo makuu ambayo sharia ya kiislamu inakusudia kuyafikia katika miamala ya kifedha kama vile; kusudio la uadilifu kwenye muamala, mizunguko ya fedha na kuenea, kuyahifadhi mali na kuyakuza.

Tatu: Mabaraza na Bodi za kisharia zinatakiwa kuzingatia na daima kujikumbusha; makusudio makuu ya sharia kwenye miamala na vidhibiti (vigezo) vyake, aidha, wanatakiwa kuyafanyakisha kazi makusudio hayo kulingana na hali halisi ilivyo; miongoni mwa vigezo hivyo ni kama vifuatavyo:

1) Yasikinzane na dalili za kisharia zinazozingatiwa.
2) Kuchunga aina na daraja za makusudio kwa kuzingatia ‘uasili’ na ‘ufuasi’, na kwa kuzingatia ‘ujumuishi’ na ‘ubaadhi’, na pia kuzingatia ‘uhakika’ na ‘dhana’; kwa namna ambayo dhana haitangulizwi mbele ya uhakika, na ubaadhi hautangulizwi mbele ya ujumuishi lakini pia ufuasi hautangulizwi mbele ya uasili.
3) Kuchunga ‘Makusudio Makuu Matano’ ya sharia wakati wa kuyafanyisha kazi makusudio mahsusi ya kimiamala.
4) Kupambanua kwenye hukmu za miamala baina ya yepi ni makusudio na yepi ni ‘*wasila*’ njia ya kufikia makusudio yenyewe, ili isije *wasila* ikapelekea kupangua au kubatilisha kusudio, na pia isije likaachwa kusudio lililothubutu kwa kuzuia mojawapo wa njia ‘*wasila*’ za kusudio hilo.
5) Inawezekana kuyafanyisha kazi makusudio ya kisharia kwenye miamala ya kifedha katika kubuni na kutafsiri mikataba na miamala ya kifedha ya kisasa, na kutatua migogoro inayojitokeza kutokana na majanga au mazingira ya dharura kwa mujibu wa ‘Kusudio la uadilifu’ na makusudio mengine ya miamala ya kifedha kama ile ya: uhamasishaji (*promotion*), uwazi na utulivu.
6) Kuyafanyia kazi ‘makusudio ya kisharia’ ili kubaini uhalisia dhidi ya dhana ya miamala ya kisasa.
7) Kuzingatia hatima za miamala ya kifedha kwa mujibu wa makusudio ya kisharia.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kuvitataka vyuo vikuu, taaasisi za kielimu na vituo vya kiutafiti kuongeza juhudi katika suala zima la ‘Mkusudio ya Kisharia’ kwa kulifundisha somo hilo na kulifanyia utafiti wa kina ili kuweza kuandaa kizazi chenye uwezo wa kuzifahamu *nususi* (maandiko ya Qur’an na ya Hadith) na makusudio yake kwa upande mmoja na pia kufahamu *nususi* na hali halisi iliopo kwa upande mwingine.
2) Kuelekeza juhudi za watafiti na wasomi wa tahasusi ya Fiqh na Usul al-Fiqh na Ilmul-Maqasid (Makusudio ya Kisharia) katika nyanja za elimu za uchumi na mas’ala ya kifedha ya kisasa.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 248 (10/25)

Yanayohusiana na ‘Hukmu za Matumizi ya Kisasa ya Upangaji upya wa Madeni (*Debt rescheduling*) na Sukuk-Mchanganyiko’

Baraza la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha’ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye ‘Kongamano’ kuhusiana na maudhui ya **Hukmu za Matumizi ya Kisasa ya Upangaji upya wa Madeni (*Debt rescheduling*) na Sukuk-Mchanganyiko,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Hukmu za Matumizi ya Kisasa ya Upangaji upya wa Madeni (*Debt rescheduling*):

1) Upangaji upya wa Madeni: Ni uhaulishaji wa deni liliopo kwenye dhimma na kulifanya kua deni kubwa zaidi kutokana na nyongeza ya malipo ya wakati, ni kufuta deni kwa deni lingine.
2) 'Kongamano' linapenda kuweka msisitizo juu ya 'Azimio lake' namba 101 (11/4) lililohusiana na: 'Kuuza Deni na Hati za Mikopo (*Loan Debentures*) ambalo lilisema hivi:

   "***Moja:*** *Haijuzu kuuza deni la baadae kwa asiedaiwa kwa malipo ya sasa hivi ya jinsi ya deni hilo au isiokua jinsi hio, kufanya hivyo kunapelekea kuingia kwenye riba. Aidha, haijuzu kuliuza deni hilo kwa malipo ya baadae ya jinsi ya deni hilo au isiokua jinsi hio, kufanya hivyo kunapelekea kuuza deni kwa deni ambayo hio imekatazwa kisharia*."

   Aidha, 'Kongamano' linapenda kuweka msisitizo juu ya 'Azimio lake' namba 158 (17/7) ambalo lilisema hivi:

   "*Moja:* *Kunahesabiwa ni kufuta deni kwa deni ambayo imekatazwa kisharia; kila jambo liatakalopelekea nyongeza ya deni kwa mdaiwa mkabala wa kuongeza mda wa deni (maturity); mfano wa hilo ni kufuta deni kwa deni kwa njia ya muamala baina ya mdai na mdaiwa; kwenye muamala huu panaibuka mkataba mpya wa deni jipya kwa mdaiwa ili ionekane amelipa deni lake la kwanza lote au baadhi yake, sawa awe mdaiwa ni muweza au amelemewa, ni kama tuseme: mdaiwa ananunua bidhaa kwa mdai kwa thamani ya kulipwa baadae kisha anaiuza bidhaa hiohio kwa thamani ya sasa ili alipe deni la kwanza lote au baadhi yake*."

3) Aina yoyote ya kuligeuza deni au kulihaulisha na ikawa inaongeza malipo juu ya deni hilo kwa mdaiwa kulingana na nyongeza ya wakati au ikapelekea hivyo; inahesabiwa ni kufuta deni kwa deni jambo ambalo limekatazwa kisharia.
4) Nafasi ya waliokubaliana kimkataba wanaruhusiwa kubadilisha vifungu vya mkataba kwa sharti ya kua mabadiliko hayo hayapelekei kukhalifu hukmu za sharia au kupelekea nyongeza juu ya deni ililiopo kwenye dhimma kwa ajili ya nyongeza ya wakati, ni sawa asili ya deni hilo liwe ni kutokana na *Murabaha* au *Istisnaa* au *Salam* au miamala

mengineyo, kwa hio marekebisho yoyote hayatakiwi kukhalifu yaliyokubalika kwa *Ijma* kua ni haramu kama vile 'riba ya madeni'.

Mbili: Sukuk-Mchanganyiko na Mseto: Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kuhusiana na maudhui haya; 'Baraza la Kongamano' limeamua kuakhirisha uchukuaji wa maamuzi ili kutoa nafasi ya tafiti za ziada.

Inausiwa yafuatayo:

Moja: Kurejea mapendekezo yenye suluhisho la wanaodaiwa waliolemewa yaliyotolewa na 'Kongamano' kwenye 'Azimio lake' namba 218 (23/2) lililohusiana na: '*Hukmu za Kulemewa na Kufilisika Baina ya Sharia ya Kiislamu na Mifumo ya Kisasa (Kukamilisha Yaliyotangulia)*'.

Mbili: Kuzitaka taasisi za kifedha za kiislamu ziwasaidie wanaodaiwa waliolemewa kupitia mpango maalum wa kuwawezesha watu kama hawa kuinuka tena na kuwawezesha kulipa madeni yao.

Tatu: Kuzitaka 'Bodi za Sharia' za taasisi za kifedha za kiislamu kusimamia na kujilazimisha kutekeleza 'Maazimio ya Kongamano' yanayohusiana na kuuza deni, kulifuta na kulihaulisha.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 249 (11/25)

Yanayohusiana na 'Athari ya Magonjwa ya Kisaikolojia ya Kisasa juu ya Ustahiki katika Sharia ya Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Athari ya Magonjwa ya Kisaikolojia ya Kisasa juu ya Ustahiki katika Sharia ya Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha uchukuaji wa maamuzi ili kutoa nafasi ya tafiti za ziada, pamoja na kuusia uandaaji wa warsha ya tahasusi juu ya kadhia hii.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 250 (12/25)

Yanayohusiana na 'Utoaji Mimba Iliyotokana na Ubakaji'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Utoaji Mimba Iliyotokana na Ubakaji,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha uchukuaji wa maamuzi ili kutoa nafasi ya tafiti za ziada, pamoja na kuusia uandaaji wa warsha ya tahasusi juu ya kadhia hii.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 251 (13/25)

Yanayohusiana na 'Hukmu ya Kugeuza Jinsia katika Uislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Hukmu ya Kugeuza Jinsia katika Uislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: 'Ugeuzaji wa Jinsia' ni ile hali ya mwanamume kujibadilisha na kua mwanamke, au mwanamke kujigeuza na kua mwanamume.

Mbili: 'Ugeuzaji wa Jinsia' Ni haramu kisharia, kwa kua ni katika kubadilisha maumbile ya Allah SWT na inaingiana na neno la Allah pale aliposema kuhusiana na Iblisi (*Laanatullah Alayh*):

> "*Na hakika nitawapoteza na nitawatia matamanio, na nitawaamrisha, basi watakata masikio ya wanyama, na nitawaamrisha, basi watabadili aliyo umba Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumfanya Shet'ani kuwa ni mlinzi wake badala ya Mwenyezi Mungu, basi huyo amekhasiri khasara ya dhaahiri*"[1].
>
> Na kwa hadith iliyopokewa kutoka kwa Anas RA aliposema: "Mtume SAW amewalaani wanaume wanaojifanya makhanithi (wanawake) na wanawake wanaojifanya wanaume", akaendelea kusema: "watoeni

[1] Surat al-Nisaa: 119.

majumbani mwenu”[1].

Tatu: Iwapo mume amejigeuza kua mwanamke, basi ni haki ya mke wake kudai kufusakhi (kufuta) ndoa yao kutokana na aibu (kasoro) hio, na iwapo mke amejigeuza kua mwanamume, basi mume anatakiwa amtaliki mke huyo.

Nne: Hukmu za kisharia zinazokhusiana na mwanamume na mwanamke miongoni mwa nyajibu na haki za kidini na za kiraia zitaendelea kubaki hivyo hivyo kabla na baada ya huyu anaejigeuza kufanya hivyo; mwanamume kujifanya mwanamke au mwanamke kujifanya mwanamume, hasahasa zile zinazokhusiana na hukmu za *hadhana* (ulezi), *nafaqa* (usimamizi a kifedha) na mirathi, hii ni kwa sababu mgeuzaji jinsia kujipeleka kua mwanamume au mwanamke ni ugeuzaji wa kiinje tu na si ugeuzaji wa kiuhalisia, na hivi ndivyo wanavyothibitisha wataalamu wa tiba, kwa hivyo hakuna athari yoyote katika hukmu za kisharia kuhusiana na ugeuzaji huu.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kuzitaka nchi na serikali mbalimbali kuzuia ugeuzaji wa kijinsia na kuhamasisha umma juu ya uhatarishi wa jambo hili na natija zake angamizi kwa wanaotenda ugeuzaji lakini pia na kwa jamii nzima, aidha kuwataka watu wenye ugonjwa wa msongo-mawazo au kuchanganyikiwa kijinsia kutokana na sababu za kisaikolojia au nyenginezo watafute matibabu.
2) Uhamasishaji juu ya uhatarishi wa ‘ulinganizi wa upotoshaji wa kijinsia na ugeuzaji wa kimaumbile’wenye lengo la kueneza uchafu, maporomoko ya kimaadili na ushoga kwa kisingizio cha kutetea haki na uhuru wa mtu binafsi.
3) Kuwataka watu warudi kwa Mola wao Allah *Azza Wajalla*, na kutekeleza yale yaliyoruhusiwa na kuhimizwa kisharia katika kutafuta tiba kwa kufuata maelekezo ya sharia tukufu ambayo ina kila aina ya ponyo ya kila gonjwa hususan magonjwa ya kisaikolojia na mengineo.

[1] Imepokewa na imam al-Bukhari.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 252 (14/25)

Yanayohusiana na 'Nafasi ya Mifumo ya Ugharamiaji ya Kijamii-Kiislamu katika Kusaidia Shughuli za Kibinadamu kwenye Maeneo Yaliyokumbwa na Majanga, Migogoro na Vita Pamoja na Kuhamasisha Utamaduni wa Kujitolea ili Kuimarisha Huduma za Kiislamu za Pamoja'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia 'Azimio la Kongamano' namba 165 (18/3) lililohusiana na '*Kutanashati Mfumo wa Zaka katika Kupambana na Ufukara*', na baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Nafasi ya Mifumo ya Ugharamiaji wa Kijamii-Kiislamu katika Kusaidia Shughuli za Kibinadamu kwenye Maeneo Yaliyokumbwa na Majanga, Migogoro na Vita Pamoja na Kuhamasisha Utamaduni wa Kujitolea ili Kuimarisha Huduma za Kiislamu za Pamoja,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Moja: Ugharamiaji wa Kijamii-Kiislamu; ni kutoa fedha kwa malengo ya kijamii lakini kwa mujibu wa sharia na misingi ya kiislamu kwa namna ambayo utoaji huo wa fedha unachangia katika uwezeshaji wa kiuchumi na uendelezaji wa jamii na kuamirisha dunia, zana za ugharamiaji za kijamii-kiislamu zipo zile za lazima kama Zaka, lakini pia zipo zisizokua za lazima kama kukopesha (*Qard Hasan*), kuazima, sadaka na waqfu.

Mbili: Inajuzu kutumia zana za ugharamiaji za kijamii-kiislamu kwa minajili ya kuwaokoa na kuwasaidia waliofikwa ma mikasa, majanga, na

walioathirika na magonjwa na wakimbizi wa vita nyakati za migogoro.

Inausiwa yafuatayo:

1) Kutoa wito juu ya uingizaji wa utamaduni wa ‘kazi za kujitolea na kubainisha umuhimu wake’ kwenye mitaala ya masomo mashuleni na vyuo vikuu ili kuimarisha uelewa na kuzidisha idadi ya wanaojitolea.
2) Kuwataka wanazuoni, wanafikra na walinganizi (madu’at) kuzihimiza jamii juu ya suala la kufanya kazi za kujitolea zinazoratibiwa kitaasisi kwa njia na aina mbalimbali.
3) Kudhihirisha umuhimu wa ‘kazi za kijamii-kibinadamu’ na umuhimu wa kusaidia kazi za kujitolea katika nyanja mbalimbali ambazo zinafaidi binadamu wote hususan nyakati za mikasa na majanga na wanapoongezeka idadi ya wakimbizi, wasaidiwe bila kujali tofauti za kidini au za kikabila.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 253 (15/25)

Yanayohusiana na 'Nafasi za Nyasia Zitumikapo kama Mojawapo ya Vifaa Yakinifu Katika Kupambana na Ufukara na Kuhakikisha Mzunguko na Ukuaji wa Fedha Katika Shari'a ya Kiislamu'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Nafasi za Nyasia Zitumikapo kama Mojawapo ya Vifaa Yakinifu Katika Kupambana na Ufukara na Kuhakikisha Mzunguko na Ukuaji wa Fedha Katika Shari'a ya Kiislamu,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha uchukuaji wa maamuzi ili kutoa nafasi ya tafiti za ziada, pamoja na kuusia uandaaji wa warsha ya tahasusi juu ya kadhia hii.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 254 (16/25)

Yanayohusiana na 'Kutizama Upya Kadhia Zilizoibuka Katika Utekelezaji wa Kisasa wa Ijara Inayoishia Kumiliki'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia 'Azimio la Kongamano' namba 44 (5/6) lililohusiana na '*Kukodi Inayoishia Kumiliki*', na baada ya kupitia 'Azimio la Kongamano' namba 110 (12/4) lililohusiana na '*Kukodisha Inayoishia Kumiliki na Hati za Uajiri*', na baada ya kupitia 'Azimio la Kongamano' namba 115 (12/9) lililohusiana na '*Mfumuko wa Bei na Kubadilika kwa Thamani ya Sarafu*', na baada ya kupitia 'Azimio la Kongamano' namba 228 (23/12) lililohusiana na '*Mapendekezo ya Kamati Iliyoundwa na Sekreterieti ya Kongamano Kufanyia Tafiti za Ziada Juu ya Baadhi ya Mas'ala ya Sukuk*', na baada ya kupitia 'Azimio la Kongamano' namba 238 (24/9) lililohusiana na '*Miamala ya Kujikinga Katika Taasisi za Kifedha za Kiislamu*', na baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Kutizama Upya Kadhia Zilizoibuka Katika Utekelezaji wa Kisasa wa Ijara Inayoishia Kumiliki,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha uchukuaji wa maamuzi ili kutoa nafasi ya tafiti za ziada, pamoja na kuusia uandaaji wa warsha ya tahasusi juu ya kadhia hii.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Bwana wetu Muhammad SAW Mtume wa mwisho, na Aali zake na maswahaba wake wote

Maamuzi nambari 255 (17/25)

Yanayohusiana na 'Barua ya Udhamini na Barua ya Mkopo'

Baraza la 'Kongamano la Kimataifa la Fiqh' lilio chini ya 'Jumuiya ya Nchi za Kiislamu' (OIC), katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha'ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Baada ya kupitia tafiti zilizowasilishwa kwenye 'Kongamano' kuhusiana na maudhui ya **Barua ya Udhamini na Barua ya Mkopo,** na baada ya usikivu wa makini wa hoja zilizoibuka kwenye maudhui haya kwa ushiriki wa wajumbe na wataalamu wa Kongamano;

Imeamuliwa yafuatayo:

Kuakhirisha uchukuaji wa maamuzi ili kutoa nafasi ya tafiti za ziada, pamoja na kuusia uandaaji wa warsha ya tahasusi juu ya kadhia hii.

Allah Ni Mjuzi Zaidi

Tamko la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’

Kuhusiana na:

‘Mtetemeko wa Ardhi Turkiye na Syria’

Lililotolewa kwenye katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha’ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Bismillah al-Rahman al-Raheem

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

Kwa mioyo iliyojaa imani na kuamini mipango na qadari ya Allah SWT, kwa vifua vilivyoridhia na kusalimu amri kwa matakwa ya Mola Mkarimu; ‘Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), linatoa hisia zake za ndani na huhzuni kubwa juu ya tukio la mtetemeko mkali wa ardhi uliopelekea maelfu ya raia wa Turkiye na Syria kupoteza maisha yao, huku tukimuomba Allah SWT awatakabalie waliokufa kwenye mtetemeko huu wawe ni ‘*Mashahidi*’ na awape shifaa na ponyo ya haraka wale waliojeruhiwa pamoja na kuwafariji familia za walioguswa na msiba huu: ‘*Inna Lillah Wainnaa Ilayh Raajioon*’.

Mbele ya janga hili la kibinadamu linalohuzunisha na kufadhaisha; ‘Baraza la Kongamano’ linatoa salamu za rambirambi (taazia) za dhati kwa familia zote za watu wetu wa Turkiye na Syria, huku tunamuomba Allah SWT awamiminie huruma zake na awasaidie kuvuka kipindi hiki kugumu kilichosababishwa na janga hili, yeye Allah SWT ndie msikivu na kujibu maombi yetu.

‘Baraza la Kongamano’ linaongeza msisitizo wake kua linasimama pamoja na watu wetu wa Turkiye na Syria, huku likiwataka umma wa kiislamu na jamii ya kibinadamu kuharakisha kuwasaidia na kuwafikishia misaada inayohitajika kupitia taasisi zinazoaminika, aidha, kwa mnasaba

huu, tunapongeza juhudi kubwa za misaada zilizosimamiwa na serikali ya *Khadimul Haramain* Mfalme Salman Bin Abdulaziz Aal-Saud yeye binafsi na ndugu zake viongozi wakuu wa nchi wanachama wa ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC) kwa ujumla, Tunamuomba Allah SWT awaondeshee athari za mtihani huu kwa haraka.

Rehema na amani za Allah zimfikie Bwana wetu Mtume Muhammad SAW yeye na watu wake na maswahaba zake, ameen.

Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 3 Sha’ban, 1444 Hijria,
sawa na 23 Februari, 2023

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu

Tamko la ‘Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’

Kuhusiana na:

‘Kukemea Tukio la Kuchomwa kwa Qur’an Tukufu Sweden (Uswidi), Denmark na Kwengineko’

Lililotolewa kwenye katika kikao chake cha ishirini na tano (25) kilichofanyika Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 29 Rajab (Rajabu) – 3 Sha’ban (Shaabani), 1444 Hijria, sawa na 20 - 23 Februari, 2023.

Bismillah al-Rahman al-Raheem

Himdi na sifa njema zote ni za Allah Mola wa viumbe wote, Na swala na salamu zimfikie Mtume wetu na Aali zake na maswahaba wake wote

‘Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ lilio chini ya ‘Jumuiya ya Nchi za Kiislamu’ (OIC), linakemea vikali na kwa lugha nzito kitendo cha magaidi wenye siasa kali nchini Sweden (Uswidi), Denmark na kwengineko; tunalaani kitendo cha kuchoma nakala za kitabu cha Allah SWT ‘Qur’an Tukufu’ kama njia yao ya kudhihirisha chuki na husda iliyomo vifuani mwao dhidi ya dini hii ya kiislamu yenye wafuasi na waumini wanaokaribia watu bilioni mbili (2 B) duniani, ikiwa ni muendelezo wa kasumba za gonjwa lijulikanalo kama ‘*Islamophobia*’ liliopo kwenye fikra na matendo yao.

kwa nafasi ya ‘Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu’ kama rejea kuu ya Kifiqhi kwa waislamu wote ulimwenguni, na kwa hisia za uwajibikaji wa *Ulamaa* wenye kunasihi, na kwa kulinda mahusiano ya kale baina ya waislamu na jamii nyengine zote, na kwa uwajibu wa kulinda amani ya dunia, na kwenda mbio katika kuimarisha uwiano miongoni mwa binadamu wote duniani; ‘Baraza la Kongamano’ linaweka msisitizo tena na tena kua matendo kama haya ya kihuni na yasiyokua mas’uli katu hayawezi na wala hayatoweza kugusa heshima na utukufu wa ‘Qur’an Tukufu’ kivyovyote, kwani kitabu hiki kitukufu kinalindwa na kuhifadhiwa

na Mwenye-Hikma na Mjuzi wa kila kitu, kitabu hiki hakifikiwi na batili yoyte itoke itokapo, kitabu hiki kimetermshwa kiwe ni uongofu kwa wachamngu na mawaidha kwa waumini, hali kadhalika, ni kitabu kinachoongoza binadamu wote. Aidha, ‘Baraza la Kongamano’ linasisitiza kua vitendo vya kihuni kama hivyo kamwe havitaathiri nafasi ya Qur’an Tukufu ndani ya nyoyo za waislamu, bali vinawazidishia imani na yakini na kushikamana zaidi na kitabu chao.

‘Baraza la Kongamano’ linapenda kurudia wito wake wa kuzitaka nchi, taasisi na jumuia za kimataifa kuimarisha ushirikiano na uratibu kwa minajili ya kupambana na matendo kama haya ya kihuni ambayo yanaonyesha dharau na kejeli kwa matakatifu ya kidini, na washirikiane kwa pamoja ili kupitisha ‘Maamuzi ya Kimataifa’ yatakayochukulia matendo kama hayo kua ni makosa ya jinai yanayojificha chini ya kisingizio cha uhuru wa maoni.

Aidha, ‘Baraza la Kongamano’ linazitaka nchi na jumuia za kiislamu zisimame kidete na kufikisha kesi ya jinai katika mahkama husika za ndani na zile za kimataifa dhidi ya kila anaetenda maovu haya ya dharau dhidi ya Uislamu, Mtume Muhammad SAW na Matakatifu ya Kiislamu.

Rehema na amani za Allah zimfikie Bwana wetu Mtume Muhammad SAW yeye na watu wake na maswahaba zake, ameen.

Jeddah (Saudi Arabia) tarehe 3 Sha’ban, 1444 Hijria,
sawa na 23 Februari, 2023

Baraza la Kongamano la Kimataifa la Fiqh ya Kiislamu